

*Maarifa Asilia*

# Mbinu za Wenyeji za Kuleta Maendeleo ya Dunia

*Kuadhimisha Miaka Mitano ya  
Mpango wa Benki ya Dunia wa  
Programu ya Maarifa Asilia kwa  
Ajili ya Maendeleo*

© 2004

Kikundi cha Maarifa na Ujifunzaji  
Kanda ya Afrika  
Benki ya Dunia

***Tini za Maarifa Asilia (MA)*** huripoti kila baada ya kipindi fulani masuala yahasuyo maarifa asilia katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na pengine masuala ya nje ya Kanda hii. Huchapishwa na Kikundi cha Maarifa na Ujifunzaji cha Kanda ya Afrika kama sehemu ya ushirikiano unaoendelea kati ya Benki ya Dunia, Jumuiya, Asasi Zisizo za Serikali (AZISE), asasi za maendeleo, na mashirika ya kimataifa.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tuma barua pepe kwenye anuani ifuatavyo:

ik-info@worldbank.org. Programu ya Maarifa Asilia kwa ajili ya Maendeleo inaweza kupatikana kwenye tovuti:  
<http://worldbank.org/afr/ik/default.htm>

Maoni yaliyoelezwa ndani ya kitabu hiki ni yale ya waandishi na si lazima kwamba yanaakisi maoni au sera za Benki ya Dunia au asasi zinazoshirikiana na Benki hiyo.

This publication has been translated by a panel of Tanzanian translators under the coordination of Prof Hermas JM Mwansoko, the Head of the Terminology and Translation Section of the Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam. It has been edited by Walter Bgoya, the Managing Director of Mkuki na Nyota Publishers, Dar es Salaam.

# Yaliyomo

Dibaji	vii
Utangulizi	.ix
Shukrani	.x
Orodha ya maneno magumu	.xi
Vifupisho	.xii

## SEHEMU YA KWANZA: MAKALA ZINAZOONGOZA

1. Maarifa Asilia—Mbinu ya Wenyeji ya Kuleta Maendeleo Duniani	.1
2. Uongezaji wa Uwezo Asilia: Ukuzaji wa Maarifa ya Jumua	.4
3. Elimu na Maarifa Asilia	.9
4. Maarifa Asilia ya Wanawake: Kujenga Madaraja kati ya Mapokeo na Uasiria	.13
5. Mbinu za Wenyeji za Kupambana na UKIMWI Barani Afrika	.18
6. Kilimo Endelevu na Njia za Kujitafutia Maisha Vijijini: Ubunifu wa Maarifa Asilia Katika Maendeleo	.24
7. Maarifa Asilia na Usimamizi wa Rasilimali za Asili	.30
8. Maarifa Asilia na Sayansi na Teknolojia: Mgongano, Ukinzani na Utangamano?	.34
9. Njia za Kienyeji katika Usuluhishi wa Migogoro Afrika	.39
10. Maarifa Asilia: Mambo ya Usoni	.45
Marejeo	.57
Waandishi wa Makala Yanayoongoza	.61

## SEHEMU YA PILI: *TINI ZA MA*

Mihutasari ya Tini za MA	.67
<i>Tini za MA</i>	
1. Mifumo ya maarifa asilia katika Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara	.73
2. <i>Zimbabwe</i> : Mifumo Endelevu ya Maarifa Asilia Katika Kilimo katika Maeneo ya Matebele Vijijini	.77
3. Wanawake wa KiSenegali Waunda Upya Utamaduni Wao	.79
4. <i>Ghana</i> : Kutoka “Kufuru” hadi Uendeleu: Ustawishaji Misitua na Kilimo cha Kutumia Mbolea ya Viumbe Hai	.83
5. <i>Burkina Faso</i> : Ujuzi wa Kusoma na Kuandika kwa “Watoto Wadogo” huko Nomgana	.87
6. <i>Senegali</i> : Wanakijiji-wamiliki Benki: Uzoefu wa Fandène	.90
7. <i>Ghana</i> : Kisomo cha Watu Wazima na Utawala wa Wenyeji katika Jumua za Vijijini	.93
8. Utunzaji wa Mazingira katika Pwani ya Magharibi ya Senegali	.96
9. <i>Mali</i> : Maendeleo ya Umoja wa Kilimo nchini Mali: Kuongezeka kwa Viwango vya Uwezeshwaji wa Wenyeji	.98
10. Njia Asilia za Uponyaji wa Watoto Walioathirika na Vita, barani Afrika	.101
11. Elimu na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika Kurani huko Afrika Magharibi	.105
12. <i>Mali</i> : Rasilimali za Utamaduni na Afya ya Mama na Mtoto nchini Mali	.108

13. Lugha za Kisaheli, Maarifa Asilia na Kujiongoza	113
14. Uenezaji wa Tafiti kwa Watu wa Kawaida katika Afrika: Ukusanyaji na Uunganishaji	117
15. Afya: Maarifa Asilia, Manufaa kwa Usawa	120
16. <i>Senegali</i> : Nguvu ya Demokrasi ya Wananchi wa Kawaida	125
17. Mipango ya Kieneo, Dira za Wenyeji: Ushirikishwaji katika Kuandaa Mustakabali huko Afrika Magharibi	128
18. Usimamizi Shirikishi na Utamaduni wa Mhali: Methali na Mikabala	132
19. Maarifa Asilia na Haki za Amali za Kiakili	136
20. Ufufuaji wa Uanagenzi na Mila za Kuingia kwenye Utu-Uzima: Nama ya Kupenya katika Uchumi wa Mijini, Afrika, Kusini mwa Sahara	139
21. Maarifa Asilia kwa ajili ya Maendeleo: Uzoefu wa Miaka Miwili	143
22. MA Yaingizwa Shuleni. Matarajio na Hofu Zinazoikabili Elimu ya Jumua huko Saheli ya Magharibi	146
23. Mbegu za Uhai: Wanawake na Kilimo Bio-anuwai katika Afrika	150
24. Uimarishaji wa Maarifa Asilia ya Kiufundi: Mfano wa Mvinyo wa Miwa	153
25. <i>Mali</i> : Maarifa Asilia: Kuchanganya Mambo Mapya na ya Kale	156
26. Dawa za Jadi na UKIMWI	160
27. <i>Uganda</i> : Teknolojia ya Habari na Maendeleo Vijijini: Kituo cha Nakaseke cha Mawasiliano Anuwai	162
28. Maarifa Asilia na Sauti ya Wenyeji katika Kupigania mabadiliko huko Afrika ya Magharibi	165
29. Lugha za Afrika ya Magharibi: Njia na Ujumbe	168
30. Ghana na Zambia: Maarifa Asilia na VVU/UKIMWI	172
31. Malicounda–Bambara: Matokeo	175
32. Waganga wa Jadi wa Kiafrika: Uchumi wa Tiba	179
33. Kukarabati Athari za Vita Nchini Msumbiji: <i>Jamii za Jando na Unyago na Shule za Jumua</i>	182
34. <i>Tanzania</i> : Usambazaji wa Maarifa ya Wenyeji kuhusu Kilimo	185
35. <i>Ethiopia</i> : Dawa za Jadi na Daraja la Kuelekea kwenye Afya Bora	188
36. <i>Eritrea</i> : Mchakato wa Kumiliki Maarifa Asilia	191
37. VVU/UKIMWI: Waganga wa Jadi, Jitihada ya Jumua Kuji-tathmini na Uwezesaji	194
38. <i>Senegali</i> : Lugha za Asili, na Fasihi kama Biashara Isiyolenga Faida	197
39. <i>Burkina Faso</i> : Uunganishaji wa Vigezo vya Kisayansi na Asilia katika Utabiri wa Mvua	201
40. Huduma ya Akinamama Wajawazito Maeneo ya Vijijini Uganda: Uboreshaji wa Mifumo ya Maarifa Asilia na ya Kisasa	205
41. <i>Eritrea</i> : Kufutia Mbali Desturi Mbaya	208
42. Kuendeleza Maarifa Asilia katika Nchi Zinazozungumza Kifaransa barani Afrika	210
43. Maonyesho ya Mbegu Kusini mwa Tanzania	213
44. <i>Uganda</i> : Mchango wa Mbogamboga kwa Uhakika wa Chakula cha Kaya	216
45. <i>India</i> : Utumiaji Maarifa Asilia Kuinua Tija ya Kilimo	219
46. Dhima ya Visasili na Kaida katika Kusimamia Maliasili Kwenye Mwambao wa Msumbiji	223
47. Kutumia Maarifa Asilia ya <i>Jatropha</i>	226
48. <i>Ethiopia</i> : Uwezo wa Bima ya Jamii ya Kijadi katika Kusaidia Huduma ya Afya	230
49. Wakulima Wafanya-Majaribio: Teknolojia ya Kujibunia	233
50. <i>Eritrea</i> : Majukumu ya Pamoja kwa Ajili ya Yatima wa Vita	237
51. Tiba ya Jadi huko Tanga katika Zama Hizi	239
52. Uelewa wa Kina wa Maarifa ya Jadi na Mimea ya Dawa	243
53. <i>Ghana</i> : Uchumi wa Maarifa Asilia ya Kiafrika	247

---

54. Matumizi ya Dawa za Jadi nchini Uganda katika Zama Zetu . . . . .	250
55. Maarifa Asilia: Ubadilishanaji wa Mafunzo Afrika Mashariki na Asia ya Kusini . . . . .	253
56. <i>Ghana</i> : Kanye Ndu Bowi: Muktadha wa Falsafa wa Utatuzi wa Migogoro . . . . .	257
57. Haki za Kitamaduni katika <i>Upekee</i> wa Mfumo wa Sheria za Zimbabwe . . . . .	260
58. Mbinu za Wanawake wa Kawaida za Kujiwezesha . . . . .	264
59. <i>Adzina</i> : Mfumo Asilia wa Uendeshaji Mashtaka wa Wazee wa Mahakama katika Eneo la Mpakani mwa Togo na Ghana . . . . .	268
60. Vikwazo vya Kitaasisi katika Uhamasishaji wa MA: Ufikiaji wa Jumua katika Mitandao ya Kijamii na Taasisi Rasmi . . . . .	271



# Dibaji

Mwaka 1996 tulibuni dira kwa ajili ya Benki ya Dunia kuwa Benki ya Maarifa inayotoa mawazo na hali kadhalika rasilimali za kifedha. Kwenye Mkutano wa Kwanza wa Maarifa ya Dunia mjini Toronto mwaka 1997, viongozi wa kisiasa na wawakilishi wa jumua za kiraia kutoka nchi zinazoendelea waliunga mkono dira hii. Waliitaka Benki ya Dunia sio tu kutoa ujuzi wake, iliyojipatia kutokana na uzoefu wake wa maendeleo wa zaidi ya miaka 50, bila pia kujifunza kutoka kwenye utendaji wa jumua ili kuleta ushawishi mzuri zaidi kwenye mifumo ya maarifa ya kimataifa na ya ndani ya nchi mahususi.

Benki ya Dunia imeitikia changamoto hii. Tunatambua kwamba maarifa sio mali ya jamii zilizoendelea kiteknolojia tu. Tunahitaji kutoa fasili mpya ya uwezeshwaji wa watu masikini na kuwasaidia kuwapatia sauti—si kama wapokeaji wa maarifa, bali kama wachangiaji na wahusika wakuu wa maendeleo yao wenyewe.

Mnamo mwaka 1998, tulizindua Programu ya Maarifa Asilia kwa ajili ya Maendeleo ili kusaidia kujifunza kutoka kwenye mifumo ya maarifa na maendeleo ya jumua, na kuijumuisha katika programu zinazofadhiliwa na Benki. Shughuli kuu ilikuwa uchapishaji na usambazaji wa mfululizo wa *Tini za MA*, ambamo watendaji wa maendeleo huripoti mafanikio ya mbinu za kienyeji katika utatuzi wa matatizo yao ya maendeleo. Chapisho hili, la kuadhimisha nusu muongo wa programu ya MA, ni mkusanyiko wa makala 60 ya ripoti hizo. Makala zinazoongoza mada hutambulisha makala ya kikundi, ikikusanya pamoja mafunzo yaliyojitokeza na kujadili athari ya maarifa asilia katika juhudi zetu za maendeleo na katika kusaidia kufanikisha Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM).

Makala yaliyomo katika kitabu hiki yanaonyesha jinsi jumua na watendaji wake wenyeji wanavyotumia mifumo ya maarifa asilia ili kuwasaidia kuongeza mavuno yao, kuelimisha watoto wao, kupunguza mateso ya VVU/UKIMWI, kupunguza vifo vya watoto wachanga na kina mama, kuondoa athari za migogoro, jumua kujifunza kutoka jumua nyingine, na jumua kujiwezesha zenyewe. Makala yanaonyesha pia kwamba jumua ziko tayari, na kwa hakika zina shauku, kuunganisha maarifa ya dunia na teknolojia ya kisasa na maarifa asilia na taasisi zao ili kupata matokeo bora zaidi. Wakunga wa jadi katika Wilaya ya Iganga nchini Uganda, kwa mfano, hutumia redio za mawasiliano za mikononi kupeleka habari za wagonjwa mahututi kwenye mfumo wa afya wa umma, na hivyo kuchangia katika kupunguza vifo vya akinamama kwa kiwango kikubwa. Na hii ni moja ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM).

Nina imani kuwa mkusanyiko huu wa makala ya uzoefu wa jumua zenye mafanikio utakuwa na manufaa makubwa katika kuboresha uelewa wetu na jinsi jumua zinavyojiwezesha zenyewe kusimamia maendeleo yao katika muktadha mpana wa utandawazi. Kutumia matukio haya kama msingi wa kusonga mbele na kusaidia jumua zenye mafanikio kupata mafanikio makubwa zaidi ni jambo muhimu sana. Aidha kutasitawisha mchakato wa maendeleo, na kuufanya kuwa wa haki na endelevu zaidi.

James Wolfensohn  
Rais  
Benki ya Dunia





# Utangulizi

Chapisho hili ni tukio muhimu la kihistoria la miaka mitano ya Programu ya Maarifa Asilia kwa ajili ya Maendeleo katika Kanda ya Afrika ya Benki ya Dunia. Lengo kuu la programu ni kujifunza kutokana na maarifa yatokanayo na utendaji wa jumua za kienyeji. Shughuli muhimu ya programu ni kuchapisha *Tini za MA*—jarida la kila mwezi linalochapwa na pia kutolewa katika mtandao wa Intaneti kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa, na pengine katika Kireno, Kiswahili na Kiwolofu. Katika chapisho hili tunatoa *Tini za MA 60*, ambamo watendaji wa maendeleo wanaeleza jinsi gani maarifa asilia yenye mafanikio yanavyositawisha mchakato wa maendeleo.

Tunajifunza, kwa mfano, jinsi jumua zilivyotumia mfumo wa mahakama za kijadi kupunguza au kuzuia migogoro nchini Ghana, jinsi wanawake wa vijijini nchini India walivyojiwezesha wenyewe kwa kujijengea uwezo wao wenyewe, jinsi vijana nchini Senegali walivyoboresha stadi na ushindani wao, jinsi ushirikiano wa waganga wa jadi unavyoimarisha ufanisi wa miradi ya VVU/UKIMWI, na jinsi jumua nchini Uganda zinavyounganisha maarifa ya kimapokeo na ya kisasa katika kupunguza vifo vya akinamama.

Kwa nyongeza, chapisho hili linaleta makala zinazohusu mada mpya za viongozi, wasomi na watendaji wa kazi za maendeleo zinazokusanya mafunzo kutokana na mada mbalimbali za *Tini* na kujadili hali inayofanya uingizaji wa maarifa asilia katika shughuli za maendeleo kufanikiwa. Na kama Mheshimiwa Rais wa Tanzania anavyohitimisha utangulizi wake wa chapisho hili, muhimu kushinda yote ni kuwa watoa maamuzi na washirika wa maendeleo hawana budi kuwa tayari kujifunza kwa jumua za wenyeji na kuwasaidia kumilika agenda za maendeleo yao.

Benki ya Dunia imechangia katika mchakato huu wa kuwasaidia wateja kujenga uwezo wao wa kuendeleza

maarifa asilia na kwa kutoa fursa zaidi za kushirikisha jumua katika maendeleo. Nchini Uganda, kwa mfano, Benki imefadhili uendelezaji wa mkakati wa kitaifa unaojumuisha maarifa asilia kwenye programu ya nchi ya kupunguza umaskini. Nchini Ethiopia, Benki inafadhili usitawishaji wa miti ya dawa kwa ajili ya soko la ndani. Benki pia iliwezesha ushirikiano kwa ajili ya uthibitishaji wa kisayansi wa dawa za kienyeji kati ya mashirika ya utafiti, AZISE, watendaji wa nchi mbalimbali, na jumua nzima ya wanasayansi duniani.

Benki imeingiza pia maarifa asilia katika programu zinazofadhiliwa na Benki ili kupata matokeo bora zaidi. Katika nchi kadhaa za Afrika Magharibi, programu za kupambana na VVU/UKIMWI zinajumuisha mashauriano ya mara kwa mara na waganga wa jadi. Kule Burkina Faso, Benki inasaidia kukuza teknolojia asilia ya uvunaji wa maji na uhifadhi wa udongo nchini kote. Miradi ya kulinda jamii inayofadhiliwa na Benki nchini Malawi, Tanzania na Uganda Kaskazini inaendelezwa kwa kutumia msingi wa asasi za kijumua na usimamizi wa wenyeji wa miradi.

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita tumejifunza mengi kuhusu ufanisi na uendeleo wa maarifa asilia katika maendeleo. Tunaona pia kuongezeka kwa utaratibu mzima wa uunganishaji wa maarifa asilia katika programu za maendeleo kwa ajili ya matokeo bora zaidi. Kwa toleo hili jipya la *Tini za MA* na makala zinazoongoza mada mbalimbali, tunaipatia jumua ya maendeleo mkusanyiko wa utendaji bora na fikra zinazo-weza kusaidia katika kuandaa programu zinazoziwezesha jumua kwa kupitia uhalalishaji na utumiaji wa mifumo ya maarifa asilia.

Callisto E. Madavo  
Makamu wa Rais  
Kanda ya Afrika

Chapisho hili ni matokeo ya ushirikiano wa kimataifa wa mtandao wa wakuzaji, watendaji na watetezi wa maarifa asilia. Wahariri wanawashukuru wale wote waliochangia kwa makala zao. Kwa zaidi ya miaka mitano, waandishi wa *Tini za MA* wametumia muda na juhudi zao kuchangiana uzoefu, maoni na mafunzo waliyojifunza. Wahariri wanaamini kwamba waandishi watapeleka shukurani zao kwa wale ambao ndio chanzo cha maarifa yanayojadiliwa hapa: jumua, wakulima wanawake, waganga wa jadi, wakunga, wazee wa vijiji, wafugaji na wengine wengi.

Wahariri wanatoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benjamin W. Mkapa, ambaye ameandika utangulizi wa chapisho hili na ambaye ujumbe wake mkuu tumeutumia kwenye jina la kitabu hiki: *Mbinu za Wenyeji za Kuleta Maendeleo ya Dunia*.

Waandishi wa makala zinazoongoza walitekeleza bila manung'uniko mapendekezo ya masahihisho ya muundo, mtindo na matumizi ya maneno yaliyotolewa na wahariri. Tunawashukuru kwa kushirikiana nasi katika majadiliano kuhusu muktadha na maudhui hadi dakika ya mwisho.

Zaidi ya hayo, wahariri wanapenda kuwashukuru wajumbe wa timu ya Programu ya Maarifa Asilia kwa ajili ya Maendeleo, na wafanyakazi wengine wa Benki ya Dunia, waliotoa maoni na michango yenye manufaa.

Kwa niaba ya Programu ya MA kwa ajili ya Maendeleo ya Kanda ya Afrika, wahariri wanapenda kutoa shukurani zao kwa Rais wa Benki ya Dunia, James D. Wolfensohn, na Makamu wa Rais wa Kanda ya Afrika, Callisto E. Madavo. Dibaji na Utangulizi wa chapisho hili na maadhimisho ni ishara ya dira yao, ambayo ilisaidia kukuza kutambuliwa kwa umuhimu mkubwa wa maarifa asilia katika mchakato wa maendeleo. Chapisho hili lisingetoka bila msaada na uongozi wao.

Wahariri wanawajibika kwa makosa yoyote yatakayojitokeza katika chapisho hili.

Reinhard Woytek  
Preeti Shroff-Mehta  
Prasad C. Mohan

# Orodha ya maneno magumu kama yalivyotumika kwenye kitabu hiki

<b>Bidaa</b>	innovative
<b>Changamani</b>	complex
<b>Dafina</b>	asset
<b>Dhuria</b>	descendants
<b>Dutu</b>	substances
<b>Gatua</b>	decentralize
<b>Hataza</b>	patent
<b>Kaida</b>	Norms/Rites
<b>Kilimo mahuluku</b>	organic farming
<b>Kiuakuvu</b>	fungicide
<b>Kiunzi</b>	Framework
<b>Kome</b>	mussels
<b>Kuamilisha</b>	activate
<b>Mbarika</b>	castor plant
<b>Mfiko</b>	range
<b>Miamala</b>	transactions
<b>Mkabala (mi-)</b>	approach(es)
<b>Mwani</b>	algae
<b>Rusu</b>	tier
<b>Ruwaza (taratibu)</b>	pattern(s)
<b>Suhula (kiambajengo)</b>	facility
<b>Thakili (janga)</b>	epidemic
<b>Uasiri</b>	modernity
<b>Uchunguzi-kifani</b>	case study
<b>Uhawilishaji</b>	transfer
<b>Ujasiriamali</b>	entrepreneurship
<b>Usanisi</b>	synthesis
<b>Vidukari</b>	aphids
<b>Visasili</b>	myths

# Vifupisho

<b>AISE</b>	Asasi Isiyo ya Serikali
<b>ARV</b>	dawa za kurefusha maisha kwa waathirika wa UKIMWI
<b>AZISE</b>	Asasi Zisizo za Serikali
<b>CIDA</b>	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Kanada
<b>FAO</b>	Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa
<b>GTZ</b>	Shirika la Misaada ya Kiufundi la Ujerumani
<b>ILO</b>	Shirika la Kazi Duniani
<b>IPR</b>	Hakimiliki ya Amali ya Kiakili
<b>MA</b>	Maarifa Asilia
<b>MDJ</b>	Maarifa ya Dawa za Jadi
<b>MMM</b>	Malengo ya Maendeleo ya Milenia
<b>NARO</b>	Asasi ya Utafiti wa Kilimo ya Taifa (Uganda)
<b>NORAD</b>	Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Norway
<b>UMADEP</b>	Mradi wa Maendeleo ya Kilimo katika Milima ya Uluguru
<b>UN</b>	Umoja wa Mataifa
<b>USAID</b>	Shirika la Marekani la Misaada ya Kimataifa
<b>VVU/UKIMWI</b>	Virusi vya Ukimwi/ Upungufu wa Kinga Mwilini
<b>WHO</b>	Shirika la Afya Duniani
<b>WIPO</b>	Shirika la Haki Miliki Duniani
<b>WTO</b>	Shirika la Biashara Duniani
<b>JZK</b>	Jumuia za Kijamii

Sehemu ya Kwanza

# Makala Zinazoongoza



# 1. Maarifa Asilia—Mbinu ya Wenyeji ya Kuleta Maendeleo Duniani

*Benjamin William Mkapa*

*Benjamin Mkapa ni Rais wa Jamhuri  
ya Muungano wa Tanzania*

Huko Laetoli, karibu na korongo la Olduvai, Kaskazini mwa Tanzania, wanapaleontolojia wamegundua nyayo za watu (hominidi) wa awali, pengine zikiwa ni za watu wazima wawili na mtoto, na hawa wakifikiriwa kuwa ni baba, mama na mtoto. Hatuelewi watu hao watatu katika ‘chimbuko la binadamu’, walitoka wapi, walikwenda wapi na walikuwa na mipango gani. Lakini wangukuwa na uwezo wa kusema, kufikiri kuwa wangebadihishana mawazo, fikra na maarifa wakati wakitembeatembea katika uwanda tambarare miaka takribani milioni tatu na nusu iliyopita.. Tangu binadamu wajitokeze duniani, wametafuta maarifa zaidi ili kulisha familia zao, kuwa wenye afya nzuri, kujadiliana na majirani zao, kuyaelewa vema zaidi mazingira yao au kujiburudisha tu na changamoto za maisha.

Kwa mamia ya milenia, mahitaji na matatizo ya wenyeji na changamoto za kila siku zilitoa msukumo wa kutafuta maarifa. Mbinu za kisayansi ya uzalishaji wa maarifa, kama tunavyoifahamu leo, ni jambo la hivi karibuni sana, kihistoria. Mbinu hii ya kisasa imeleta matokeo makubwa mno: tunao uwezo wa kuwalisha vizuri watu zaidi ya bilioni sita; chanjo huwakinga watoto wetu dhidi ya magonjwa ambayo awali yalikuwa ya kufisha; tunawasiliana dunia nzima kwa msaada wa satelaiti na tunashindanisha bidhaa zetu kwenye soko la kimataifa.

Hata hivyo, licha ya mafanikio haya, bado tuna matatizo makubwa ya njaa, VVU/UKIMWI, ujinga, utengano, migogoro na umasikini uliokithiri. Wakati mjadala kuhusu sababu za umaskini haujafungwa, tumejifunza kwamba sayansi na teknolojia peke yake haviwezi kutoa majibu na masuluhisho yote ya matatizo yaliyopo au jinsi gani tunaweza kumudu kuishi katika dunia yenye tofauti nyingi na isiyo na mgawano sawa wa utajiri na fursa mbalimbali.

Kadiri wanasayansi wanavyojitahidi kutafuta ufumbuzi wa changamoto za dunia, ndivyo wamezidi kujitenga na mbinu za wenyeji za kutatua matatizo. Ufumbuzi wa matatizo wa wenyeji ulitengwa na kuchukuliwa kuwa unazuia maendeleo, umepitwa na wakati, “simulizi za bibi” au tu kwamba hauko katika mtindo wa kisasa. Wakati “tukiasirisha” jamii zetu, “shahada”, katika maarifa ya kimapokeo au asilia haikuwepo katika mipango yetu. Hivyo, tulisahau umuhimu wake kama rasilimali na zaidi hata hatukujali maarifa

ambayo wanawake na wanaume, familia na jumua zimeyakua zenyewe kwa karne nyingi.

Makala sitini zilizomo katika chapisho hili la *Tini za MA* zinaonyesha kuwa maarifa asilia (MA) ni rasilimali inayoweza kusaidia kutatua matatizo ya wenyeji, rasilimali ya kusaidia kulima chakula kingi na bora zaidi, kudumisha maisha yenye afya, kugawana utajiri, kuzuia migogoro, kusimamia masuala mbalimbali ya wenyeji, hivyo kuchangia katika masuluhisho ya matatizo ya dunia. Maarifa asilia yamechangia kujenga mshikamano miongoni mwa jumua zilizoathirika na utandawazi na kuzikinga dhidi ya taathira za utandawazi huo. Hakuna hata moja katika malengo ya Maendeleo ya Milenia lisiloweza kusaidiwa katika utekelezaji wake na maarifa asilia. Makala sitini yaliyomo katika chapisho hili yanasisitiza mchango mkubwa unaoweza kutolewa na maarifa asilia katika maendeleo: MA yamesaidia kupunguza njaa nchini India, yameboresha elimu ya msingi na uandikishaji wa wanafunzi kwa kutumia lugha za kienyeji kama lugha za kufundishia huko Afrika Magharibi, yamewasaidia wanaume nchini Senegali kuelewa athari ya ukeketaji kwa wanawake na kuwawezesha wanawake kuchukua hatua madhubuti kukomesha desturi hiyo, yamesaidia kupunguza vifo vya watoto huko Eritrea na vifo vya akina mama nchini Uganda, yametoa afya ya msingi kwa mamilioni ya Waafrika, yamezisaidia jumua huko Msumbiji kusimamia maliasili zao za pwani, na yamesaidia kujenga ubia kati ya wanyonge na wenye nguvu nchini Ghana ili kugawana utajiri.

Hoja sitini zenye ushawishi, lakini bado inatuwira vigumu kuwashawishi wanasayansi, wanasiasa, wataalamu wa maendeleo na viongozi wengi kuyatumia kwa utaratibu wa kudumu maarifa asilia katika mchakato wa maendeleo. Wao husema kuwa wingi wa maelezo yamatukio sio ushahidi, na kuwa ushahidi wa kisayansi kwa madai mengi bado haujapatikana. Hata hivyo, kwa jumua ambamo maarifa asilia yameleta ufanisi, yanayoelezwa katika makala haya sio visa bali ni ukweli. Wangukuwa wamesubiri uthibitisho wa kisayansi wa tiba waliyopatiwa na waganga wa jadi, wagonjwa elfu nne wa VVU/UKIMWI wa Tanga, Tanzania, wasio na fursa ya kupata dawa za kisasa za kurefusha maisha (ARV) wasingekuwa hai leo.

Lakini makala hizi sitini zinatoa mafunzo zaidi kuliko faida tu za mbinu na mikabala mahususi ya maendeleo. Mafunzo yaliyo muhimu zaidi yanahusiana na umiliki wa maendeleo, uwezo wa wenyeji, kujitegemea na uwezeshaji.

Umiliki limekuwa jambo muhimu katika mjadala wa maendeleo katika miaka hii iliyopita. Uendeleo wa miradi mingi ya maendeleo iliyoanzishwa kwa ushawishi wa nje unategemea zaidi huwa haliko kabisa. Maarifa asilia husimamiwa na kumilikiwa na wenyeji. Kuchunguza, kuelewa na kujenga maendeleo kwa misingi ya maarifa ya jumua kutapunguza kwa kiasi kikubwa hatari ya kushindwa kwa mkabala wa maendeleo na mitaji iliyowekezwa na serikali na wahisani mmoja mmoja au serikali na wahisani wengi wa kimataifa. Uendeleo ulioongezeka hautokani tu na utendaji asilia mahususi ambao ungejumuishwa katika muhtadha wa mradi wa maendeleo. Ule tu mchakato wa kujifunza kutoka kwenye jumua huitambua jumua na wenye maarifa asilia kama wenza katika maendeleo ambao wanachangia vya kutosha, kama sio zaidi, katika mchakato kama watoaji wa maarifa ya dunia.

Ujengaji wa uwezo, kimsingi, unachukulia kwamba hakuna chochote kwa upande wa wafaidika wa juhudi za kujenga uwezo, hasa kwa kuwa daima zinafidiwa kidanganyifu kwa isitilahi ya uimarishaji wa uwezo. Hapana shaka, wakulima, jumua, viongozi, wahandisi na wanasiasa wa Kiafrika wana mengi ya kujifunza ili kumudu mazingira ya dunia ya kiuchumi na kisiasa yanayozidi kuwa magumu na yasiyokwisha kubadilika. Lakini, je, jumua na wakulima hawakuyamudu mazingira yaliyokuwa yakibadilika badilika huko nyuma? Majaribio ya kisiasa, asasi pungufu za kuuza mazao yao au kushindwa kwa huduma mbalimbali hakujawazuia kudumu na kujirekebisha ili kupata ufumbuzi wao wenyewe wa kuendelea kuishi. Sio tu kwamba jumua zina maarifa kuhusu utendaji, bali pia zina maarifa ya kujirekebisha ili kukabili mazingira, taasisi na sera pingamizi.

Kujitegemea, kama mila ya kisiasa nchini Tanzania tangu uhuru, ni mojawapo ya sifa muhimu za ujenzi wa maendeleo kwa kutegemea maarifa asilia. Lakini wengi walichagua kuifasili dhana ya kujitegemea kama kujitenga, kwa nia ya kutaka kuonyesha juwa ugawanaji wa maarifa na kujifunza miongoni mwa jumua za Kiafrika kunapingana na jadi, na hatari inayohusiana nao ni upotezaji wa mamlaka na udhibiti. Makala ya chapisho hili zinatueleza mambo tofauti. Jumua zina shauku ya kujifunza na kugawana, kwa sababu mazingira yao yanawafundisha somo moja takriban kila siku: ni wale tu wanaojifunza ndio watakaodumu. Kujitegemea kwa hakika ndio mkabala wa wenyeji wa maendeleo hasa kwa maana ya kiuchumi. Wakati Rais wetu wa kwanza, Marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere, alipokuwa



akikuza sera ya kujitegemea kwa mara ya kwanza baada ya uhuru wa Tanzania, kujifunza ilikuwa njia ya msingi ya maendeleo ya nchi. Endapo sayansi zingekuwa tayari kujifunza kutoka kwenye maarifa asilia, kama jumuaia za wenyeji zilizavyo tayari kujifunza kutoka kwa wengine na ulimwengu wa nje, pande hizi mbili zingefaidika sana.

Uwezeshaji ni jambo muhimu sana katika mjadala kuhusu maendeleo. Wapangaji na watekelezaji wa maendeleo hujitahidi sana kuwawezesha masikini, wanawake, na walio dhaifu. Makala katika hizi *Tini za MA* zinatufundisha kuwa uwezeshaji hauwezi kutoka nje. Uwezeshaji wa kudumu ni ule wa kujiwezesha. Jumuaia, wakulima, wanawake, wabunifu, waalimu ambao maelezo yao yametolewa hapa wote wameamua kujiwezesha wenyewe. Walipatiwa nafasi na fursa ama kupitia elimu, kupitia mawakala kama vile AZIE, kituo cha utafiti, wakala wa ugani au wizara, lakini wote walipaswa kutumia juhudi zao hadi hatua ya mwisho. Hii inaakisi vema kile Mwalimu Julius K. Nyerere alichokisema kwenye sherehe za ufunguzi wa Tume ya Kusini tarehe 20 Oktoba 1987:

“Kutoka kwa wazee wa kabila langu nilijifunza hadithi. Katika lugha asili hadithi inasema:

*Wakasusu, nihe wagya?*

*Nagya kwita Wanzugu*

*Oragya kutura?*

*Ndagya kusaya—sayamu, Ndinukira!*

*Sungura, unakwenda wapi?*

*Nakwenda kumuua Tembo.*

*Utaweza kufanya hivyo?*

*Naam, nitajaribu na kujaribu tena?*

Ni katika roho hii kwamba ninawaomba wataalamu na wapangaji wa maendeleo, watafiti na watendaji, wanasiasa na viongozi warasimu, walimu na wanafunzi kujifunza kwa unyenyekevu kutokana na mifano na makala hizi. Makala hizi si mipango makini au mbinu au njia za mkato za kuleta maendeleo, wala hazidhamirii kufanya maarifa au mapokeo asilia kubaki katika mawazo au kupendekeza kuwa maarifa ya dunia kuwa hayafai. Badala yake, yanaonyesha kwamba maarifa asilia na ya dunia yakifanya kazi pamoja kidemokrasia na kwa dhati ni mfungamano ulio bora zaidi wa kukuza maendeleo endelevu. Tunachopaswa kufanya sisi, wanasiasa na watoa maamuzi, ni kutoa nafasi kwa jambo hili kutokea.

Ni wale tu wanaojifunza ndio watakaodumu.

## 2. Uongezaji wa Uwezo Asilia: Ukuzaji wa Maarifa ya Jumua

*Frannie Leautier*

*Frannie Leautier ni Mkamu wa Rais wa Taasisi ya Benki ya Dunia*

Zikiulizwa, jamii hubainisha kwa haraka sana ufumbuzi wa matatizo ya maendeleo ya wenyeji. Ili jumua zielewe njia tofauti za maendeleo, na zipi zinawafaa uongezaji wa uwezo wao na kutoa na kusimamia ufumbuzi huo ni jambo muhimu sana. Kwenye utangulizi wa chapisho hili Mheshimiwa Rais wa Tanzania amesema kwamba jumua na wakulima wa Kiafrika daima wamemudu kukabiliana na mazingira yanayobadilika na kuwa “sio tu kwamba jumua zina maarifa kuhusu utendaji, bali pia zina maarifa ya kujirekebisha ili kukabili mazingira, taasisi na sera pingamizi.” Tini za MA katika chapisho hili zinaeleza kwa yakini misingi mitatu ya uongezaji wa uwezo katika muktadha wa maarifa asilia (MA). Kwanza, uongezaji wa uwezo usichukulie kwamba kuna ombwe la maarifa, ombwe la taasisi, ukosefu wa stadi au upungufu wa ustashi. Makala mengi yanaonyesha kwamba kukiwepo mkabala sahihi, watendaji wa maendeleo wanaweza kubaini mambo yanayofaa kuimarisha maarifa na stadi. Pili, jitihada za uongezaji wa uwezo bila fursa ya kuutumia uwezo huo katika muktadha wa wenyeji hazitakuwa na manufaa yoyote. Watu wazima hujifunza mambo vema zaidi wakati maarifa na stadi wanazozipata zinatatua moja kwa moja matatizo yao. Tatu, uongezaji wa uwezo asilia ni ufunguo wa uwezeshaji wa jumua za wenyeji na ushiriki wao thabiti katika mchakato wa maendeleo. Watu huweza kuchukua mawazo mapya yanapoonekana katika muktadha wa utendaji wa mambo uliopo.

Katika muktadha huu, tunaweza kubainisha ngazi tatu za uwezo: ngazi ya kwanza ni ya stadi za kiufundi zinazopatikana kuhusiana na matatizo halisi ya maendeleo ya hali mahususi (k.m. usimamizi wa kituo cha yatima, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, uendeshaji wa kampeni za uhamasishaji). Ngazi nyingine inahusika na stadi na mikabala iliyo muhimu kwa uendeshaji wa asasi.. Hii huhusu, kwa mfano, usimamizi wa shughuli za wenyeji na kutimiza matakwa ya wakazi wenyeji. Ngazi ya tatu inahusiana na suala la kuleta urari wa maslahi na kushauriana na serikali kuu na za mitaa, ni muhimu sana kwa uwezeshaji wa jumua na kwa maendeleo ya jamii. Kwa mfano, stadi za kiufundi zinazopatikana wakati wa kujenga shule katika jumua zinaweza kuwa na umuhimu mdogo ikilinganishwa na uzoefu wa jumua uliopatikana katika kuongoza mradi, kusimamia makandarasi, kufanya mchakato uwe wa wazi, na kukamilisha mradi bila msaada mkubwa

kutoka nje. Yakitumia baadhi ya maoni kutoka kwenye Tini za MA hizi, makala haya yanajadili jinsi jumua zinavyoweza kujijengea uwezo wake katika ngazi zote tatu na nini wenzi wa maendeleo wanaweza kufanya kuunga mkono mchakato huu.

### **Jumua zinaweza zikasimamia zenyewe jinsi ya kujiongeza uwezo**

*Tini za MA* zilizomo katika chapisho hili zinaonyesha shughuli nyingi za uongezaji uwezo zinazofanywa na jumua. Zinajumuisha urekebishaji wa programu za kujua kusoma na kuandika; uanzishaji wa mikabala ya maarifa ya wenyeji katika mitaala ya shule; shughuli za wanawake za usimamizi wa maliasili; kuonya watoto walioathirika na vita; upatikanaji wa masoko, teknolojia inayofaa, na taasisi za fedha kwa ajili ya wakulima; uandaaji na usambazaji wa utafiti; uhifadhi katika maandishi wa maarifa asilia na ulinzi wa hakimiliki za maarifa ya jumua.

Tini zinahadithia watu mashuhuri, au watu wa kawaida wanaofanya kazi nzuri ajabu, kuhusu Jumua za Kijamii (JZK) au AZISE zinazofanya kazi kwa dhati, kuhusu watafiti au watendaji wenye shauku—wote wakishughulikia kutimiza lengo moja lile lile: kuboresha hali ya maisha ya jumua wanamoishi. Mwisho, zinaeleza jinsi ambavyo jumua zimejiwezesha zenyewe kushikamana na mamlaka au wenzi wa maendeleo kusaidia zaidi maendeleo ya wenyeji.

Maelezo yafuatayo katika visanduku vitatu yanaonyesha jinsi watendaji mbalimbali walivyojiende-

leza kwa kutumia mifumo yao ya maarifa, walivyohamasisha utaalumu kutoka nje na walivyosaidia kuboresha maisha katika jumua zao.

Nchini Mali, jumua za wenyeji hutumia programu za kusoma na kuhesabu kama jukwaa la kuongeza uwezo wa kusimamia shughuli za maendeleo zinazoathiri maisha yao ya kila siku. Jumua zinatumia stadi mpya zilizopatikana kuandaa mifumo yao ya usimamizi wa vyama vya ushirika na kilimo.

Mfano huu unaweza kuonekana kama ni uchochezi dhidi ya upangaji mipango ya maendeleo uliozoeleka. Kama tatizo lingekuwa limebainika kuwa ni “udhaifu katika uendeshaji wa vyama vya ushirika” mkabala wa kawaida ungekuwa kuwapatia mafunzo wahasibu wengi zaidi katika ngazi zote (kufunza stadi sahihi za udhibiti), kuendesha semina za uhamasishaji (kuwajulisha wateja ili wajiunge), na kufunga kompyuta na kuweka mfumo wa usimamizi wa taarifa (mchakato wazi wa kutoa habari na kufuatilia maamuzi muhimu). Mradi wa aina hiyo bila shaka ungewalenga wenye elimu na wale wanaoufahamu mfumo uliopo. Badala yake, shughuli isiyo na uhusiano kabisa—programu ya kisomo cha watu wazima—iliwawezesha washirika washiriki kuanzisha mifumo yao ya uhasibu na kanuni za vyama vya ushirika, kwa kiwango cha uelewa kilichohitajika mara moja kijijini, na hivyo kuiwezesha mifumo hiyo kujirekebisha polepole ili kuendana na teknolojia mpya, kwa msingi sahihi na imara. Hatimaye, sio tu kwamba vyama vya ushirika vilisimamiwa vizuri zaidi, bali umiliki wa udhibiti uliwekwa katika mikono na ngazi sahihi.

Mfano unaofuata kutoka India unaonyesha kwamba hata katika mazingira ya kimapokeo kabisa, mtu ambaye

### **Uanzishaji upya wa usimamizi wa uzalishaji na wakulima wa nchini Mali**

Pamba imekuwa ikilimwa na kuuzwa katika Kusini mwa nchi ya Mali kwa zaidi ya miaka thelathini na ufumaji wa nguo ni utamaduni wa karne nyingi. Hivi karibuni, makampuni ya pamba na washirika wake walikuwa wakidhibiti ununuzi wa pamba kutoka kwa wakulima na usafirishaji wake hadi kwenye vituo vya kuchambulia. Leo hii, mashirika ya vijiji yamechukua karibu shughuli zote hizi. Wawakilishi wa vyama vya wakulima au vyama vyao vya muungano sasa wanawajibika kikamilifu kupima uzito wa pamba, kuwalipa wazalishaji, kuhifadhi pamba, kuisafirisha hadi kwenye vituo vya kuchambulia, na kuiuza tena kwa wazalishaji wa viwandani, na pia kwa kazi za uongozaji na uhasibu, na uandaaji wa sera

inayohitajika. Jambo hili kubwa limetekelezwa kutokana, kwa kiwango kikubwa, na programu za kusoma na kuandika na za elimu isiyo rasmi, ambazo ziliwezesha kikundi cha vijana na watu wazima kupata stadi za kusoma, kuandika na uhasibu katika lugha yao ya kienyeji. Kwa kutumia msingi wa stadi hizi mpya, washiriki walibuni na kutumia mifumo yao ya usimamizi ya lugha moja ua mbili katika vyama vya mkulima.<sup>1</sup> Wakulima nchini Mali sasa wanasimamia shughuli zote za uzalishaji na usindikaji, kama walivyokuwa wakifanya kwenye karne zilizopita, wakati vijiji vilipotengeneza nguo zake vyenyewe. Stadi asilia za usimamizi zilizokuwa zimefichika kwa miaka mingi zinatumiwa tena sasa.

### **Kichocheo cha mwenyeji chaleta mabadiliko vijijini India**

Huko vijijini India mwanamke mmoja wa daraja la chini kijamii alikubaliwa katika jumuiya yake na nje ya jumuiya kwa kupinga muktadha wa wenyeji kupitia kipaji chake cha kiufundi na uwezo wake wa kuingiza maarifa ya nje ndani ya jumuiya. Alizishawishi jumuiya kuchukua hatua za kuboresha maisha yao. Alifanya hivyo kwa kuanzisha usimamizi wa ufugaji ng'ombe wa maziwa na wa ardhi, kwanza shambani mwake, kisha katika jumuiya yake, hatimaye kwenye kanda yote. Hadi wakati huo mawakala wa ugani walikuwa wameshindwa kufanya hivyo, hasa kwa sababu jumuiya

iliwachukulia mawakala wa ugani kuwa watu wa nje ambao “wasingeweza kufahamu na kuzingatia muktadha na mazingira ya wenyeji”. “Kwa kuishi katika mazingira yanayofanana au hata yaliyo duni zaidi ya yale ya wanajumuiya wengine, kulimpatia mwanamke huyu katika kuchochea mabadiliko na si kukubali tu kuongeza uwezo, kichocheo cha kuleta mabadiliko na kuongeza uwezo lakini huku akijua aanzie wapi, na jinsi gani mawazo yake mapya yaweze kukubalika na umma mpana zaidi.<sup>2</sup>

hafikiriwi kabisa—mwanamke wa tabaka la chini—anaweza kuleta mabadiliko kwanza kwa yeye kujiongeza uwezo na kuwapa wengine kile anachokifahamu. Kujiamini katika kutekeleza mabadiliko yeye mwenyewe, kunamwezesha kuwajengea moyo wa kujiamini watu wengine. Ufahamu wa kile kitakachofaa zaidi kwake na kwa jumuiya yake unatumika vema kufanya mawazo ya aina hiyo kukubalika katika kanda yote.

Kwa miaka mingi wafanyakazi wa ugani walikuwa wamejitahidi kuanzisha usimamizi bora wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na wa teknolojia ya matumizi ya ardhi katika jumuiya zilezile, lakini walishindwa—kulingana na uchunguzi uliofanywa—kwa sababu ya kutofahamu muktadha wa wenyeji. Mfumo wa usimamizi ulioboreshwa na kutekelezwa kwa mafanikio na mwanamke wa tabaka ya chini hautofautiani sana na ule ulio-pendekezwa na wafanyakazi wa ugani. Lakini kubadili mleta mabadiliko kuwa wa kutoka nje na kuwa wa ndani, ndiko kulikoweza kufanikisha matokeo yaliyotakiwa.<sup>3</sup>

Mfano wa mwisho kutoka kwenye mradi wa utafiti uliofadhiliwa na Shirika la Misaada ya Marekani, USAID, huko Afrika Magharibi una taarifa ya erevu inayocha kabisa mada ya “ujenzi wa stadi”. Baada ya kubainisha mapengo ya stadi na mahitaji, watendaji waligeuza mkabala, wakachunguza maarifa asilia yaliyopo, na kuyaakisi matokeo kwa watafitiwa na jumuiya zao. Mkabala huu ulitoa msingi mzuri wa maarifa kuhusu stadi zilizopo za kiufundi, kiutendaji na kiusimamizi katika sekta isiyo rasmi. Lakini jambo muhimu zaidi, ni kwamba mkabala huu ulisaidia pia kuziwezesha jumuiya kwa kuzifanya zitambue kuwa maarifa yao ni muhimu na yanafaa.

Changamoto kwa watendaji wa maendeleo, serikali, na mashirika ya wenzi wa maendeleo ni kuamua yatafanya nini ili kuhamasisha michakato inayofanana na hii iliyochoambuliwa kwenye mifano hii mitatu.

### **Kuachia huru uwezo wa maarifa ya wenyeji katika Afrika Magharibi**

Mradi wa ABEL unaofadhiliwa na USAID (Kupata Elimu ya Msingi na Kusoma na Kuandika) umefaulu kuandaa mbinu za kusambaza matokeo ya utafiti unaofanywa na watafiti wa Kiafrika kuhusu mada ya “ugatuaji madaraka na ujenzi wa uwezo wa wenyeji”. Mada za utafiti zilijumuisha ujifunzaji stadi za sekta isiyo rasmi, usimamizi wa vyama vya ushirika vya wanawake, ushirikiano wa AZISE—serikali katika kutoa huduma za elimu isiyo rasmi, na majaribio katika elimu ya msingi isiyo rasmi. Mkabala wa utafiti ulisisitiza kuwashirikisha wasambazaji na hadhira

lengwa katika tathmini ya masomo, uandishi na uchambuzi wa uzoefu binafsi, na uandaaji wa sera sadifu kutokana na matokeo ya utafiti. Mkabala wa mradi wa ABEL unafasili utafiti kuwa “mazungumzo kuhusu maarifa asilia, uboreshaji wake, matumizi yake”. Wale wanaohusika na kazi walijitahidi kufanya masomo yaliyopo yaeleweke vema na yawasaidie “wateja” wao kubaini kuwa matunda ya uzoefu wao yanaweza kutafitika kama ilivyo kwa kazi zilizofanywa kwingineko.<sup>4</sup>

## Waleta mabadiliko wenyeji huchangia kuongeza uwezo wa wenyeji

Uzoefu wa awali wa ushirikiano na serikali na miradi ya maendeleo mara nyingi ulizifanya jumua zichukue mtazamo wa kusubiri ili kuona kitatokea nini. Mara nyingi, si jumua nzima au kiongozi wake, bali ni mtu binafsi au kikundi ndani ya jumua chenye maslahi mahususi, kinachoanzisha mchakato wa mabadiliko: wanawake, wazee, vijana, wazalishaji wa kahawa au hata tabaka la masikini kabisa katika jumua au pengine mtu binafsi wa kipekee. Mifano mitatu iliyomo kwenye visanduku, na uzoefu kutoka sehemu nyingine, inaonyesha kwamba hakuna njia moja “bora kabisa” ya kuleta mabadiliko na uwezeshaji kupitia uongezaji wa uwezo wa wenyeji. Isipokuwa zinapokabiliwa na mishituko mikubwa toka nje, jamii huelekea kupendelea mabadiliko ya pole pole ya kijamii na kiuchumi, hasa iwapo mazingira yaliyopo ni ya wasiwasi. Badiliko lo lote, hasa la haraka, huleta hatari ambazo tabaka za watu masikini hazitarajii na wala haziwezi kuzikabili. Ukwepaji wa hatari ndio mkakati unaotumika zaidi kukataa mikabala mingi ya mabadiliko inayoletwa toka nje. Mawakala wa mabadiliko wa nje huelekea kutoziwekea uzito unaostahili hatari hizi, kwa vile kwa kawaida huwa haziwaathiri wao moja kwa moja.

Hata hivyo, mafunzo ya uzoefu pia yanatueleza kwamba kuwa mwenyeji haitoshi kumfanya mtu alete mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Mwenyeji anahitaji angalau awe na uelewa kidogo wa maarifa yanayotoka nje, na uwezo wa kuonyesha kwamba inawezekana kuunganisha maarifa ya wenyeji na ya nje katika modeli ya utendaji. Faida ya wakala wenyeji wa mabadiliko ni

kwamba wanaufahamu muktadha wa wenyeji, “jinsi ya kuufanikisha mfumo wa kazi”. Taarifa za jinsi wanawake wa Malikunda, Senegali, walivyopinga na kisha kukomesha ukeketaji wa wanawake ni mfano hai wa faida kwa jumua ya wakala wenyeji wa mabadiliko ambao wamepatiwa uwezo kutokana na ufahamu wao wa maarifa ya nje.<sup>5</sup>

Muktadha wa wenyeji, upekepeke wa kiutamaduni, na kwa kawaida usimamizi wa umiliki wa wenyeji huelekea kuathiri kasi na mwelekeo wa mabadiliko. Mara jumua zinapokubali kusaidiwa, kuvutwa au kuendeshwa na wakala wa maendeleo, basi huelekea kutumia waziwazi maarifa yao na yale ya mawakala kukubali kutatua matatizo yao ya kijamii, kitaasisi au ya kiuchumi.

Kujifunza kwa kasi yao wenyewe kwenye ngazi ya wenyeji kupitia programu zilizopangwa vema za kusoma na kuandika aghalabu huwa kichocheo cha mabadiliko. Matokeo ya kujifunza kwa kasi yao wenyewe yanaweza kuonekana kirahisi tukiangalia elimu ya watu wazima vijijini, ambayo imekuwa na dhima kubwa kwa kuwafanya wanajumua kuwa wepesi kupanga na kuanzisha utatuzi wa matatizo.<sup>6</sup> Wakati malengo ya miradi ya elimu katika programu za kusoma na kuandika kimsingi ni kuongeza ujuzi wa kusoma na kuandika, miradi hiyo huwa na matokeo mengine yaliyolenga zaidi suala la uwezeshaji. Kwa mfano, zaidi ya kupata mafunzo ya kusoma na kuandika, washiriki wa programu kama hizo wangeamua kushughulikia utatuzi wa tatizo fulani lililomo katika jumua yao na hivyo, kuyafanya mafunzo yawe na manufaa mara moja na kuwaruhusu wenyeji kujifunza ujuzi unaoweza kutumika kutekeleza shughuli nyingine kijijini.

## Uwezo umo ndani ya shughuli za jumua

Huko Nwodwa, wakulima wasio na elimu, vijana waliokatisha masomo, na mamlaka za vijiji zilianzisha na kusimamia shughuli za ubunifu za afya, uchumi, na elimu. Mkabala huu ulikuwa wa manufaa zaidi kuliko mawazo ambayo wangependekezewa na mawakala wa mabadiliko ya nje. Katika mazingira ambamo shughuli pekee iliyobaki ya kiuchumi inayosimamiwa na kudhibitiwa na jumua ya wenyeji ni kilimo cha kujikimu, shughuli yoyote ya maana ya nyongeza inayoweza kumilikiwa na kusimamiwa na wenyeji inashabikiwa.<sup>8</sup> Watafaulu kwa sababu wanaweza kutumia uwezo wa ndani uliomo katika mbinu walizotumia kuendesha kilimo cha kujikimu, katika kusimamia shughuli za kilimo na elimu.

Mfano mwingine unaeleza kufaa kwa mbegu zilizochaguliwa na kuhifadhiwa na wenyeji kwa ajili ya kuboresha ardhi. Jumua ziliweza kuchota kutoka kwenye maarifa yao (kama yaliyohifadhiwa katika aina za kienyeji za mbegu) na uwezo uliopo tayari (wakulima wamekuwa wakilima na kuchagua mbegu kwa karne nyingi), sio tu kupanua uwezo huu lakini pia kuugeza kuwa fursa ambayo haikuwepo wakati wa huduma za ugani za kilimo za awali.<sup>9</sup> Mfano huu unaonyesha jinsi huduma za kimapokeo kutoka juu kwenda chini zinavyoweza kugeuzwa kuwataasisi kuendeleza uwezo wa wenyeji.

Kinyume na hisia za jumla<sup>7</sup> kuhusu usiri wa aina fulani za MA, na kutopenda kwa wajuzi wa maarifa asilia kujifunza kutoka kwa watu wengine, waandishi wa *Tini za MA* waligundua hamu kubwa miongoni mwa jumua ya kujifunza, kutoka jumua nyingine na pia kutoka maarifa ya dunia yaliyopo. Kujua kusoma na kuandika ndio msingi unaoziwezesha jumua kushughulikia mabadiliko hayo ya maarifa.

Juhudi za kibunifu za kusoma na kuandika zilizomo katika *Tini za MA* zinaonyesha kwamba ufundishaji kwa lugha za wenyeji na matumizi ya vifaa vya kienyeji vya kufundishia (vinavyosisitiza muktadha wa wenyeji kupitia usimuliaji hadithi, historia ya wenyeji na fasihi) huelekea kuinua zaidi viwango vya kusoma na kuandika. Matumizi ya lugha ya wenyeji sio tu yanafaa zaidi, bali pia husisitiza thamani ya utamaduni katika upangaji mipango na utekelezaji wa maendeleo. Hii pia hutoa fursa za uongezaji wa uwezo kutoka ndani ya jumua, kama mifano miwili katika visanduku vifuatavyo inavyoonyesha.

### Dhima ya wenzi wa maendeleo

Kama ilivyo katika maeneo mengine ya ushirikiano wa maendeleo, wenzi huweza kusaidia serikali kuanzisha mazingira ya kisiasa na kiuchumi yanayokuza uongezaji wa uwezo wa wenyeji, yanayosaidia jumua moja kwa moja kwa kuzipatia fursa za kuonyesha ubunifu wao, na kuwa mawakala wa kusaidia kubadilishana uzoefu baina ya jumua, nchi, na hata kanda. Mazingira wezesaji hujumuisha taratibu za kuwabaini wabunifu wenyeji, na wakati huo huo yakihakikisha kuongezeka kwa mafunzo kwa kutoa nafasi za kubadilishana maarifa na kujifunza. Mkabala wenye mantiki wa kusaidia shughuli za uongezaji wa uwezo wa wenyeji utamakinikia pia maeneo yanayozihusu sana nchi; mathalani, nchi kadhaa za Kiafrika zimeanza sasa kuwaunganisha waganga wa jadi na huduma za afya za umma. Licha ya afya, maeneo yanayoweza kutoa matokeo mazuri ni kilimo, usimamizi wa maliasili, elimu, na muhimu zaidi, uziujaji na usuluhishi wa migogoro.

Wenzi wa maendeleo wana dhima kubwa katika kusaidia kuongeza mafanikio ya vifaa vilivyobuniwa na vinavyoweza kuhawilishwa au kunakiliwa. Mara ikithibitika kwamba vifaa vilivyobuniwa na uwezo wa kuvisimamia unaweza kunakiliwa mahali pengine katika nchi au kanda, kwa faida ileile au inayofanana, wenzi na maendeleo na serikali wangeweza kuwekeza katika usambazaji wa vifaa vilivyobuniwa na wenyeji na kadhalika katika kuongeza zaidi uwezo wa wenyeji. Kama hatua ya kwanza, serikali zitie katika maandiko kiwango

cha uwezo wa kubuni katika ngazi ya jumua nchini. Kisha zisaidie shughuli za kugawana ujuzi na kujifunza. Hatimaye, zingesaidia kutia katika maandiko na kusambaza mafunzo yaliyopatikana kutoka kwenye jumua na nchi mbalimbali.

Baadhi ya mikabala mipya ya maendeleo, kama vile aina ya miradi ya Maendeleo Yanayosukumwa na Jumua au Mfuko wa Maendeleo ya Jamii<sup>10</sup> sio tu hutoa fursa za kuongeza uwezo, lakini pia fursa ya kutumia uwezo huo.

### Hitimisho

Hatua za ujenzi au uongezaji uwezo mara nyingi ni muhimu kwa programu au miradi inayolenga kuanzisha teknolojia mpya, kubadili taasisi au kuboresha huduma. Mawakala wengi wa maendeleo hutumia mkabala huu tendaji, unaozingatia mahitaji ya uwezo wa mifumo inayotarajiwa kuanzishwa. *Tini za MA* zimeonyesha kwamba uzingatiaji wa mitazamo ya jumua na uwezo wake—yaani maarifa na taasisi zilizopo husaidia kuleta umiliki zaidi, uendelevu na ufaaji wa hatua za kuongeza uwezo. Hii huhusisha utumiaji wa kanuni zilizojitokeza kutoka kwenye mifano iliyoelzwa katika *Tini za MA*—yaani, kuamini kuwepo kwa maarifa na uwezo wa kutosha wa taasisi, ikiwa ni pamoja na maarifa asilia; kutoa fursa za kutumia uwezo ulioongezwa na kukubali uongezaji wa uwezo usiwe mwisho wa mambo, bali njia ya uwezeshaji. Ingawa mantiki inaonyesha kuwa haya ni mambo yaliyo wazi, tumeona pia kwamba matokeo yaliyoelzwa ya kijamii au kiuchumi yanaweza kutimizwa tu baada ya watendaji wa maendeleo kuzikubali kanuni hizi kinadharia na kama miongozo mahususi ya maingiliano ya kijumua na ya mikabala ya utekelezaji. Matumizi ya kanuni tulizozipendekeza yatachangia kwa ufanisi zaidi kuzipatia uwezo jumua, kadiri zinavyoacha kuwa wapokeaji wa misaada na kuandaa majaliwa yao zenyewe.

1 *Tini za MA* 9

2 *Tini za MA* 58

3 *Tini za MA* 60 inaelezea mifano yenye sifa bainifu kama hizi kutoka India.

4 *Tini za MA* 14

5 *Tini za MA* 3

6 *Tini za MA* 3

7 *Tini za MA* 53

8 *Tini za MA* 7

9 *Tini za MA* 43

10 Katika miaka michache iliyopita Benki ya Dunia ilianzisha miradi ya Maendeleo Yanayosukumwa na Jumua na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii kukabili vema zaidi umasikini kwa kuwashirikisha wafaidika kubaini matatizo na kuyapatia ufumbuzi wa wenyeji, kila inapowezekana.

### 3. Elimu na Maarifa Asilia

Peter B. Easton

Peter B. Easton ni Profesa wa Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Rasilimali Watu katika Idara ya Misingi ya Kielimu na Elimu ya Sera, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida.

Uhusiano kati ya elimu na maarifa asilia (MA) katika nchi za Kiafrika ni muhimu na changamani. Pia kimsingi ni ya pande mbili kama inavyoonyeshwa na baadhi ya *Tini za MA* katika chapisho hili jumuiko. Shughuli za kielimu ni mojawapo ya njia kuu za kuhaulisha, kukusanya, kukuza, na kuleta mageuzi katika MA; na mapokeo ya maarifa asilia na ujifunzaji yanaweza kutoa modeli au ruwaza ya kutolea elimu. Uelewa wa uhusiano huu husaidia, kwanza kabisa, kupata ufahamu wa kila dhana katika mlinganyo.

#### Maana ya maarifa asilia

Wanachama wa *ENDA-Tier Monde* ya kule Dakar, AZISE inayojishughulisha sana na maendeleo ya wenyeji, wamebainisha vyema tofauti kadhaa ambazo zenyewe tu ni matokeo ya moja kwa moja ya MA katika elimu na zinaweza kutusaidia sana katika kuelewa vizuri zaidi uhusiano wa pande nyingi kati ya mambo hayo mawili.<sup>1</sup> Wanapendekeza kwamba kuna maana au ngazi tatu za uendeshaji wa maarifa asilia:

- MA kama urithi wa *mambo ya kale*, ikiwa ni pamoja na maarifa maalumu katika maeneo kama vile ya botania, tiba na uongozi wa kijamii;
- MA kama mkusanyiko wa aina tofauti za fikra na hasa za Kiafrika ambazo wanafunzi na walimu wa *sasa* wanazitumia katika kujifunza na kufundishia;
- MA kama njia ya kueleza nini watu wanajua na—*kwa baadaye*—kubuni maarifa mapya kutokana na kukutanika kwa uwezo wao (kwa maana mbili za mwanzo hapo juu) na changamoto za maendeleo.

Ngazi ya tatu ya MA—ubunifu wa maarifa mapya kutokana na makutano ya urithi wa utamaduni, vipaji vya pekee vya binafsi, stadi na umaizi vilivyokusanywa maishani, na changamoto nzito za maendeleo ya wenyeji—inapanua mjadala na kuonyesha kuwa mkubwa zaidi. Hususani, inadhihirisha kuwa shughuli kubwa ya MA kimsingi ni elimu, kwa vile haiwahusishi watu katika uvumbuzi na uhifadhi wa maarifa yaliyopo—bali inawawezesha “kuzalisha” maarifa mapya. Na kwa kweli mengi ya makala yanayounganisha MA na elimu yaliyomo katika chapisho hili ni ya aina hii: yanaeleza watu wanaotafuta njia za kubuni, kupanua na kubuni upya mapokeo.<sup>2</sup>

## Maana ya elimu

Elimu yenyewe huja katika namna mbalimbali. Utofautishaji baina ya elimu “rasmi,” “isiyo rasmi” na “ya wenyeji” uliofanywa mwanzo na Coombs na Ahmed (1974) bado unaweza kutusaidia kufasili vipengele vya msingi ambavyo vina maana kwa uelewa wetu wa matumizi ya maarifa asilia.

*Elimu rasmi* katika istilahi zao humaanisha namna ya “upangiliaji wa kitaasisi katika madaraja kuanzia ngazi ya juu hadi ya chini” unaoishia katika kutunukiwa cheti au kitu chenye hadhi kama hiyo—kwa kifupi, aina zote za mifumo rasmi ya elimu, kuanzia shule za msingi hadi vyo vikuu.

*Elimu isiyo rasmi*, kwa upande mwingine, humaanisha “shughuli yoyote ya kielimu iliyopangiliwa na kufumwa vizuri inayoendeshwa nje ya mfumo rasmi kutoa aina teule za ujifunzaji kwa vikundi maalumu vidogovidogo miongoni mwa watu, kuanzia watu wazima na pia watoto.” Hivyo inajumuisha mambo mengi—kutoka makundi ya rika ya jando na unyago au uskauti, kupitia programu za elimu ya watu wazima na elimu ya msingi, na pia elimu ya dini au uraia itolewayo nje ya shule na elimu ya ufundi au mafunzo ya biashara na viwanda inayotolewa kwa zaidi na wenyeji.

*Elimu ya wenyeji*, hatimaye, humaanisha “mchakato wa maisha mazima ambamo kwamo kila mtu hupata na kulimbikiza maarifa, stadi na umaizi kutokana na uzoefu wa kila siku na kukutana kwake na mazingira”—iwe kwa mpangilio au kwa kubahatisha, kulingana na mazingira, lakini bila kuwa yamepangiliwa, yametambuliwa na kuwekwa katika mfumo mmoja.

Hapana shaka kwamba mipaka baina ya makundi haya ya maana haiko bayana sana na hivyo mara nyingi huchanganywa, lakini maingiliano ya tofauti mbili zilizotajwa hivi punde—yaani kati ya elimu kama chombo cha MA na MA kama modeli ya elimu, kwa upande mmoja; na miongoni mwa ujifunzaji ulio rasmi, usio rasmi na wa wenyeji, kwa upande mwingine—inatoa mwanga kwa njia zile zote zinazoyaunganisha yote mawili. Matokeo yake yameonyeshwa kwenye jedwali la hapo chini. Baadhi ya vipengele vya uhusiano huo uliyoonyeshwa jedwalini umejadiliwa katika makala ya *Tini za MA yaliyomo katika chapisho hili yanayohusu elimu, moja kwa moja au kwa namna nyingineyo.*

Kama ilivyoonyeshwa kwenye safu ya kati ya jedwali, pengine sifa kuu bainifu ya mchakato wa ujifunzaji maarifa asilia ambayo inaweza utoaji wa elimu ni *umuktadhiswaji* wake. Maarifa asilia kimsingi yamefungamanishwa na shughuli za kijamii, kiutamaduni, kiuchumi za jumua husika, hupatikana kwa namna moja ama nyingine ya kushiriki katika shughuli hizo. Nyingi ya elimu rasmi na/au iliyopangiliwa katika jumua za Kiafrika *haikumuktadhiswa* na kuhusu kujifunza mambo—na kujifunza kwa njia—ambazo huonyesha uhusiano kidogo sana na tabia za kijamii, kiutamaduni, na kiuchumi za jumua enyeji.

## Athari za pande zote za jinsia na dini

Maarifa asilia si kwamba hayajali jinsia, na ukweli huu huathiri kazi zake za kielimu. MA katika tamaduni nyingi ni dhamana maalumu ya wanawake (ingawa si ya peke yao

### Mifano ya mahusiano kati ya maarifa asilia na elimu yanayopatikana kutokana na kuchanganya aina mbalimbali za elimu na njia mbalimbali za uhusiano

	Elimu kama chombo cha MA		MA kama modeli ya elimu
<b>Elimu rasmi</b>	Uanzishwaji wa historia ya mahali, ujuzi wa kiethino-botania, muziki wa asili au sanaa, n.k. katika elimu rasmi au mtaala wa chuo kikuu	Ongezeko la matumizi ya kujifunza kimuktadha na maendeleo yaliyomuktadhiswa	Matumizi ya lugha za kienyeji kama lugha ya kujifunza shuleni; utumiaji wa miundo ya uanagenzi wa kiasili kama sehemu ya ufundishaji mzima
<b>Elimu isiyo rasmi</b>	Kuwafundisha wakala wa ugani wa wenyeji au watumishi wa utawala katika hatua za kuingilia kati ambazo zinaunganisha MA na miikabala ya kisayansi ya “kimagharibi”		Juu ya hilo, ujenzi wa wigo mpya za kielimu katika makundi ya rika yaliyopo na mijumuiko ya kidesturi
<b>Elimu ya wenyeji</b>	Kuzifanya ziweze kufikiwa kwa kupitia njia mbalimbali za habari kuhusu aina anuwai za MA na matumizi yake		Katika ngazi ya jumua, kukuza makusano na biashara baina ya mafundi stadi na wananchi wengine



kabisa), ambao huhifadhi maelekezo na uelewa, hadithi, taarifa za ndani za kibotania kutoka kwenye hifadhi ya mapokeo simulizi na uzoefu wa kihistoria—hata pale ambapo mambo haya yanatawaliwa na utamaduni wa mfumo dume na kuitwa “simulizi za akina bibi.”

Mambo mengi yanaweza kusemwa kuhusu maingiliano ya MA na jinsia. Yatasha hapa kutoa mfano wa walimu. Katika nchi ambamo shule za msingi, na hasa zile za vijijini kabisa, zina walimu wengi wa kike wenye sifa zinazohitajika—kama ilivyo nchini India na baadhi ya nchi chache, lakini katika idadi inayozidi kuongezeka, za mataifa ya Afrika—waalimu kwa kweli wanaweza kupata njia, kwa kudhamiria au la, za kuingiza maudhui na mikabala waliyoitoa toka kwenye MA ya wenyeji na kupeleka katika uzoefu wa madarasa yao. Katika nchi nyingi za Kiafrika zilizotawaliwa na Ufaransa, hata hivyo, wengi wa waalimu wake wa shule za msingi za vijijini ni wanaume—na mara nyingi, kutokana na sera mahususi ya kiutawala, wanaume hao hutoka kwenye maeneo ya nchi yaliyo na utamaduni tofauti. Hali hii imeimarisha kazi yao ya mfumo wa ufundishaji usiojali muktadha uliobuniwa ili kuwaingiza watoto kwenye jamii ya *kisasa* na katika utamaduni wa kilimwengu au wa kitaifa ambao hauna uhusiano na mila na desturi za wenyeji.

Maingiliano ya dini na maarifa asilia hali kadhalika yana maana nyingi kwa elimu barani Afrika. Kuna mambo makuu matatu hapa: (a) mila za kidini za wenyeji; (b) imani na matendo ya dini za dunia (aghalabu Ukristo au Uislamu, na pengine zote mbili kwa pamoja); na (c) utamaduni wa shule za “kilei” au kiserikali. Dini zote mbili—Ukristo na Uislamu—zimetamadunishwa ziendane na utamaduni wa Kiafrika na hata “Kuafrikanishwa” katika viwango vinavyotofautiana katika mchakato wa kuhawilishwa kwao barani Afrika—kulikofanywa zaidi kupitia *elimu* ya aina moja au nyingine—ingawa watetezi wa Uislamu watapinga dai hili kwa nguvu zao zote kushinda wamisionari wa Kikristo (taz. k.m. Mughambi 2002, Monteil 1964). Na dini zote mbili hali kadhalika zimeathiri na kuathiriwa kwa viwango vinavyotofautiana na itikadi za kitaifa za maendeleo, kutegemeana na mtazamo wa kidini wa dola wa kipindi mahususi kinachohusika.

Dini hutatiza zaidi kwa sababu ya namna inavyoathiri maana ya kile kilicho cha asili ya mahali na kile kinachoringizwa toka nje. Tofauti baina ya athari za utamaduni wa wenyeji, dini za kimataifa, na ubepari wa zama za ukoloni zinajidhihirisha bayana kwenye kazi kama vile *Ceddo*, filamu mashuhuri ya mwandishi na mwongozaji wa sinema wa KiSenegali, Ousmane Sembene (2001 [1977]), ambamo imam wa Kiislamu, mmisionari wa Kikatoliki, watetezi wa mila na desturi za wenyeji, na

wawakilishi wa utawala wa kikoloni—wameonyeshwa wote wakichuana kuthibitisha nani ana nguvu zaidi. Katika mazingira kama yale ya Senegali ya karne ya 20, ambapo shule na nguvu ya dola kwa kiasi kikubwa zilishikiliwa na *entente* (mshikamano) kati ya dola na misheni za Kikristo, asasi za Kiislamu zinazoonekana kama wahifadhi wa maarifa “asilia”—yaani, vyanzo vya mila na desturi za Kiafrika zinazopingana na dola la kikoloni zikiwa na mizizi katika vizazi vingi vya wenyeji vya nyuma. Sembene anawakumbusha watazamaji wa sinema kwamba Uislamu pia ni dini iliyoingizwa nchini toka nje wakati fulani. Tukio limefanana sana na yale yanayoelezwa katika *Tini za MA* namba 4, “Kutoka Kufuru hadi Uendeleu,” kuhusu upandaji upya miti na kilimo cha kutumia mbolea ya kimaumbile huko Farikrom, Ghana, ingawa nguli huko ni Ukristo wa Kiinjilisti.

### Kuuelewa uhusiano

Kwa namna fulani, mengi ya makala katika chapisho hili yazungumzia, japo si kwa njia ya moja kwa moja, uhusiano wa maarifa asilia na elimu, kwa sababu ili njia za “kimila” na wahifadhi wake wawe na taathira katika uendeshaji wa maendeleo, ni lazima maarifa hayo yaelezeke na wahifadhi wa maarifa wahamasishwe kuyatoa. Mara yakiwa hivyo, kwa lengo lolote lile, basi mijumuiko hiyo ya maarifa na uzoefu hupata umbo muhimu linalohitajika kwa uhawilishwaji na uingizwaji katika mifumo iliyopo ya ujifunzaji wa jamii, kama maudhui au kama modeli ya mchakato.

Lakini yale makala yanayojadili kwa uwazi zaidi masuala ya elimu (rasmi, isio rasmi na ya wenyeji),<sup>3</sup> hata kama ni kwa sehemu tu, ni machache kwa idadi, na yaliyo muhimu zaidi inafaa kuyawekea msisitizo hapa. Mgawanyo na namna yake vinaonyesha mambo kadhaa yaliyozungumziwa hapo juu, ingawa, zikisomwa kwa makini, matini hizo zinaonyesha ukweli changamani na wenye nguvu unaovuka usemaji kadhaa wa kijumla kuhusu mambo.

Ni jambo la kushangaza kwamba hakuna makala yanayojadili kwa kina matumizi ya MA katika elimu rasmi, iwe katika ngazi ya shule za msingi au chuo kikuu. Ingawa mifano yake haikuonyeshwa katika makala haya, maingiliano hayana matatizo makubwa katika elimu ya juu, ambako usahihi wa kisiasa na hali ya mada kama vile historia, antropolojia, falsafa, na sosiolojia vyote vinaweza kutoa nafasi kubwa zaidi ya uzingatiaji wa maarifa ya wenyeji na desturi za Kiafrika—kama sio kwa ajili ya ufundishaji na aina ya ujifunzaji uliomuktadhiswa ambao ni wa kawaida kwa elimu ya wenyeji. Hata hivyo,

kwenye ngazi ya shule za msingi na sekondari, mapambano ni magumu zaidi. Hata matumizi ya lugha za Kiafrika—zenyewe zikiwa zimegawanyika katika idadi kubwa ya lugha za makabila na idadi ndogo za lugha za mawasiliano mapana kama vile Kiswahili na Kihausa—yamekuwa yakipendekezwa zaidi kuliko kutekelezwa kwa matendo na uendeleu (taz. k.m. Bunyi 1999).

Hata hivyo, baadhi ya makala<sup>4</sup> yanahusu uingizaji wa maudhui na mchakato wa ujifunzaji wa MA kwenye *elimu ya jumuiia*—zile aina za mafunzo zisizopimwa za msingi au sekondari zilizoanzishwa na vijiji na vyama vya wenyeji, na pengine kukuzwa na mamlaka za dola pia, kama njia ya kupunguza mahitaji makubwa ya elimu au kukabili matatizo makubwa kama vile kukosekana kwa ajira za vijana na matatizo sugu ya kijamii. Kwa bahati mbaya, kama yalivyobainisha makala, kadiri elimu hii iliyomo hatarini inavyokaribia mfumo rasmi wa elimu, ndivyo zinavyozidi kutengana na maudhui na michakato ya MA, kama matumizi ya lugha za wenyeji.

Aina nyingi za elimu isio rasmi zimejidhihirisha katika makala—kama njia ya kuhamisha nguvu za wenyeji na kupanua stadi za mahali kwa ajili ya changamoto za maendeleo;<sup>5</sup> kama suhula ya kunasa maarifa asilia na kuyatumia kwenye changamoto za sasa kama vile uletaji wa demokrasia;<sup>6</sup> na kama kitovu cha maarifa mbadala kama vile masomo ya Kurani<sup>7</sup>. Uanuwai wa mambo katika fani hii, ambao, kwa namna ya kawaida kabisa katika elimu isio rasmi, unahusu masuala kuanzia ya masoko ya bidhaa za kilimo hadi utawala wa wenyeji, afya na haki za binadamu, unatoa sura nyingi za kueleza na kukuza maarifa asilia. Ruwaza mbalimbali za maingiliano zinajidhihirisha, ambako elimu ya watu wazima na kozi za kiufundi hutumika kuimarisha tena serikali ya wenyeji huko Ghana vijijini<sup>8</sup>, ambayo inahadithia jinsi mifumo mbadala ya uanagenzi na “kanuni ya kuingia utu uzima” zilivyoandaliwa kwa ajili ya vijana wa mijini na jumuiia zilizoathiriwa vibaya na vita nchini Kenya, Sudani na Msumbiji<sup>9</sup>, na, ambako programu inayoelezea “njia za kufahamu” za wanawake wa Senegali iliishia kuwa mbinu mpya ya kupambana dhidi ya ukeketaji wa wanawake, bila kulaani utamaduni ulimochipukia.<sup>10</sup>

Mwisho, mahali na njia za kupatia elimu ya wenyeji na mahusiano yake na maarifa asilia bado ni pana zaidi, kwa vile karibu kila shughuli inayozalisha maarifa ya wenyeji na kisha kuyatumia katika kutatua matatizo ya sasa ya maendeleo—au kuyaunganisha na vyanzo vingine vya maarifa kwa namna inayohifadhika—inaweza kuleta kishindo kikubwa cha kielimu kwa washiriki na pia watazamaji. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa mifano inayochambuliwa kuhusu utafiti wa elimu nchini

Benini,<sup>11</sup> kuhusu waendesha benki wa vijijini huko Fandene, Senegali<sup>12</sup>, kuhusu wanawake wakulima wa maharage nchini Kenya,<sup>13</sup> kuhusu mikakati ya wenyeji ya kutunza mazingira kwenye pwani ya Afrika Magharibi,<sup>14</sup> na kuhusu fasihi ya Kifulani kama biashara isiyo na faida.<sup>15</sup> Kwa asasi za elimu kuweza kuchopoa mafunzo yanayofaa kutoka kwenye maarifa asilia, lazima mtu fulani aanzishe matumizi na urandamishaji wa maarifa hayo na hali halisi. Shughuli za “elimu ya wenyeji” kama zile zilizoandaliwa katika masuala yaliyorejelewa, zinatimiza, *miongoni mwa mambo mengine*, kazi hii.

### Kuyaweka yote pamoja

Kusema kweli, kuna kitu kama saketi kinachounganisha maingiliano ya maarifa asilia na aina tatu za elimu zilizozungumziwa kwa juujuu hapa. Uzoefu wa elimu ya wenyeji kama vile uchapishaji, utunzaji wa mazingira, na uendeshaji benki wa wenyeji unaohusisha matumizi au utangazaji wa maarifa asilia katika maeneo mapya hutoa fursa za mizunguko ya mafunzo yasiyo rasmi na hivyo kuboresha masomo, matumizi na uelewa ambao hatimaye unaweza kuingizwa kwenye elimu rasmi pia. Utambuzi na usambazaji wa uzoefu huo hugeuza kidogo hali ya mazingira, huimarisha elimu ya wenyeji, na kuchochea upya mzunguko husika.

Hata hivyo, hakuna hatua yoyote katika mzunguko huu ambayo imehakikishwa. Kila hatua inahitaji kujitolea kwa dhati, bidii na bahati njema au majaliwa. Ingawa upangaji wa kawaida wa mfumo wa elimu kuweka elimu rasmi katikati na asasi za elimu ya juu kileleni, ipo hoja kwamba mwanzo wa mchakato unaoelezwa hapa umo katika kile kinachoitwa na wafanyakazi wa mradi wa ENDA uwezo wa kubuni maarifa mapya katika utamaduni asilia na hivyo shughuli zisizo rasmi ambamo kwanza kipaji hicho kinapata fursa ya kuwepo.

1 *Tini za MA 42*

2 *Tini za MA 3, 4, 6, 7, 8, 16, 17, 20, 22, 23, 25, 31 na 46*

3 *Tini za MA 5, 7, 11, 13, 18, 25, 27, 29, 31, 33, 38 na 42*

4 *Tini za MA 5, 29 na 42*

5 *Tini za MA 9*

6 *Tini za MA 16*

7 *Tini za MA 11*

8 *Tini za MA 7*

9 *Tini za MA 20 na 33*

10 *Tini za MA 3 na 31*

11 *Tini za MA 14*

12 *Tini za MA 6*

13 *Tini za MA 23*

14 *Tini za MA 8*

15 *Tini za MA 38*

## 4. Maarifa Asilia ya Wanawake: Kujenga Madaraja kati ya Mapokeo na Uasiria

*Mamphela Ramphela*

*Dk. Mamphela Ramphela ni  
Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya  
Dunia*

Wanawake katika jamii nyingi duniani, wakiwa kama akinamama, akinabibi, wake, akinadada, mara nyingi huwakilisha mstari wa mbele katika huduma za afya, kutayarisha chakula kwa ajili ya familia, kutoa maadili mema, na ndio watu wa kwanza wanatoa mifano ya kuigwa katika ujenzi wa tabia. Katika jamii nyingi za vijijini za nchi zinazoendelea, wanawake hubeba mzigo wa kulima mashambani na kusafirisha mazao; hutafuta nishati kwa matumizi ya nyumbani (mara nyingi kuni) na maji. Wakati wa vipindi vya njaa, wanawake wanafahamu mimea ipi inaweza kutumiwa kama chakula cha dharura ili kunusuru familia.

Licha ya kutoa riziki kwa jumua ya wenyeji katika nyanja za afya ya familia, ulimaji wa mazao ya chakula, utatuzi wa migogoro, na uhifadhi wa bio-anuwai, wanawake pia wamekuwa wakitafuta ufumbuzi wa masuala mbalimbali ya wenyeji kama vile biashara, utalii, elimu, afya na ajira.

Licha ya mchango mkubwa kwa maisha ya familia na jumua zao, wanawake bado wanakabiliana na matatizo mengi katika kuboresha hali za maisha yao. Matatizo hayo yanajumuisha mzigo mkubwa mno wa kazi, ugumu wa kuzifikia au kuzidhibiti njia kuu za uzalishaji, na kukosekana kwa fursa za mafunzo na taarifa sahihi, huduma za ugani na za ushauri.<sup>1</sup>

Baadhi ya *Tini za MA* katika chapisho hili zinatoa mifano mahususi ambapo maarifa na matendo asilia ya wanawake huwasaidia wao, familia zao, na jumua zao kukabili kwa mafanikio changamoto za wenyeji za maendeleo. Makala haya yanatoa msisitizo wa baadhi ya mifano na kutoa mwito wa kutambua zaidi maarifa asilia ya wanawake na kuingizwa kwake katika mchakato wa maendeleo. Katika kipindi cha nyuma, maarifa asilia yanayohusiana na matunzo ya afya ya familia na uzalishaji wa chakula cha kujikimu haukufanyiwa utafiti wa kutosha. Matatizo yaliyopo yanaongezeka, yakizidisha tofauti za kijinsia kwa kiasi fulani kwa sababu maarifa ya kiufundi au kiasasi yanayohusiana na kazi za wanawake aghalabu huwa hayathaminiwi.<sup>2</sup> Wakati desturi za mfumo dume katika jamii nyingi zimechangia kuendeleza mitazamo hii, tunazidi kuona ushahidi wa jinsi wanawake wakiwa wakuzaji wa vipaumbele vyao vya maendeleo, wakiwa ni pamoja na njia za kupinga desturi za namna hiyo.

## Kushughulikia changamoto za wenyeji

Tunafahamu kutokana na matokeo yaliyomo katika *Tini za MA* kwamba nchini Senegali, wanawake wa Malikunda walianzisha kampeni iliyokomesha ukeketaji wa wanawake.<sup>3</sup> Kwa miaka mingi, mawakala wa nje, kama vile mashirika ya maendeleo, na vikundi vya ushawishi vimekuwa vikihimiza ukomeshwaji wa mila hii nchini humo. Hata hivyo, mabadiliko yalikuja baada ya wanawake wa Malikunda kuamua kutumia maarifa asilia ili kutatua tatizo hilo katika jumua zao, badala kuletewa ufumbuzi toka nje.

Hili ni tukio kubwa la uwezesaji na mabadiliko ya kijamii, lenye mafunzo muhimu. Kwa kifupi, wanawake walilishawishi baraza la kijiji kukomesha tendo la ukeketaji kijijini hapo. Hata hivyo, wakiwa hawajaridhishwa na matokeo haya, wanawake waliunda timu (iliyojumuishwa wanaume wachache) kutembelea vijiji vya jirani. Walizungumza na wanawake wa huko na kuwasaidia ili wapate uungwaji mkono na jumua zao. Pia walifaulu kuwashawishi waganga wa jadi, ikiwa ni pamoja na Imam wa Malikunda, kuunga mkono ajenda ya wanawake na kushiriki kwa nguvu kama mawakala wa mabadiliko. Mkabala huu umeongeza umiliki wa mchakato wa mabadiliko katika jumua hizo na hata nje. Matokeo yake ni kwamba, tapo hili lililoanzia kwa watu wa chini lilisababisha kuwepo kwa “Azimio la Malikunda” lililofikiwa na mkutano mkuu wa viongozi wa vijiji 18 kutoka katika kanda hiyo walioazimia kukomesha ukeketaji wa wanawake kwenye jumua zao. Mwaka mmoja baadaye, Rais wa Senegali alipendekeza “Kiapo cha Malikunda” kiigwe na taifa zima. Katika kipindi kisichozidi miaka mitatu, tapo hili lililoanzishwa na watu wa chini lilikuwa limeenea katika zaidi ya jumuiya 200 nchini kote na pia katika jumua kadhaa za nchi nyingine.<sup>4</sup>

Watafiti wamebaini pia kuwa wanawake wamekuwa mstari wa mbele katika kuhifadhi misitu ya asili na bioanuwai katika maeneo yaliyo hatarini zaidi kuharibiwa na ya pembezoni. Katika eneo la Pwani ya Magharibi ya Senegali la Popenguine, kwa mfano, wanawake wenyeji walianzisha chama kwa ajili ya ulinzi wa mazingira<sup>5</sup> ili kukabili masuala yaliyowahusu zaidi. Nayo yalijumuisha upotevu wa bio-anuwai, upungufu wa mboga za majani, mkakati usio sahihi wa utalii, kukosekana ajira za vijana, na ukosefu wa mtaji. Chama kilijumuisha waganga wa jadi, wanawake wa mijini, na vijana, kikihimiza jumua zote kwenye kanda kushiriki. Chama kilipanda miti maalumu ya kuzuia mioto kuzunguka eneo lote la misitu, kilianzisha utaratibu mzuri wa kugawana kuni, mkaa, na gesi ili kudhibiti

matumizi ya nishati, na kwa kufanya hivyo, kuunga mkono juhudi za wenyeji za kuzuia ukataji ovyo wa miti. Walikusanya uchafu wa majumbani kwa ajili ya mboji iliyotumiwa kwenye vitalu vya miche na wakaanzisha vikundi vya kuweka na kukopa fedha na mtandao wa kanda wa vyama vya wanawake.<sup>6</sup>

*Tini za MA*<sup>7</sup> nyingine zinaonyesha mchango mkubwa wa wanawake katika kutunza bioanuwai ya kilimo. Ukame huathiri mara kwa mara maeneo mengi ya Afrika, aghalabu ukisababisha njaa. Wakiwa ndiyo wazalishaji wakuu wa chakula, panapotokea upungufu wa chakula, wanawake wamebuni mikakati ya kuwa na uhakika wa chakula kwenye ngazi ya kaya. Aghalabu hutegemea mazao kutoka kwenye aina za mimea zinazostahimili ukame na wadudu waharibifu, ambayo hutoa akiba ya chakula kwa vipindi virefu vya dhiki ya kiuchumi.<sup>8</sup> Mingi ya mimea wanayoitumia wanawake vilevile hutumika kwa tiba.<sup>9</sup> Hata hivyo, teknolojia za wanawake wenyeji za baada ya mavuno, kama vile uhifadhi na usindikaji wa mazao, zimo kwenye hatari ya kupotea.<sup>10</sup> Leo hii, miradi ya uhifadhi na utumiaji endelevu wa mimea ya dawa huwashirikisha sana wanawake, waliomo na wasiomo katika maeneo ya asili ya mimea hiyo, kwenye juhudi za uhifadhi, kama vile kulima miti ya dawa katika bustani za nyumbani.<sup>11</sup>

Dhima ya MA ya wanawake yanayohusu ufugaji wa wanyama pia imedumishwa. Ingawa umiliki wa wanyama katika jamii nyingi ni wa wanaume, hata hivyo wanawake hutafuta malisho ya ng'ombe, huwatunza, huwakamua maziwa, na hukusanya na kutumia kinyesi cha ng'ombe kama nishati.<sup>12</sup> Kutokana na hali hii, utafiti uliotofautishwa kijinsia katika eneo hili umeanza kubaini kuwa wanawake wamepata ujuzi mkubwa wa ufugaji na maarifa ya tiba ya wanyama yanayojaliza maarifa ya kisayansi yaliyopo.

## Kuchangia kwenye malengo ya dunia

Utafiti kuhusu maarifa asilia umeonyesha njia ambamo wanawake wamebuni mikakati thabiti ya kusaidia kutimiza Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM). Katika Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania, kwa mfano, AZISE ya wenyeji inayoendeshwa zaidi na wanawake, hutoa kinga, upimaji, ushauri nasaha, matunzo ya nyumbani na fursa za kuzalisha mapato kwa wagonjwa wenyeji wa UKIMWI. Kutokana na tiba itolewayo na waganga wa jadi, wagonjwa wanaweza kuendelea na maisha yao ya kawaida na kuishi kwa muda mrefu zaidi. AZISE huwasaidia wanawake wanaotoa matunzo ya nyumbani ya wagonjwa wa VVU/UKIMWI. Aidha AZISE

imeanzisha vituo vya matunzo ya kutwa kwa yatima wa VVU/UKIMWI, inatoa elimu kwa watoto wa shule, na inawashirikisha wakunga wa jadi katika kampeni zake dhidi ya VVU/UKIMWI.<sup>13</sup> Kazi ya AZISE ina athari ya moja kwa moja kwa watu waishio na VVU/UKIMWI kwa kuwawezesha kuishi kwa matumaini tena. Kwa kutoa matunzo ya jumua kwa watu waishio na VVU/UKIMWI, AZISE pia husaidia kuleta usimamizi mzuri wa mzigo unaozidi kuongezeka wa kazi za wanawake, na hivyo kuwapatia nafasi kushughulikia majukumu yao mengine muhimu kama vile uzalishaji wa chakula na matunzo ya afya ya familia.

Huko Afrika Magharibi, wanawake wamefasili upya programu za elimu ya watu wazima kuhusu kisomo chenye manufaa na ujenzi wa stadi. Kufuatia ushiriki wao katika programu za kisomo chenye manufaa, wanawake walirejea kwenye jumua zao, wakiwa na uwezo zaidi sio tu kutokana na stadi zao mpya, bali pia kwa kutambua kwamba stadi na maarifa yao ya kimapokeo, yaliyojalizwa na maarifa ya nje, yanaweza kutumika kutatua matatizo ya jumua za wenyeji. Utambuzi wao mkubwa wa mambo uliwawezesha kushughulikia kero nyingine za jumua kama vile ukeketaji wa wanawake, jambo lililoogopwa kukemewa hapo awali.<sup>14</sup> Kwa kuanzisha vyama vya kanda na kuhimiza programu za kisomo cha watu wazima, waliwatia moyo wanawake wengine kuiga uzoefu wao.<sup>15</sup> Mradi mwingine wa ubunifu wa elimu nchini Mali ulitumia ishara za kiutamaduni na maarifa asilia kuanzisha mjadala kuhusu hatari za mimba na afya za wanawake katika familia na jumua. Washiriki wa mradi wamejifunza pia kutumia vifaa vya kutolea habari vya kisasa, kama vile video, chati mgeuzo na beji ili kukuza utambuzi wa jumua kuhusu hatari za afya za wanawake.<sup>16</sup>

Mifano inayohusu elimu inaonyesha uchangamani wa maarifa asilia na kusisitiza dhima ya wanawake katika muktadha huu. Wakati wanawake, hapana shaka, ni rasilimali muhimu ya maarifa asilia, baadhi ya matatizo yaliyotajwa hapo juu yanatokana na mila na desturi halisi (au za mwelekeo huo) za kiutamaduni. *Tini za MA* kuhusu elimu zinapelekea kwenye hitimisho la kushangaza: mazoea ya kiutamaduni lakini yenye madhara kama vile ukeketaji wa wanawake yameonyesha ukinzani mkubwa kwa juhudi za nje za kuyakomesha, ilihali njia za ndani na hata za wenyeji za kukabiliana nayo kwa uendeleu zinapelekea kuwa na nafasi zaidi ya kufaulu. Hata hivyo, mikabala hii ya wenyeji ilihitaji vichocheo toka nje—k.m. programu ya kisomo cha manufaa cha watu wazima—kilichowapatia wanawake hali ya kujiamini kulikabili suala, kulipeleka kwa viongozi wao wa kimapokeo, na kuwashawishi walione

lao pia. Matokeo ya michakato yote miwili—kisomo cha manufaa na pia vita dhidi ya ukeketaji wa wanawake—yalifanya wanawake watambuliwe kama kikundi chenye uwezo katika jumua zake na nje ya hapo.

Katika mfano mwingine, ushirikiano kati ya sekta ya afya ya umma ya kisasa na waganga wa jadi katika Wilaya ya Iganga nchini Uganda unaonyesha jinsi maarifa ya kisasa na asilia ya wanawake yanavyoweza kuimarishwa ili kusaidia kufanikisha mojawapo ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Mradi uliweza kupunguza pengo kati ya mifumo ya maarifa ya kimapokeo na ya kisasa na kutoa matokeo mazuri kabisa: upunguzaji wa asilimia 50 wa vifo vya kima mama katika kipindi cha miaka mitatu.<sup>17</sup>

Kando ya kisomo chenye manufaa, uzalishaji wa mapato hutoa fursa zaidi za uwezeshwaji wa wanawake. Kwa mfano, vikundi kadhaa vinavyojisaidia vyenyewe vimejitokeza kuwapatia wanawake stadi za maendeleo na fursa za kuzalisha mapato. Ni jambo la kawaida kwa wanaume kuchukua shughuli toka kwa wanawake mara shughuli hizo zinapoanza kuzalisha mapato ya fedha (k.m. wakati mazao ya chakula yanapokuwa mazao ya biashara) na kuchukua wajibu kutoka kwa wanawake mara unapotoa mapato ya fedha, hasa katika uzalishaji wa chakula. Hivyo, juhudi za kusaidia miradi ya wanawake inayozalisha mapato lazima izingatie dhima hizo za jinsia ili kuhakikisha kwamba fursa zinazotolewa zitatumia kikamilifu na wanawake. Uunganishaji wa juhudi kama hizo na mipango ya uwekaji akiba ya fedha huongeza uwezekano wa wanawake kuendelea kudhibiti mapato yao.

Nchini India, kwa mfano, wanawake waliunda zaidi ya vikundi 175 vya kujisaidia wenyewe kwenye wilaya ya vijijini ya Pratabghar huko India Kasikazini, kwa mfano kikundi cha kujisaidia wenyewe cha Kaveri Mahela. Kikiwa kimeanzishwa mwaka 1995, kikundi cha Kaveri mwanzoni kilijumuisha wanachama 15. Mwanzo, kila mwanachama aliweka akiba inayoligana na senti 10 kwa mwezi, ambayo waliiongeza mara nne hadi nane katika kipindi cha miezi sita iiyofuata. Leo hii, kila mwanachama anaweka akiba ya \$6 kwa mwezi. Fedha huhifadhiwa kwenye benki ya kijijini katika akaunti iitwayo Mfuko wa Kaveri wa Kujisaidia Wenyewe. Baada ya kuwa na akiba ya kutosha, wanawake walianzisha utaratibu wa ndani wa kukopeshana miongoni mwao kikundini. Pia walichukua mikopo binafsi hadi \$100—200 kutoka kwenye benki ya kijijini ili kuwekeza katika teknolojia za kisasa, kama vile mashine za kutengeneza sukari. Vikundi hivi vya kujisaidia wenyewe pia vimekuwa mawakala thabiti wa mabadiliko ya kijamii vijijini na vimeshughulikia masuala kadhaa nyeti kama vile mfumo

wa mahari. Leo hii, idadi kubwa ya wanawake katika wilaya hii wanaweza kusoma, kuandika, na kuelewa taratibu za uendeshaji wa biashara.<sup>18</sup>

Kwa kutumia uzoefu huu, katika mji mdogo wa Embalam huko India Kusini, wanawake wanaendesha “Vituo vya Maarifa vya Vijiji” kwa ajili ya kijiji chao na vijiji vya jirani. Hii huwawezesha wanawake kujielimisha zaidi, sio tu katika fani wanazopatiwa kupitia serikali na AZISE nyingine, bali pia katika masomo mengine ya chaguo lao, kama vile magonjwa ya kienyeji na tiba kwa binadamu na mifugo.<sup>19</sup> Kama ilivyo nchini Senegali, uwezeshwaji wa wanawake kupitia elimu nchini India umewapatia nguvu za kukabili vikwazo vya kiutamaduni vya maendeleo yao.

### Ushawishi wa maarifa asilia ya wanawake

Mfululizo wa maelezo kutoka kwenye *Tini za MA* unatoa utambuzi wa kuvutia wa maeneo mbalimbali ambao MA ya wanawake yanaweza kuwa na athari katika maendeleo. Iwe ni uzalishaji wa kienyeji au ushawishi wa kisiasa, wanawake wameweza kuwaathiri viongozi wa jumua, wanasiasa na wenzi wa maendeleo. Wameanzisha na kushughulikia masuala mazito, kama vile ukeketaji wa wanawake, VVU/UKIMWI, uhakika wa chakula, na ukosekanaji wa uzalishaji endelevu huku wakikuza asasi za ubunifu za jumua, kama vile vikundi vya kuweka fedha na kukopa, na kamati ya kudhibiti ukame.

Utafiti zaidi unahitajika kujaliza tafiti zinazohusu dhima za kijamii na kiuchumi za wanawake katika jamii zao na kuhusu mahusiano ya kimamlaka, kwa kutilia maanani zaidi maarifa asilia na busara zao. Hii itawasaidia wenzi wa maendeleo kuelewa vema zaidi, kuthamini, na hatimaye kuhalalisha michango ya aina hiyo katika maendeleo. Hasara ya kutotilia maanani MA ya wanawake nje ya maeneo yao ya “kimapokeo” na ya ndani inaweza kuwa hatimaye kupoteza kiwango kikubwa cha maarifa yao. Hii inatoa changamoto maalum kwa wenzi wa maendeleo: wanahitaji kusaidia kubuni nafasi na fursa zaidi kwa wanawake kuelezea, kutumia na kuchangia maarifa yao ya kutatua matatizo ya maendeleo.

Wanawake kama wabebaji wa maarifa asilia, wanaweza pengine vema zaidi ya wanaume kutoa huduma kama daraja kati ya wawakilishi wa mifumo mbalimbali ya maarifa. Katika eneo la afya ya familia, kwa mfano, ambako wanawake wana manufaa mahususi ya kuchukuliwa na watu wengi kuwa watendaji wakuu, fursa za maingiliano na ujifunzaji wa pande mbili zipo, kama uzoefu wa Iganga unavyoonyesha.<sup>20</sup> Wanawake

wenyeji pia wamo kwenye nafasi nzuri kushinda kero zinazoletwa na mila na desturi potovu, kuliko matumizi ya mikabala ya kutoka nje, kama mfano wa Malicounda unavyoonyesha.<sup>21</sup> Mifano hii inaonyesha fursa kwa serikali, wenzi wa maendeleo, na Benki ya Dunia pia za kuweza kuunganisha mifumo ya maarifa mbalimbali kwa ajili ya kuboresha jumua za wenyeji.

### Hitimisho

Moja ya taarifa muhimu za *Tini za MA* ni kwamba MA ya wanawake yanaweza kutoa mchango mkubwa katika kuleta matokeo endelevu katika maendeleo. Kwa hiyo, kuna haja ya kufanya kila juhudi kujumuisha maarifa ya wanawake kwenye juhudi pana zaidi za maendeleo.

Ili kuwawezesha wanawake wachangie zaidi MA yao kwenye mchakato wa maendeleo, serikali za taifa na wenzi wa maendeleo wanahitaji kuchukua hatua zaidi za kuhakikisha kuwa kuna ushiriki wenye urari kijinsia katika maendeleo. Hususani wanahitaji kuandaa mikabala inayowapatia wanawake mambo yafuatayo:

- *Nafasi*, kwa maana ya jukwaa ambako wanawake wanaweza kutoa uzoefu wao, wakijfunza kutoka kwa wenzi wao, na wakakutana na wawakilishi kutoka mifumo thabiti ya maarifa kwa ajili ya mabadilishano na ujifunzaji wenye usawa.
- *Fursa*, kwa maana ya ufukio mkubwa wa wanawake kwenye mifumo na miundo mbinu ya maarifa nchini mwao kwa namna ambayo sio elekezaji tu katika mbinu na matokeo yake. Kutoka shule ya msingi hadi kwenye programu za kisomo chenye manufaa cha watu wazima, elimu ndio kitovu cha mkabala huo, ufanisi wake unategemea ushiriki sahihi sio tu wa washiriki wa maendeleo, bali pia wa wachangiaji wa ufumbuzi wa matatizo ya maendeleo.
- *Kutambuliwa* kupitia kujitua kwa moyo thabiti kwa serikali na wenzi wa maendeleo kufanya utafiti mahususi wa MA ya wanawake; kubaini, kuweka katika maandiko, na kusambaza ipasavyo MA ya wanawake; kusaidia kuimarisha mitandao ya maarifa ya wanawake iiyopo; na kutoa jukwaa la mabadilishano ya maarifa kati ya wanawake na sayansi rasmi. Kutambuliwa, bila shaka, kunajumuisha pia uwezekano wa wanawake watendaji wa kimapokeo kupata mapato kutoka kwenye MA yao na sio kudhumuliwa na wajanja. Zaidi ya yote, “kutambuliwa” hutegemea mchakato jumuishu na shirikishi kati ya watendaji wa umma na binafsi katika maendeleo. Kwa kuwapatia fursa za aina iliyoelezwa katika *Tini za MA*, wanawake wanaweza kuwa mawakala wa mabadiliko wenye mizizi ndani ya mila na

desturi zao na bado wakaweza kushawishi ujifunzaji kutoka nje ya jumuiya zao.

- 1 Shirika la Maendeleo ya Austria, CTA, Shirika la Maendeleo la Hellen; 1999: "Dhima ya kiuchumi ya wanawake katika maendeleo ya kilimo na vijiji: Kukuza shughuli za uzalishaji mapato" Ripoti ya Semina (<http://www.ita.int/pubs/erw/english-intro.pdf>)
- 2 Madge, Clare; 1994: Mkusanyiko wa maarifa ya chakula na ya ndani nchini Gambia, Afrika Magharibi. Jarida la Jiografia, Juzuu 160, Toleo 3.
- 3 *Tini za MA 3*
- 4 *Tini za MA 31*
- 5 *Regroupment des Femmes de Popenguine pour la Protection e la Nature or RFPPN*
- 6 *Tini za MA 8*
- 7 *Tini za MA 8, 23*
- 8 Moja ya mimea hiyo ni "sharubu za paka" (Cleome gynandra L./Gynandropsis gynandra (L) Brig.) ambao umefanyiwa utafiti mwingi. (<http://www.ipgri.org/publications /pdf/350.pdf>)
- 9 *Tini za MA 44, 58.*
- 10 Nchini Kenya, vijana wanaweza kukataa kula mboga za majani kwa sababu wanadai kuwa ni chungu. Wanawake watu wazima wanasema kuna pengine hii ni kwa sababu chakula hakipikwi vizuri. (<http://www.ipgri.cgiar.org /Institute/fact-gender.htm>)
- 11 *Tini za MA 35*
- 12 *Tini za MA 58*
- 13 *Tini za MA 51*
- 14 *Tini za MA 31, 58*
- 15 *Tini za MA 3, 8*
- 16 *Tini za MA 12*
- 17 *Tini za MA 40*, mfano umewekwa kwa muhtasari kwenye makala tangulizi ya mwisho: Maarifa Asilia: Mwelekeo wa Baadaye.
- 18 *Tini za MA 45*
- 19 *Tini za 63*, haimo kwenye toleo hili: inapatikana kutoka <http://www.worldbank.org/afr/ik/iknt63.pdf>
- 20 *Tine za MA 40*
- 21 *Tini za MW 3, 31*

## 5. Mbinu za Wenyeji za Kupambana na UKIMWI Barani Afrika

*Edward C. Green*

*Edward C. Green, Mwanasayansi  
Mtafiti Mwandamizi katika Kituo cha  
Havard cha Idadi ya Watu na  
Maendeleo.*

*Tini za MA*, katika toleo hili zinaonyesha kwamba masuluhisho mengi ya matatizo ya watu masikini yamo ndani ya jamii zenyewe na watu wake. Mjadala wa mapambano dhidi ya janga la VVU/UKIMWI barani Afrika yanaonyesha kuwa masuluhisho ya wenyeji dhidi ya ueneaji wa ugonjwa huo pia yanafaa zaidi na yana ufanisi kuliko yale yanayobuniwa toka nje.

Ushahidi unazidi kuonyesha kuwa modeli ya dunia ya kuzuia UKIMWI haifai katika Afrika. Msingi wa modeli hiyo ni kupunguza hatari au kutoa “tiba” (kondomu, kutibu magonjwa yaenezwayo kwa ngono kwa dawa), badala ya kujiepusha na hatari (kuwa na mke/mume mmoja, kutofanya kabisa tendo la ndoa, au kusubirisha umri wa kuanza ngono).<sup>1</sup> Modeli ya uzuiaji iliyokitwa kwa tiba haihamasishi kupunguza idadi ya wapenzi, au hata kukemea ngono ya wenzi wengi.

VVU/UKIMWI uliojitokeza kwa mara ya kwanza barani Afrika, serikali nyingi ziliamua kutolishughulikia suala hilo. Kulikuwa na hasira kutokana na kuilaumu Afrika kama chanzo cha ugonjwa huo wa kufisha. Pia kulikuwa na woga kwamba ushahidi wa kuwepo kwa UKIMWI ungeliuma utalii na uwekezaji wa biashara za nje. Hata hivyo, angalau nchi mbili za Afrika zilipambana na UKIMWI mara moja: Uganda na Senegali. Nchi hizi mbili sasa zinatambuliwa kuwa nchi mbili za mwanzo kufanikiwa kupambana na UKIMWI katika Afrika; na ni muhimu kuziangalia kwa makini programu hizi, ambazo kwa kiasi kikubwa zilibuniwa na nchi zenyewe, na kabla mashirika ya UKIMWI ya nchi za Magharibi hayajaanza kuisaidia Afrika kupambana dhidi ya UKIMWI.

Nchi zote mbili—Uganda na Senegali—zilibuni programu za kujikinga na UKIMWI zinazosisitiza kubadili tabia,<sup>2</sup> pamoja na huduma za kupunguza hatari ya ugonjwa. Kwa maneno mengine, mbinu zilizoshughulikia UKIMWI kama suala la tabia linalohitaji ufumbuzi wa kitabia, na sio tu tatizo la kitiba linalohitaji ufumbuzi wa kitiba. Nchi zote mbili zilifanikiwa sana kupunguza ueneaji wa UKIMWI (Uganda) au kuzuia maambukizo ya UKIMWI kwa wananchi wa kawaida (Senegali). Hakuna nchi duniani inayofikia kiwango cha Uganda cha upunguzaji wa maambukizo cha asilimia 66.

Ni sahihi kusema kuwa serikali hizi za Afrika, baadaye zikisaidiwa na AZISE zake, zilitumia maarifa asilia kubuni programu sadifu. Na hili sio jambo la kushangaza. Kuathiri tabia, au kubadili ruwaza za ndani kabisa za



tabia na za kijamii, sio sawa na kuhamasisha matumizi ya dawa au chanjo.

### Modeli ya kupunguza hatari

Mfumo wa kinga dhidi ya UKIMWI ulioletwa Afrika toka nje mwishoni mwa miaka ya 1980 ulibuniwa kwa ajili ya vikundi vilivyo hatarini zaidi kuambukizwa, kama vile mabasha/mashoga wa miji mikuwa ya Marekani, mathalani San Francisco. Sehemu ya modeli ya kupunguza hatari *haikupaswa* kubadili tabia ya ngono. Ilitolewa hoja kwamba hii ilikuwa sawa na kuwahukumu watu, jambo ambalo sio la kisayansi na lingezuia ufikwaji wa wale wanaotakiwa kufikiwa na kusaidiwa. Wataalamu wa UKIMWI wakachagua mikabala ya kupunguza hatari au madhara, inayochukulia kwamba ni ngumu au haiwezi kubadilishwa, na kwamba juhudi zinafaa kuchukuliwa kupunguza matatizo yanayoletwa na tabia za hatari. Hivyo, kondomu na sindano safi (inaporuhusiwa kisheria) zilitolewa ili kupunguza maambukizo ya UKIMWI ya kupitia ngono na kuongezea mtu damu, kwa mfuatano huo. Hakukuwapo na bado hakuna kampeni yoyote ya kuzuia aina yoyote ya ngono, au udungaji wa dawa za kulevya. Wataalamu wa UKIMWI walijipongeza wenyewe kwa uwazi na uhalisia wao.

Mkabala huu pengine ungefaa kwa San Francisco, au hata Sao Paulo au Bangkok. Lakini ulipoletwa Afrika, kulikuwa na jitihada kidogo za kuirekebisha modeli iendane na mila na ruwaza za magonjwa ya Afrika, pamoja na kuwapo madai ya kinyume chake. Huko Marekani, Ulaya na sehemu kubwa ya Asia, maambukizo ya UKIMWI yamekusanyika zaidi katika vikundi vichache vya hatari kubwa kimaambukizo. Katika Afrika kusini mwa Sahara, maambukizo mengi ni dhidi ya wananchi wa kawaida. Kusema kweli, wengi wanapinga mtazamo huu, wakidai “tusibague vikundi fulani tu na kusema vimo hatarini. Kwa kufanya hivyo, tutawanya-nyapaa—kuwalaumu waathirika—na kufanya wananchi wengine wadhania hawako hatarini.” Hivyo ujumbe wetu lazima uwe, “*sote* tuko hatarini kuambukizwa UKIMWI.” Hii italeta usawa; *sote* tumo katika janga hili kwa pamoja. Hata hivyo, tofauti za ruwaza za kiepidemiolojia na za kiutamaduni ni halisi, hivyo panahitajika—pamoja na mambo mengine—mikabala tofauti ya kujikinga kutegemeana na mazingira mahususi.

### Kinga ya UKIMWI barani Afrika

Je, modeli ya kupunguza hatari imefanikiwa vipi katika Afrika? Juhudi zaidi zilielekezwa kwenye ugawaji

kondomu na uhamasishaji wa matumizi yake. Hakuna ushahidi hadi leo kwamba uhamasishaji wa kondomu umepunguza viwango vya maambukizo ya UKIMWI miongoni mwa wananchi. Utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na UKIMWI—UNAIDS -, na kuchapishwa katika toleo maalumu la *UKIMWI* mwaka 2001, ulibaini kuwa matumizi ya kondomu hayakuchangia chochote katika kuukilia ueneaji wa UKIMWI (Bure na wenzake 2001). Na tathmini ya hivi karibuni ya UNAIDS ya ufanisi wa kondomu (Hearst na Chen 2003) imehitimisha, “hakuna mifano dhahiri ya magonjwa ambayo ueneaji wake umezuiwa na programu ambazo msingi wake ni uhamasishaji wa kondomu.”

Baadhi wanadai kuwa hazitumiki kondomu za kutosha barani Afrika kuweza kuleta mabadiliko, na kwamba kondomu zingeleta nafuu kama zingepatikana kirahisi katika mabilioni badala ya makumi ya mamilioni tu yaliyopo. Pengine, lakini tunachojua kutoka kwenye data za hivi karibuni za USAID ni kwamba, baada ya zaidi ya miaka 15 ya uhamasishaji wa matumizi ya kondomu katika Afrika (fani niliyoifanyia kazi), matokeo ni wastani wa kondomu 4.6 tu zinapatikana (sio lazima kwamba zinatumiwa) kwa kila mwanamume kwa mwaka barani Afrika katika miaka ya hivi karibuni (Shelton na Johnston 2001). Idadi hiyo ilikuwa kubwa kidogo katikati ya miaka ya 1990; imeshapungua kwa kiasi fulani tangu wakati huo licha ya mfumuko wa UKIMWI Afrika ya Kusini. Tatizo yaelekea ni mahitaji madogo, na sio ugavi haba.

### Mkabala wa Uganda uliobuniwa na nchi yenyewe

Licha ya kondomu, programu nyingine ambazo ni aghali kidogo za kuzuia UKIMWI zinazofadhiliwa sasa na wahisani wakubwa ni tiba pana ya magonjwa ya ngono, ushauri nasaha wa hiyari, upimaji virusi na uzuiaji wa maambukizo ya mama kwa mtoto kupitia dawa zijulikanazo kama ‘Nevirapine.’ Kama uhamasishaji wa kondomu, haya ni masuluhisho ya kitiba, na sio uhamasishaji wa kubadili tabia. Programu hizi, pamoja na uhamasishaji wa kondomu, zilikuwa hazijaanzishwa Uganda wakati wa viwango vya maambukizo vilipoanza kupungua mwishoni mwa miaka ya 1980. Hata hivyo, Uganda ndiyo iliyopunguza maambukizo ya UKIMWI kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko nchi zote. Msingi wa mkabala wake uliobuniwa nchini ulibebwa na ujumbe katika sitiari (msemo) ya wenyeji: “malisho ndani.” Hii inamaanisha lisha wanyama wako shambani mwako; usilishe nje ya hapo (yaani, usifanye ngono nje ya ndoa au mpenzi umwaminie). Akijibu ushauri wa wataalamu wa

nje kuhusu UKIMWI, Rais Museveni alisema mwaka 1991, “kama tulivyopatiwa risasi ya kiinimacho” mwanzoni mwa miaka ya 1940, sasa tunapewa kondomu kwa ajili ya “ngono salama.” Tunaambiwa kwamba kipande chembamba tu cha mpira kimesimama kati yetu na kifo cha bara letu. Ninadhani kwamba kondomu zina dhima kama njia ya kuzuia, hasa kwa wapenzi wenye VVU, lakini haziwezi kuwa njia kuu ya kuzuia UKIMWI”.

Ndani ya kipindi cha miaka minne tu tangu programu ya kinga ya Uganda kuanza, tafiti za tabia (zilizothibitishwa na data za kibiolojia) zilianza kuonyesha kupungua kwa ngono za kizembe, ucheleweshaji wa umri wa kuanza ngono, na matumizi makubwa ya kondomu miongoni mwa wale wachache walioendekeza ngono za kizembe. Uganda pia ilikuwa ya kwanza kubuni mikabala ya kupunguza unyanyapaa, ikiweka mahali pa wazi mijadala kuhusu tabia za ngono, ikiwashirikisha waathirika wa VVU katika elimu ya umma, ikishawishi watu binafsi na wapenzi (wanandoa) kupimwa na kupatiwa ushauri nasaha, na ikiboresha hadhi ya wanawake. Busara ya programu ya Uganda ya ABC (Jinyime [Abstain], Kuwa mwaminifu [Be faithful] au Tumia Kondomu [use Condoms]) ni kwamba inalenga “viukilia vya karibu” au sababu za mara moja za maambukizo ya VVU, na pia kuhusu nini *watu binafsi* wenyewe wanaweza kufanya kubadili (au kudumisha) tabia, na hivyo kukwepa au kupunguza hatari za maambukizo. Lakini ilishughulikia pia matatizo magumu ya kijamii na kiasasi ambayo ni serikali zenye mwito tu zinaweza kuyashughulikia. Programu hizi ziliongozwa na serikali (hasa Wizara ya Afya), lakini pia zilishirikisha AZISE nyingi na asasi za jumua za kijamii.

### Masuluhisho asilia ya Senegali

Kama Uganda, Senegali ilikuwa miongoni mwa nchi za kwanza barani Afrika kukubali kuwepo kwa VVU/UKIMWI na kuanza kutekeleza programu kamambe za kuzuia na kudhibiti VVU/UKIMWI. Kulingana na Idara Kuu ya Sensa ya Marekani (BUCEN—Bureau of Census), kama Uganda, “Senegali imekuwa na mafanikio makubwa, kwani serikali imeweza kuudhibiti ugonjwa” (BUCEN 2000: 1). Kwa mujibu wa UNAIDS, Senegali kwa sasa ina kiwango cha chini kabisa cha ueneaji wa VVU katika Afrika Kusini mwa Sahara, na yaonekana kutoyumba, ikiwa na chini ya asilimia 1 au chini ya hapo ya maambukizo (BUCEN 2000).

Tathmini ya UNAIDS ya mapambano ya Senegali dhidi ya UKIMWI (Sittitrai 2001:9) inabainisha mambo muhimu yafuatayo:

- Kama nchini Uganda, wanasisia nchini Senegali walishughulikia haraka ugonjwa mara tu ulipozuka katika nusu ya pili ya miaka ya 1980.
- Kwa vile asilimia 93 ya WaSenegali ni Waislamu, serikali ilifanya juhudi za kuwashirikisha viongozi wa dini; VVU/UKIMWI ukawa mada ya kawaida kwenye sala za Ijumaa misikitini, na viongozi waandamizi wa dini waliuzungumzia katika televisheni na redio.
- Ngazi nyingine za jamii za WaSenegali zilijiunga kwenye kampeni. Kufikia mwaka 1995, AZISE 200 zilikuwa katika harakati za mapambano, na pia vikundi vya wanawake vyenye takribani wanachama nusu milioni.
- Uzuiaji wa VVU uliingizwa kwenye mitaala wakati elimu ya ngono ilipoanza kufundishwa shuleni. Juhudi sambamba na hizi zilifikishwa kwa vijana walio nje ya shule (Sttitrai 2001:9).

Tena, kama nchini Uganda, tunabaini mabadiliko ya msingi ya tabia huko Senegali, yaani upunguzaji wa wenzi na ongezeko la umri wa kuanza ngono. Kulingana na tovuti ya DHS,<sup>3</sup> umri wa kati wa kuanza ngono umepanda zaidi kuliko katika nchi yoyote ya Afrika yenye data za DHS, kuanzia 16.6 hadi 17.4. Na mwandishi wa UNAIDS anasema yafuatayo kutokana na tathmini ya data za kidemografia na kitabia:

Wanawake wa KiSenegali wenye umri wa mwanzoni mwa miaka 20 hawakufanya ngono hadi walipokuwa takribani na miaka 19 au zaidi. Kwa kizazi cha mama zao—wanawake waliokuwa na umri w kati ya miaka 40 na 49 mwana 1977—umri wao wa kati ulikaribia miaka 16 (Sttitrai 2001:11).

Utafiti wa mwaka 2001 wa wanawake ambao hawajawahi kuolewa jijini Dakar wa umri wa miaka 15-23 ulifanywa na Shirika la Kimataifa la Afya ya Familia, (Family Health International—FHI), kwa ufadhili wa USAID na CDC, kupitia Wizara ya Afya ya Senegali. Wanawake 29 tu kutoka sampuli ya majaribio ya wanawake 699 walisema kuwa tayari wamefanya ngono. Hii inamaanisha kwamba asilimia 95.6 walijichelewesha kufanya ngono; asilimia 4.1 tu ndio walikuwa wakifanya ngono (Hyggea/FHI 2001:31). Hii inawakilisha idadi ndogo sana ya wasichana na vijana wa kike wanaofanya ngono mapema, kwa viwango vya nchi yoyote, hasa kwa vile takribani asilimia 11 ya sampuli imo kwenye kundi la umri wa miaka 20-23. Idadi kubwa zaidi (asilimia 55) ya vijana wa kike 29 wa utafiti wa FHI walioripoti kuwa na *idadi fulani* ya wenzi mwaka 2001, walisema kwamba wamekuwa na mwenzi mmoja (Hyggea/FHI 2001:35).

Kama Uganda, Senegali ilipata msaada wa mashirika ya kidini katika uzuiaji wa UKIMWI, ilianza elimu ya

UKIMWI katika shule za msingi, na kwa makusudi ilitumia mbinu za kuibua hofu kama mkakati wa kuzuia maambukizo. Hii haifanani na modeli ya Magharibi ya kupambana na UKIMWI. Yaliyotokea nchini Uganda na Senegali ni mbinu asilia za Kiafrika za kupambana na UKIMWI. Na zinaafikiwa.

### **Mkabala wa Kiafrika ulifanikiwa zaidi**

Kuhusu hatua za kuingilia kati, kuna ufanano kati ya nchi mbili za Afrika zilizofanikiwa, kuanzia na ukweli kwamba programu zote mbili zilikuwa kwa kiwango kikubwa za kiasili. Kusema kweli, Senegali inaonekana ilikuwa jasiri kupita Uganda katika kuyaeleza mashirika ya ufadhili makubwa kwamba, ingawa ufadhili wa ulihitajika, wasithubutu kuwaambia Waafrika jinsi gani inafaa zaidi kuzuia UKIMWI. Kulingana na tafiti za kidemografia na kiafya, Senegali na Uganda ndizo nchi pekee miongoni mwa nchi za Afrika ambamo idadi kubwa zaidi ya wananchi wake wanasema kuwa walijifunza kuhusu UKIMWI kutokana na makusano ya uso—kwa—uso, na sio kutoka kwenye redio, machapisho, au wafanyakazi rasmi wa sekta ya afya. Senegali inajidhihirisha kuwa ni nchi ambamo wanawake hujihisi kuwa hatarini kupata UKIMWI (ingawa ueneaji wa VVU ni wa chini kabisa katika Afrika kusini mwa Sahara, takribani asilimia 0.50), na Uganda inajidhihirisha kuwa ni nchi ambamo wanawake hujihisi kuwa wanaweza kukataa ngono wasizozitaka au kusisitiza matumizi ya kondomu.

Nchi hizi mbili pia ziliwahamasisha viongozi wa kidini na waganga wake wa jadi kushiriki katika kupambana na UKIMWI mara tu ulipoingia nchini mwao. AZISE dhidi ya UKIMWI ya waganga wa jadi na wa kisasa ya Uganda iitwayo THETA (Traditional Healers and Modern Practitioners Together Against AIDS) hukuza ushirikiano kati ya waganga wa jadi na madaktari wa kisasa katika mapambano dhidi ya UKIMWI.<sup>4</sup> AZISE hii ilibuni modeli shirikishi ya uzuiaji na tiba ya UKIMWI, ikishirikisha maarifa ya maelfu ya waganga w jadi nchini Uganda. AZISE ya Afrika nzima—PROMETRA -, yenye makao yake makuu nchini Senegali, inaratibu programu za UKIMWI zinazowashirikisha waganga wa Kiafrika barani kote.<sup>5</sup>

Serikali za Uganda na Senegali zilitambua nguvu zake zilikuwa wapi wakati wa kuhawilisha ujumbe unaofaa kiutamaduni kwenda kwa wananchi wengi wa kawaida. Kwa kiwango kikubwa nguvu hizo zilitoka kwa viongozi wa jumua. Katika zoezi la Benki ya Dunia la mwaka 1998, mwandishi wa sura hii aliweza kukadiria kwamba kati ya

makasisi wa Uganda 4, 500 na 6,750 walipatiwa mafunzo kila mwaka ya kuzuia UKIMWI kwenye ngazi za wilaya kati ya 1995-1998. Aidha theluthi moja ya wilaya za Uganda iliwapatia mafunzo waganga wa jadi, ikimaanisha kuwa zaidi ya waganga 1,800 walipatiwa mafunzo kila mwaka kwa miaka minne. Bila shaka, msingi wa makadirio haya ni rekodi zilizoko katika maandiko. Hata kama namba hizi zimeongezwa kidogo, bado hii inaonyesha kuwa ni idadi kubwa zaidi ya waganga wa jadi wanaoshiriki kuzuia UKIMWI kuliko katika nchi yoyote barani Afrika. THETA, AZISE ya Uganda, ilikuwa modeli ya kuwapatia mafunzo waganga wa jadi.

Kwa kifupi, nchi mbili za Kiafrika zilitumia utamaduni wake, pamoja na kile kilichokuwa maarifa ya kawaida kwao, na zinaendelea kufanya kile kilichohitajika kuzuia kwa ufanisi UKIMWI. Na zilifanya hivyo kwa kiwango kikubwa zenyewe, pasi na usaidizi toka nje. Jambo la kusikitisha ni kwamba nchi nyingi za Kiafrika zilichukua hatua kidogo tu au hazikuchukua kabisa hatua yoyote mpaka walipofika wataalamu wenye nia safi, na kutokana na hali hiyo, nchi nyingi zaidi za Kiafrika zina programu za UKIMWI zinazoelekea kuakisi mtazamo wa nje wa nini kifanyike. Tukitaka kuwa wakweli kabisa, ni vigumu kuhitimisha kuwa programu za kuzuia VVU/UKIMWI zimefanikiwa sehemu nyingine, kwa vile viwango vya maambukizo ya VVU vinaelekea kuongezeka (tena) miongoni mwa vikundi muhimu vya Marekani na Ulaya (k.m. Gross 2003; MAP 2000).

### **Kutoa nafasi zaidi za kuchagua**

Imekuwa vigumu kwa mashirika ya wafadhili na ya washauri yanayoshughulikia uzuiaji wa UKIMWI kuku-bali ushahidi unaonyesha kwamba kile walichokuwa wakikifanya pengine hakikuwa na manufaa makubwa barani Afrika; wakati huohuo programu ambayo hawakuiunga mkono moja kwa moja imefanikiwa vizuri zaidi. Baadhi wamepuuza mkabala wa ABC kuwa ni sahili mno na finyu. Lakini, mkabala wa ABC unaongeza kipengele cha kubadili tabia ya msingi (A na B ya ABC) kwenye programu zinazopendelewa na wafadhili, programu ambazo kwa kiwango kikubwa haziendi mbele ya "C", mbele ya kondomu na D- ya tiba kwa dawa. Kwa hiyo uongezaji wa mabadiliko ya msingi ya tabia huwapatia watu nafasi zaidi za kuzuia maambukizo ya VVU kuliko zile zilizopo sasa katika programu nyingi. Na hizi ni nafasi za uchaguzi zilizo endelevu ambazo hazitegemei dawa za gharama kubwa kutoka nchi za nje.

## Matunzo, msaada na tiba

Licha ya kinga, yapo masuala mengine yanayohusu matunzo, msaada na tiba kwa watu waishio na VVU/UKIMWI na familia zao. Suala la tiba linalotawala sasa majadiliano ya dunia linahusu dawa za kurefusha maisha ya waathirika (ARV) na jinsi ya kupunguza bei zake ili kuwawezesha watu masikini kumudu kuzinunua na kuzitumia. Bila shaka, dawa nzuri (hata kama ni ya gharama) lazima ipatikane kwa wale wanaohitaji sana, hata kama ni maskini au hawafikiki kirahisi. Lakini ni lazima itambulike kuwa itachukua angalau miaka kadhaa kutatua matatizo yote yanayohusu utoaji wa ARV unaozingatia usawa barani Afrika. Wakati huohuo yapo matunzo ya gharama nafuu yanayotolewa nyumbani na programu za misaada zinazoendeshwa sasa katika Afrika ambazo zinaweza kupata misaada kutoka kwa wafadhili wa nje. Kikundi cha kupambana na UKIMWI cha Tanga (TWWG) ni mfano mzuri wa programu ya gharama nafuu na endelevu ambayo msingi wake ni maarifa asilia<sup>6</sup>.

“Kazi ya TAWG ni mfano bora wa namna ya kupata mafanikio mazuri katika mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuunganisha kwa dhati ujuzi wa wenyeji, maarifa asilia, na wafanyakazi wa afya ya sasa ili kutoa tiba nzuri na yenye gharama nafuu kwa watu waishio na VVU/UKIMWI.”<sup>7</sup>

TAWG nchini Tanzania na THETA nchini Uganda ni programu za kijumuia zinazotoa dawa za mitishamba ili kutibu magonjwa dowezi ya VVU/UKIMWI. Zaidi ya ushahidi wa simulizi, zipo data za majaribio ya hospitalini ( ambayo daima ni magumu kugharamiwa kwa vile yanajumuisha bidhaa asilia zisizo na hataza) zinazoonyesha kwamba baadhi ya dawa hizi zinafaa. Kwa mfano, majaribio ya hospitalini yamethibitisha ufanisi wa mojawapo ya dawa za mitishamba za THETA kwa ajili ya Mkanda wa Jeshi na kuhara kunakohusiana na UKIMWI (Homsy na wenzake 1999). Kutokana na bei na matatizo ya upatikanaji, inaelekea kuwa Waafrika wengi zaidi watategemea dawa za mitishamba au tiba asilia kwa kutibu maambukizo yanayohusiana na UKIMWI. Tasnia ya ufamasia imeanza kutambua thamani ya mikabala ya tiba inayotumia mitishamba kwa kuanza na utafiti kuhusu dawa zinazotokana na mimea asilia ambazo zinatumiwa sasa na waganga wa jadi na /au wananchi wenyeji kwa ujumla wao.<sup>8</sup> Na Benki ya Dunia imetambua thamani ya maendeleo ya kiuchumi ya kuhifadhi mimea ya dawa katika mazingira yake ya asili au kuizalisha kibiashara katika mazingira unde.<sup>9</sup>

“Kutokana na dhima kubwa ya kiutamaduni ya waganga wa jadi katika jumuiia, wanatoa matumaini bora ya kutibu na kupunguza ueneaji wa UKIMWI. Lakini waganga wanategemea miti ya dawa na kumekuwepo na kupungua kwa kasi kwa spishi nyingi muhimu za miti ya dawa kutokana na huharibiwa kwa mazingira yao ya asili kwa sababu ya ukataji miti ovyo, ulimaji , uchungaji wa kupita kiasi uhomaji mioto, ukame na upanukaji wa jangwa n.k.”<sup>10</sup>

Baadhi ya programu za kijumuia za kuwahudumia waathirika wa UKIMWI hutoa taarifa na ushauri kuhusu lishe bora, maswala ya kisaikolojia na kiimani, ushiriki katika vikundi vya kusaidiana, ukwepaji wa mafadhaiko, ukuzaji wa afya ya mfumo wa kinga wa kawaida, uachaji wa kuvuta sigara na kunywa pombe, ujenzi wa matumaini, na mengineyo kama hayo. Tukichukua tu dhima ya lishe bora. Imedhihirishwa kwamba mshindilio wa VVU kwenye njia ya ginitalia husababishwa na ukosefu wa vitamini A (Mostad na wenzake 1997), hivyo kupatikana kwa wingi kwa vitamini hii peke yake kunaweza kuwa na dhima ya kuzuia na pia tiba kwa VVU. Na vitamini A inaweza kupatikana toka kwenye matunda na mbogamboga zinazolimwa katika jumuiia husika. Kusema kweli, programu bora za jumuiia hazitegemei teknolojia, bidhaa na mawazo toka nje.

“Serikali ya Ethiopia, kwa msaada wa Benki ya Dunia, hivi karibuni itaanza kutekeleza mradi wa kwanza wa uhifadhi na utumiaji endelevu wa mimea ya dawa katika Afrika Kusini mwa Sahara. Lengo kuu la mradi ni kuwezesha uhifadhi, usimamiaji na utumiaji endelevu wa mimea ya dawa kwa ajili ya matunzo ya afya ya binadamu na mifugo.”<sup>11</sup>

Programu za kijumuia zinazohusu UKIMWI zinaweza kuleta matumaini kwa wale walio na VVU au wanaoshuku kuwa wanavyo. Ujumbe wa programu hizi ni kuwa waathirika wanaweza kuishi maisha marefu zaidi, maisha yenye faida zaidi kama hatua kadhaa za matunzo binafsi zitachukuliwa. Mkabala na ujumbe huu vinakinzana na imani iliyoenea Afrika kwamba UKIMWI ni kama hukumu ya kifo. Vinakinzana na hofu, unyanyapaa wa kijamii na mawazo ya kukata tamaa. Hofu na unyanyapaa huwafanya waishio na VVU/UKIMWI kuficha hali yao (na kwa hiyo kutopima VVU), kukata tamaa, kudhoofisha zaidi mfumo wao wa kinga ya mwili na bila shaka kutoshiriki katika elimu ya UKIMWI kama ilivyotokea nchini Uganda.

Wapo baadhi ya watu wanaodai kuwa programu zinazotegemea mitishamba na rasilimali asilia zinaakisi tu “matunzo ya afya ya kikauleni,” kukiwa na “dawa za daraja la pili kwa ajili ya umma wa vijijini” huku dawa nzuri za kisasa zimehifadhiwa kwa ajili ya nchi tajiri na wakazi wa mijini wenye uwezo kifedha. Kwa muda mrefu hii imekuwa moja ya hoja zinazotumiwa dhidi ya ushirikiano wa aina yoyote kati ya madaktari wa kisasa na waganga wa jadi katika Afrika (taz. Green 1994). Naam, kwa nini dawa ghali zisikazaniwe pia kwa masikini? Jibu la swali hili, bila shaka, ni tukazanie kupata dawa bora kwa watu masikini, *endapo* tutapata njia ya kuzilipia. Lakini zingatia kuwa ARV ni ghali sana, hata zile za kawaida, na tunazungumzia kuhusu kuzitoa mwa nchi ambazo hutumia chini ya dola za Marekani 10 kwa mwaka kwa mtu mmoja kwa afya yake yote, kutoka kuzaliwa hadi kifo. Zaidi ya hayo, hatupaswi kudharau dawa za kienyeji na tiba za kienyeji bila kuwa na ushahidi thabiti unaohusu ufanisi wake.

Hapana shaka kwamba litakuwa ni jambo la hiyari kutafuta njia za kulipia dawa za ARV, kuzigawa kwa usawa, na kuzisaidia programu za kujitegemea za kijumuia zinazotegemea maarifa, teknolojia na miundo asilia. Mengi ya mashirika ya wafadhili yanaonekana kuzingatia tu ulipiaji na ugawaji wa dawa za ARV. Programu ya Benki ya Dunia ya Maarifa Asilia kwa ajili ya Maendeleo haifuati msimamo huo, na kwa hiyo ina mambo kadhaa ya kutoa kuhusu masuala mengi muhimu yanayohitajika, zaidi ya dawa za ARV. Hata wakati dawa za ARV zitakapokuwa zinapatikana kwa wingi, bado

kutakuwepo na mahitaji ya programu endelevu ya kijumuia za matunzo, msaada na tiba, zinazotegemea dawa asilia, tiba asilia, vyama vya wenyeji na mifumo yenye taratibu nzuri zaidi za kugharamia huduma za afya.

“Katika nchi nyingi zinazoendelea, ufinyu wa mipango ya sasa ya ugharamiaji wa huduma za afya, unaojidhihirisha wazi kutokana na kuzidi kupungua kwa bajeti na kuibuka kwa mipango mingi ya uchangiaji wa gharama, umesababisha kutafuta mikabala ya ziada na mbadala ya kuboresha hali ya upatikanaji wa fedha za kulipia gharama. Miongoni mwa mikabala iliyopendekezwa ni taratibu za kuchangia hatari zinazojumuisha mipango ya kijumuia inayojengeka kwa mifumo asilia ya kijamii.”<sup>12</sup>

- 1 Utenganishaji huu si kamili kwa sababu upunguzaji wa idadi ya wenzi katika ngono ungeweza kubainishwa na upunguzaji wa hatari na si ukwepaji.
- 2 John Richens alipendekeza istilahi mabadiliko ya msingi ya tabia ili kueleza mabadiliko ya msingi katika tabia za ngono, kama vile upunguzaji wa idadi ya wenzi, au kuacha ambavyo vyote havitegemei vitu au dawa.
- 3 <http://www.measuredhs.com/>
- 4 *Tini za MA 26, 54*
- 5 *Tini za MA 26*
- 6 *Tini za MA 51*
- 7 kama iliyotangulia
- 8 *Tini za MA 15*
- 9 *Tini za MA 35*
- 10 *Tini za MA 30*
- 11 *Tini za MA 35*; mradi tayari umeanza na sasa hivi uko katikati
- 12 *Tini za MA 48*

## 6. Kilimo Endelevu na Njia za Kujitafutia Maisha Vijijini: Ubunifu wa Maarifa Asilia Katika Maendeleo

*John Aluma*

*John Aluma, ni Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Asasi ya Taifa ya Utafiti wa Kilimo (NARO) nchini Uganda*

Bila shaka shughuli nyingi zaidi zinazofanywa na wenyeji duniani kote zinahusiana na kilimo. Wakulima na wafugaji walipanda mazao na kufuga wanyama katika maeneo ya unyevu, makame au ya joto wastani, wakijenga mifumo ya uzalishaji iliyotangamana vyema na maeneo hayo na ambayo hatimaye ilikuwa hatua kwa hatua kulingana na hali ya mabadiliko ya mazingira. Mifumo mingi ya aina hii ilidumu kwa kujiegemeza katika himaya za uwekezaji—uvunaji duni. Matumizi ya mashine, mbolea na dawa za kilimo yamebadili baadhi ya mifumo hii na kuifanya kuwa mifumo ya uwekezaji—uvunaji mkubwa, mifumo ambayo kwa kiasi kikubwa kudumishika kwake hutegemea msaada kutoka nje.<sup>1</sup> Hata hivyo idadi kubwa ya mifumo hii ya uwekezaji mkubwa ama haikuweza kudumishika au ilishindwa kutoa mavuno makubwa kama ilivyokuwa imetarajiwa.

Wakati ambapo mara nyingi mazingira ya kisiasa<sup>2</sup> ndiyo yaliyokuwa kikwazo kwa mzalishaji wa mazao cha kuingia katika mifumo hii mipya, hasa kutokana na ama vikwazo vya masoko au haki ya kutumia ardhi, kikwazo kingine bayana kilikuwa uhawilishaji mbovu wa teknolojia. Mifano ni pamoja na (a) matumizi ya aina chache za mbegu katika mazingira ya aina tofautitofauti (b) matumizi ya ulimaji unaotumika katika maeneo ya joto la wastani ambao unapotumika katika maeneo ya unyevu au ya kitropiki husababisha upotevu wa mbolea asilia na mmomonyoko wa udongo (c) mimea na bridi za wanyama zilizoshambuliwa na magonjwa na wadudu na ambazo hazikuwa na kinga au ustahimilivu.

Uasirishaji wa kilimo na mabadiliko mengine ya matumizi ya ardhi pia vimesababisha upungufu wa mabadiliko ya kijeni. Watafiti na wazalishaji wanakabiliana na tatizo hili kwa kuanzisha tena spishi asilia katika kapu la jeni za mazao wanayolima na la mifugo. Wakati ambapo juhudi za kufanikisha jambo hili zinaimarika, kiasi cha fedha kilichoko kwa ajili ya utafiti ni kidogo, kwa vile, kwa jumla hakuna rasilimali za utafiti wa kilimo kwa ajili ya uma.<sup>3</sup> Hata hivyo idadi inayoongezeka ya asasi za taifa za utafiti wa kilimo katika nchi zinazoendelea hujishughulisha na utafiti, maendeleo, na uingizaji wa uzalishaji unaotokana na maarifa asilia katika biashara, hususan uzalishaji wa mazao ya mimea yanayoweza kutumika katika dawa, tibalishe na viwandani.<sup>4</sup>

Bila shaka manufaa ya kilimo cha kisasa na yale ya mapinduzi ya kilimo hayana mjadala—na kama yasingekuwapo, basi ingekuwa vigumu kuwapatia lishe watu zaidi ya bilioni sita walioko duniani. Hata hivyo ushahidi unaonyesha kwamba unapotokea upungufu mkubwa wa vyakula vikuu, jumuiya nyingi katika Afrika, hurejea katika mazao ya asili kama njia ya kujihami. Mazao hayo ya asili kwa kiasi kikubwa hayajafanyiwa utafiti kama ule unaofanyiwa mazao makuu. Tabia hii inaashiria jambo muhimu ambalo limesahaulika na ambalo linastahili kufanyiwa utafiti. Jambo hilo ni ubainishaji wa mbinu za kujikimu zinazotumiwa na jumuiya mbalimbali katika kukabiliana na changamoto za namna ya kujipatia maisha. Kwa mujibu wa jambo hili, yanaibuka maswali makuu matatu:

- Ni kwa vipi maarifa, utendaji na ubunifu asilia vimeimarisha njia za kujipatia maisha katika hali endelevu kiikolojia, toshelevu kiuchumi na kubalifu kijamii, na hasahasa, MA yamechangia je katika mambo matatu yaliyo muhimu sana kwa upande wa uhakika, uwepo, upatikanaji na utumiaji wa chakula?
- Ni nani wenye usukani katika ubunifu au utumiaji wa MA
- Ni mazingira gani yanayowaendeleza au yanayowakwaza wenye usukani hao katika juhudi zao au ambayo ni changamoto kwa upanuzi wa mafanikio yaliyopatikana?

*Tini za MA zilizomo katika andiko hili zinatoa mfano wa mikabala ya wenyeji ambayo inaweza kutoa majibu kadhaa ya maswali haya. Inaonekana kuwa kanuni msingi ya utendaji asilia katika kukabiliana na changamoto za maisha ya vijijini ipo katika matumizi ya mkabala jumuishi uliovuka mipaka ya 'utaalamu pekee'. Kwa upande wake mkabala wa kijumuiya kwa jumla unahusiana na namna ya kushughulikia maswala ya umaskini, chakula cha kaya na uhakika wa lishe, afya, kilimo endelevu, ajira nje ya kilimo, ushirikishwaji, uendelezaji wa rasilimali za kijamii na nguvukazi, utumiaji wa asasi na mitandao ya kijamii.*

### **Ufufuaji wa shughuli asilia kwa ajili ya kuinua hali ya maisha katika Mali**

Mradi wa mmea wa Mjatrofa Kakasi<sup>5</sup> huko Mali unaendeleza uzalishaji na usindikaji wa Jatrofa (Njugu za familia ya Ufobiasea). Upandaji wa mmea huu husaidia kudhibiti mmomonyoko na kuboresha udongo katika mazingira ya ardhi kame ya kijangwajangwa. Kusindika (kuondoa mbegu) Jatrofa husaidia kuinua kipato (hasa kwa kina mama) na kuchangia katika uondoshaji wa

umaskini. Mjatrofa, ambao asili yake ni huko Amerika Kusini, kwa mara ya kwanza ulipandwa kwa ajili ya kutengeneza mafuta ya kulainishia. Mmea huu huvumilia ukame na ni wa kudumu na huweza kutumika kama uzio wa asili. Uzio wa Mjatrofa huzuia wanyama wasile mazao na kuharibu mashamba na hivyo hupunguza mmomonyoko wa udongo. Aidha uzio husaidia kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji kwa vile huzuia wanyama wasiingie katika mashamba na kuharibu mazao.<sup>6</sup> Ufufuaji wa shughuli asilia uliofanywa na wanawake ambao huvuna mbegu za Mjatrofa kwa ajili ya kutengeneza dawa na sabuni umewezeshwa uanzishwaji wa kiwanda chenye faida cha sabuni kinachosimamiwa na kinamama na ambacho husaidia katika kupunguza umaskini. Machicha yanayobakia baada ya kukamua mafuta ni aina nzuri ya mboji. Mafuta ya Mjatrofa pia hutumika kama dizeli ya kuendeshea mitambo midogomidogo ya mashine za kusaga nafaka na pampu za maji.

Awali, kilimo cha Mjatrofa kiligharamiwa kwa msaada kutoka Shirika la Misaada ya Kifundi la Ujerumani (GTZ) chini ya mpango wa nishati rudifu, lakini baada ya kujifunza kwa jamii mradi huo sasa umepanuka na kuingia katika mpango mpana wa maendeleo ya kilimo, udhibiti wa mazingira, uongezaji kipato, na mshikamano wa kijamii. Wahusika walijifunza mambo yafuatayo:

Mkabala huo uliotumika:

- Hujengeka katika desturi za manufaa za Maarifa asilia ya wenyeji
- Hudhihirisha matumizi mbalimbali ya mazao (mmea, mafuta ya mbegu, uzuiaji wa mmomonyoko, upangaji wa mali)
- Hujishughulisha na maswala yenye umuhimu kwa jamii kwa wakati husika
- Huhimiza uhusishwaji wa wanawake katika kubuni miradi ya kiuchumi na huendeleza viwanda vidogovidogo
- Huoanisha udumishikaji wa kiikolojia na maendeleo ya kilimo.
- Huhimiza matumizi ya malighafi za asili.

Wakati ambapo sio jambo la kawaida kuwa na mmea wenye matumizi mengi kiasi hicho,<sup>7</sup> matumizi ya Mjatrofa yamekuwa na manufaa makubwa katika kuinua kipato cha jamii husika: matumizi hayo yamekuwa chanzo cha kipato kwa wanawake na yamesaidia kuiwezesha jamii kiuchumi.

### **Kujenga ubunifu wa wenyeji**

Katika mwaka 1999 Huko Hondurasi Chama cha Washauri wa maswala ya Kilimo Endelevu, cha Kiikolojia

Ubunifu wa wakulima katika teknolojia asilia katika Hondurasi (1999)	
Kategoria ya teknolojia	Kategoria ya teknolojia
Udhibiti wa wadudu	15
Urutubishaji	10
Udhibiti wa magonjwa ya mimea	8
Udhibiti wa magugu	2
Utayarishaji wa chakula	2
Ufugaji wa wanyama	2
Uzalishaji wa mimea	1
Kutumia mboji	1
Uhifadhi wa udongo	1
Mengine	3
Jumla	45

na chenze kulenga mahitaji watu, (COSECHA) kiliamua kufanya utafiti juu ya ubunifu mbalimbali wa wakulima. Hatimaye kiliweza kuorodhesha aina 82 za teknolojia zilizobuniwa na wakulima 52.<sup>8</sup> Zile ambazo zimeainishwa kuwa zinahitaji utafiti zaidi na usambazaji zimeonyeshwa katika jedwali lililopo hapo chini.

Idadi inaashiria vikwazo halisi vya msingi vya kibiofizikia vinavyowakabili wakulima wadogo wa nchi zinazoendelea: wadudu, magonjwa na magugu. Hivyo shughuli za udhibiti zimechangia zaidi ya nusu ya idadi ya ubunifu. Utafiti huo ulionyesha pia kuwa hapakuwa na ubunifu uliohusu maeneo ambayo kwa watafiti na wanasayansi yangeonekana kuwa ya muhimu mkubwa kama vile uvunaji wa maji na utunzaji wa mazao ya miti. Utafiti ulihitimisha kuwa wakulima hawakuonyesha juhudi zozote katika ubunifu wa teknolojia ambayo waliona kuwa hawana uwezo wa kuitumia (uvunaji wa maji ya mvua) au teknolojia ambayo matunda yake yangechukua muda mrefu kupatikana (utunzaji wa miti).

#### Kuwasaidia wakulima wafanyao majaribio na kuwekeza

Serikali ya Jimbo la Uta Pradesh huko Kaskazini mwa India iliingiza swala la maarifa asilia katika Mradi wa Benki ya Dunia wa Uondoshaji Magadi katika Ardhi. Mradi huo ambao ulianza mwaka 1993 umewasaidia

wakulima kuondosha magadi katika zaidi ya hekta 68,000 za ardhi yenye magadi.<sup>9</sup> Katika maeneo ya utekelezaji wa mradi wakulima wa Uta Pradesh waliunda kamati za utekelezaji na vikundi vya kujitegemea ambavyo vilifanya kazi kwa kushirikiana na mameneja wa mradi na asasi zisizo za kiserikali kwa lengo la kutumia maarifa ya wenyeji na kujenga ubunifu kazini ili kujenga mikakati inayotokana na inayokubaliwa na wenyeji. Mradi uliimarisha asasi za wenyeji, uliwanufaisha na kuwajengea mfano ufaao kwa uenezaji wa shughuli zao kwa kamati husika.

Mbinu za kisasa kama vile matumizi ya mbolea za kemikali, dawa za kulia wadudu na teknolojia mpya ya kilimo ambazo hutumiwa na serikali ziliunganishwa na teknolojia asilia ziliyogunduliwa na wakulima, kama vile matumizi ya jasi katika ufufuaji wa ardhi, ujenzi wa vizuizi vya mmomonyoko, kuchuja udongo, kilimo mchanganyiko, kutumia mboji, ubadilishaji mazao, mbolea za asili na utifuaji wa ardhi. Mbinu hizi asilia hazikuhitaji gharama kubwa na hazikuwa na madhara kwa mazingira.

Matokeo ya mbinu hizo ni kuwa wakulima wameweza kufufua ardhi kwa matumizi ya familia 247,000, upandaji wa mazao umeongezeka kutoka asilimia 37 hadi asilimia 200, mavuno na kipato cha wakulima vimeongezeka kwa asilimia 60 katika kipindi cha miaka mitano, na ubora wa ardhi umeongezeka mara nne. Matokeo fiche ni pamoja na kuingiza kipato kwa vikundi vya kujitegemea vya

Masuala ya usalama wa chakula	Dhima/mchango unaoweza kutokana na MA
Uwepo	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uzalishaji bora/endelevu Uwepo<sup>11</sup></li> <li>Teknolojia<sup>12</sup></li> <li>Njia nzuri zaidi za kuhifadhi mazao na kupunguza upotevu<sup>13</sup></li> </ul>
Upatikanaji	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uthabiti wa uzalishaji (uzalishaji usio na madhara kiikolojia)<sup>14</sup></li> <li>Masoko, huduma, taarifa, haki, hadhi za kijamii<sup>15</sup></li> <li>Uwezo wa kununua<sup>16</sup></li> </ul>
Utumiaji	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ulaji<sup>17</sup></li> <li>Usafi wa mwili, maji, usafi wa mazingira, usalama wa chakula, ubora<sup>18</sup></li> <li>Uleaji wa watoto, desturi za ulishaji, utayarishaji, mienendo, ugawanyaji wa chakula katika kaya<sup>19</sup></li> </ul>
Masharti ya kiunzi	<ul style="list-style-type: none"> <li>Utafiti<sup>20</sup></li> <li>Kujitayarisha kwa ajili ya dharura ya chakula<sup>21</sup></li> <li>Afya ya mwili ya walaji na wazalishaji<sup>22</sup></li> </ul>



kinamama kwa njia ya shughuli mbalimbali kama vile ufungaji wa kuku na bustani za mboga, na mishahara ya vibarua imepanda mara mbili kutokana na ongezeko la shughuli za uzalishaji katika eneo husika. Matokeo muhimu sana ya kuzipa mbinu hizo nafasi na kuzitilia mkazo hutoka katika shule za wakulima, ambako wakulima wenyewe hufundisha na kubuni mitaala kwa kushirikiana na wakufunzi kwa lengo la kudumisha na kuendeleza zaidi ubunifu wa maarifa asilia.

### Maendeleo vijijini, uhakika wa chakula na maarifa asilia

Mifano hii na mingine iliyotolewa katika *Tini za MA*<sup>10</sup> kuhusu kilimo, uhakika wa chakula na maendeleo vijijini inajibu mswali matatu yaliyoulizwa mwanzoni mwa makala hii: mchango wa MA katika uhakika wa chakula na kipato cha vijijini, vichocheo vya mchakato wa uvumbuzi vijijini na masharti ya uwezeshaji. Mchango ambao hutokana na maarifa asilia na ubunifu wa wakulima katika mazingira ya uhakika wa chakula ni mkubwa. Jedwali hapo chini linaonyesha mambo muhimu yanayohusu chakula cha uhakika—uwepo, upatikanaji na utumiaji—pamoja na vikorombwezo vyake ambavyo vina-weza kunufaishwa na mchango wa MA.


Majadiliano ya *Tini za MA* kuhusu kilimo na uhakika wa chakula—au shughuli za kuendesha maisha vijijini kwa jumla—zinaonyesha kuwa msukumo wa msingi kwa mabadiliko ya wenyeji ni kudhoofika kwa misingi ya rasilimali asilia (kutoweka kwa makazi asilia, kutoweka kwa misitu, na kuchakaa kwa udongo), kushuka kwa uzalishaji wa kilimo, kupuuzwa kwa mbinu za wenyeji za kilimo, na migogoro juu ya upatikanaji na utumiaji wa rasilimali asilia. Uendeleu wa kiikolojia wa mbinu zilizoborehwa umekuwa msingi wa aina nyingi za uvumbuzi.

Wakati ambapo mifano iliyotolewa haisadifu tathmini ya matokeo ya muda mrefu ya MA katika upatikanaji shughuli za kuendesha maisha, matokeo ya muda mfupi na ya kati ni dhahiri katika mifano yote. Washika usukani wa ubunifu na mabadiliko kwa kiasi kikubwa ni watu binafsi, aghalabu wakijishughulisha wao

wenyewe au kama sehemu ya vikundi (wanawake, vijana, wakulima, washiriki wa kisomo chenye manufaa, nk.) vilivyoanzishwa kutokana na misukumo na malengo ya pamoja na wala sio kwa taratibu tu za kiserikali. Kwa kiasi kikubwa ‘wabunifu hawa wameshapitia ‘maarifa ya dunia’ kiasi kwamba wao pia wangependa kuona maarifa na uzoefu vilivyomo kwenye mazingira yao na kubaini uwezekano wa kuleta mabadiliko kutokana na wenyeji. Utambuzi huu ni muhimu kwa ajili ya majukumu ya mawakala wa nje, kama vile wafadhili, watafiti wa kilimo na wa ugani pamoja na wahusika wengine wa maswala ya vijijini yenye lengo la kuvisaidia vijiji katika kuboresha shughuli za kuendesha maisha ya watu wake. Wakati ambapo asasi hizi zimebadili majukumu yao ya kuwa wasambazaji wa maazimio ya serikali hadi kuwa wabia wa jumuiya, bado kwa kiasi kikubwa hazijajipa jukumu la kuelewa au la kutathmini maarifa asilia.

Mazingira ambayo ni mazuri kwa ukadiriaji na ukuzaji wa matumizi ya maarifa asilia sio tu kwamba

### Uingizaji wa MA katika matriksi ya NARO



yanawezesha asasi kutumia MA kwa njia inayofaa na ya ufanisi zaidi, bali pia huionyesha jamii kwamba michango yao katika sayansi na teknolojia ina thamani na bila shaka kuchochea zaidi udadisi wa kibunifu. Kwa mfano, Shirika la Taifa la Utafiti wa Kilimo (NARO) nchini Uganda hivi karibuni limebuni mkabala wa kuingiza maarifa asilia katika shughuli zake katika uungaji mkono wa Programu ya Taifa ya Kuasirisha Kilimo. Kwa kutumia matriksi sahili, lakini yenye kufaa, ya mtiririko wa maamuzi, jitihada za wenyeji huchekechwa na ama kusambazwa kwa ajili ya kufanyiwa utafiti zaidi au kukataliwa. Kwa msingi wa matriksi hiyo, asasi inaweza kuamua kwa haraka mahali pa kuingiza rasilimali, mahali pa uhusiano na wahitaji na mahali pa kutoa ushauri dhidi ya mila potofu za wenyeji.

Mkabala wa Shirika la Taifa la Utafiti wa Kilimo (kwa kushirikiana na wahusika wengine nchini Uganda) umeanzisha mchakato unaochochea utafiti na matumizi ya maarifa na ubunifu asilia pamoja na maendeleo yake ya baadaye. Katika muktadha wa mkakati wa kitaifa wa maendeleo endelevu ya MA na uingizwaji wake katika mchakato wa kitaifa wa uondoshaji umaskini, Uganda inatoa kielezo cha namna ya uhamasishaji wa watendaji na watafiti katika ukuzaji na usambazaji wa utendaji asilia. Wakati huohuo sheria imetungwa ambayo itawalinda wabunifu wa maarifa asilia.

### Changamoto

Wakati ambapo bioteknolojia inaendelea kuchukua nafasi muhimu na kujenga matumaini ya kuongeza uzalishaji katika ardhi chakavu na bila kutegemea sana dawa za kuulia wadudu, jumuiya na watendaji wa vijijini, hususan katika Afrika, bado wataendelea kutegemea teknolojia ya kawaida kwa siku za usoni. Watafiti na watendaji wanaendelea kuzifanyia marekebisha teknolojia hizi. Ili kubainisha na kutumia maarifa asilia katika uboreshaji wa teknolojia hizo, watafiti na wadau wengine hawana budi kupiga hatua moja zaidi kuelekea maarifa asilia. Watafiti na watunga sera hawana budi kufahamu fika kuwa shughuli za kuendeshea maisha ni zaidi ya maswala ya utamaduni pekee. Badala yake iko haja ya kutambua kuwa utendaji wa wenyeji ni matokeo ya majaribio yaliyochukua muda mrefu (na yanayoendelea) katika mazingira yasiyo rasmi. Watendaji hawa wenyeji kwa kiasi kikubwa hawakuingiza itifaki katika matokeo ya utafiti wao na kwa sababu mbalimbali wamekuwa wakiyatumia matokeo wao wenyewe bila ya kuwa na utaratibu wowote wa kuyasambaza nje ya jamii zao.

Utafiti wa kilimo na maendeleo vijijini vinakabiliwa na mahitaji kinzani ya aina mbili pale vinapokabiliana na changamoto ya kuvihusisha na maarifa asilia. Watu wengi wenye maarifa asilia ni wa kizazi cha zamani na wataondoka na maarifa hayo pale watakapofariki. Na wakati huohuo, maswala ya kuchangia uondoshaji wa umaskini na uzuiaji wa upungufu wa chakula mara nyingi huhitaji suluhisho zenye kuhusisha mambo mengi. Shughuli nyingi za MA huendeshwa katika maeneo mahususi na haziwezi kupanuliwa kirahisi kabla ya kuhakikishwa kuwa zina manufaa. Kwa hali hiyo utafiti utakabiliwa na uamuzi wa ama kubainisha shughuli nyingi kadri iwezekanavyo au kuchagua, huku kukiwa na hatari ya kuziacha zilizo nzuri zaidi, shughuli chache kwa ajili ya kuziendeleza na kuzihifadhi kwa lengo la kuzisambaza na kuziendeleza. Pamoja na hivyo, uendelezaji wenye ufanisi unawezekana (kwa mfano Kenya inakuza mimea michache ya dawa na manukato kwa matumizi ya viwanda na biashara), hasa pale ambapo sekta binafsi inaweza ikahusika katika uwekezaji unaohitajika. Hata hivyo, hii yaweza isiwe njia tosha ya kuzuia kutoweka kwa mazao na mboga<sup>23</sup> zenye matumizi machache au ambazo matumizi yake hayajagundulika.

### Jumuiya hupanua msingi wa maarifa

Miundombinu ya usafiri na simu hatimaye inaenea hata katika maeneo ya ndani kabisa ya vijijini katika Afrika. Hali hii inazipa jumuiya hizo nafasi ya kuanza kushiriki pamoja na jumuiya nyingine katika uchangiaji wa matatizo, uzoefu na masuluhisho na kwa pamoja kujenga mweka wao wenyewe wa maarifa. Katika Afrika ya Kusini kikundi cha Rooibos cha wakulima wa chai walitembelea kikundi kingine kujifunza kushua masoko. Kutokana na ziara hiyo kikundi hicho kiliunda ushirika wa wakulima, kikaboresha mfumo wake wa soko, na sasa kinauza chai Ulaya, na kujiongezea kipato. Watendaji kutoka Afrika Masahriki na Asia Kusini walikutana katika mabadilishano ya kikanda kufunzana juu ya uhifadhi na ukuzaji wa miti ya dawa.<sup>24</sup> Watafiti, mawakala wa ugani na watoa huduma wengine wa vijijini wanaweza kuzisaidia jumuiya katika kutafuta jumuiya nyingine kwa ajili ya ushirikiano, utafiti unaweza kujenga mahusiano baina ya watendaji, ukahusika katika majaribio yanayosimamiwa na wakulima na ukasaidia katika mawasiliano ya mbali.

Mfano ufuatayo unaonyesha jinsi jumuiya zinavyoweza kuhifadhi maarifa yao zenyewe na namna teknolojia ya habari ilivyozisaidia jumuiya kusambaziana uzoefu. Mradi wa Maendeleo ya Kilimo wa Milima ya Uluguru (UMADep) nchini Tanzania umebuniwa kuwashirikisha

wakulima wenyeji katika uhifadhi wa maarifa asilia juu ya Uhifadhi wa Mazao Asia (NCP). Kisha wakulima husambaza maarifa hayo kwa wenzao kwa kutumia mafunzo na warsha ambazo huwavutia wengi na zenye manufaa katika mazingira husika.<sup>25</sup> Mkabala huu huhusisha jumuiya ya eneo husika katika mchakato mzima wa ukusanyaji, uhifadhi na usambazaji wa maarifa.

## Hitimisho

Mifano ya Tini za MA iliyojadiliwa hapo juu inadhihirisha kuwa jumuiya za vijijini zinaelewa fika maswala yanayohusu njia zao za kujitafutia maisha. Hubadili maarifa asilia kwa lengo la kufanyia mageuzi asasi za kimila na kuzalisha rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya ushughulikiaji wa maswala mahususi ya jumuiya. Serikali mbalimbali pamoja na wabia wa maendeleo zinaweza kutoa mchango muhimu katika kusaidia uanzishaji wa utaratibu kwa ajili ya uhifadhi, uthibitishaji, usambazaji, ubadilishanaji na uingizaji wa maarifa asilia katika mchakato wa maendeleo ya taifa. Hatimaye, mafanikio ya aina mbalimbali yanaweza kuletwa na misaada ya aina hii ya kiasasi na kifedha inayotolewa na serikali pamoja na mawakala wa maendeleo kwa lengo la uendelezaji wa juhudi za jumuiya ya kujitafutia maisha zinazotokana na wenyeji.

- 1 Kutoka nje sio kwa maana ya misaada ya nje ya maendeleo bali kwa maana ya nje ya mfumo wa uzalishaji wa wenyeji, km. mbolea za chumvichumvi badala ya mboji iliyotengenezwa shambani
- 2 Sera za kuwezesha huhusisha mambo mengi zaidi ya teknolojia na uchumi wa uzalishaji chakula—ama kwa ngazi ya kujikimu au ya biashara. Mambo mengine ni pamoja na akiba ya chakula, msaada wa chakula na bei ya chakula, utafiti, huduma za ugani, na kukabili changamoto za utandawazi wa teknolojia ya chakula, biashara na ushindani na uharibifu wa soko unaosababishwa na ruzuku katika nchi za viwanda.
- 3 “Inafahamika, kwa mfano, kwamba Monsanto, kampuni la kimataifa la sayansi-uhai lenye makao yake makuu huko Missouri, lina bajeti ya utafiti na maendeleo ambayo ni mara mbili zaidi ya bajeti ya R&D ya mtandao wa dunia nzima wa sekta ya taasisi za utafiti wa umma” J. Sachs, 1999  
<http://www.cid.harvard.edu/cidinthene/article/sf9108.htm>
- 4 GFAR (Foramu ya Dunia kwa ajili ya Utafiti wa Kilimo) hivi karibuni ilizindua tovuti ya maswala ya spishi ambazo hazitumiki kikamilifu <http://www.underutilizes-species.org/>
- 5 *Tini za MA 47*
- 6 Mjetrofa ni mmea wenye matumizi mengi. Wakulima wa Uganda huutumia kama kizuio cha mimia ya vanilla. Jumuiya za wenyeji huutumia mmea huu kwa matumizi ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa mapambo.
- 7 Kwa taarifa, mmea wenye matumizi mengi kuliko yote ni mnazi ambao hutumika kwa lishe, afya, kujengea, usafiri, kazi za sanaa, nzuri, na nyingine nyingi. Hata hivyo, kama ilivyo kwa mimea mingine, utafiti wa mnazi umejikita zaidi katika uzalishaji wa mafuta yake, hapa ndipo ambapo mnazi hukabiliwa na ushindani mkubwa kuliko yote kutoka kwa mimea mingine.
- 8 *Tini za MA 49*
- 9 *Tini za MA 48*
- 10 *Tini za MA 2, 4, 24, 43, 44, 45, 49*
- 11 *Tini za MA 2, 4, 44, 45, 58*
- 12 *Tini za MA 23, 24, 43, 47, 58*
- 13 *Tini za MA 47*
- 14 *Tini za MA 2, 8*
- 15 *Tini za MA 9, 15, 19, 23, 27, 28, 34, 43, 57, 58*
- 16 *Tini za MA 6*
- 17 *Tini za MA 47*
- 18 *Tini za MA 44, 47 52*
- 19 *Tini za MA 36*
- 20 *Tini za MA 14, 36, 39, 49, 54*
- 21 *Tini za MA 39, 44*
- 22 *Tini za MA 15, 26, 30, 32, 35, 37, 41, 51, 52, 54*
- 23 Kama ilivyofafanuliwa katika Tini za MA 44, ziko aini nyingi za mimea ambazo hazitumiki, na hazilimwi ambazo hutumika wakati wa dharura. Mimea ya aina hiyo haijatumika wala kutafitiwa ipasavyo. Wakati ambapo katika mazingira ya kawaida, watu hula tu vyakula vikuu, mimea hii ya ‘akiba’ inaweza kuwa na sifa ambazo zinaweza kugunduliwa zaidi
- 24 *Tini za MA 55*
- 25 *Tini za MA 34*

## 7. Maarifa Asilia na Usimamizi wa Rasilimali za Asili

*Achim Steiner  
Gonzalo Oviedo*

*Achim Steiner, ni Mkurugenzi Mkuu wa IUCN—Umoja wa Wahifadhi Duniani, Gland, Uswisi*

*Gonzalo Oviedo, ni Mshauri Mkuu wa Sera za Kijamii wa IUCN. Taarifa kwa ajili ya makala hii zimetolewa na Ofisi ya Kanda ya IUCN kwa nchi cha Kusini mwa Afrika (ROSA)*

Kwa kipimo cha yaliyomo katika Tini hizi za MA ni dhahiri kwamba sasa hivi umuhimu wa maarifa asilia katika maendeleo na mazingira unaendelea kutambulika miongoni mwa watafiti na watendaji. Uzoefu wa kiutafiti na wa kiutendaji kutoka duniani kote, na labda hasa kutoka Afrika, unaonyesha kuwa si tu kwamba maarifa asilia yamekuwa na mchango muhimu katika maendeleo ya tamaduni za wenyeji na katika mabadiliko yanayoendelea kuzikumba tamaduni hizo kwenye mazingira yao, bali pia zimekuwa na mchango muhimu sana kwa mambo yanayofanyika nje ya ulingo wa jumuiya zinazoyabuni.

Uanzishwaji wa Programu ya Maarifa Asilia na Benki ya Dunia lilikuwa jambo jema kwa IUCN—Umoja wa Wahifadhi Duniani, ambao ulishaanza kujishughulisha na maswala ya maarifa asilia katika Kusini mwa Afrika tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990. Leo hii IUCN bado inajishughulisha na maswala ya maarifa ya asili ya kiikolojia katika eneo hilo, kupitia Ofisi yake ya Kanda kwa nchi za Kusini mwa Afrika, pia na duniani kote, na imeunganisha vizuri mada zinazohusiana na maarifa na jumuiya za wenyeji katika programu zake za dunia.

Afrika ni bara tajiri kwa rasilimali za asili, kama vile misitu, ardhi tepe, wanyama pori, madini, uvuvi, na nyingine nyingi. Mifumo yenye ufanisi ya usimamizi inaweza kuhakikisha kuwa rasilimali hizi sio tu kwamba zinaishi bali pia zinaongezeka huku zikiwa zinatumika kiadilifu, na kwa hali hiyo kujenga msingi kwa ajili ya maendeleo endelevu na kwa uchumi imara wa taifa.

Kwa kipindi kirefu rasilimali za asili zimekuwa sehemu muhimu ya lische ya binadamu, uchumi na utamaduni. Kwa watu wanaoishi kando ya misitu, mimea na wanyama huwapatia chakula, dawa, ngozi, mahitaji ya ujenzi, kipato, na ni chimbuko la kujituma. Mito huwapatia usafiri na samaki, na maji na udongo huwapatia njia za kudumisha maisha yao.

Zipo kumbukumbu tosha za kudhihirisha kuwa jumuiya za asili hujenga utambulisho wao wa kijamii na kiroho kutoka kwenye ardhi. Heshima ya ardhi ilitokana na matumizi yake. Shughuli za asili zilijikita kwenye ufahamu wa kuishi kirafiki na mazingira, ambao ulisababisha kuweko kwa shughuli na matumizi endelevu. Kijadi matumizi ya rasilimali yalifanywa kulingana na maadili ya kijadi. Katika nchi zinazoendelea, matumizi ya rasilimali za asili kama vile wanyama pori ni ya lazima kwa ajili ya kuboresha maisha ya watu wa nchi hizo. Kwa karne nyingi, njia za maisha katika nchi hizo zimekuwa na utaratibu wa kuhifadhi au kuhakikisha

### Usimamizi endelevu wa wanyamapori

Katika Barotseland huko kwenye Bonde la Mto Zambazi katika Afrika ya Kusini, ilikuwa mwiko kuua mnyama jike mwenye uwezo wa kuzaa. Wanyama waliouliwa walikuwa wa kiume na wale waliozeeka. Spishi fulani za wanyama hazikuruhusiwa kuwindwa katika majira fulani (kama vile majira ya kuzaliana), ili kuepuka hatari ya kuangamiza rasilimali hiyo. Mfumo huu unafanana na ule wa kuvuna wanyama pori kwa utaratibu maalum wa kuchagua ili kudumisha uendeleu. Jumuiya zilikuwa na uwezo wa kuhakikisha kuwa rasilimali ya wanyamapori inaongezeka, na wakati huohuo inawapatia protini ambayo haikupatikana mahali pengine katika mazingira yao ambayo haya-kuruhusu ufugaji wa ng'ombe kutokana na kuweko kwa mbung'o. Kwa Wabarotse, kama pia ilivyokuwa kwa Wabemba wa Jimbo la Luapula huko Zambia, kulikuwa na utamaduni wa kutoruhusu uvuvi wa samaki wadogo sana. Jumuiya zilizingatia misimu ya uvuvi hasa kwa njia ya sherehe za kijadi ambazo kwa kawaida ziliashiria mwanzo wa kipindi mahususi cha msimu wa uvuvi. Taratibu za namna hii zilihakikisha kuwa matumizi ya rasilimali yanakuwa endelevu.

matumizi endelevu ya rasilimali za aina hiyo kwa njia ya miiko au heshima (tazama boksi)

Kwa mfano katika Barotseland huko kwenye Bonde la Mto Zambezi katika Afrika ya Kati, lilikuwa kosa kubwa sana kuua mnyama anayeweza kuzaa. Wanyama waliouliwa walikuwa wa kiume na wale waliozeeka. Spishi fulani za wanyama hazikuruhusiwa kuwindwa katika majira fulani (kama vile majira ya kuzaliana), ili kuepuka hatari ya kuzi angamiza. Mfumo huu unafanana na ule wa kuvuna wanyama pori kwa utaratibu maalum wa kuchagua ambao huhakikishia uendeleu. Jumuiya zilikuwa na uwezo wa kuhakikisha kuwa rasilimali ya wanyamapori inaongezeka, na wakati huohuo inawapatia protini ambayo haikupatikana mahali pengine katika mazingira yao ambayo hayakuruhusu ufugaji wa ng'ombe kutokana na kuweko kwa mbung'o. Kwa Wabarotse, kama ilivyokuwa pia kwa Wabemba wa Jimbo la Luapula huko Zambia, kulikuwa na utamaduni wa kutoruhusu uvuvi wa samaki wadogo sana. Jumuiya zilizingatia misimu ya uvuvi hasa kwa njia ya sherehe za kijadi ambazo kwa kawaida ziliashiria mwanzo wa kipindi mahususi cha msimu wa uvuvi. Taratibu za namna hii zilihakikisha kuwa matumizi ya rasilimali yanakuwa endelevu.

Katika jumuiya hizi iliwezekana kufanya mgawanyo wa kuridhisha wa kipato baina na kati ya vizazi kwa sababu

rasilimali ziliheshimiwa kama sehemu muhimu ya maisha ya kila siku. Rasilimali zilikuwa mali ya jumuiya na kwa hiyo jumuiya ilizitumia huku ikiwa inatafakari maslahi ya vizazi vijavyo. Chini ya utaratibu wa kijadi wa usimamiaji rasilimali urithishaji kwa vizazi vijavyo ulikuwa jambo lililokubalika.

Kwa kawaida jumuiya zilirithisha maarifa yao ya asili juu ya usimamiaji wa rasilimali kwa vizazi vijavyo kwa njia ya masimulizi. Kuendelea kuwepo kwa amali za jumuiya hizo kulitegemea kwa kiasi kikubwa utaratibu wa kurithishana maarifa. Kwa hali hiyo kuweko kwa udumishaji na urithishaji wa maarifa hayo pamoja na utamaduni wake kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuyachuja vizuri kwa kuyaweka kwenye matendo yenye manufaa kijamii na kiuchumi ndizo hasa sababu za msingi za kuwepo na kuendelea kukuwa kwa utamaduni wa jumuiya hizo.

Endapo shughuli za kijadi hazitakuwa na manufaa na motisha ya kiuchumi, baadhi ya maendeleo na matumizi vitasababisha kutoweka kwa maarifa na taratibu zenye kuzingatia uendeleu. Chitemene ni mfumo wa kilimo kinachotumia maarifa ya wenyeji ambao uko hatarini kutoweka. Hii ni kwa sababu jumuiya za wenyeji katika Majimbo ya Kaskazini, Luapula, Kaskazini-Magharibi, na Kati huko Zambia ambazo hutumia mfumo wa 'chitemene' hazina motisha ya kuendelea na mfumo huo. Sheria ya Misitu imetenga maeneo makubwa ya ardhi kama hifadhi ya misitu isiyoruhusiwa kutumiwa na jumuiya za wenyeji. Na zaidi, sheria hiyo imepiga marufuku au kupinga mfumo wa kilimo wa chitemene, ambao wataalamu wa serikali waliuchukulia tu kirahisi kama mbinu ya kilimo cha kukata na kuchoma. Hata hivyo chitemene ulikuwa mfumo muhimu sana kwa ajili ya kilimo cha kijadi cha mazao ya kujikimu ambacho kimedumishwa kwa karne nyingi.

Leo hii kutokana na ongezeko kubwa la watu pamoja na uhaba wa ardhi uliotokana na uzuiji wa ardhi kwa matumizi ya umma mfumo wa chitemene umepoteza umaarufu kutokana na upungufu wa ardhi ambayo ingetumika kwa kilimo cha mzunguko. Kwa kawaida wanavijiji walifyeke maeneo yaliyoachwa hadi yakawa mapori ya muda mrefu kabla ya kupanda, lakini sasa maeneo huachwa kwa muda wa miaka mitano tu au sanasana miaka kumi. Hapo mwanzoni aina mbalimbali za mazao zilizolimwa zilipunguza uwezekano wa kukosa kabisa mavuno na kuongeza aina ya vyakula katika lishe. Upandaji wa mazao mchanganyiko na upumzishaji wa ardhi vilidumisha ubora wa ardhi na kuongeza mazao. Sasa hivi kutawala kwa kilimo cha biashara kama kinavyohimizwa na baadhi ya sera za umma kunasababisha kuanguka kwa mifumo ya kijadi ya

kilimo. Hali hii inasababisha kumomonyoka na kupotea kwa maarifa asilia katika maeneo hayo.

### MA na maswala ya kiimani

Karibu nusu ya *Tini za MA* zinazohusu rasilimali za asili zinaonyesha kuwa imani imekuwa na nafasi kubwa katika usimamiaji wa rasilimali hizo.<sup>1</sup> Mbinu asilia za kulinda vyanzo vya maji huko Forikrom Ghana, ambapo taratibu za kupata na kutumia maji zimekitwa katika imani ni mfano mmoja wa matumizi ya imani katika kulinda rasilimali asilia.<sup>2</sup> Kwa jumuiya nyingi za wenyeji, dunia hii na rasilimali zake ni vitu vitakatifu vyenye kustahili kuheshimiwa sana. Hali hii mara nyingi husababisha kuundwa kwa mifumo iliyojikita katika kaida na asasi za kiimani kwa ajili ya kusimamia rasilimali muhimu na nyeti za asili.

Moja ya asasi muhimu sana zilizotokana na maarifa na taratibu asilia ni maeneo matakatiifu ya asili. Miiko na kanuni za usimamiaji za kijadi kwa kawaida haziruhusu baadhi ya mambo kufanyika au baadhi ya watu kufika katika maeneo hayo. Maeneo mengi matakatiifu yamedumu kwa karne nyingi hali ambayo imeyageuza kuwa hifadhi ya bioanuai. Aidha, maeneo hayo hutumika kama utambulisho wa koo au kabila na yana nafasi muhimu katika utamaduni na mtindo wa maisha wa jumuiya asilia.

Hata hivyo serikali na mawakala wa hifadhi, sera na sheria vimepuuza na kudharau mchango wa maeneo matakatiifu katika uhifadhi. Wakati ambapo mbinu za hifadhi zilizotokana na jumuiya zililinda maeneo matakatiifu hapo nyuma, sasa hivi jumuiya za wenyeji zinazidi kusukumwa na nguvu za kisiasa na kiuchumi ambazo hawana uwezo wa kuzidhibiti. Bila ya kuweko kwa uhakika wa upatikanaji wa ardhi na nafasi ya kushiriki kikamilifu katika maamuzi yanayowagusa wao na matumizi ya ardhi yao, ni muhali kwa jumuiya za asili kuweza kudhibiti ardhi na rasilimali zake kikamilifu.

### Uingizaji wa MA katika mazingira yanayobadilika

Moja ya mambo mazuri sana yaliyoibuliwa na *Tini za MA* katika maeneo mengi yanayohusiana na usimamizi ya rasilimali za asili ni matumizi ya MA katika mazingira ya mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Hadithi za mafanikio kuhusu matumizi ya maarifa asilia katika kushughulikia changamoto halisi za mabadiliko ya kima- zingira hubainisha kwamba dhima ya MA ina sifa zifuatazo:

- Baadhi ya mambo katika maarifa asilia kama yalivyohifadhiwa na wazee na asasi za kimila, wakati mwingine yakihusishwa na itikadi ya kiimani, yamefanya kazi kwa ufanisi kwa kipindi kirefu.<sup>3</sup>

- Sababu za ndani na za nje zimesababisha kumomonyoka hatua kwa hatua maarifa na taratibu asilia; mahitaji mapya yameibuka na kusababisha shinikizo katika mifumo asilia ya usimamiaji; upatikanaji wa ardhi na rasilimali umepungua kutokana na ongezeko la watu na ushindani na watumiaji wengine,<sup>4</sup> ambavyo vimesababisha kupungua uwezo wa mazingira asilia wa kuipatia jumuiya shughuli za kuendeshea maisha. Katika mifano mingi, hali hii imezingiza jumuiya katika migongano ya kimatakwia iliyosababisha kuvunjika kwa asasi za kijadi.<sup>5</sup>
- Nguvu zinazoimbuka—kama vile vijana na vikundi vya wanawake vilivyowezeshwa, zikisaidiwa na vichocheo vya nje—zinaingiza maarifa na taratibu mpya kwa njia ya mikabala ya vikundi ambayo inakwenda mbele zaidi ya asasi za kijadi.<sup>6</sup>
- Nguvu hizi zinazoibuka zinapambana kufanikisha lengo la msingi: kufanya maarifa asilia na kanuni za kijadi kuwa asasi za kisheria zinazokubalika serikalini na kwa jamii yote.<sup>7</sup>

Hivyo *Tini za MA* zinatoa funzo muhimu linalopaswa kutafakariwa. Ili maarifa asilia yaweze kudumu kama sehemu muhimu ya maisha ya jumuiya na mbinu ya kujipatia maisha, ni lazima maarifa hayo yaingizwe katika muktadha wa mabadiliko ya sasa ya kijamii, kiuchumi na kitamaduni, na yaweze kuhimili vishindo vya kuingizwa katika mazingira mapya. Ili jambo hili lifanikiwe, mikabala miwili inaonekana kuwa ni muhimu:

- Uunganishaji wa maarifa asilia na sayansi, vikipewa umuhimu sawa katika ngazi ya jumuiya na vikifanya kazi kwa kukamilishana.
- Uunganishaji wa asasi na taratibu za kijadi na miundo na kanuni rasmi ili kujenga msingi mpya imara wa maarifa asilia na kuifanya jamii pana itambue umuhimu na mchango wake. “Changamoto ... ni namna ya kuunganisha mifumo ya kijadi ya kaida na imani katika mfumo wa utawala wa kawaida na kujenga mambo mapya yanayokubalika kwa pande zote na utamaduni mpya wa usimamiaji wa rasilimali za asili.”<sup>8</sup>

### MA kama yanavyoonekana

Katika dunia ya sasa yapo mambo mengi yanayotokea kinyume katika historia ya maarifa asilia. Moja ya mambo hayo kwamba karne nyingi zilizopita jumuiya zilitenga maeneo ya hifadhi au ya asili kwa kuyalinda kwa kutumia kanuni kali za kiimani. Katika enzi ya sasa maeneo ya hifadhi yaliyotengwa chini ya taratibu zisizo za kiimani za Hifadhi ya Yellowstone huko Marekani kwa kiasi kikubwa yanafanana na ardhi na rasilimali za jumuiya za kijadi. Hata hivyo, mara nyingi kanuni zinazinyima jumuiya za kijadi zilizomo humo haki ya

kutumia ardhi au rasilimali, na hata wakati mwingine kuzifukuza au kuzichukulia kama wavamizi. Kwa bahati nzuri leo hii dunia inatambua umuhimu wa kubali sera na taratibu za maeneo ya hifadhi ili kutoa kipaumbele kwa mahitaji na haki za jumuiya za wenyeji. Hii ni pamoja na kurejesha hadhi kwa maarifa asilia ya wenyeji na kuyaingiza katika usimamizi wa maeneo ya hifadhi.<sup>9</sup>

Jambo lingine lililo kinyume, ambalo matokeo yake ni karibu sawa au mabaya zaidi, ni ukweli kwamba, maarifa asilia—ambayo kwa kawaida hutazamwa kama ujinga na ushirikina—yamesaidia katika kunufaisha kwa kiasi kikubwa viwanda vya kibioanuai. Kiwanda cha dawa, kwa mfano, kimezalisha dawa kwa ajili ya masoko ya dunia nzima kutokana na mimea au wanyama ambao uwezo wao wa kitiba ulianza kugunduliwa na jumuiya za kijadi. Vivyo hivyo kwa kiwanda cha vyakula. Mara chache sana waganga wa kijadi na jumuiya za wenyeji zinazotoa maarifa hayo zimeweza kulipwa mirabaha ya kutosha kutoka kwa viwanda hivyo. Wakati huohuo ufukara katika jumuiya hizo umezidi kuongezeka.

Mkataba wa Bioanuai ulianzisha mjadala na hatua kuhusu maswala yanayohusu matumizi mapana ya maarifa asilia au ya kijadi nje ya jumuiya za wenyeji zilizoyagundua. Serikali na Jumuiya za kirai zinatakiwa kutazama maswala kama vile: Kimsingi ni nani anayestahili kunufaika na maarifa hayo? Je matumizi ya maarifa hayo kibiashara yatiliwe mkazo au la? Ni nini jukumu la serikali. Makala haya hayana dhamira ya kujadili mambo haya kwa undani. Tunaamini katika manufaa na thamani ya maarifa asilia katika usimamiji wa rasilimali za asili, na kwa hali hiyo msimamo wetu ni kuwa matumizi mapana ya maarifa hayo yatakuwa na manufaa makubwa kwa dunia yote; lakini fursa sawa na haki ni mambo ya msingi katika kushughulikia swala hili.

Jambo la mwisho katika makala hii ni kuhusu changamoto kubwa ya kuhifadhi maarifa asilia. Katika hali ya kuwepo kwa nguvu kubwa za mabadiliko ya kiutamaduni, maarifa asilia yanakabiliwa na hatari kubwa. Maarifa asilia kama yalivyosisitizwa katika ufafanuzi uliotolewa kwenye Programu ya Maarifa Asilia kwa Maendeleo pamoja na uzoefu ulioonyeshwa katika *Tini za MA*, kwa kiasi kikubwa hayajawekwa kwenye maandishi, huhifadhiwa kichwani na kutolewa kwa masimulizi au kwa kutumia mfano. Kwa siku hizi, maarifa yenye sifa za aina hii sio rahisi kudumu. Bila shaka kiasi kikubwa cha maarifa asilia duniani yatatoweka katika miongo michache ijayo kama hayataimarishwa kwa katika hali itakayoyawezesha kuhimili mikikimikiki ya mabadiliko ya kiutamaduni. Hili linahitaji ubunifu mkubwa, hatua za ubunifu ambazo zitajali mahitaji na haki za jumuiya, na kujitolea kwa bidii kwa asasi zote muhimu za—kielimu, kizingira, ushirikiano wa maendeleo na fedha.

Kwa kuongozwa na sera, mtazamo na malengo yake yenyewe, IUCN imejitolea kikamilifu kusaidia uhifadhi, ufufuaji na utumiaji wa maarifa asilia katika kuhifadhi bioanuai, na katika matumizi endelevu, chini ya utaratibu wa fursa sawa na uzingatiaji wa tofauti za kitamaduni, kama ilivyofanyiwa marekebisho na Mkutano wake Mkuu. Kwa kumalizia hili, IUCN hufanya kazi pamoja na jumuiya za wenyeji pamoja na asasi zao, na kujenga ubia na wahusika wengine wa kitaifa na wa dunia.

Bado tunayo nafasi ya kuokoa moja ya hazina kubwa kabisa ya matunda ya akili ya binadamu—hazina ambayo yaweza kuwa imebeba utatuzi kwa matatizo dunia ya sasa na ya baadaye. Sote hatuna budi kujitolea kwa ajili ya utekelezaji wa jambo hilo.

1 *Tini za MA 4, 46, 48.*

2 *Tini za MA 4.*

3 *Tini za MA 4, 46, 48.*

4 *Tini za MA 23, 46, 48.*

4 *Tini za MA 23, 45.*

6 Kinaweza kuwa kikundi cha vijana kinachofanya kazi zinazohusiana na mazingira, kama vile “Mobisqud” huko Forikrom, (*Tini za MA 4*) au cha wanawake kama vile Umoja wa Wanawake wa Popenguine wa Kulinda Mazingira huko Senegali (*Tini za MA 8*) au kamati za wazalishaji kama vile Kamati ya Uongozi ya Mussel Rocks ya Zimelene, Msumbiji (*Tini za MA 46*).

7 Hili wakati mwingine huhusisha majadiliano na mamlaka ambayo kwa kawaida huwa marefu, magumu na ya kukatisha tamaa, kutokana na mamlaka kutokuwa tayari kuridhia kauli za jumuiya.

8 *Tini za MA 46.*

9 Huu ulikuwa ujumbe mzito ulitolewa na Mkutano Mkuu wa Maeneo ya Hifadhi Duniani ulioandaliwa na IUCN mwaka 2003, huko Durban, Afrika Kusini, mwezi wa Septemba. Mikutano ya aina hiyo ambayo hufanyika mara moja kwa kipindi cha miaka kumi hukutanisha pamoja asasi na wataalamu na kuwapa nafasi ya kujadili pamoja uzoefu wao na kupendekeza mikabala na hatua za kuchukuliwa kuimarisha dhima ya maeneo ya hifadhi katika kulinda bioanuai.

## 8 Maarifa Asilia na Sayansi na Teknolojia: Mgongano, Ukinzani na Utangamano?

*Sibusiso Sibisi*

*Dkt Sibusiso Sibisi, ni Rais na Mtendaji  
Mkuu wa Baraza la Utafiti wa  
Kisayansi na Kiviwanda (CSIR) Afrika  
Kusini*

Leo hii maarifa asilia yanachukuliwa kuwa yenye manufaa katika nyanja za maendeleo ya kijamii na ya binadamu. Aghalabu mchango wake katika sayansi na teknolojia ama hupuuzwa au haufahamiki. Kwa mfano wafugaji wa Kimasai huchanja mifugo yao kwa kutumia povu la mate ya ng'ombe ambao ndio tu wamepona. Vivyo hivyo wakunga wa Kiingereza walihifadhi mkate wao wa kusubia pamoja na vifaa na nguo za kuzalishia. Kinyume chake, Pasteur alitambuliwa kwa kuwa mstari wa mbele katika ugunduzi wa chanjo na Fleming naye kwa kugundua penisilini.

Kwa karne nyingi, jumuiya za wenyeji zimekuwa zikitegemea maarifa na utaalamu asilia katika kukabiliana na changamoto za mazingira magumu: ukame wa muda mrefu, mafuriko, wadudu wa maradhi, au udongo chakavu. Wakulima walijijengea utaratibu wao wa kubashiri mvua kwa kutazama mwenendo wa mawingu, tabia za kuhama kwa ndege, pepo za msimu na matukio mengine ya kimsimu. Aidha wakulima walibuni mifumo changamano ya matumizi endelevu ya ardhi. Kutokana na hali hiyo, MA iligeuka kuwa sayansi na teknolojia ya aina yake, ambapo wakulima na wanajumuiya walikuwa ndio wanasayansi na wagunduzi—wakichunguza, wakifikia mahitimisho na wakichukua hatua za utekelezaji. Katika Bukinafaso wataalamu wa hali ya hewa sasa hushirikiana na wakulima katika kufanya utabiri wa hali ya hewa.<sup>1</sup>

Sayansi na teknolojia ya sasa imesaidia kuongeza uhakika wa kupatikana kwa chakula na uzalishaji wa kilimo duniani kote kwa kutumia aina ya mbegu zenye uwezo wa kutoa mazao mengi. Nyakati fulanifulani, mbegu hizi zenye uwezo wa kutoa mazao mengi zilifahamika kama aina ya mbegu inayokubali vizuri: mbegu hizi hukubali vizuri pale tu zinapopata mahitaji yao muhimu ya mbolea, maji na kukingwa vyema dhidi ya wadudu, magonjwa na magugu. Katika maeneo mengi, uzalishaji unaotumia mbegu hizi ulihitaji ujenzi wa mfumo mzuri wa kusambaza pembejeo, kumwagilia, kutoa huduma za ugani, na taratibu nyingine za maswala ya masoko na usindikaji. Kutokuwepo kwa vitu hivi kulisababisha kushindwa kwa mapinduzi ya kilimo katika Afrika kuliko ilivyokuwa katika Asia. Matumizi mabaya ya mbolea na dawa za kuulia wadudu pia yalisababisha uharibifu wa mazingira na madhara ya kiafya. Asasi za utafiti na za tasnia ya kilimo zilitatua tatizo hili kwa kuzalisha aina ya mbegu ambayo haikuwa na



mahitaji mengi sana, aghalabu uzalishaji huo ulihusisha mbegu zilizotumiwa na wakulima kwa miaka mingi “mbari asilia”.

Pamoja na hivyo, wakulima wengi pia walianza kukabiliana na tatizo hilo. Walirejelea maarifa na taratibu asilia. Huko Bokinafao wakulima walizuia mmomonyoko wa udongo kwa kutumia teknolojia ya zamani ya Zai au kwa kujenga kingo. Katika kaskazini mwa Tanzania na Kenya wakulima wadogowadogo walirejea kilimo cha mazao mchanganyiko, mfumo wa kuchanganya mazao ya kudumu na yale ya muda mfupi ambao sasa utafiti wa kimataifa umeanza kuutambua kwa undani. Pamoja na kwamba mifumo ya kilimo ya namna hii haitoi mavuno mengi kama ile ya zao moja inayotumia pembejeo nyingi, mifumo hii haina madhara makubwa, ni rafiki zaidi wa mazingira ya wenyeji, na kwa kawaida ni endelevu zaidi. Huko Malawi, teknolojia za zamani na sasa za maswala ya usafi wa mazingira, urutubishaji wa ardhi na elimu zinaunganishwa kwa ajili ya kuendeleza ajenda kwa watafiti na wakulima.<sup>2</sup> Huko Amerika Kusini, wakulima wameonyesha uwezo wao wa ubunifu kwenye shughuli za maendeleo shirikishi ya teknolojia.<sup>3</sup> Mtandao wa Nyuki wa Asali huko India husaidia wabunifu wenyeji pamoja na kuhamasisha ubunifu mbalimbali.

Huduma za afya ni eneo lingine ambalo maarifa asilia huchukua nafasi ya dawa za kisasa ambazo ama hazipo au ni ghali mno. Katika Afrika watu wengi hawafikiwi na dawa za kisasa na uwiano wa waganga wa jadi na wale wa kienyeji ni wa 8 kwa 1. Kutokana na hali hiyo, bado tiba za jadi zina mchango mkubwa katika huduma ya afya ya msingi na waganga wengi wa jadi wamegundua dawa za magonjwa mengi ya kawaida.

Dunia inafahamu kuhusu kiwango kikubwa cha maambukizo ya VVU/UKIMWI katika Afrika. Hata hivyo ni mambo macheche sana yanafahamika kuhusu namna waganga wa jadi walivyogundua dawa za kutibu magonjwa dowezi yanayoandamana na VVU/UKIMWI.<sup>4</sup> Kikundi cha Wanaharakati wa Kupambana na Ukimwi Tanga (TAWG) ambacho ni mjumuiko wa waganga wa jadi, madaktari wa kisasa, manesi na waathirika wa UKIMWI kimetibu zaidi ya wagonjwa 400 kwa kutumia mitishamba na kwa maelekezo ya waganga wa jadi. Tiba hiyo imewawezesha wagonjwa kurejea katika maisha yao ya kawaida na hurefusha maisha kwa miaka 5 hadi 10. TAWG kimekusanya taarifa nyingi kuhusu ukusanyaji wa mitishamba, mbinu za kutengeneza dawa, za kutibu na za kutambua mafanikio ya tiba.

## Changamoto za sayansi ya sasa

Mifano iliyotolewa hapo juu ni kielelezo cha utajiri wa mifumo ya maarifa asilia na mchango wake katika sayansi na teknolojia. Misingi ya astronomia, famakolojia, na hata ya hisabati, teknolojia ya chakula au metalujia imetokana na maarifa na taratibu za kijadi. Hata hivyo, maendeleo mapya ya sayansi na teknolojia katika kipindi cha miaka 100 iliyopita yamejenga fikra za kudunisha na kudharau jambo lolote lisilotokana na majaribio ya kimaabara au na idara za utafiti na maendeleo (R&D). Aidha fikra hizo huhusisha mafanikio au ugunduzi wa kiteknolojia na watafiti wasomi au wahandisi. Swala la kujifunza kutokana na maarifa asili bado ni la kuwazika tu badala ya kanuni.

## Uthibitisho wa kisayansi

Maarifa asilia na sayansi ya sasa vimeweza kukamili-shana kwa njia mbalimbali; kama livyokwishaoonyeshwa kwa upande wa kilimo na huduma za afya. Pamoja na hivyo, uthibitishao wa kisayansi bado ni changamoto kubwa kwa upande wa watendaji wa maarifa asilia. Kanuni za afya na itifaki za utafiti huhitaji kwamba matibabu katika tiba au michakato katika taaluma nyingine vifafanuliwe bayana na viweze kufanyiwa uchunguzi wa kina na matokeo yake yasiwe yanabadilika. Aidha kumbukumbu za ithibati ya ukweli wa madai yaliyotolewa hazina budi kutolewa kwenye majarida ya kitaaluma. Hata hivyo msingi wa kiasi kikubwa cha maarifa asilia ni simulizi za kijadi na hayakuhifadhiwa katika maandishi (isipokuwa kwa tiba za jadi za India na China). Kwa kiasi kikubwa maarifa asilia humilikiwa na wazee katika jumuiya na kwa kawaida sio kila mtu kwenye jumuiya ana stahili kuwa nayo. Kadri lugha nyingi za wenyeji zinavyopotea bila shaka ndivyo pia maarifa mengi na tamaduni nyingi vinavyotoweka. Hivyo changamoto inayowakabili wanasayansi wa sasa na watendaji wa kijadi ni kuziba pengo linalogawa dunia zao zinazotofautiana katika mbinu, ubadilishanaji, uhakikishaji na uthibitishaji na hatimaye utumiaji wa maarifa.

Ili jambo hili liweze kufanikiwa, jumuiya za wanasayansi na watafiti (pamoja na maeneo yao husika) hazina budi kuunda ushirikiano wa kimkakati wa wanasayansi na watendaji wa MA. Jambo hili linahitaji uelewa wa pande zote mbili na uhitaji wa kujifunza kutoka kila upande. Wanasayansi wanapaswa kuuelewa na kuukubali uhusiano bayana wa MA na mazingira

halisi. Vivyo hivyo watendaji wa MA wanapaswa kuelewa na kukubali kuwa kuchangia maarifa na kukosoana ni mambo ya msingi katika kudumisha na kuendeleza maarifa yoyote yale.

Pia juhudi hazina budi kufanyika ili kuimarisha uwezo wa watendaji wa MA wa kuhifadhi vizuri kazi zao ili ziweze kukabiliana na uchunguzi makini wa sayansi ya sasa. Hili linahitaji rasilimali pamoja na msaada wa kiufundi kutoka kwa jumuiya ya wanasayansi na kwa mashirika ya kimataifa. Kwa kuzingatia hili, Programu ya Benki ya Dunia kwa ajili ya Maarifa Asilia, iliandaa warsha kuwakusanya pamoja watendaji wa maendeleo wa Afrika Mashariki, Wanasayansi wa Taasisi za Afya za Marekani, Hospitali ya Chuo Kikuu cha George Washington na watumishi wa Benki hiyo. Lengo kubwa likiwa ni kujifunza kutokana na shughuli za kijadi za Afya barani Afrika. Jambo kubwa lililotokana na warsha hiyo lilikuwa ni makubaliano baina ya washiriki ya kushirikiana katika kuthibitisha uwezo wa tiba za mitishamba katika kutibu magonjwa dowezi kwa wenye VVU/UKIMWI.

Huko Afrika Kusini, mashirika ya utendaji kama vile Kituo cha Utafiti wa Tiba (MRC) na Baraza la Utafiti wa Sayansi na Viwanda (CSIR), yakisaidiwa na serikali, yanaandaa mbinu za zitakazotumika katika kuthibitisha dawa za kienyeji kisayansi. Programu za Uchunguzi wa Kibiolojia za CSIR, zilizoanzishwa mwaka 1988, zimelenga katika kuzifanyia mageuzi Dawa za Kijadi za Kiafrika. Mageuzi hayo ni pamoja na kuzifanyia usindikaji rahisi na kuzipatia ithubati ya kisayansi dawa za mitishamba; kugundua chembechembe zinazofaa kitiba tiba ambazo bado hazijafahamiki na kuanzisha uzalishaji wa kibiashara wa mimea ya dawa na manukato kwa kutumia wanajumuiya.

### Hakimiliki za kitaalamu

Sayansi hufanya kazi katika mazingira ya uthibitishaji, ukanushaji, viunzi imara na uthibitishaji wa kimajaribio. Aidha huhitaji uchangiaji na ukosoaji wa pamoja kwa lengo la uimarishaji wa maarifa ikiwa ni pamoja na ubadilishaji wa viunzi. Leo hii teknolojia (na ubunifu) vinastawi chini ya ulinzi wa haki miliki, hasa katika miaka ya awali ya uzalishaji. Watendaji wa kijadi hususan katika sekta ya afya hupendelea kuchangia maarifa yao pamoja na familia zao kwa lengo la kujiongeza tu kipato kutokana na maarifa na shughuli zao. Watendaji wa kijadi watakapopewa nafasi ya kuchangia na kubadilishana maarifa kidunia, pia watahitaji ulinzi wa aina fulani utakaowahakikishia usalama wa ajira zao.

Shirika la Mali za Kitaalamu la Dunia (WIPO) limeshirikiana na vyombo vingine vya Umoja wa Mataifa (UN) kuzungumzia changamoto hii ya haki ya mali za kitaalamu (IPR) kwa ajili ya wataalamu wa kijadi.<sup>5</sup> Katika mwaka 1992, Makubaliano juu ya Uanuai wa Kibiolojia (CBD) yalilenga swala hili kwa kutambua thamani ya maarifa na rasilimali asilia. Shirika lilibuni mfumo wa kuruhusu upatikanaji wa rasilimali za kijeji na mbinu za uchangiaji mzuri na wa fursa sawa.<sup>6</sup> Miaka miwili baadaye, maridhiano yalifikwa juu ya Maswala la Kibiashara ya Haki za Mali za Kitaalamu (TRIPS) ya Shirika la Biashara Duniani (WTO). Makubaliano hayo yaliweka viwango vya kimataifa vya ulinzi wa msingi wa Haki za Mali za Kitaalamu.

Shirika la Mali za Kitaalamu la Dunia (WIPO) limeanza kutoa mafunzo kwa ofisi za Mali za Kitaalamu, kwa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na kwa jumuiya za wananchi ili kuongeza kiwango cha kuelewa jukumu la Haki za Mali za Kitaalamu katika ulinzi wa maarifa ya jadi. Kuweka viwango vipya kwa ajili ya uhifadhi kutajenga mfumo utakaosaidia katika usimamiaji wa athari za Haki za Mali za Kitaalamu katika mchakato wa uhifadhi wa MA. Hili litaziwezesha ofisi za Mali za Kitaalamu kuingiza maswala ya uhifadhi wa Maarifa Asilia katika taratibu zao za uchunguzi wa awali wa kubaini maombi yanayohusiana na ubunifu katika MA.<sup>7</sup>

Mikabala ya kiuvumbuzi kwa ajili ya kulinda MA ni ya lazima kwa sababu taratibu zinazotumika sasa zinaweza zisifae katika uwanja wa MA. MA haina kigezo cha jumla kwa ajili ya kushughulikia maswala yake ya hati miliki. Maarifa Asilia huhifadhiwa kwa njia za masimulizi na matumizi badala ya maandishi. Baadhi ya juhudi zinaweza kuwa na manufaa, kwa mfano, uhimizaji wa watendaji wa kijadi waweze kuandikisha shughuli zao za kijadi. Aina nyingine zinazojitokeza za ulinzi wa MA ni pamoja na Mikataba ya Kuhamisha Vitu (MTA), ambayo inahusu utoaji wa vitu (rasilimali au maandishi) kwa kubadilisha na fedha au vitu vingine visivyo fedha. Mifano ya ugawanaji mzuri na usio na upendeleo wa faida baina ya watumiaji na wamiliki wa maarifa ya kijadi inaweza kuonekana katika nchi nyingi leo hii.<sup>8</sup>

Kwa mujibu wa ripoti ya hivi karibuni ya WIPO,<sup>9</sup> “wakazi wenyeji wana mifumo yao wenyewe ya mambo ya kisheria kwa ajili ya kusimamia uanishaji wa maarifa mbalimbali, taratibu stahiki za kupata na kutumia maarifa pamoja, na haki na majukumu yanayofungamana na kumiliki maarifa, mambo yote haya yakiwa ndani ya tamaduni na lugha zao”. Hivyo jumuiya ya wanasayansi haina budi kujifunza na kuelewa itifaki zinazotawala

mifumo ya wenyeji ya maarifa, na kuipa utambuzi na heshima inayostahili.

Pamoja na hayo, japo ulinzi wa Haki za Mali za Kitaalamu unaweza kuwa sharti muhimu katika kuzungumzia, kutathmini na kuthibitisha MA, ulinzi huo wenyewe haitoshi. Sehemu kubwa ya maarifa na taratibu asilia ipo katika sekta ya umma (kwa mfano katika kilimo). Uanzishaji wa Haki za Mali za Kitaalamu hautazuia uhalifu, na watendaji wa kijadi au jumuiya za wenyeji, kwa kawaida, hazina uwezo wa kukabiliana na maswala ya kisheria. Kama ilivyo kwa tiba za kisasa, watendaji wa jadi wanaweza tu kuthibitishwa na kuthamanishwa endapo wataweka viwango vyao vya ufanisi na umadhubuti (na vya usalama, kwa upande wa dawa) na kuwa na itifaki zinazokubalika kwa ajili ya utendaji na maadili ya kitaalamu. Viwango hivyo si lazima viwe kinyume au vifanane moja kwa moja na vile vya sayansi ya sasa.

Katika kutengeneza viwango hivi, watendaji wa kijadi hawana budi kuhimizwa (na kusaidiwa) katika kufanya tafiti zao wenyewe kwa kuzingatia zaidi taratibu maalumu. Kwa kawaida jumuiya za wenyeji hazina maabara wala wataalamu wa utafiti. Asasi zilizo katika nchi zinazoendelea kwa kawaida hazipewi fedha na rasilimali za kutosha. Ili kuhamasisha matumizi ya MA katika ugunduzi wa dawa mpya na kuzawadia wagunduzi wake, asasi za utafiti za nchi zilizoendelea hazina budi kushirikiana na zile za nchi fukara. Hali hii itasaidia kuimarisha uwezo wa utafiti wa watendaji wa kijadi pamoja na kuinua utafiti na maendeleo na uwezo wa maabara za taifa za dawa wa kuchunguza uwezo wa kitiba wa dawa zilizotokana na MA. Ubia utakaojengeka baina ya waganga wa kienyeji na wanasayansi utawawezesha kuchangia maarifa yao ya miti ya dawa na manufaa ya kiuchumi yanayoweza kupatikana kutokana na bidhaa zilizouzwa. Vitivo vingi vya utafiti katika nchi za viwanda vina programu za kubadilishana na kufadhili wataalamu kutoka katika nchi zinazoendelea ili kuwapa nafasi ya kujifunza teknolojia za kisasa na kufunza mambo maswala ya maarifa na utaalamu asilia. Hii ni njia nyingine ya kuziba pengo baina ya sayansi ya jadi na ya sasa.

Ili kuunga mkono juhudi hizi za kuendeleza sayansi ya MA, ni muhimu pia kwa serikali kubuni mikakati ya kitaifa ya kusaidia utafiti na maendeleo ya MA. Wizara za Afya na Kilimo, kwa mfano, zingeweza kuongoza katika kufanya tathmini ya mchango wa MA katika kufanikisha malengo ya maendeleo ya wizara hizo. Kwa mfano huko Uganda, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (UNCST) imeanza kuingiza MA katika vipaumbele vyake

vya utafiti. Katia ngazi ya sera, tayari Tume imeingiza MA katika Programu ya Kuondoa Umaskini ya nchi.

Hivi katibuni huko Afrika ya kusini kumekuwa na mfano unaowakilisha mkabala wa kuvutia unaoweza kuwa kifani cha kujengea ubia wenye lengo la kuinua na kulinda mifumo ya MA kwa ajili ya kunufaisha mchakato wa maendeleo yake.

Kitendo cha Baraza la Utafiti wa Sayansi na Viwanda cha kutoa hakimiliki kwa fomula ya kifamasia ya dawa ya kudhibiti vitambi kiligusa duniani nzima. Hadithi hii ya P57—kama dawa hiyo ya asili inayodhibiti kitambi ilivyoitwa—na ugunduzi wake vina mizizi katika miti asilia, ambayo kwa muda wa karine nyingi ilikuwa ikitumika kama sehemu ya mlo wa watu wa Afrika Kusini.

Mwanzoni mwa miaka ya 60 uchunguzi ulianzishwa kwa lengo la kubaini thamani ya kilishe pamoja na uwezekano wowote wa madhara ya muda mrefu ya sumu ya “chakula toka mbugani.” Uchunguzi huo ulisimamiwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Chakula ya Baraza la Utafiti wa Sayansi na Viwanda.

Jinasi ya *hoodia* ilichunguzwa kwa sababu ilifahamika kuwa baadhi ya spishi za mmea huu mweroro zililiwa na Wasani kama chakula na maji. Baada ya miaka sita ya majaribio ya kutenga na kubainisha dutu kemikali katika mmea wa *mhoozi* zenye uwezo wa kuzuia unene, mradi ulisimamishwa kwa sababu ya vifaa vilivyokuwa vikitumika havikufaa kwa utafiti uliokuwa umekusudiwa.

Katika mwaka 1983, miaka 20 baada ya utafiti wa P57 kuanzishwa na Baraza la Utafiti wa Sayansi na Viwanda, Taasisi ilipata vifaa vyenye uwezo wa kufanya kazi ya kutambua muundo wa kikemikali wa mazao asilia na uchunguzi ulianza tena. Matokeo yake aina mpya ya kemikali iligunduliwa, ikisawiri familia ya molekuli mpya yenye sifa za kuzuia unene.

Matukio mengine muhimu yalifuatia: Baraza la Utafiti wa Sayansi na Viwanda lilitoa hatimiliki ya P57 mwaka 1996, na mwaka 1997 likatoa leseni kwa Phytopharm plc, kampuni ya Uingereza, ya kuendeleza na kuzalisha kibiashara ugunduzi huo lilioupatia hatimiliki. Katika juhudi zake za kuingiza P57 katika soko, Phytopharm ilifikia makubaliano na Pfizer Inc. mwaka 1998. Uwezekano wa kuingia kwenye soko ukiwa unaonekana dhahiri, Baraza la Utafiti wa Sayansi na Viwanda liliingia katika majadiliano na Wasani mwaka 2002, na kuutangazia umma kuwa linatambua umuhimu wa maarifa ya kijadi ya Wasani katika aina hiyo ya utafiti. Machi 2003 Hati ya Makubaliano kuhusu kushiriki pamoja katika matunda yanayoweza kupatikana ilitiwa

saini baina ya Baraza la Utafiti wa Sayansi na Viwanda na Baraza la Wasani la Afrika Kusini. Katika makubaliano hayo Baraza la Utafiti lilijikubali kulipa Wasani asilimia 8 ya mapato ya awali kutokana kwa Kampuni ya Uingereza iliyopewa kibali cha kutengeneza na kuuza dawa hiyo, na asilimia 6 ya mirabaha yote itakayopokea pale dawa hiyo itakapoanza kuuzwa. Mfano huu wa kunufaika pamoja unahakikisha kuwa Wasani watapata mafao ya haki kama bidhaa itafanikiwa kuingia kwenye soko.

Wakati ambapo kampuni ya Pfizer ilishakabidhi haki zake kwa kampuni ya Phytopharm na juhudi za kuingiza P57 katika soko zinaendelea, tayari Afrika Kusini imeshanufaika kwa njia ya kupokea teknolojia ya kisasa ya kutengeneza dawa. Baraza za Utafiti wa Sayansi na Viwanda lina uwezo wa kukusanya, kuchopoa na kuchekecha sampuli za mimea kutokana na spishi 24,000 za mimea ya asili ya nchi hiyo. Uhusiano wa kikazi na makubaliano rasmi baina ya Baraza na waganga wa kijadi pamoja na jumuiya yaliyofikiwa vitakuwa ufunguo kwa mafanikio ya baadaye ya ushirikiano wa sayansi na maarifa asilia.

Baraza la Utafiti wa Sayansi na Viwanda la Afrika Kusini ni kituo kinachoongoza katika ufanisi wa maswala ya sayansi na teknolojia katika Afrika. Katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita, Baraza hilo limekuwa likifanya kazi pamoja na Wasani ya kuunda modeli ya kiunzi kwa ajili ya kushughulikia maswala mawili yaliyokwishataja hapo nyuma ya muhimu ya ithibati ya kisayansi na haki za mali za kitaalamu. Mfano huu uliotolewa hapa unawasilisha mkabala wa kuvutia ambao unaweza kuwa kifani cha kuundia mahusiano ya namna hii ambayo lengo lake ni kuinua na kulinda mifumo ya MA kwa ajili ya kuimarisha mchakato wa maendeleo.

## Hitimisho

Swali lililoulizwa kwenye kichwa cha makala haya linaweza kujibiwa kusesitiza jambo moja la makubaliano. Maarifa hukuwa tu pale yanapohusisha watu wengi, yanapotumika na kuhojiwa. Leo hii dunia haiwezi kuikwepa hazina kubwa ya maarifa asilia na matatizo yanayoikabilia hazina hiyo kama yalivyofafanuliwa katika Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Migongano na tofauti baina ya “dunia tofauti za maarifa” vitatoweka mara tu baada ya kuzibwa kwa pengo lililopo baina ya wanasayansi na watendaji wa jadi na wale wa sasa. Pengo hilo litazibwa kwa njia ya wote kuafikiana kuhusu viwango, mabadilishano ya mara kwa mara, ulinzi wa haki, pamoja na kutambua na kuzawadia wale wote wanaochangia. Hali hii pia itajenga mazingira ambayo yatatokomeza mambo ya asili ambayo yana madhara na ambayo yamekuwa yakichangia katika kuharibu jina la tamaduni na watendaji wa kijadi.

1 *Tini za MA 39*

2 *Tini za MA 25*

3 *Tini za MA 49*

4 *Tini za MA 51*

5 *Tini za MA 19*

6 *Tini za MA 15*

7 *Tini za MA 61*

8 *Tini za MA 19*

9 WIPO, 2001: “Ripoti ya Tume ya Kutafuta Ukweli juu ya Mahitaji ya Mali za Kitaalamu na Matarajio ya Mabingwa wa Maarifa Asilia” Geneva.

## 9. Njia za Kienyeji katika Usuluhishi wa Migogoro Afrika

*Ben Fred-Mensah*

*Ben Fred-Mensah ni Profesa Msaidizi wa Uhusiano wa Kimataifa, Chuo Kikuu cha Howard, Washington*

Uhalali, usahihi, ufanisi, manufaa na uendelevu wa usuluhishi wa kienyeji<sup>1</sup> wa matatizo ya wenyeji ni mada za uandishi wa Tini sitini za MA. Yale yaliyohakikishwa kufaa katika nyanja za elimu, kilimo na usimamizi wa maliasili na afya, yanaonyesha ukweli kwa mifumo ya usuluhishaji wa migogoro katika Afrika.<sup>2</sup> Kushindikana kwa juhudi za kutatua migogoro katika Afrika katika ngazi ya taifa limekuwa tatizo kuu la kuzidi kuhusika kwa mashirika ya kanda, kampuni binafsi za majeshi, asasi zisizo za serikali (AZISE) na Umoja wa Mataifa, ingawa kwa mafanikio kidogo. Taratibu na njia za kisasa za usuluhishi wa migogoro kwa kawaida si uendelezaji au kukubaliwa na watu wake wa kawaida.<sup>3</sup> Kuna tofauti iliyo wazi au “muachano” kati ya filsofia na taratibu za usuluhishi wa migogoro wa kisasa na wav kienyeji. Nafasi ya usuluhishi wa migogoro ya Afrika kwa njia ya amani inaweza kuongezwa sana iwapo kanuni, maarifa, na njia za usuluhishi wa migogoro zitaeleweka na kulinganishwa na zile za sasa za serikali kwa ngazi ya taifa.

Tini za MA katika chapisho hili zinagusa vigezo muhimu vya mifumo ya kienyeji ya usuluhishi wa migogoro ya Afrika, taratibu, uunganishaji upya wa askari washirika na misaada kwa waathirika wa vita.

Mbali na migogoro inayojulikana, kama vile vita vya wenyewe kwa wenyewe Somalia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Liberia, Sierra Leone, Cote d'Ivoire, Guinea Bissau na Senegali, migogoro mingi ya nchi za Afrika ni ya kijumuia. Hutokea bara mbalimbali na mara chache huripotwiwa, ingawa ina kila dalili za kuendelea. Hupoteza maisha ya melfu ya watu, na kusababisha watu ndani ya nchi kukosa makazi na kuwa wakimbizi, na kuzuia shughuli za kiuchumi hivyo kuzuia taifa au jamii kupanua maeneo yake ya uzalishaji.<sup>4</sup>

Maswali machache makuu yanahitaji kupatiwa majibu: nini kilikuwa chanzo cha migogoro Afrika kabla ya ukoloni? Kulikuwa na njia zipi za usuluhishi wa migogoro? Migogoro ya Afrika zamani inalingana vipi na ile ya sasa? Kwa njia gani, kama ipo, uelewa wa njia za kienyeji za usuluhishi wa migogoro unaweza kupunguza migogoro iliyopo? Taratibu rasmi na moyo wa usuluhishi wa migogoro kienyeji zinaweza kurekebisha kuunda mfumo mpana zaidi wa usuluhishi wa migogoro? Je, njia za kienyeji zinaweza kuchanganywa na za kisasa na njia ngeni?<sup>5</sup> Je, kanda inaweza kuandaa

mfumo mbadala wa suluhisho la migogoro (ADR)<sup>6</sup> ambao utaiwezesha kumudu migogoro yake inayoongezeka na inayoonekana kuwa sugu?

### Migogoro katika Afrika ya asili

Sehemu muhimu ya utafiti wa anthropolojia katika maeneo ya Afrika inaweka msisitizo kwenye uratibu wa mwafaka ambamo jumua zinaonekana kuwa mifumo iliyoshikamana ambamo shughuli za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kidini hukamilishana na kuimarishana katika mpangilio mzuri na wenye amani. Uhusiano wa kutokana na ndoa, kwa mfano, au ushirikiano kati ya vikundi mbalimbali vya kikabila au nasaba, utaelekea kuendeleza kanuni fulani za kisheria ambazo huweka vikwazo kwa wanajamii ambao watachagua kutumia vurugu katika mgogoro wa maslahi.<sup>7</sup> Kukiwa na aina hii ya udhibiti wa jamii, migogoro ilisuluhishwa kwa kutumia taasisi za jamii, desturi, kanuni, maadili, imani, na taratibu za kimaadili, ambazo kimsingi husisitiza tabia ya usawa wa kijamii.<sup>8</sup> Hivyo, kazi za msingi za sheria zilikuwa kuzingatia maeneo ya manufaa ya pande mbili badala ya kuvutia kusababisha madhara kwa wengine.

Inathibitika wazi pia kuwa kama ilivyo katika jamii yoyote ya binadamu, migogoro ilikuwa sehemu ya jamii asilia za Kiafrika. Migogoro ingesababishwa na kuvunjwa kwa mkataba, wizi, kashfa na uchawi pamoja na tuhuma za uchawi. Inaweza pia kutokana na kutoelewana katika ndoa, watu kuumizwa, na uharibifu wa mali. Mapigano yanaweza kutokana na kutoelewana katika urithi na ugumu wa kugawa mipaka ya ardhi, na vilevile juu ya kushika uongozi wa kisiasa. Migogoro pia inaweza kutokea baina ya watu wa jamii mbalimbali au vikundi vya kikabila hasa juu ya haki ya umiliki wa maliasili na ufugaji wa wanyama.

Hivyo, utafutaji unaofaa wa mifumo mbadala inayofaa kwa usuluhishi wa migogoro ya Afrika lazima uanzie na usuluhishi wa tofauti hizi. Jamii nyingi za Kiafrika zimesisitiza mwafaka wa jamii kama itikadi muhimu sana ya udhibiti wa jamii. Haya yameonyeshwa vizuri katika nadharia na matumizi ya filozofia za *ubuntu* miongoni mwa jamii asilia za Afrika Kusini na *kanye ndu bowi*<sup>9</sup> miongoni mwa Buem wa mpakani mwa Ghana na Togo.

### Mifumo ya Kienyeji ya Kiafrika ya usuluhishi wa Migogoro

Mabaraza makuu ya kienyeji ya Kiafrika ya kushughulikia migogoro yamefupishwa hapo chini:

*Usuluhishi* ni baraza maarufu zaidi la kusuluhisha migogoro katika utamaduni wa Afrika. Wasuluhishi wakuu huwa ni wazee, viongozi wa kidini, na watu maarufu wanaojulikana kwa busara zao, ujuzi, na uaminifu katika wadhifa wao rasmi na utaalumu pamoja na shughuli binafsi. Watu hawa, ambao hutajwa kwingineko<sup>10</sup> kama *du nkuwo*, (au macho ya mji au jamii) hupata heshima kubwa katika jamii zao na wana uwezo wa kuwasihia watu walioshtakiwa wahudhurie kusikiliza mashtaka yao. Mara nyingi hutokea kwamba wakuu wa ukoo au watu maarufu walio mahiri katika ujuzi wa kujadiliana, kusihi, upatanishi, na kushauri mara nyingi hualikwa kusuluhisha migogoro nje ya ukoo wao au jamii. Usuluhishi kwa kawaida huepuka kuonyesha wazi nguvu, fikra za mshindi-mshindwa, makovu ya kijamii, na uchungu ambao kwa kawaida huambatana na hukumu. Wasuluhishi hutafuta suluhisho la jumla kwa sababu inaonekana kuwa rahisi, kuweza kubadilika, na kukubalika. Kama njia ya kutatua migogoro, usuluhishi husaidia kupata suluhu kwa majadiliano, suluhisho, kusihi, ushawishi, na makubaliano. Kwa kawaida, lilikuwa ni jambo la mantiki kwa watu kutafuta usuluhishi kwa sababu wasuluhishi kwa kawaida hutafuta usuluhishi wa migogoro kirafiki zaidi na usiokuwa wa kiadui ili kuendelea kuishi pamoja kirafiki.

*Hukumu* ni utaratibu ulio mpana zaidi kuliko usuluhishi. Kwa kawaida huendelea kwa hatua na kwa hali ya kawaida huhusisha uchunguzi wa karibu na kukusanya mashahidi na inapolazimu, vizibiti hutolewa kama ushahidi.<sup>11</sup> Watu kwa ujumla hupendelea usuluhishi kuliko hukumu, kimsingi kwa sababu usuluhishi si tu kuwa huchukua muda mfupi na rahisi, pia huepuka matokeo ya mshindi na mshindwa, ambayo hufanya upatanishi baada ya usuluhishi kuwa ngumu. Pia, kesi zilizofikishwa kwa ajili ya kupatiwa hukumu kwa kawaida ni pamoja na zile ambazo ama zimeshindikana kutatuliwa kwa njia ya usuluhishi au uamuzi au kikatiba zilijulikana kama jinai.<sup>12</sup>

Uamuzi wa kutumia *nguvu za miujiza* kutatua migogoro ilikuwa jambo la kawaida katika Afrika kabla ya ukoloni. Majaribu ya mateso yalikuwa ya kawaida ambapo kwa mambo ya miujiza kama mzimu kuonyesha hatia na/au kutokuwa na hatia lingeweza kufanywa. Kama ushahidi unaleta migongano kiasi ambacho waamuzi au wasuluhishi wakaona shida kufikia uamuzi waliweza kuamua kutumia majaribio ya mateso. Hizi kwa kawaida ni kesi ambazo ushahidi ulikuwa mgumu kukubalika kwa kutumia njia za kidunia.<sup>13</sup> Pia ilikuwa kawaida kwa watu kuamua kutumia uchawi/au ulozi kutatua migogoro katika Afrika. Watu waliweza kuamua

kutumia njia hizi za miujiza walipokuwa hawataki kuleta manung'uniko yao hadharani ili kurekebisha ama kwa hukumu au upatanishi. Kwa fikra za Kiafrika kwa ujumla, uchawi unahusishwa na matumizi ya miujiza kwa kushambulia adui, wakati matumizi ya uchawi ni pamoja na matumizi ya njia za miujiza na vifaa. Ufanisi na nguvu za uharibifu za uchawi na ulozi ziliaminiwa sana na kuogopwa katika jumua nyingi za Kiafrika.

Jamii na jumua za asili ya Kiafrika zimeshughulikia changamoto za kuendeleza uhusiano wa amani na koo nyingine majirani kwa kutumia *diplomasia*. Kushindwa kwa diplomasia kungesababisha vita au kuibuka upya na au ongezeko la migogoro. Waliosimamia juhudi za kidiplomasia ni wazee, au, kwa suala la mifumo imara ya kisiasa, wajumbe wa uongozi unaotawala. Wanadiplomasia hawa—mara nyingi hutajwa kama “matarishi,” “wataalamu wa lugha,” au “wapiga mbiu” walikuwa kama wapatanishi, watu ambao wamepata ujuzi wa aina yake katika matumizi ya lugha na wamejitokeza na kutambulika katika sanaa ya majadiliano, ushawishi, na upatanishi.<sup>14</sup>

Njia nyingine za usuluhishi wa migogoro katika Afrika ya asili ni pamoja na utenganisho, “kutukanana,” na uhusiano wa utani. *Utenganisho*, hujulikana kama “mgawanyiko” au “kujitenga” ilikuwa tabia ambayo kikundi kimoja au upande mmoja wa mgogoro kilihama na kujenga makazi mapya mahali pengine.<sup>15</sup> Jamii ziliamua “kutukanana” pale pande mbili za mgogoro zilipotaka kupunguza makali ya ugomvi, ambao, kama usipofanyika hivyo, unaweza kusababisha vurugu. Pande zinazohusika na mgogoro hupeana changamoto kwa kutumia nyimbo na maneno ya matusi. *Uhusiano wa utani* ulikuwa unasaidia kupooza hisia zilizochemka kama kutukanana. Pande mbili za mgogoro zilifanya mchezo wa kutukanana, lakini, zilipewa changamoto na jamii au jumua kubwa zaidi kuwa zisifikie hatua ya kupigana au kulipiza kisasi wakati wa utani kama huo. Kwa hakika, mtani alitakiwa kuwa mvumilivu kwa mtani wake. Wakati utani ulifanyika kwa watu wa jumua au jamii moja (kama ilivyo kwa Wafulbe wa Nigeria, Senegali na Niger), pia ulifanyika baina ya watu wa jamii au jumua tofauti (kama ilivyo kwa Wafulbe na Wativ wa Nigeria).<sup>16</sup>

**Uhusiano wa watu binafsi na jumua na usuluhishi wa migogoro.** Kulikuwepo uhusiano wa karibu baina ya watu na koo zao na/au hata jumua pana zaidi kuhusiana na usuluhishi wa migogoro. Kama kikwazo cha jina la ukoo au jumua, watu walitegemewa kuonyesha tabia nzuri katika masuala ya kijamii. Wanaukoo na wanajumua pia walitegemewa kuwa bega

kwa bega na mwanaukoo au mwanajumua aliyekuwa katika aina yoyote ya mgogoro. Wakuu wa koo hasa hutegemewa kuhakikisha kuwa mwanaukoo au mwanajumua yeyote ambaye ameshtakiwa kutokana na kosa lolote anahudhuria kusikiliza mashtaka yake na kulipa faini yoyote itakayopangwa na mahakama. Hivyo, uhalifu hasa ulipigwa vita vikali na viongozi wa ukoo na jumua kwa ujumla, ambao kazi yao ilikuwa kuwapatia viongozi wa umma msaada wa kuimarisha amani katika jumua.<sup>17</sup>

Katika mchango wake, Wolff ameelezea jukumu la usuluhishi wa migogoro wa miundo ya koo na itikadi yao ya msingi, alipojadili majaribio huko Eritrea kutoa ulinzi kwa maelfu ya watoto waliokuwa waathirika wa mgogoro wa kivita nchini humo uliochukua muda wa miaka thelathini.<sup>18</sup> Katika programu hii, si wanandugu pekee waliotafutwa ili wapewe jukumu la kuwalinda yatima hao, mpango mbadala ulibuniwa pia ambapo nyumba, zenye kufuata maadili na miundo asilia ya kifamilia, ziliundwa kwa ajili ya ulinzi wa watoto ambao wazazi na ndugu zao wa damu hawakuweza kupatikana.

Katika jamii/jumua nyingi za Kiafrika, mpango wa kijamii umeendelezwa kwa kutumia “adhabu halisi.” Hizi ni njia ngumu lakini iliyoenea ambayo wanajumua waliweza kunyooshwa kuheshimu kanuni za udhibiti wa jamii. Adhabu hizi halisi ni chanya—zawadi ya kiakili watu wanayopata wanapofuata tabia njema zinazokubalika—na hasi—hisia za kero za kimaadili wanazopata wanapotenda maovu. Hivyo, kuendelea kwa itikadi ya amani kama ilivyo kwa *kanye ndu bowi* miongoni mwa Wabuem<sup>19</sup> au *ubuntu* kusini mwa Afrika (imefananuliwa hapo chini) inahusisha msisitizo kuhusu visasili, imani, maadili na nia.

**Utekelezaji wa maamuzi ya mahakama.** Udhaifu wa mpangilio wa kisiasa na uwezo mdogo wa vyombo vya dola umeathiri utekelezaji wa maamuzi ya mahakama kabla ya ukoloni. Tofauti na mataifa ya sasa, jamii nyingi za Kiafrika kabla ya ukoloni zilikosa polisi walio na mpangilio rasmi na magereza.<sup>20</sup> Jamii hizi ziliendeshaje maamuzi yao ya kisheria ili kuwepo sheria na usalama? Utafutaji wa ufafanuzi kuhusu fumbo hili linalotatanisha unaelekeza umakini wetu katika vipengele vifuatavyo vya miundo ya kijamii.

**Kuaminika kwa asasi na watu.** Mafanikio ya kusuluhisha migogoro katika Afrika kabla ya ukoloni yaliyofanywa na wanasheria yangekidhi si matarajio pekee ya wagomvi kuwa mgogoro wao umesuluhishwa, lakini pia yangeimarisha mashtaka ya washtakiwa wao ambao maofisa wa kisiasa na kisheria wangetoa uamuzi wa migogoro mingine siku za baadaye. Jamii nyingi za

Kiafrika kabla ya ukoloni, viongozi wa kisiasa—machifu, viongozi wa dini za kale, wakuu wa koo, na watu mashuhuri—pia walikuwa viongozi wa mahakama, kama vile mahakimu, wasuluhishi, na waamuzi.<sup>21</sup> Kinyume na uzoefu wa sasa ambapo mkusanyiko wa nguvu kama hizo za kijamii unaweza kuwa mbinu za udikteta na udhalimu, viongozi wa kisiasa wa Kiafrika kabla ya ukoloni walitumia vyeo vyao katika usuluhishi wa migogoro kwa kuonyesha ujuzi, uwezo, na uaminifu wao, na kwa kufanya hivyo, waliongeza uhalali wao na uwezo wa kisiasa kwa watu wao.

**Muktadha wa mtazamo.** Katika Afrika kabla ya ukoloni, mwelekeo wa kifalsafa, ambao ulisimamia usuluhishi wa mgogoro katika mazingira ya watu wachache, ulikuwa muhimu kama ujuzi na msimamo wa kimaadili wa viongozi wasuluhishi wa migogoro. Kwa mfano, katika jumua nyingi za Kiafrika, pande zenye mgogoro hutaka kushinda maamuzi ya mahakama kuona mgogoro umetatuhiwa. Kwa mfano, Wativ wa Nigeria huamini kuwa “hakimu mzuri halazimishi uamuzi kuhusu pande mbili lakini huwaruhusu kushinda kama akiweza.”<sup>22</sup> Katika muktadha huu, maafisa wa kisiasa na kisheria walitegemewa kuhakikisha kuwa pande zenye mgogoro zingeshinda kwa kauli moja katika haki ya mfumo wa uamuzi wa mahakama.<sup>23</sup> Athari za utaratibu huu wa kiasili kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya kuleta amani kwa sasa katika kanda ni kubwa.<sup>24</sup>

**Matumizi au vitisho vya kutumia adhabu za kichawi** kwa pande zisizotaka kupatana na kufikia makubaliano ya amani vitu hivi vilikuwa muhimu. Kama mtu amekataa kufuata maamuzi ya mahakama, kiongozi mkuu na walio chini yake wanaweza, kwa maapizo kumlazimisha kufanya hivyo.<sup>25</sup> Kama uimarishaji wa utaratibu wa hukumu, maapizo yalitumika kama adhabu kali kuhakikisha utiifu wa maamuzi ya mahakama. Kwa kuwa dini za jadi Afrika zilikuwa zikiabudu mizimu, jukumu la nguvu za miujiza kuimarisha maamuzi ya mahakama katika kanda hazuwezi kuelezwa vingine zaidi ya kutekeleza jukumu la kusaidia wanaukoo au wanajumuia. Matambiko ya kidini na msaada wa jumua yalikuwa mambo muhimu katika marekebisho baada ya migogoro katika baadhi ya jumua huko Msumbiji na Angola, katika uchumi, siasa, na tiba ya kisaikolojia na kuwaunganisha waliokuwa wapiganaji na wahanga wa vita.<sup>26</sup>

Ufukuzaji ni utaratibu wa kisheria unaotumika dhidi ya wanajumuia ambao ni wahalifu sugu. Watu hawa—hujulikana kama “wahalifu”<sup>27</sup>—ni wahalifu wazoefu, wasiorekebishika, ambao wamezoea kuiba, kubaka, au kuua lakini hushindwa kuheshimu amri ya mahakama. Wabuem wa Ghana walifikiri kufukuza ni sawa na

kifungo cha maisha. Hii ilikuwa kwa sababu, mara anapofukuzwa, mtu huondolewa katika tukio lolote la kijamii, hivyo kuwa na hadhi ya “mtu asiyeweza kuvumiliwa kamwe,”<sup>28</sup> mtu aliyetengwa na jamii na laana kwa ukoo wake. Alikuwa “amenyimwa roho.”<sup>29</sup> Hivyo, hofu ya kutengwa katika mpangilio wa Afrika ya asili ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba iliwapatia viongozi wa jumua pale ilipotumika nafasi ya kulazimisha pande zisizokubali kupatana kufika mahakamani wenyewe kusikiliza mashtaka wanapoitwa na kuheshimu maamuzi ya mahakama.

Mara tu baada ya kupata uhuru wa kisiasa, mababa wa Afrika walikubali kuwepo “kutofautiana” kati ya utamaduni na mila za Kiafrika na zile zilizopandikizwa na wakoloni. Pia waliona haja ya kutumia taratibu asilia, maadili na alama zenye mantiki za kanda kama msingi wa kufanya mageuzi ya kisiasa, ujenzi wa taifa, na uanzishaji wa utawala wa kidemokrasia. Katika mtazamo huu Leopold Senghor alitunga nadharia ya “kujitambua kama mnegro au Unegro,” Kwame Nkrumah “Udhama-mira,” Julius Nyerere “Ujamaa,” na Keneth Kaunda “Utu.”<sup>30</sup> Majaribio kama hayo yanaweza kuonekana katika kuanzisha itikadi ya uhusiano wa damu wa Waafrika yaliyofanywa na viongozi wa Kiafrika baada ya ukoloni ili kuongeza uhalali wao. Kuanzia mhafidhina Houghuet-Boigny wa Cote d’Ivoire hadi Nkrumah wa Ghana mwenye siasa kali, viongozi wengi kati yao kwa njia moja au nyingine wameita itikadi ya uhusiano wa damu kama msingi wa kuunda utawala halali. Hii ilichukua muundo wa “sitiari ya baba na familia,” ambayo ilikuwa mtazamo wa utawala uliotokana na dhana iliyoungwa ya mamlaka na tabia ndani ya mifumo ya familia za Kiafrika.<sup>31</sup>

Mifumo ya kisheria ya taifa inatambua kuwepo kwa mifumo ya asili ya usuluhishi wa migogoro kwa uwezo wao mzuri katika masuala ya utamaduni na mila za wenyeji. Hata baadhi ya nchi zimeingiza mifumo hiyo katika sheria za nchi.<sup>32</sup> Hivyo, kesi zilizoonekana kufaa kuendeshwa chini ya sheria za asili huhamishwa kutoka mahakama za taifa kwenda katika mahakama za jadi kusikilizwa. Mahakama za jadi huonekana kuwa na uzoefu zaidi katika kesi zinazohitaji ujuzi wa mila na historia ya wenyeji tangu zilipoandikwa na wakuu wa makabila na wazee wao ndio wanaoweza kutegemewa kama vyanzo vya maarifa hayo.<sup>33</sup>

Hata hivyo, kumekuwa na matatizo katika utekelezaji wa juhudi hizi za kuweka sambamba sheria hizi. Hii ni kwa sababu baadhi ya taratibu za mifumo ya kisheria ya majimbo ya kikabila yapo katika migogoro isiyoweza kusuluhishwa na vyombo vya kisasa vya sheria vya



mataifa vilivyoweka mamlaka ya kisheria juu yao. Baadhi ya waandishi huamini kuwa utekelezaji wa sheria ya ardhi ya taifa pamoja na sheria ya asili ya ardhi inaweza kusababisha “utata baina ya sheria,” hali ambayo watu wawili au zaidi au vikundi vinaweza kutoa madai tofauti, ingawa halali, kwa sehemu moja ya ardhi kwa wakati mmoja. Hii imechangia kwa kiasi kikubwa katika sababu za migogoro ya jamii ambayo imeimeza sehemu kubwa ya jumua za Kiafrika vijijini. Kufuatia umuhimu uliopo wa ardhi katika maisha ya kiuchumi, kisiasa, na kijamii na kiutamaduni wa jumua hizi, migogoro inayotokana na matatizo ya kuamua haki ya ardhi inaweza kuonekana kuwa chanzo cha migogoro katika kanda.

## Hitimisho

Mawazo na mapendekezo yafuatayo yanaweza kuwa na manufaa kwa serikali za Kiafrika, wabia wao wa maendeleo, na wasomi wa Kiafrika wenye nia ya kusuluhisha migogoro ya Kiafrika:

1. Haipendekezwi kuwa matumizi ya jumla ya taratibu na mbinu asilia za Kiafrika zitatatua migogoro yote iliyopo katika kanda. Hata hivyo, watunga sera wa Afrika na washirika wao wa kimataifa lazima watafute njia ambazo masuala halisi ya taratibu za sheria za asili zinaweza kuchanganywa na kulinganishwa na zile za serikali za mataifa ya kanda na vilevile miongoni mwa mifumo kadhaa ya asili.<sup>34</sup>

2. Filosofa za asili pamoja na jukumu la kusuluhisha kama vile *ubuntu* katika fikra za Kamati ya Ukweli na Maridhiano ya Afrika Kusini (TRC) baada ya kuondoa siasa ya ubaguzi na pendekezo la kupitisha “gacaca” huko Rwanda lazima ikubalike, zimetumika kwa kuchagua, na mawazo yao yameingizwa katika sheria, siasa, na utamaduni wa uraia wa nchi. Kwa mfano, kuhusu Afrika Kusini fikra za TRC, matumizi ya mawazo ya *ubuntu*—msemu wa “mkusanyiko wa utu” ambao huishi katika maadili kama hayo kama umoja wa kikundi, makubaliano, kujali, kuona hisia za mwingine, ushirikiano, na umoja—yalilingana na lengo kuu la TRC, kujenga uhusiano usiokuwa wa kiadui baina ya wakosaji na wahanga wao.<sup>35</sup>

3. Watunga sera wa Afrika pia wanaweza kuangalia baadhi ya ubora unaovumilika wa taratibu za asili za Kiafrika za usuluhishi wa migogoro na kutafuta njia na jinsi ya kuzitumia katika sheria za sasa za usuluhishi wa migogoro katika kanda. Hizi ni pamoja na:

- utakatifu wa uongozi wa wasuluhishi au mahakimu kuhusu usahihi kimaadili unaonekana, kutoegemea

upande mmoja, na ukweli katika tabia zao binafsi na kikazi;

- majadiliano ya jumla na bila woga ya malalamiko yanayotolewa na wanaogombana, yatakayosababisha kiwango kikubwa cha makubaliano ya wote waliopo; na
- kukubali kwa upande ulioshindwa kuhusu haki ya upande ulioshinda na kukubali kwake usawa katika uendeshaji wa kesi.

4. Matumizi ya taratibu na maadili ya asili ya Kiafrika kama msingi wa maendeleo ya kisiasa, pamoja na usuluhishi wa migogoro, hayatoi mafanikio ya moja kwa moja. Haya yameonyeshwa na kiwango cha matatizo ya uongozi katika nchi nyingi za Kiafrika hata kama nchi nyingi kati ya hizi viongozi wao baada ya ukoloni kwa njia moja au nyingine walitumia taratibu na maadili ya asili lakini walishindwa katika wajibu wa kitabia uliohifadhiwa katika taratibu asilia na kanuni na maadili yao.

5. Kupitisha, kurekebisha, na kuendeleza taratibu za asili za Afrika za usuluhishi wa migogoro, masuala makuu matatu lazima yazingatiwe. Kwanza, kuna haja ya kuwa na mifano ya wajibu, kwa hali hii matumizi kamili ya wanaume na wanawake katika upatanishi. Watu hawa lazima wawe *du nkuwo* (macho ya jumua) ambao wamekubalika, si kwa ufanisi bora katika maeneo fulani ya juhudi za watu kama vile siasa, uongozi wa raia, usomi, jeshi, mapambano ya ukombozi, na biashara tu, bali pia kwa kuonyesha uadilifu ulio wazi. Pili, usuluhishi mzuri wa migogoro hutegemea uongozi bora. Tatu, serikali za Kiafrika na wakala mbalimbali wa ujamiishaji wa siasa katika kanda wanahitaji kuelimisha umma kwa ujumla na kizazi kipya hasa kuhusu taratibu muhimu za kiasili za maeneo ambazo zimerithishwa kwa miaka mingi.

Serikali za Kiafrika na asasi za kanda ya Afrika zinahitaji kupanga njia na nia ya kisiasa kutatua migogoro ya kutisha na inayorudisha nyuma maendeleo katika kanda. Kwa jumla, uwezo wa taifa au jumua kupitisha na kuimarisha sheria zinazoongoza tabia, ikiwa ni pamoja na usuluhishi wa migogoro, ni hatua isiyopingwa ya uwezo wake kimaendeleo.<sup>36</sup>

- 1 Kwa malengo ya makala hii, neno “asilia”, limetumika kwa kubadilishana na maneno “jadi”, “kawaida”, na “kabla ya ukoloni”
- 2 Neno “usuluhishi wa migogoro” limetumika katika makala haya kwa maana pana kuhusisha njia zote za usimamizi, ambazo huzuia, hupunguza, au hata husuluhisha migogoro. Hii pia ni pamoja na shughuli za baada ya mgogoro zinazotumika kuwaingiza upya, kuwaunganisha tena na kuwarekebisha wapiganaji na watu walioathirika na vita.
- 3 Woodman and Morse, 1987.
- 4 Fred-Mensah (1999).
- 5 Zartman, 2000, uk. 9
- 6 Nader, 1995, uk. 64.

- 7 Angalia Gluckham, 1965.
- 8 Bates, 1993.
- 9 Tini za MA 56.
- 10 Kouassi, 2000, uk. 64.
- 11 Swartz, 1966 Fred-Mensah, 2000, Tini za MA 56.
- 12 Fred-Mensah, 2000.
- 13 Radcliffe-Brown 1940, uk. Xviii. 1985, uk. 225.
- 14 Schraeder, 2000, kur. 74-77. Smith (1976), Adjaye, 1996, na Kouassi (2000).
- 15 Merry, 1989.
- 16 Wilson-Fall, 2000, kur. 55-56.
- 17 R.D. Cooter, op. cit., uk. 22.
- 18 Tini za MA, 50
- 19 Tini za MA 56.
- 20 Cooter (1996) citing J. Locke's *The second Treatise of Civil Government*.
- 21 J.F. Holleman (1974) kur. 16-17.
- 22 Tazama Bohannan, 1957.
- 23 Tazama pia Fred-Mensah, 2000, 2001, Tini za MA 56, 59.
- 24 Tazama Stedman *et al.*, 2002.
- 25 Tazama A.R. Radcliffe-Brown, 1940, uk. Xviii.
- 26 Tini za MA 10.
- 27 Radcliffe-Brown, cited by Gluckman, 1965.
- 28 Llewellyn and Hoebel, also cited by Gluckman, 1965.
- 29 Fred-Mensah, 2000, uk. 43.
- 30 Tazama Deng and Zartman, 1991, uk., 14.
- 31 Tazama Schartzberg, 1986, kur. 14-15.
- 32 Woodman and Morse, 1987.
- 33 Ghana, 1960, uk. 8.
- 34 Easton and Belloncle, 2001, kur. 170-179.
- 35 Tazama Masina, 2000, kur. 170-179.
- 36 Tazama Brautigam, 1996.

# 10. Maarifa Asilia: Mambo ya Usoni

*Nicolas Gorjestani*

*Nicolas Gorjestani, ni Mshauri Mkuu  
na Ofisa Mkuu wa Maarifa na Mafunzo  
katika Benki ya Dunia, Kanda ya Afrika*

Makala hii ya kuhitimisha inahakiki muktadha wa Mpango wa Maendeleo ya Maarifa Asilia ulioandaliwa na Benki ya Dunia pamoja na mafanikio yake kwa jumla, inajadili mafunzo makuu ya mpango huo yaliyojitokeza mpaka hivi sasa pamoja na kutayarisha mikakati ya kuuwezesha Mpango huo kusonga mbele katika siku zijazo kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM). Katika kufanya hivyo, makala inatumia mafunzo yaliyojitokeza kutokana na Tini 60 za MA pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na waandishi wachangiaji katika makala zilizotangulia na ambazo zimepangiliwa kwa kuzingatia dhamira mahususi, mwisho, makala inatumia uzoefu uliopatikana katika kipindi cha kwanza cha miaka mitano ya Programu ya Maarifa Asilia. Kwa pamoja, mambo yote haya yanadhihirisha yafuatayo: uko uwezekano mkubwa wa mafanikio endapo maarifa asilia yatatumika, maana ni chachu katika kuongeza uendeleo na msukumo wa jitihada za maendeleo, hali kadhalika, jumua yenyewe ya maendeleo haina budi kuunga mkono programu zinazosaidia kuziwezesha jumua za wenyeji wa mahali kushirikishana maarifa asilia pamoja na kuyatumia ili wapate matokeo bora zaidi ya maendeleo.

## **Muktadha**

Kama ilivyodokezwa katika utangulizi wa chapisho hili, Benki ya Dunia ilianzisha Programu ya Maendeleo ya Maarifa Asilia mwaka 1998 hatua hii ilikuja ili kukabili changamoto zilizotokana na matamshi ya viongozi wa serikali na jumua za wananchi kwa jumla katika mkutano mkuu wa Maarifa ya Dunia uliyofanyika Toronto Canada mwaka 1997. Kuanzishwa kwa programu hiyo kulitokea sambamba na kubuniwa kwa dira mpya ya Benki ya Maarifa. Kwa kuzingatia mazingira ya dira hii, na kwa kutambua kuwa benki hiyo ya maarifa haitakuwa tu ghala la maarifa ambayo yanaweza kuhamishiwa mahali popote ulimwenguni kwa matumizi, Benki ingetafuta uwezekano wa:

- Kuwawezesha wateja wake kutumia maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na maarifa asilia yaliyomo ndani ya jumua zao,

- Kusaidia katika kuwaunganisha wateja wake pamoja na kwenye vyanzo vingine vya uzoefu,
- Kujifunza kutoka kwa wateja na pia pamoja nao yale yanayowezekana katika mazingira yao pamoja na sababu zake.

Kwa “suala la biashara” uwezekano wa kutumia MA uko katika misingi ifuatayo: kwamba kuelewa vyema mazingira ya wenyeji kunaruhusu urekebishaji mzuri zaidi wa maarifa ya dunia; kwamba matumizi ya vyanzo vya maarifa ya wenyeji huongezea walengwa umiliki na hatimaye kuifanya miradi ifanikiwe na kuwa uendelevu;<sup>1</sup> kwamba kujifunza na kujenga kutokana na mifumo ya maarifa iliyomo ndani ya jumua za wenyeji, husaidia katika kuziwezesha jumua hizi kuimarisha fikra kuhusu fursa sawa katika uhusiano wao na serikali pamoja na wabia wa nje wa maendeleo yao; kwamba matumizi ya MA hayawezi kufanikiwa bila ya kuwako kwa ubia baina ya jumua zenyewe, serikali na jumua za wananchi, na baina ya wabia wa maendeleo na wanataaluma, ili kuwa na msingi wa matumizi bora ya maliasili adimu na unufaishaji wa wadau;<sup>2</sup> na muhimu zaidi, uwekezaji katika MA na uingizaji wa maarifa hayo katika programu za maendeleo ambazo zinasaidiwa na Benki pamoja na wabia wake wa maendeleo, ungesaidia katika kufikia lengo kuu la maendeleo ambalo ni kupunguza umaskini.

### Mafanikio

Wakati wa uzinduzi wa Programu ya maarifa asilia, Benki ya Dunia ilichapisha “Mwongozo wa Utekelezaji”<sup>3</sup> Mwongozo huu ulikuwa sehemu ya mkakati uliolenga katika uboreshaji wa viwango vya mipango ya maendeleo pamoja na uwezesaji wa jumua za wenyeji wa mahali kwa kuwashirikisha katika maeneo makuu matatu ya shughuli: (a) kuinua kiwango cha uelewa wao kuhusu muhimu wa MA; (b) kuimarisha uwezo wa wenyeji wa kuhifadhi na kubadilishana MA; na (c) kutumia wa MA katika Programu za maendeleo. Ufuatao ni muhtasari mfupi wa mafanikio ya awali wa mambo ambayo juhudi za programu ya MA zimeyapigania mpaka sasa.<sup>4</sup>

### *Kuuongeza utambuzi*

Umuhimu wa MA ndani ya mchakato wa maendeleo umezidi kuongezeka kama inavyoonekana kwa ushahidi huu ufuatao:<sup>5</sup> machapisho yanayohusu MA yameongezeka kwa kiasi kikubwa;<sup>6</sup> kumekuwa na ongezeko la kasi la mfululizo wa washiriki mbalimbali, AZISE na hata taasisi za utafiti, katika masuala ya MA; watendaji wa

shughuli za maendeleo pamoja na watoa maamuzi wanazidi kutambua kwamba MA ni chanzo muhimu cha maarifa ambacho hakitumiki ipasavyo<sup>7</sup>; MA yanazidi kupata umaarufu katika majadiliano kuhusu maendeleo ya dunia;<sup>8</sup> mivutano ambayo ilikuwa jambo la kawaida kuhusu MA, imepungua kwa kiasi ambacho wadau wa MA sasa ni pamoja na watendaji wa shughuli za maendeleo, watafiti na mabingwa wengine kutoka sayansi asilia na sayansi za jamii;<sup>9</sup> na jumua yenyewe ya maendeleo inaanza kutambua na haki za kitaalamu zinazohusiana na MA.<sup>10</sup>

Mabadiliko haya pia yanaonekana dhahiri kwenye Benki ya Dunia. Maarifa “Asilia” au “ya wenyeji wa mahali” yameongezeka katika machapisho ya Benki na mazungumzo yake na wateja wake. Hii ni tofauti na ilivyokuwa huko nyuma, ambapo Benki kwa kawaida ilizingatia zaidi maarifa ya “dunia.”<sup>11</sup> Hali kadhalika, katika kuonesha muhimu wa mifumo ya maarifa asilia, katika Mikutano yake ya mwaka 2001, ilisambaza kijitabu kiitwacho: “Mafunzo Kutokana na Jumua za Wenyeji wa Mahali: Changamoto na Fursa zake” ambapo ndani ya kijitabu hiki kilichosambazwa kwa wajumbe wa utawala wa Benki, mlikuwa na mifano mahususi ya mafanikio ya MA ambayo wajumbe walipewa wazingatie. Mwisho, mahitaji ya maandiko yanayohusu MA kutoka kwenye Benki yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku: tovuti ya Benki kuhusu MA ni ya pili kati ya zile zinazoangaliwa sana kwenye Lango Kuu la Benki ya Dunia, Ukanda wa Afrika;<sup>12</sup> na matoleo ya Kiswahili na Kiolof ya tovuti ya MA hupokea wasomaji kwa idadi takribani maradufu ya wale wa Kifaransa. Hii ni dalili ya kuwa kuna mwitikio mkubwa wa kupokea MA kwa lugha za wenyeji.

### *Kuimarisha uwezo wa wenyeji*

Kumekuwa na maendeleo makubwa ya kuimarika kwa uwezo wa jumua za wenyeji wa mahali na vituo vya MA katika ubadilishanaji wa uzoefu wa wenyeji katika kushirikishana mafunzo, maendeleo haya yanathibitishwa na yafuatayo: kuna urahisi sasa hata katika nchi za Kiafrika, wa kupatikana kwa taarifa zilizochapishwa za kumbukumbu mbalimbali, hali hii imetokana na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za mtandao wa Intaneti, huduma za mtandao za washiriki wa MA zinaongezeka kwenye nchi mojambo na hata katika kanda (vyama vya waganga wa jadi nchini Uganda, Tanzania pamoja na nchi nyingine, vyama vya kanda vya uwindaji wa jadi huko Afrika Magharibi, n.k.), vituo vya ukusanyaji na usambazaji wa kumbukumbu vimeanzishwa katika jumua za wenyeji, (k.m. nchini Uganda);

### Jedwali 1. Mifano ya matumizi ya MA katika miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia

Mradi	Nchi	Kipengee husika cha MA
Mradi fungamani wa maendeleo ya hatua za awali za utoto	Eritrea	Kukusanya na kusambaza shughuli za kijadi kwa kuzingatia migogoro ya nyuma
Mradi wa lishe na maendeleo ya hatua za awali utotoni	Uganda	Kubadilishana mafunzo ya shughuli za MA katika miradi ya maendeleo ya hatua za awali utotoni nchini India Sri Lanka pamoja na matumizi ya ICTS
Mradi wa hatua za Awali utotoni	Kenya	Kubadilishana mafunzo ya shughuli za MA katika miradi ya maendeleo ya hatua za awali utotoni nchini India Sri Lanka pamoja na matumizi ya ICTS
Mradi wa chachu ya maendeleo ya wanawake	Ethiopia	Shughuli asilia za wanawake zilizokusanywa na kuunganishwa: uzoefu wa miradi midogomidogo ya SEWA huko India uliohamishiwa Ethiopia
Mradi wa II wa utafiti wa kilimo na mafunzo	Uganda	Shughuli asilia za kilimo zilizounganishwa na upelekaji huduma kwa wahitaji pamoja na programu za usambazaji
Mradi wa taifa wa huduma za ushauri wa kilimo	Uganda	Msaada kwa ajili ya huduma za ugani kwa wakulima
Mradi wa taifa wa utafiti wa kilimo	Kenya	Shughuli asilia za kilimo zilizounganishwa na upelekaji huduma kwa wahitaji pamoja na programu za usambazaji
Mfuko wa kijamii wa Malawi (MASAF 3)	Malawi	MA ni chombo cha mawasiliano kwa ajili ya uwezesaji na maendeleo ya jumua
Mfuko wa Jamii wa Uganda Kaskazini (NUSAF)	Uganda	Kutumia MA katika kuhamasisha ujenzi mpya wa jumua zilizoathiriwa na migogoro ya vita
Mradi taifa wa huduma za ushauri wa kilimo	Uganda	Kuweka vidokezo vya MA vinavyoonesha kuridhia wakulima katika huduma zao za ugani
Mchakato wa PRSP/CAS	Kenya	Kuainisha nafasi ya asasi za wenyeji zenye ushiriki na uwazi wa huduma
Programu ya VVU/UKIMWI Ya Nchi nyingi pamoja	Burundi	Kutumia MA kusaidia Wenyeji kupambana na VVU/UKIMWI kwa kushirikiana na Waganga wa jadi
Programu ya VVU/UKIMWI Ya Nchi nyingi pamoja	Guinea	Kutumia waganga wa jadi ili kusaidia kupunguza maambukizi yanayohusiana na VVU/UKIMWI
Mradi wa Uhifadhi na Matumizi Endelevu ya Mimea ya Dawa	Ethiopia	Kipengee cha MA kitasaidia ukusanyaji na uchambuzi wa data kuhusu manufaa ya mimea yenye sifa za dawa
Mradi wa Uhifadhi wa Bioanuai katika Savana	Ghana	Kukuza moyo wa uhifadhi na matumizi endelevu ya mimea yenye sifa za dawa

kubadilishana kikanda mafunzo yanayotokana na MA kumejenga mazoea ya kusambaza shughuli za asili;<sup>13</sup> na kushirikiana maarifa kati ya jumua moja na nyingine pamoja na kubadilishana mafunzo ndani ya kila nchi na baina ya nchi mbalimbali (C2C) kumeimarisha uwezo wa wenyeji wa kujifunza kutoka kwa wenzao.

Hii 2C2 inawakilisha moja ya mbinu bora za kushirikishana mazoea asilia ambayo ni maarifa yenye nguvu kimaudhui. Kwa mfano, huko Afrika ya Kusini C2C ilikuwa na matokeo makubwa katika uboreshaji wa hali za washiriki. Washiriki walijifunza kwa kutumia C2C, namna ya kuboresha mikakati ya masoko na wakafanikiwa kupata mkataba mkubwa wa kuuza mazao

yao ya bishara nje.<sup>14</sup> Mapato kutokana na mauzo yale yalikuwa mengi zaidi yakilinganishwa na gharama ndogo ya utayarishaji na uuzaji. Mafunzo ya uzoefu kutokana na C2C kadhaa, pamoja na vidokezo vya mbinu zenye mafanikio kwa maandalizi, usimamizi na tathmini ya C2C, vimeandaliwa kuwasaidia washiriki katika kupanga mabadilishano hayo.<sup>15</sup>

### **Kutumia MA katika maendeleo**

Ziko jitihada za wazi zinazoongezeka za uingizaji wa MA katika programu za upunguzaji wa umaskini kwa lengo la kuleta ufanisi bora zaidi kama inajidhihirisha katika matokeo yafuatayo: nchi kadhaa zimeanza mchakato wa maandalizi ya mikakati ya MA kwa njia ya warsha za kitaifa na matukio mengine (k.m. Uganda imemaliza mkakati wa MA kitaifa na Burkina Faso, Malawi, Mali, Kenya, Sri Lanka na Tanzania zimefanya warsha za kusaidia uzinduzi wa mchakato); nchi chache zimekwisha ingiza MA katika programu zao za upunguzaji umaskini (kwa mfano, Mpango wa Utekelezaji wa Uondoshaji wa Umaskini Uganda (PEAP) umeingiza MA kama kipengee cha sayansi na teknolojia; jimbo la Kerala huko India linaingiza MA katika Mpango wake wa 10 wa kila Miaka Mitano n.k.) na miongozo ya uingizaji wa MA katika upangaji na maandalizi ya miradi imetayarishwa kwa kushirikiana na CIDA, ILO na Mpango wenyewe wa MA.<sup>16</sup> Baadhi ya asasi za kikanda pia zimeanza kuingiza MA katika mikakati yao, (kwa mfano, SADC imejumuisha MA kuwa kipengee kimojawapo chini ya sayansi na teknolojia katika Mpango wa Mikakati wa Maendeleo wa Kanda).<sup>17</sup>

Hatua zilizopatikana katika uingizaji wa MA katika juhudi za maendeleo zimeonekana kuongezeka pia kwenye miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Iliyokuwa, miaka mitano iliyopita miradi michache sana ilikuwa na kipengele maalumu kilichohusiana na MA, hivi leo, zaidi ya miradi ishirini na nne ambayo ama iko katika kutekelezwa au kuandaliwa ina vipengele maalumu vya MA. Jedwali la 1 linaonesha baadhi ya miradi hiyo barani Afrika.

### **Mafunzo na Changamoto.**

**Kujifunza MA kunasaidia kujenga mbinu mchanganyiko katika jitihada ya kuleta maendeleo.**<sup>18</sup> Mbinu hizo mchanganyiko husaidia uwezesaji wa jumua za wenyeji wa mahali na huwajengea msingi wa kuleta mabadiliko. Mbinu hizo huhusisha jitihada za

### **Wakunga wa jadi na wafanyakazi wa Afya wanashirikiana kuokoa maisha huko Uganda vijijini**

Katika wilaya ya Iganga nchini Uganda, mradi unaofadhiliwa na UNFPA (maarufu kwa jina la MWOKOAJI) uliwapatia wakunga wa jadi teknolojia ya kisasa ya mawasiliano kwa nia ya kutafuta mbinu za kupunguza vifo vya kina mama wajawazito. Mradi ulihakikisha kuwako kwa mfumo wa mawasiliano ya redio ambayo yaliambatana na kuwako kwa vituo vya msingi ndani ya Kituo cha Afya cha Msingi, vyombo vya mkono vya mawasiliano kwa ajili ya wakunga wa jadi, gari la kuchukulia wagonjwa na akiba ya kuaminika ya damu. Mawasiliano ya kuaminika na vyombo vya usafiri vinavyounganisha walipo wakunga wa jadi na vituo vya afya ni mambo yaliyosaidia katika kuhakikisha kuwa wagonjwa waliohitaji utaalamu zaidi walifikishwa mapema kutakiwako. Papo hapo, utoaji wa huduma kwa wagonjwa uliimarika zaidi na zaidi kwa kuwafikia akinamama wengi zaidi. Kuunganishwa kwa wakunga wa jadi na wafanyakazi wa afya kumenyanyua mifumo yote miwili: maarifa asilia na maarifa ya kisasa. Matokeo makubwa ya mradi ni kule kupungua kwa vifo vya akinamama wajawazito. Inasemekana vifo hivyo vilipungua kwa zaidi ya asilimia 50 katika kipindi cha miaka mitatu, yaani, robo tatu ya Lengo la Maendeleo la Melenia la mwaka 2015!<sup>22</sup>

kujifunza undani wa mazingira kimaumbile, uhusiano wa watu kijamii, uchumi wa wenyeji, historia na utamaduni pamoja na maarifa ya jumla yaliyo sehemu ya uzoefu wa jumua. Matumizi ya mbinu jumuishi kama hizi husaidia uelewa bora zaidi wa hali halisi ya wenyeji kwa ukamilifu; kubuni mipango endelevu na yenye kuzaa matunda; kujifunza kutokana na jumua na kuzisaidia jumua kujifunza mazoea ya dunia na kuyatumia ipasavyo. Matokeo yake, mchakato wa maendeleo huwa imara zaidi na wenye kuzaa matunda. Aidha, kwa njia hii, utapatikana urari wa dhana za maendeleo za “wageni” na “wazawa” katika maendeleo.<sup>19</sup>

Kwa kutokana na asili jumuishi ya MA, ubadilishanaji wa taarifa zake unaweza kuwa na thamani ambayo ni zaidi ya mazoea fulani mahususi. Uvushaji na upashanaji wa taarifa jumua kwa jumua, yaani C2C, uliogusiwa huko nyuma, kwa mfano, umeonesha kwamba washiriki hawajifunzi stadi maalumu au mazoea fulani tu, bali pia, na muhimu zaidi, huzingatia mbinu tofautitofauti za

kupatia ufumbuzi wa matatizo. Mbinu hizo huwaibulia fursa ya kufikiria kwa makini mikakati yao wenyewe kwa kulinganisha na ile mipya wanayopata katika muktadha wa shughuli mahususi. Hivyo C2C imeonesha uwezekano mkubwa wa kuziwezesha jumua za wenyeji wa mahali na kuzisaidia kwa kuimarisha pumzi ya kuleta mabadiliko zaidi ya kujifunza teknolojia maalumu iliyopo. Kwa kuwa maendeleo, kwa dhati yake, ni mchakato wa mabadiliko yanayotakiwa, mbinu zilizofafanuliwa hivi punde, zitachangia kikamilifu katika kufikia malengo ya msingi ya jumua.

**MA hufungamana sana na mazingira maalumu na kwa hivyo yasingeweza kuigizika isipokuwa kama yangerekebishwa au yangechanganyika na mifumo mingine ya maarifa.** Kwa maana yake, MA ni ya mazingira maalumu.<sup>20</sup> Kwa sababu hiyo, yana miiko yake inayohusiana na uvushikaji wake kutoka mazingira mengine na uenezaji. Kinachofanikiwa katika mtaa fulani au ndani ya jumua moja kinaweza kusifanikiwe kwingine.<sup>21</sup> Hata hivyo, baadhi ya shughuli asilia huweza kurekebika kwa ajili ya matumizi ya mazingira mengine ya kitaasisi au ya kijamii-utamaduni au yanaweza kunyanyuliwa kiwango kwa kuchanganywa na ya mifumo mingine hadi yakaleta matokeo ya sifa. Sanduku la hapa chini linaonesha jinsi msukumo wa maendeleo uliotokana na wenyeji ulivyofanikiwa katika wilaya ya Iganga huko Uganda, inasemekana wilaya hiyo ilipata mafanikio katika kupunguza vifo vya akinamama wajawazito kwa asilimia 50 katika kipindi cha miaka mitatu, kwa matumizi ya teknolojia rahisi ambayo ilinyanyua ubora wa maarifa asilia pamoja na mifumo ya maarifa ya kisasa. Mifano hii ya mafanikio inaweza kuigizwa katika jumua nyingine (nchini Uganda pamoja na nchi nyingine) zenye sifa zinazofanana (k.m. sehemu zenye waganga wengi na wakunga wa jadi katika maeneo ya vijijini.)

**Uhalalishaji wa MA ni muhimu katika kuthibitisha matokeo na thamani yaliyo nayo endapo yatapelekwa kwingine, ila inahitajika itifaki inayoendana na hali maalumu ya MA na inayoweza watumiaji wake.** Wanasayansi wanaotilia shaka uhalali wa uzoefu wa watendaji asilia huelekea kudai kwamba “wingi wa vituko si ushahidi.” Ziko njia mbili za kuijibia changamoto hii. Njia ya kwanza (ambayo ni maarufu kuliko hiyo nyingine) ni kutaka uzoefu huo upimwe na kuthibitishwa kwa mbinu za utafiti na kufuata taratibu zote za uchambuzi wa kisayansi. Mathalani, baadhi ya nchi zimewekeza katika uanzishaji wa maabara ya kifamasia kwa ajili ya uchambuzi wa mimea ya dawa ili kugundua thamani ya mimea hiyo katika tiba; wengine wamewekeza katika utafiti wa mifumo ya kilimo kwa nia ya kuelewa mifumo asilia ya

mbegu zinazostawi katika maeneo husika.<sup>23</sup> Kwa bahati mbaya, matokeo ya jitihada hizi hayakuwa ya kuridhisha. Jitihada hizi zimeleta mapendekezo machache sana yenye mashiko ambayo yanaweza kuwafaa watendaji wa asili. Kwa mfano, mabwana shamba wanaendelea kutilia mkazo jumbe zinazohusiana na mazao “makuu” kwa kuzingatia kanuni za utaratibu wa uhusiano wa pembejeo-mazao.

Hata hivyo, bado inabakia haja ya kuweka kumbukumbu na kuthibitisha madai kuhusu taathira ya MA, hususani katika maeneo kama vile tiba za jadi ambazo huhusisha maisha ya watu. Mtu anajuaje kuwa ni kweli dawa fulani inaponya na mimea itumikayo ni salama? Iko haja ya kutengeneza taratibu zitakazotumika kwa kulingana na sifa mbalimbali za umahususi wa MA. Jitihada za hivi karibuni katika suala hili zimeonesha dalili za kupatikana kwa maendeleo ya kuridhisha. Mathalani, Mpango wa MA umeanzisha ubia wa mwanzo baina ya kundi la kupambana na UKIMWI la Tanga, nchini Tanzania na Taasisi ya Afya kitaifa ya Marekani ili washirikiane katika uthibitishaji wa nguvu za dawa zinazotumiwa na waganga wa jadi kutibu magonjwa dowezi yanayowapata maelfu ya watu wenye VVU/UKIMWI katika wilaya ya Pangani. Mfano mwingine wa taratibu hizo unahusu utayarishaji wa mwongozo ambao kwa huo Shirika la Afya Duniani (WHO) linataka utumike kuamulia namna bora za kuhakikisha usalama, nguvu na viwango vya ubora wa mimea yenye sifa za dawa.<sup>24</sup>

Njia ya pili ni kuweka taratibu za maadili kwa watendaji wa jadi wote wa MA ambazo hulingana kitaifa na pengine kimataifa. Njia hii ya pili inaweza kuwa na manufaa zaidi ya uwezeshaji wa wenyeji wanaohusika na MA. Mathalani mafanikio ya dawa za kisasa hutokana na utaasisishaji wa vyombo vya weledi wa tiba vyenye taratibu, wakala za kiserikali na zifaazo kwa tasnia yenyewe. Vyombo hivi vya wataalamu na jumua zinazojishughulisha na tiba zimeunda viwango na maadili yao. Hatua hii ambayo kwa sehemu kubwa imeleta mafanikio, husaidia katika udhibiti wa matumizi mabaya, kughushi na uovu wa namna yoyote.

Hata hivyo, kwa upande wa watendaji wa jadi, uwakilishi wa aina hii ni wa nadra kuliko kawaida (k.m. katika baadhi ya nchi kuna vyama vya waganga wa jadi). Pamoja na matatizo yote hayo ziko dalili za maendeleo. Kuna mtandao wa dunia nzima unaoibuka wa vituo vya rasilimali ya MA. Huu ni mtandao wa taasisi za kitaaluma, AZISE, jumua za wananchi na watu binafsi wanaojishughulisha na utafiti huu, ukusanyaji kumbukumbu, uenezaji na utetezi wa MA. Mitandao ya

kikanda imeanza kuibuka pia. Miongoni mwa mitandao hiyo ni Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi Kiikolojia maarufu kama PELUM. Mtandao huu umeanzishwa katika baadhi ya nchi za Afrika Mashariki na Kusini kwa ajili ya kushirikishana na kuunganisha uzoefu, stadi na maarifa katika shughuli za kilimo cha wakulima wadogowadogo vijijini.

Mitandao yenye vuguvugu kubwa na yenye kuendeshwa na wananchi wenyewe inaweza kufanya kazi nzuri ya uenezaji na utetezi wa MA. Hata hivyo, mpaka hivi sasa wenyeji watendaji wa jadi hawana umoja; kila mmoja na lwake, tena wanashindana wao kwa wao au “kulinda” maarifa yao kwa kutumia mipango ya siri au kushirikisha watu waliomo katika familia zao tu. Matokeo yake ni kwamba watendaji wa jadi wa MA hawashirikishwi kikamilifu katika mijadala inayohusu maarifa na bado hawana mkakati mzuri wa kuwawezesha kufundishana kwa lengo la kupanua maarifa yao. Hali hii huwafanya watendaji wazuri wa kijadi kutofahamika (na kutuzwa) nje ya sehemu zao. Aidha hupunguza kasi ya kuwagundua watendaji matapeli na hivyo kuchafua jina zima la utaalamu wa jadi.

Mbinu mbili zilizotajwa hapo juu hazitofautiani moja kwa moja na utafiti unahitajika kama vile utetezi unavyohitajika. Hata hivyo, bila ya utetezi kwanza utafiti hautaweza kufanikiwa kufikia lengo kuu la watendaji wa jadi: kazi zao kutambuliwa kama zenye uwezo na za kitaalamu. Watendaji wa jadi watakaopewa uwezo kwa kutamubaliwa ndio watakaoshirikiana na jumua ya watafiti katika kuhimiza mambo yao na kutafuta mbinu za kulinda haki zao za kitaalamu. Aidha watashirikiana na watunga sera pamoja na wawakilishi wa sayansi zinazokubalika. Wabia wa maendeleo wanaweza kuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha mchakato huu.

**Kapanga mbinu za kiubunifu kwa ajili ya kulinda haki za kazi za kitaaluma zinazohusiana na MA ndiyo changamoto kubwa inayoikabili jumua ya maendeleo ya dunia.** Mikabala (mbinu) ya kiubunifu inatajikana kwa sababu taratibu zilizoko zinaweza zisifae kwa masuala ambayo ni maalumu kwa MA tu. Kwa mfano, MA kwa kawaida huhifadhiwa kwa njia ya simulizi za mdomo na kimatumizi badala ya maandishi. Kwa kawaida maarifa haya huibuka hatua kwa hatua na ni nadra sana yakahusisha michakato ya kiviwanda. Aidha sio rahisi kumtambua mgunduzi binafsi wa maarifa haya. Hizi zote ni sifa muhimu katika mchakato wa kubainisha haki miliki ya mchakato au ya teknolojia chini ya kanuni zinazotawala sasa haki ya mali za kitaalamu (IPR). WIPO ambaye ni mbia katika programu ya MA, imekuwa msitari wa mbele katika kuendeleza mdahalo wa dunia na ubia kuhusu

changamoto ya namna ya kupata mkabala wa kiubunifu kwa ajili ya haki ya mali za kitaalamu za maarifa asilia.

Yako maeneo kadhaa ambayo yakichukuliwa hatua kwa vitendo, yanaweza kusaidia katika kulikabili suala hili. Katika eneo la uhifadhi, jumua za wenyeji zingeweza kutiwa msukumo wa kutangaza na kusajili shughuli zao za kijadi. Mifano ipo<sup>25</sup> ya uhifadhi ambayo haina gharama kubwa wala ugumu wa kutekelezeka. Mikataba ya Kuhamisha Vitu ni njia nyingine ya kulinda MA. Mikataba hii inahusisha kupatiana (sampuli ua taarifa) kwa ajili ya kubadilishana na fedha au manufaa mengine yasiyo ya kifedha. Mifano ya mapatiano ya haki katika ushirikishanaji baina ya watumiaji na walinzi wa MA huweza kupatikana katika nchi kadhaa hivi leo. Mathalani, serikali ya Cameroon, inasemekana kuwa, imeingia mkataba na Taasisi ya Taifa ya Kansa huko Marekani, baada ya kugunduliwa kwa aina ya mmea wa msituni ulioonesha kuwa na nguvu za kikemikali za kupambana na UKIMWI. Cameroon inatoa mimea hiyo kwa malipo ya fedha ambayo inatumika katika miradi ya maendeleo ya jumua.<sup>26</sup>

Mikataba ya kanda pia ingeweza kusaidia upatikanaji wa ulinzi wa gharama ndogo wa mali za kitaalamu kwa ajili ya jumua za wenyeji wa mahali. Mathalani, Mikataba wa Andes wa 1996 ulioridhiwa na Bolivia, Colombia, Ecuador, Peru na Venezuela huwezesha mamlaka ya kitaifa na jumua za wenyeji katika kila nchi kuwa wamiliki halali wa maarifa na rasilimali za kijadi, kwa mujibu wa mkataba huo, wao hutoa kibali cha matumizi ya maarifa na maliasili zao kwa mapatano ya mabadilishano ya haki.

Haja ya MA ya kulishupalia suala la haki ya mali za kitaalamu (IPR) isiwe kikwazo cha maendeleo na utekelezaji wa miradi ya MA yenyewe ambayo ina manufaa kwa jumua pamoja na mchakato mzima wa maendeleo. Hata hivyo, baadhi ya asasi zilizo ndani ya jumua zenyewe pamoja na AZISE huendelea kuchukua hadhari kubwa kuhusu sababu ya maslahi ya wabia wa maendeleo katika MA. Moja ya hofu zao ni kwamba wabia hao wanaweza kuwapora wenyeji maarifa yao (pamoja na mazao ya maarifa hayo, michakato yake, haki kadhaa na manufaa mbalimbali). Ingawa hakuna anayetilia shaka ile haja ya, na muhimu wa, kuwa na haki ya kumiliki mali za kitaalamu, lakini wabia wa maendeleo, pamoja na watu wa serikali hawana budi kukumbuka, bila ya makosa, kuwa MA ni rasilimali iliyo hatarini kutoweka kama haitahifadhiwa, ikafanyiwa uchambuzi na kukosolewa, ikaenezwa na kurekebishwa.<sup>27</sup> Changamoto inayoikabili jumua ya maendeleo ni kubuni mkabala usio na upendeleo ambao utasimamia uhifadhi wa mifumo ya MA na wakati huohuo kulinda wamiliki wake.



## Jedwali 2. Mchango unaoweza kutokana na MA katika kufanikisha Malengo ya Maendeleo wa Milenia (MMM)

Malengo ya Maendeleo ya Milenia	Mifano ya MA	Vyanzo
<b>Ondoa umaskini na njaa</b>	Katika jimbo la Uta Pradesh nchini India, wakulima walitumia maarifa ya asilia na ufundi wao katika kuongoza tija katika kilimo na mapato yao kwa asilimia 60 katika kipindi cha miaka mitano.	<i>Tini za MA Na. 45</i>
<b>Jenga uwezo wa kutoa elimu ya msingi kwa wote</b>	Katika Afrika ya Magharibi, matumizi ya lugha za wenyeji kwa kufundishia kumefikishia watu wengi wa vijijini ujuzi wa kusoma na kuandika pamoja na vijana wengi kupata ajira ya ualimu.	<i>Tini za MA Na. 5</i>
<b>Hamasisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake</b>	Wanawake ni chachu kubwa ya kuleta mabadiliko ya kijamii kote barani Afrika. Nchini <i>Senegali</i> , wanawake wa Malicounda walijiwezesha kukomesha mila ya wenyeji ya ukeketaji.	<i>Tini za MA Na. 3</i>
<b>Punguza vifo vya watoto</b>	Kote barani Afrika, jumua za wenyeji hutumia mazoea asilia ya kulea katika kuongeza lishe ya watoto zaidi ya maziwa ya mama. Huko <i>Ethiopia</i> , dawa za jadi hutumika katika tiba ya magonjwa ya kawaida ya watoto.	<i>Tini za MA Na. 35</i>
<b>Inua kiwango cha afya ya kina mama wajawazito</b>	Nchini <i>Uganda</i> , wakunga wa jadi, kwa kushirikiana na watumishi wa vituo vya afya, kwa kutumia Teknolojia ya habari, walisaidia katika kupungua kwa vifo vya kina mama wajawazito kwa zaidi ya asilimia 50 katika kipindi cha miaka mitatu.	<i>Tini za MA Na. 40</i>
<b>Pambana na VVU/ UKIMWI, malaria na magonjwa mengine</b>	Nchini <i>Tanzania</i> waganga wa jadi wamefanikiwa kutibu maambukizi dowezi ya wagonjwa 4,000 wa ukimwi na hivyo kuwarefushia maisha.	<i>Tini za MA Na. 51</i>
<b>Hakikisha kuwako kwa mazingira endelevu</b>	Jumua za vijijini huko <i>Msumbiji</i> zinasimama kidete kulinda misitu ya ufukweni isifyekwe ovyoovyo kwa kutumia masimulizi ya jadi pamoja na miviga yao. Kwa njia hii mali hizi asilia huendelea kuwako hadi vizazi vijavyo.	<i>Tini za MA Na. 46</i>
<b>Jenga ubia wa maendeleo katika kiwango cha dunia</b>	Kikosi cha wataalam wa MA kutoka Afrika ya Mashariki hutembelea wenzao huko Asia ya Kusini kujenga ubia wa kupatia ushirikiano wa Nchi Kusini ya shughuli zinazohusiana na MA.	<i>Tini za MA Na. 55</i>

### Mambo ya usoni

Mambo yaliyo kwenye chapisho hili yanaonyesha kuwa katika miaka michache iliyopita kumekuwepo na maendeleo mazuri katika uwekaji wa MA katika ajenda ya maendeleo: utambuzi wa thamani ya MA katika mchakato wa maendeleo unaongezeka; ingawa ushirikishanaji wa MA unaovuka mipaka ya nchi na jumua limekuwa ni suala la wataalamu zaidi kuliko watendaji wa jadi wenyewe. Haya ni mabadiliko ambayo yanakwenda polepole, lakini pia kuchanganywa kwa MA katika mchakato mzima wa maendeleo kunaanza kujitokeza. Hata hivyo, jambo la msingi ni kwamba, kuna mambo mengi yanayopaswa kufanya ili kuimarisha mabadiliko hayo yaliyopo sasa na kupanua wigo wa mabadiliko hayo pamoja na upeo wake. Baadhi ya maeneo yanayohitaji hatua za haraka yamo katika sehemu za

mwanzomwanzo za chapisho hili zinazohusu mafunzo na changamoto. Ni dhahiri kuwa, wahusika wa msingi ni jumua zenyewe na watendaji wake wa jadi. Hata hivyo, serikali zinazohusika pamoja na wabia wao zinaweza kuchangia vyema katika ufanikishaji kwa kuwasaidia wadau hao katika sera, programu, tafiti pamoja na kuwaonya inapobidi lakini kwa malengo maalumu.

Je, itakuwa ndoto ya kweli kufikiria kuwa miaka mitano ijayo, mafunzo ya MA pamoja na ushirikishaji wa mazoea yake ndani ya programu za maendeleo utakuwa mtindo utakaokuwa umekubalika badala ya kuwa jambo linalopuuzwa kama hali ilivyo sasa? Tuangalie, ajenda ifuatayo yenye vipengele sita, inayotangaza vitendo ambavyo serikali na wabia wanapaswa kutekeleza ili kuiota ndoto hiyo. Mpango wa MA umejitoa kwa dhati kuunga mkono ajenda hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine wanaohusika. Misingi ya ushirikiano itakuwa

kufuata kanuni zenye manufaa kwa kila upande pamoja na ushirikishanaji wa uzito wa majukumu.

### **1. Kutia nguvu shughuli za MA zilizofanikiwa ili kufikia Malengo ya Maendeleo Milenia**

Uko ushahidi kamili kuwa miongoni mwa njia bora za kuziwezesha jumua ni kuzipa fursa ya kutumia mazoea yao asilia katika shughuli za maendeleo ambazo zinawagusa moja kwa moja. Ingawa kuna mvuto wa taasisi za wenyeji wa mahali pamoja na serikali, ambao unatilia mkazo kuingizwa kwa MA ndani ya programu na miradi, lakini, viwango hivyo vya mvuto unaokua vinahitilafiana. Kwa upande mmoja, hali hii inatokana na baadhi ya serikali kutokuwa na hakika bado na dhamira ya kujitoa kwa dhati kwa wabia wa nje wanaounga mkono shughuli za aina hii, ambao wanaweza kuwa na shaka kuhusu matunda ya njia nzima inayotumiwa. Jedwali (2) linaonyesha wazi jinsi ambavyo MA yanaweza kutoa mchango wa hakika katika ufanikishaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM). Mifano hii ifuatayo inaonyesha kuwa ikiwa MA yatafanyiwa marekebisho yanayopasa, pamoja na kuchuchuliwa kwa vyanzo vingine vya maarifa, kuna hakika ya MA kutoa mchango mkubwa katika uokoaji maisha, uelimishaji wa watoto, ongezeko la uzalishaji katika kilimo, uinuaji wa viwango vya utawala bora, n.k. Basi, kwa akili ya kawaida, inawapasa wabia wote wa maendeleo kuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono shughuli za kijumuia zinazoezamia kwenye MA.

### **2. Kuimarisha uwezo wa jumua za wenyeji wa kuchuchua, kushirikisha na kutumia MA yao**

Miongoni mwa njia bora za kuziwezesha jumua za wenyeji ni kuzisaidia kuimarisha kiwango cha uwezo wao wa kubadilishana na kutumia mazoea yao ya jadi (ama moja kwa moja ama yanapounganishwa na mengine). Uzoefu unaonyesha dhahiri kuwa kuunganisha maarifa ya aina mbalimbali pamoja na kuunganisha wale wanaoyatafuta na wale waliyo nayo kuna manufaa ya kuongeza uwezo wa jumua za wenyeji wa kutanzia matatizo kwa kuongeza washiriki. Hatua mahsusi na muafaka katika eneo hili zingeweza kujumuisha uungaji mkono wa:

- Kubuni mikakati ya MA kitaifa pamoja na kuiingiza katika programu za upunguzaji wa umaskini.
- Kunadi Maarifa ya Nchi za Kusini pamoja na ubadilishanaji wa mafunzo.

- Kuwezesha ubadilishanaji maarifa baina ya jumua.
- Kuunda vyama vya Kitaalamu, viwango na kaida za MA
- Kuunga mkono juhudi za jumua za kuanzisha shughuli za biashara zinazohusiana na MA.

Serikali zenyewe zingeweza kuwa mstari wa mbele katika kuandaa sera ya mazingira yanayoweza jitihada hizi zichuchuke. Wabia wangeweza kuziunga mkono kwa kutoa maliasili za kuunganisha, kusuhulisha na kueneza masomo ya uzoefu yanayotokana na jitihada hizo, (wabia wanaweza kutumia kwa mfano vifunge na miongozo, na sampuli kifani ambazo tayari zimeandaliwa). Miradi, vyombo vya kati na wakala za serikali hupaswa kuunga mkono kwa kudhirishia watendaji wa jadi katika jumua za tafiti za kisayansi pamoja na wadau wengine walio weledi wa nyanja hizo. Wakati huohuo, sekta binafsi ingehamasishwa, kwa kuwako kwa sera zifaazo ili kuwekeza katika uendelezaji wa mazao yanayotokana na mazoea asilia au kwa kuanzisha ubia unaofaa kati ya jumua na sekta binafsi.<sup>28</sup>

### **3. Kuendeleza itifaki bunifu kwa kupatia ithibati na ulinzi wa MA**

Kama ilivyodokezwa mwanzoni mwa makala hii, misingi ya itifaki/protokali za kimataifa zinazolinda haki za umiliki wa mali za kitaalamu (IPR), kwa dhati yake, imo katika dhana ya hataza. Hali kadhalika, protokali/itifaki za kupatia ithibati ya dawa za jadi, kwa nafsi yake, huruhusu kufanyika kwa utafiti wa nguvu za dawa mojamoya kwa tiba ya ndwele mahususi au ugonjwa. Hali hii husababisha matumizi ya itifaki/protokali hizo katika dawa za jadi kuleta mushkeli kwa sababu tiba ya dawa za jadi hushirikisha, kwa pamoja, aina nyingi za vipengee vya mitishamba. Hivyo iko haja ya kupatikana kwa mbinu mpya zitakazoleta ufumbuzi wa suala la haki za umiliki wa mali za kitaalamu na upatikanaji wa ithibati ya kisayansi ya dawa zinazofungamana na MA. Ingawa hatua za mwanzomwanzo zimekwisha kuonekana, kama ilivyodokezwa huko nyuma, lakini itabidi juhudi zizidishwe katika ufumbuzi wa suala hili. Serikali zinaweza kusaidia kwa kutunga sera zifaazo pamoja na mikataba ya kisheria. Wadau wote, wakiongozwa na WIPO, kwa upande wa masuala ya haki za umiliki wa mali za kitaalamu (IPR) na Shirika la Afya Duniani (WHO), kwa upande wa dawa za jadi, wangeweza kuchangia kwa kukazania matumizi yanayofaa ya protokali/itifaki za kimataifa na kuzieneza kwa kutumia

kampani za kupeana habari ambazo zitawafikia washiriki na jumua zao za wenyeji, vyama vyao vya utafiti, n.k.

#### **4. Kutengeneza kiunzi cha kufuatilia matokeo ya usimamizi wa MA na kupima taathira zake**

Wakati miradi na shughuli zinazoshirikisha MA zinaongezeka, pia kuna kuongezeka kwa ushahidi ambao utakuwa na manufaa katika upanuzi wa matumizi ya MA yanayovuka mipaka ya nchi mojamoja. Ni dhahiri kuwa kuna haja ya uandaaji wa seti za vidokezo mahususi, mwafaka kwa sekta binafsi. Vidokezo hivyo vitaonesha maarifa ya ushirikishwaji wa MA au ubaya na mazoea mabaya katika maendeleo. Kiunzi hicho cha vidokezo pia kitasaidia kuchuja mbinu zilizofanikiwa ili ziweze kupanuka kimatumizi kwingineko. Kiunzi chenye kihusishwe na Malengo ya Maendeleo Milenia ili kioneshe jinsi kitakavyochangia mafanikio ya malengo hayo. Ama, kwa njia hii, masuala ya upatikanaji ithibati na ya haki ya umiliki wa mali za kitaalamu (IPR) kuhusu miradi yenye mnasaba na MA kushughulikiwa, serkali zinaweza kuhakikisha kwamba mikakati ya MA kitaifa ina mipango ndani yake inayofaa kwa upimaji wa matokeo. Wabia wenyewe wanaweza kusaidia kutayarisha mbinu mbalimbali kwa kuongozwa na mafanikio yaliyopatikana katika nchi pamoja na kuzieneza mbinu hizo kwenye jumua zinazokusudiwa.

#### **5. Kuanzisha mfuko wa uvumbuzi wa kuhamasisha utundu wa MA wenye mafanikio**

Wakati kimsingi MA hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, maarifa haya huwa hayabakii kama yalivyo, kila kizazi huyapokea na halafu huongeza, hupunguza au kubadili mambo fulanifulani kwa kulingana na mazingira mapya. Jumua za wenyeji wa mahali zina fursa na uwezo wa ubunifu na sanaa ya kubadili MA. Uko ushahidi kwamba jumua na watendaji wa jadi, wapatapo fursa, wanaweza kuchukua mbinu mpya za kutanzua matatizo mapya mbinu ambazo kimsingi, hutokana na mifumo yao ya MA. Pia uko ushahidi kuwa mfuko wa uhamasishaji wa uvumbuzi wa mbinu mpya ni chachu nzuri ya kuisimua fikra za kibunifu katika jumua. Kwa mfano, shirika la misaada ya kiufundi la Ujerumani (GTZ) limefanya tathmini ya miradi midogomidogo pamoja na ubunifu ndani ya jumua. Hali kadhalika, soko/kongamano la Maendeleo la Benki ya Dunia limeibua aina mbalimbali za utatuzi wa matatizo zinazotokana na jumua zenye, baadhi ya mbinu zilizosaidia kupatikana

kwa ufumbuzi zimehusisha MA.<sup>29</sup> Mfuko wa kuhamasisha ubunifu maalumu wa MA ungeweza kuanzishwa kwa muundo wa ule wa uhamasishaji wa uvumbuzi na kuwapatia washirika fursa ya kuchangia rasilimali ili kupata mtaji wa “ujasiraji” kwa ajili ya ubunifu unaohusiana na MA.

#### **6. Kuandaa Kongamano la MA la Dunia ili kuhamasisha ajenda iliyotajwa hapo juu**

Licha ya maendeleo yote yanayoonekana mpaka sasa, bado uelewa wa mchango ambao MA yanaweza kutoa katika maendeleo, kwa jumla uko chini. Bado uko ushahidi unaozidi kuongezeka kuhusu jinsi mazoea ya kijadi yalivyochangia kikamilifu katika ajenda nzima ya maendeleo. Katika muktadha huu, litakuwa jambo mwafaka kuitisha kongamano ambalo litakusanya watunga sera wawakilishi wa jumua za MA ambazo huzitumia kimazoea, asasi nyingine za ndani ya jumua, wabia wengine wa maendeleo, n.k. kwa pamoja wataitumia fursa hii kusaidia kujenga dhamira madhubuti ya utekelezaji wa ajenda iliyotajwa hapo juu. Mwaka wa 2005 utakuwa mwafaka kwa ajili ya kongamano hilo na litaweka msingi wa MA katika hima ya kusaidia kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo ya Milenia kwa muongo uliobakia ili kufikia tarehe ilivyowekwa ya mwaka 2015. Mpango wa MA wa Benki ya Dunia uko tayari kushirikiana na wabia wengine, mamlaka za nchi mbalimbali, pamoja na mashirika yaliyo ndani ya jumua katika uandaaji na uitishaji wa kongamano la namna hiyo. Kongamano la kimataifa litazingatia na kudhihirisha dhamira ya wabia wa maendeleo ya kukuza matumizi ya MA katika mchakato wa maendeleo.

#### **Hitimisho**

Chapisho hili la sasa limejaribu kuweka pamoja ushahidi unaounga mkono dhima muhimu ambayo MA inaweza kutoa katika mchakato wa maendeleo. Ni chapisho linalokumbusha miaka mitano ya Programu ya Maarifa Asilia ambayo ni miongoni mwa jitihada kadhaa za Benki ya Dunia katika miaka michache iliyopita. Jitihada hizi ni za kujaribu kuleta mabadiliko ya kimsingi katika mwelekeo wa Benki katika kukabiliana na changamoto za kuleta maendeleo. Programu ya MA pamoja na jitihada nyingine huenda zinaifanya Benki yenyewe iwe na mwtikio kwa wateja kuhusiana na mahitaji yao, kwa kulenga haja ya kuziwezesha jumua wenyeji. Aidha,

Benki imedhamiria kujifunza kutoka kwa wengine ili kuneemesha maarifa yake yenyewe kuhusu maendeleo ambayo harakaharaka yanazidi kuwa sarafu yake ya pili.

Kama vile Mheshimiwa Raisi wa Tanzania alivyohitimisha katika utangulizi wa chapisho hili: ni wale tu wanaojifunza ambao wana fursa ya kufanikiwa. Tumejifunza kuwa MA ni jambo kubwa kwa ajili ya maendeleo endelevu na uwezeshaji wa jumua za wenyeji wa mahali. Kuingizwa kwa MA ndani ya mchakato wa maendeleo kutasaidia kuyaneemesha na kuyafanya yawe wa sawa zaidi. Kama yalivyo maarifa mengine yoyote, MA huhitaji kutumiwa, kupewa changamoto na kurekebisha kwa kadiri mazingira yanavyobadilika. Kuunga mkono mitandao ya wenyeji mahali na ile ya kikanda ya watumiaji wa MA na kuwezesha ubadilishanaji wa maarifa na mafunzo jumua-kwa-jumua ambao utasaidia kuzipatia jumua fursa ya kushiriki kikamilifu zaidi katika mchakato wa maendeleo, zenyewe zikiwa wahusika wakuu wa maendeleo yao. Hali ya kuwa iko haja ya ujenzi wa mfumo mpya na imara wa kupatia ithubati pamoja na ulinzi wa MA, mazoea ya wenyeji yaliyopo yanaweza, wakati huohuo, kurekebisha na kuunganishwa na juhudi za maendeleo kijumua, kitaifa na kikanda. Kuendelea mbele na mwelekeo huu wa maendeleo kunahitaji dhamira imara kutoka serikalini, wabia, mashirika yaliyo ndani ya jumua na watu wengine wanaopenda kushiriki kazi za pamoja katika ubia wa kutumia MA, kwa ajili ya maendeleo katika mchakato wa kujifunza kutoka kwenye jumua na kuzisaidia jumua zenyewe kujifunza.

- 1 Kabla ya uzinduzi wa programu ya MA katika miaka ya themanini Benki yenyewe ilikuwa na jitihada iliyokuwa imehusiana na maarifa asilia katika sekta ya kilimo kwa nia ya kunyanyua ubora wa uundaji wa miradi ya maendeleo (Warren D.M. 1991)
- 2 Kwa mfano WIPO italenga masuala ya haki za umiliki wa mali za kitaalamu (IPR), IFAD, mada za kilimo; asasi zisizo za serikali (NGOs) zingekuwa kiungo cha jumua n.k. Wabia wa mwanzo waliosaidia kuzindua programu ya Maarifa Asilia walitoka ECA, CISDA, IDRC, ITU, UNESCO, UNDP na shirika la Afya Duniani (WHO) katika muktadha wa PICTA (Ubia wa ICT barani Afrika). Baadaye Programu ya MA ilishirikiana pia na watu wengine pamoja na CIDA, CIRAN huko NUFFIC (shirika la ushirikiano wa kimataifa la Elimu ya juu la Uholanzi), FAO, GM/CCD,GTZ, IFAD, ILO, shirika la ushirikiano la Uholanzi, NORAD, Ushirikiano wa maendeleo wa Uswiss, UNCED, UNCTAD, WIPO na asasi nyingine nyingi zisizo za serikali, asasi za kijamii na vituo vya ubora, hususani barani Afrika na Asia ya Kusini.
- 3 Angalia Maarifa Asilia kwa ajili ya Maendeleo: Msingi wa utekelezaji (Indigenous knowledge for Development :n Framework for Action) November, 1998, <http://www.worldbank.org/off/ok/ikrept.pdf>. Kwa majadiliano ya awali ya madhumuni ya Programu pia Tini za MA na kwa hatua zake zilizofuata punde, Tini za MA za 21.

- 4 Angalia. Muhtasari uliotolewa kijedwali mwishoni kwa makala hii uone shughuli na mafanikio mbalimbali ya Programu ya MA.
- 5 Programu ya MA haidai kuwa shughuli zake pekee ndiyo zilizosababisha kuongezeka kwa uelewa. Programu inakiri kuwako kwa sababu nyingine zilizochangia.
- 6 Taftiti za tovuti kuhusu maarifa asilia zilitoa takribani mapigo 10,000 mnamo 1998, zinazidi 120,000 mwishoni mwa 2003.
- 7 Kwa mfano, washiriki kwenye makongamano ya hivi karibuni yaliyoandaliwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa (FAO, UNCTAD, WHO, WIPO, WTO) wameanza kushirikishana taarifa na uzoefu kuhusiana na uhamasishaji, utumiaji na uhifadhi wa MA katika mchakato wa maendeleo.
- 8 Kwa mfano Lango kuu la maendeleo lina tovuti iliyo mahususi kwa MA ambayo ni miongoni mwa kurasa zenye kutembelewa sana. Angalia: <http://www.development.gateway.org/node/130646/>.
- 9 Hii ina maana ya kuwako kwa mabadiliko makubwa ya kiwango cha juu na ambayo yameleta hali iliyo bora zaidi kuliko yale yaliyotokea katika nusu ya mwisho ya miaka ya tisini wakati (i) wanaanthropolojia jamii waliposhika hatamu za mjadala wa MA kwa sehemu kubwa kinyume cha hao ni ushiriki wa wataalamu wa kilimo walioshiriki baadaye, Michael Warren, na (ii) watu wote kwa jumla ambao waliunga mkono kwa kuwa na mtazamo chanya kuhusu MA ilihali wachache waliona MA ni kifani cha uchawi au visa vya vikongwe.
- 10 WIPO ambayo imeunda kitengo cha kushughulikia masuala ya MA inatoa fursa ya mjadala katika kiwango cha ulimwengu unaohusu mali za kitaalamu (Intellectual property) na MA. Aidha, kitengo kinajishughulisha na utengenezaji zana zinazokusudiwa kuboreshea maslahi ya mali za kitaalamu za wamiliki wa MA.
- 11 Kwa mfano, matokeo ya taftiti za “maarifa asilia” katika kumbukumbu za Benki, yanaonesha kuongezeka kwa kiwango kikubwa kutoka 13 ya mwaka 1998 hadi 237 ya mwaka 2003.
- 12 Viwango vilivyo vingi vya wastani vilivyopatikana kwa kila mwaka huonesha: watu kati ya ~ 120,000 waliotembelea, ~ 500,000hits (hodi?) za kuingia kwenye vitu vinavyohusika na MA. Viko vitabu vya taarifa vipatavyo 25,000 ambavyo vimepigwiwa hodi. Isitoshe Tovuti ndogo ya Tini za MA ina kiwango kikubwa cha matumizi (yaani kila mpiga hodi huangalia kwa wastani, tini zipatazo 20 za MA).
- 13 Kundi la watu wapatao 20 ambao miongoni mwao kuna watunga sera, waganga wa jadi na maofisa wa mradi kutoka Ethiopia, Kenya na Uganda na wenzao wa Benki ya Dunia walitembelea Sri Lanka na India mnamo Septemba 2002 kujifunza mafanikio yaliyopatikana kutokana na uhusishaji wa MA kwa njia ya dawa za jadi katika mradi ya maisha ya awali ya utotoni. Ubadilishanaji huu ulipelekea ubadilishanaji kati ya Nchi za Kusini baina ya Asia ya Kusini na Afrika ya Mashariki (kama kundi la akinamama wa Ethiopia lilichukua na kutumia miongozo kutoka SEWA (Ushirika wa wanawake kwa kujijari nchini India). Miongozo hiyo iliwasaidia katika uboreshaji wa uuzaji wa kazi zao za sanaa za mikono.
- 14 Maelezo zaidi yanapatikana katika tovuti ya Ushirika wa Herveld: <http://www.Indigo.dc.org/history.html>.
- 15 Taratibu za kiwango cha Dunia zilizoko katika IFAD (GM/CCD) na programu ya MA kwa pamoja waliibuia ile jitihada ya C2C ambayo iliungwa mkono kwa moyo mmoja na Serikali ya Uholanzi. Kifungu cha zana kimetayarishwa kwa ajili ya maandalizi, utekelezaji na tathmini ya maarifa baina ya jumua-na-jumua pamoja na ubadilishanaji wa mafunzo. Kifungu hicho kinapatikana kwenye tovuti: <http://www.worldbank.org/afr/ik/communitoolkit/starthere.htm>.
- 16 Miongozo hii inapatikana kwenye tovuti: <http://www.worldbank.org/afr/ik/guidelines/>
- 17 Angalia URL:( URL <http://www.sadc.int/index.php?lang=English&path=about/risd&page=risd+p>

- 18 Matumizi ya istilahi taaluma shirikishi katika muktadha huu ni ya makusudi: ina maana ya mgusano na maathiriano baina ya taaluma mbalimbali (kama uchumi, sosholojia, tiba, mbinu za ufundishaji n.k.), kinyume chake ni istilahi sekta-changilizi yenye maana ya kila sekta kuchangia mazoea kwa wakati mmoja (k.m. katika elimu, afya, usafirishaji n.k).
- 19 Tasnifu ya hivi karibuni juu ya shahada ya udaktari kuhusu maendeleo kwenye Chuo Kikuu cha Toulouse, Ufaransa inafanana mvutano baina ya dhana ya maendeleo yenye msukumo "nje" na ile yenye msukumo "ndani" katika kuchambua programu ya MA, mwandishi anaunga mkono mbinu shirikishi-taaluma zinazotumika katika MA kwa ajili ya maendeleo. Angalia Virginie Escudie, 'Du de'veloppement' et la technologie': impasses des representations exogenes e't e'merrgence de programmes alternatifs" January 2004
- 20 Kwa makusudi ya utekelezaji Programu ya MA ya Benki ya Dunia kutumia fasihi hii MA yana upekee wa *kila* utamaduni au jamii, yamo katika mazoea ya kila jumua, asasi, uhusiano na miviga, hutegemeza mbinu za uamuzi katika kiwango cha jumua za wenyeji; MA huzipatia jumua mikakati ya kutanzulia matatizo yanayozikabili kwa kutumia zana au maliasili ndani ya mazingira yao. Programu ya maarifa Asilia hutofautisha maarifa ya "wenyeji" na maarifa ya "kimila" kwa kuwa MA (i) hayatokani na mafunzo rasmi ya kishule (ingawa inawezekana maarifa hayo hukuzwa kwa kuingizwa katika mfumo wa elimu (ii) bado yanaendelea kutumika na (iii) yamo katika kukua na kupanuka wakati wote. "Maarifa ya kimila" pamoja na kuendelea kutumika hadi sasa, si maarifa yanayoendelezwa kipekee kwa sasa. Maarifa ya wenyeji (pamoja na weledi wao) hujumuisha maarifa yote yaliyomo ndani ya nchi mahususi au jaribu fulani ambayo ni pamoja na maarifa ya hao wenyeji wenyewe ya kijadi na ya kisasa. Angalia, <http://www.worldbank.org/afr/ik/what.htm>.
- 21 Katika miaka ya awali ya mashirikiano katika masuala ya maendeleo, teknolojia zilihawilishwa moja kwa moja kutoka nchi zenye viwanda hadi nchi zinazoendelea kwa matumaini kwamba zitasaidia chumi zinazoendelea kwa kasi ya 'kuruka kichura' Wahamasishaji wa 'teknolojia mwafaka' walirudia mbinu hiyo hiyo kwa kiwango ambacho kilipungua walipofikiria kuwa, kilichofaa India kwa mfano, kitafaa Tanzania pia jitihada hizo za mwanzo za uhawilishaji wa teknolojia kwa baadhi, ziligeuka kuwa 'vyama fulani' hasa teknolojia mwafaka-mkanganyo wa malengo na mbinu, jambo ambalo waunga mkono wa MA wanatakiwa waepuke.
- 22 *Tini za MA za 40*
- 23 Jitihada za uwekezaji katika tafiti za aina hii, kwa hali ilivyo, umebanwa mno na ufinyu wa bajeti pamoja na kudumishwa kwa makusudi na bajeti za Serikali na sekta binafsi ambazo hutegemeza tafiti hiyo. Hata hivyo kwa kadri uelewa wa muhimu wa MA yameingizwa Kitaifa katika Programu ya upunguzaji wa Umaskini kwa ajili ya kuchangia katika sekta ya Sayansi na teknolojia, ni dhahiri kuwa MA hutambuliwa kuwa kitovu halali cha eneo la utafiti wa Kisayansi.
- 24 Angalia mkakati wa dawa za jadi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), wa 2002-2005, Shirika la Afya Duniani (WHO)2002.
- 25 Kwa mfano Taasisi ya Ujenzi Upya vijijini (IIRR) imetoa mwongozo. "Uwekaji kumbukumbu na utumiaji wa Maarifa Asilia." Mwongozo huu huwapatia watumishi wa maendeleo vijijini taarifa na zana zinazohitajika katika kuingiza MA katika mchakato wa maendeleo na hufafanua zaidi ya mbinu thelathini za ukusanyaji na uhifadhi wa MA. Angalia, <http://www.panasia.org.sg/iirr/ikmanual/>
- 26 Posey, D na Dutfield G.(1996).Ng'ambo ya Mali za kitaalamu: Kuelekea Haki za Maliasili za kijadi za wenyeji na jumua za wenyeji. IDRC. Ottawa.
- 27 Matokeo mengine ya mjadala wa Haki za kumiliki mali za kitaalamu(IPR)kuhusu MA ni kwamba Mashirika ya wenyeji na ya Taifa yaliyojitoa katika uhamasishaji wa MA yanaibuka na mbinu za kujihami katika suala hili, kwa kujenga mazingira ya utengano badala ya ushirikiano. Baadhi ya mashirika, kwa mfano, hushindania mafungu ya fedha(ambayo ni adimu) au hushindania kutambulika kuwa wawakilishi pekee wa MA ya kweli. Hivyo uwekezaji katika uendelezaji wa mikakati ya MA au mipango ya utekelezaji huweza kukabiliwa na gharama za miamala inayohitajika kuwaweka washiriki pamoja na kuwajengea moyo wa ushirikiano.
- 28 Kuna mifano mizuri huko Afrika ya Kusini wakulima wa chai wa Suid Bokkeveld wametumia mazoea ya asilia (yaliyotoka kwa wakulima wa Wupperthal huko jimbo la West Cape) kwa ajili ya kuboresha michakato ya kilimo chao baadhi ya mavuno na kuunda ushirika ambao umefanikiwa kuwapatia soko la chai yao huko Ulaya. Nchini Uganda, Serikali inaunga mkono uuzwaji wa dawa ya mswaki inayotokana na mimea asilia.
- 29 Kwa kweli, Programu ya MA ya Benki ya Dunia ilizinduliwa kutokana na ruzuku iliyoitolewa na Kiwara -soko cha ubunifu mpya ambacho kilitangulia dhana nzima ya Kiwara-soko cha Maendeleo, kisha ikabanwa na mapendekezo yaliyotokana na timu za Benki. Kiwara-soko cha Maendeleo kilipanua dhana ile kwa kujumuisha mapendekezo ya kutoka kwenye makundi ya jumua za kiraia ya nchi zinazoshiriki katika Viwara-Soko vya Maendeleo ambavyo kwa kawaida hutokea mara moja katika kipindi cha miaka miwili (Matukio matatu yamekwisha kupangwa yakatimia mpaka sasa),benki inatoa ruzuku (za wastani wa dola 100,000) kwa ajili ya miradi kadhaa ya ubunifu mpya ambayo inateuliwa miongoni mwa maelfu ya mapendekezo yanayopokewa. Kiwara-Soko cha mwisho kilikuwa Desemba2003, kikaruzuku takribani dola milioni sita kwa mapendekezo 47 yaliyotolewa kwenye nchi 27.

## Tathmini ya Jumla ya Programu ya Maarifa Asilia kati ya 1998–2003

Malengo	Shughuli	Mafanikio
<b>Kukuza utambuzi wa umuhimu wa MA</b>	Kuanzisha hifadhi data ya shughuli za MA, mafunzo yapatikanayo, vyanzo, washirika n.k.	Hifadhi data yenye viingizo zaidi ya 260 <a href="http://www.worldbank.org/afr/ik/datab.htm">http://www.worldbank.org/afr/ik/datab.htm</a> ; imeanzisha mawasiliano na zaidi ya vituo 20 vya MA ulimwenguni kote; hifadhi data imeunganishwa na mlango mkubwa wa WIPO wa hifadhi data za MA ili kusaidia ofisi za hataza
	Kubainisha na kupima vifaa vya kupatia na kusambazia MA	Ilianzisha mtindo wa kutoa ripoti bila kuweka wazi undani wa shughuli husika kwa ajili ya uingizaji kwenye hifadhi data; ilifanyia majaribio teknolojia ya kutolea taarifa, kuhifadhi kumbukumbu za video na mahojiano kwa vyombo vya kurekodia sauti, gegezugumu la njia nyingi za mawasiliano (vifurushi vya maarifa, juu ya matumizi ya maarifa asili katika kusaidia kufikiwa kwa MMM)
	Kuchapisha shughuli zilizoteuliwa katika mitindo ya karatasi na kielektroni	Zaidi ya Tini za MA 60 zimechapishwa kila mwezi <a href="http://www.worldbank.org/afr/ik/iknotes.htm">http://www.worldbank.org/afr/ik/iknotes.htm</a>
	Kukuza utambuzi wa umuhimu wa MA miongoni mwa wabia wa maendeleo	Wabia wengi wa maendeleo sasa wanachukua jukumu la kuingiza au kujenga juu ya MA katika programu za maendeleo
<b>Kuongeza uwezo wa wenyeji wa kuhifadhi na kubadilishana MA</b>	Kusaidia kuongeza uwezo wa wenyeji kushirikishana MA hasa miongoni mwa vituo mahalia vya MA	Ilisaidia kuundwa kwa mitandao ya kieneo; ilisaidia vituo vitano kuanzisha uunganishaji; ilisaidia nyumba za kumbukumbu za vijiji kwa ajili ya utamaduni wa desturi za Wamasai
	Kubainisha njia sahihi za kukusanya, kusambaza MA miongoni mwa jumua mbalimbali	Ilisaidia Baraza la Taifa la Sayansi na Teknolojia la Uganda kuanzisha uwekaji wa kumbukumbu vijijini na vituo vya usambazaji
	Uwezesaji wa ubadilishanaji wa maarifa na mafunzo miongoni mwa jumua	Ilisaidia zaidi ya dazeni mbili za ubadilishanaji wa MA wa mahali, kieneo na katika eneo kubwa zaidi kwa ajili ya jumua na kuzalisha sanduku la vifaa kwa ajili ya maarifa ya jumua na ubadilishanaji wa mafunzo.*
<b>Utumiaji MA katika mchakato wa maendeleo</b>	Kuzisaidia nchi kuandaa mikakati ya kitaifa ya kusaidia uingizaji wa MA katika mipango ya upunguzaji umaskini	Ilisaidia Uganda kuunda mkakati wa kitaifa wa MA; ilisaidia Jimbo la Kerala, India kuingiza MA katika mpango Mpango wa 10 wa Maendeleo wa kila miaka mitano; ilisaidia Malawi, Kenya, Uganda, Tanzania, Burkina Faso, Mali na Sri Lanka katika kuendesha warsha za kitaifa juu ya MA ambazo zilisababisha shughuli za ufuatiliaji katika kupendekeza vipengele kwa ajili ya mikakati ya kitaifa
	Ujumuishaji wa shughuli za wenyeji katika programu/ miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia na wabia wengine wa maendeleo.	Zaidi ya dazeni mbili za miradi zilifadhiliwa na Benki ya Dunia, baadhi kwa ushirikiano na wabia wengine wa maendeleo, kuwa na vipengele na vifungu maalumu vya MA. Hivi vinajumuisha miradi ya maendeleo ya awali ya utoto, afya, VVU/UKIMWI, kilimo, mitishamba, na usimamizi wa maliasili

\* Kubainisha moja kwa moja kwa shughuli za programu na uhusikaji wa MA wa wabia wa maendeleo sio rahisi. Hata hivyo, upitiaji wa tovuti za wafadhili mbalimbali unaonesha kwamba jitihada za jumla katika eneo hili zimeongezeka kwa kiasi kikubwa ukilinganishwa na mwaka 1998.

# Marejeo

## **Uboreshaji wa Uwezo Asilia: Kukuza Maarifa ya Jumuiya kwa ajili ya Uwezeshaji.**

Allen, Tim & Thomas, Alan (2000). *Poverty and Development: Into The 21st Century*. Oxford University Press, UK.

Ashman, Davey (2001). "Civil Society Collaboration with Business: Bringing Empowerment Back In." *World Development*, Vol. 29 (7): 1097-1113.

Brinkerhoff, Derick W. (1996). "Enhancing Capacity for Strategic Management of Policy Implementation in Developing Countries." *IPC Monograph* No: 1, United States Agency for International Development.

Defilippis, James (2004). *Unmaking Goliath: Community Control in the Face of Global Capital*. Routledge, New York.

Desart, Michel & Ubogu, Roland E. (2001). *Capacity Building, Governance and Economic Reform in Africa. International Monetary Fund*.

Eade, Deborah (1997). *Capacity-Building: An Approach to People-Centered Development*. Oxfam, UK.

Grindle, Merilee S. (Ed.). (1997). *Getting Good Government: Capacity Building in the Public Sectors of Developing Countries* (Harvard Studies in International Development). Harvard University Press.

Iverson, D., Patton, P. and Sanders, W. (Eds.). *Political Theory and the Rights of the Indigenous Peoples*. Cambridge University Press.

Siri, Gabriel (2002). *The World Bank and Civil Society Development: Exploring Two Course of Action for Capacity Building*. WBI Working Papers. World Bank Institute.

Stern, Nicholas (2002). *A Strategy For Development*. The World Bank, Washington, DC.

## **Elimu na Maarifa Asilia**

Bunyi, Grace (1999). "Rethinking the place of African indigenous languages in African education." *International Journal of Educational Development*. Vol. 19: 337 -350.

Coombs, Philip and Manzoor Ahmed (1974). *Attacking Rural Development: How Non formal Education Can Help*. Baltimore: John Hopkins Press.

Dyer, C. (2001) "Nomads and Education for All: Education for Development or Domestication?" *Comparative Education*, Vol. 37 (3): 315-327.

May, S. and Aikman, S. (2003). "Indigenous Education: Addressing Current Issues and Developments." *Comparative Education*, Vol. 39 (2): 139-145.

Monteil, Vincent (1964). *L'islam noir*. Paris : Editions du Seuil

Mugambi, J.N. Kanyua (2002). *Christianity and African Culture*. Nairobi, Kenya: Acton Publishers.

Sembène, Ousmane. (2001). *Ceddo* [videorecording]. New York: New Yorker Films. (Originally released in 1977 by Filmi Doomi Reew in Dakar, Senegali).

Vergas, C. (2000). "Sustainable Development Education: Averting or Mitigating Cultural Collision." *International Journal of Education Development*, Vol. 20: 377-396.

Smith, J. and Eterovic, I. (2000). "From Altruism to a New Transnationalism? A Look at Transnational Social Movements." In Giugani, M. and Passy, F. (Eds.). *Political Altruism?: Solidarity Movements in International Perspective*. 197-218. Rowman & Littlefield Publishers, Inc. New York.

## **Maarifa Asilia ya Wanawake—Chimbuko la Uwezeshaji**

Benavides, M.(2000). "New Challenges for Alternative Ways of Development Among Indigenous Peoples of the Amazon." In Peters, P (Ed.) *Development Encounters*. 61-75. Harvard Institute for International Development.

Howitt, Richard (2001). *Rethinking Resource Management: Justice, Sustainability and Indigenous Peoples*. Routledge, New York.

Mihesuah, Devon Abbott (2003). *Indigenous American Women: Decolonization, Empowerment, Activism*. University of Nebraska Press, London.

Murdoch, J. (1994). "Sustainable Knowledge," *Geoforum*, Vol. 25 (2): 115-132.

Nussbaum, Martha C. (2001). *Women and Human Development*. Cambridge University Press, UK.

## **Kukabili UKIMWI Barani Afrika kwa Kutumia Maarifa Asilia**

Bessinger, Ruth, Priscilla Akwara & Daniel, Halperin (2000). "Sexual Behavior, HIV and Fertility Trends: A Comparative Analysis of Six Countries. Phase I of the ABC Study. Calverton, MD: ORCBUCEN (US. Bureau of the Census). *HIV/AIDS profile: Senegali*. Washington, DC: U.S. Bureau of the Census.

- Buve, A., Carael, M., Hayes, R., Auvert, B., Ferry, B., Robinson, N., et al. (2001). "Multicentre study on factors determining differences in rate of spread of HIV in sub-Saharan Africa: Methods and prevalence of HIV infection." *AIDS*, 15(Supp1.), S5-S14.
- Green, E.C. (1994) *AIDS and STDs in Africa: Bridging the Gap Between Traditional Healers and Modern Medicine*. Boulder, Co. and Oxford, UK: Westview Press.
- Green, E.C. (2003) *Rethinking AIDS Prevention*. Westport, Ct.: Praeger Press, Greenwood Publishers.
- Green, E.C., V. Nantulya, R Stoneburner, J. Stover, (Hogle, J. editor) (2002) *What Happened in Uganda? Declining HIV Prevalence, Behaviour Change and the National Response*. USAID/Washington and The Synergy Project, TvT Associates, Washington, D.C.
- Green, Edward c., (2003) Vinand Nantulya, Yaa Oppong, Teresa Harrison, "Literature Review and Preliminary Analysis of "ABC" factors in six developing countries." Cambridge: Harvard Center for Population and Development Studies.
- Gross, Michael, (2003) *The Second Wave will Drown Us*. *AJPH* 93(6):872-882.
- Hearst, N., and S. Chen. (2003). *Condoms for AIDS prevention in the developing world: A review of the scientific literature*. Geneva: UNAIDS.
- Homsy, J., Katabira, E., Kabatesi, D., Mubiru, F., Kwamya, L, Tusaba, C., et al. (1999). *Evaluating herbal medicine for the management of Herpes zoster in human immunodeficiency virus-infected patients in Kampala, Uganda*. *Journal of Alternative and Complementary Medicine*, 5, 553-65.
- Hygea/FHI. (2001). *Enquete de Surveillance du Comportement ESC 2001*. Senegali Ministry of Health. Republique du Senegali, Ministere de la Sante et de la Prevention, Comite National de Prevention du SIDA CNPS, FHI/USAID Senegali, Eleves Filles-Dakar.
- MAP (Monitoring the AIDS Pandemic) Network Symposium. (2000, July). *The status and trends of the HIV/AIDS in the World*, Durban, South Africa.
- Mostad, S. 8., Overbaugh, J., DeVange, D. M., et al. (1997). *Hormonal contraception, vitamin A deficiency, and other risk factors for shedding of HIV -1 infected cells from the cervix and vagina*. *Lancet*, 350, 922-927.
- Shelton, J. & Johnston, 8. (2001). *Condom gap in Africa: evidence from donor agencies and key informants*. *BMJ*, 323, 139.
- Sittitrai, W. (2001). *HIV prevention needs and success: A tale of three countries*. Geneva: UNAIDS.
- Kilimo Endelevu na Riziki za Vijijini : Ubunifu wa Maarifa wa Maarifa ya Wenyeji katika Maendeleo Sustainable Agriculture and Rural Livelihoods: Local Knowledge Innovations in Development
- Ellis, Frank (2000). *Rural Livelihoods and Diversity in Developing Countries*. Oxford University Press, Oxford.
- Ellis, Frank & Bahigwa, Godfrey (2003). "Livelihoods and Rural Poverty in Uganda." *World Development*, Vol. 31 (6): 997-1013.
- Francis, Elizabeth (2000). *Making a Living: Changing Livelihoods in Rural Africa*. Routledge, New York.
- Tripp, Robert (1993). "Invisible Hands, Indigenous Knowledge, and Inevitable Fads : Challenge to Public Sector Agriculture Research in Ghana." *World Development*, Vol. 21 (12) : 2003-2016
- World Bank (2003). *World Development Report 2003: Sustainable Development in a Dynamic World: Transforming Institutions, Growth, and Quality of Life*
- Maarifa Asilia na Usimamizi wa Maliasili**
- Fabicius, Christo (Ed.) (2004). *Rights, Resources and Rural Development: Community Based Natural Resource Management in Southern Africa*. Earthscan Publishers Ltd., London.
- Knight, Richard L & Bates, Sarah F (Eds.) (1995). *A New Century for Natural Resources Management*. Island Press.
- Matowanyika Joseph Z. Z (1995). 'The Missing Links: Reviving Indigenous Knowledge Systems in Promoting Sustainable Natural Resource Management in Southern Africa : Proceedings of a Regional Workshop Held in Midmar, KwaZulu-Natal Province.' IUCN, *Southern African Research & Documentation Centre, Zimbabwe*.
- Warren, D. Michael, Slikkerveer, L Jain & Brokensha (1999) (Eds.). *The Cultural Dimensions of Development: Indigenous Knowledge systems*. Intermediate Technology Publications. UK.
- Maarifa asilia na Sayansi na Teknolojia: Mgogoro Msigano au Utokeaji Sawia?**
- Gupta, Ann K. et al. (2003). "Mobilizing Grassroots' Technological Innovations and Traditional Knowledge, Local Pathways to Global Development Knowledge, Values and Institutions: Articulating Social and Ethical Capital." *Futures*, Vol. 35: 975-987.



- Jagged, O. (1999). "Science Education in Non-Western Cultures: Towards A Theory of Collateral Learning." In Samali, L. and Kincheloe, J. (Eds.). *What 15 Indigenous Knowledge?: Voices from the Academy*. PP. 119-142. Falmer Press, New York.
- Nader, L. (1996). *Naked Science: Anthropological Inquiry into Boundaries, Power, and Knowledge*. Routledge, London.
- Niamir, M. (1999). "Indigenous Systems of Natural Resource Management among Pastoralists of Arid and Semi-Arid Africa." In Warren, D., Slikkerveer, L., and Brokkensha, D. (Eds.) *The Cultural Dimensions of Development: Indigenous Knowledge systems*. PP. 245-257. Intermediate Technology Publications, London.
- Mikabala Asilia ya Utatuji wa Migogoro Barani Afrika**
- Adjaye, J. K. (1996), *Diplomats and Diplomacy in 19th Century Asante*, Trenton: Africa World. RH. Bates, 1983. The Preservation of Order in Stateless Societies: A Reinterpretation of Evans-Pritchard," (in his book), *Essays on Political Economy of Rural Africa*, New York: Cambridge University Press.
- Bentsi-Enchill, K. (1964), *Ghana Land Law: An Exposition, Analysis, and Critique*, London: Sweet & Maxwell.
- Bercovitch, J. (1989). "International Mediation: A Comparative Empirical Analysis," D. G. Pruitt and K. Kressel, (eds.), *Mediation Research: The Process of Effectiveness of Third Party Intervention*, San Francisco: Jossey-Bass Publishers.
- Bohannan, P. J. (1957). *Justice and Judgement among the Tiv*, London: Oxford University Press.
- Brautigam, D. (1991), *Governance and Economy: A Review*, Policy and Review Department, WPS 818, Washington, DC: World Bank, 1991.
- Brautigam, D. (1996), "State Capacity and Effective Governance," B. Ndulu and N. van Walle, eds., *Agenda for Africa Economy Renewal*, New Brunswick: Transaction Publishers.
- Cohen, A. (1974), *Two-Dimensional Man: An Essay on the Anthropology of Power and Symbolism in Complex Society*, Berkeley: University of California Press.
- Cohen, R (2001), "Language and Conflict Resolution: The Limits of English," *International Studies Review*, Vol. 3, Issue 1, Spring.
- Cooter R D. (1996) *The Rule of State Law Versus the Rule-of-Law State: Economic Analysis of the Legal Foundations of Development*, Washington, DC: World Bank, April.
- Deng, F. M. Zartman, I.W. (1991) "Introduction", *Conflict Resolution in Africa* ed. by F.M. Deng and I.W. Zartman (Brookings Institute, Washington, D.C.
- Dia, M. (1996), *Africa's Management in the 1990s and Beyond: Reconciling Indigenous and Transplanted Institutions*, Washington, D.C: The World Bank.
- Downs, . R E. Reyna, S. eds., (1988). *Land and Society in Contemporary Africa*, Hanover: University Press of New England.
- Englebort, P. (2000), *State legitimacy and Development in Africa*, (Boulder: Lynne Reinner publishers.
- Evans-Pritchard, E. E. (1940), *The Nuer: The Description of the Modes of Livelihood and Political Institutions of a Nilotic People*, Chapter IV, "The Political System," Oxford: The Clarendon Press.
- Fukuda-Parr, S. Lopes, C. Malik, K. (2002), eds. "Institutional Innovations for Capacity Development," , *Capacity for Development: New Solutions to Old Problems*. Sterling, VA: Earthscan.
- Fred-Mensah, B. K. (2000), "Bases of Traditional Conflict Management among the Buems of the Ghana-Togo Border," 1. William Zartman, ed., *Traditional Cures for Modern Conflicts: African Conflict "Medicine*, Lynne Reinner Publishers.
- Fred-Mensah, B. K. (2001), "Indigenous African Conflict Management Schemes: Analyses and References," *A Current Bibliography on African Affairs*. " Vol. 32, No. 1.
- Fred-Mensah, B. K. (2003)a, "Ghana: 'Kanye Ndu Bowi,' An Indigenous Philosophical Context for Conflict Management," *IK Notes*, No. 56, May.
- Fred-Mensah, B. K. (2003)b, "'Adzina:'" An Indigenous Trial by Jury on the Ghana-Togo Border, *IK Notes*, Washington, DC: World Bank, No. 59, August.
- Ghana, (1960). *Interpretation Act, (1960)*, Accra: Assembly Press.
- Gluckman, M. (1965), *Politics and Ritual in Tribal Society*, Chapter Chicago: Aldine Publishing Company.
- Green and A. Honwana, E. C. (1999). "Indigenous Healing of War-Affected Children in Africa," *IK Notes*, No. 10, July.
- Kenyatta, J. (1985) *Facing Mountain Kenya: The Traditional Life of the Kikuyu*. London: Heinemann.,
- Khadiagal, G. M. (1994), *Allies in Diversity: The Front-line States in Southern Africa Security, 1975-1993*, Athens: Ohio University Press.
- Kouassi, E. K. 1. William Zartman, ed. (2000), "West Coast Diplomacy among the Akan and their Neighbors," , *Traditional Cures for Modern Conflicts: African Conflict "Medicine*, Lynne Reinner Publishers.

- Magistro, J. (1997), "An Emerging Role for Applied Anthropology: Conflict Management and Dispute Resolution", *Practising Anthropology*, Winter, Vol. 19, No.1.
- Masina, N. (2000) "Xhosa Practices of Ubuntu for South Africa" *Traditional Cures for Modern Conflicts: African Conflict "Medicine"*, I. William Zartman, ed., Boulder: Lynne Rienner Publishers.
- Merry, S. E. "Mediation in Nonindustrial Societies" In *Mediation Research: The Process of Effectiveness of Third-Party Intervention*, San Francisco: Jossey-Bass Publishers.
- Nader, L. , (1995), "Civilisation and its Negotiations", P. Carlan, ed., *Understanding Disputes: The Politics of Argument*, Providence: Berg Publishers.
- Nukunya, G. K. (1992), *Tradition and Change in Ghana: An Introduction to Sociology*, Accra: Ghana University Press.
- Osaghae, E. E. (2000), "Applying Traditional Methods to Modern Conflicts: Possibilities and Limits," I.W. Zartman, ed. *Traditional Cures for More Conflicts: African Conflict "Medicine"*, "Boulder: Lynne Reinner Publishers.
- Radcliffe-Brown, A. R (1940), "Preface" M. Fortes and E.E. Evans-Pritchard, eds., *African Political Systems*, London Oxford University, for the International African Institute.
- Roehl and RF. Cook, J. A. (1989). "Mediation in Interpersonal Disputes: Effectiveness and Limitations" D. G. Pruitt and K. Kressel, (eds.), *Mediation Research: The Process of Effectiveness of Third Party Intervention*, San Francisco: Jossey-Bass Publishers.
- Rose, L. L. (1992). *The Politics of Harmony: Land Dispute Strategies in Swaziland*, Cambridge: Cambridge University Press.
- Schatzberg, M. G. (1986), "The Metaphor of Father and Family", M.G. Schatzberg and I. William Zartman, eds. *The Political Economy of Cameroon*, New York: Praeger.
- Smith, R S. (1976), *Warfare and Diplomacy in Precolonial West Africa*, Madison: University of Wisconsin Press.
- Stedman, D. Rothchild, and E.M. Cousens, eds., S. J. (2002), *Ending Civil Wars, The Implementation of Peace Agreements*, Boulder: Lynne Reinner.
- Swartz, M. J. Turner, V.W. and Tuden, A. eds. (1966), "Bases for Political Compliance among Bena Villages," *Political Anthropology*. Chicago: Aldine Publishing Company.
- Wilson-Fall, W. Zartman, I.W. ed. (2000), "Conflict Prevention and Resolution among the Fulbe," *Traditional Cures for More Conflicts: African Conflict "Medicine"*, "Boulder: Lynne Reinner Publishers.
- World Bank, ed., (1989), *The Long-term Perspective Study of Sub-Saharan Africa: Volume 3. Institutional and Sociopolitical issues*, Washington DC: World Bank.
- Zartman, I. W. (2000), "Introduction: African Traditional Conflict "Medicine," *Traditional Cures for More Conflicts: African Conflict "Medicine"*, "Boulder: Lynne Reinner Publishers.
- Maarifa Asilia: Hatua ya kwenda Mbele (Indigenous Knowledge: The Way Forward)**
- Escudie, Virginie. "Du développement et la technologie: impasses de représentations exogènes et émergence de programmes alternatifs." University of Toulouse, January 2004.
- Southern African Development Community, (2003) *Regional Indicative Strategic Development Plan*
- Warren, D. M. (1991). "Using Indigenous Knowledge in Agricultural Development"; World Bank Discussion Paper No.127. Washington, D.C.: The World Bank
- World Bank (1998). *Indigenous Knowledge For Development-A Framework For Action*, Washington, D.C.: The World Bank.

# Waandishi wa Makala Zinazoongoza

(Majina yamepangiliwa kialfabeti, na majina ya makala yao yakiwa katika mabano)

**John Aluma** (Kilimo Endelevu na Uendeshaji wa Maisha ya Vijijini: Ubunifu wa Maarifa Asilia katika Maendeleo), raia wa Uganda, ni Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Asasi ya Taifa la Uganda ya Utafiti wa Kilimo (NARO). Dkt. Aluma ni mwanasayansi aliyebobea na mwalimu wa masuala ya misitu. Alisoma katika Chuo Kikuu cha Makerere, nchini Uganda, nchini Norway na nchini Uholanzi na akatokea kuwa mwakilishi wa Uganda mwenye sifa za pekee katika mabaraza ya kitaifa na kimataifa, asasi za utafiti, makongamano na vyama. Alisadia katika kutoa mwelekeo kwa maarifa asilia kwenye utafiti wa kilimo katika mradi uliofadhiliwa na Benki ya Dunia, Utafiti wa Kilimo na Mafunzo, Awamu ya II. Ameongoza juhudi katika nchi yake na kwingineko juu ya dhima ya jumua katika maendeleo, ubunifu wa wakulima na maarifa asilia.

Mawasiliano: ddgr@infocom.co.ug

**Peter Easton** (Elimu na Maarifa Asilia), raia wa Marekani, ni Profesa wa Maendeleo ya Elimu ya Watu Wazima na Rasilimali Watu katika Idara ya Misingi ya Kielimu na Stadi za Sera katika Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida. Amejikita hasa katika uchumi wa mafunzo na elimu ya watu wazima, mbinu za utathmini, vuguvugu shirikishi, na ulinganifu wa kimataifa katika elimu ya watu wazima. Ana zaidi ya miaka thelathini ya uzoefu katika elimu ya watu wazima na masuala yanayohusiana na hilo huko Marekani, Afrika, Visiwa vya Karibea na Kusini-Mashariki mwa bara la Asia. Ameshughulikia miradi kadhaa inayohusiana na masuala ya elimu ya watu wazima, ikiwa ni pamoja na mradi wa elimu-tumikivu ya usomaji ya watu wazima huko katika Jamhuri ya Niger, uborashaji wa elimu ya msingi katika Jamhuri ya Haiti, uwezesaji wa jamii na mradi wa mafunzo ya watu wazima katika maeneo ya watu wa kipato cha chini huko Florida, na mradi wa utafiti-stadi linganifu wa elimu ya watu wazima huko Afrika ya

Magharibi uliofadhiliwa na OECD. Profesa Easton pia ametumika kama mkufunzi wa mbinu za kutathmini elimu ya watu wazima kwa Tasisi ya Elimu ya UNESCO. Mawasiliano: easton@coe.fsu.edu

**Nicolas Gorjestani** (Maarifa Asilia: Nini Kifuate), raia wa Iran, ni Mshauri Mkuu na Ofisa Mkuuwa Maarifa na Ujifunzaji, Mkoa wa Afika katika Benki ya Dunia. Ni mchumi kwa taaluma, Bw. Gorjestani ameshika nyadhifa kadhaa za juu na utumishi katika Benki. Mwaka mmoja uliopita aliongoza menejimenti ya maarifa katika Benki na tangia hapo amekuwa mtaalamu mwenye sauti katika matumizi ya ushirikishanaji wa maarifa katika muktadha wa maendeleo. Ni Mkurugenzi wa Programu ya Maarifa Asilia kwa Programu ya Maendeleo, ambayo aliibuni kwa usaidizi wa wenzi wengine wa maendeleo. Kama kiongozi wa Kundi la Maarifa na Mafunzo wa Mkoa wa Afrika, pia anasimamia shughuli kadhaa zinazohamasisha ushirikishanaji wa maarifa na mafunzo miongoni mwa wafanyakazi wa Benki na kati ya Wafanyakazi wa Benki na nchi zilizo wateja katika kusaidia kutia nguvu uzoefu wa wadau wote katika kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Bw. Gorjestani ameandika vya kutosha juu ya masuala ya maarifa na maendeleo.

Mawasiliano: ngorjestani@worldbank.org

**Edward Green** (Ukabilianaji wa Kienyeji dhidi ya UKIMWI), raia wa Marekani, ni Mwanasayansi Mtafiti Mwandamizi katika Kituo cha Masomo ya Idadi ya Watu na Maendeleo katika Chuo Kikuu cha Harvard. Amefanya kazi kwa zaidi ya miaka 25 katika Afrika, Asia, Amerika ya Kati, na Ulaya Mashariki, katika masuala ya UKIMWI na maradhi ya ngono, huduma za msingi za afya ya familia, watoto walioathiriwa na vita, afya ya kimazingira, bioanuwai na uhifadhi. Ametumikia kama mshauri kwa serikali za Msumbiji na Swaziland. Bw. Green ni mtetezi mwenye sauti katika uunganishaji wa

mifumo ya Kiafrika na tiba-hai na watumiaji wa taaluma katika eneo hilo katika kufikia malengo ya jamii ya afya. Amechapisha vitabu vitatu juu ya waganga wa jadi wa Kiafrika na mifumo ya kiimani. Alichunguza mambo yalivyokuwa huko Uganda na Senegali, akithibitisha kwamba masuala ya ubadilishaji wa tabia yamesaidia kwa kiasi kikubwa sana katika kupunguza viwango vya uambukizaji wa VVU.

Mawasiliano: egreen@aol.com

**Frannie Leautier** (Ukuzaji wa Uwezo wa Wenyeji: Undelezaji wa Maarifa ya Jamii kwa ajili ya Uwezeshaji), raia wa Tanzania, ni Makamu wa Rais wa Taasisi ya Benki ya Dunia. Kabla ya kuchukua wadhifa huu, Bi Leautier alikuwa Mkuu wa Watumishi wa Rais wa Kundi la Benki ya Dunia. Bi. Leautier ni maarufu katika ubunifu wa mkakati wa miundo-mbinu. Amefundisha katika Kituo cha Utafiti na Elimu ya Ujenzi, katika Idara ya Mipango-Miji, katika Taasisi ya Teknolojia ya Massachusetts. Ni Mhariri Mshiriki wa Jarida la Mifumo ya Miundo-mbinu na mwanachama wa kamati mbalimbali za kimataifa juu ya maendeleo ya miundo-mbinu.]

Mawasiliano: fleautier@worldbank.org

**Callisto E. Madavo** (Dibaji), raia wa Zimbabwe, na kwa sasa ni Makamu wa Rais wa Mkoa wa Afrika. Bw. Madavo alipata shahada zake za Kwanza, Uzamili na Udaktari wa Falsafa katika Uchumi katika Chuo Kikuu cha Notre Dame. Kabla ya uteuzi wake kama Makamu wa Rais wa Mkoa wa Afrika, alishika nyadhifa mbalimbali za juu katika idara za sekta na za mikoa za Benki ya Dunia. Bw. Madavo amekuwa mhamasishaji mkuu katika Programu ya Maarifa Asilia kwa Mandeleo na ameshajiisha utoaji wa mwelekeo kwa MA katika muktadha mpana zaidi wa kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Mawasiliano: cmadavo@worldbank.org

**Ben K. Fred-Mensah** (Mikabala ya Wenyeji katika Utatuzi wa Migogoro katika Afrika), raia wa Ghana, ni Profesa Msaidizi wa Uhusiano wa Kimataifa na mshauri katika Maendeleo ya Kamataifa katika Chuo Kikuu cha Howard huko Washington, DC. Ni tunda la vyo vikiu vya Johns Hopkins, Cambridge na Cape Coast. Profesa Mensah alifanya masomo yake ya baada ya shahada ya udaktari wa falsafa katika Chuo Kikuu cha Brown. Amefanya kazi kama mshauri wa Benki ya Dunia, Taasisi ya Utafiti wa Sera ya Kimataifa ya Chakula, miongoni mwa mambo mengineyo kadhaa. Amechapisha juu ya masuala ya migogoro, ardhi, na maendeleo katika Afrika na kwa sasa anafanya kazi kuhusu uongozi wa kieneo,

usalama wa Kiafrika na mitaji-jamii inayohusiana na ukarabati wa baada ya migogoro.

Mawasiliano: bmens@earthlink.net

**Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa** (Utangulizi: Njia Asilia katika Maendeleo ya Ulimwengu) ni Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Ameshika nyadhifa mbalimbali za uwaziri, zikiwemo za Uwaziri wa Mambo ya Nje; Habari na Utamaduni; Mawasiliano na Utangazaji; na Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Pia amewahi kutumika kama Balози wa Nchi yake huko Canada na Marekani. Pia aliwahi kuwa Mhariri Mwendeshaji wa magazeti ya serikali ya 'Daily News', 'The Nationalist' na 'Uhuru' na Mkurugenzi mwanzilishi wa Shirika la Habari la Tanzania (SHIHATA).

**Prasad C. Mohan** (Mhariri), raia wa India, ni Mtaalamu Mwandamizi wa Mawasiliano katika kitengo cha Maarifa na Mafunzo cha Mkoa wa Afrika, Benki ya Dunia. Ana zaidi ya miaka 20 ya uzoefu kazini katika kuzisaidia serikali kusanifu mikakati ya maendeleo ya mawasiliano. Kabla ya kujiunga na Benki ya Dunia mwaka 1991, alikuwa akifanya kazi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo (FAO) huko Roma na Shirika la Umaja wa Mataifa la Makazi ya Binadamu huko Nairobi na Bangkok.

Mawasiliano: pmohan@worldbank.org

**Gonzalo Oviedo** (Maarifa Asilia na Usimamiaji wa Maliasili), raia wa Ecuado, ni Mshauri Mwandamizi wa Sera-Jamii katika IUCN. Amejifunza kuhusu Anthropolojia Jamii, Sayansi ya Mazingira na Usimamizi wa Maeneo Yaliyotengwa Makusudi. Amefanya kazi katika masuala yanayohusu mitizamo ya hifadhi ya asili, sera za wenyeji, uhusikaji wa jumua katika uhifadhi na maendeleo, sera za maeneo yalihohifadhiwa na mazingira, na elimu ya vijijini. Kabla ya kujiunga na Sekretariati ya IUCN huko Gland, Switzerland, alifanya kazi na WWF ya Kimataifa huko Switzerland kama Ofisa wa Uhifadhi na Kiongozi wa Watu na Uhifadhi. Amefanya kazi huko Amerika ya Kati kwa AZISE kadhaa za mazingira na maendeleo, kama vile the Charles Darwin Research Station ya Visiwa vya Galapos, UNESCO, na asasi nyinginezo za huko Ecuado na za kimataifa.

Mawasiliano: gonzalo.oviedo@iucn.org

**Mamphela Ramphela** (Maarifa Asilia ya Wanawake—Chanzo cha Uwezeshaji), raia wa Afrika ya Kusini ni Mkurugenzi Mtendaji katika Benki ya Dunia. Kimsingi yeye anahusika na usimamizi wa ushiriki wa Benki katika maendeleo ya maarifa na uchumi-jamii,

kufuatilia masuala ya muhimu ya kiulimwengu, kujenga ushirika uliopo na vyama vya kiraia na wadau wengine. Dkt. Ramphele anaongoza utungaji wa sera za Benki katika masuala ya afya na elimu, na ni msimaizi wa uingizaji, usimamizi na tathmini ya maendeleo kuhusu ufikiwaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Dkt. Ramphele alikuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Cape Town. Alipokuwa mwanafunzi alikuwa na dhima kubwa katika kuhamasisha Vuguvugu la Utambuzi wa Mtu Mweusi huko Afrika Kusini. Ameandika vitabu kadhaa na makala kuhusu elimu, afya, na maendeleo ya jamii.

Mawasiliano: [mramphele@worldbank.org](mailto:mramphele@worldbank.org)

**Preeti Shroff-Mehta** (Mhariri), ni raia wa India, anaongoza Jitihada za Kidunia za Mafunzo Asilia na anafundisha kozi za uzamili katika Elimu na Maendeleo ya Kimataifa kwenye Idara ya Sera za Elimu na Uongozi, Chuo Kikuu cha Maryland, Marekani. Ana miaka kumi na mitano ya uzoefu katika usimamizi wa miradi ya elimu rasmi na isiyorasmi, mafunzo katika mafunzo ya vyama vya kiraia, ukuzaji wa uwezo wa ndani na utafiti katika maendeleo ya kimataifa huko Kusini mwa Asia, Ulaya na Amerika ya Kaskazini. Amepata mafunzo ya uzamili na tuzo nyingi katika nyanza za Uchumi, Masomo ya Maendeleo, Elimu ya Kimataifa na Mipango Miji kutoka kwenye taasisi maarufu za kitaaluma nchini India, Uingereza na Marekani.

Mawasiliano: [prrshroff@aol.com](mailto:prrshroff@aol.com)

**Sibusiso Sibisi** (Maarifa Asilia na Sayansi na Teknolojia: Migogoro, Mikinzano au Michangamano?), raia wa Afrika ya Kusini, ni Rais na Mtendaji Mkuu wa CSIR ya Afrika ya Kusini. Kabla ya uteuzi wake, alikuwa Kaimu Makamu wa Mkuu wa Chuo, Utafiti na Ubunifu katika Chuo Kikuu cha Cape Town ambapo aliongeza "Ubunifu" kwenye idara ili kuhakikisha msisitizo wa kijamii na kiuchumi unarejea katika tafiti za chuo kikuu. Dkt. Sibisi alijiunga na Plessy Ltd., mnamo mwaka 1997, akishughulikia na kuongoza utafiti na maendeleo katika teknolojia za mawasiliano ya simu. Amekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Taifa kuhusu Ubunifu (NACI). Dkt. Sibisi amejiimarisha juu ya usuli wake wa sayansi na teknolojia (Shahada ya Sayansi katika Fizikia, London; Shahada ya Udaktari wa Falsafa katika Hisabati Tumivu na Nadharia za Fizikia, Chuo

Kikuu cha Cambridge; Fulbright Fellowhuko katika Taasisi ya Teknolojia ya California) pamoja na usimamizi wa utendaji na harakati za kibiashara. Alianzisha uundaji wa miradi ya kibiashara iliyojisheheneza kwa habari kedekede kote katika vyuo vikuu vya Cambaride na Cape Town.

Mawasiliano: [ssibisi@csir.co.za](mailto:ssibisi@csir.co.za)

**Achim Steiner** (Maarifa Asilia na Usimamizi wa Rasilimali), Mjerumani mwenye asili ya Brazil, Mkurugenzi Mkuu wa IUCN, Umoja wa Uhifadhi wa Ulimwengu. Ana Shahada ya Kwanza katika Sanaa kutoka Chuo Kikuu cha Oxford, Shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu cha London na alipata mafunzo katika Taasisi ya Ujerumani ya Maendeleo na Shule ya Biashara ya Harvard. Kabla ya uteuzi wake katika nafasi ya Mkurugenzi wa IUCN, Bw. Steiner alikuwa Katibu Mkuu wa Tume ya Dunia ya Mabwawa. Kama Mshauri Mwandamizi wa GTZ na Tume ya Mto Mekong na Mshauri Mwandamizi wa Sera wa IUCN katika kitengo cha Sera ya Ulimwengu, alianzisha ushirika mpya miongoni mwa jumuiya za uhifadhi, Benki ya Dunia na Umoja wa Mataifa. Pia amefanya kazi katika Afrika na Asia. Bw. Steiner ni mwanachama wa bodi mbalimbali za kitaifa na kimataifa, zikiwemo Baraza la Ushauri la Umoja wa Mataifa, Baraza la Ushauri la Mazingira la EBRD, Baraza la Uchina la Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Mazingira na Maendeleo.

Mawasiliano: [achim.steiner@iucn.org](mailto:achim.steiner@iucn.org)

**James D. Wolfensohn** (Utangulizi), raia wa Marekani mwenye asili ya Australia, ni Rais wa Tisa wa Kundi la Benki ya Dunia, na ambaye hivi sasa yuko katika muhula wake wa pili wa uongozi. Alianzisha uwekezaji wa kimataifa katika biashara za kibenki kwa kuhimiza ushirikishwaji katika masuala ya maendeleo na sanaa. Ameweka mkakati wa upunguzaji umaskini kama mhimili wa lengo kuu Benki na kuelekeza kazi ya taasisi katika kusaidia juhudi za jumuiya ya kimataifa za kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Bw. Wolfensohn amekuwa mtetezi mkubwa wa Maarifa Asiliakwa Programu za Maendeleo, ikiwemo uzinduliwaji wa programu za tovuti za Kiswahili na Kiwolof. Pia ameongoza mikakati mingine ya Benki katika kutambua dhima ya utamaduni na mila katika maendeleo.

Mawasiliano: [jwolfensohn@worldbank.org](mailto:jwolfensohn@worldbank.org)

**Reinhard Woytek** (Mhariri), raia wa Ujerumani, anashughulikia Programu ya Maarifa Asilia katika Maendeleo katika Mkoa wa Afrika wa Benki ya Dunia. Kabla ya hapo, aliendesha Huduma za Ushauri na Habari kwa Teknolojia Sahihi za GTZ/GATE, kusaida AZISE za mahali katika kujenga mtandao wa maarifa kuhusu maendeleo ya vijijini. Pamoja na GTZ na EU, alifanya kazi kwa miaka 10 nchini Tanzania katika sekta za kilimo na mazingira. Uzoefu wake wa kazini unajumuisha maendeleo ya jamii yaliyojikita katika MA na hasa katika mifumo ya matumizi ya ardhi. Kama mshauri wa Katibu Mkuu katika Wizara ya Fedha, alihusika katika uboreshaji wa sekta za kahawa, usalama wa chakula na vyama vya ushirika.

Mawasiliano: [rwoytek@worldbank.org](mailto:rwoytek@worldbank.org)

Sehemu ya Pili

**Tini za MA**





# Mihutasari ya *Tini za MA*

Na.	Jina la <i>Tini za MA</i>	M/waandishi	Muhtasari	Makala za Rejea
1	Mifumo ya maarifa asilia katika Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara. Muhtasari Okt. 1998	Donnelly-Roark, P.	Tini ya kwanza ya utangulizi huunganisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi na mbinu ya ushiriki. Jitihada za ujenzi wa uwezesaji na wa taasisi ni muhimu na unaohusu uunganishaji wa mbinu asilia na za kisasa. Vipengele muhimu vya mbinu ya MA katika maendeleo ni: ushiriki wa jumua katika kufasiri mchakato wa maendeleo na matokeo yake, ukuzaji wa mbinu za wenyeji za umamizi wa miradi na uwezo na kulenga matokeo ya miradi ambayo huakisi mahitaji ya jumua.	2, 10
2	Mifumo Endelevu ya Maarifa Asilia Katika Kilimo katika Maeneo ya Matebele Vijijini, Majimbo ya Kaskazini na Kusini, mwa Zimbabwe; Novemba 1998	Larson, J; Sibana, H	Utafiti huu unaakisi athari ya MA, kisiasa—jamii, kimazingira, kiuchumi na kidini katika shughuli za kilimo; kunabainisha na kuchambua mbinu za usimamizi wa maliasili na kufanya tathmini ya ubora na kasoro za mifumo ya MA. Utafiti unadai kuwa kuna haja ya kutambua na kuingiza teknolojia asilia katika jitihada za maendeleo. Mkakati wa msingi ni ule utakaojumuisa uboreshaji wa uwezo wa jumua katika kutengeneza na kuhifadhi kumbukumbu na ubadilishanaji wa MA	6
3	Wanawake wa Senegali Wanaunda Upya Utamaduni wao, Desemba 1998	Easton, P	Baada ya kuhudhuria mafunzo ya ufundishaji wa Elimu ya Watu Wazima, akinamama wa jumua ya Malicounda wanakabiliiana na suala la ukeketaji. Kwa kuwashirikisha viongozi wa kimila na wa kidini, wanafanikiwa kukomesha tabia hiyo ndani ya jumua yao na nyingine nyingi nchini kote.	2, 3, 4
4	Kutoka “Kufuru” hadi Kuendelezwa: Ukuzaji Misitu na Kilimo cha Kutumia Mbolea ya Mimea Asilia huko Forikrom Ghana, Januari, 1999	Easton, P	Vijana nchini Ghana—hukusanya makundi mbalimbali ya jumua kujadili uharibifu wa misitu pamoja na matatizo mengine ya maeneo yao. Kundi lililoundwa hivi karibuni limeweka pamoja vijana waliokuwa tayari kupanda misitu ili kuondoa hatari ya jangwa. Zaidi ya mafanikio ya misitu chama chao kinapata mafanikio katika misitu kilimo, kilimo cha kutumia mbolea ya mimea asilia, elimu ya watu wazima na mafunzo kwa kufanya kazi na uongozi wa wenyeji pamoja na taasisi ya elimu ya watu wazima, idara ya misitu na wakala za maendeleo ya kimataifa.	3, 6, 7
5	Burkina Faso: “Kisomo cha Ujuzi-Herufi kwa Watoto Wadogo” huko Nomgana; Februari, 1999	Easton, P	Chama cha Manegbzange cha Burkina Faso kilingiza jitihada mpya mbadala kwa ajili ya ufundishia shule za msingi na elimu ya watu wazima kwa kufundishia lugha ya wenyeji ya Kimoore. Walitengeneza mtalaa wenye maudhui ya kilimo na utafiti unaoangalia nafasi ya utamaduni katika mafunzo darasani. Matokeo yanaelekeza kiwango cha juu cha mafanikio kuliko ilivyokuwa kabla na hasa kikilinganishwa na kufundisha kwa kutumia kifaransa.	3
6	Wanakijiji Wamiliki Benki: Uzoefu wa Fandene, Senegali; March 1999	Easton, P	Chama cha vijana wa Fandene, AJF nchini Senegali kinaunga mkono jitihada za kutafuta ufumbuzi wa tatizo la vijana kukimbilia mijini, matatizo ya njaa yanayoikumba nchi kila mara, kukosekana kwa mitandao ya kitaasisi na kukosekana kwa ushiriki wa wenyeji katika jitihada za maendeleo. Kuanzishwa kwa mtandao uliobuniwa kimuktadha, kwa ajili ya kuweka na kukopa, hupanuka haraka na kuingia katika jumua nyingine katika kanda na ni chachu ya maendeleo kiuchumi, uwezeshwaji akinamama, kilimo, programu za mafunzo ya stadi za kilimo na ufundi.	3, 6
7	Kisomo cha Watu Wazima na Utawala Bora wa Wenyeji katika Jumua za Vijijini: Uzoefu wa Nwodua, Ghana; Aprili, 1999.	Easton P n.w.	Jitihada za kamati za maendeleo ya Nwodua nchini Ghana, inaanzisha aina za utawala bora kutokana na uzoefu wa wenyeji baada ya kuingiza marekebisho. Chama kinafanya kazi kwa njia ya kamati za sekta. Kila kamati inashughulikia suala moja: elimu ya watu wazima, huduma ya afya ya msingi, michakato ya chakula, kilimo cha misitu, mafunzo ya ufundi, kilimo na usimamizi wa ujenzi wa barabara.	2, 3
8	Utunzaji wa Mazingira katika Pwani ya Magharibi mwa Senegali, Mei, 1999	Easton P n.w	Ukame, mifugo mingi, mioto misituni, kilimo kilichozi uwezo wa ardhi, yote haya yamekuwa tishio kwa viumbe (miti na wanyama) wanaozunguka hifadhi ya maliasili ya Ker Cupaam, iliyoko “Petite Cote” katika mkoa mmoja wa Senegali. Jitihada za Wanawake wenyeji zilizoanzishwa mwaka 1988 ni juhudi zenye msingi katika jadi kwa makusudi ya kuhifadhi mazingira na kupanua tasinia ya utali. Shughuli kuu zinahusiana na mtandao wa ushirika wa mgao wa kuni na malisho, vyanzo mbadala vya nishati vitalu vya miti na utoshelevu wa upatikanaji wa nishati ya kupikia.	2, 3, 6
9	Maendeleo ya Umoja wa Kilimo nchini Mali: Kuongezeka kwa Viwango vya Uwezeshwaji wa Wenyeji wa Mahali; Juni 1999	Easton P n.w.	Chama cha Ushirika nchini Mali kimeibuka ndani ya vyama vidogovidogo vya vijijini vyenye nasaba na jadi na taratibu za kisasa za kufanya kazi. Ushirika wa Wakulima wa Pamba na Chakula hutumia lugha mbili za mawasiliano: Kibambara na Kifaransa ili kuwapa uwezo wenyeji kushiriki kikamilifu katika vyama vyao. Ushirika unaratibu uzalishaji wa chakula, na shughuli katika uuzaji wa mazao sokoni, za kifedha, usimamizi na mafunzo ya wanachama wao.	2, 3, 6

10	Uponyaji Asilia wa Watoto Walioathirika na Vita, Barani Afrika, Julai, 1999	Green, E.C.; Honwana, A.	Waganga wa jadi na viongozi wa jumua wanasaidia watoto walioathirika na vita warudie hali yao ya kawaida kwa kutumia matambiko. Mbinu zenye msingi wa kijamii zilizofanikiwa kwa watoto wa Angola na Msumbiji huonesha kuwako kwa haja ya kuutumia vizuri msingi huu katika hima ya kuwarudisha tena watoto waliotawanywa na maafa mbalimbali kwa kuwako kwa ubia kati ya waganga wa jadi na wanasaikolojia wanaofadhiliwa kutoka nje. Kwa kuwa jitihada za kukabiliana na matatizo ya kijamii, kiakili na ya mihemko kwa watoto walioathirika na vita, migogoro ya kikabila ziko katika hatua za awali, utafiti wa mazoea ya uponyaji wa kijadi unaweza kusaidia katika kupatikana kwa mbinu mwafaka za kuwasaidia wahanga.	9
11	Elimu na Ujuzi wa Kusoma Kuran huko Afrika ya Magharibi, Agost, 1999	Easton, P, n.w.	Shule za kufundishia Kurani ni mfumo wa muda mrefu unaoendesha elimu isiyo rasmi katika Afrika. Shule hizo hufundisha ujuzi wa kusoma na kuandika na sayansi ya Kiislamu, mifumo ya mafunzo ya viwango vingi ambavyo si rasmi, vipengele fulanifulani vya mfumo wa shule rasmi na huunganika zinazoendesha za elimu ya juu barani Afrika pamoja na uhusiano wa karibu na mtandao wa Kiislamu, kijamii na kiuchumi katika bara zima.	3
12	Maliasili za Kitamaduni na Afya ya Mama Wajawazito nchini Mali; Septemba, 1999	Clemmons, L; Coulibaly, Y	Mradi wa nusura ya mtoto wa <i>Africare</i> katika wilaya ya Dioro, mkoa wa Segou, kusini mwa Mali uliendesha utafiti unaozingatia mwelekeo katika vitendo ili kutafiti, maarifa, mitazamo na mazoea kuhusu afya ya mama mjamzito, mimba na uzazi wa mtoto, ukionesha haja ya mazungumzo ya wazi ndani ya jumua kuhusu afya ya akinamama wajawazito, matumizi ya mbinu mwafaka kiutamaduni kwa kutolea elimu ya mimba na utambuzi wa nafasi ya sanaa inayofaa (hadithi, visa, nyimbo za asili, n.k.)	4
13	Lugha za Kisaheli: Maarifa Asilia na Kujiongoza	Easton, P	Program za ujuzi wa kusoma na kuandika nchini Burkina Faso zinazidi kutambua, matumizi ya lugha nyingi, elimu ya msingi iliyojikita kwenye maarifa asilia na dhima ya mitandao ya shule za kufundishia kusoma na kuandika zinazoendesha na jumua, matumizi ya programu za ujuzi wa kusoma na kuandika zinazotumia lugha za kinchi yamenyanzua viwango vya mafanikio ya wanafunzi, jitihada za wanawake kiuchumi, machapisho ya lugha za kinchi na kikanda, na kuongezeka kwa ujuzi wa kusoma na kuandika kwa watu wazima	3
14	Uenezaji wa Utafiti Vijijini katika Afrika: Kukusanya na Kuunganisha Novemba.1999	Easton, P	Mafanikio ya Mradi wa Elimu ya Msingi na ujuzi wa kusoma na kuandika pamoja na chama cha maendeleo ya Elimu barani Afrika huelezea uzoewu wa kuunda, kueneza na kutoa madaraka ya utafiti wa maendeleo kwa makusudi ya kuwajengea wenyeji uwezo. Jitihada za miradi ambayo ni mahususi huelekea kwenye maswali kama: ni kwa mara ngapi kazi za utafiti wa Kiafrika hushirikishwa watu ambao wanaweza kufaidika nao? Mikondo gani ya mawasiliano na kuna ngazi gani za kupandia ili kufanikisha kudhihirika kwa manufaa ya utafiti wenyewe?	2, 3, 6
15	Afya: Maarifa Asilia, Mafao ya Haki; Desemba 1999	Moran, K	Kampuni ya Dawa ya Shaman imeanzisha uhusiano wa kushirikishana faida na taasisi za kisayansi za Nigeria, jumua za vijijini na waganga wa jadi. Kampuni ina malengo ya ugunduzi wa dawa imara/zenye nguvu pamoja na michakato ya kuzichuchua/kuziendeleza kwa hali inayohakikisha kulindwa kwa haki za umiliki mali akili pamoja na za kibiashara kwa ushirikiano kati ya kampuni na nchi, tamaduni na jumua husika. Utafiti unaonesha jinsi faida inavyoweza kupatikana kwa kuunganisha mifumo ya tiba za jadi na taasisi za tiba za kisasa	5, 6, 8
16	Senegali: Demokrasia Vijijini katika Matendo, Januari, 2000	Easton P	AISE moja ya Senegali, TOSTAN hutoa elimu ya demokrasia na haki za binadamu inayohudhuriwa na wanawake, wanaume, watoto na vikongwe waliomo katika jumua ya wenyeji. Vifaa vya kufundishia vilivyoandaliwa kwa pamoja na shirika na jumua zenyewe huingatia elimu isiyo rasmi ya wanawake wa vijijini, njia za kuingizia mapato na elimu ya afya. Kwa sababu ya jitihada hizi wanawake wamechukua uongozi katika masuala ya kuzima migogoro, jumua za wenyeji zimeibuka na vigezo vipya vya kufanyia tathmini ya wagombea wa vyeo vya kisiasa, wanawake wanasimamia kwa karibu sheria za kitaifa kuhusu haki za wanawake, jumua zimeanzisha miradi ya bustani na ushirika wa matunda.	3
17	Mipango Kimkoa, Ndoto za Wenyeji: Ushiriki huko Afrika ya Magharibi, Februari, 2000	Easton, P	Wakulima, wanawake na watu wengine ndani ya jumua walishiriki kuendeleza 'mitazamo wa mfumo' kwa ajili ya mipango ya kanda, kubainisha mielekeo ya hapo baadae ambayo huenda ikaitolea jumua ya wenyeji athari fulani. Kulikuwa na mfululizo wa mazoezi yenye nguvu za utabiri huo yaliyofanyika katika nchi fulanifulani za Afrika ya Magharibi. Mazoezi yale yalionesha masuala yafuatayo: mabadiliko ya kisaikolojia na kiuchumi, kupatikana kwa kiungo kati ya maeneo ya mijini na vijijini, haja ya kutegemea rasilimali za wenyeji na utundu, kuimarika kwa muundo ya kifamilia, tafsiri ya hati mbalimbali za kiserikali pamoja na miongozo kwa lugha za kinchi, kuimarika kwa ushirika vijijini, kuibuka kwa ushirikisho baina ya vijiji kwa nia ya ushiriki wa kisiasa	3
18	Usimamizi Shirikishi na Utamaduni wa Wenyeji: Methali na Vielelezo; Machi 2000	Easton, P	Methali za wenyeji ambazo zinachukua mitazamo ya wenyeji pamoja na ufahamu wao kuhusu masuala kama uwajibikaji, utendaji na upokeaji wa majukumu, huweza kutoa miongozo inayofaa katika kuelewa mitazamo wa wenyeji, mambo wanayopenda na uzoefu wao kuhusiana na masuala haya, katika kufanya tathmini ya utendaji unaohusika na programu za umma na miradi yake	3

19	Maarifa Asilia na Haki za Umiliki Mali Akili, April, 2000	Prakash, S	Hizi <i>Tini za MA</i> hudhirisha baadhi ya midahalo kuhusu faida na hasara za taratibu za Haki za Usimamizi Mali Akili. Mapendekezo yanayojitokeza ni ya kuhakikisha kuna mfumo wa sheria za mila wenye kujumuisha haki za umiliki wa mali akili kwa namna ya kipekee, uwekaji kumbukumbu wa maarifa asilia ndani ya nyaraka za jumla za umma pamoja na kukuzia mifumo ya ushirikishanaji faida kiasasi	6, 8
20	Kugundua Tena Uanagenzi na Kupitia Jando na Unyago: Kiingilio cha Uchumi wa Mijini, Afrika, Kusini mwa Sahara Mei, 2000	Easton, P.	Kuwapa vijana mafunzo ya kuingia maisha ya utu uzima katika jamii pamoja na taratibu zake na stadi, ni mazoea ya kawaida ndani ya jumua za vijijini, barani Afrika. Mifumo ya namna hii haipatikani mijini kwa ajili ya watoto wa mitaani. Ziko jitihada tatu za kujaribu uwezekano wa kuzirekebisha taasisi za vijijini ili ziwafae vijana waishio mijini: mtandao wa "shule zisizo rasmi" kwenye mitaa ya watu fukara jijini Nairobi na vitongoji vyake; zile jitihada za shirika la kimataifa la watoto wa mitaani ambalo hutegemea maarifa na nguvu za watoto wenyewe wa mitaani huko Sudani, na jitihada za ubunifu za kusaidia wahusika wa sekta isiyo rasmi huko Senegali	3
21	Maarifa Asilia kwa Maendeleo: Safari ya Miaka miwili Barabarani; Juni, 2000	Prakash, S	Hizi <i>Tini za MA</i> hutathmini shughuli, mafanikio na changamoto za 'Maarifa Asilia kwa Programu na Maendeleo' baada ya miaka miwili. Baada ya hapo, hatua zilizobainishwa ni kuzidisha nguvu za kujengea mkondo ili MA yawe sehemu ya maendeleo, kuanzisha jumua za mazoea; na kuimarisha watu katika utayari wa kufundishana mambo.	10
22	Maarifa Asilia Yaingia Shule. Matarajio na Hofu Zinazoyakabili Elimu ya Jumua katika Saheli ya Magharibi; Julai, 2000	Easton, P, Capacci, C, Kane, L	Kuingizwa kwa MA na kuwa sehemu ya mfumo wa elimu rasmi na kuunganishwa kwa ujuzi wa kusoma na kuandika na mahitaji ya jumua barani Afrika kunakwenda polepole sana. Baadhi ya serikali za kitaifa zimeanza kujaribu mbinu za jamii zisizo rasmi katika elimu kwa maudhui ya lugha za kinchi. Baadhi ya mbinu hizi huwapa moyo watu wa jumua kushiriki katika maeneo ya fedha, utawala na ukuzaji mitalaa ya elimu ya msingi na sekondari.	3
23	Mbegu za Uhai: Wanawake na Kilimo cha Bio-anuwai barani Afrika, Agosti 2000	Easton P, Ronald, M	Wanawake walimao maharagwe nchini Kenya wanachangia sana katika uhifadhi wa aina za Kijenetiki na kilimo cha bio-anuwai. Kilimo cha zao moja hulingana na Kilimo cha jadi nchini Kenya kwa kupunguza mchanganyiko wa mazao na usalama wa chakula. Kutambua na kuelewa maarifa ya wanawake katika eneo hili kungewasaidia kubadilisha mwelekeo.	3, 4, 6, 7
24	Uimarishaji wa Maarifa Asilia ya Kiufundi: Mfano wa Mvinyo wa Miwa. Septemba, 2000	Ngula, L, Khonde, B, Charles, P, Pruzabana, J-J	Jumua katika Jamhuri ya Kidemokrasi Kongo huhamisha maarifa ya utengenezaji wa mvinyo wa miwa kwa njia teule za uanafunzi pamoja na ushirikishanaji maarifa. Wazee wa jumua na wanawake ndiyo walioruhusiwa kushiriki mchakato wa mwisho. Uchambuzi unaelekeza haja ya kuimarisha MA kwa kuyachaganya na maarifa ya kisasa ili kuboresha malighafi na upatikanaji wake, uboreshaji wa mazao na uuzaji wake	6
25	Mali: Maarifa Asilia Mchanganyiko wa Mapya na ya Kale; Octoba 2000	Easton,P, Bellonde, G	Timu ya utafiti nchini Mali iliyotoa tathmini ya programu ya ujuzi wa kusoma na kuandika inayoendelea inapendekeza kuhusishwa kwa viongozi wa jadi na wazee wa jumua katika uhamasishaji wa mafunzo ya ujuzi wa kusoma na kuandika. Wizara ya Elimu inaunga mkono matumizi ya zana na mbinu zinazotokana na maarifa ndani ya jumua kwa ufundishaji wa ujuzi kusoma na kuandika ambazo zinatilia mkazo stadi za ufundi, tathmini ya mahitaji na uelewa wa mbinu zenye msingi wa MA katika ufumbuzi wa matatizo	3, 8
26	Dawa za Jadi na UKIMWI; Novemba 2000	Bodekar, G, Kabatesi, D, King, R, Homsey, J.	Katika kupendekeza ufumbuzi fulani wa Kiafrika katika kupambana na Ukimwi barani Afrika, makala hii inaeleza haja ya kufanya dawa za jadi kuwa sehemu ya mbinu pana ya uzuiaji wa VVU/UKIMWI na inajadili njia za uboreshaji wa mtandao wa wadau wake kusini mwa Afrika.	5, 6
27	Uganda: Teknolojia ya Habari na Maendeleo Vijijini; Desemba 2000	Prakash, S	Kituo cha mawasiliano cha matumizi mengi huko Nakaseke kimeanzisha teknolojia mpya ya habari na mawasiliano kwa ajili ya kuleta msisimko katika maendeleo vijijini kwa kuratibu upatikanaji wa taarifa, visaidizi vya kujifunzia, mafunzo ya matumizi ya kompyuta na teknolojia za mawasiliano, kujenga kumbukumbu za mazoea ya kilimo cha wenyeji na kuboresha huduma za afya.	3, 6
28	Maarifa Asilia na Sauti ya Wenyeji katika Kupigania mabadiliko huko Afrika ya Magharibi Januari, 2001	Easton, P	Utafiti wa kutoa tathmini ya jitihada zinazoendelea za ujuzi wa kusoma na kuandika nchini Mali, unaelekeza kuwa, miradi mingi ya mafunzo ya ujuzi herufi imekuwa haifanikiwi kwa sababu ya vikwazo hivi vifuatavyo: washiriki wa vijijini walikuwa na fursa chache za kutumia huko vijijini wanakoishi maarifa ya Kibambara kilichoandikwa. Serkali za mitaa na huduma za kilimo hazikuwa zikitumia lugha za kinchi wakati wote, shule zilitegemea Kifaransa kwa kufundishia na kulikuwa na uhaba wa fursa za mikopo au uwekezaji mwafaka wa vitegauchumi mbadala vilivyopo	6
29	Lugha za Afrika ya Magharibi: Mkondo na Ujumbe, Februari 2001	Easton, P	Uchunguzi wa muundo na kamusi ya Kihausa huelekeza kuwa kuelewa lugha ya kinchi kunaweza kusaidia katika mchakato wa maendeleo kwani zinaakisi uzoefu mahususi wa kitamaduni	3
30	Maarifa Asilia na VVU/UKIMWI: Ghana na Zambia: Machi 2001	Naur, M	Tunapolinganisha Ghana na Zambia inathibitika kuwa serikali za kitaifa zina wajibu mkubwa wa kutayarisha mbinu za mafunzo yanayoandikwa kwa lugha ya kinchi kwa ajili ya waganga wa jadi pamoja na mikakati ya elimu kwa ajili ya kukabiliana na janga la VVU/UKIMWI	3, 6

31	Malicounda-Bambar, Matokeo, Safari ya Mapinduzi ya Wenyeji; Machi, 2001	Easton, P	Baada ya kujiunga na wazee na wanajumuia wengine, akinamama wa Kibambara walifanikiwa kukomesha mila mbaya ya ukeketaji katika jumuiya yao, kwa kutumia mitandao ya kanda na jitihada za elimu, akinamama wale walifanikiwa kuondoa mila hiyo katika jumuiya nyingine hadi kuvuka mipaka ya nchi yao.	3, 4
32	Waganga wa Jadi wa Kiafrika: Masuala ya Uchumi katika Uponyaji; Mei, 2001	Leonard. K.L	Pamoja na upanukaji wa dawa za kisasa, waganga wa jadi bado wangali maarufu barani Afrika na hupata malipo ambayo si haba na wakati mwingine yaliyo juu ya yale ya tiba za kisasa. Utaratibu wao wa malipo baada ya kupona na mikataba inayotegemea uponaji huwapatia sifa ya motisha mwafaka wa kuvutia kwa wagonjwa wengi.	6
33	Kukarabati Athari za Vita Nchini Msumbiji Jamii za Jando na Unyago na Shule za Jumuiya	Easton.P, Mahade. A, Ahmed. Z.	Shirika asasi moja isiyo ya serikali nchini Msumbiji ya "Watoto, Familia na Maendeleo" huonesha kuwa jitihada zenye mmsingi ndani ya jumuiya zipatapo kukolezwa kwa mtalaa wenye maudhui ya modeli ya mafunzo ya kijadi, zikatekelezwa kwa maelekezo ya wenyeji kwa ajili ya vijana waliosambaratishwa na migogoro ya kivita, zimesababisha kuongezeka kwa wanafunzi shuleni pamoja kiwango cha ushiriki wa wanajumuia katika mageuzi ya mtalaa	3
34	Tanzania: Usambazaji wa Maarifa la Wenyeji kuhusu Kilimo; Julai 2001	Mgumia A.H	Mradi wa Maendeleo ya kilimo wa milima ya Uluguru hufanya kazi na wakulima wengine katika mkoa. Utafiti huu unaohirikisha taaluma nyingi hutegemea kupatikana kwa elimu inayofaa na utekelezaji ya mawasiliano na ushirikishanaji wa maarifa baina ya wakulima	6
35	Ethiopia: Tiba ya Jadi na Daraja la Kuingilia kwenye Afya Bora; Agosti 2001	Lambert, J.	Uharibifu wa misitu, kilimo, mifugo mingi ndani ya eneo dogo la malisho, mioto, mmomonyoko wa udongo n.k., ni tishio kwa mimea yenye thamani ya dawa pamoja na maliasili nyingine ambazo zimewanufaisha watu wengi Afrika kusini mwa Sahara. Ufumbuzi wa tatizo la kuzidi kupungua kwa mimea yenye thamani ya dawa, kunahitaji utambuzi wa mchango mkubwa ambao mimea hiyo hutoa kwa ajili ya afya ya wanadamu na mifugo barani Afrika. Mapendekezo ya msingi yanayojitokeza ni kuchanganya sayansi za kisasa na MA kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa kuhifadhi mazoea ya kupanda mimea yenye nguvu za dawa	4, 5, 6
36	Eritrea: Mchakato wa Kumiliki Maarifa Asilia; Septemba, 2001	Pidatala, K.	Hizi <i>Tini za MA</i> hufafanua jitihada za kimfumo za kuweka kumbukumbu na kuthibitisha uhakika/uhalali wa maarifa asilia katika mikoa ndani ya Eritrea, kupendekeza mafunzo ya mtu mmojammoja au makundi ili kutengeneza kumbukumbu na kuchambua MA kwa kuhusisha taasisi za kitaaluma zilizomo nchini Eritrea	6
37	VVU/UKIMWI: Waganga wa Jadi, Jitihada ya Jumuiya Kuji-tathmini na Uwezeshwaji, Octoba 2001	Naur, M	Waganga wa Jadi na Maarifa Asilia huweza kuziwezesha jumuiya kukabili athari za VVU/UKIMWI na kuchangia katika mgawanyo wa maliasili unaofanywa na serikali kwa ajili ya matumizi yenye manufaa zaidi. Kwa mfano, jitihada za uhamasishaji jamii za Afrika ya Kusini zinaonesha kuwako kwa haja kubwa ya kutambua umuhimu wa msingi wa jumuiya kuhusu haki za binadamu kwa kutumia kanuni za elimu za Paulo Frevre	6
38	Senegali Lugha za Asili, na Fasihi kwa Biashara isiyo na Faida—Masimulizi ya ARED, Novemba 2001	Easton. P, Fagerberg—Diallo, S.	Kukosekana kwa maandiko ya wenyeji ni kikwazo kikubwa katika ufanikishaji wa mafunzo ya ujuzi wa kusoma na kuandika. Ujuzi wa kusoma na kuandika Kipullar na chama cha kujitambua kitamaduni huelekeza kuongezeka kwa haja ya kuwako kwa matini za Kipullar. Maudhui ya lugha za kinchi yaliyochapishwa ni pamoja na miongozo ya ujuzi- herufi, ujuzi- hesabu; riwaya na maandiko mengine vitabu vya MA, vya dini na vya mafunzo ya kamili	3
39	Burkina Faso: Uunganishaji wa Vigezo vya Kisayansi na Asilia katika Utabiri wa Mvua; Desemba, 2001	Roncoli. C, Ingram. K, Jost, C	Tini hii ya MA inalinganisha mbinu za utabiri wa hali ya mvua kijadi na kisayansi ikionesha kwamba wakulima wanategemea aina zote mbili za utabiri: kijadi na za kisasa	6, 8
40	Huduma ya Akinamama Wajawazito Vijijini Uganda: Uboreshaji wa Mifumo ya Maarifa: Asilia na ya Kisasa: Januari; 2002	Musoke, M.G.N.	Huduma za vijijini zinazofadhiliwa na UNFPA na Mradi wa Misaada ya Dharura ni jitihada ambazo, zimeboresha huduma kwa akinamama wajawazito kwa kuwafunza wakunga wa jadi na kuwapatia zana za mawasiliano, usafiri na upatikanaji wa hakika. Wa damu ulio ns viwango vya vifo vya akinamama vimepungua kwa asilimia 50 katika kipindi cha miaka mitatu	3, 4, 10
41	Eritrea: Kuondoa Mila Zinazodhuru; Februari 2002	Wolff, P H	Mila ya ukeketaji imeenea katika jumuiya nyingi za Kiafrika, na, kihistoria, akinamama wenyewe waliingia katika mila hiyo kwa ridhaa yao kwa sababu mbalimbali. Uzoefu wa majeshi ya ukombozi ya Eritrea yanaelekeza kuwa makatazo dhidi ya mila hii hayawezi kufanikiwa kwani huleta athari ya kuzitenga jumuiya na kuzilazimisha zieledele mila hiyo kwa siri. Kushirikiana na wakunga wa jadi, kuwaelimisha kuhusu hatari za mila kiafya kumedhihirika kuwa mwafaka zaidi	6
42	Kuendeleza Maarifa Asilia katika nchi zinazozungumza Kifaransa barani Afrika: Muhtasari wa Nchi Nne Machi 2002	Easton. P, Nikiema. E, Essama, S.	Kuwako kwa makabila mengi, sera za taifa na utekelezaji wake na nafasi ya AZISE kuingizwa kwa MA ndani ya maendeleo. Taasisi zilizomo ndani ya jumuiya (k.m. shule) hazina budi kuchukua nafasi muhimu katika kushiriki kazi zenye mmasaba na MA pamoja na jitihada za serikali za kugawa madaraka ili kuyawezesha MA kuingia katika mkondo wa maendeleo kwa matokeo bora zaidi	4

43	Maonesho ya Mbegu Kusini Tanzania: Kwa nini Maonesho ya Mbegu Ukanda wa Kusini?	Mponda O.KK, Kafiriti, EM	Maonesho ya mbegu bora nchini Tanzania husaidia kupatikana kwa mtandao wa watafiti, wakala wa uenezaji huduma, wakulima wadogo wadogo, wazalishaji wanyama na watoa mbegu. Manufaa ya mara moja, kwa kipindi cha kati na cha muda mrefu cha matazamio ya mafanikio ni kuongezeka kwa aina mbalimbali za mbegu, umilikaji wa ushirika wa kanda, kuongezeka kwa tija katika kilimo na usalama wa chakula, kuongezeka kwa mapato na ubadilishanaji wa maarifa asilia	2, 6
44	Uganda: Mchango wa Mboga Asilia kwa Uhakika wa Chakula cha Kaya; Mei, 2002	Rubaihayo, E.B	Mboga asilia zinazooteshwa, aghalabu na akinamama, katika bustani zao za nyumbani au zilizochumwa makondeni ni lishe kuu katika familia za vijijini zilizo nyingi katika nchi nyingi za Afrika. Lakini sera kuhusu usalama wa chakula katika familia hazitili mkazo ukulima wa mboga hizi. Walaji wa mboga mijini na vijijini wangepaidika zaidi kama wangepewa faida ya mboga hizi kwa afya zao, uchumi wa nchi na mazingira yao.	4, 6
45	Utumiaji Maarifa Asilia Kuinua Tija ya Kilimo: Mfano kutoka India Juni; 2002	Prakash, S	Wakulima walifanya ushirikiano katika kuinua tija ya kilimo huko Uttar Pradesh katika mradi wa urutubishaji ardhi ambao uliongozwa na wakulima wenyewe. Kwa kutumia uzoefu wao wenyewe, waliweza kurutubisha ardhi ikaweza kutumika tena kwa kilimo. Matokeo ni kwamba kulikuwa na ongezeko la mazao kwa mara nyingi sana kupanuka kwa shughuli za kiuchumi, kuongezeka kwa mara mbili kwa viwango vya ujira, kupungua kwa uhamaji na kuongezeka kwa thamani ya ardhi.	4, 6, 7
46	Dhima ya Visasili na Mila katika Kusimamia Maliasili Kwenye Mwambao wa Msumbiji	Easton, P; Dava, F; Ahmend, L	Msumbiji ina maliasili nyingi lakini kupanuka kwa miji kuanguka kwa bei ya mazao na mabadiliko makali ya hali ya hewa huathiri uendeleu wa maliasili hizi. Taasisi mahalia, kanuni zisizo rasmi, visasili na miviga na mfumo wa usimamizi wa pamoja zimekuwa na maanufaa makubwa katika usimamizi wa maliasili hizo. Mfano mzuri wa mafanikio ni ule wa uongozi wa makazi ya aina fulani ya samaki mwenye gamba ambaye huliwa, kwa njia mchanganyiko za usimamizi wa familia na baraza la jumua kuonesha kuwa kuna tofauti kati ya mbinu za kisasa na NRM	3, 7
47	Utumiaji wa Maarifa Asilia ya <i>Jatrofa</i> : Matumizi ya mafuta ya <i>Jatrofa curcas</i> kama malighafi na nishati	Henning, R. K	Jitihada za mmea uitwao <i>Jatrofa</i> zimehamasisha maendeleo ya kiuchumi, kisaikolojia na nishati. Jitihada zenyewe ni za kuhifadhi maarifa mahalia na mazoea ya matumizi mengi ya <i>Jatrofa</i> katika kuzuia /kudhibiti mmomonyoko na kuboresha ardhi, kupunguza umaskini na kuhakikisha kuwako kwa nishati inayoweza kutumika zaidi ya mara moja kwa kuwahamasisha wanawake wawe na maarifa	6
48	Ethiopia: Uwezo wa Bima ya Jamii ya Kijadi katika Kusaidia Huduma ya Afya	Haile, D	'Eder' ni taasisi ya kijadi iliyoanzishwa kwa msingi wa jumua ambayo hunufaisha watu kwa kuwa chombo cha fedha cha kijamii nchini Ethiopia. Katika maeneo mengi ya vijijini Eder hutoa msaada kwa ajili ya tiba kwa familia za wenyeji. Asasi kama hizi zisizo za kibiashara zinazotumia kanuni za mshikamano, urafiki na kusaidiana, hutoa vivutio vya vya ushiriki na uimarishaji wa taratibu fulanifulani za jumua	6, 7
49	Wakulima Wafanya Majaribio: Teknolojia ya Kujibunia	Bunch, R. Canas, M	Chama cha washauri wa kilimo endelevu cha kiikolojia chenye msingi wa wanufaika wake kina taarifa kwa kilicho kikubwa cha uzukaji wa mambo mapya katika teknolojia ya Kilimo. Tini za MA zinajadili aina za teknolojia zinazofanyiwa majaribio na wakulima, teknolojia gani zinaleta mafanikio na wakulima wanahitaji msaada gani wa kimtandao pamoja na masoko	6, 8
50	Entrea: Majukumu ya Pamoja ya Yatima wa Vita; Novemba 2002	Wolff, P.H.	Mitandao ya jumua mahalia iliyojiwajibisha kulea yatima na maskini ilisambaratishwa wakati wa mgogoro wa Eritrea. <i>Tini za MA</i> zinajadili muhimu wa vyandarua katika maeneo ya vijijini kwa ajili ya watoto pamoja na jitihada za nchi nzima ya wakala wa huduma ya kijamii. Jitihada hizo zinatilia mkazo haja ya kuunganishwa kwa watoto yatima wa vita katika familia kubwa za kiukoo. Kwa wale watoto ambao familia zao za kiukoo hazifahamiki, mpango unasaidia kuundwa kwa kaya za makundi	9
51	Dawa za Jadi Tanga Hivi leo: Enzi za Kale na za Leo Zakutana; Desemba 2002	Scheinman, D	Waganga wa jadi, waganga wa kisasa na wahudumu wa afya wameunda kundi la kazi za UKIMWI la Tanga. Msingi wa asasi hii isiyo la serkali ni matumizi ya maarifa ya jadi na ya kisasa katika kulikabili janga la VUU/UKIMWI. Wataalamu wenyeji wa mitishamba wamegundua matibabu ya maradhi dowezi ya VVU/UKIMWI, ambayo hayana gharama kubwa lakini yenye uwezo wa tiba. Asasi hii ya kazi za UKIMWI linatafuta ushirikiano kimataifa kwa ajili ya kuthibitisha kisayansi nguvu za mimea inayotumika katika tiba	4, 5, 6, 8
52	Ethiopia: Kiwango Bora cha Uelewa Maarifa ya Jadi na Mimea ya Dawa	Fassil, H	Utafiti uliofanyika Ethiopia ulikusudia kupata undani kuhusu utapakazaji wa maarifa yanayohusu afya ya kijadi na matumizi ya mimea mbalimbali miongoni mwa wanaume na wanawake katika jumua za vijijini. MA hayawi na wataalamu wa dawa za kienyeji lakini pia ni ya wanawake ambao ndio wanaotoa sauti ya kwanza katika suala zima la afya ya mtoto katika familia zao. Utafiti unaelekeza haja ya kuwako kwa mbinu za utafiti shirikishi za utaalumu na wadau katika jumua husika	6
53	Maswala ya Uchumi katika Maarifa Asilia ya Kiafrika, Februari 2003	Nwokeabia, H	Ukosefu wa vivutio kwa waganga mmojammoja pamoja na desturi zilizo kumesababisha kutokuwako kwa ushirikishanaji wa maarifa ndani ya jumua mahalia, na kwa sababu hiyo, kupunguza kasi ya uibukaji wa mambo mapya. Maamuzi ya waganga wa jadi ya kushirikishana maarifa hukwama kutokana ya kufikiria matokeo ya kufichua siri zao, kupoteza hadhi ya utaalumu, haki za ugunduzi	2

54	Matumizi ya Dawa za Jadi nchini Uganda ya Leo, Machi 2003	Weisheit, A; Moses, M.	Waandishi wanapendekeza mkondo mkubwa wa kuingiza dawa za jadi ndani ya mfumo wa afya ya msingi ya umma na kusaidia ukuaji wake. Mikakati ya msingi iliyojitokeza ni uhifadhi wa mimea ambayo inaanza kutoweka na ubadilishanaji wa taarifa, kuanzisha na kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya kujengea mkondo, mazoea ya kijadi yaingie katika mfumo wa mazoea ya afya, kuwekea viwango dawa zinazotokana na kazi za waganga wa jadi, taratibu za utengenezaji na ufungaji wa dawa hizo, mafunzo ya waganga wa jadi kuwa waelimishaji wa jumua.	5, 6
55	Maarifa Asilia: Ubadilishanaji wa mafunzo, Mfano wa Ushirikiano wa Kusini kwa Kusini; April 2003	Prakash, S	Ubia wa Asia—Afrika ulioendelezwa na kanda ya Afrika ya Benki ya Dunia ni jitihada za kukusanya na kueneza maarifa ya wenyeji kwa kuvuka mipaka ya jumua na kanda. Mafunzo yaliyotokana na jitihada hizo yameingizwa katika miradi ya washiriki	6
56	Ghana: Kanye Ndu Bowi—Muktadha wa Kifalsafa wa Udhhibiti wa Migogoro; Mei 2003	Fred-Mensah, B.	Jumua ya 'Buem' huendeleza tangamano ndani ya mfumo wa kijamii bila ya kujali migogoro na tangamano hili huendeshwa kwa mfumo wa utanzuaji wa migogoro ambao unatoa zawadi na makatazo kwa wahusika. Pendekezo linalojitokeza ni kutumia sawia vipengele husiani vya aina zote katika uingiliaji kati wa udhibiti wa migogoro	9
57	Haki za Kitamaduni katika Upekee wa Mfumo wa Sheria za Zimbabwe, Juni 2003	Frommer, C	Utafiti wa maliasili ya kijenetiki ya mmea na maarifa ya utabibu hudhahirisha nafasi ya maarifa asilia na jinsi yanavyopatikana, kuhifadhiwa, kutumika, kushirikishwa na kufanyiwa tathmini kwa mbinu asilia na zisizo asilia Barani Afrika	6
58	Mbinu za Wanawake Vijijini za Kujiwezesha; Julai 2003	Shroff-Mehta, P	Mwanamke mmoja, mkulima na mfugaji sawia, anachangia mageuzi ya mikakati ya shughuli za uchumi na maisha ya kijiji chake na maendeleo yanayokizunguka huko Gujarati nchini India. Mfano wa umiradi ya usimamizi wa mifugo ambayo imestawi vizuri huonesha uelewa wake wa muktadha wa jumua, mahitaji pamoja na vikwazo na uwezo wake wa kutafuta ufumbuzi ulio pekee na wa kudumu; na ujenzi wa uwezo wa jumua kwa kuunganisha maarifa ya jadi na ya kigeni	2, 4, 6
59	Adzina: Mfumo Asilia wa Uendeshaji Mahakama Mpakani mwa Togo na Ghana; Agost 2003	Mensah, B.K	<i>Bate Kate</i> na <i>Adzina</i> ni mifumo ya kitaasisi iliyotengenezwa na jumua ya wenyeji katika eneo la kijadi la Buem nchini Ghana. Inawakilisha mfumo wa kijadi wa kuendeshea mashtaka ulio mpakani mwa Ghana na Togo. Mfumo una taratibu zake mahususi zenye uso wa kiasasi na wa kijumua wa mbinu za usuluhishi na utatuzi wa migogoro. Kuwako kwa wazee wa jumua na kuingilia kati kwao kwa hekima isiyo ya kawaida na rai za wanajumua ni muhimu katika mchakato mzima wa usuluhishi na utanzuaji wa migogoro ya jinai na isiyo ya jinai	9
60	Vikwazo vya Kitaasisi katika Uhamasishaji wa MA: Upatikanaji wa Mitandao ya Kijamii na Taasisi Rasmi, Septemba, 2003	Shroff-Mehta, P	Uchambuzi wa tafiti ndogo kumi na sita za wanajumua waliokuwa watundu wa kuleta mabadiliko unaonesha jinsi wanajumua hai wanavyoshinda vizuizi vya familia/jumua vya muda na vya kitaasisi na kuvumbua mkakati wao wenyewe; ushirikiano na mitandao ya kijamii inayowakilisha mashirika AZISE, wakala za serkali, taasisi za kitaaluma na jumua nyingine ndani ya ukanda husika	2

# Mifumo ya Maarifa Asilia Katika Afrika Kusini mwa Sahara: Kwa Muhtasari

Makala hii imerekebisha na Paula Donnelly-Roark kutokana na makala ya “Mitazamo Kuhusu Mifumo ya Maarifa Asilia Kusini mwa Afrika”.

***Tini za MA 1  
Oktoba 1998***

Watu wa vijijini barani Afrika daima wamehifadhi nguvu fulani za kutisha zinazolinda taasisi za asili na mifumo ya maarifa ya asili na kwa kufanya hivyo wameweza kudumisha kiwango fulani cha kujitegemea. Nguvu hizi zimekitwa kwa uwezo wa kuyakataa mambo ambayo hawana sauti nayo. Ripoti za hivi karibuni kutoka kwa mashirika ya wahisani zinazoeleza kushindwa kwa miradi ya kupunguza viwango vya umasikini barani Afrika kwa kipindi cha miaka ishirini iliyopita, zinathibitisha mtazamo huu. Miongo hii ya mipango iliyoshindwa kutekelezeka haikutokea kwa sababu wafanyakazi wa mashirika ya uhisani hawakuwa na moyo wa kufanya kazi, wala si kwa vile jumuiya za Kiafrika hazikupenda maendeleo. Miradi haikutekelezeka kwa sababu sauti za wanavijiji—ushirika na udhibiti wao ulichukuliwa kuwa ni sehemu ya lengo la maendeleo, na sio njia (mchakato) yenyewe ya maendeleo.

Nguvu za watu wa vijijini za kukataa miradi ya maendeleo yenye mtazamo huu kwao, na inayowajumuisha kama “wafaidikaji” tu, lakini sio “watendaji” bila shaka hazipanua msingi wao wa viingiziamali; na sasa uharibifu wa mazingira na kuzorota kwa uchumi kumeudhofisha zaidi msingi huo. Pamoja na matatizo yote haya, watu wengi

Afrika kote wanaamini kwa dhati kwamba maendeleo chanya mapya yanaweza kutokea, lakini iwapo tu watu wenyewe watadhibiti viingiziamali, uchumi na utamaduni.

Hata hivyo, uwezo huu wa wananchi kudhibiti mambo yao, hutokea tu pale wananchi wanaporuhusiwa kufanya kazi ndani ya, kupanua na kubadili taasisi zao na mifumo yao ya maarifa. Hivyo fursa za kuleta pamoja mifumo ya maarifa ya asili na uhifadhi wa maliasili ni nyingi—lakini hatari pia ni nyingi. Fursa ni uwezekano wa kuanzisha miradi ya usitawishaji wa maliasili inayoendana vema na taasisi na mifumo iliyopo na hivyo kuwa endelevu. Hatari yake ni kwamba mazao yanayotokana na maarifa ya asili—ubainishaji wa mipango, au mbinu za upangaji mipango, kwa mfano—huweza kubainishwa bila kujali vipengee vyake vingine vya kanuni na dhima-ambavyo pia ni muhimu sana kwa vile aghalabu havionekani kwa mtu wa nje. Muunganiko wa namna hii unapotokea, umiliki ambao ni muhimu kwa uendelevu na kujitegemea huanza kudhoofika; na wananchi hujikuta wamepokonywa zaidi urithi wao wa kujitegemea.

Lengo la makala hii ni kueleza baadhi ya fursa ili ziweze kuendelezwa kwa ufanisi zaidi. Ili kutimiza lengo hili, masuala kadhaa yanaja-

diliwa kwa kifupi hapa chini ambayo yanahusiana na hatari na fursa hizo.

### Kuelezea Tumefika Wapi

Kwa kipindi cha zaidi ya miaka 40 iliyopita, jumuiya ya maendeleo ya kimataifa ilichukulia kwamba mtindo wa maendeleo wa kuingiza pembejeo na kuzalisha mazao ndio ulikuwa muhimu zaidi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi. Hata hivyo, kushindwa kwa programu na taasisi hizi kupata uendeleu na ufanisi, ambayo ni matokeo muhimu ya mtindo wa uchumi wa “pembejeo—mazao”, hatimaye kumesababisha mkabala huu wa uchumi kutiliwa mashaka. Utambuzi wa hali hii umesababisha kuiacha mifumo ya uchumi inayoanzia juu kwenda chini na kuzingatia zaidi mifumo shirikishi inayohusu nyanja zote za maendeleo ya wananchi. Nguvu ya mkabala huu mpya ni kwamba sio tu unatoa ufumbuzi mpya wa matatizo; bali pia unatoa ufumbuzi mpya wa kutambua matatizo.

Jambo linaloweza kutuonyesha tumefika wapi katika kuzingatia mitazamo hii mipya ni kuangalia mabadiliko yaliyokwisha tokea katika kufasili matatizo yaliyopo. Hapa “hoja ya uendeleu” imetimiza yale yaliyoshindikana kutimizwa na dhana za “usawa” na “mahitaji ya msingi ya binadamu”. Yaani kuonyesha kuwa maendeleo yanayowategemea na kuwashirikisha watu sio tu hupendelewa kwa vile yanazingatia haki, bali pia yanahitajika kutokana na ufanisi wake. Hata hivyo, utambuzi huu unaolingana wa matatizo, haumaanishi kuwa utatuzi wa matatizo hayo umelingana pia. Kwa hakika hakuna ulinganifu wa namna hiyo.

Hatari hapa ni ya aina mbili. Kwanza, wale ambao wamekuwa wakiunga mkono mabadiliko haya kwa miongo mingi wanaweza wakaendelea kudhani kwamba hapakuwepo na mafanikio kwa vile mafanikio hayo hayakuwa kamilifu; bila kugundua kuwa ingawa sera za zama za uchumi wa pembejeo—mazao zinaweza kuwa hazijabadilika bado, “sauti” ama haja ya kuwa na mkabala mbadala tayari imeshajitokeza wazi. Hatari mbadala ni kufikiria kwamba kwa vile kuna utambuzi linganifu wa matatizo, basi kutakuwa na upatanifu vilevile wa kutatua matatizo haya.

Hivyo inaonekana fursa na namna ya kusonga mbele inategemea kuzingatia mambo mawili: kwa upande mmoja kwa vile “sauti” imejitokeza na watu wako tayari kuisikiliza na kutoa ushirikiano, jitihada zaidi zinahitajika kuwekwa kwenye kipengee cha jinsi gani; kwa upande mwingine majaribio yanayohusu “jinsi gani” hayawezi kuchukulia kuwa watu waliokubaliana juu ya

nini kibandilike, wana mtazamo mmoja ule ule wa namna ya kuleta mabadiliko hayo. Hivyo majaribio haya ya awali, yanayohusu mifumo ya maarifa ya asili na taasisi yatahitajika kubainisha wazi mifumo yake ya kidhana na athari zake za nguvu/udhibiti ili kwamba tofauti katika mitazamo na mikabala iweze kubainishwa na kushughulikiwa kwa makubaliano, badala ya kuendelezwa katika malumbano yasiyo kikomo.

### Kudhani Huleta Tofauti

Tofauti kuu katika kuleta mabadiliko hutegemea kama mtu anatarajia maendeleo ya kiuchumi na kijamii yaanzia ndani ya nchi ama yategemea msukumo toka nje. Jumuiya ya maendeleo ya kimataifa na serikali za Kiafrika ambazo zina upendeleo wa muda mrefu wa mfumo wa uchumi wa pembejeo—mazao kwa kawaida zimekuwa zikikumbatia msukumo wa maendeleo unaotoka nje. Kadiri dhana ya uendeleu ilivyoanza kutilia mkazo umuhimu wa umiliki wa washiriki na uwajibikaji unaotokana na umiliki huo, haja ya kuwashirikisha wananchi katika miradi ya maendeleo imeongezeka sana. Hapa, hata hivyo, mashirika ya wahisani aghalabu yamekuwa yakidhani kwamba harakati za ushirikishwaji zingetumika kuwaelevesha wananchi mifumo mikuu ya sasa ya kiuchumi na kiutamaduni ya nchi za magharibi—lakini kwa uangalifu zaidi na kulingana na muda wao wenyewe. Kimsingi hali hii hufanya mambo yanayodhaniwa kuhusu msukumo huu wa maendeleo toka nje yasisigwe na yasitafakariwe.

Uwezekano kwamba taasisi za asili za Kiafrika—aghalabu hubainishwa kama za “kimila” ama “zisizo rasmi”—zinaweza kuwa msingi wa maendeleo yanayoanzia ndani ya nchi haujachunguzwa sana. Hata hivyo, mkazo wa sasa wa maendeleo unaolenga kuongeza uwezo wa wananchi na taasisi umeanza kutathimini upya ufanisi wa taasisi hizi. Kwa mfano, Mamadou Dia, katika makala yake “kwanini utamaduni ni muhimu” ya 1991 alipendekeza kwamba utambuzi na utumiaji wa taasisi za asili za Afrika ni muhimu katika kuleta usitawi wa bara hili. Kufuatia pendekezo hilo utafiti wa kikanda ujulikanao kama “Menejimenti ya Afrika kwa ajili ya miaka ya 1990” uliandaliwa ili kuchunguza ufanisi wa kutumia taasisi za asili, hasa menejimenti na upangiliaji wa shughuli. Matokeo ya utafiti yameonyesha umuhimu wa utamaduni na taasisi za asili katika uongozi bora, hasa unaoshirikisha wananchi katika uzalishaji mali. Wakati huo huo, matokeo yameanza kuonyesha viwango vikubwa vya utengano katika taasisi zilizo rasmi na jumuiya za kiraia za Kiafrika.



Hatari kubwa hapa ni ile ya kupanua kiwango kilichopo cha utengano. Uwezekano huo ni mkubwa iwapo matumizi ya mifumo ya maliasili za Kiafrika hayatakwepe athari za kigeni katika ngazi zote. Kwa upande mwingine, ingawa zipo fursa nyingi za kuziba utengano na kupanua mifumo ya maarifa ya asili, ili jambo hili lifanikiwe viunzi vya kidhana lazima vibadilike, na kazi halisi, kwa kiwango kikubwa, itakuwa tata na isiyopimika.

### **Kubainisha Mikakati ya Ushirikishwaji**

Mikabala inayotumika kushirikisha wananchi ni mingi na ina malengo, mikakati ya utekelezaji na matokeo tofauti tofauti. Tathmini ya viwango vya udhibiti na uendelevu hutoa viwango vya ushirikishaji vilivyo dhahiri zaidi. Hali hii, kwa upande wake, inatoa kipimo kinachofanya mashirika wezesaji kuwa makweli kuhusu juhudi za ushirikishaji na matokeo yake. Uwezo huu ni muhimu hasa pale vikundi vinapoamua kuacha mifumo ya maendeleo ya nje na kuanza kutumia msukumo na taasisi za ndani ya nchi.

Ili kuweka viwango vya msingi mikakati ya ushirikishaji imegawanyika katika kategoria nne. Mikakati hii imeanishwa zaidi kufuatana na kiwango cha udhibiti cha watendaji/washirika. Uimarishaji huu, ambao msingi wake ni kipimo cha nguvu/uhamishaji wa udhibiti, unaelezea jinsi mikakati ya ushirikishwaji mbalimbali inavyofanya kazi na nini inaweza kutarajia kutimiza kwa mtazamo wa “ mtendaji/mshiriki” na “nguvu za nje”. Mikakati ya msingi na msisitizo wa udhibiti ni kama ifuatavyo:

#### ***Mkakati wa Uhamasishaji***

Mradi wa maendeleo huchaguliwa na kuandaliwa na watu wa nje, kwa kawaida na wataalam wa taasisi za wahisani au serikali zilizobuni mradi, kabla ushirikishaji wa watu haujaanza. Kisha uongozi wa programu “huwahasisha na kuwakusanya” “wafaidika walengwa” ili kuidhinisha, kushiriki na kupitisha maamuzi yaliyokwisha chukuliwa. Mikakati huu unaliachia shirika la nje udhibiti kamili.

#### ***Mkakati wa Maendeleo ya Jumuiya/Taasisi***

Tafiti za kijamii au mikutano hufanywa ili kupata uelewa mzuri zaidi wa mtazamo wa jumuiya/taasis kuhusu tatizo maalum lililoainishwa kuwa linakwamisha maendeleo. Vikundi vya wenyeji vinaweza kuhusishwa, kwa kutumia mbinu za ushirikishaji, katika kupanga na kutekeleza utatuzi wa tatizo. Mtendaji/washiriki huchangia kwa viwango maalum udhibiti na wakala wa nje, lakini uamu-

zi juu ya kiwango mahususi cha udhibiti kuamuliwa aghalabu toka nje.

#### ***Mkakati wa Kujikusanya Pamoja***

Vikundi vya watu waliotengwa kwa namna fulani hujikusanya pamoja, au hukusanywa ili viwe na nguvu zaidi na uwezo zaidi wa kuwaathiri wale wanaofanya maamuzi juu ya vikundi hivyo. Vyama vya ushirika, vyama vya vijijini na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) ya kwenye jumuiya, ni mifano ya mkakati huu. Mtendaji/washiriki huchangia kwa viwango maalum udhibiti na wakala wa nje au na viongozi waliochaguliwa.

#### ***Mkakati wa Uwezesaji***

Vikundi vya kijumuiya, mara nyingi kwa msaada kutoka nje, huanzisha mpango wa mafunzo/uwezesaji unaovivezesha kuandaa malengo yao; kutathimini matokeo ya fursa mbadala zilizopo; kuamua na kuchukua hatua za kutekeleza malengo yao. Mikakati wa uwezesaji huweka udhibiti mikononi mwa mtendaji/washiriki, ambao ndiyo wenye haki na wajibu.

Kwa matokeo endelevu, swali muhimu ni: je, udhibiti unakuwa kwa nani hasa? Mikakati wa “uhamasishaji” huweka udhibiti wote mikononi mwa mameneja wa mradi na hivyo ni rahisi kuanzisha na kuusimamia. Lakini, kwa vile udhibiti wa wenyeji ni mdogo mno, mkabala huu aghalabu huhatarisha msingi wa uendelevu. “Maendeleo ya jumuiya” na “mikakati ya kujikusanya pamoja” kuchangia kiwango fulani cha udhibiti na washiriki na hivyo ina uwezo wa kuwa na uendelevu wa kutosha, lakini kwa masharti yafuatayo: (a) Kwamba usimamizi wa mradi uzingatie mitindo ya asili; na (b) zao la mradi likidhi mahitaji muhimu ya jumuiya, kama vile uimarishaji wa huduma ya upatikanaji wa maji. Mikakati ya “uwezesaji” huwawezesha washiriki kubuni miradi yao na kutekeleza na hivyo kuweka udhibiti na wajibu mkubwa mikononi mwa washiriki, pakiwepo na kiwango kikubwa cha uendelevu. Lakini udhibiti mkubwa mno unaweza pia kuingeza utengano.

Kila moja ya mikakati hii ya ushirikishaji, licha ya kuwa na kipengee cha udhibiti, huwa pia na “kipengee cha matendo”. Katika kuchagua mkakati ni muhimu kuweka wazi kipengee hiki cha matendo. Na jambo muhimu zaidi kwa mafaniko ya mradi ni kuelewa jinsi kipengee cha matendo kinavyohifadhika ama kukengeuliwa wakati wa utekelezaji. Mikakati ya uhamasishaji hutumia washiriki kupata ushauri; mikakati ya maendeleo ya jumuiya na ya kujikusanya pamoja hutumia washiriki kufanya mapatano; na mikakati ya uwezesaji huwatumia kuanzisha kujitawala. Kuelewa kipengee cha matendo cha mikakati mbalimbali ya ushirikishwaji na

pia tofauti muhimu miongoni mwake, huweza kutusaidia kuamua wapi uwekwe udhibiti kwa ajili ya uwezekano mkubwa wa uendelevu.

Hatari hapa ni kwamba ili kufanya kazi kwa ufanisi kwa kutumia mifumo ya maarifa ya asili, mikakati yote miwili ya mapatano na uwezesaji lazima itumike na iwe endelevu kwa muda mrefu, kwa ngazi za chini na pia zile za sera. Kuhifadhi mikakati hii bila kurejea nyuma kwenye ngazi za mapatano ni jambo gumu sana. Kwa upande mwingine, fursa iliyopo ni kwamba ulazima wa lengo hili utasababisha kuvumbuliwa maarifa mengi ya “jinsi gani” ambayo yatafanya juhudi za baadaye katika eneo hili kuwa rahisi zaidi kutekelezeka.

### **Hitimisho**

Kwa kifupi, mikabala ya ushirikishaji inayoweza kufanya kazi vizuri na mifumo ya maarifa ya asili badala ya kupingana nayo haichanganuliwi kirahisi au kutoa utatuzi rahisi wa matatizo. Hata hivyo, ushirikishaji huu hukabili vema utata na utegemeano wa masuala menyewe. Aidha huelekeza kwa ufanisi mbinu zinazohitaji kutatua matatizo kwa ajili ya kupata masuluhisho endelevu. Lakini jambo la muhimu zaidi ni kwamba hii ni hatua ya kwanza ya kurejesha maendeleo ya Afrika kwenye msukumo wa ndani badala ya ule unaotoka nje ya bara la Afrika.

# **Mifumo Endelevu ya Maarifa Asilia Katika Kilimo katika Maeneo ya Matebele Vijijini**

*Makala hii iliandikwa na Harold Sibanda, Ofisa Mipango wa Umoja wa Vyama vya Vijiji kwa Maendeleo ya Bulawayo, Zimbabwe. Imerudiwa kuchapishwa kutoka Mitazamo juu ya Mifumo ya Maarifa Asilia Kusini mwa Afrika iliyoandikwa na Jeri Larson, Aprili 1998, katika Mada ya Majadiliano Na.3, Kundi la Mazingira, Kanda ya Afrika, Benki ya Dunia. Iliandikwa pamoja na IUCN (World Conservation Union). Mawasiliano: jlarson@worldbank.org*

## ***Tini za MA 2 Aprili 1998***

Utafiti huu ulichunguza Mifumo ya Maarifa ya Asili katika kilimo kwenye maeneo ya vijijini ya nchini Zimbabwe, ukilenga hasa katika kilimo cha mimea cha Watonga wa Wilaya ya Binga ya Jimbo la Kaskazini la Matabeleland, na ufugaji wa kabila la Wakalanga la Wilaya ya Plumtree katika Jimbo la Kusini la Matabeleland. Utafiti ulilenga kubaini baadhi ya maarifa ya asili yaliyotumiwa na watu kuhimili maisha katika mazingira magumu ya hali ya hewa na ya maumbile ya nchi.

Malengo mahususi katika Wilaya zote mbili za Binga na Plumtree yalikuwa: (i) kubaini athari za kijamii, kisiasa, kidini, kiuchumi na kimazingira za mifumo ya maarifa ya asili katika kilimo; (ii) kubaini na kuchambua mbinu za menejimenti (usimamizi) ya maliasili; na (iii) kutathmini thamani na upungufu wa mifumo ya maarifa ya asili katika kilimo.

### **Mbinu za Utafiti**

Taarifa zilikusanywa kupitia mapitio ya machapisho mbalimbali ya kitaaluma yanayohusiana na mada, mahojiano na wakulima, kutembelea maeneo ya kilimo, majadiliano katika vikundi na matumizi ya watafiti walioko vijijini. Watafiti walioko viji-

jini waliandaa jumuiya kwa ajili ya utafiti wa uwandani na pia waliandaa majadiliano. Utafiti wa uwandani huko Kamaziya katika Wilaya ya Binga ulitembelea kaya 40; huko Plumtree takribani kaya 100 zilitembelewa.

### **Matumizi ya Rasilimali**

Katika Wilaya ya Binga, wanaume hudhibiti rasilimali za familia na kuona kwamba rasilimali hizo zinagawanywa na kutumiwa vema. Rasilimali hizi hujumuisha ardhi, maji, mazao ya mimea, mifugo, na nguvu-kazi ya familia. Ardhi hugawanywa kwa familia mpya na chifu wa eneo ambaye, kwa kushauriana na wazee wengine, hugawanya ardhi kwa ajili ya makazi na kilimo. Usimamizi wa ardhi na rasilimali zake katika Wilaya ya Binga hufanywa na Kamati za Maendeleo za Vijiji zilizoanzishwa na serikali miaka ya 1980.

Wakazi wa Wilaya ya Plumtree hujishughulisha zaidi na kilimo cha kujikimu na ufugaji wa wanyama. Ingawa mbao ni nyingi, wakazi wa eneo hili huona kuwa rasilimali hizi hazitumiwi kwa ufanisi kuwa chanzo cha ajira na mapato. Mbao nyingi hutumika kama kuni na kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na nyua.

## Desturi za Mifumo ya Maarifa ya Asili

Mifumo ya Maarifa ya Asili imo katika maeneo yote mawili na bado inawahimilisha wanavijiji katika ukulima wa mazao—ikiwa ni pamoja na utayarishaji wa ardhi, uchaguaji wa nafaka, upandaji, uvunaji, na kadhalika uhifadhi wa nafaka na usimamizi wa mifugo.

Desturi iliyozeleka zaidi ya mifumo ya maarifa ya asili ya Wakalanga ilihusu maarifa yao ya asili ya nyasi na udongo unaofaa kutengwa kwa ajili ya malisho. Viongozi wa familia walikutana nyumbani kwa chifu kila majira ya kuchupua ili kujadili mipango ya malisho kwa majira hayo. Tarehe za kuanza na kumaliza kuchungia katika malisho maalum pia zilipangwa kisha wajumbe na wakuu wa vijiji walisimamia utekelezaji wa wanavijiji wa kanuni hizi.

Jumuiya zote mbili za Binga na Plumtree walithamini mambo matatu kuhusiana na mifumo ya maarifa ya asili. Kwanza, maarifa ni nguvu. Watu walioishi Plumtree kwa miaka mingi walifahamu ruwaza za mvua na vipindi vya kupanda mazao ili kupata mavuno mazuri. Thamani ya pili ya mifumo ya maarifa ya asili ilihusu msingi wa maarifa unaoweza ugawanyaji mzuri wa chakula na pia mgawano mwafaka wa kazi. Jambo la tatu muhimu mintarafu mifumo ya maarifa ya asili lilihusiana na upatikanaji wa hudumu wa rasilimali kwa ajili ya maisha endelevu.

## Hitimisho

Wakati wa utafiti wake wa uwandani, mwandishi wa makala hii aligundua jinsi jumuiya za wenyeji zinavyoithamini mifumo ya maarifa ya asili. Makabila yote mawili ya Watonga na Wakalanga wanathamini mifumo ya maarifa ya asili kama msingi wa maarifa na wa uzalishaji wa chakula na ugawanaji wa kazi kati ya jinsia na marika na pia kama sehemu ya uendelevu wa uhai wao. Mwandishi anapendekeza kwamba mifumo ya maarifa ya asili ijalize, badala ya kushindana na ile ya Magharibi, katika utekelezaji wa miradi. Funzo kwa mashirika ya kimaendeleo sharti liwe kuchunguza kwanza nini wenyeji wanajua na wanacho, na kisha kuziendeleza na kuziboresha teknolojia za asili.

Katika Wilaya ya Plumtree, wananchi walionyesha kwamba ukame unaotokea mara kwa mara na kukose-

kana kwa nyasi na ardhi za malisho umefanya uchungaji wa mzunguko, ambao ni wa mapokeo, kuwa ngumu. Athari za Magharibi pia ziliitishia mifumo ya maarifa ya asili. Wilaya ya Binga ilionyesha kuwa mbinu za kulima za asili zimeachwa na badala yake zinatumika zile za Magharibi; mazao ya mapokeo yamebadilishwa na mazao ya biashara.

Moja ya upungufu wa mifumo ya maarifa ya asili ni kukosekana kwa nyaraka inayohusu mifumo hiyo. Maarifa ya Waafrika juu ya mimea ya asili pamoja na majina yake yanapungua kwa kasi kubwa. Ubora wa mifumo ya maarifa ya asili ni finyu pia kutokana na maarifa haya kutokitwa kwa utafiti wa kisayansi. Kinachoelezwa zaidi ni kwamba ni mwiko kufanya mambo fulani. Mifumo ya maarifa ya asili pia ina hatari ya kutoweka kwa vile inategemea wale wanaohadhi maarifa hayo kuwa tayari kuwagawia wenzao. Aidha vijana wengi huyaona maarifa haya kuwa yamepitwa na wakati ikilinganishwa na maarifa ya utamaduni na desturi za Magharibi.

Utafiti unapendekeza mambo yafuatayo:

- Andaa programu imara za utambuzi wa mifumo ya maarifa ya asili na nafasi yake katika menejimenti (usimamizi) ya utumiaji wa rasilimali.
- Tafiti, weka katika nyaraka na sambaza taarifa za kina kuhusu mifumo ya maarifa ya asili.
- Kuza na hamishia mifumo ya maarifa ya asili kwenye maeneo yenye sifa bainifu zinazofanana. Kutembeleana baina ya vikundi vinavyoendesha miradi inayofanana ni njia mojawapo ya kutekeleza azima hii, kama zifanyavyo warsha juu ya masuala muhimu ya mifumo ya maarifa ya asili.
- Toa machapisho juu ya mifumo ya maarifa ya asili, hasa katika lugha za kienyeji za jumuiya lengwa.
- Patia mafunzo wafanyakazi wa mashirika ya maendeleo, hasa wale wanaofanya kazi moja kwa moja na jumuiya za asili.
- Jenga uwezo wa wenyeji wa kutambua thamani ya mifumo ya maarifa ya asili na kuza mifumo hii kupitia: mikusanyiko ya kimapokeo ya jumuiya; mafunzo juu ya utafiti wa mifumo ya maarifa ya asili; uandaaji nyaraka na usambazaji wake; na msaada toka sekta rasmi wa kuziwezesha jumuiya za asili kuendeleza zenyewe mifumo ya maarifa ya asili.

# Wanawake wa Kisenegali Waunda Upya Utamaduni Wao

*Makala hii imeandikwa kutokana na utafiti uliofanywa na watafiti wa Senegali kwa msaada na usimamizi wa kitaalamu wa Peter Easton, Profesa Mshiriki wa Masomo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, na kwa ushirikiano hai wa jumuiya husika za Kiafrika. Utafiti ulifanywa chini ya ufadhili wa pamoja wa Klabu ya Saheli/OECD, CILSS na Chama cha Maendeleo ya Elimu barani Afrika (ADEA).*

## ***Tini za MA 3 Desemba 1998***

Ingawa kwa miongo mingi Senegali imekuwa Makao Makuu ya Afrika Magharibi iliyokuwa imetawaliwa na Wafaransa, nchi hii kama zilivyo nchi nyingine za ukanda wa Saheli, sehemu kubwa ya nchi bado ni vijijini. Wakati asilimia 62 ya watu hukaa vijijini, zaidi ya asilimia 85 ya utajiri wa nchi uko mijini. Kama ilivyo katika nchi nyingi, dhiki hulundikana na kuwakumba wanawake na wasichana. Katika mwaka 1995 kiwango cha wanawake wanajua kusoma na kuandika nchi nzima kilikuwa juu kidogo ya nusu ya kile cha wanaume (yaani asilimia 23 ukilinganisha na asilimia 44) na tofauti ilikuwa kubwa zaidi katika sehemu za vijijini.

Neno TOSTAN, kwa maana nye-pesi, linamaanisha yake ni “kuangu-liwa kutoka katika yai” kwa lugha ya Kiwolof ambayo huzungumzwa na idadi kubwa ya watu wa Senegali wapatao milioni 7.9 kwa jumla, na ni kati ya mambo kadhaa ya ubunifu kwa maendeleo ya vijijini na juhudi za elimu ya wanawake ambayo yanafanywa ili kulikabili tatizo hilo kutoka kwenye chanzo chake. Juhudi hii hutoa programu ya mafunzo ya miezi 18 ambayo huhusisha elimu ya msingi kwa kutumia lugha za taifa na masuala halisi ya maendeleo, na kuwapa watu wa vijijini rasilimali ya kuboresha kiwango cha maisha yao

huku wakiongeza hali ya kujiamini zaidi katika maisha yao. Zaidi ya kujua kusoma na kuandika, programu hii yenye mwelekeo mpya huwapa washiriki zana za kukabiliana na masuala ya jamii mathalani afya, elimusiha na mazingira. Programu hii hutumia mada sita ambazo huunganisha kujua kusoma na kuandika na stadi za maisha kwa mchakato shirikishi wa hali ya juu katika utatuzi wa matatizo. Shirika la TOSTAN kwa ufanisi linaendelea kuimarisha uhusiano baina ya elimu ya msingi na maendeleo vijijini sio tu kwa kuwawezesha watu wazima kujua kusoma na kuandika na stadi za kuhesabu katika lugha zao za taifa bali pia kutoa uwezo wa kuelewa na kutatua matatizo ya mahali wanapoishi.

Miaka kadhaa iliyopita, asasi hii isiyo ya serikali iitwayo TOSTAN, ilijibu maombi ya viongozi wa kijiji katika eneo la Malicounda ambao walikuwa wameona matokeo ya programu za mafunzo yake kwa wanawake wa jamii za jirani na kusaidia jamii hii ya Kibambara ya eneo la Kati ya Magharibi nchini Senegali kuanzisha kituo chake yenyewe. Programu hiyo iliweka msisitizo maalumu kwenye utambuaji na utatuzi wa matatizo ya kawaida, na mojawapo ya mada za mwisho za mfululizo wa mafunzo hayo ilihusu

suala la afya ya wanawake na ujinsia. Kupendwa kwa mada hiyo miongoni mwa wanawake washiriki kutoka vijijini kulitia fora kuliko mada nyingine zote. Mara tu baada ya kumaliza mafunzo yao, wanawake hawa wapya kutoka Malicounda waliokuwa wamehitimu kujua kusoma na kuandika, waliamua kwamba tatizo walilotaka kukabiliana nalo lilikuwa mila ya ukeketaji wa wanawake—desturi iliyokuwa imeendelezwa kwa muda mrefu katika jamii za Wabambara/Wamandingue na Wapulaar. Kutokana na kupeana taarifa kuhusu desturi za mahali kwingine na athari za ukeketaji kwenye afya ya wasichana na kadhalika maisha yao ya kijinsia, wanawake hawa waliunda silaha za hoja ambazo mwishowe zilishawishi baraza la kijiji kukomesha rasmi mila hiyo. Kati ya miezi ya Mei na Julai mwaka 1997—kipindi ambacho kimila huwa ni kipindi cha kukeketa wasichana wadogo—vitendo kama hivyo havikufanyika katika eneo la Malicounda kwa mara ya kwanza katika historia ya jamii hiyo.

TOSTAN na UNICEF ziliwasaidia wanawake kwa kuandaa ziara ya waandishi wa habari ishirini nchini Senegali kuwahoji kuhusu msimamo wao. Wanawake waliwaonyesha wageni mchezo wa kuigiza ili kueleza sababu kwa nini walikuwa wamechukua uamuzi na hoja walizokuwa wametumia pamoja na wanakijiji wengine. Ziara hii ililitangaza suala hili, lakini pia ilikaribisha maoni yenye vitisho na shutuma kutoka kwa jamii za jirani za kabila lilelile. Huku kikiwa kimehuzunishwa lakini kimsingi bila kukatishwa tamaa, kikundi cha Malicounda kiliamua kuandaa ujumbe kwenda katika vijiji viwili vya jirani kuwashawishi wanawake wa huko kuona umuhimu wa uamuzi wa kupiga marufuku ukeketaji wa sehemu za siri.

Katika mojawapo ya jumuiya hizi—jumuiya ya Ngerin Bambara—wanawake ambao ndio kwanza walikuwa wamemaliza mafunzo ya programu ya TOSTAN waliamua kuafikiana na “kiapo cha Malicounda.” Rais wa Chama chao cha Wanawake, yeye mwenyewe akiwa binti wa ngariba wa jadi, alisema kwamba binti yake yeye binafsi alikuwa ametokwa damu nyingi sana wakati wa kukeketa na kwamba wakati wa mabadiliko ulikuwa umefika.

Wakazi wa jumuiya ya pili, Ker Simbara, waliamua kwamba wasingeweza kuamua kuandaa mila hiyo bila kwanza kusikiliza maoni ya ukoo wao katika mtandao mzima wa vijiji vya jirani. Kwa hiyo, kwa kipindi cha majuma manane, wanaume wawili waliokuwa wameshiriki katika mafunzo ya TOSTAN—mmoja akiwa mraghibishaji na mwingine, Imamu (ambaye ni kuhani wa Kiislamu mwenye umri wa miaka 66)—walisafiri kijiji hadi kijiji kujadili na watu wa huko athari hasi za ukeketaji wa wanawake. Mwanzoni wanaume hawa

walihofu kwamba wangepukuzwa na jamii nyingi watoke haraka. Lakini badala yake waligundua kwamba habari za Malicounda zilikuwaa zimefungua milango na nyoyo za watu na walisikia visa vya kutisha kutoka kwa wanawake, wakizungumzia kwa mara ya kwanza, yale yaliyowafika.

Wanaume hawa walirejea wakiwa wameamini umuhimu wa yale waliyokuwa wamesikia na kile walichokuwa wakifanya. Waliwasaidia wanawake wa Malicounda, Nigerin na Ker Simbara katika kuandaa mkutano baina ya vijiji, mjini Diabougou kwa wale wote waliopenda. Mnamo mwezi Februari 1998, wawakilishi watatu watatu—chifu wa kijiji na wawakilishi wawili wanawake—kutoka vijiji kumi na vitatu mbalimbali walikutana kwa siku mbili kujadili tatizo hili na kuunda “Azimio la Diabougou” ambalo lilikuwa azma ya wanakijiji 8,000 kusitisha ukeketaji wa wasichana tangu hapo.

Kisha habari kuhusu juhudi hizi zilifika katika eneo la Casamance la Kusini mwa Senegali, ambako kundi jingine la vijiji—vyote vikiwa vya watu wa koo za Kipulaar, kabila ambalo lilifanya ukeketaji wa wasichana kwa asilimia 88—viliungana ili kufanya mkutano na azimio kama hilo. Mkutano huo ulihudhuriwa na wawakilishi kutoka jumuiya 18, wafanyakazi wa idara ya afya, na Imamu wa Medina Cherif, anayeheshimiwa sana, ambaye aliwathibitishia wanawake ya kwamba dini ya Kiislamu haihitaji tohara ya wasichana na inadhamini haki za wanawake kiafya na heshima ya binadamu. Wanawake wengi walieleza madhara yaliyotokana na desturi hii. Mmojawao aliombeza vifo vya mabinti wake wawili baada ya kufanyiwa desturi hii; na “mkataji” wa jadi (ngariba) alikubali kwamba msichana mmoja alikuwa amefariki kijijini mwake mwaka uliokuwa umetangulia. Wanawake wengine walizungumzia matatizo wayapatayo wakati wa kujifungua na maumivu yao wakati wa tendo la ndoa. Kikundi hiki kilihitimisha mkutano kwa kutoa azimio lake chenye kulaani desturi hiyo.

Jitihada zimeendela kuenea. Mapema katika mchakato huo, Rais Abdou Diouf wa Senegali mwenyewe alipendeleza “Kiapo cha Malicounda” kiwe mfano wa kuigwa kitaifa. Kutokana na mikutano ya eneo la Casamance, wanawake katika eneo la St. Louis la Senegali sasa wanaandaa mahafali ya vijiji vya kwao, yatakayofanyika mwezi Februari, 1999.

Aina ya “mafunzo hai” inayoendelezwa miongoni mwa wanawake na programu ya TOSTAN nchini Senegali inaelekea umesababisha kutokea mabadiliko makubwa ya kitamaduni. Vipengele vinavyochangia kwenye matokeo yenye ufanisi katika elimu na maendeleo endelevu vinaelezwa zaidi hapa chini.

## Masuala

*Mizizi ya Utamaduni.* Kwa kujumuishwa na matumizi ya lugha za taifa, thamani mzito ya utamaduni wa Kiafrika ndio msingi wa mpango wa elimu ya TOSTAN, inayoonyesha uhusiano wa hali halisi baina ya utamaduni na elimu.

*Lugha za Taifa.* Ingawa Kifaransa ni lugha rasmi ya Senegali, lakini serikali imekuwa kila mara ikizidisha upendeleo wa kutumia lugha za taifa katika mafunzo ya kujua kusoma na kuandika, kwa kutambua kwamba kujifunza kunarahisishwa na kuwa kwenye manufaa zaidi kiakili, kwa kutumia lugha ya nyumbani ya mwanafunzi na itaweza kuharakisha kipindi cha mpito katika kujifunza lugha za kimataifa. Kujifunza kwa kutumia lugha mama huchochea kuona fahari, na kuwawezesha wanawake kutoa mawazo yao nyumbani kwao na katika jumuiia zao; na kuonea fahari nyumbani kwao, na huku wanaume wakihimizwa kuwekeza katika jumuiia zao kuliko kuhamia mijini. Aidha huondoa ile fikra potofu kwamba mtoto anayejifunza kwa Kifaransa huwa ameijenga pale nyumbani, na hivyo kuendeleza mawasiliano na mshikamano baina ya vizazi;

*Utatuzi wa matatizo* ndio uti wa mgongo wa mafunzo na ni kichocheo cha kutaka kujua kusoma na kuandika. Stadi zinazofundishwa katika mchakato huu wenye hatua tano ni pamoja na (i) kutambua na kuchanganua tatizo; (ii) kuchunguza masahihisho yaliyotolewa kwa kuzingatia rasilimali za kifedha, rasilimali watu, pamoja na suala la muda; (iii) kupanga suluhisho: nini kinachotakiwa kutimizwa? Lini hatua mbalimbali zina-paswa kukamilishwa? Nani anawajibika? Rasilimali zipi za watumishi, vitu halisi na kifedha ni za lazima? Vikwazo gani vyaweza kuwapo? (iv) utekelezaji wa suluhisho; na (v) kutathimini matokeo: Je tulitatu tatizo?

*Ushiriki.* TOSTAN ilianzishwa pamoja na wakijiji wakiwa katika mchakato wa ushiriki wa hali ya juu wa miaka kumi. Mada za mitalaa ya programu zilitokana na hadithi, methali, nyimbo na mila za kitamaduni za kila mahali husika zilizokusanywa wakati wa kusafiri kutoka kijiji hadi kijiji, kwa kusikiliza na kurekodi masimulizi ya jadi. Njia ya ufundishaji huzingatia mbinu ya ushirikishaji na daima wanafunzi huhusisha familia zao na jumuiia katika mchakato wa ufumbuzi wa tatizo.

*Wanawake.* Kwa kuwa na kiwango cha asilimia 74.9 cha wanawake wasiojua kusoma na kuandika hadi mwaka 1990, wanawake ndilo kundi lisiloelimishwa kabisa nchini Senegali. Wanawake ndio hasa wamekuwa wakinufaika na mkabala wa TOSTAN wa kutumia lugha kwa jumla ambao huanza na uzoefu halisi husika kutokana na maisha yao ya kila siku kuliko mambo ya

dhahania tu. TOSTAN imekuwa uwanja wa mafunzo ya uongozi na kadiri wanawake wanavyopata hali ya kujiamini ndivyo wanavyoanza kutambua matatizo kama vile upatikanaji wa maji, na kuanza kuleta mabadiliko katika jumuiia zao. Hata hivyo wanaume hawakutengwa: karibu theluthi moja ya washiriki ni wanaume, na—kama kisa cha jumuiia ya Ker Simbara kinavyodhihirisha—huweza kufanya juhudi nyingi muhimu sana kwa kuwaondolea wanawake mizigo mizito inayowalemea.

## Mchakato wa kuendeleza mikabala

Mbali na utaratibu wa ushirikishaji uliokwisha kutajwa, wanafunzi walihusishwa pia katika ukuzaji wa maudhui ya programu kwa njia ya majaribio, mazungumzo na maoni-rejea. Mbinu hii mwanzo ilikuwa aghali lakini mwishowe ilithibitisha kustahili gharama hizo kutokana na kiwango cha ufanisi wa kuchukuliwa na kutumiwa na AZISE. Elimu ya Msingi, kama Kabrasha la UNESCO kuhusu TOSTAN lise mavyo “hugusa ufito wa ndani katika maisha ya watu kuliko mradi wa moja kwa moja wa kujua kusoma na kuandika. Kuelewa jinsi kila mada itakavyochangia katika kubadili maisha yao na mazingira yao ni jambo la motisha yenye nguvu sana kwa wanafunzi.” Mchakato wa utatuzi wa matatizo ni wa msingi katika mkabala wa TOSTAN na wenye kuweza kuchukuliwa na kutumiwa kwa urahisi katika mazingira mbalimbali.

## Matatizo yaliyojitokeza

Mnamo mwaka 1987 hapakuwa na programu za elimu ya msingi kwa kutumia lugha za taifa nchini Senegali, na wizara mbili za serikali zilichangia jukumu la mafunzo ya kujua kusoma na kuandika na mara nyingi zilikuwa zikitapatapa. Programu zilizokuwapo hazikuhusishwa na maisha halisi na zilitumika katika mazingira ambamo watu hawakujua kusoma na kuandika, na stadi zilizofundishwa lakini bila kutumika zilisahaulika baada ya muda mfupi. Programu ya TOSTAN ya elimu ya msingi ilijihusisha na tatizo jingine la uchoshi, kwa kuhusisha kujua kusoma na kuandika na jumuiia ya maisha ya mtu binafsi na kuanzisha vitu vya kuvutia kwa kuzingatia yale yaliyohitajika na mahali hapo. Kuwatafuta waraghabishaji wenye sifa zinazohitajika haikuwa kazi rahisi tangu mwanzo, na pia kulikuwa na upinzani kutoka kwa washiriki kutokana na wazo la kuwalipa waraghabishaji kutoka kwenye rasilimali za mahali hapo. Walitamani fedha hizo zingetumika kwa ajili ya vifaa au kwa ujenzi wa madarasa. Wahitimu wa TOSTAN hivi sasa wame-

kwishapata mafunzo ya kuwa waraghabishaji na wao ndio wenye idadi kubwa ya walimu.

### **Mahitimisho**

Stadi za utatuzi wa matatizo zilizowasilishwa katika mada ya kwanza zinatumiwa katika mada zote zinazofuatia zinazohusu kwa mfuatano huu wa shughuli za elimusiha, stadi za utunzaji wa fedha na vifaa, uendeshaji wa rasilimali watu, upembuzi yakinifu na miradi ya uingizaji mapato. Kwa kutumia stadi hizi wanawake washiriki wameanzisha shughuli kadhaa za biashara. Mbinu ya TOSTAN pia imetumiwa kuwafikia watoto walio nje ya shule kwa mtalaa unaoshughulikia masomo ya kusoma, kuandika, hisabati, utatuzi wa matatizo, afya na elimusiha, lishe, uendeshaji wa familia, haki za watoto, historia, jiografia, elimu kwa ajili ya amani, stadi za uongozi na elimumwendo ya vikundi. Kwa kutumia mkabala wa ushirikishaji, vijana balehe hujifunza kutengeneza matini zao wenyewe.

Kipeperushi cha UNESCO kuhusu TOSTAN kinatoa hitimisho maridadi: “Kuwepo kwa programu kamilika inayowapa washiriki zana za utatuzi wa matatizo na ambayo hushughulikia masuala muhimu ya afya, elimusiha na mazingira ni nyenzo kubwa kwa maeneo mengi ya Afrika yanayokabiliwa na viwango vikubwa vya kutojua kusoma na kuandika hasa miongoni mwa wanawake. Uangalifu mkubwa unapaswa uwekwe zaidi kwenye utekelezaji wa programu hizi zilizofanyiwa utafiti mzuri na majaribio kuliko kuanzisha orogramu mpya nyingine. TOSTAN imeonyesha kwamba watu binafsi hata bila elimu yoyote ya shuleni, watokao katika vijiji vyenye rasilimali ndogo kabisa, wanaweza kuboresha maisha na mazingira yao kwa kupitia programu imara inayopelekea kwenye uwezo zaidi wa kujiamulia mambo na kujitosheleza.



# Kutoka “Kufuru” hadi Uendelevu: Ustawishaji Misitu na Kilimo cha Kutumia Mbolea ya Viumbe Hai huko Forikrom Ghana

Makala hii imeandikwa kwa msingi wa utafiti uliofanywa na wachunguzi wa kutoka Ghana, Kanada na Marekani kwa msaada na usimamizi wa kitaalamu wa Peter Easton, Profesa Mshiriki wa Mafunzo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, na kwa ushirikiano wa jumua husika. Ufadhili wa kifedha ulitolewa na Klabu ya Saheli/OECD, CILSS na Chama cha Maendeleo ya Elimu katika Afrika (ADEA).

***Tini za MA 4  
Januari 1999***

Forikrom, jumua yenye watu 6,000 katika Wilaya ya Techiman (Jimbo la Brong Ahafo) nchini Ghana, iko katika eneo pana la nyasi ambalo wakazi wake hudai kwamba wakati fulani lilikuwa msitu mnene. Kilimo, ambacho ndiyo shughuli yao kuu, huhusu hasa kilimo cha mahindi, viazi, migomba na mihogo kwa matumizi ya wakulima wenyewe na kuuza katika soko la Techman; na kuhusu mazao ya biashara kilimo hulima tumbaku, michikichi na tangu hivi karibuni wanalima korosho. Hapo awali eneo hili lilizalisha kokoa lakini shughuli hii ilikoma mwaka 1983 baada ya mioto kuteketeza mashamba mengi ya kokoa. Ufyekaji zaidi wa misitu ulitokana na njia zisizofaa za kilimo—hasa utumiaji sana wa matrekta uliofanyika katika miaka ya 1960 ambao sasa umetelekezwa—ambao ulidhofisha rutuba ya ardhi na kukausha mito na vijito.

Hivi sasa Forikrom imegeukia kwenye jitihada za urudishaji wa misitu katika mazingira yake, lakini jitihada hizi hazikufanikiwa bila kutokea mgogoro mkubwa wa kitamaduni na wala jitihada hizo zisingeweza kuwa zimefikia kiwango cha mafanikio ya sasa bila msukumo wa kutafuta ufumbuzi mpya yaliyosababishwa na mgogoro huo.

## **Mzozo wa kidini kuhusu maji**

Tatizo lilianza kwa mzozo kuhusu kuweza kutumia “Asukantia” kijito ambacho daima kilikuwa kikiupa maji, lakini kikaanza kukauka. Kili-kuwa kimetengwa kama eneo takatifu kwa muda mrefu katika jadi, na mwiko wa pale ulizuia kuzuru kwenye eneo hilo siku za Jumanne. Amri hii ilifuatwa kidini mpaka mwaka 1989, mwaka ambao ulikuwa wa ukame wa ajabu nchini Ghana. Wakati wa majira ya kiangazi, madhehebu Fulani mpya katika jumua hiyo ilitangaza kuwa mwiko hao ulikuwa umepitwa na wakati na kuwashauri wafuasi wake kutotii amri hiyo. “Kufuru” hiyo mara ilisababisha mgogoro baina ya madhehebu mapya na viongozi wa jadi wa jumua hiyo ambao ndio waliokuwa na jukumu la kutekeleza sheria zilizosimikwa katika jadi: Viongozi hao walishutumua madhehebu hayo mapya kwa kuikasirisha miungu na kuchochea kukauka kwa chanzo hicho cha maji; nayo madhehebu mapya yalilaani desturi hizo za kipagani za utawala wa kijiji.

Mambo yalikuwa yamefikia hali mbaya sana wakati kikundi cha vijana kilipojitokeza. Walitaka kurejesha amani; na walikuwa na maarifa kuhusu uhusiano wa kimazingira kuliko wazee wao, mathalani ule

uhusiano uliopo baina ya urudishaji misitu, ukame na upungufu wa rutuba ya ardhi.

Wakiwa wameongozwa na Katibu Mipango wa chama cha pale kiitwacho “*Mobisquad*”—ambacho ni chama cha vijana kilichoanzishwa chini ya Programu ya Uhama-sishaji ya Taifa mnamo mwaka 1983, ili kuzisaidia jumua za wenyeji mahalia kutekeleza programu za uboreshaji na ukabilianaji na maafa asili—kikundi hiki kilipendekeza kwa jumua kwamba ijaribu kupanda miti karibu na chanzo cha kile kijito kama njia moja ya kurejesha uhai wa kile kijito. Wazo hili, hata hivyo halikumpendeza chifu wala wale wazee ambao waliendelea kujihisi ya kwamba walidharauliwa na viongozi wa yale madhehebu na hivyo wakaamua kwenda mahakani kudai fidia.

Huku wangali wakiamini kuwa suluhisho lilikuwa kupanda miti katika chanzo, kikundi kiliamua kufuatilia na kutekeleza wa wazo lao, wao wenyewe. Kwa bahati nzuri walifurahishwa na manufaa ya kuwepo uongozi wenye mwamko. Uchanganyaji wa mafunzo ya shuleni na uzoefu wa hali halisi ulimpa Katibu Mipango mtazamo muhimu na mpya kuhusu matatizo ya mahali pale. Alikuwa amepitia mafunzo ya msingi, na ya kati pamoja na ya ufundi stadi na alikuwa amefanya kazi katika nyadhifa mbalimbali kama vile ualimu, umlipaji fedha wa serikali mahali pengi nchini Ghana na uuzaji bidhaa nchini Nigeria. Zaidi ya hayo, yeye binafsi alikuwa na “vitambulisho” vya Uinjili kama mtaalamu wa fasihi wa chama fulani cha kimisionari. Baadaye kidogo ilidhihirika, hata hivyo, kwamba si yeye wala si wanakikundi wengine pia, wote waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu changamoto maalumu ya ukuzaji wa miti ili kufanikisha juhudi zao. Ukosefu wao huo wa uzoefu ulisababisha kuwepo na ugumu kwa viongozi wa jadi kuwaamini.

### Kupata maarifa ili kuanza upya

Kwa kujua kikwazo hiki, Katibu Mipango aliwasih wenzake kutafuta maarifa na stadi ambazo hawakuwa nazo. Kwanza walimwendea ofisa mwandamizi mmoja na mjumbe wa ofisi ya Jimbo ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima mjini Sunyani yenye jukumu la kazi za uenezi za Jimbo la Brong Ahafo. Ofisa huyo alikitembelea kijiji hiki na hatimaye akasaidia kikundi kutembelea mara kadhaa shule ya Misitu na Idara ya Misitu, Sunyani, yapata kama kilomita 100 kutoka Forikrom. Kila waliporudi nyumbani, walijadiliana walichokuwa wamejifunza katika jumua, hasa chifu pamoja na wazee. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 1989 kile kikundi kilikuwa kime-wafanya wale viongozi wa jadi waamini kwamba kufungua madai mahakamani hakukuwa suluhisho la mata-

tizo ya jumua. Pia kikundi kilikuwa kimefanikiwa kupata msaada kutoka kwenye Shule ya Misitu pamoja na Idara ya Misitu ili kuanza mradi wa upandaji misitu (miti).

Mradi ulizunduliwa rasmi mnamo mwaka 1990, katika mkutano ulioandaliwa na kikundi kwa kushirikiana na Ofisi ya Sunyani ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Katika mkutano huo, wataalamu kutoka Shule ya Misitu ya Sunyani na kutoka ofisi za Idara ya Misitu za Sunyani na Kumasi, ambao kikundi kilikuwa kimefanya kazi nao, walizungumza kwa zamu kuelezea umuhimu wa kupanda misitu (miti). Walisisitizia manufaa yake kama njia ya kuleta ukanda wa hifadhi kandokando ya vyanzo vya maji, hifadhi dhidi ya uharibifu mbaya utokanao na hali ya hewa, kuwa kinga dhidi ya upepo na kuwa kanda za kuzuia moto kuzunguka makazi ya jumua, kusaidia kuhifadhi rutuba ya ardhi na pia kuzalisha kuni na mkaa kwa kupikia.

Wakiwa wameridhishwa na hoja hizo, wazee wa jumua waliridhia wazo la kuzindua mradi wa kupanda misitu, na kisha wakashiriki katika masomo ya mwanzo kuhusu uandaaji vitalu vya miti yaliyotolewa na Maofisa Misitu wawili kutoka Sunyani ambao walikuwa wawezeshaji. Wakati wa mfululizo wa ziara za mafunzo ya uenezi muda wa saa sita yaliyotolewa na maofisa hawa kwa kipindi cha miezi sita, vikundi vya watu 30 waliongozwa na kukamilisha mambo muhimu jinsi ya kutayarisha ardhi na kutengeneza matuta, kutunza miche, kuhamisha miche na kuitunza hiyo mimea michanga. Jumla ya watu kama 2,000 hivi wengi wao wakiwa watu wazima wa Forikrom walishiriki katika mafunzo haya.

Kwa msaada wa kitaalamu kutoka kwa wawezeshaji na kiasi kidogo cha msaada kutoka mashirika ya nje kama shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Wakala wa Misaada ya Maendeleo la Waadventista Wasabato, kikundi kilianzisha baadaye bustani ya kuotesha miti mipya, hasa kwa lengo la kurudisha misitu na polepole kwa kilimo cha biashara kadhalika. Miche ya mikoroshu, michikichi na mivule ilitolewa kwa wanajumua kila mmoja akapande nyumbani kwake. Kufikia mwezi Oktoba mwaka 1993, mradi ulikuwa umegawa miche 15,000 bure kwa vikundi vingi vilivyotoka sehemu nyingine kutembelea bustani ile. Katika kufanya hivi Katibu Mipango na watu wengine kumi walipata maarifa ya kutosha na kuwa wawezeshaji wa kutumainiwa. Taratibu mradi ulikuwa kitovu cha uenezaji misitu kwa ajili ya eneo lote la jirani.

Mwishoni mwa mwaka 1995, baada ya kuanzisha kwa ufanisi soko la miti ya mivule, michikichi na mikoroshu, aina zilizokuwa na uwezekano wa kupata mauzo mazuri, mradi uliamua kufanya shughuli za uoteshaji na ugawaji

wa miche kuwa shughuli za kibiashara; na mapema mwaka 1996 mradi ulishuhudia mauzo yake ya kwanza ya miche ya michikichi. Mahitaji ya mvule ilielekea yangeongezeka kadiri wakulima wa eneo lile walivyoendelea kupanda miti kama kinga dhidi ya moto na kwa kutazama mbali, pia mahitaji ya jumla kwa ajili ya milingoti ya simu na umeme yaliongezeka. Kuhusu korosho, kilimo chake kimezua mvuto wa kutosha ndani ya jumua ya Forikron na katika maeneo ya jirani pia. Katika jumua yenyewe, katika miaka ya karibuni wakulima wamepanda mikorosho zaidi ya ekari 100, kufuatia kuanza kuongezeka kwa bei ya korosho kadiri mikorosho inavyozidi kukomaa.

### **Upanuaji wa taathari: uhifadhi wa mazingira na kilimo cha kutumia mbolea za asili**

Ile jitihada iliyotokana na mgogoro kuhusu chanzo cha maji ilikuwa na matokeo mengine mazuri pia. Chama cha kuhifadhi Mazingira cha Forikrom (EPA) ambalo ni chipuo la mradi wa kupanda misitu, kilipiga hatua na kupata heshima wakati shirika la Wakala wa Kuhifadhi Mazingira nchini Ghana lilipotumia tawi la Forikrom kama makao ya kupanulia wito wake wa matumizi mazuri ya mazingira katika jumua zilizo kati ya Techman na Nkoranza. Tangu mwaka 1994, tawi la Forikrom la EPA limekuwa likialikwa kwenye mfululizo wa warsha za shughuli za bustani na utunzaji miti zilizoandaliwa na wakala wake mjini Kumasi. Kisha walitayarisha warsha kama hizo kwa ajili ya wateja wa mahali mbalimbali na polepole Forikrom yakawa makao ya mfululizo mzima wa matukio ya mafunzo ya usimamizi wa maliasili na misitu, yaliyokuwa yakifadhiliwa na wafadhili mbalimbali.

Chipuo la pili la mgogoro kuhusu haki za maji limekuwa kuanzishwa kwa Mradi wa Kilimo cha kutumia mbolea za mimea ya asili wa Abrono (ABOFAP). Ukiwa umebuniwa na Katibu Mipango na wenzake mwaka 1992, mradi huu ulianzishwa ili ushughulikie mambo yanayohusu upungufu wa rutuba uliosababisha kuzuka kwa mgogoro wa "Asukantia." Malengo yake mahususi yalikuwa kuwafunza wakulima vijana uzalishaji mazao kwa kilimo cha kutumia mbolea za mimea, kukuza matumizi ya mbolea-vunde ili kuboresha hali ya udongo (na kuzuia utumiaji wa dawa za kemikali), njia za kilimo cha kiangazi cha bustani ya mbogamboga na uzalishaji wa uyoga.

Katika kipindi cha mwisho cha mwaka 1990, Katibu Mipango akifuatana na mwanamke mmoja (aliyekuwa amehitimu shule ya Kati) na mwingine ambaye hakuwa na ajira, kutoka Forikrom walihudhuria mafunzo ya siku

tano mjini Kumasi yaliyoandaliwa na Programu ya Africa 2000. Kwa kuunganisha saa kumi na mbili za masomo darasani na saa kumi na nane za vitendo halisi na kwa kuangalia kwa makini kwenye mashamba ya maonyesho, mafunzo yao yalihusu shughuli za bustani ya miche, kilimo misitu na utengenezaji wa mbolea-vunde. Ujuzi huu ulifuatwa na kushiriki katika warsha nyingine kadhaa na kutembelea mahali halisi ambako kuliongeza kitu zaidi kwenye maarifa ya awali kuhusu mbinu za kilimo cha kutumia mbolea za mimea.

Hivi karibuni Katibu Mipango alianzisha mashamba ya maoneysho shambani kwake kule Forikrom ili kuchochea ari kuhusu kilimo cha kutumia mbolea ya mimea miongoni mwa vijana. Alianza na wanamafunzo ishirini—kumi wanaume na kumi wanawake—wote wamehitimu shule lakini wasio na ajira wenye umri kati ya miaka 17 na 25. Aliwagawa katika makundi ya wannewanne na kila kikundi kukipa maeneo ya kushughulikia karibu na kijito cha Asukantia.

Kufikia mwaka 1996 ABOFAP ilikuwa imetoa mafunzo kwa vijana 130 (75 wanaume na 55 wanawake), wengi wao wakiwa waliohitimu shule ya kati lakini wasio na ajira na waishio na wazazi wao; katika kilimo cha kutumia mbolea ya mimea na kilimo cha kiangazi cha bustani za mbogamboga. Mafunzo haya ya miezi mitatu ambayo vijana hawa walipata, yalifungua mlango muhimu wa kujiajiri wao wenyewe. Mathalani, wakati wa duru ya kwanza ya miezi mitatu, kundi la wanamafunzo ishirini na watano wa kwanza walizalisha pato la jumla ya cidi 200,000 au dola za Marekani 355, kutokana na mauzo ya mbogamboga, wakagawana sawa pato halisi la cidi 160,000 au dola za Marekani 308 kila mmoja (thamani ya fedha za kigeni mwezi Desemba, 1992 ilikuwa cidi 519 = dola za Marekani 1.00).

Isipokuwa kama kiasi cha asilimia 10 ya wanamafunzo walioona kuwa kilimo ni kazi ngumu mno wakaacha, washiriki wengine wote sasa wanajitegemea na wanaendelea vizuri. Wanamafunzo wa mwanzo wamejiunga katika kilimo cha korosho na wana matumaini makubwa sana kwa siku za usoni. Karibu vijana 200 kati yao wamejiundia ushirika katika vikundi vya watu 6 mpaka 10 kuanzisha kilimo cha mapande ya maeneo baina ya ekari 1 mpaka 2 kando ya kile kijito.

Jambo la kufurahisha ni kwamba Katibu Mipango hakujitwalia uongozi katika asasi zozote alizozianzisha na kuziendeleza. Badala yake amewashauri wengine kushiriki katika uongozi wao wenyewe. Mathalani, mzee mmoja mkulima asiyejua kusoma na kuandika ndiye rais wa mradi wa kupanda miti wa Forikrom wenye wana-chama 2000, na Katibu Mipango anaongoza kama Katibu; ambaye pamoja na wengine watatu anashiriki kama

mjumbe wa Kamati Tendaji. Vivyohivyo, mkulima mzee wa miaka 60 ambaye ana cheti cha kuhitimu Shule ya Kati ndiye rais wa chama cha Kuhifadhi Mazingira cha Forikrom chenye wanachama 90. Na kijana wa umri wa miaka 23 aliyehitimu elimu ya sekondari ndiye Katibu wa ABOFAP chenye wanachama 20.

#### **Uletaji amani kati ya jumuiia na mazingira**

Kumefanyika maendeleo makubwa katika jumuiia ya Forikrom ndani ya kipindi cha pungufu ya muongo mmoja. Vyanzo vipya vya utajiri vimeanzishwa. Lakini matokeo muhimu kuliko yote ya juhudi za Furikrom, kwa kweli ni yale yasiyoweza kushikika kwa mkono. La kwanza kati ya hayo ni uhusiano wa kidugu katika jamii. Utengano wa jumuiia uliokuwa umeoteshwa na mzozo baina ya madhehebu ya kidini na wakuu wa kijadi ulitulia baada ya jumuiia yote iliposhikamana na kuzungushia ukanda wa kuhifadhi eneo la kijito cha Asukantia.

Mwamko uliotokana na jumuiia kuhusu upandaji miti, mazao mapya, zana bora, na utambuaji wa bidii ya kazi kutoka kwa asasi zilizo nje ya jumuiia vimesaidia sana kila mmoja kusahau tukio moja lililoanzisha yote haya. Kuwa na jumuiia inayotambua muhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira ambayo inakuwa kama mfano kwa miji mingine katika eneo hili; sio jambo dogo lisilo na umuhimu. Wakati wa miaka sita iliyopita ukanda mzuri wa hifadhi ukiwa na ekari nne za miti ya mivule na ekari tatu za *leucenea* umejengeka kuzunguka chanzo na kijito cha Asukantia.

Sasa hivi yapo maji mengi katika kijito, na hiyo imewafanya watu katika siku za karibuni kuwa huru na kujiamini vya kutosha kutumia maji hayo kwa shughuli za bustani wakati wa kiangazi. Zaidi ya hayo, viongozi wa hapo wanasema kwamba watu hawachomi tena vichaka hovyoy, na kutokana na hayo hapajawa na mioto ya vichakani tangu mwaka 1990.

# Ujuzi wa Kusoma na Kuandika kwa “Watoto Wadogo” huko Nomgana

Makala hii imetokana na utafiti uliofanywa na wachunguzi Waburkinabe, Wakongo na Wamarekani kwa msaada na usimamizi wa kitaalamu wa Peter Easton, Profesa Mshiriki wa Mafunzo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, na kwa ushirikiano wa jumuiia husika. Ufadhili wa kifedha ulitolewa na Klabu ya Saheli/OECD, CILSS na Chama cha Maendeleo ya Elimu barani Afrika (ADEA).

**Tini za MA 5  
Februari 1999**

Nomgana ndiyo jumuiia kitovu ya muungano wa vijiji hai sana katika Wilaya ya Loumbila, iliyo kilometa 30 Mashariki mwa Ouagadougou, Mji Mkuu wa nchi ya Burkina Faso. Chama cha pale kijulikanacho kwa jina la kupanga kama Manegbzanga (“Maendeleo kwa Wote” katika lugha ya Moore) kiliundwa katika eneo hilo zaidi ya muongo mmoja uliopita kutokana na juhudi za pamoja za wahamiaji waliorudi kutoka nchi ya jirani ya Côte d’Ivoire na mwenyeji mmoja aliyekuwa amekwenda kufanya kazi katika asasi moja ya Kiswisi isiyo ya Kiserikali, Organisme Suisse d’Entraide Ouvrière (OSEO). Katika miaka ya karibuni, chama hiki kimezindua programu ya majaribio kwa kutumia ujuzi wa kusoma na kuandika wa lugha ya Kimoore kama misngi wa kujifunza Kifaransa. Shughuli hii imeumuka kwa miaka kadhaa iliyopita na kujibadili kuwa mkakati mbadala wa ufundishaji katika shule za misngi.

**Kutoka ujuzi wa kusoma na kuandika kwa watu wazima mpaka kupata mbadala wa kujifunza shuleni**

Jitihada zilianza, hata hivyo, kwa watu wazima. Chama cha Manegbzanga kilikabiliwa mapema na tatizo la

kuwawezesha wanachama wake, wengi wao wakiwa wale ambao walikuwa wamesoma shule kidogo tu au hawakuwa wamesoma kabisa—kuendeleza shughuli zao zilizokuwa zikikua kutokana na kuwashughulikiwa na watoaji wa pembejeo za kilimo na wanunuaji wa mazao yao katika eneo la mji wa Ouagadougou. Mtu mmoja wa jumuiia hii ambaye alikuwa amekuwa mfanyakazi wa serikali na kisha akawa Mkurugenzi wa ugani wa Asasi Isiyokuwa ya Serikali ya Kiswisi, alianza kushirikiana na wanakijiji mnamo mwaka 1988 kuanzisha mfumo wa ufundishaji ambao ungewawezesha watu wazima waliofundwa katika vituo vya kusoma na kuandika kuendelea kutoka kujua Kimoore’ kilichoandikwa na kujifunza kifaransa cha kuzungumza na cha kuandika.

Programu hii ilipata mafanikio mengi na baadaye kidogo ilikabiliwa na tatizo la kuongezeka kwa mahitaji ya kujisajili kwa vijana—watoto na vijana wenye balehe—ambao walikuwa wamekosa masomo ya shule za msingi au walikuwa wamelazimika kuacha shule. Kamati ya kujua kusoma na kuandika ya kijiji mwishowe iliamua kukubali changamoto ya kuanzisha programu ya “Ujuzi wa kusoma na kuandika kwa watoto wadogo” (*alphabelisation des tout petits*). Mkakati wa ufundishaji

ulianzishwa kwa msaada wa wanaisimu wa Chuo Kikuu cha Ouagadougou. Unaendelea kuanzia kupata stadi za kujua kusoma kuandika na kuhesabu kwa lugha ya Kimoorè mpaka kujifunza Kifaransa na kujifunza masomo yote ya shule ya msingi. Watoto wanaoashiriki humaliza kiwango kama kile kiwango rasmi cha masomo shuleni kwa miaka minne, badala ya miaka sita iliyo-wekwa (na mara nyingi hata miaka mingi zaidi kwa sababu ya kurudia darasa). Zaidi ya hapo, hupata ujuzi wa umbo la maandishi la lugha yao wenyewe.

“Nadharia yetu ya kutumia” anaeleza profesa mwanaisimu wa Chuo Kikuu cha Ouagadougou, ambaye alisaidia kuanzisha programu hii; “ni kwamba ujuzi wa lugha ya Kiafrika na kuitumia katika kujifunza kusoma na kuandika kwa lugha hiyo unasaidia sana kwa kiwango kikubwa kuzipata stadi zilizopangwa shuleni na ni kipunguzo cha muda unaotakiwa kumaliza rasmi mafunzo ya shule ya msingi, na uboreshaji wa kiwango cha ushindi wa mitihani ya masomo ya shule ya msingi. Lakini programu ya vituo vya Nomgana pia ilianzishwa kwa kutilia maanani vipengele vingine kadhaa vya sifa ya kisomo cha shuleni. Ubunifu wenye mpangilio imara ulifanywa ili kuzingatia shughuli za uzalishaji mali katika kilimo pamoja na utafiti wa utamaduni wa mahali husika katika mtalaa, wazazi walipewa nafasi ya pekee ya kushiriki katika uendeshaji wa shule, na “wawezeshaji” wenyeji wa pale—hasa wasanii na magrioti (wanahistoria wa jadi na watamba hadithi)—walialikwa kufundisha madarasani.

### **Kukidhi haja ya watoto walioachwa**

Kazi za ufundishaji zilifanywa na vijana wa mahali pale wale ambao hawakuwa na ajira kwanza na ambao angalau walikuwa na sehemu ya elimu ya sekondari, ingawa hapo awali hawakuwa na ujuzi wowote wa kufundisha. Walifunzwa kwa njia iliyoenezwa na wafanyakazi wasimamizi kutoka Chuo Kikuu cha Ouagadougou. Idadi kubwa ya wanafunzi walitokana na watoto wa Nomgana na kijiji cha jirani cha Gouè ambao walikuwa hawajapata kuandikishwa katika shule ya msingi ya pale, mara nyingi kwa sababu familia zao zilikuwa zimemchagua ndugu mwingine katika familia kusoma. Kwa hiyo, hawa walikuwa wamevuka kabisa ule umri wa kuanza shule uliowekwa kinadharia (miaka 7) walikuwa wenye wastani wa miaka 10 wakati wakiingia katika programu hii, na kwa mawazo ya jamii waliitwa “wenye matumaini madogo ya kufaulu”. Watayarishaji walihakikisha ya kwamba karibu idadi ileile iliyo sawa ya wasichana na wavulana inaandikishwa katika programu. Kwa jumla

watoto 55 walishiriki katika awamu ya kwanza, wakagawanywa katika madarasa mawili; kwa uwiano wa Wanafunzi na Mwalimu wa 28:1. Kama maandalizi muhimu, wote walitakiwa kumaliza kozi ya haraka (ya miezi 6) ya kujua kusoma na kuandika katika lugha ya Kimoorè.

Miaka miwili ya mwanzo ya ufundishaji ilifanyika kwa Kimoorè, ingawa Kifaransa kilifundishwa kama somo. Kufikia mwaka wa tatu, wanafunzi walikuwa wakitumia vitabu vilevile vya Kifaransa kama wale wenzao waliokuwa katika mfumo wa elimu ya msingi shuleni: Zaidi ya hayo, walifuga mifugo ambayo—katika kipindi cha masomo cha mwaka 1997-1998—iliwapa faida halisi ya Faranga za CFA 233,000 (karibu \$ 425) na walilima karanga na kunde (nièbè) kama sehemu ya masomo yao. Hapakuwa na aliyeshindwa katika programu hiyo, ambapo kiwango cha wastani wa msuguanu wa kushindwa baina ya mwaka wa kwanza na wa mwisho katika mfumo rasmi wa elimu ya msingi shuleni nchini Burkina Faso ni zaidi ya asilimia 40.

### **Matokeo ya kushangaza**

Mitihani iliyotolewa mnamo Desemba 1996 katika shule iliyotumia lugha ya Kimoorè na shule ya msingi ya jirani, ilidhihirisha kwamba wanafunzi katika kituo walikuwa mbele kimasomo kuliko wale wa shule ya msingi ya kawaida katika masomo ya Kifaransa na Hisabati, na zaidi ya hapo bila shaka, walikuwa na manufaa ya kuwa na ujuzi mzuri wa kuandika lugha yao ya mama. Cha kufurahisha pia ni kwamba kiwango cha uwezo wa wasichana katika kundi lile (ambao walikuwa wengi kidogo) kilikuwa juu kabisa ya kile kiwango cha wavulana wa ile shule ya msingi ya kawaida, ingawa kiwango hicho kilikwua chini ya kiwango cha wavulana waliokuwa katika kituo cha majaribio. Matokeo haya yalithibitishwa zaidi katika mwaka uliofuata wakati kundi la kwanza la shule iliyotumia lugha ya Kimoorè lilipofanya mtihani wa cheti cha kumaliza elimu ya msingi. Viwango vya mafanikio miongoni mwa wanafunzi 53 waliofanya mtihani huo vilikuwa asilimia 53 (asilimia 62 kwa wavulana na 44 kwa wasichana) ukilinganisha na kiwango cha asilimia 62 cha wastani cha taifa kwa shule zote rasmi nchini Burkina Faso (asilimia 47 katika Jimbo la Oubritenga) na kiwango kipana zaidi cha tofauti baina ya usawa wa kijinsia.

Wakati watayarishaji wa progamu na viongozi wa jumua wameridhika na matokeo ya programu mpaka leo, wanataja vikwazo vichache vilivyotokana na jitihada zao za kutaka kupatana na mfumo rasmi wa shule ya msingi na kuhakikisha ulinganifu kamili wa vyeti.

Ugumu wa mipango iliyowekwa awali na ugawanyaji wa muda kwa mada mbalimbali unaotakiwa kwa ajili ya tathmini katika mfumo rasmi ulipingana na baadhi ya mambo muhimu sana ambayo yalikuwa yakijaribiwa na kituo cha Nomngana—kwa mfano kuingiza katika mtalaa vifaa vilivyo katika mazingira pamoja na wawezeshaji wa mahali pale, na kujihusisha moja kwa moja na kazi za shamba.

- Baadhi ya maudhui katika vitabu vya Kifaransa hayakufaa kabisa tena kutumika mara baada ya kufasiriwa kwa Kimoorè.
- Kupatana na mapigo na mahitaji ya mtalaa rasmi—na kuukamilisha katika wakati mfupi ulitolewa—walimu iliwabidi kwa kiasi kikubwa kufundisha kwa Kimoorè moja kwa moja baada ya mwaka wa pili, pamoja na ukweli kwamba baadhi ya matokeo mazuri ya kujifunza yalitokea katika masomo yaliyokuwa yamefundishwa katika lugha mama ya wanafunzi. Kusema kweli, mara nyingi wanafunzi waliofaulu kidogo sana katika eneo la lugha ya Kifaransa katika mtalaa na mitihani iliyofuata ya kuingia darasa lingine walikuwa wale ambao pia hawakuwa wamepata msingi “mzuri” katika kujua kusoma na kuandika lugha ya Kimoore kabla ya kuandikishwa.

### Uthibitisho kutokana na wenyeji

Kwa upande mwingine takriban wadau wote walikuwa wamekubali kwamba jitihada zilifanikiwa pale ambapo, kwa wakati huu, palikuwa muhimu sana: katika kuwawezesha wale watoto “waliotelekezwa” kupata idhini rasmi huku wakiimarisha uwezo wao katika Lugha yao na utamaduni: na kwa kuonyesha uwezekano na umuhimu wa ufundishaji wa mikabala ya lugha za Kiafrika katika kujifunza Kifaransa na kujua maudhui ya

shule ya msingi. Mazingira ya kuvutia kiasi cha shule ya majaribio ni wazi sharit yazingatiwe katika kulinganisha matokeo ya aina mbili za madarasa hayo—hasa upatikana kwa uhakika wa vifaa vya kufundishia na ukweli kwamba hakuna yeyote kati ya wanaosoma hapo aliye-toka nje ya uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu kama ilivyogusiwa; ukilinganisha na uwiano katika sehemu za vijijini, hakuna aliyetoka jumua nyingine au anayelazimika kila siku kwenda safari ndefu kwa miguu. Lakini tofauti katika mifululizo miwili ya data hizi, ambayo kwa hakika haizingatii mtalaa uliozingatia hali halisi ya mahali ilimo ile shule mbadala iliyotia fora angalau inaelekea kueleza kwa dhati kwamba mbinu kama hizo zinaweza kutoa matokeo yaliyo na kiwango kama kile cha masomo yanayofundishwa rasmi shuleni.

Profesa wa isimu aliyezungumziwa hapo awali anaeleza jambo hili kinagaubaga akisema: ‘Tunatumaini kwamba jaribio hili litachangia katika kupanda vikwazo vya kutumia lugha za Kiafrika katika mfumo wetu wa elimu, kama njia fupi ya kufupisha muda na kupanua upatikanaji wa elimu ya msingi na pia kama daraja jipya baina ya elimu itokanayo na mfumo rasmi na ile isiyotokana na mfumo huo’.

“Wakati huohuo” anaongeza “uzoevu huu unatuwezesha kufikiria upya njia za kushughulikia hali yetu ya ulumbi, ambalo ni jambo moja lenye ukweli usiopukika katika mazingira ya bara la Afrika. kufupisha mzunguko mrefu wa masomo ya shule ya msingi kunaruhusu kuwepo muda wa kutosha kupata ujuzi ipasavyo na nafasi ya kutumia lugha ya taifa iliyoandikwa katika mtalaa wa shule...kwa kifupi, lugha zetu zimekuwa, nyathirika za mtazamo wa kudharauliwa bila sababu uliopandikizwa na vitendo vya kikoloni; na hivyo ubishi unaosisitizwa na baadhi ya watu kuhusu kupambanua lugha za Kiafrika na Kifaransa hatimaye hauna maana.”

## Wanakijiji-wamiliki Benki: Uzoefu wa Fandène

Makala hii imeandikwa kutokana na utafiti uliofanywa na wachunguzi wa Senegali, kwa msaada na usimamizi wa kitaalamu wa Peter Easton, Profesa Mshiriki wa Masomo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, na kwa ushirikiano wa jumua husika za Kiafrika. Utafiti huu ulifanyika chini ya ufadhili wa ushirikiano wa Klabu ya Saheli/OECD, CIILSS na Chama cha Maendeleo ya Elimu barani Afrika (ADEA).

### **Tini za MA 6 Machi 1999**

Fandène, kijiji cha Waserere na Wawolof ni kijiji kilichoko umbali wa kilometa sita kutoka mji wa Thieś, nchini Senegali, katika eneo linalolima karanga kwa wingi. Ni Makao Makuu ya Asasi ya Akiba na Mikopo iliyoanzishwa pale na inayotoa huduma bora. Kwa sasa inahudumia vijiji 34 katika eneo zima, imelimbikiza mtaji wa zaidi ya milioni thelathini za faranga za CFA (takribani dola za Marekani 60,000) ilitoa mikopo zaidi ya 1500 kwa watu wa jumua hizo. Hata hivyo, chombo hiki kilikua kutokana na kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya ukame na upungufui wa rutuba mashambani, matatizo ambayo yanayolikumba eneo lote la kati-kati mwa Senegali.

Kijiji cha Fandène chenye matokeo ya mwingiliano wa kihistoria baina ya makabila ya Waserere na Wawolof. Kwa kiwango kikubwa, hiki ni kijiji cha Kikristo na kwa miaka mingi kilikuwa ni makao ya misheni ya Kikatoliki na kituo cha ustawi wa jamii (*"Maison Familiale Rurale"*), lakini hugawana rasilimali inayodidimilia iliyo katika bonde la mito ya majira ya mvua na jumua za Kiislamu na zile zinazoamini dini za jadi kutoka makabila mbalimbali. Jitihada za maendeleo za hivi karibuni zimejitokeza kiasi kutokana na vitendo vya wahamiaji kutoka Fan-

dène kuhusu mateso ya janga kuu la ukame wa ukanda wa Saheli mwanzoni mwa miaka ya 1970. Katika juhudi za kusaidia jumua zao kupata unafuu wa janga hilo na kuepuka watu kupukutika, vijana waliokuwa wamehama kwao kwa ajili ya masomo au kutafuta ajira walisaidia katika uanzishaji wa Chama cha Vijana wa Fandene (*"Association des Jeunes de Fandène AJF"*) mnamo mwaka 1972.

### **Kutoka utamaduni mpaka kilimo**

Kwa miaka kumi na mitano ya mwanzo ya kuanzishwa kwake chama cha AJF kilijishughulisha katika kusaidia matukio ya kitamaduni ambayo yangewavutia vijana kuzingatia au kurejea katika jumua zao za nyumbani na wakati huohuo kuimarisha utambulisho wa utamaduni wao. Juhudi za kuanzisha miradi ya maendeleo zilikuwa ndogo sana, lakini shughuli za AJF ziliwafikia vijana wa makamo na wasomi wazuri wakarudi wakaishi tena kijijini na kuanza kuungana wao kwa wao kama wakulima wadogo wa kisa na makini. Polepole kikundi hiki kilizidi kukua na kuzidi kutoridhika na programu ya AJF iliyojishughulisha tu na matukio ya kitamaduni



na pia uongozi ambao kwa kiasi kikubwa ulikuwa umeshikwa na watu waliokaa nje.

Kwa hiyo, mnamo mwaka 1987, chama hiki kilianzisha mtazamo mpya. Kwa kuzingatia matukio yaliyojirudia-jirudia kwa mzunguko ya upungufu wa chakula katika eneo lile, wanachama wa chama hiki walianzisha mfululizo wa uchunguzi wa “utafiti-vitendo” na watu wa vikundi vingine vya jirani ili kuelewa vizuri zaidi jinsi tatizo lilivyo na utatuzi unaoweza kufanyika. Mambo matatu yaligundulika katika utafiti huu:

- Kikundi kiligundua kwamba kumbe tayari kulikuwapo juhudi nyingi ndogondogo zilizokuwa zikifanywa na vikundi vya wakulima wenyewe—jitihada ambazo zilikuwa na matumaini ya kuweza kufanya shughuli anuwai za uchumi wa pale na pia kuboresha msingi wa maliasili ya pale. Lakini vyote hivi vilikuwa vimedumazwa kutokana na kutokuwepo utaratibu wa kufaa kujipatia mikopo na rasilimali ili kuendeleza hazina hii.
- Kukosekana kwa mikopo kulitokana kwa kiasi kikubwa na kutokuwepo vyombo madhubuti au asasi ambavyo vingewawekea dhamana wenyeji ili wachukue mikopo na kuwasimamia.
- Wakati huohuo wanachama wa AJF walijifunza utaratibu na matokeo ya miradi iliyoendeshwa na AZISE katika eneo lilelile na kuhitimisha kwamba miradi mingi ilishindwa kwa sababu ilikuwa imeundwa kwingine na haikuwa imetokana na juhudi zilizopo za wenyeji wa pale.

### Utatuzi wa vikwazo vya mikopo

Uamuzi ulikuwa kukabiliana na matatizo haya kwa kuanzisha aina fulani ya asasi isiyo rasmi ya akiba na mikopo ya mahali husika. Kusema kweli hatua za mwanzo zilikuwa ndogo: kila mwanachama alichanga faranga 250 (takribani dola za Marekani 1.00 kwa wakati ule) kwa ajili ya mfuko wa pamoja na mikopo midogo ikaanza kutolewa kwa wanakijiji waliokuwa na miradi ya kuaminika kwa kutoza kiasi cha asilimia 15 cha riba ya mtaji kwa mwaka, huku zikitafutwa njia zingine za kutunisha mfuko. Mojawapo ya njia hizo ilikuwa ni kupanua uanachama kwa jumua mpya katika mkoa wa jirani. Hapakuwa na haja kubwa ya kutangaza jambo hili. Jitihada hizi zilikutana na hisia changamfu na zenye mahitaji ya dhati kiasi kwamba wakazi wa vijiji vingine baada ya muda si mrefu walipata uvumi kuhusu nini kilichokuwa kinatokea na wao wenyewe wakaanza kuuliza kama wangeweza kushiriki.

Kwa njia hii, mtandao wa akiba na mikopo ulienea polepole katika jumua zote 34 za eneo la Fandène na polepole ukaanza kupata utaratibu mzuri wa kutumika. Kila tawi la taasisi hiyo—19 kwa jumla—lilikuwa na sehemu ya wanawake na sehemu ya wanaume, na viongozi wa kila sehemu walipata mafunzo ya msingi ya uhasibu, ukopeshaji mikopo, tathmini ya utoaji mikopo na usimamizi wa mikopo. Wakazi wa jumua zilizohusika walihimizwa kupeleka maombi ya mikopo kwa maandishi kupitia kwa maofisa wenyeji wa mahali pao, na uongozi wa taasisi ulijifunza polepole katika kufanya tathmini yakinifu ya mikopo iliyopendekezwa na kuwapa misaada ya kitaalamu wale ambao wangepokeshwa ili kuhakikisha kwamba shughuli zao zinastahili mikopo. Hatimaye timu ya watathmini iliundwa kusaidia kamati za akiba na mikopo za mahali husika ili kujifunza mbinu za kuthamini maombi ya mikopo na kutambua pamoja na kuoanisha miitikio ya mahitaji ya utaalamu ya shughuli ndogondogo za biashara.

### Kutoa msaada kwa ajili ya uvumbuzi wa kiuchumi wa mahali

Chama cha akiba na mikopo kilichopanuka kiliweka msisitizo wa pekee kwenye kuwasaidia wakulima na shughuli ndogondogo za biashara kwa mbinu mpya ya kufufua kilimo na uuzaji wa mazao yaliyopatikana. Ifuatayo ni mifano ya mambo yaliyofanywa yaliyoandikwa wakati wa miaka mitano ya utekelezaji:

- Vikundi vya wanawake vya uzalishaji vilisaidiwa kuanzisha mipango ya soko kwa ajili ya kuwaruka walanguzi na kuuza matunda ya *bissap* yaliyovunwa katika misitu ya jirani na pia vikapu vilivyotengenezwa kutokana na mimea ya pale kuuzwa moja kwa moja katika soko la Dakar na kadhalika katika vyama vingine vya vijiji vya eneo hilo. Kufikia mwaka 1995 kila wiki vikapu elfu moja vilikuwa vikitengenezwa kwa njia hii.
- Chama kilitoa mikopo kwa wakulima waliopenda kuanzisha tena kilimo na uuzaji wa muhogo katika eneo hili na upanuzi wa upandaji na matumizi ya kunde.
- Mikopo ilipelekwa kwa vikundi vya wanawake kwa ajili ya kuanzisha ushirika wa kutengeneza sabuni na kuuza mazao yake.
- Taasisi za akiba na mikopo zilitoa mikopo mingi kwa ajili ya uchimbaji wa visima, uendelezaji wa bustani za kumwagilia na mauzo ya mazao yake.

Kadiri shughuli zilivyoendelea na dau la mtaji kuongezeka, ndivyo pia viwango na ukubwa wa mikopo vilivyoongezeka. Kwa kipindi cha miaka mitano ya mwanzo ya utekelezaji, wastani wa matumizi ya kila mwaka ulikuwa wa aina zifuatazo:

Uendelezaji mifugo na uuzaji—Faranga za FCFA 5,600,000

Biashara ndogondogo na viwanda—Faranga za FCFA 2,800,000

Kilimo bora faranga za FCFA—500,000

Uchimbaji wa visima—500,000 FCFA

Faida za kila mwaka kutokana na usimamizi wa mikopo zilipanda kutoka kuwa chini ya Faranga za FCFA 100,000 mnamo mwaka 1991 kufikia zaidi ya 700,000 katika mwaka 1994 na kufikia mwaka 1998 dau la mtaji wa Chama cha Vijiji cha Akiba na Mikopo lilikuwa limeongezeka kwa zaidi ya Faranga za FCFA milioni 30 au takribani dola za Marekani 60,000.

### Usukaji wa mfumo mpya wa kijamii na kiuchumi

Jambo la kuvutia kushinda yote lilikuwa ni yale matokeo ya ujenzi wa taasisi za shughuli hizi na uhusiano wa bega kwa bega kati ya jumua za Senegali na vikundi mbalimbali vya watu yaliyolelewa na jumua hizo. Kwa upande wa dini, vijiji vyote thelathini na vinne vya eneo la Fandene ni vya Wakristo, Waislamu na watu wanaoamini miungu ya jadi na pia kuna mchanganyiko wa makabila mbalimbali (Waserere, Wawolof, Wabambara, Wafulani). Hata hivyo, vimeshirikiana pamoja kwa mafanikio makubwa katika kuanzisha taasisi mpya za akiba na mikopo na kushiriki katika uendeshaji wa shughuli na rasilimali zao. Matawi ya wanaume na wanawake ya chama yamepewa uzito uleule wakati wote.

Zaidi ya hayo, chama kimeanzisha mipango ya soko na ushirika wa wakulima katika maeneo mengine ya Senegali ambako mazao yake mengi huuzwa na pembejeo zake nyingi hutoka kwa mpango huu wa kubadilishana. Pengine jambo la kufurahisha zaidi, chama cha Fandene kimeanzisha timu za kitaalamu ili kutoa msaada kwa vikundi vichanga katika maeneo maskini ya jirani yaliyo karibu na jiji la Thie? na pia mji mkuu wa nchi, Dakar, ambayo yanataka kuanzisha mipango yao peke yao ya akiba na mikopo—kwa hakika hiki ni kinyume cha utoaji misaada kutoka vijijini kwenda mijini!

# Kisomo cha Watu Wazima na Utawala wa Wenyeji katika Jumua za Vijijini

Makala hii imeandikwa kutokana na utafiti uliofanywa na wachunguzi wa kutoka Ghana, Kanada na Marekani kwa msaada na usimamizi wa kitaalamu wa Peter Easton, Profesa Mshiriki wa Masomo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida. Ufadhili wa kifedha ulitolewa na Klabu ya Saheli/OECD, CIILSS na Chama cha Maendeleo ya Elimu barani Afrika (ADEA).

**Tini za MA 7  
Aprili 1999**

Nwodua ni mji mdogo wenye wakazi 640 ulioko kilometa 20 kutoka jiji la Tamale, Kaskazini mwa Ghana na kilomita 3 kando ya uliyokuwa barabara mbaya itokayo barabara kuu ya Tamale-Kumbungu. Hadi kufikia miaka ya 1980, kwa kiasi kikubwa Nwodua ulibaki imetengwa na biashara ya jimbo na ilikuwa na huduma chache sana za jamii na wala haikuwa na shule. Njia inayoiunga Nwodua na barabara kuu sasa imetiwa changarawe na mji una maji ya bomba. Jumua hii pia sasa ina bustani ya miche ya miti; mashine mbili za kusagisha ambazo husagisha chakula cha kulikiza watoto, shule ya msingi, kituo cha mafunzo ya ufundi kwa watu wazima, ongezeko kubwa la mazao ya kilimo na mbinu mpya ya utawala wa jumua. Mafanikio haya yaliyotajwa mwishoni huenda ni ufunguo wa mafanikio mengine yote yaliyopatikana.

Mnamo mwaka 1979, mkulima mmoja ambaye hakujua kusoma wala kuandika kutoka Nwodua aliamua ya kwamba wakati ulikuwa umewadia wa kuleta mafunzo ya kujenga Ghana ya kisasa katika jumua yake. Alianza kwa kumshawishi mhitimu mmoja wa shule ya kati kutoka kijiji cha jirani aje aanze kufundisha kusoma na kuandika Nwodua. Mafunzo yalitolewa kwa lughamama ya Nwodua, am-

bayo hayakuwaridhisha vijana wengi waliokuwa wameandikishwa. Walitaka Kiingereza na hivyo wakaacha mafunzo. Lakini yule mkulima aliyekuwa na jukumu la kuendelea na programu hii pamoja na rafiki yake wa karibu walivumilia tu, wakiwa wamamlipa mwalimu kwa kumfanyia kazi mashambani mwake pale waliposhindwa kumlipa mshahara wowote.

## **Kuwezesha ujuzi wa kusoma na kuandika ufanye kazi**

Baada ya muda mfupi Mwalimu wa kwanza aliondoka ili akahudhurie mafunzo katika Chuo cha Mafunzo ya Ualimu kisha apate kazi nzuri zaidi. Wale wanafunzi wake wawili walimwajiri mwalimu mwingine badala yake na wakaweza, wakati huohuo kuwarudisha shuleni baadhi ya wale waliokuwa wameacha shule. Walitumia mafanikio haya madogo kama nyenzo ya kuishawishi dayosisi ya Kanisa Katoliki kuanzisha shule ya msingi kijijini Nwodua mwaka 1984. Miaka miwili baadaye, wote wawili walifaulu mtihani wa kitafia wa kujua kusoma na kuandika na kupata sifa zinazotakiwa kufungua vituo vyao wenyewe vya kufundisha kusoma na kuandika katika mazingira yao.

Mafanikio yao katika juhudi hii yalisababisha kuwapa majukumu na fursa zaidi. Wale watu wawili walichaguliwa kama wasimamizi wa ugani na mradi mpya wa Dagbani Functional Literacy Project ambao wakati huo ulikuwa unaanza, baada ya muda mfupi ukawa na madarasa sabini na sita yaliyoendeshwa katika jumuiia mbalimbali katika eneo lote. Kwa sababu ya dhima yake kama makao makuu ya mafunzo ya kusoma na kuandika ya eneo lile, Nwodua iliweza mnano mwaka 1989, kufungua shule kamilifu ya msingi kwa watu wazima ambamo zaidi ya wakazi wa jumuiia walifanikiwa katika miaka iliyofuata, kupata cheti cha kumaliza mafunzo ya shule ya msingi, baadhi yao wakaendelea na elimu ya sekondari. Wakati huohuo jitihada za kujua kusoma na kuandika ziliendelea kuwa egemeo zaidi na zaidi la mfululizo wa shughuli za maendeleo ya mahali pale.

Shughuli ya kwanza kati ya hizo ilikuwa kuanzishwa kwa Kamati ya Huduma ya Afya ya Msingi, ambayo ilipeleka timu ya wakazi kwenye mafunzo katika kituo cha Huduma za Afya za Taifa jijini Tamale na kisha ikafadhili kampeni za kuondoa utapiamlo na degedege za watoto. Juhudi hizi zililivuta shirika la UNICEF ambalo liliisaidia Kamati hiyo kuanzisha mradi wa kusagisha ili kutayarisha mchanganyiko wa chakula cha kulikiza watoto wachanga. Wakati huohuo kamati ilihakikisha kwamba mapato kutokana na kodi ya mashine ya kusagisha na malipo ya shughuli zake yanalipia mashine ya pili, na hivyo kuiweka jumuiia kwenye njia ya kuwa kiwanda endelevu cha utayarishaji wa vyakula.

### **Kurejesha mazingira**

Juhudi nyingine zilikuwa katika eneo la kilimo cha misitu juhudi ambazo pia, kama kawaida, zilitokana na masomo yaliyofundishwa darasani na mada zilizochunguzwa katika kujifunza kusoma na kuandika katika vituo vya Elimu ya Msingi kwa Watu Wazima. Washiriki watano walihudhuria semina moja iliyofadhiliwa na shirika la UNDP mjini Tamale kuhusu matatizo ya eneo kugeuka jangwa katika sehemu za kaskazini mwa Ghana na mambo ambayo jumuiia zingeweza kufanya kukabili tatizo hili kwa njia ya upandaji miti, Waliporudi Nwodua, walishawishi kundi muhimu sana la wakazi wenzao kuchukua jukumu la kuanzisha bustani ya miche ya miti. Ingawaje kazi yote ya msingi ilikamilishwa miaka ya 1991 na 1992, ilibainika baadaye kidogo kwamba juhudi hizo zingeshindwa kuendelea kutokana na ukosefu wa maji kama njia isingetafutwa kuleta maji zaidi kwa jumuiia hiyo.

Chama cha Wakulima Vijana wa Nwodua (Nwodua Young Farmer's Club) kiliuomba uongozi wa Programu ya Mafunzo Kujua Kusoma na Kuandika ya Dagbani kuliendea shirika la UNDP ukiwa na pendekezo la kutaka kuongeza mabomba ya maji kutoka Tamale kufikia Nwodua kwenyewe, umbali wa takribani kilometa 5. Shirika la UNDP lilikubali kusaidia jitihada hizo na wanakijiji walichimba mtaro wa kilometa 5 ili kuandaa njia za kupitishia mabomba. Uunganishwaji huo wa mabomba ulifanikiwa na Kamati ya Maji ya Nwodua huweza kulipa gharama za kila mwezi kwa Tume ya Maji Machafu kwa kutoza fedha kila kaya katika kijiji kinachotumia maji. Wakati huohuo, upatikanaji wa maji uliondoa vikwazo vikuu vya maendeleo ya bustani ya Nwodua na juhudi za upandaji wa miti. Bustani ilianza kugawa miche ya aina za miti ya biashara na kivuli bure kwa wakazi wa Nwodua na kuwauzia watu wa nje. Mathalani, katika mwaka 1995, zaidi ya miti 2000 ya miembe ya kupandikizwa na miche 4000 ya mikoroshu ilichukuliwa na vikundi na pia watu binafsi katika eneo lote la jirani, ikiwa ni pamoja na asasi kama Baraza la Wilaya ndogo ya Kumbungu. Kwa sasa bustani ina mfuko wa mtaji unaoendelea kukua kwa ajili ya uanzishaji wa miradi mipya.

Ongezeko hili la biashara kati ya Nwodua na eneo la nje ulilazimisha kuboreshwa kwa ile barabara itokayo Nwodua hadi barabara ya Tamale. Kamati ya barabara ilianzishwa mnamo mwaka 1991 na kufikia mwaka uliofuata maofisa wa Benki ya Dunia walikuwa wameonwa na kushawishiwa kusaidia utengenezaji wa barabara inayopitika na motokaa kwenye kile kiungo cha kilometa 3, kwa masharti kwamba kijiji kingetoa nguvukazi na makazi ya wafanyakazi wataalamu na mafundi ambao wangepelekwa kwa ajili ya kazi hiyo. Barabara ilikamilika kwa mafanikio katika mwaka uliofuata na kamati ya barabara ilikabidhiwa jukumu la kuitunza na kufikiria uboreshaji mpya wa njia za pembeni.

### **Kuanzia na watu wazima**

Urahisi wa kupeleka nje mazao kutoka Nwodua pia ulimaanisha urahisi wa kufikika. Hivyo, kwa mfululizo mbalimbali, jumuiia ilianza kuchukua dhima ya kuwa kitovu cha shughuli za upanukaji katika eneo zima la jirani. Nyongeza nyingine ya dhima hiyo ilikuwa ujenzi, katika mwaka 1999, wa kituo cha kuvutia cha ufundi stadi kilichofadhiliwa na msaada wa kigeni kutoka Denmark. Kutokana na kuwapo kwake kijiji kilijilundikia vyuo kadhaa vya elimu—vitabu vya watu wazima (kituo cha kufundisha kusoma na kuandika, shule ya msingi

kwa Watu Wazima na Kituo cha ufundi stadi) vikiwa vimeizingira shule ndogo ya serikali ya watoto wadogo.

Kamati za Maendeleo za Nwodua mara kwa mara huulizwa kwa nini, kwa kuzingatia hatua hiyo kubwa ya porogramu za elimu iliyoifikia, inaelekea kuwa imeweka umuhimu zaidi kwa watu wazima kuliko watoto. Jibu lao ni rahisi: Ndiyo njia bora zaidi ya zote ya kuingia katika jumua za vijijini zilizokuwa maskini kama yetu hapo mwanzo. Iwapo watu wazima zaidi wataanza kukutana na fursa mpya na kjifunza jinsi ya kunufaika nazo, wengi zaidi watakuwa na hamu ya kuwapeleka watoto wao katika shule za msingi.

### **Kutengeneza upya utawala kutoka kwenye kiini**

Ingawa juhudi hizi ni za ajabu na aina kwa aina, moyo wa uvumbuzi wa Nwodua uko katika kiini chake—yaani katika umbo jipya la utawala wa jumua unaodhihirishwa na viongozi wa kijiji na washiriki vijana katika juhudi mpya za kutoa msingi wa kuendesha na kupanua shughuli zao. Viongozi wa kwanza wa wimbi la kujifunza kusoma na kuandika walifanya makubaliano na mtemi wa jadi wa Nwodua na baraza lake kuunda Kamati ya Maendeleo kwa Jumla (GDC) yenye jukumu la jumla la kuhakikisha kuwa kuna utekelezaji wenye utaratibu wa miradi na kuhifadhi maslahi ya jumua. Kikundi hiki kwa kulipa wema huo kimeanzisha kamati za utekelezaji zinazoshughulikia kila moja ya sekta za maendeleo ya mahali husika na kuiletea Kamati ya Maendeleo ripoti. Kamati ya Maendeleo ya Jumla huongozwa na mkulima mwenye umri wa miaka sitini na mitano ambaye hajui kusoma na kuandika na ambaye anaheshimiwa sana katika jumua, lakini kwa wajumbe wanane wengine ni yeye tu aliye na zaidi ya miaka arobaini na mitano; na wajumbe wengine saba ni wahitimu wa ama mafunzo ya

kujua kusoma na kuandika au wa madarasa ya Shule ya Msingi kwa Watu Wazima.

Kamati ya Maendeleo ya Jumla hufanya kazi kwa kupitia kamati nane za sekta, mojamoya kwa watu wazima kujua kusoma na kuandika, usimamizi wa afya ya msingi, utayarishaji wa chakula, kilimo misitu, mafunzo ya ustadi, mafunzo ya kilimo na ujenzi/ukarabati wa barabara. Katika mchakato wa kuunda kiunzi cha mtandao huu mkubwa, mambo mawili yametokea. Kwanza uendelevu wa jitihada karibu umehakikishiwa kuwepo kwa ufuatiliaji na pia ufadhili huu. Pili, kwa kutumia ngazi za ziada, Kamati ya Maendeleo ya Jumla imekuwa serikali tendaji ya kijiji katika Nwodua—ingawa si kama ile ya heshima—na imefanikiwa katika kuunda mazingira ambayo yanawezesha juhudi za ujasiriamali na inaunga mkono utoaji huduma bora kwa watu.

Lakini mafanikio ya Kamati ya Maendeleo ya Jumla yanapaswa kufuatiliwa tangu nyuma kwenye mambo mawili mengine kwa upande mmoja, kuna ile hamu kubwa ya mabadiliko iliyoanzishwa na mfuatano wa mafunzo ya watu wazima na vipindi vya elimu isiyo rasmi vilivyofanyika ndani na jirani na kijiji—na kwa upande mwingine; kuna ile nguvu ya msukumo uliokuwa ume-wekwa na wale wakazi wawili waasisi waliokuwa hawajui kusoma au kuandika walioanzisha utaratibui huu takribani miaka ishirini iliyopita na wakakataa kushindwa na vikwazo. Jitihada binafsi pamoja na kuendelea kupatikana kwa mafunzo na fursa mpya na kuzitumia zilitoa kichocheo cha mafanikio ya maendeleo ya mahali husika ambayo miaka ishirini iliyopita yalionekana yasingewezekekana. Lakini pia kuna ubunifu wa mfumo mpya wa utawala wa mahali uliochochea kuunda kiunzi ambacho bila kuwepo leo hii kusingekuwa na hata moja kati ya haya ambalo lingekuwa na kutimizwa.

# Utunzaji wa Mazingira katika Pwani ya Magharibi ya Senegali

Makala hii imeandikwa kutokana na utafiti uliofanywa na watafiti wa Senegali kwa msaada na usimamizi wa kitaalamu wa Peter Easton Profesa Mshiriki wa Masomo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, kwa ushirikiano mzuri na jumuiya husika za Kiafrika. Utafiti huu ulifanyika chini ya ufadhili wa pamoja na Klabu ya Saheli/OECD, CILSS na Chama cha Maendeleo ya Elimu barani Afrika (ADEA).

**Tini za MA 8  
Mei 1999**

Hifadhi ya asili ya Kër Cupaam iko katika eneo la “Petite Côte” la nchi ya Senegali, kilomita 45 kusini mwa Dakar, pwani ya Bahari ya Atlantiki. Kipande hiki cha uliokuwa msitu wa taifa chenye eneo takribani hekta 100 kilitengwa kwa agizo la serikali katika miaka ya mwanzo ya 1980 ili kuhifadhi eneo la makazi ya wakati wa baridi la Kwale bluu na Kwale mawe ambazo ni aina mbili za ndege zilizo katika hatari ya kutoweka na pia kutoa hifadhi kwa njia wanazopita ndege wanaoambaa pwani ya Bahari ya Atlantiki. Yale magende yaliyo pembezoni mwa ufukwe wa bahari katika ukanda huu ni sehemu nzuri ya kutengeneza viota na ya kupatia chakula kwa aina nyingi za ndege.

Mimea kadhalika na wanyama wa eneo hili vilikuwa vimeathirika sana katika miaka iliyotangulia kutokana na athari za ukame, kuongezeka kwa eneo la malisho na uvunaji wa kuni. Hata hivyo, pwani karibu na Popenguine, bado ni sehemu inayopendelewa kwa utalii na watu wotokao Dakar na pia kituo maarufu cha hija kwa madhehebu ya Kikatoliki: Lakini shughuli hii haijawanufaisha sana wenyeji na ongezeko la idadi ya watu umengeza shinikizo zaidi kwenye hazina ya rasilimali inayozidi kupungua.

## Kuikabili changamoto

Ingawa katiba ya hifadhi asili katika miaka ya 1980 ilisaidia kuzuia uhari-bifu zaidi wa mazingira mimea ya eneo hili ilikuwa imeharibiwa mno tayari kiasi kwamba jitihada zaidi zilikuwa zinahitajika kurejesha ekolojia ya eneo hili na kuanzisha aina ya shughuli za utalii ambazo zingewanufaisha wenyeji wa pale. Kwa hali yoyote ile hilo ndilo lililokuwa hitimisho lililofikiwa na kikundi cha wanawake wa kijiji cha Popenguine, ambao mnamo mwaka 1988 waliamua kuanzisha Chama cha Wanawake wa Popenguine cha Kuhifadhi Mazingira (*Regroupement des Femmes de Popenguine pour la Protection de la Nature* au “RFPPN”). Mwanzo kikundi hiki kilikuwa na wanawake 119 na mwanume mmoja ambaye alitokea tu kuwepo siku ya mkutano wa kwanza. Walimchagua kama mungu mlezi wao *Mama Cumba Cupaam* “mungu aongozaye wavuvi wa pwani.”

Kwa miaka minane iliyofuata chama cha RFPPN kilitumia rasilimali zake chenyewe na zile za nyongeza zilizotolewa na wafadhili waliovutiwa na shughuli hii mpya ya usimamizi wa maliasili ili kurejesha mimea ya eneo la hifadhi na lile la jirani. Hatua zilizochukuliwa na chama zilikuwa ni pamoja na kuweka vizuizi vya moto kwa kupanda miti kuzunguka eneo

zima, kupanda tena aina ya miti ya kienyeji iliyotolewa na bustani ya miti iliyoanzishwa na wanawake wakati huohuo, na kuendesha warsha ambamo vijana wa kujitolea kutoka maeneo ya vijiji na miji ya jirani waliletwa ili kujifunza uhifadhi wa asili na kufanya kazi za mikono zilizotakiwa.

### **Kwenda kwenye mzizi wa jambo**

Zaidi ya hayo wanachama wa RFPPN walijihusisha haraka sana na hatari iliyokuwa inayakabili mazingira ya kurejeshwa na kuhifadhi mazingira: ufyekaji wa misitu kwa ajili ya kukusanya kuni kulikokuwa kukifanywa na watu wa eneo lile lote. Wale wanawake waliamua kuchukua hatua za kuwa na vyanzo mbadala vya nishati na kufanya jamii zijitosheleze kwa nishati ya kupikia.

- Kwanza, walianzisha mtandao wa ushirika wa ugavi wa kuni, mkaa na gesi ili kudhibiti matumizi na kusaidia wanachama wao kukidhi mahitaji ya kaya zao.
- Pili, walianzisha bustani ya kijiji ya miti na msitu wa jumua ili kuanza kuendelea kupata chanzo cha maada ya kukoeka moto.
- Hatimaye, waliandaa ukusanyaji wa takataka za majumbani na kuziweka vyomboni ili kuondoa hatari za afya ya jamii zitokanazo na utupaji ovyo wa takataka na kuzitumia kutengeneza mboleavunde kwa ajili ya ile bustani.
- Kwa njia hii, wanawake hawa si kwamba walifaulu tu kupanga upya bio-anuwai ya mahali pale na kurejeshwa mimea ya asili ya pale, bali pia juhudi zao zilichangia waziwazi kwenye kujitokeza tena kwa aina za wanyama waliokuwa hawaonekani sehemu zile kwa miaka mingi: aina nyingi za ndege na nungunungu, nguchiro, mbega, mbweha, pakashume na hata paa.

### **Kujenga mtandao**

Bidii zao baadaye kidogo zilifikia kiwango ambacho urejeshaji wa mazingira ya eneo lile usingeweza kukamilika kwa uhakika bila ushiriki mpana zaidi kutoka vijiji vya jirani. Kusema kweli, programu na mfano wa bidii za RFPPN vilikuwa, vimeamsha hamu iliyokuwa inazidi kuongezeka miongoni mwa watu wa jumua za jirani. Kuliko tu kupanua chama cha RFPPN, wanachama wa chama cha Popenguine waliamua kuhimiza wanawake wa vijiji vya jirani kuanzisha vyama vyao wenyewe na kuanzisha bustani zao, kupanga kwa undani shughuli zao na kuweka mtandao wa ugawaji wa nishati za kupikia. Jumua nane hatimaye ziliungana na Popenguine chini ya uelekezi wa Kamati ya utaratibu iliyochaguliwa na wote, na idadi ya jumla ya wanachama iliongezeka kutoka ile ya 119 wa mwanzo hadi kufikia zaidi ya 1500. Makumi ya maelfu ya miche mipya sasa huoteshwa kila mwaka na mtandao wa vyama hivi.

Wakati huohuo, vikundi vya wanawake viliongeza shughuli mpya kwenye programu yao. Kumeanzishwa mielekeo saidizi ya aina tatu, na kwa hili tunashukuru kiasi kwa msaada mzuri kutoka Jumua ya Uchumi ya nchi za Ulaya (EEC).

*Mikopo na huduma za benki:* Ili kusaidia kuondoa umaskini mkubwa uliosababisha kuendeleza udhoofishaji wa mazingira wenye kujirudiarudia, vyama vilianzisha benki za nafaka, mikopo mdigomidogo kwa watu binafsi na shughuli za kilimo cha umwagiliaji wa mbogamboga katika kila kijiji. Hili la mwisho liliongeza hamu ya kuendeleza shughuli ya ukusanyaji wa takataka na utengenezaji wa mbolea.

*Miundombinu na mafunzo ya utalii:* Kutokana na ongezeko la hamu ya kujaribu kufanya programu kama ile ya Popenguine nchini Senegali na hata nje, wanawake hawa waliamua kuweka muundombinu mwepesi kwa ajili ya kuwapokea wageni na wajumbe, baadae walianzisha Kituo cha Mafunzo ya Usimamizi wa Ekolojia "Centre for Training in Ecological Management." Mpaka sasa wamekuwa wakipata makundi ya wageni kutoka nchi kadhaa za kigeni zilizovutiwa na mfano huu wenye mafanikio ya Eko-maendeleo (Ecodevelopment).

*Ajira ya Vijana:* Ili kusaidia kuondoa uhamiaji kwenda nje wa vijana wanaomaliza shule na kukomesha ukosekanaji wa fursa ya shughuli za uzalishaji kwa vijana katika eneo lote hili, vyama hutoa vivutio ili kuwaingiza vijana katika shughuli mbalimbali za kikazi na za kiuchumi zitokanazo na hifadhi hii mpya. Vijana wa kujitolea kutoka vijiji vya jirani na maeneo ya mjini ya jirani wameajiriwa ili kusaidia kurejeshwa hifadhi na pia kujifunza misingi bora ya usimamizi wa mazingira (ecomangement), ambapo mara nyingi huwa ajira mpya ya kudumu. Kiasi kikubwa cha uajiri hufanywa na vyama vya vijana wa Senegali vilivyoshirikishwa na Mfuko wa Nicolas Hulot, ambayo ni Asasi Isiyo ya Serikali kutoka Ufaransa, inayojishughulisha na hifadhi ya mazingira.

### **Mfano wa kuigwa**

Hifadhi hii na maeneo ya jirani yaliyohifadhiwa sasa yana zaidi ya eneo la maili 50 za mraba na yanatoa fursa za kiuchumi zaidi kwa jumua zote zilizolizunguka eneo hili: Uchangamano huu baina ya hifadhi ya kitaifa ya Kiafrika na binadamu walio katika maeneo ya ujirani, wakati huohuo pia ni nembo ya mtindo mpya wenye matumaini kuhusu hifadhi ya mazingira. Chama cha RFPPN kimeipa Senegali na vikundi vinavyojibidisha na shule kama hizo katika nchi mbalimbali za Afrika.

# Maendeleo ya Umoja wa Kilimo nchini Mali: Kuongezeka kwa Viwango vya Uwezeshwaji wa Wenyeji

Makala hii imetokana na taarifa zilizokusanywa na Peter Easton, Guy Belloncle Cheibane Coulibaly, Simon Fass, Laouali Malam Moussa na timu tano za utafiti wakati wa kuendesha utafiti wa elimu wa PADLOS, Uchunguzi kuhusu "Ugatuaji Madaraka na Ujenzi wa Uwezo katika Nchi za Afrika Magharibi" uliofadhiliwa na Klabu ya Saheli/OECD na CILSS. Ukitaka kupata nakala ya ripoti kamili ya utafiti huu, wasiliana na Peter Easton, wa Kituo cha Masomo ya Sera katika Elimu 312STB, Chuo cha Elimu katika Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, Tallahase, FL-32306 USA; Simu (850) 644-5042; Faksi (850) 644-15 95; baruapepe: easton@coe.fsu.edu

**Tini za MA 9  
Juni 1999**

Katika miaka ya mwanzoni ya 1990 wanachama wa vyama vya vijijini (Associations Villageoises au AV) katika eneo la Koutiala la kusini mwa Mali walikuwa na tatizo waliohitaji kulitatua dhidi ya kampuni ya Nguo ya Mali (Compagnie Malienne des Textiles, CMDT). Kulikuwa na uvumi uliokuwa unaenea kwamba CMDT ilikuwa imepanga kuongeza malipo ya wafanyakazi wake (yaani kuongeza hisa zao za faida kutokana na pamba), bila kupandisha bei wanaolipwa wazalishaji. Mnamo mwaka 1989 wawakilishi wa vyama mbalimbali vya eneo lile walikuwa wamekwishaungana kudai malipo kutokana na sera iliyokuwa inatumika na CMDT kuhusu majukumu ya kifedha ya vyama vya wazalishaji, kesi ambayo hatimaye wazalishaji waliishinda.

Kutokana na kutiwa nguvu na ushindi huo wazalishaji waliunganisha nguvu tena ili kukabili tatizo la bei na hivyo wakaunda Kamati ya Uratibu kwa ajili ya Vyama vya Vijijini na Tons ya Koutiala, iliyokuwa na wawakilishi wa vyama vya huko. Wajumbe wa Kamati ya Uratibu walikuwa ni pamoja na wakulima walio-kuwa wamepata mafunzo ya kujua kusoma na kuandika na wenye uzoe-fu katika maendeleo ya kutwaliwa masoko na wenyeji yaliyokuwako huko sehemu za kusini mwa Mali

tangu miaka ya 1970, pamoja na wawakilishi wachache wa tabaka jipya la watu waliokuwa wamejito-keza katika kipindi cha muongo ulio-pita: wahitimu wa elimu ya sekondari au elimu baada ya sekondari walio-kuwa wamerudi na kujiunga na jumuiya za nyumbani kwao ili kuanzisha mashamba yao wenyewe.

## **Kubadili hali ya kitaasisi katika maeneo ya vijijini**

Mfululizo wa mikutano na usikilizaji wa matatizo vilisababisha kikundi cha Kamati ile kuweka orodha rasmi ya madai na malalamiko yao. Wakati huohuo mikikimikiki ya kisiasa iliyo-kuwa ikiitikisa nchi ya Mali, ilicho-cha mageuzi ndani ya vyama vya vijijini, kupunguza kiwango cha faida ambayo tayari ilikwishakuwa ndogo kwenye mauzo ya mazao na hivyo kuilazimu kamati kuchukua hatua. Mnamo mwaka 1991, kikundi hiki kiliamua kukasimu mamlaka kwa msomi aliyekuwa na elimu kuwashinda wote, mhitimu wa chuo cha kilimo kitoacho mafuzo baada ya elimu ya sekondari, aliyekuwa amerudi shamba, ili azungumze na wanachama wa vyama vya vijijini, aondoe woga wao na kupeleka madai na maswali yao kwa CMDT. Juhudi hizi zilizolenga vyama vya vijijini



(AVs) zilikuwa zenye mafanikio makubwa: wawakilishi waliunga mkono kikamilifu jitihada za kamati ya uratibu. Lakini menejimenti ya CMDT ikiwa imetiwa hofu na hali ya wasiwasi ya kisiasa, ilikataa kufanya upatanisho wowote na umoja huu wa wakulima. Matokeo yake Kamati iliitisha mgomo wa wakulima wa pamba, na wanachama wake walihamasisha kanda ile yote kuunga mkono shabaha ya vyama vya vijijini. Kwa muda wa miezi miwili, vyama vilikataa kupeleka pamba yao CMDT, mpaka Waziri wa Maendeleo ya Vijijini yeye binafsi akaja Koutiala kusuluhisha mgogoro. Matokeo ya maelewano hayo yalikuwa ni kwamba CMDT ilikubali msingi wa kuwapo madai ya pamoja kwa asasi isiyo ya kiserikali inayowakilisha wazalishaji wa pamba na pia ikakubaliana na Kamati kushiriki kwenye Bodi ya Taifa ya Bei ya Mazao ya Kilimo.

Kwa njia hii SYCOV (*Syndicat des Producteurs du Cotton et du Vivrier*) au Chama cha Wazalishaji wa Pamba na Mazao ya Vyakula, kilizaliwa ingawa kisheria, kisingeweza kudumu kwa mwaka mwingine, kutokana na mahitaji mengine ya sifa kwa taratibu za kiutawala. Viongozi wake mara ile walianza kushughulikia kupanua masuala ya chama kipya cha kilimo kwa vyama vyote vya vijijini vya sehemu ya Kusini mwa nchi ya Mali, na hata wakaamua pia kufuta, kwa idhini yake, ugombeaji wa kiongozi mkuu wa mwaka 1999 wa hiki kwa ajili ya uongozi wa chama kipya ili kumwunga mkono mwakilishi kutoka mojawapo ya maeneo ambayo yalikuwa hayajawahi kuhusishwa. Chama hiki ambacho hutumia lugha mbili (Kibambara na Kifaransa), kimeendelea kukua mbali na kuwepo upinzani fulani wa CMDT na matatizo ya ndani kwa ndani yanayotokana na uundwaji wa Vyama vya Vijijini vyenyewe, baadhi ya uamuzi unaotatiza unao-fanywa na uongozi na misigano baina ya viwango vya mahali husika na vile vya Makao Makuu. Hivi sasa limekuwa jambo muhimu la mandhari nzima ya kitaasisi na kisiasa kuanzia ngazi ya taifa, kuwepo kisheria kwa haki za wakulima kushiriki katika uamuzi wote unaowahusu. SYCOV pia inaandaa kozi za mafunzo za Kifaransa cha kuzungumza na cha kuandika kwa ajili ya Wabambara wawakilishi wa vyama vya vijijini wanaojua kusoma na kuandika na SYCOV imeelekeza matumizi ya lugha zote mbili katika nyaraka zote inazotumia na katika shughuli zote inazoshiriki.

#### **Mizizi ya mabadiliko: uhamishaji wa nguvu ya kiuchumi mikononi mwa wenyeji**

Kwa hakika, pamoja na ubora na udhaifu wake, jaribio la SYCOV tayari linawakilisha hatua ya pili ya kutoa uwezo kwa wenyeji vijijini katika eneo la Kusini mwa nchi ya

Mali na pia hudhahirisha baadhi ya faida zinazoweza kupatikana kwa uhamishaji halisi wa mamlaka ya kiuchumi na kuwekwa mikononi mwa vyama vya wakulima. Wakati pamba imekuwa ikilimwa katika maeneo haya kwa zaidi ya miaka thelathini, kumetokea hali, katika kipindi cha miaka kumi na mitano, ambapo wafanyakazi wa mashirika makubwa kama CMDT na washirika wake walidhibiti ununuzi wa mazao katika eneo yanakolimwa, na usafirishaji wake mpaka kwenye vituo vya usindikaji wa mazao hadi kuingia katika mfumo ambamo shughuli hizi karibu zote zilifanywa na vyama vya vijijini. Wawakilishi wa vyama hivi au mashirika yake kwa sasa ndiyo wenye wajibu kamili wa kupima mazao, kuwalipa wakulima, kuhifadhi mazao hayo, kuyasafirisha hadi vituo vya kuyasindikia, kuyauza tena kwa wasindikaji na kadhalika, na pia, kwa ajili ya majukumu muhimu ya utayarishaji na uhasibu pamoja na kuanzisha sera zinazohusika. Hatua hii ilifikiwa, kwa kiasi kikubwa, kutokana na kujua kusoma na kuandika na pia programu ambazo hazikuwa za mfumo rasmi wa elimu, ambazo zili-fadhiliwa na hizo kampuni zenyewe za pamba (au wakati mwingine na kampuni zilizorithiwa na serikali zilizopita au kwa juhudi za AZISE), ambazo ziliwezesha makundi ya vijana balehe na watu wazima ambao walikuwa na kiwango kidogo sana cha elimu kuweza kusoma, kuandika na kupata stadi za kuhesabu katika lugha zao wenyewe na pia kupata ujuzi wa kuitumia ipasavyo na kuidhibiti lugha ya kikabila aumfumo wa lugha zote mbili.

Wala si kutia chumvi kusema kwamba juhudi hizo zimeokoa katika makampuni ya pamba mabilioni ya Faranga za CFA (kadirio ni kuwa Faranga 500 (CFA) = dola 1 ya Marekani). Sehemu kubwa ya kutosha ya makusanyo ya fedha imerudishwa katika Vyama vya Jumua na zikagawiwa na vyama hivyo kati ya watu binafsi kwa mikopo nafuu kwa wakulima na mifuko ya uwekezaji wa ushirika. Matokeo ya jambo hili la mwisho (yaani mifuko ya uwekezaji wa ushirika) yamechochea mfululizo wa uwekezaji wa aina nyingi nyingine, kama vile uanzishaji wa vyama vya akiba na mikopo, ununuzi wa zana za kisasa zaidi za kilimo; uchimbaji wa visima, ujenzi wa zahanati za jamii na shule, n.k. Hali hii ya uwezo wa vijiji kuendesha na kusimamia mambo si kwamba hauhusiani na ongezeko kubwa la uzalishaji wa pamba katika eneo la Afrika, Kusini mwa jangwa la Sahara katika muongo uliopita, bali pia ni maendeleo ambayo yameliweka eneo hili kufikia nafasi ya nne katika soko la dunia na kuweza kujaza bajeti za taifa ambazo zime-minywa vibaya kutokana na masharti ya Programu za Kurekebisha Mifumo ya Uchumi.

Zao la pamba haliwezi kufikiriwa sana kama nguvu kuu ya kutegemeza maendeleo endelevu, hasa ikizinga-

tiwa athari mbaya za zao hilo ambazo zimesababishwa nalo kwenye rutuba ya udongo, angalau katika mfumo mbaya wa kilimo cha ubadilishaji wa mazao na uhifadhi wa ardhi unaotumika katika Afrika Magharibi. Hata hivyo, uzoefu wa zao la pamba ulisaidia kuonyesha, kwa kiwango kikubwa, uwezo wa wazalishaji wadogo wa mahali husika kuandaa na kuendesha shughuli za kibiashara wao wenyewe-mradi tu mafunzo muhimu yakiweza kupatikana wakati huohuo. Na pia umesababisha kuanzishwa kwa kundi la asasi za vijijini zilizoimarika ambazo zinatoa “vigezo” vya maendeleo katika nyanja nyingine za maendeleo za huko.

### **Mazingira ya kufaa: Uoanishaji wa changamoto ya kiuchumi na mtaji jamii**

Kwa hakika vyama vya vijijini viliibuka kutokana na mambo mawili kukutanika, moja la “kijadi” na jingine la kisasa; na msukamano wa mikondo hii miwili ndio chanzo cha matokeo hayo mazuri. Jumuiya za kusini mwa Mali kwa kawaida ziko katika mfumo wa “ton” (neni la lugha za Kibambara na Kimalinke) au mifumo sawa na hiyo katika makabila ya jirani. Makundi haya ambayo hugawanywa kwa msingi wa umri wa marika ya jando au unyago, mara nyingi huwa yamesukana kwa imara sana na yamejidhibiti kindani kwa kiwango kikubwa sana. Hizi “ton” ndivyo vyama ambavyo vilikuja vikawa moja kwa moja au kwa namna nyingineyo kushika wajibu wa kuendesha shughuli za masoko na uwekezaji tena wakati CMDT ilipofanya majaribio yake kule vijijini, na hizo kazi zake mpya zikavihitaji vijiingize katika mwelekeo mpya, vikue katika mfumo mpya wa uwajibikaji na mafunzo ya hali ya juu kuliko mambo yalivyokuwa katika vile vikundi vya kijadi vya jando na unyago tu.

Kwa namna fulani, kushindwa, mafanikio na juhudi za uanzilishi wa SYCOV zinawakilisha “rusu ya pili” tu ya kampeni ya ukuzaji wa uwezo na uongezekaji wa uwezeshwaji wa vyama vya vijijini ambayo ilianza tangu kuanzishwa mfumo mpya wa soko la pamba miaka kadhaa iliyopita, na kuchochewa na uhamasishaji wa mifumo ya kijamii iliyopo. Na pia wakati huohuo vyama hivi vimesaidia kuchochea kuanzisha jitihada nyingine.

### **Kupeleka maendeleo katika rusu ya pili**

Mfano mwingine maridhawa: ili kuboresha uendeshaji wao, vyama vya vijijini vya kusini mwa Mali, kwa msaada wa CMDT na msaada wa nje, vilianzisha mnamo mwaka 1993 taasisi iliyohusika na ukaguzi wa hesabu zao na kutoa msaada wa kitaalamu kwa viongozi wa mamlaka ya fedha vijijini. Kitengo hiki kiliitwa “Kituo cha Uongozi cha Koutiala”; matawi kadhaa ya ziada yameanzishwa tangu wakati huo. Kituo hiki kina wafanyakazi walioajiriwa kutoka katika vyama vya vijijini, ambao wanawajibika kuweka wakaguzi wa aina ya tatu wa akaunti za Vyama vya Vijijini. Watumishi wenyeji wa mahali hupewa mafunzo na msaada wa kitaalamu kutoka nje, ambao kwa muundo wake umekusudiwa uwe mdogo. Usimamizi mzima wa sera wa Kituo unafanywa na Baraza la Utawala ambalo limeunganishwa kwenye Shirikisho la Vyama vya Vijiji vya kusini mwa Mali. Kinadharia, kituo hiki kinatazamiwa kuendesha kwa bajeti inayotokana na mapato ya mauzo ya huduma zake tu kwa vyama vya vijijini. Kwa hali hiyo uendeshaji huu ni nusu kati ya “kumilikiwa kikamilifu” na shirikisho na shirika binafsi la ukaguzi wa hesabu.

Kwa hakika tangu Kituo kilipoanzishwa, na mpaka sasa, kinaendelea kwa kiasi fulani kutegemea ufadhili wa nje. Lakini inaelekea kimekwishapita awamu ya kwanza ya kukamilisha uanzishwaji, kuanza kuendesha shughuli na urasimishwaji kwa hakika sasa kinatoa huduma zinazotakiwa na kuzalisha mapato. kwa hiyo, Kituo cha Uongozi kinaonyesha uwezo wa vyama vya mahali husika katika kukua kwa kiwango kizuri na kuingia katika taratibu za shughuli zitakiwazo ili kujitegemea kwa mambo ya fedha. Pia kinadhihirisha hatua muhimu isiyosahaulika na fursa kwa ajili ya vile vyama vilivyo katika rusu ya pili ambayo kwayo vinaweza kutoa msaada wa kitaalamu kwa shughuli mpya za kijamii ya raia. Mbegu zilizopadwa na uhamishaji wa kweli wa rasilimali na jukumu la kisoko na kupeleka kwenye vyombo vya vijiji sasa zimeanza kuzaa matunda ya aina mbalimbali.

# Njia Asilia za Uponyaji wa Watoto Walioathirika na Vita Barani Afrika

Makala hii iliandikwa na Edward C. Green, Ph.D, na Alcinda Honwana, Ph.D. Waandishi hawa wangependa kushukuru mashirika ya *The Chiristian Childrens Fund, Save the Children (USA), the Children and War Project na The Dispalaced Children and Orphans Fund, USAID*, kwa kutumia baadhi ya taarifa kutoka katika programu zao. Tungependa kumshukuru pia Mike Wessells kwa maoni na mapendekezo yake yenye manufaa. Kwa mawasiliano Edward C. Green anaweza kupatikana kwa baruapepe ifuatayo: [egreendc@aol.com](mailto:egreendc@aol.com) Alcinda Honwana anaweza kupatikana kwa baruapepe: [honwana@beattie.uct.ac.za](mailto:honwana@beattie.uct.ac.za)

***Tini za MA 10  
Julai 1999***

Watoto katika nchi zilizoathiriwa na vita katika Afrika na kwingineko mara nyingi ni waathirika wa machafuko wa moja kwa moja au wasio-kusudiwa, na/au pia ni mashahidi wa mambo ya aina mbalimbali ya kutisha yanayohusiana na vita. Watoto wadogo wenye umri wa miaka saba au minane huandikishwa kwa nguvu katika jeshi na hulishwa kasumba kama askari wadogo au wapagazi katika nchi kadhaa za Kiafrika. Wasi-chana kwa wavulana mara nyingi huteseka, baadhi yao hulazimishwa kufanya ngono au kutoa huduma ya aina nyingine katika umri mdogo. Katika mfumo wa migogoro ambamo utishaji wa raia umekuwa njia ya kawaida ya kupata malengo ya kisiasa au ya kijeshi, wanawake na watoto hulengwa kwa makusudi mazima kupata mateso au vifo. Hivi sasa ulimwenguni wapo watoto wasiopungua milioni moja waliotengwa na wazazi wao kwa sababu ya vita na yapo maelfu mengi kadhaa ya watoto walioumizwa kiakili au kisaikolojia kutokana na vitendo vya vita. Kwa mujibu wa kitambulisho kitolewacho na Saikatria ya Kimagharibi watoto waathirika wa aina hii mara nyingi huonyesha dalili za vurugu za mfadhaiko baada ya kupata kiwewe (PTSD). Dalili dhahili za PTSD na vitendo vya mfadhaiko unaohusishwa ni pamoja na: uepaji/purukusha-

ni, kama vile katika kukatiza ghafla hisia na uepaji wa mazingira ambayo huweza kukumbusha matukio ya kutia viwewe; paramo la usingizi, kushindwa kutuliza akili, “kuona maluweluwe” kama vile majinamizi na makumbusho ya ghalifa; uchovu wa akili, kuchanganyikiwa, hofu, tabia za shari, kujitenga na kijamii, na ukataji tamaa kuhusu maisha yajayo, na uchangamfu wa kupindukia kama idhihirishwavyo hata katika lengo la kutahadhari; kiasi cha kupindukia na pia kujibu kwa kutumia mwitiko mkubwa wa ghalifa wa matukio kuliko kiasi kilichotazamiwa.

Katika miaka ya karibuni, mashirika ya UNICEF, USAID na asasi binafsi nyinginezo, asasi ya hiari kama vile “Save the Children” na Christian Children’s Fund” yameanzisha aina mbalimbali za programu zijiitazo saikojamii ili kuwasaidia watoto walioathiriwa na vita. Hata hivyo, mbinu za tiba kwa ajili ya watoto walioathirika na vita bado zingali katika hatua za mwanzo tu zinazoendelea kukuza. Haijulikani ni kwa kiwango gani mbinu za tiba ya Kisaikolojia za Kimagharibi kuhusu PTSD—ambazo zilianzishwa kwanza ili kutibia Wamarekani wapiganaji wa vita ya Vietnam—zingeweza kufaa na kutibu kweli watoto wa Afrika na maeneo mengine ambayo haya-

jaendelea sana. Mojawapo ya mambo yanayoigusa PTSD ni ile dhana ya vurugu za mfadhaiko *baada* ya kuwewe-seka. Katika mazingira haya, ni tatizo kuzungumzia mfadhaiko kama jambo la baada (post) iwapo mtu anaelewa kuwa dhana ya vurugu ni pana kuliko tu kuwa katika matukio ya vita (mashambulizi ya kijeshi; mabomu ya ardhini, n.k) na kuzingatia pia kuwa maeneo mengine ya maisha kama vile umaskini, njaa, ukimbizi wa ndani na mengine kama hayo. Jambo lingine linaloigusa PTSD linahusu mbinu zake za tiba zinazojikita kwa mgonjwa mmoja binafsi. Mtazamo wa namna hiyo hudharau imani za wenyeji katika nafasi ambayo mizimu shupavu ya wahenga huweza kuwa na nguvu ya ajabu katika kusa-babisha na kuponyesha huzuni na mfadhaiko. Kadhalika mtazamo huo unadharau kuhusika kwa familia na jamii na mchango wao hai katika mchakato wa uponyaji huo.

Wakati katika proramamu za awali za watoto walioathiriwa na vita nchini Msumbiji na Angola viongozi wa jumua, waganga wa jadi na familia walionyesha hazina kubwa ya maarifa ya namna ya kutibu majeraha ya jamii ya vita katika watoto na watu wazima walioathiriwa na vita. Kusema kweli vurugu kama hizo zinaweza kutibika kabisa na waganga wa jadi, kutokana na kuelewa kijadi jinsi vita inavyoathiri akili na tabia za watu binafsi, na kwa imani za pamoja kuhusu jinsi nguvu za kiroho zinavyoingia katika taratibu hizo. Wakati wa utekelezaji wa programu hizi, watu walisema hawakuhitaji msaada wowote kushughulikia matatizo ya watoto, ya akili au tabia maalumu zilizojitokeza. Walichohitaji, kama walivyosema, ulikuwa ni msaada wa kuwapata watu waliokuwa wakikosekana katika familia na katika kuanzisha shule, shule za awali, kuanzisha fursa za ajira kwa vijana, na kuweka mazingira imara na mwafaka ya kijamii ya kuweza kufanyia kazi.

Upo ushahidi tosha kutoka kote Afrika ya kwamba matatizo ya kuchanganyikiwa na kurukwa akili ni miongoni mwa magonjwa ambayo, mara chache sana dawa za kisasa au msaada wa tiba za Kimagharibi hutafutwa ili kuyatibu. Kwa jumla Waafrika hukimbilia aina za tiba za asilia katika matibabu ya maradhi ya akili. Tafiti thabiti kuhusu uwiano wa ubora wa aina mbalimbali za tiba za Magharibi za maradhi ya akili kwa hakika zinaonyesha kwamba takriban tiba zote, kwa namna fulani, humsadia mgonjwa na kwamba zote zinao uwezo wa kutibu zinapokuwa zimehusishwa na mazingira mahususi ya jamii na utamaduni. Hii inaweza kuonyesha kwamba kama waganga wa akili, waganga asilia wa Kiafrika wanaweza angalau kuwa wenye manufaa kama walivyo madaktari bingwa wa kisasa, hasa wawapo kati ya watu wanaochangia nao utamaduni.

Utafiti miongoni mwa makabila mbalimbali uliofanywa nchini Msumbiji na Angola unaonyesha kuwa muwewe-seko wa akili unaohusiana na vita unahusishwa moja kwa moja na nguvu pamoja na hasira za mizimu ya watu waliokufa. Kule kushindikana kufanyiwa mazishi yastahiliyo katika nyakati za vita hakuruhusu mizimu hii kuhifadhiwa mahali pao katika dunia ya wahenga, kwa hiyo hudhaniwa kwamba mizimu huona uchungu na ina nguvu zenye uwezo wa kuwaduru wauaji wao na wapita njia. Uchafuzi wa jamii huweza kuzuka kutokana na jamii kugusana pamoja na kifo na umwagaji wa damu. Watu ambao wamekuwa vitani; walioua au waliokuwa karibu na kushudia mauaji husadikiwa kuwa wao pia huweza kuwa wachafuaji wamtengamao wa jamii. Hivyo matambiko ya kusafisha na kutakatishwa ni ya muhimu ili waweze kupokelewa tena katika jumua.

Mnamo mwaka 1994, wakati wa mradi wa kwanza nchini Angola uliokuwa mahususi kwa kuwasaidia watoto walioweseshwa na vita, iligundulika kwamba watoto walikuwa tayari wakisaidiwa kwa matibabu asilia ya kiakili yaliyokuwa yakitolewa na waganga wa jadi katika hali ya shughuli za mila za utakaso. Matibabu haya yalikuwa yakitolewa kadhalika kwa waliowahi kuwa wapiganaji na watoto ambao ama walikuwa wameshiriki au kushuhudia umwagaji wa damu. Ule mradi wa kwanza wa Watoto na Vita (Children and War Project) nchini Msumbiji ulikuwa umegundua kuwepo matibabu kama hayo kwa ajili ya watoto. Katika nchi zote mbili, tiba hizi zilielekea kufaa, angalau kwa kipindi kifupi. Uponyaji wa jadi kwa watoto walioathiriwa na vita nchini Angola na Msumbiji inaelekea unazingatia hasa matambiko ya kusafisha na kutakasa, huhudhuriwa na watu wa familia na wanajumua na watoto hupewa dawa ya kuharisha na hutakaswa “uchafu” wote wa vita na vifo, kadhalika na uchafu wa dhambi, hatia na mizimu ya kulipiza kisasi ya wale waliouliwa na askari watoto. Shughuli hizi hushehenezwa na mila za matambiko na ishara ambazo ufafanuzi wake hubainika vema katika kundi maalumu linalozungumza lugha ya kabila husika, lakini ambayo dhamira yake ya juma hujulikana kwa makabila yote.

*Siku ile alipofika, ndugu zake walimpeleka mpaka kwenye ndumba (nyumba ya mizimu). Humo alikabidhiwa kwa mizimu ya familia. Babu wa mvulana yule aliiambia mizimu akiarifu kwamba mjukuu wake alikuwa amerudi na akaishukuru mizimu kwa ulinzi wao kwa vile mjukuu wake aliweza kurudi mzima ... Baada ya siku chache roho mpatanishi alikaribiswa na familia ili kuwasaidia kuendesha shughuli za tambiko la kumsafisha yule mvulana. Mtambikaji alimpeleka yule mvulana kichakani, na huko kijumba kidogo*

*kilichoezekwa kwa nyasi kavu kilijengwa. Yule mvulana, akiwa amevaa nguo chafu alizokuwa amekuja nazo kutoka kambi ya RENAMO aliingia kibandani akavua nguo zote. Kisha kibanda kiliunguzwa moto, na nduguye mtu mzima mmoja, akamsadia kumwoko. Kile kibanda, nguo na kila kitu kinginecho alichokuwa ameleta yule mvulana kutoka kambini ilibidi kiunguzwe. Kuku alitolewa kafara kwa ajili ya mizimu ya watu waliokufa na damu ilinyunyiziwa kuzunguka mahali pale pa tambiko. Baada ya hapo yule mvulana alipaswa avute moshi wa dawa za mitishamba fulani, na kuoga kwa maji yaliyokuwa yametiwa dawa (Kutoka Tini za Ugani, Msumbiji).*

Tambiko hili la uponyaji hujumuisha kwa pamoja mfululizo wa maana na maashirio vinavyokusudiwa kumwezesha mvulana yule kukata uhusiano na mambo yote yaliyopita (yaani vita). Wakati desturi za tiba za kisasa za magonjwa ya akili husisitizwa katika utamkaji kwa sauti kuhusu mateso au huzuni, hapa katika tiba ya asilia, kwa kutumia maana za kiishara mambo yaliyopita hufungiwa na kusahauliwa. Hii inajidhihirisha katika uchomaji wa kibanda na nguo na usafishwaji wa mwili. Kuzungumzia na kukumbuka yaliyopita si lazima kuonekane kama utangulizi wa uponyaji au upunguaji wa maumivu. Kwa hakika mara nyingi huaminika kuwa kunafungua nafasi ili nguvu zenye uovu ziweze kujiingiza. Hii pia inajidhihirisha katika mfano ufuatao kutoka Uige (nchini Angola).

Mtoto au kijana anaporudi nyumbani, hufanywa asubiri viungani mwa kijiji. Bibi kikongwe kabisa katika kijiji kile humtupia unga wa mahindi yule mvulana na humzungushia kuku mwili mzima. Ataweza tu kuingia kijijini baada ya mila hii kufanyika. Baada ya mila hii, huruhusiwa kuisalimia familia yake pale kijijini. Mara salamu ikiisha, lazima amue kuku, ambaye hupikwa na kuliwa na familia yake. Kwa siku nane za kwanza baada ya kuwasili kwake, haruhusiwa kulala kitandani kwake, bali hulala kwenye mkeka tu sakafuni. Wakati huo, hupelekwa mtoni na humwagiwa maji kichwani kwake na hupewa mhogo kutafuna. Na aondokapo kutoka kwenye sehemu ya tambiko, hapaswi kutazama nyuma.

Mfano huu unasisitiza kule kutochangamana na familia na marafiki kabla ya tambiko la kutakaswa. Yule mtoto huwekwa nje ya kijiji mpaka tambiko lifanyke, na hawezi kusalimia watu au kulala kitandani kwake mpaka taratibu za tambiko ziishe. Kama ilivyosemwa awali, ingawa watoto wanaweza kuulizwa kuhusu mambo ya vita kama sehemu ya tiba, hili silo jambo la msingi kwa uponyaji: shughuli zinalenga kumsafisha kiishara yule mtoto aliyechafuka na kumfanya asahau kabisa mambo

ya vita “kusahau” (zingatia uashiraji wa kuzuiwa kutotazama nyuma, katika mfano wa Uige). Miiko ya vyakula na vizuizi vya mila nyingine pia hutumika. Mathalani katika vyakula, samaki na kuku lazima viepukwe na mtu aliye-takaswa kwa muda wa mwezi 1 hadi 2, na baada ya hapo mtu huyo lazima atambulishwe tena kwenye vyakula hivyo na mponyaji wa jadi aliyeendesha shughuli ile.

Mila ya *Okupiolissa* ya Huila nchini Angola hudhihirisha waziwazi ushiriki mkubwa sana wa jumua katika mila hizi, na husisitiza wazo la utakasaji kutokana na “takataka”.

Jumua na watu wa familia kwa kawaida husisimka na kufurahi mtu anaporudi nyumbani. Wanawake hujiandaa kwa ajili ya sherehe ya kusalimia naye (...). Sehemu ya unga unaotumika kupaka mapaji ya nyuso za wanawake hutupiwa mtoto na mwanamke, bibi anayeheshimiwa pale kijijini, humtupia miguuni yule mtoto kibuyu kilichojaa majivu. Wakati huohuo maji safi hurushwa juu yake kama njia ya utakaso (...) wanawake wa kijijini hucheza wakimzunguka yule mtoto huku wakiashiria kwa mikono na viganja vyao hufukuza pepo wasiotakiwa au athari zake (...) kila mmoja humgusa kwa mikono yote miwili tangu kichwani mpaka miguuni ili kumtakasa maovu yote. Ngoma hii huitwa: Ululando-w-w-w. Mila hii inapokwisha, yule mtoto hupelekwa kijijini kwake na kijiji husherehekea kurejea kwake. Tafrija maalumu huandaliwa nyumbani kwao ambako vinywaji vya Jadi tu (...). Mtoto huyo hana budi akabidhiwe rasmi na wazazi wake, kwa machifu wa pale kijijini, anywe na kuzungumza nao na kitendo hiki huashiria kubadilika kwa hadhi yake pale kijijini.

Mila hizi za kusafishwa na kutakaswa ambazo huhusu askari watoto zina sura ya dhana ambayo wanaanthropolojia huiita ibada za mpito. Yaani mtoto hupitia katika mabadiliko ya hadhi kiishara kutoka kuwa mtu ambaye alikuwa akiishi katika vitendo vilivyokiuka taratibu za heshima au vilivyoasi taratibu (yaani kuua, vita) na kuwa mtu ambaye sasa anapaswa kuishi katika mazingira ya taratibu za tabia ya utulivu na za jamii, na kuzifuata. Katika mfano ulitolewa wa Huila, mtoto aliyetakasika hupata hadhi mpya inayomwezesha kukaa kando ya machifu na kuzungumza nao. Mpaka pale kipindi hiki cha mpito kinapokuwa kimekamalishwa (kwa kufanya tambiko) mtoto yule bado hutazamwa kuwa yuko katika hali ya hatari, ya ukingoni “miongoni na baina ya” masuala yaliyobananishwa na hali ya utata. Kwa sababu hii, mtoto hawezi kurudi katika familia yake au kibanda chake, wala kulala kitandani kwake na pengine hata kuingia kijijini mwake, mpaka pale mila itakapokuwa imekamalishwa.

Dalili zenye kujitokeza zihusianazo na PTSD na vurugu nyinginezo za mifadhaiko husemekana zinaondoka mara baada ya shughuli hizi ambazo baadaye familia, waponyaji asili na machifu wa pale huelekeza ili kusaidia kurudisha uhusiano wa kudumu, wa kuaminika baina ya yule mtoto mwenye miweweseko na watu wa familia yake na watu wazima wenye mwenendo mwema kwa jumla. Vitendo hivi vya kuingiza mila vinakusudiwa pia kuanzisha upya upatanisho wa kiroho, hasa ule baina ya yule mtoto na mizimu ya wahenga. Kurejeshwa tena kwa uhusiano wa kawaida na shughuli na watoto wengine kunaweza kusiwe sehemu—au sehemu kuu—ya mila hizi za uponyaji asilia. Lakini waponyaji, wazee wa kijijini, walimu na waangalizi wengine wa watoto huelewa mara moja wazo hili linapolewa katika semina za mafunzo zilizofadhiliwa na mradi, katika nchi zote Angola na Msumbiji. Tiba ya michezo, kuchora, drama, ngoma na kusimulia hadithi ni kati ya mbinu zinazowasilishwa katika semina hizi.

Hapana shaka yoyote kwamba mila hizi ni muhimu sana katika kujenga mwambatano wa familia na mshikamano wake, na katika kushughulikia masuala ya maradhi ya akili jamii na upande wa matatizo ya hisia za watoto hawa. Lakini hata hivyo, ukweli ni kwamba, watoto hawa hurejea katika maeneo ya vijijini yaliyo maskani yanayopambana kupata hata mahitaji ya msingi ili kuweza kuishi na mengi ya mazingira haya yakiwa hayana shule, hospitali, hakuna mafunzo au fursa za ajira ambazo zingewawezesha kuona fursa za maisha bora zaidi kwa siku za usoni. Hivyo ingawa mila hizi ni muhimu lakini zinatakiwa zisaidiwe na programu za maendeleo ya jamii ili kuendeleza matokeo mazuri yali-yopatikana katika maeneo ya akili jamii na hisia ambayo hayawezi kutenganishwa na mazingira mengine halisi.

Kwa hiyo, mtazamo wa mashirika ya misaada, AZISE na asasi nyingine zinazohusika na utoaji misaada ya binadamu kwa ajili ya watoto walioathiriwa na vita zinapaswa pia kuzingatia uelewa wa mahali kuhusu miweweseko ya vita na mbinu asilia za namna ya kuishughulikia. Wafadhili wanapaswa kulenga kukuza mazingira imara, salama na yanayoeleweka kitamaduni ambamo watoto wanaweza kuwa na hisia za kupata ustadi na usalama katika dunia yenye mipango inayobashirika kwa kuhimiza moyo wa kujitegemea, kwa kupitia miradi ya maendeleo ya jamii inayoaminika na kwa kukaa na familia zao au familia zinazofaa, za walezi kama itabidi.

Mradi wa Mfuko wa Kikristo wa Watoto nchini Angola unajaribu kujenga tiba kwa kutumia msingi wa desturi zilizopo na uimara wake katika shughuli zake, na kwa kuoanisha haya na muingiliano ya kijamii akili kama ile iliyoelezwa. Tathmini ya mradi huu na ule wa mwanzo wa “Watoto na Vita” wa nchini Msumbiji zimeonyesha kwamba uhusiano huu usio rasmi kati ya waponyaji na tiba zao zenye mila, na programu za misaada ya wafadhili; inayosisitizia marekebisho ya mtoto katika familia na jamii inaweza kuonyesha mfano jinsi mikabala ya kiasilia na ya kisayansi ya Magharibi inavyoweza kutumika pamoja ili kufikia kiwango cha juu cha manufaa kwa watoto wenye mahitaji. Zaidi ya hayo mfumo kama huo wa ushirikiano na kugawana majukumu husaidia kuthamini uponyaji asilia na imani zake, ambazo huwatia watu wa pale nguvu na kuwahamasisha na ambao hatimaye, huhitaji sana kupata majibu endelevu na yanayokubaliana na utamaduni ili waweze kujisaidia.

# Elimu na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika Kurani huko Afrika Magharibi

*Makala hii imeandikwa kutokana na utafiti ulifanywa na watafiti wenyeji kwa msaada na usimamizi wa kitaalamu wa Peter Easton, Profesa Mshiriki, Masomo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, na kwa ushirikiano hai wa jumuiia husika za Kiafrika. Utafiti huu ulifanywa kwa ufadhili wa pamoja wa Klabu ya Saheli/OECD, CILSS na Chama cha Maendeleo ya Elimu barani Afrika (ADEA).*

## **Tini za MA 11 Agosti 1999**

Je, ni stadi gani za kitendaji na za ujuzi wa kusoma na kuandika ambazo wanafunzi huzipata katika viwango mbalimbali katika shule za Kurani za Afrika Magharibi? Je ni matumizi yapi mbalimbali ya kila siku ambayo hutumia maarifa hayo na ni mitandao ipi hutumika katika kuyaendeleza na kuyatumia? Elimu ya Kurani katika namna zake mbalimbali kwa muda mrefu imekuwa haina mfumo ulio bega kwa bega na mfumo wa elimu katika bara zima la Afrika, mfumo ambao ingawa umetumika kwa karne nyingi lakini bado haujulikani sana kwa wapangaji wa maendeleo na hivyo mara chache sana huzingatiwa na kuelezwa waziwazi katika sera na mikakati yao.

Uislamu una historia ndefu Afrika Magharibi na mifumo ya elimu ya Kiislamu, kwa hakika, imetumika huko kwa muda mrefu zaidi kuliko ile ya Kimagharibi. Imani ya Kiislamu kwanza ilienea kutoka Afrika Kaskazini na kuwasili huko katika karne ya 7. Kufikia karne ya 10, jumuiia za wafanyabiashara wa Kiislamu na wasomi zilikwisha kuanzishwa katika vituo kadhaa vya kibiashara vya Sahara Magharibi na ukanda wa Saheli. Hadi karne ya 11 na 12, watawala wa falme kama Takrur, Ghana ya Kale na Gao walikuwa wamesilimishwa na walikuwa wamewateua Waislamu waliokuwa waki-

jua kusoma Kiarabu kama washauri wao.

Biashara ya kuvuka jangwa la Sahara ilishamiri sana katika enzi kabla ya ukoloni na ilisaidia kukuza bidhaa kwa kiwango cha kutosha kutokana na kubadilishana bidhaa baina ya Bara la Afrika na Bara la Ulaya kati ya karne ya 11 na karne ya 16—ndiyo kusema, mpaka kuwasili kwa vyombo vya majini vya Ulaya katika pwani ya Afrika Magharibi na taasisi iliyosimamia biashara ya utumwa ya kuwavusha Bahari ya Atlantiki na ule mfumo wa Biashara ya Pembetatu baina ya Afrika, Ulaya na Dunia Mpya ambako mfumo huo ulineemesha sana uchumi wake. Uti wa mgongo wa biashara ya kuvuka jangwa la Sahara kimsingi ulihusisha mitandao ya miji iliyokuwa imeanzishwa maalumu katika njia za misafara na wafanyabiashara wazungukaji kutoka Afrika Kaskazini, ambao baadaye waliweka maskani au walirithiwa na makundi ya wenyeji katika shughuli hizo. Mapato ya biashara hii yaligharamia mahitaji yaliyotakiwa kujenga dola.

### **Utaratibu wa mfumo uliodidimizwa**

Mfumo wa elimu ya Kiislamu katika Afrika Magharibi nzima una safu nyingi ingawa muundo wake ni

legevu ukilinganishwa na ule wa Magharibi. Zaidi ya hayo, kwa sasa unahusisha njia yake ya jadi (yaani mpangilio wa Kurani kama ulivyo), shule rasmi au ya kisasa (shule za Kifaransa-Kiarabu ambazo wakati fulani huitwa *médersa*), na elimu ya kiwango cha kati chenye mchanganyiko wa elimuasilia na ya sasa ambazo mara nyingi huitwa mafunzo ya Kurani yaliyoboreshwa. Kwenye msingi wa mtandao wa jadi wa mafunzo ya Kiislamu kuna shule ziiwazo shule za maktabor ya Kurani, ambazo ndicho kiwango cha msingi ambapo watoto huanzia wakiwa na umri kati ya miaka 3 hivi na 10. Hujifunza Kurani na kujua wajibu wa msingi wa maisha ya Kiislamu. Kisha baada ya hapo huja “*madris*” au shule za sekondari ambako wale waliokariri vizuri na kuweza kuandika vipande vikubwa (angalau) vya Kurani, huendelea ili kujifunza kile kinachoitwa sayansi ya Kiislamu, (ilm), pamoja na desturi zilizoandikwa za dini hii na aina nyingi za mambo mengi ya mahubiri. Wanafunzi wachache huchaguliwa kuendelea baada ya kiwango hiki na huingia kiwango cha juu ama kuwa marabu (marabouts) au maimamu mashuhuri wa maeneo au katika vyuo vikuu vya Kiislamu vya Afrika Kaskazini na nchi nyingine za Kiislamu.

Angalau katika hali ya hatua za mwanzo—inavyowakilishwa na shule za Kurani za mahali husika—usomaji wa Kiislamu umeenea katika Afrika Magharibi nzima. Idadi kubwa ya shule za aina hii katika nchi ya Niger peke yake mnamo mwaka 1990 ilikuwa 40,000. Aina hii ya elimu kwa hakika hujenga mbadala wa elimu na (wa mawazo ya elimu rasmi na ya Kimagharibi) hazina kubwa ya maarifa iliyofichika, mgongano wa utamaduni ambao mara hupishana au kuchanganywa na ule rasmi, ingawaje katika nchi nyingi za Afrika taasisi msingi za mfumo ule—maktab—hazithaminiwi kabisa kama shule. Lakini hata hivyo, wanafunzi wa Kurani, walimu na waumini kwa jumla katika eneo zima wanafahamu sana historia ndefu ya imani hii katika Afrika Magharibi na wengi wa wasomi wake maarufu sana na walimu, baadhi yao wakiwa wenye madaraka makubwa ya kisiasa na kiuchumi, hasa katika kanda za eneo la Saheli. Wale ambao kwa miaka mingi walijihusisha katika biashara ya mazao ya kibiashara katika nchi za Niger, Mali na Senegali, kwa mfano, wameanzisha mitandao ya mitaji ya biashara kubwa yenye matawi katika maeneo ya mijini na viwandani na inayozidi kuongezeka huko ng’ambo. Mambo yote haya kwa kiwango cha kutosha yanaimarisha mvuto kwa aina mbalimbali za elimu ya Kurani kama malango ya kuingia katika mfumo mbadala na wakati mwingine wenye ustawi zaidi wa kiuchumi na kisiasa. Kwa kifupi, kuna mfumo imara wa kuhusisha mataifa unaoendelea.

### Thamani badilifu, mweneo mpana

Licha ya mielekeo hii katika mfanano unaolingana kwa msingi wa ndani wa utamaduni wa dini na mtazamo wa msingi namna na thamani ya mafundisho katika shule za Kurani na mfumo wa Kiislamu kwa jumla hutofautiana vya kutosha kutoka eneo moja hadi jingine. Katika maeneo ambako Uislamu unazingatiwa sana, idadi kubwa ya watoto husoma katika shule za Kurani. Kimsingi watoto hujifunza kwa kukariri maandiko matakatifu. Idadi ya wanafunzi wavulana huzidi ile ya wasichana, lakini mara nyingi katika uwiano usiozidi 3:2 au 2:1 katika hatua za mwanzo. Katika maeneo machache kama vile lile la Futa Jalon la Guinea viwango vya uandikishwaji karibu vinalingana kwa kila jinsia.

Undani wa mafundisho ya Kiislamu katika maeneo haya hutofautiana sana, lakini kwa jumla idadi kubwa ya wanafunzi wa kiume huvuka ngazi ya masomo ya mwanzo ya Kurani na huingia ngazi fulani ya mafunzo ya juu. Kwa kuwa kujua ama Kiarabu cha kisasa au cha kale zaidi, mbali ya kile cha maandiko ya Kurani yenyewe, ni nadra sana (isipokuwa miongoni mwa wale waliosomea katika nchi zinazozungumza Kiarabu), kiwango cha juu sana cha ujuzi wa kusoma na kuandika Kiarabu kwa vitendo—yaani, uwezo wa kukisoma na kukiandika katika mawasiliano, kuweka kumbukumbu na kuwasiliana kwa maandishi kwa jumla—huonekana mara nyingi katika maeneo kama nyanda za juu za Guinea, Sine Saloum la Senegali na maeneo yazungumzayo Kihausa nchini Niger, ambako kuna mtindo uliokomaa wa kuandika lugha za Kiafrika kwa hati ya Kiarabu (uitwao ajami kama ilivyo katika Kihausa na Kifulani). Nchini Guinea, asilimia 93 ya sampuli ya wahitimu 77 wa Kurani wanaume waliohojiwa, walidai wanajua kusoma na kuandika ajami. Nchini Senegali kati ya asilimia 25 na 75 ya watu wazima wanaume katika vijiji vilivyotembelewa na kati ya asimilia 10 na 25 ya wanawake walidai wanacho kiwango hicho cha ujuzi pia. Katika hali zote hizo, uwiano huo ulikuwa zaidi, kama siyo maradufu zaidi, ya kile kiwango cha kujua kusoma na kuandika Kifaransa katika maeneo hayohayo ya jumuiia za vijijini.

Kwa upande mwingine, ni asilimia 26 tu ya sampuli ya Guinea ya wanafunzi waliohitimu Kurani waliosema wanajua kuhesabu ukilinganisha na asilimia 93 ya waliojiona wanaweza kuandika ajami. Hata hivyo, wengi wa marabu wa Kiislamu na maimamu wanaelekea kuwa walipata stadi za kujua kuhesabu kwa njia moja au nyingine, ambazo zinasaidia kuelewa mlolongo wa namna wanavyotekeleza majukumu ya uhasibu katika masuala ya jumuiia.



Wakati mafundisho ya ufundi sio kipengele kilicho wazi katika mitalaa ya elimu ya Kurani, wanafunzi wengi wanaoendelea baada ya kile kiwango cha mwanzo kabisa, huishia katika kufanya kazi kama wanagenzi fulani ama kwa marabu wa Kiislamu au kwa fundi stadi au mfanyabiashara mshiriki, ikiwa tu atamsaidia kwa ajili ya kulipia matunzo basi kwa ada ya masomo yake. Elimu ya Kurani hupenda kuhusisha kipengele cha vitendo kilicho ndani ya jumuiia ingawa ni mara chache huweza kutambuliwa kama mafunzo hasa, ya ufundi; na wanafunzi wa Kurani hujawa na wazo kwamba itawabidi wajitafutie riziki au wapate ufadhili wa kufaa baada ya umri fulani. Hii imesababisha mtafiti mmoja MSenegali kusema, “L'école coranique forme des créateurs d'activités, alors que le système formel forme des demandeurs d'emploi.” (Shule za Kurani huandaa watengeneza ajira, wakati mfumo rasmi huandaa watafuta ajira).

### Matumizi ya mafunzo ya Kurani

Matumizi ya kawaida sana ya mafunzo ya Kurani kwa kiwango cha mtu binafsi ni kuandika na kuwasiliana, na lengo kuu la wanafunzi waliohitimu Kurani ni wao wenyewe kuwa marabu wa Kiislamu au maimamu kwa sababu kuna mahitaji ya kutosha ya walimu na watoaji huduma za dini na za uteguzi wa matego, hasa kwa kuzingatia kwamba eneo la Afrika Magharibi ya Kiislamu katika miaka ya karibuni limepanuka. Hata hivyo, zaidi ya robo ya washirikishwaji wa Guinea wa utafiti huu walisema kuendesha shughuli za hadhara ni matokeo ya mafunzo yao ya vitendo; na mtazamo huu ndio unaojidhihirisha katika eneo hili zima.

Hata hivyo, matumizi ya pamoja na ya kijumuiia sio ya nadra kutokea. Maadili ya Kiislamu, maarifa ya sheria na mamlaka yametumika kama uti wa mgongo wa utawala wa jadi kwa karne nyingi katika eneo lote la Sahel. Kusema kweli, sehemu kubwa ya msamiati wa lugha kuu za eneo la Saheli hauhusu dini pekee bali pia ni unaohusu sheria, utawala wa mahali, diplomasia na mafunzo ya elimu ya juu umetokana au metoholewa kutoka katika Kiarabu.

### Hitimisho: Njia mbadala za maarifa

Matokeo ya mambo haya ni kwamba mafunzo ya msingi ya Kiislamu—ya ile aina inayotolewa katika shule za Korani za mahali husika—zina pande kuu tatu za matumizi ya vitendo na matokeo yafuatayo kwa Afrika Magharibi hivi leo:

- Mafunzo yanao utangulizi wa teknolojia ya kuandika, na kwa kiasi kidogo, ujuzi wa kuhesabu, kwa idadi kiasi ya watu, wanaume kwa wanawake, ambao vinginevyo wangepata mafunzo kidogo sana au kuyakosa kabisa. Wale wanaoendelea kufikia kiwango cha kupata ufasaha katika kusoma, kuandika na kuhesabu kwa ajili ya matumizi ya mahitaji ya kila siku (kwa lugha fulani za kiafrika, kama maarifa ya kutumia lugha ya kiarabu chenyewe mara nyingi hukuwama zaidi) ni sehemu ndogo tu ya idadi ya watu wote, ingawa katika maeneo mengine huwa kubwa kiasi. Zaidi ya hayo, ujuzi wa hati ya Kiarabu umekujwa ni kigezo katika maeneo mengi ya vijijini ambayo hudhaniwa, kwa kiwango kikubwa, kwamba hayajui kusoma wala kuandika kwa kutumia vigezo vya Kimagharibi.
- Ni mafunzo vilevile kwa uongozi wa mahali, kwa kuwa mafunzo ya Kiislamu hasa, kuchukuliwa kwa kawaida kama ishara ya uadilifu, uaminifu na nidhamu na hiyo ni sifa kuu ya kukabidhiwa vyeo vyenye madaraka makubwa. Zaidi ya hayo, mafunzo haya wakati wote yamekuwa—na hasa kwa kuzingatia kuongezeka kwa chuki za karibuni dhidi ya mfumo rasmi wa masomo ya shuleni—ni njia ya kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kutokana na uhusiano wa karibu uliopo kati ya mtandao wa Uislamu na ile ya biashara ya jadi katika hili eneo zima. Wahitimu wa shule za Kiislamu wana uwezo zaidi wa kupata kazi au uanagenzi kwa wafanyabiashara wa jadi na pia katika shughuli za uendeshaji soko katika sekta isiyo rasmi.

# Rasilimali za Utamaduni na Afya ya Mama na Mtoto nchini Mali

Makala hii iliandikwa na Lydia Clemmons na Yaya Coulibaly

**Tini za MA 12  
Septemba 1999**

Katika utamaduni ambamo mimba imekuwa suala la mwiko na mara chache sana lilijadiliwa katika kiwango cha kaya, Mradi wa Matunzo ya Mtoto wa Afrika Aliyenusurika (Africare's Child Survival Project) katika Wilaya ya Dioro katika Mkoa wa Segou, kusini mwa nchi ya Mali (1989-1998) uliongeza kwa mafanikio makubwa mawasiliano na tabia ya ufuatiliaji wa afya wakati wa mimba. Lengo la jumla la mradi huo lilikuwa kupunguza viwango vya magonjwa na vifo miongoni mwa watoto na wanawake waliofikia umri wa kuzaa. Mkakati wa mradi ambao ulitumia *maarifa asilia na rasilimali ya utamaduni*, unatumika sana katika wilaya nzima ya Dioro, na ume-sambaa katika sehemu zingine za nchi, na pia umetambuliwa kima-taifa. Utambulisho wa pekee ulikuwa *pendelu* ambayo ni nguo ya ndani ya jadi inayovaliwa na wanawake nchini Mali ambayo ilipakwa rangi ya kijani iliashiria maana mpya ya kuonyesha ujauzito. Masuala mengine muhimu yalikuwa ni pamoja na: afya ya mama, ufuatiliaji lishe na ukuaji, udhibiti wa magonjwa ya kuhara, huduma za kinga, huduma za mpango wa uzazi na elimu kuhusu UKIMWI na magonjwa ya kuambukiza yatokanayo na ngono.

Mnano mwaka 1992, Africare, asasi binafsi ya kujitolea yenye makao

yake nchini Marekani ifanyayo kazi za maendeleo ya jamii, ilijenga wodi mpya ya wazazi Wilayani Dioro, katika eneo la Koila, umbali wa kilometa 17 kutoka Dioro. Jumuiya za Koila zilikuwa zimeonyesha haja ya kuwa na wodi ya wazazi kama huduma kuu na wataalamu wa afya na serikali waliiona kama sehemu muhimu sana ya akinamama kwa ajili ya kuji-fungulia. Kabla ya ujenzi wake, ni vituo vitatu tu vya afya vilivyotoa huduma katika wilaya nzima ya Dioro, yenye idadi ya watu karibu 90,000. Hata hivyo, viwango vya utumiaji wa wodi ya wazazi vilikuwa asilimia 20 hadi 30 tu ya kiwango kilichopaswa kufikiwa.

## Tusilijadili

Ili kusaidia kuelewa sababu za utumiaji mdogo wa wodi ya uzazi, watumishi wa Mradi wa Dioro waliandaa mradi uliozingatia kutafiti vitendo vya mwelekeo wa tabia ili kuchunguza maarifa, mitazamo na desturi kuhusu afya ya mama (Clemmons na Coulibaly, 1994). Utafiti huu ulilenga kubainisha masuala ya jumla kuhusu mimba na uzazi wa mtoto katika eneo la mradi na kutambua rasilimali na vikwazo vinavyohusu uboreshaji wa afya ya mama na upatikana-ji wa matunzo.

Majadiliano ya vikundi wakilishi na mahojiano ya kina yalidhihirisha baadhi ya matokeo kuwa:

- Wanawake na wanaume hawakuwa wanajua tu hatari zinazohusu mimba na uzazi wa mtoto, bali pia walihofu matokeo yake:
  - “Mara mwanamke apatapo mimba, huhofia afya yake wakati wote wa ujauzito na pia mazingira atakamoji-fungulia” (Mshiriki katika kikundi wakilishi cha kike).
  - Kila mara mke wangu awapo mjamzito, nimekuwa nikihofia nini kitatokea wakati wa kujifungua” (Mshiriki katika kikundi wakilishi cha kiume).
- Utamaduni wa mahali hapo ulithamini nafasi waliyo nayo wanaume kuwasaidia wake zao wawapo wawazito. Wanawake na wanaume kadhalika walisema kuwa mume wa mwanamke mjamzito anapaswa kuwa mshauri na mlinzi mkuu wa mkewe.
  - Ingawa wanaume hawakuwa na taarifa za msingi kuhusu utunzaji wa wanawake wawazito, walionyesha mvuto mkubwa kuhusu ukuaji wa mimba na walisema kuwa wanajiona wanawajibika katika kupata matokeo salama.
- Mojawapo kati ya vikwazo vikubwa sana vya kitamaduni kuhusu tabia za upatikanaji wa huduma ya afya ya wanawake, ambao kilikuwa ni ukosekanaji wa majadiliano kuhusu mimba katika kiwango cha kaya, hasa baina ya watu wa ndoa; waume kwa wake. Washiriki wanaume kwa wanawake walitaja aibu na tahayari kuwa ndizo sababu ya msingi za kukosekana mawasiliano kwa mazungumzo kuhusu suala hili:
  - Kimsingi mwanamke huona aibu, tangu mwanzo kabisa, pale watu wanaomzunguka wanapomgundua kuwa yu mjamzito.
  - Kwa kawaida mwanamke huona aibu, tangu mwanzo, kwa watu wanaomzunguka kujua kwamba ana mimba, hasa ikiwa ni mimba yake ya kwanza.
  - Wakati wa kipindi chote cha ujauzito, mwanamke atazungumzia mimba yake na mumewe kama jambo la mwisho tu na pale anapokuwa na tatizo ambalo yeye mwenyewe hawezi kulimaliza, liwe ni la kuhusu kitu halisi, la kifedha au linahusu afya.
  - Mwanamke angeweza kujadili [mimba] na matatizo mengine yahasuyo ngono na rafiki yake au mtu mwingine kuliko na mkewe.

Watu wa ndoa waume na wake hawakutahayari tu kujadili mimba baina yao, bali pia wanawake kwa wanawake, wakiwa na mama wakwe zao, wake wenza na marafiki. Kwa hiyo kukosekana kwa majadiliano katika kiwango cha kaya juu ya mimba kunaweza kuziba kupeana taarifa baina ya watu wa familia moja kuhusu

mimba zenye hatari kubwa na dalili za kuonyesha hatari hiyo. Pia kunaweza kukazuia kuchukua hatua za uamuzi muhimu wa kugawa rasilimali za familia na kuwa na tabia zenye manufaa kwa afya ya mama. Ingawaje wanawake wa eneo la Koila walitamani huduma za afya ya mama, mojawapo ya sababu ambazo ziliwafanya wasinufaike nayo ilikuwa kwamba hawakuweza kuanzisha mazungumzo na kuomba idhini na msada wa kifedha kutoka kwa waume zao, ambao hutazamwa kama vichwa vya kaya na waamuzi wa mwisho wa masuala ya kifamilia katika utamaduni wa Mali. Je kwa hali hiyo ingeweze-kanaje kwa mradi kuwasiliana na jumuiia hizi na kukuza uchaguzi wa tabia zenye manufaa kwa afya ya mama iwapo ujauzito wenyewe lilikuwa ni suala lililosababisha hisia za kukaa kimya, aibu na tahayari kati ya wanawake na wanaume?

#### **Tuanze kujadili ujauzito: kuchota kutoka rasilimali za utamaduni**

Waelimishaji wa afya kwa kawaida hujaribu kuwafanya watu wabadilishe tabia zao kwa kutumia ushawishi wa kutoa hoja zitokanazo na mantiki au masuala ya vitendo halisi. Kama ilivyodhihirishwa na mwitikio mdogo kwa mikakati mingi ya afya ya TEM (Taarifa, Elimu na Mawasiliano), mkabala huu haukuleta mafanikio ya maana. Njia za mawasiliano za jadi, zikiwa ni pamoja na hadihti, nyimbo, methali, mashairi ya kusifia na tenzi hutoa mabadala muhimu sana kwa ajili ya mikakati ya TEM. Rasilimali hizi za kitamaduni hutoa njia ya moja kwa moja ya kuifanua mada nyeti na masuala ya mtu binafsi kupitia amali za watu, mitazamo na motisha (Hale na Stoller, 1985; Mutasa, 1994) na zinaweza kukuza mabadiliko ya tabia, katika viwango vya mtu binafsi na jamii, kwa kuvuta hisia za watu, na kwa kuwaarifu na kuwaelimisha. Kwa sababu hizi, katika muktadha wa utamaduni-jamii ulioelezwa, watumishi wa mradi waliandaa kampeni ya afya ya mama iliyotumia njia tatu za kijadi za mawasiliano: (i) Kifaa cha kijadi cha nguo ya mwanamke; (ii) Mgrioti mmoja; na. (iii) Wimbo.

#### **Pendelu ya kijani**

Kipande kidogo cha nguo (*pendelu* kwa Kibambara) ni kitambaa kifupi cha nguo ya ndani kinachofanana na nusu mkaja ambacho huvaliwa na wanawake ndani ya nguo. Kulingana na kanuni za mila ya jamii, ni wanawake walioolewa tu ndio huvaa *pendelu*, kwa sababu licha ya kuwa nguo iliyobana kwenye mwili, hutumika kwa wanandoa kufutia majimaji yanayotokea baada ya tendo

la ndoa. Ingawaje hutazamwa kama nguo ya ashiki (kama vile ambavyo vazi jeusi la kulalia (negligee) lichukuliwavyo nchini Marekani) *pendelu* ambayo kijadi hutengezwa kwa pamba nyeupe ina umuhimu wa ndani zaidi wa kitamaduni. Hutazamwa kama ishara ya majukumu, wajibu na upendeleo wa ndoa na hufasiliwa kama *ishara bila maneno au fununu* ya kutolea ujumbe mahususi wa kijinsia wa mitazamo baina ya waume na wake. Mke anapojifunga *pendelu* kiunoni hisia zinazoandamana na uvaaji wa vazi hili la jadi hutanda tangu kuonyesha hali ya kujipambanua kuwa yeye ni mwanamke na mwenye mvuto wa pekee hadi kuonyesha hisia za kujiamini na kwamba *anadhibiti hali ambayo ameianzisha*. Mwanamke atavaa *pendelu* mbele ya mumewe katika chumba cha kulala, kwa uangalifu lakini kwa kuvutia, kwa sababu huivaa ili kunasa makini ya mume, kuamsha ashiki yake na ili kuamsha hamu inayovuka himaya ya ngono peke yake. Na mume amwonapo mkewe amevaa *pendelu*, hukumbushwa si dhima yake tu kama mwenza katika tendo la ndoa, bali pia kama mshauri, mlinzi na mtu anayepaswa kumkimu mkewe. Kule kuona mkewe amevaa *pendelu* humfanya mwanaume ajisikie rijali, mwenye nguvu, anayejali na kuwajibika. Wanawake wanasema ya kwamba ndipo hapo katika undani wa siri ya chumba cha kulala, huku *pendelu* ikiwa imefungwa kwa uchokozi kiunono au ikiwa kando, basi wake huweza kusema yote waliyo nayo na kutoa maombi yao maalumu, nao waume huwa katika hali nzuri ya kuwasikiliza. *Pendelu* ingawa ni ishara ndogo lakini yenye nguvu, hatimaye ni njia ya jadi yenye uwezo mkubwa wa kuwasiliana lakini pasipo maneno, ishara inayotumiwa na wanandoa. Huanzisha kupata undani wa vitendo vya nje na hisia na huashiria kwa wanawake na wanaume kadhalika wanadhima mahususi za kitamaduni na kijinsia na wajibu. Chiwome (1994) amefafanua kwingineko ya kwamba katika Afrika, *utumiaji wa hiari wa ishara na njia nyingine bila maneno ni njia mbadala zenye uwezo mkubwa badala ya maneno, hasa katika mazingira ambamo utumiaji wa maneno usingefaa*.

Watumishi wa mradi huu waliweka oda maalumu kwa mafundi cherehani kutengeneza *pendelu* mia tatu za kugawa wakati wa uzinduzi wa kampeni ya mwanzo ya afya ya mama. Badiliko muhimu la marekebisho ya *pendelu* lilikuwa ni jinsi ya kupangilia rangi kwenye vazi hili la usiri wa ndani na kukipaka kitambaa cha pamba nyeupe cha jadi kwa rangi ng'avu ya kijani, kuashiria ujuzito na kuashiria jukumu la kitamaduni la mume kama mlinzi, mshauri na msaidizi. Kama alivyosema Comaroff (1985) "rangi ya bluu na kijani," ni rangi za mvua, maji, upya na ukuaji... zinazohusishwa na nguvu ya kuanza jambo... (na) zinaashiria nguvu ya kizazi...

Rangi ya kijani hasa huonyesha asili au mahali penye ukuaji."

### Magrioti

Magrioti ni malenga ambao dhima yao ya jadi katika utamaduni wa Mali ni mchanganyiko wa msimulizi wa historia, mwimbaji wa nyimbo za kusifu na msuluhishi wa jamii. Bakary Koita ni *grioti* ambaye ameishi Dioro-ville maisha yake yote na anajulikana vema katika Wilaya ya Dioro. Ni mmoja kati ya wanafamilia ya *magrioti* maarufu nchini Mali na alipata ujuzi wake kutoka kwa baba yake. Akiwa na gitaa lake la jadi anaweza, kwa urahisi, kuimba nyimbo za kusifu, kutamba hadithi na kuimba nyimbo mpya anazotunga yeye mwenyewe.

Uamuzi wa kuhitaji huduma za Koita kwa ajili ya kampeni ya afya ya mama ulifikwa kutokana na kutambua umuhimu wa dhima ya *magrioti* katika jamii ya Mali. *Magrioti* wametambulikana kama wanasaikolojia wa jamii, wasuluhishi/wapatanishi, wanahistoria, wasanii, wanadiplomasia, wamiliki wa uwezo usio wa kawaida, wahifadhi wa utamaduni, waelimishaji na waburudishaji. Katika historia nzima, *Magrioti* wamekuwa daima wakionyesha uwezo wao kama vichochezi vya jamii kwa kutumia nguvu ya maneno ili kuteka na kufinyanga tabia za watu kwa kupitia hisia zao (Conrad na Frank; Hale na Stoller; Finnegan; Johnson; Okpewho; Peek; Sienaert na Cowper-Lewis).

Kwa kujua majina, historia za familia/koo, wasifu na hata maisha ya kawaida ya mtu binafsi katika jamii *grioti* anayo idhini ya kijamii inayomruhusu kusema moja kwa moja na yeyote kile ambacho mtu mwingine hawezi kuki-sema katika jamii, hata kwa umri wa mtu yule, jinsia, kabila au heshima yake. Magriati hutumia vipaji vyao binafsi na nguvu za maneno kupatanisha uhusiano baina ya watu wa familia moja, baina ya majirani na hata baina ya jamii. Nchini Mali ni *grioti* peke yake mwenye uwezo wa kuendesha majadiliano kuhusu mada nyeti za ujuzito na zinazohusu *pendelu* hadharani na kadhalika mafichoni bila kufikiriwa na jamii za vijijini kuwa ayasemayo ni mambo machafu au yasiyofaa kwa jamii.

### Wimbo

Kwa kipindi cha wiki mbili, Bwana Koita alishirikiana na watumishi wa mradi kutunga wimbo ambao uliwaelimisha watu kuhusu utunzaji wa afya ya mama na pia alikuza matumizi yaliyokusudiwa ya *pendelu* ya kijani, kutokana na muhtasari uliokuwa umetayarishwa na watumishi wa mradi, ambao ulikuwa na taarifa za msingi

sana za utunzaji wa afya ya mama. Muhtasari wa kitaalamu ulihitaji kutumia *pendelu ya kijani* kama ishara ya ujauzito na mawasiliano kati ya wanandoa na uliwataja waume, wake na mama wakwe za wake kama hadhira lengwa ya wimbo ule. Ili kuondoa ile aibu, hofu na tahayari inayoelezwa na wanaume kadhalika na wanawake katika vikundi wakilishi vya majadiliano, watumishi wa mradi pia walimwomba Bwana Koita kuhusisha kuonekana kwa *pendelu ya kijani* na hisia za furaha, majivuno, uwajibikaji na kujiamini. Malengo makuu ya wimbo ule yalikuwa ni (i) kuwajulisha wanaume na wanawake wenye ndoa na wakwe wa wanawake kuhusu mimba zenye hatari kubwa, dalili za kuashiria hatari wakati wa ujauzito na tabia za kusadia kupunguza hatari; (ii) kuongeza mawasiliano kuhusu ujauzito na matunzo ya afya ya mama katika kiwango cha kaya, hasa baina ya waume na wake; na (iii) Kuongeza matumizi ya huduma za matunzo ya afya ya mama pamoja na vifaa vilivyotolewa na wagawaji wenye ujuzi.

### Kampeni ya TEM ya Afya ya Mama

Shirika la Africare liliendesha kampeni ya TEM ya Afya ya mama ya mwanzo katika vijiji saba vya eneo la Koila la Wilaya ya Dioro ili kufanya majadiliano ya kubaini nguvu ya njia za mawasiliano za jadi. Jumla ya watu wazima 600 (wanaume 300 na wanawake 300) walishiriki katika kampeni hii. Ratiba ya kampeni iliweka nafasi ya mikutano ya wanaume na wanawake ambapo taarifa kuhusu afya ya mama zilitolewa na watumishi wa mradi, na kuwezesha na vyombo vya habari vya kisasa kama vile video, mabango na beji pamoja na rasilimali tatu za kitamaduni zilizokuwa zimebainishwa.

Wakati wa mikutano ya wanawake, watumishi wa mradi waligawa jumla ya *pendelu za kijani* mia tatu kwa wanawake wote walioolewa wenye umri wa kuzaa kutoka katika kila kimoja cha vijiji saba.

### Taathari

Watumishi wa mradi walifanya tathmini miezi mitatu baadaye kupima matokeo ya kutumia *pendelu ya kijani* na njia nyingine za mawasiliano zilizokuwa zimetumiwa wakati wa kampeni ya mawasiliano ya kubadili tabia, pamoja na wimbo ule uliokuwa umeandikwa na grioti; video na beji ya kukuza shughuli za mradi zinazotokana na jamii. Tathmini ya mwisho ya kampeni ya uchunguzi wa Usambaaji-Maarifa-Vitendo ulipima zaidi ile kampeni ya Taarifa-Elimu-Mawasiliano.

Tathmini ya taathari ilizingatia uchunguzi uliohusisha watu 320, wakiwa ni pamoja na watu 205 waliokuwa wameshiriki moja kwa moja katika shughuli mbalimbali za kampeni na watu 115 waliokuwa hawakushiriki. Sampuli ilihusisha wanawake 130 walioolewa wenye umri wa kuzaa (wakiitwa wake), wanaume 127 walioa (wakiitwa waume) na wanawake wazee 63 wenye watoto wa kiume walioa (wakiitwa mama wake). Wastani wa umri wa wale waliodododwa ulikuwa miaka 36.5

Kulingana na matokeo ya uchunguzi kampeni hii iliongeza sana kiwango cha mawasiliano kati ya waume na wake kuhusu afya ya mama. Kwa jumla, asilimia 65.5 ya washiriki wote wa kampeni walisema walijadili ujauzito na masuala ya afya ya mama baada ya kampeni. Kabla ya kampeni, ni karibu asilimia 3 tu ya watu ndio waliokuwa wamejadili masuala ya afya ya mama na wenzii wao wa ndoa.

Kati ya njia zote za mawasiliano zilizotumika wakati wa kampeni, *pendelu ya kijani* ndicho kifa ambacho washiriki walikifurahia kuliko vyote (asilimia 83.9). Jumla ya asilimia 94.4 ya wale waliodododwa walisema walikuwa wamesikia habari zake.

Ni ajabu kwamba asilimia 85 ya wale waliohojiwa ambao *hawakuwa wameshiriki* katika kampeni walikuwa wamesikia habari za *pendelu ya kijani*, hali inayoonyesha jinsi *pendelu* ilivyokuwa njia ya haraka na yenye mafanikio ya kusambaza dhana hii ya ubunifu. Ama kwa hakika, tathmini ya matokeo inaonyesha kwamba ingawa ni watu 600 tu (asilimia 10 ya idadi ya watu wenye umri wa miaka zaidi ya 15) walikuwa wameshiriki katika kampeni hii, karibu watu 5,000 (asilimia 89 ya idadi ya watu) walikuwa wameona au kusikia habari za *pendelu ya kijani* miezi mitatu baadaye.

Karibu wote waliohojiwa walijua kuwa *pendelu kijani* iliwakilisha ujauzito: asilimia 89.9 ya waume, asilimia 79 ya wake na asilimia 76.9 wakwe wanawake.

Kampeni ya TEM imesababisha kuonyesha mitazamo chanya na tabia zinazohusiana na ujauzito katika kiwango cha kaya ikiwa ni pamoja na waume kuwapunguzia wake zao mizigo ya kazi za kufanya kuboresha lishe na kuwahimiza kupata huduma za matibabu pamoja na huduma za afya ya mama.

Matokeo ya tathmini ya uchunguzi yanaonyesha kwamba utumiaji wa ubunifu kwa kutumia njia za mawasiliano bila kutumia maneno na pia kuwasiliana kwa kutumia maneno baina ya waume na wake, wake na wakwe zao tu, bali pia ulichochea mabadiliko ya kijamii. Ujauzito sasa si mada ya mwiko tena katika eneo la Koila, na kwa hakika, mjadala kuhusu ujauzito na utunzaji wa afya ya mama hivi sasa ni jambo la kawaida kwa viwango vyote vya kaya na pia vya jamii. Katika mwaka ule na

mwaka uliofuata kampeni hii ya mwamko, mradi ulivuka lengo lake la kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya vizazi vilisaidiwa na wakunga waliofundishwa au wataalamu wa utunzaji afya, ukilinganisha na kiwango cha asilimia 20 wakati mradi ulipoanza. Takribani asilimia 77 ya vizazi vilisaidiwa na zaidi ya nusu ya wanawake wawawazito walitafuta ushauri kabla ya kujifungua.

### Hitimisho

Ile *pendelu ya kijani* ilikuwa ni ukunifu mwafaka katika mfumo wa maarifa asilia kwa kuwa maana yake ya kitamaduni ni na matumizi yake vilikuwa tayari vinaeleweka vema katika eneo la utafiti. Kilichotakiwa kueleza tu ilikuwa ni maana ya rangi ya kijani (mimba) na kuihusisha na vitendo mahususi vyenye manufaa kwenye afya ya mama. Ingawa maana ya *pendelu ya kijani* ilikuwa mpya, mazingira (chumba cha kulala), hali (undani wa zile zinazoonekana na zile hisia), watumiaji (wake) na hadhira iliyokusudiwa (waume) viliendelea kuwa vilevile kama vile vya *pendelu ya jadi*. Wanawake katika eneo la Koila walizoea kwa urahisi kuivaa *pendelu ya kijani* wakati wa ujauzito kwa sababu walitumia “mbinu ya mwili” waliyoizoea.

Zaidi ya hayo, dhima ya *magrioti* ilikuwa muhimu sana: ... kwa kifupi ni kwa sababu malenga ... huwasilisha njia inayoturejesha karne nyingi nyuma ili malenga aweze kuchangia kwa namna ya pekee kwenye aina ya mabadiliko ya jamii yanayotakiwa kwa ajili ya kuwanusuru watu wengi wa Afrika hivi leo (Hale na Satoller, 1985).

Wa upande wa yombo vya habari na njia zitumikazo kutoa taarifa, kuelimisha na kuwasiliana kuhusu ujauzito na afya ya mama, uchunguzi wa tathmini ya matokeo ya kampeni ya DCSP ilionyesha kuwa zile njia za jadi zilikuwa ndizo zilizokumbukwa zaidi na jamii. Karibu wahojiwa wote walikumbuka *pendelu ya kijani*, *magrioti* na ule wimbo. Hivyo, ingawa *pendelu*, *magrioti* na *nyimbo* ni njia za jadi za mawasiliano nchini Mali, matumizi yake yanaweza kubadilishwa kwa manufaa ya kukidhi mahitaji ya kisasa. Mutasa (1994) anafikia mahitimisho kama hayo katika mjadala wake wa matumizi ya kisasa ya methali za kale katika Afrika ya Kusini.

*Mabadiliko ya wakati na hali yanahitaji masuluhisho ambayo maumbo ya jadi hayawezi tena kuzalisha. Hata hivyo, mara nyingi inatosha tu kuchukua kipengele cha kale na kukitumia katika muktadha au mwendo wa kisasa. Utaratibu huu wa ubunifu huwa ushahidi hai wa mwendelezo wa maumbo ya jadi.*

Miradi mingi ya maendeleo hutokea kupuuza au kupunguza gharama ya rasilimali za kitamaduni, na badala yake kukimbilia teknolojia mpya na rasilimali “za kisasa”. Kampeni ya Africare ya Afya ya mama (TEM), kule Dioro, nchini Mali inafafanua hazina ambayo maarifa asilia yanayo pamoja na rasilimali zingine za kitamaduni ili kuweza kuchangia kwenye masuala ya afya na ustawi wa mawasiliano miongoni mwa jumuiya za vijijini katika Afrika.

# Lugha za Kisaheli, Maarifa Asilia na Kujiongoza

*Makala hii imetokana na utafiti uliofanywa na watafiti wa ndani kwa kusaidiwa na usimamizi wa kiufundi wa Peter Easton, Profesa Mshiriki, Masomo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, kwa kushirikiana na jumuiya za Kiafrika zinazojali. Utafiti ulifanyika chini ya usimamizi wa pamoja wa Klabu ya Saheli/OECD, Kamati ya Ushirikiano wa Majimbo ya Kupambana na Ukame katika Saheli (CILSS) na Chama cha Maendeleo ya Elimu Afrika (ADEA)*

***Tini za MA 13  
Oktoba 1999***

Afrika ni bara lenye lugha nyingi, zaidi ya 2,000, kufuata hesabu za hivi karibuni ijapokuwa lugha nyingi zinakaribiana na kuelewana kwa kiasi fulani. Vilevile, Afrika ni bara la watu wenye ndimi nyingi, ambapo kiasi kikubwa cha wakazi wanaongea au wanaelewa zaidi ya lugha moja. Zaidi ya hayo, mtawanyo wa lugha haufanani. Mfano mzuri ni wa Afrika Magharibi. Sehemu kubwa za maeneo ya pwani zina lugha nyingi za kikabila, na nyingi kati yao hazikutawanyika sana. Kwa upande mwingine, kwenye mikoa ya bara, na hususan maeneo ya Sahel, kuna lugha chache sana, lakini zilizosambaa katika maeneo mapana sana.

Sababu za hali hiyo ni za sura ya nchi na za kisiasa. Misititu minene, mito mingi, na kuwepo muda wote kwa mbung'o hufanya mawasiliano na usafiri wa kutumia farasi kuwa mgumu katika maeneo ya pwani na hivyo kusababisha kuwepo kwa vikundi vingi vya kimbari na jumuiya ndogondogo za kikabila. Hata hivyo, katika maeneo ya ndani ya nyanda za savanna na mbuga za pembezoni mwa jangwa, usafiri ulikuwa rahisi kwa umbali mkubwa. Falme ziliibuika ili kudhibiti na kutoza kodi biashara iliyokuwa imeshamiri ya kupitia Sahara na wakati huohuo kuenea lugha za Kibantu kama vile Kibambara, Kiwolofu na Kimooré

katika eneo kubwa. Kwa hiyo, inasemekana kuwa mtu anaweza kufasiri kwa gari kuanzia Dakar hadi Ziwa Chad akitumia lugha tatu tu za Kiafrika—Kiwolofu, Kibambara na Kihansa, ambapo safari ya umbali sawa na huo kuelekea pwani hadi Nigeria, atahitaji zaidi ya lugha 300.

Katika Mkoa wa Gulmu wa Burkina Faso, ulioko kwenye maeneo yalioendelea kidogo upande wa mashariki kabisa unaopakana na Benin, kuna asasi moja isiyo ya serikali (AISE) ya kieneo iliyoanzishwa mwaka 1985, iitwayo Ti Tua. Asasi hiyo ambayo ilianzishwa na wanajumuiya ili kuhuisha kampeni ya kufuta ujinga inayoungwa mkono na serikali na inayoelekea kushidwa, imeunda mtandao wa vituo vya kufuta ujinga vinavyojishughulisha zaidi katika kutoa mafunzo kwa lugha ya Kigulmanchema, lugha ya watu wachache nchini Burkina Faso, inayozungumzwa na watu 500,000. Vituo hivyo vimeenea katika vijiji 31 vya mkoa, na vyote (ukiondoa makao makuu ya wilaya), vilikuwa havina shule za msingi wakati mpango huu ulipokuwa unaanzishwa. Mpango huu sasa unawahudumia wanakismo balehe na watu wazima wapatao 15,000 kwa mwaka, ambao asilimia 41 kati yao ni wanawake. Tin Tua imeanzisha pia gazeti la kila mwezi katika lugha ya Kigulmanchema

liitwalo “Labaali”, ambalo lina wateja 3,000 na huajiri waandishi wa habari waliopewa pikipiki na vinasa sauti katika vijiji vyote vilivyo kwenye mtandao.

Kuhusu ubora wa matokeo ya mipango hii ya kufuta ujinga, chama kilianza miaka mingi iliyopita kujenga shule za msingi za jumua ambapo mafunzo ya madarasa ya awali hutolewa kwa Kigulmanchema na Kifaransa kinaanzishwa polepole. Miaka miwili iliyopita, kikundi cha kwanza cha wanafunzi waliofunzwa katika shule hizi za jumua, walifikia mahali pa kufanya mitihani ya kumaliza elimu ya msingi ambayo lazima ifanywe kwa Kifaransa na ndio inayotumika kuchagua watakaoen-delea na elimu ya sekondari. Kwa wastani, wanafunzi ambao walianza masomo yao kwa kutumia lugha-mama, walifaulu vizuri zaidi ikilinganishwa na wanafunzi wa shule za msingi za kawaida. Mtunga mitaala wa Tin Tua anaelezea mafanikio yao kama ifuatavyo: “Ukifikiria mazingira ambamo mambo yote haya yanatokea, na ukweli kwamba kuna mwalimu mmoja kwa kila shule anayeongea Kifaransa, kinachoshangaza ni ile kasi ya kujifunza. Je, hii inatokana na lugha-mama kuwa daraja la kujifunza vizuri Kifaransa, au inatokana na kumotishika kwa wanafunzi, mbinu nzuri za kufundishia au bidii ya walimu?”

### Lugha za Kiafrika kama chombo cha uhasibu

Sasa uelekee magharibi kwa kilometa kadhaa mpaka sehemu za kusini za Mali, jimbo linalolima pamba na ambapo kiasi cha waendao shule bado ni juu kidogo ya asilimia 20. Katika miongo miwili iliyopita, msururu wa vyama vya vijiji vilivyokua karibu na Koutiala na Bougouni, vimekuwa hatua kwa hatua vikichukua madaraka kamili ya uuzaji wa mazao ya kilimo, usimamizi wa mikopo ya kilimo, na uwekezaji upya wa mapato yatoakanayo na shughuli hizo. Na wamefanya hivyo kwa kiasi kikubwa kwa kujifunza mifumo ya uhasibu na utawala iliyotayarishwa kwa kutumia lugha ya Kibambara. Hadithi hii ni sawa kaskazini kwenye delta ya Mto Niger, ambapo mpunga ni zao la biashara. Katika kijiji cha Niono Koloni, viongozi wa vijiji hutoa mitihani ya kuhakikisha kuwa wagombea wa nafasi zenye dhamana za kuchaguliwa kidemokrasia katika vyama vya ushirika vya wakulima, wana viwango vya msingi katika kuandika kwa Kibambara, ijapokuwa fomu za mahesabu zinazotumika ni za lugha mbili na hujumuisha Kifaransa. Wanafunzi wa shule za Korani na watoro wa shule za msingi ambao wanapenda kugombea nafasi hizo, kwa ujumla wanatakiwa kujiunga na vituo vya vijiji vya madarasa ya kisomo ili kuongeza umahiri wao katika kuandika kwa fonetiki za Kibambara.

Hii sio mifano katika. sehemu kubwa ya eneo la Saheli ya Afrika Magharibi, (eneo la nchi zinazopakana na pembe za kusini za Jangwa la Sahara) hutumia sana muundo wa kimaandishi wa lugha za Kiafrika kama chombo cha mawasiliano vijijini, kama sio nchi nzima na njia ya kuelezea utamaduni wa wenyeji.

Mabadiliko haya yanaonekana zaidi katika nchi za Kiafrika zinazozungumza Kifaransa, ambako lugha za Kiafrika hazikutambuliwa na zilizoonekana kama lahaja au zinazoweza kuvunja umoja wa kitaifa na mawasiliano ya kimataifa.

### Mabadiliko ya polepole lakini yenye uhakika

Kuna mambo mengi yaliyochangia kuleta mabadiliko haya, ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa serikali nyingi za kiuwakilishi na zenye uvumilivu mkubwa wa jumua za umma, kuenea kwa lugha za Kiafrika kutokana na uhamiaji wa ndani na maingiliano ya makabila. Na mabadiliko ya polepole kuelekea kutambua thamani ya maarifa asilia na utamaduni wa Kiafrika. Wakati huohuo, uzoefu na tafiti zimeendelea kuonyesha kuwa wanafunzi wanaoanza mafunzo ya shule kwa kutumia lugha-mama au lugha ambazo tayari wanazifahamu sana, wana nafasi kubwa ya kufaulu kimasomo, 3/4 ikiwa ni pamoja na kufaulu katika kuimudu lugha ya pili kama vile Kifaransa na Kiingereza 3/4 kuliko wale wanaolazimishwa kutumia lugha ya kigeni tu kutoka mwanzo. Watu wazima pia wanaonekana kujifunza lugha ya pili kwa urahisi zaidi kwa kutumia maarifa yao ya kujua kuandika kwa lugha zao.

Mabadiliko yamekuwa ya polepole sana hususan katika ngazi ya kati, ambapo mengi yamezungumzwa kuliko vitendo. Uanzishwaji wa lugha za Kiafrika katika elimu ya msingi, kwa mfano, kwa muda mrefu umebaki katika kiwango cha majaribio katika nchi kama vile Mali, Niger, Burkina Faso na Senegali. Kumekuwepo na ushirika mdogo kati ya mawakala wa elimu isiyo rasmi, ambao hutumia lugha za kitaifa na wa elimu rasmi ambao hawatumii lugha hizo.

Hata hivyo, katika kipindi cha miaka ya 1990, kasi imeanza kupanda katika ngazi ya vijiji. Kasi hiyo imechochewa kwa kiasi kikubwa na kule kuanzishwa kwa shughuli za uzalishaji mali vyama vya ushirika, biashara, asasi zisizo za serikali (AZISE) na serikali za mitaa ambazo zimeimarika zaidi wakati wa enzi ya shinikizo la kidemografia na soko huria. Ili kuziendesha shughuli hizi, wananchi wanahitaji kwa kiasi fulani kikundi cha watu wanaojua kusoma; kuhakikisha kiwango fulani cha uwajibikaji wa kidemokrasia na wanahitaji njia ya kuhakikisha kuwa kiasi kikubwa cha wanachama wana-



jua kusoma na kuhesabu. Lugha za Kiafrika ambazo nyingi kati yao siku hizi zinaandikwa kwa hati za Kirumi au za Kiarabu, zinatoa njia rahisi ya kufikia lengo hili kuliko utoaji wa mafunzo kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kireno.

### **Mafanikio ya kisomo nchini Burkina Faso**

Kuna mifano mingi sana Burkina Faso, nchi ambayo jina lake pekee ni muunganisho wa lugha mbili maarufu za Kiafrika. Burkina ni Kimooré na humaanisha “mtu mkweli”, na “Faso” ni Kijula na Kifulfulde, kwa maana ya “taifa” taifa la wasema kweli. Katika mji wa Bouloulou, mji mdogo ulioko kaskazini mwa nchi, sio mbali sana na Ouahigouya, wanawake wanajazana kwenye vituo vya kisomo vilivyofunguliwa kwa ajili yao kutokana na ombi kutoka kwenye chama chao cha maendeleo ya kiuchumi. Katika mji mkuu, Wagadugu (Ouagadougou), kikundi cha wanawake waliohitimu kisomo hivi karibuni, kimejiunga na kuunda chama chao kiitwacho “Song Taaba”, chama ambacho kimejizatiti kutengeneza na kuuza sabuni na siagi ya karanga. Baada ya jitihada za awali za kuwapa madaraka ya uongozi wanachama wachache wenye elimu ndogo ya msingi, wameamua kuunda mfumo wa mahesabu na uongozi katika lugha ya Kimooré na tangu wakati huo wameunda mtandao wa kitaifa wa wanawake wafanyabiashara.

Kusema kweli, nchini kote, idadi ya wanakisomo wanaohitimu masomo yao imeanza kuchuana na ile ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi, muundo wa elimu ambao bado una upungufu kutokana na uhaba wa walimu wanaojua Kifaransa na ufadhili. Mnamo mwaka 1996, kulikuwa na vituo vya kisomo 4,000 ukilinganisha na shule za msingi 3,000. Katika mwaka huohuo, wanakisomo 46,000 kati ya 72,000 waliofanya mtihani, walitangazwa kuwa wamefuta ujinga katika mojawapo ya lugha za kitaifa nchini. Kwa upande wa shule za msingi, ni wanafunzi 11,000 tu kati ya 86,000 wa darasa la sita waliochaguliwa kuingia kwenye shule za kati. Asilimia 52 kati ya wanakisomo waliofuta ujinga ni wanawake, ambapo kwa upande wa wanafunzi wa darasa la sita katika shule za msingi ni asilimia 40 tu, na wale wa shule za kati ni asilimia 8.5 tu. Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa Taasisi ya Kitaifa ya Kisomo, nane kati ya wanawake kumi waliohitimu kisomo hivi karibuni ni wanachama hai katika vyama vya ushirika na vyama vya wanawake.

### **Kueleza Maarifa Asilia**

Miaka 25 iliyopita, wakati vuguvugu la kwanza la kampeni za kitaifa za kufuta ujinga lilipokuwa linafifia,

katika nchi za Kisaheli, na minong’ono ya kwanza kuhusu kampeni za kisomo zinazoendeshwa na wananchi wenyewe ilipoanza kusikika, tathmini kubwa kuhusu athari za kisomo katika Mali ya Magharibi ilifanywa. Tafiti zilifanywa katika maeneo maalumu, na timu ya watathmini wa Mali walitumia siku kadhaa katika kijiji kiitwacho Sirakoro, kilicho kusini mwa Kita. Waligundua kuwa ijapokuwa msaada wa serikali haukutolewa kwa mfululizo, kulikuwa na matokeo mazuri.

Kikundi cha kwanza cha vijana waliohitimu kisomo kijijini, ambao baadaye walishika nafasi za uongozi za kusimamia manunuzi katika soko la wenyeji la karanga, wao wenyewe walikuwa wakufunzi wa kufundisha kundi la pili la wanakisomo. Muda mfupi baadaye, watu wazima wengi katika kijiji hicho wakawa wamejifunza kusoma na kuandika katika Kibambara/Kimalinke, na Serikali za vijiji zikaamua kutia mkazo mkubwa kwenye elimu ya watoto. Waliamua kuwa hakuna mtoto yeyote atakayefikia miaka ishirini pasipo kujua kusoma na kuandika katika lugha yake. Kwa kuwa hapakuwepo na shule ya msingi rasmi ya karibu, kijiji kilijenga shule yake na kuunda mtaala wake chenye. Pamoja na hayo, vijana waliofuzu kisomo wameamua kuandika historia ya kijiji chao na mkoa wao na kuifundisha historia hiyo kwa watoto wao.

Mfumo huu umekuwa ukiongezeka na kurudiwa kwa miaka kadhaa katika sehemu mbalimbali za Saheli. Lugha za Kiafrika zinapata mfumo wa kimaandishi na kutumika kama njia ya kusimamia vitegauchumi na kuweka kumbukumbu za maarifa asilia. Madarasa ya kisomo yaliokuwa yakipata mafanikio ya kupishanapishana kwa kuongozwa kutoka juu hususan kwa kupitia kampeni za kufuta ujinga, yalianza kupata kasi miaka ya 1980 japo yalichukuliwa na kuendeshwa na vyama vya wananchi na asasi zisizo za serikali. Madarasa hayo yamesaidia kwa njia kuelezea vema utamaduni wa wenyeji.

### **Umahiri wa lugha-tatu wenye manufaaa**

Tofauti mojawapo kati ya mvuvumko wa kwanza wa shughuli za kisomo na huu wa hivi karibuni ni umiliki wa wenyeji. Jambo la pili ni kwamba kisomo cha kufuta ujinga katika lugha za Kiafrika sasa hivi hakitolewi kama njia mbadala ya kufidia lugha za kimataifa kama vile Kiingereza na Kifaransa au kama mfumo wa “elimu vijijini” au “elimu ya Kibantu” kwa wale ambao hawakustahili kupata “elimu halisi,” bali kuwa yenyewe ni rasilimali ya kisiasa na ya kitamaduni na pia daraja la kujifunzia lugha ya pili.

Zaidi ya hayo, kukamilishana kupya kwa lugha mbalimbali kunaanza kujitokeza polepole, mojawapo

ikiwa dhana ya uwezo wa kumudu lugha tatu wenye manufaa. Mpango huu wenye ngazi tatu unalenga kumfanya kila mtu anayefuta ujinga kwa lugha yake mama, apate pia kujuwa lugha mojawapo ya Kiafrika inayozungumzwa na watu wengi (kama vile Kimooré, Kiwolofu, au Kibambara), na mwishowe ajifunze lugha ya mawasiliano ya kimataifa kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu. Mfumo huu unaonekana kwa wazungumzaji wa lugha moja wa nchi za Kaskazini kuwa kinyume cha kawaida lakini si vigumu kuelewa au kuona katika bara hili asilimia 50 ya wakazi wake tayari wanzungumza angalau lugha mbili.

### **Kuzipa sauti tamaduni za wachache**

Tuchukue tena mfano kutoka Burkina Faso. Nchi hii, iliyo mpakani kati ya nchi za Saheli na majimbo ya pwani, ina lugha zipatazo 71, ingawa asilimia 75 ya wakazi huzungumza mojawapo kati ya lugha kuu tatu zilizoenea sana (Kimooré, Kijula na Kifulani) kama lugha ya kwanza au lugha ya pili. Karibu lugha zote zinazozungumzwa Burkina Faso, isipokuwa chache sasa hivi zinatumika katika maandishi. Kwa hiyo, polepole, mzungumzaji wa lugha ya Kimanchema ana uwezekano mkubwa wa kujifunza Kimooré au Kifulani pamoja na Kifaransa wakati wa kupata elimu, ama katika shule za mkondo rasmi au kupitia madarasa ya kisomo.

Kwa sababu hizo, wimbi linalokuwa katika ngazi za wenyeji la matumizi ya lugha za Kisaheli limesaidia pia tamaduni za jumuiia ndogondogo za Afrika Magharibi kuimarisha utambulisho wao kama sehemu ya taifa na kuhifadhi mila na desturi za kale, wakati huohuo wakifungua milango ya mawasiliano kwa jumuiia kubwa zaidi. Chama cha Tin Tua ni mfano mzuri, kama ule wa uzoefu wa mkoa wa Todor ulioko Kaskazini-Magharibi mwa Senegali.

Tangu mwaka 1986, chama kinachojulikana kama ARED (Chama cha Utafiti wa Elimu) kimejitosa kwenye

uchapishaji wa machapisho ya kujisomea katika lugha ya Kipulaar kwa wanakisomo walioko kwenye maeneo ya Senegali yanayopakana na bahari kati ya miji ya Dakar na St. Louis. Kipulaar ni lugha ya Kifulani, Kipeulh au Kifulfulde cha mkoa maalumu, kinachoongewa kwenye nchi zote za Kisaheli, lakini bila kuwa lugha ya wengi popote pale, isipokuwa katika maeneo fulani ya Kaskazini mwa Kameruni na milima ya Futa Djalon nchini Guinea. Mpango wa ARED ni mojawapo ya mfululizo wa jitihada zikiwa ni pamoja zile zinazoratibiwa na APESS (Chama cha Peulh cha Elimu ya Sayansi) kilichopo Burkina Faso, ambacho kwa miaka ya hivi karibuni kimejikita kwenye kuendeleza matumizi ya lahaja mbalimbali za Kifulfulde za kijimbo.

Shughuli za ARED zimekuwa zikisaidiwa fika na vyama vya Wazungumzaji wa Kipulaar ambao wamehamia Saudi Arabia, Misri, Maghreb na Ulaya. Msaada huu umekiwezesha ARED kuchapisha mfululizo wa vitabu na magazeti katika Kipulaar na kutoa msisimko mpya kwa kisomo cha kufuta ujinga kwa watu wazima. Wakati huohuo, ARED imekuwa ikichapisha vijarida vinavyohusu maendeleo mbalimbali ya wenyeji, kilimo, na mada za utafiti katika Kipulaar. Kujua kusoma na kuandika katika Kipulaar kumekuwa ni kielelezo cha heshima kwa jumuiia ya kijijini katika eneo hili la Senegali. Kampeni za kufuta ujinga zilizoinduliwa kwa msingi huu, zimechangia sana katika uhuishaji wa kitamaduni katika eneo lote la mkoa.

Hizi ndizo jitihada hasa za wenyeji za kujenga elimu ambayo zinazoibuka kwa wingi zaidi na zaidi. Haijulikani ni umbo gani mfumo huu utachukua huko baadaye. Hata hivyo, inaelekea kwamba mfumo huu utadumu ukilinganishwa na kampeni za kitamaduni na za kufuta ujinga za miongo ya mwanzoni ya uhuru. Ukweli ni kwamba mfumo huu unamilikiwa na watendaji wenyeji na umeundwa kutokana na haja za kiuchumi na za kijamii.

# Uenezaji wa Tafiti kwa Watu wa Kawaida katika Afrika: Ukusanyaji na Uunganishaji

*Makala hii imetokana na utafiti uliofanywa na watafiti wa ndani kwa kusaidiwa na usimamizi wa kiufundi wa Peter Easton, Profesa Mshiriki, Masomo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, kwa kushirikiana na jumuiya za Kiafrika husika. Utafiti ulifanyika chini ya usimamizi wa pamoja wa Klabu ya Saheli/OECD, Kamati ya Ushirikiano wa Mataifa ya Kupambana na Ukame katika Saheli (CILSS) na Chama cha Maendeleo ya Elimu Afrika (ADEA)*

***Tini za MA 14  
Novemba 1999***

Ni mara ngapi tafiti ambazo kwanza ni chache zinazofanywa na watafiti wa Kiafrika zinaifikia hadhira ya Kiafrika ambayo iko tayari kutumia matokeo yake? Mawasiliano haya yanafanywa kwa njia gani na ni kwa mbinu gani yanaweza kuwa na matokeo mazuri zaidi?

Njia za usambazaji kwa umma wa matokeo ya tafiti za Kiafrika zinatayarishwa katika kiwango cha vijiji kwa msaada wa USAID, mradi wa ABEL (Kupata Elimu ya Msingi na Kufuta Ujinga).

Mradi unajumuisha usambazaji wa tafiti zilizofanywa na watafiti Waafrika walioandika juu ya mada ya “Madaraka Vijijini uwezeshaji wa umma”, lakini kufanya hivyo kwa utaratibu unaojumuisha wasambazaji na walengwa katika kukosoa tafiti hizo, kuweka kumbukumbu na kuchambua uzoefu wao.

## **Kufanya tafiti zinazofaa kusambazwa**

Utafiti wa kwanza kwa ajili ya majaribio ulifanywa kati ya mwaka 1996 na 1998, kwa msaada wa ABEL, ukifanywa na vikundi vya watafiti Waafrika katika nchi mbalimbali. Njia hii ilikuwa ya kibunifu kwa namna nyingi, hasa kwa kutumia njia kutoa tenda ndogondogo

katika tenda kubwa. Badala ya kutumia watafiti kama bunduki zilizoazimwa ili kufanya utafiti ulioelekezwa na asasi za kaskazini, asasi inayoshirikiana na ABEL (Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida) imetoa kondrati kwa timu za watafiti kwa gharama maalumu na timu hizo zipendekeze na kufanya utafiti juu ya mada mbalimbali. Mada zilibunywa kutokana na orodha ya malengo ya utafiti yaliyowekwa na Kikundi cha Utendaji cha Elimu isiyo Rasmi (WG/NFE) cha Chama cha Maendeleo ya Elimu Afrika (ADEA).

ADEA ni muungano wa Mawaziri wote wa Elimu wa Afrika na wawakilishi wa mashirika makuu ya ufadhili. Hufanya kazi kupitia Makundi ya Utendaji ya sekta ndogo mbalimbali za elimu zinazoongozwa na muungano wa waelimishaji wa Kiafrika wa elimu pamoja na wawakilishi wa wafadhili. Makundi haya ya Utendaji ya Elimu Isiyo Rasmi na Mafunzo yaliyobuniwa baada ya mkutano wa ADEA wa mwaka 1995 unaofanyika kila baada ya miaka miwili, na kufadhiliwa na Shirika la Uswisi la Ushirikiano wa Kimataifa na Mawaziri wa Elimu wa Ghana, Mali na Senegali yalikutana kwa mara ya kwanza mwaka 1996 mjini Dakar na kuidhinisha orodha ya mada za aula za utafiti.

Sera iliyopitishwa ilikuwa ni kuzialika timu za watafiti wa Kiafrika kuleta mapendekezo yao ya utafiti juu ya mojawapo ya mada zilizopendekezwa na kisha kuingia mkataba na wale walio na uwezo wa kufanya utafiti kwa kutumia utaratibu wa kandarasi. Utaratibu huu uliwataka watafiti kutoa kazi bora kwa viwango walivyokubaliana katika kipindi fulani maalumu na walipewa uhuru mkubwa; uhuru ambao kweli unahitajika kutokana na hali za kiutafiti zisizotabirika zilizoko Afrika. Hii ilisaidia katika kuamua njia bora ya kugawa fedha ili kupata malengo yaliyowekwa. Uwajibikaji mkali wa matumizi ya fedha ulitakiwa, lakini timu hazikulazimika kufuata sisizi mchanganuo wa bajeti wa awali.

Tafiti nyingi za kulisimua zilifanywa, nyingi kati yao zilihusisha zaidi ya lugha moja na ziliingiza vipengele vilivyofanywa na vikundi vingine, na hivyo kutoa fursa ya kulinganisha matokeo. Mada zilizotafitiwa ni pamoja na: (a) upatikanaji wa ujuzi katika sekta isiyo rasmi ya uchumi wa mjini; (b) matumizi ya manufaa ya elimu ya kusoma na kuandika; (c) ujenzi wa ufundi katika vyama vya ushirika vya wanawake; (d) mfumo mpya wa ushirikiano kati ya AZISE na serikali katika kutoa elimu isiyo rasmi na (e) majaribio katika elimu ya msingi isiyo rasmi.

### Kutoa habari

Suala sasa ni jinsi ya kusambaza utafiti huu kwa wale walioko vijijini na mitaani ambao watatumia matokeo yake. Kwa ufadhili wa ABEL mlolongo wa tafiti kuhusu upatikanaji wa ujuzi katika vyama vya ushirika vya wanawake na matatizo wanayopata katika kukabiliana na changamoto za uongozi zimefanywa huko Ghana vijijini na Mali kati ya mwaka 1996 na 1997. Matokeo yalikusanywa, kuandikwa na kuripotiwa katika makongamano na kutolewa kama nyaraka na kwa njia ya intaneti katika nchi zote mbili. Hata hivyo njia hizi za usambazaji hazikuwasaidia sana wanawake walioko kwenye mazingira hayohayo katika sehemu nyingine za Afrika Magharibi ambao wangaliweza kunufaika na uzoefu wa Ghana na Mali, licha ya kutoweza kuhudhuria makongamano ya kimataifa au kuingia kwenye mtandao wa intaneti.

Maofisa wa mradi waliamua kufikiria kuanzishwa kwa awamu ya usambazaji. Nia ilikuwa ni kuwashirikisha watafiti walio katika nchi nyingine za Kiafrika zenye raghba katika:

- Kusoma tafiti hizo;
- Kubainisha tafiti ambazo zinafaa zaidi kwa matatizo ya jamii katika kila nchi;
- Kupendekeza makundi lengwa ambayo yanaweza kunufaika na matokeo ya utafiti; na

- Kubuni mbinu za kuwafanya watu hawa kujua matokeo na kuwasaidia kulinganisha na kufanya mahitimisho kutokana na uzoefu wa Ghana na Mali.

Muundo wa kati wa kiasasi wa kutekeleza kazi hii ulikuwa ni ule wa Makundi ya Utendaji ya Elimu Isiyo Rasmi, muungano wa mashirika ya umma na binafsi (AZISE), zinazojishughulisha na elimu isiyo rasmi na zinazoshirikiana na Chama cha Maendeleo ya Elimu Afrika (ADEA).

### Matokeo nchini Benin

Katika nchi ya Benin, Kikundi cha Watendaji cha Elimu isiyo Rasmi kilipitia tafiti zote zilizofanywa na watafiti wa Kiafrika chini ya Awamu Kwanza ya Miradi ya ABEL na kuchagua tafiti tatu ambazo zinafaa kwa waelimishaji wa uwandani: (a) ujenzi wa ujuzi katika vyama vya ushirika vya wanawake; (b) matumizi ya manufaa ya elimu ya Korani ya kusoma na kuandika (utafiti ulioelezwa katika Tini za MA 11, Agosti, 1999) na (c) upatikanaji wa ujuzi katika sekta isiyo rasmi ya uchumi wa mjini. Kisha kikundi hicho kilialika makundi yake na timu nyingine za watafiti nchini Benin kupendekeza njia za kusambaza matokeo ya tafiti hizi uwandani. AZISE Benin "RAMPE" zilipendekeza kuzipeleka tafiti za vyama vya ushirika vya wanawake wa Ghana na Mali kwa maafisa na wanachama wa asasi kama hizo waliopo katika jimbo la Toviklin lililoko Kaskazini mwa Benin, ambako pamoja na mafanikio ya awali, walikuwa wanapata shida ya kuanzisha chama chao.

Watafiti waliwapelekea muhtasari wa chanzo na matokeo ya utafiti viongozi wa vyama mbalimbali vya ushirika na wakafanya ugunduzi wa kwanza. Kati ya zaidi ya vyama 100 vilivyoorodheshwa kama wanachama wa mtandao, ni vyama 21 tu ndivyo vilivyokuwa vinajishughulisha na vitegauchumi vya wanawake. Kati ya vyama hivyo 21, timu ya watafiti ilibaini vyama 10 ambavyo vimeonyesha nia ya kushirikiki, vilibuni njia ya kuwasilisha chanzo na matokeo ya utafiti uliofanywa Mali na Ghana kwa wanachama wa vyama vyote kumi vya ushirika. Kisha waliwakusanya viongozi wao kujadili uzoefu wa nchi hizi mbili kwa kuulinganisha na wa Toviklin na ni mahitimisho gani ya kiutendaji yanaweza kufikiwa kutokana na zoezi hili.

Zoezi hili lilichochea jitihada za dhati za vikundi vya Benin za kujitathmini na kufanya uchanganuzi wa hali halisi, baada ya kufurahishwa sana na mafanikio ya wenzao katika nchi mbili za jirani. Walisonga mbele kwa kubainisha vikwazo mbalimbali katika mazingira yao vili-

vyowazua kujitegemea. Kikwazo kikubwa kilikuwa upungufu katika mafunzo na hivyo kushindwa kusimamia mambo ya kifedha ya vitegauchumi vyao. Waliamua kutafuta mfungamano wa haraka, na kuanzisha kampeni za kufuta ujinga kama zinavyoendelea kaskazini mwa Benin, na kwamba kampeni hizo zidhaminiwe mahali pamoja, na vilevile kuwapatia mafunzo viongozi wao waliochaguliwa. Mambo mengine mengi kuhusiana na chama cha ushirika wa wanawake nchini Mali na Ghana, na majukumu yanayofanywa na wanaume katika vyama hivyo yalijadiliwa na kulinganishwa na hali ilivyo nchini Benin.

### **Unadishaji wa masuala ya kijamii kama panga lenye makali kuwili**

Mtazamo huu umetokezea kuwa njia ya unadishaji wa masuala ya kijamii na tafiti za kiutendaji na kama mbinu ya kusambaza ugunduzi. Uboreshaji wake uko katika ushirikishwaji wa makundi lengwa, umilikaji wa mada husika, ikiwa ni pamoja na athari zake na matokeo ya kujifunza. Lakini uzoefu katika awamu zote mbili za tafiti za ABEL, unaonyesha kuwa kuna athari katika ngazi mbili: Kwanza, ndani ya jumuiya inayohusika, na miongoni mwa watafiti wanaowajibika katika utekelezaji wa zoezi hili.

Utafiti huu ni tofauti na ule tuliozoea kufunzwa na kutekeleza. Ni utafiti unaohusu maarifa asilia, uboreshaji wake na matumizi yake. Wale wanaowajibika na kazi hii wanatakiwa kufanya bidii kufanya tafiti zilizopo zieleweke kiutendaji na kuwasaidia wateja wao kuona umuhimu wa matunda ya uzoefu wao kama utafiti ambao una faida katika kuulinganisha na tafiti zilizofanywa mahali pengine. Zaidi ya hayo kipengele kilichokuwa kigumu na cha kiugunduzi kilikuwa ni kiwango cha uwajibikaji, ikiwa ni pamoja na bajeti na uwajibikaji, kinachohusiana na wata-

fiti waliohusika. Kupeleka maofisa kukamilisha malengo magumu na yanayofungamana na hali ilivyo uwandani kama hii ya kusambaza matokeo ya utafiti ilikuwa kazi ngumu, kwani watafiti washiriki wachache walikuwa na uzoefu wa kusimamia kazi hii. Hata hivyo, kazi ilikuwa ya kuvutia na changamoto zake zilitoa mafunzo.

Mtindo wa usambazaji nchini Benin sio pekee uliobuniwa. Nchini Botswana, Kikundi cha Watendaji cha Kitaifa kilifanya zoezi kama hili. Wao walichagua pia seti ya tafiti zilizofanywa na watafiti wa Kiafrika ambazo zimegusa masuala ya wanachi. Hata hivyo wao waliwaleta viongozi vya AZISE kwa kila mada ili kupata uzoefu wa kitaifa na kuulinganisha na data na mahitimisho ya tafiti. Ijapokuwa mbinu hii imekaa mbali na uwanda, ilikuwa na uwezo wa kuweka mazingira mazuri ya kutolea maamuzi ya kisera na mifumo mipya ya ushirikiano miongoni mwa wahusika.

### **Baada ya hapa je?**

Jitihada nyingine zilikuja miezi ya Septemba/Oktoba 1999 nchini Gambia na Chad na zimezingatia tafiti zilizofanywa katika nchi tano nyingine za Afrika Magharibi zinazohusiana na mada za madaraka mikoani na ujenzi wa uwezo wa wenyeji. Yaani, ni kwa jinsi gani jamii ya kijijini, vitegauchumi na vyama vimepata umahiri wa kuanzisha mipango mipya ya kimaendeleo katika kipindi cha madaraka mikoani. Watafiti wa Gambia na Chad walioitwa kutoka kwenye vikundi vya watendaji vya elimu isiyo rasmi, na kutoka Wizara za Kilimo na Maendeleo Vijijini, walianza kwa kuweka orodha ya maeneo ambapo vikundi vya wenyeji vimeanza kubainisha wale ambao watashiriki katika kusambaza na kulinganisha. Matokeo yatapatikana mwishoni mwa mwaka.

Na Katy Moran

## Afya: Maarifa Asilia, Faida Linganifu

Makala hii imerekebishwa kidogo kutokana na makala inayoitwa “Moving ON: Less Description, More Prescription for Human Health (Kuendelea Mbele: Maelezo Madogo, Maagizo Zaidi Juu ya Afya ya Binadamu)” iliyoandikwa na Katy Moran, katika Jarida la Ecoforum, la Kituo cha Kimataifa cha Uhusiano wa Kimazingira, Kitabu cha 21, Na. 4, Januari 1998. Kwa taarifa zaidi juu ya somo hili, tafadhali wasiliana na Katy Moran, Mkurugenzi Mtendaji, Hifadhi ya Msitu wa Dawa, Mtaa wa 3521 S, NW-Washington, DC 20007. Moran HFC@aol.com

**Tini za MA 15  
Decemba 1999**

Tangu Mapatano kuhusu Bioanuwai (Convention on Biological Diversity—CBD) yalipoafikiwa huko Rio (Juni 1992), tumejifunza mengi kutokana na maelezo juu ya mahusiano mapya yaliyochochewa na CBD. Nchi zenye utajiri wa bioanuwai, tamaduni za kiasili na maarifa yao ya matumizi ya rasilimali za kibiojia kama dawa, na makampuni yanayojitahidi kugundua tiba mpya kwa kutumia mimea inayotoa dawa, na maarifa ya asili—vyote hivi sasa vina shauku na lengo moja. Thamani ya mimea kwa ajili ya dawa sasa inajulikana zaidi na “haki za uvumbuzi” za dawa hayo zimeshajadiliwa duniani kote. Kwa hakika, haki za uvumbuzi limekuwa ni jambo la kawaida kwa udhibiti wa miliki ya wenyeji ya maarifa ya kimapokeo kwa lengo la kuhakikisha kuwa faida za uvumbuzi zinarejeshwa kwa tamaduni na nchi zilizo vyanzo vya uvumbuzi husika (Mays, et al., 1997). Lakini, kadiri muda unavyopita, kiwango cha kutoweka kwa spishi na tamaduni kinaongezeka na afya ya binadamu imezidi kuzorota kutokana na magonjwa ambayo bado hadi sasa hayana tiba. Tunawezaje kutumia mafunzo ya CBD na tukaharakisha kutafuta mbinu za utekelezaji wake? Je, nchi zinaweza kutoa fursa za utafiti na uwekezaji kwa makampuni, ambayo, kwa upande wake,

yatauza bidhaa zao kwa bei nafuu? Je, kuna uchunguzi kifani wowote uliofanywa unaoonyesha uwezekano huu, na kuna maswali gani ambayo bado yanahitaji majibu.

### Mimea kama dawa

Mjadala wa haki za uvumbuzi unaonyesha umuhimu wa bioanuwai kwa afya ya binadamu. Tangu zama za kale hadi sasa, mimea imekuwa msingi wa famasia. Spishi kutoka nchi za tropiki zina utajiri mkubwa wa bioanuwai na biokemikali kutokana, kwa kiwango fulani, na hali ya hewa ya maeneo hayo. Katika maeneo yenye halijoto wastani, majira ya baridi kali huwaua wadudu waharibifu wa mimea, na mimea inayohimili halijoto wastani husitawi majira ya kuchipua kabla idadi ya wadudu waharibifu wa mimea haijaongezeka. Lakini kwa vile spishi za tropiki haziathiriwi sana na wadudu waharibifu wa mimea wa majira mbalimbali, nyingi zimejitengenezea kinga ya kikemikali dhidi ya wadudu wengi waharibifu wa mimea. Kemikali hizi za mimea ya tropiki zilizoongeza ustahimilivu wa mimea hiyo dhidi ya bakteria na vijidudu vingine viharibifu zinaweza pia kutoa kinga na zikatumiwa kutengenezea dawa kwa afya ya binadamu. Leo hii, robo ya

dawa yetu yanatokana na mimea. Katika nchi zinazoen-delea, asilimia themanini ya wananchi wake hutegemea mimea kwa matunzo ya afya yao ya msingi.

## Nchi

Nyingi ya nchi zenye utajiri wa bioanuwai hupatikana kwenye tropiki za Kusini, ilihali nchi zenye utajiri wa teknolojia, zenye rasilimali kwa ajili ya maendeleo endelevu ya bioanuwai, hupatikana zaidi Kaskazini kwenye halijoto wastani. Kabla CBD haijafungamanisha mataifa na bioanuwai zao, bioanuwai hizo zilichukuliwa kuwa ni “urithi wa binadamu wote”. Kila mtu aliruhusiwa kutumia rasilimali za kibiotiki, na zilikuwepo taratibu chache mno za kisheria za kurejesha faida zilizotokana na uvumbuzi wa dawa katika nchi zilizo chimbuko la uvumbuzi huo. CBD sasa inajitahidi kuleta urari wa jinsi wahusika wote wa harakati hizi wanavyoweza kufaidika na matumizi endelevu ya bioanuwai na viambato vyake. Nchi za Kaskazini zinaweza kutumia bioanuwai ya nchi za Kusini kwa kushirikiana teknolojia na faida inayotokana na matumizi ya kibiashara ya bioanuwai. Ni jukumu la kila nchi mwanachama wa CBD, hadi sasa ziko nchi 169, kutunga sera ya taifa ya bioanuwai ikielekeza namna ya utekelezaji wa suala hili nchini, ikiwa ni pamoja na kutunga sheria za utekelezaji huo. Baraza la Utafiti wa Kisayansi na Viwanda la India, linalopata ruzuku kutoka serikalini, kwa mfano, hivi karibuni limeanzisha programu ya kuzuia uigaji wa uvumbuzi wake ili kulinda mkusanyiko wa maarifa yake kuhusu dawa yatokanayo na mimea.

## Makampuni

Tangu CBD ianzishwe, hakuna dawa kutoka nchi za tropiki iliyotengenezwa kwa maarifa ya kimapokeo inayouzwa kibiashara. Faida za kiuchumi bado hazijapatikana. Utengenezaji wa dawa kwa kawaida huhitaji utafiti ghali na wa muda mrefu ili kupata ithibati ya serikali kabla dawa husika haijaanza kuuzwa. Nchini Marekani, dawa mpya huchukua, kwa kawaida, miaka 10 hadi 15 kuwa tayari kwa matumizi, baada ya uwekezaji wa zaidi ya \$ milioni 300 na kampuni na wawekezaji wanaokubali kuchukua dhima ya kuitengeneza, kuifanyia majaribio na kuiuza dawa hiyo mpya. Kwa kampuni mpya, miundombinu kama vile majengo, vifaa na mishahara ya wanasayansi watafiti lazima vigharamiwe kabla dawa yenyewe haijaanza kuzalisha mapato. Ili kupata fedha hizi nyingi zinazohitaji kugharamia utafiti na maendeleo ya dawa, makampuni hutegemea mtaji wa

kijasiri, faida za hisa, ubia na mashirikiano ya namna hiyo—uwekezaji na watu wa nje katika mradi wa kampuni wenye hatari nyingi, lakini pia wenye faida kubwa. Wawekezaji waweza kuwa watu binafsi ama mashirika na uwekezaji wao una hakimiliki ya ruhusa ya kutengeneza, kuuza, na kutumia dawa yatakatayovumbuliwa. Hakimiliki hutoa kinga ya uvumbuzi kwa kampuni, na hivyo kuwawezesha wawekezaji kurejesha fedha walizowekeza kwenye utafiti na maendeleo ya dawa, pale dawa hayo yanapouzwa kibiashara. Hayamkiniki kwamba kampuni yoyote ama mwekezaji yeyote atahatarisha mtaji wake kugundua au kuendeleza dawa fulani bila uwekezaji huo kulindwa kwa hakimiliki dhidi ya ushindani na makampuni mengine.

## Tamaduni

Asilimia sabini na nne ya dawa makuu 121 yatokanayo na mimea yana matumizi yanayofanana kwa tamaduni nyingi za asili. Badala ya kuchagua na kuichunguza mimea kiholela, mkakati ulio bora zaidi ni kwa baadhi ya makampuni kutumia maarifa ya asili ili kuitambua miti bora zaidi kwa dawa mapya. Lakini mikakati michache sana inayojishughulisha na jinsi maarifa ya asili yanavyoweza kufikiwa na faida linganifu zinavyoweza kugawanywa kwa kuzingatia utamaduni unaohifadhi mifumo ya kijamii iliyoujenga. Tofauti kati ya uchumi wa soko, uliokitwa kwa umiliki wa watu binafsi, na uchumi wa kijumuiya, ambao kwa kawaida huwezesha kumiliki pamoja rasilimali za kibiojia na kiutamaduni, humaanisha kwamba kikundi kizima cha kitamaduni lazima kifaidike. Ni vikundi vichache sana vya asili vimeshirikishwa katika mijadala ya kitaifa kuhusu masuala haya, au kuhusu ufafanuzi na utekelezaji wa CBD katika nchi zao.

## Uchunguzi kifani: Nigeria

Kiutendaji, uchunguzi kifani wa jinsi gani nchi mbalimbali, makampuni na tamaduni zinaweza kushirikiana na kutekeleza malengo ya CBD ni ule wa Kampuni ya Dawa ya Shaman (Shaman Pharmaceuticals, Inc.) ya Nigeria. Kwa mujibu wa daktari Tom Carlson, Mkurugenzi Mwandamizi wa Utafiti wa Uwandani wa Etinobiotiba wa kampuni ya Shaman, “Katika nchi hii ya Afrika Magharibi, yenye utajiri wa bioanuwai na tamaduni, mifumo ya dawa ya asili inasitawi sambamba na fursa za dawa za Magharibi. Mnamo mwaka 1995, serikali ya Nigeria iliwaunganisha rasmi waganga wa kienyeji katika huduma ya afya ya taifa kama watoaji wa matunzo ya afya na leo hii theluthi mbili ya watoaji wa matunzo ya

afya ni waganga wa kienyeji wa namna moja au nyingine” (Carlson et al., 1997).

Nchini Nigeria, Profesa Maurice Iwu ni mwanasayansi na Mkurugenzi wa Programu ya Maendeleo na Hifadhi ya Rasilimali za Kibiolojia (Bioresources Development and Conservation Programme—BDCP), ambalo ni shirika lisilo la kiserikali (NGO) la Nigeria. Iwu anafafanua, “BDCP ilianzishwa mwaka 1991 kama kitovu cha mashirikiano ya kitafiti yanayojenga stadi za kiufundi nchini Nigeria ili kwamba rasilimali za kibiolojia ziwe chombo imara cha maendeleo endelevu. Stadi zilizoborreshwa zinapelekea kwenye uchunguzi wa makini zaidi wa dawa ya magonjwa ya kitropiki yanayopatikana kwa wingi nchini Nigeria kama vile malaria, leishimaniasisi, na tripanosomiasisi” (Iwu, 1996).

### ***Kampuni ya Dawa ya Shaman***

Kampuni ya Dawa ya Shaman ilianzishwa mwaka 1990 na, kupitia BDCP, ikaanzisha ushirikiano wa kitafiti na asasi za kisayansi za Nigeria, jumuiya za vijijini, na waganga wa kienyeji na vyama vyao. Kampuni hii ndogo, ambayo makao yake makuu yako California, ilianza utafiti ukilenga katika uvumbuzi na uendelezaji wa dawa mapya yanayotokana na mimea yenye historia ya kutumiwa na wenyeji. Lisa Conte, Rais na mwasisi wa kampuni anaeleza juu ya suala hili, “Kama jina lake linavyoashiria, Shaman hutumia sayansi ya etnobotania, na pia kemia ya kutenga na ya mazao asilia, sayansi ya tiba ya maradhi na famakolojia ili kupata mbinu bora zaidi ya ugunduzi wa dawa. Wakati ikiundwa kama kampuni ya kuzalisha faida, Shaman ilianzisha pia Hifadhi ya Msitu wa Dawa (Healing Forest Conservancy), shirika lisilo la kutafuta faida lililoanzishwa mahususi kutafuta utaratibu wa kurejesha faida kwa nchi na tamaduni zinazoshirikiana na Shaman baada ya dawa kuuzwa kibiashara.” Ingawa kampuni hii changa bado haijauza dawa yake, matumizi ya etnobotania katika utafiti yamewezesha dawa zinazotafitiwa na kampuni kuanza kufanyiwa majaribio ya matumizi mapema sana (King, et al., 1996).

### ***Faida za Moja kwa Moja na za Muda wa Wastani Zilizosambazwa Nchini Nigeria***

Iwu na mwanasayansi mwingine wa Nigeria, Cosmos Obialor, walipendekeza majadiliano ya awali na waganga na viongozi wa kimapokeo kuzungumzia juu ya kushirikiana na kampuni ya Shaman muda mrefu kabla ya kuanzishwa kwa CBD huko Rio mwaka 1992. “Tulizitembelea jumuiya ambako tulikuwa tumefanya kazi kwa miaka kadhaa,” alisema Iwu, “ikiwa ni pamoja na vijiji alikozaliwa Obialor na nilikozaliwa mimi. Kimsingi, kila

jumuiya, au kijiji hujitawala chenyewe kikiwa na chifu na serikali yake. Utaratibu wao wa kufikia maamuzi ya kijumuiya hujumuisha chifu wa kijiji, washauri wake, waganga wa kienyeji na wazee,” aliongeza Iwu. Baada ya majadiliano ya muda mrefu, vikundi hivi viliafiki kwamba kampuni ya Shaman ilikuwa na malengo kama yao na yaliyozingatia utamaduni kuhusiana na afya ya binadamu. Kutokana na majadiliano haya na yale ya awali, sera mwafaka za ushirikiano na kampuni zilifikwa. Majadiliano yaliyopelekea kwenye makubaliano yalijumuisha maswala kama vile nia na malengo ya mradi; vipi na wapi mimea itachanganuliwa; fursa ya kibiashara ya mimea hiyo na namna ya kugawana faida.

“Tangu wakati huo, utafiti wa uwandani wa kietnobotania umeshafanyika mara nne,” alisema Steven King, Makamu wa Rais Mwandamizi wa Etnobotania na Hifadhi wa Kampuni ya Shaman. “Kwa uchaguzi wa washirika wa Kinigeria, faida zimechukua umbo la warsha na programu za mafunzo juu ya afya ya jamii, botania, hifadhi na etnobotania; msaada kwa hifadhi ya mimea ya dawa; vifaa kwa ajili ya shule za vijijini; ukusanyaji wa vifaa vya kibotania kwa ajili ya hebaria (mahali pa kuhifadhi mimea iliyokaushwa); vifaa vya maabara kwa ajili ya utafiti wa kisayansi wa mimea inayotibu magonjwa ya vimelea yaliyoenea sana Afrika Magharibi na kuwasaidia wanasayansi wa Kinigeria ili waweze kutumia mbinu mpya za uchanganuzi. Kutimiza sera ya kampuni, faida za moja kwa moja na za muda wa wastani, kama za hapo juu, zenye jumla ya thamani ya dola za Marekani 200,000 (elfu miambili) zimegawanywa kupitia katika programu mbalimbali kwa washika dau wanaoshiriki katika mpango huu”.

Iwu aliongeza, “Kampuni hupeleka ripoti za uchunguzi wa maabarani mara kwa mara kwa jumuiya zinazoshiriki kwenye mradi. Maandiko ya kawaida kuchapishwa kuhusu mimea ya dawa kutoka Nigeria yakionyesha utambuzi wa umma wa faida za maarifa ya kimapokeo ya Nigeria kwa jamii na afya ya binadamu”.

### ***Faida za Muda Mrefu***

Baada ya dawa kuuzwa kibiashara, kampuni ya Shaman itatoa asilimia fulani ya faida zake kwa Nigeria na makampuni mengine yaliyoshiriki mradini kupitia kwenye Hifadhi ya Msitu wa Dawa kwa kipindi chote kampuni itakapokuwa na faida. Hifadhi itagawa faida hizi, kwa usawa, kwa nchi na tamaduni zote zilizo washirika na kampuni ya Shaman, bila kujali nchi ama utamaduni ulio chanzo cha mmea wa dawa au maarifa ya kimapokeo yanayouzwa kibiashara. Katika mradi kama huu ambapo mapato yake ya kifedha hayatabiriki, kusambaza faida na hatari za hasara miongoni mwa



washirika wote wa Shaman kunaongeza fursa za fidia (Moran, 1997).

Kampuni ya Shaman na Hifadhi zinafuata kanuni ya CBD kwamba wahifadhi wenyeji wa bioanuwai wanapofaidika kutokana na matumizi endelevu ya mimea yao ya dawa na watu wengine wa nje, basi fursa za uhifadhi huongezeka. Ili kuzuia shinikizo la uchumi mwingine ambao unaweza kuwa na athari mbaya kwa bioanuwai, faida za kuilinda bioanuwai hiyo lazima zionekane mahali bioanuwai ilipo. Hata hivyo, kukosekana kwa modeli mwafaka kunafanya nadharia tete hii isithibitishwe. Ili kujaribu uwezekano wa kutumia mapatano ya dhamana kama chombo cha kugawana faida, Hifadhi imetoa \$ 40,000 (dola elfu arobaini) kwa mfuko wa dhamana nchini Nigeria kwa ajili ya mradi wa majaribio.

Mfuko wa Maendeleo Uganifu ya Vijijini na Dawa ya Kienyeji (Fund for Integrated Rural Development and Traditional Medicine—FIRD—TM), mfuko huru wa dhamana, ulianzishwa na BDCP kama chombo cha fedha kwa ajili ya maendeleo endelevu ya vijijini na kwa ajili ya kusambaza faida miongoni mwa washika dau wa Nigeria. Bodi ya mfuko huu inajumuisha vikundi vyote vya washika dau, yaani viongozi wa vyama vya waganga wa kienyeji, maofisa waandamizi wa serikali, wawakilishi wa mabaraza ya vijiji ya makabila mbalimbali na wataalam wa kiufundi kutoka kwenye asasi za kisayansi. Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi wa Mfuko, Mtukufu Eze E. Njemanze wa Owerri, ni mtawala wa kimapokeo anayeheshimika sana. Nafasi kubwa inayochukuliwa na mifumo ya mshikamano wa kimapokeo, kama vile vyama vya kikabila na vyama vya kitaalam vya waganga, hutoa muundo wa kijamii unaohakikisha ushiriki wa jumuiya. Vikundi mbalimbali vya kitamaduni vya Nigeria vitapatiwa fedha kupitia vyama vya waganga wa kienyeji na vijiji kulingana na desturi zao. Vyama vya mijini, wakuu wa vijiji na vyama vya kitaalam vya waganga vimepewa uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu miradi ya maeneo yao. Miradi itakayopatiwa fedha itafuata vigezo vya kusitawisha hifadhi ya bioanuwai na kuendeleza dawa, na kadhalika usitawi wa kijamii na kiuchumi wa tamaduni za vijijini. Kwa ngazi ya kijiji, stadi za kiufundi zilizopatikana kutokana na kugawana faida husaidia kusanifisha na kukuza dawa fita (phytomedicines), kusambaza na kushirikiana taarifa zinazowafaidisha waganga wa kienyeji na afya za jumuiya wanazozihudumia.

Uzinduzi wa FIRD-TM ulitangazwa jijini Abuja, Nigeria, kunako Septemba 30, 1997, wakati wa kongamano la kimataifa juu ya mimea ya dawa lililohudhuriwa na mawaziri watano wa Nigeria na wakuu kadhaa wa mashirika ya serikali ya Nigeria, ikiwa ni pamoja na

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Hifadhi ya Mazingira la Shirikisho la Nigeria. Waziri wa Makao Makuu ya Shirikisho ya Abuja alisema, "... stadi za waganga wa kienyeji ambao pia ni wahifadhi wa utamaduni wetu wa dawa ya asili sasa zinapatiwa nafasi yake mwafaka katika jamii".

Dhana ya mfuko wa dhamana inatoa fursa zaidi ya kushawishi na kusimamia vyanzo vya fedha kutoka NGO nyingine, mashirika au makampuni yenye wito wa kuchangia katika mfuko ulio imara. Wakati mchango wa Hifadhi ulipotangazwa, Chama cha Wazalishaji wa Dawa ya Asili na Kampuni ya Dawa ya Orange za Nigeria ziliahidi kuchangia fedha zaidi kujaliza mchango wa Hifadhi. Mwaka ujao, mradi utatathiminiwa na kutumiwa kuiongoza Hifadhi kuanzisha mfuko wa dhamana wa kiolezo utakaotumiwa na washirika wote wa kampuni ya Shaman, makampuni na mifuko mingine ya kutoa misaada.

### **Masuala yaliyobakia**

Uchunguzi kifani wa kampuni ya Shaman nchini Nigeria unatoa mfano wa jinsi nchi, vikundi vya utamaduni na makampuni yanavyoweza kushirikiana kwa faida ya washika dau wote kuleta maendeleo endelevu ya bioanuwai kwa ajili ya afya ya binadamu. Ni njia mojawapo ya kutimiza malengo ya CBD na kila mshiriki anapaswa kuendelea kutafuta, kubainisha na kuagiza mbinu mpya zinazofaa zaidi kwa mazingira yake. Nchi, tamaduni na makampuni yanayoshirikishwa yametofautiana mno kiasi kwamba hatua zinazochukuliwa zitafaa tu iwapo zitazingatia miktadha mahususi ya kiutamaduni, kiuchumi na kimazingira. Masuala yafuatayo bado hayajapatiwa ufumbuzi.

- Nigeria ilitoa mkakati wa ushirikiano kwa ajili ya kampuni ya Shaman, kwa kushirikisha asasi zenye uwezo kamilifu, hasa kwenye ngazi ya kijiji. Mifumo hii inayojitegemea, ikiwa na machifu wao na serikali zinazofanya kazi, ilichagua kutumia maarifa yao ya kimapokeo kuhusu ulimwengu wa nje kufikia malengo ambayo iliyaona muhimu kwake. Vikundi mbalimbali vya asili vina imani zinazotofautiana kuhusu shughuli za biashara na vina mitazamo inayotofautiana kuhusu dhana ya soko. Tofauti hizi hazipashwi kamwe kuwa kisingizio cha kuvitenga vikundi vya kiasili na matumizi endelevu ya bioanuwai, kwani huu ndio uamuzi wao pekee wa kufanya, na sio ufanywe na NGO zisizo za kiasili, kama inavyofanyika mara nyingi, NGO zinazodai kuwakilisha mawazo ya wenyeji katika kutoa uamuzi juu ya masuala haya.
- Kifungu 8 (j) ni sehemu ya CBD inayozungumzia kuhifadhi na kuheshimu maarifa ya asili. Lakini kinatoa ulinzi hafifu sana wa vikundi vya utamaduni

- na kina- lazimisha CBD ifuate sheria za nchi. Kisheria, ni washiriki wa CBD, sio sera za makampuni, wenye mamlaka ya kuamua jinsi ya kutekeleza maendeleo endelevu ya bioanuwai katika maeneo yao. Hali ya kisiasa ya nchi vinamoishi vikundi vya kiasili ni muhimu kwa mafanikio ya maendeleo ya bioanuwai. Kwa vile vikundi vya kiasili ni washika dau wakubwa wa masuala ya CBD, ni lazima vishirikishwe kwenye mijadala ya mataifa yao kuhusu ufafanuzi na utekelezaji wa CBD. Ili kuhakikisha kudumishwa kwa mifumo yao ya kiutamaduni, ni lazima vishiriki na vipigania vyenyewe masilahi yao. Kama nchi zinataka kufaulu vema kuhifadhi spishi za dunia, mikakati yao lazima ilenge kuwashirikisha watunzaji wa bioanuwai, na sio ilazimishwe juu yao kutoka kwenye ngazi za juu.
- Kufungamanishwa kwa wenyeji na maeneo ya kimapokeo kunaongoza matendo yao yanayohusiana na ikolojia. Utambuzi wa kisheria na serikali wa haki za maeneo unavipatia mamlaka vikundi vya wenyeji kuwakatalia ama kuwaruhusu watu wa nje kuingia katika maeneo hayo—hatua ya kwanza ya kuhifadhi bioanuwai kupitia usimamizi wa kimapokeo wa ardhi na rasilimali. Lakini suala hili muhimu lilipewa uzito

mdogo sana kwenye warsha ya hivi karibuni ya CBD iliyofanyika Madrid na kuhudhuriwa na wawakilishi wa serikali na vikundi vya wenyeji. Watu wengi waliona kuwa hii ilikuwa ni fursa iliyopotezwa. Wengine waliiona warsha hiyo kama hatua ya kwanza ambako maagizo ya kimaendeleo kuhusu hifadhi ya bioanuwai kupitia haki za maeneo, kama vile Sheria Na. 8371 ya Philippines, yangeweza kutangazwa. Jambo lililobaki ni kuangalia endapo katika mikutano inayofuata suala la hifadhi ya bioanuwai kupitia haki za maeneo litabanwa tena na madondoo mengine ya ajenda (Burgiel, et al., 1997).

- Taarifa sahihi ni jambo muhimu. Ni wajibu kwa washika dau wote wa CBD kuwa na uelewa sahihi wa dhana ya haki za uvumbuzi. Haki hizi si mbadala wa haki za ardhi na haki za binadamu na kukatishwa tamaa hujitokeza pindi watu wanapojaribu kuzitumia haki za uvumbuzi kwa malengo yasiyo yake. Jambo litakalofaulu ni kwa nchi, tamaduni na makampuni kuchangia pamoja uzoefu wao, kwani hakuna mfumo mmoja pekee unaoweza kufaa katika mazingira yote. Hifadhi na maendeleo endelevu ya bioanuwai yanahitaji mikabala tofautitofauti.

## Demokrasia ya Umma Ikifanya Kazi

*Msingi wa makala hii ni utafiti uliofanywa na watafiti wa Senegali kwa msaada na ushauri wa kiufundi wa Profesa Peter Eastom wa Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, wakishirikiana na baadhi ya jumuiya za Kiafrika. Utafiti ulifadhiliwa na Club du Sahel OECD, CILSS na ADEA.*

***Tini za MA 16  
January 2000***

Katika vijiji vya bonde la walima karanga wa Kiwolof na Wafulani wa Fouta Toro nchini Senegali, “demokrasia” limekuwa ni neno litumikalo na wengi. Shirika la Senegali lisilo la kiserikali (NGO) “Tostan” (jina la Kiwolof linalomaanisha kujitoka kati-ka yai), ambayo ni programu ya elimu isiyo rasmi ya wanawake wa vijijini, kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili limekuwa likiendesha mafunzo ya misingi na mienendo ya demokrasia. Mpango huu umefuatia programu ya mafunzo na uwezesaji ambayo imekuwa ikiendeshwa na NGO hii katika eneo lote la Senegali ya kati kwa muongo (miaka kumi) uliopita. Mpango huu ulikuwa wazi kwa watu wote, lakini uliwalenga hasa wanawake na ulijumuisha mafunzo katika utatuzi wa matatizo, uzalishaji mapato, kusoma na kuan- dika katika lugha ya Kiafrika na afya ya mtoto. Ili kukidhi mahitaji yaliyo- jitokeza na kadiri mpango ulivyokua, maudhui mapya ya mafunzo yalita- yarishwa kwa kuwashirikisha wana- funzi walengwa. Mojawapo ya mau- dhui ya mwisho yalijumuisha afya ya wa- nawake, ikiwa ni pamoja na majadi- liano juu ya somo nyeti lililohara- mishwa—yaani nafasi ya wanawake katika ngono-mada iliyowavutia wa- shiriki wengi vijijini kote. Wafanya- kazi wa Tostan waligundua kwamba chanzo cha hamasa kubwa na yenye

nguvu katika mada hii kilikuwa msisitizo wa mada juu ya haki za binadamu, hasa haki za wanawake na watoto kutobaguliwa na kutotish- wa na vurugu. Watu walitaka kufa- hamu zaidi juu ya mambo haya.

### **Demokrasia kuanzia kwenye familia hadi kwenye ngazi ya Taifa**

Kabla ya kuandaa maudhui mapya, wafanyakazi wa NGO waliamua ku- fanya utafiti uliowashirikisha wa- nanchi ili kujua mahitaji muhimu ya wananchi hao katika mafunzo ambayo yangetolewa. Matokeo ya utafiti yalikuwa ya kushangaza. Wananchi walihitaji sana kupanua uelewa wao wa masuala ya haki za binadamu na kuangalia kwa makini masharti yake na hata aina ya jamii, ambamo haki hizi zinaweza kuteke- lezeka kwa uthabiti zaidi. Neno “demokrasia” lilijitokeza mara nyingi, likiwa limesikika kutoka kwenye mjadala wa kisiasa wa kitai- fa, lakini hakukuwa na mtu aliyeku- wa na uhakika wa maana ya neno hilo. Hivyo wafanyakazi waliamua ku- fanya majaribio ya utaratibu wa ma- funzo uliohusisha dhana ya demo- krasia na mfumo wa kijamii uliopo ambamo haki za binadamu zinaweza kutekelezwa kwa ufanisi na watu wa aina zote wanaweza kushiriki kua-

mua majaliwa yao. Maudhui ya mafunzo yaliyotokana na majaribio haya yaliyodumu kwa miezi kadha yalijumuisha taarifa (habari), majadiliano, uigizaji na shughuli zenye matumizi yenye manufaa—vyote vikisisitiza juu ya haki za binadamu ambazo jamii lazima izilinde, jinsi maadili binafsi na ya vikundi yanavyowekwa sawa, kwa njia gani wale walionyang'anywa haki zao wanaweza kuzidai, jinsi gani mizozo hutatuliwa, na mikakati ya uongozi bora inayohitajika kwa ajili ya malengo ya aina hii. Waandaaji waliona ni vema kurejea maana ya msingi ya “demokrasia” katika Kigiriki—yaani serikali inayoen-deshwa na watu—na kutoa nafasi kwa majadiliano mapana juu ya kilichomaanishwa hasa na dhana hii na jinsi ilivyohusishwa na madai ya haki za binadamu na utatuzi wa mizozo. Demokrasia ilifasiliwa na kujadiliwa kama mpango unaoathiri maisha ya familia na jumuiya za vijiji kama unavyoathiri pia siasa katika ngazi ya mkoa au taifa. Mjadala na mabadilishano ya mawazo juu ya mada hizi katika jumuiya zilizoshiriki ulikuwa wa kulisimua na punde ukavuka mipaka ya kozi ya elimu isiyo rasmi. Mazungumzo mengi ya pande mbili kati ya wanaume na wanawake, vijana na wazee, na hata baina ya kabila mbalimbali yalijitokeza katika maeneo mengi yaliyohusishwa kwenye mradi huu.

### Kutunza imani ya wananchi

Waandaaji walijali sana kushirikisha mamlaka za vijiji na viongozi wa kidini katika programu hii. Kusema kweli, pengine kichocheo kikuu cha mpango huu ulikuwa mwingiliano na maadili ya kidini, hasa ile ya Kiislamu, katika maeneo husika. Mtazamo wa waumini wengi ulikuwa kwamba haki na kanuni za kidemokrasia zilizokuwa zikijadiliwa ziliakisi vema zaidi maadili ya Kiislamu kuliko ya jamii ya kisasa au desturi za kileo.

Matokeo ya dhahiri yalionekana punde katika nyanja mbalimbali. Msukumo mkubwa ulielekea kutokana na falsafa ya Gandhi ya kutotumia nguvu—yaani, kutokana na juhudi za makusudi za kuwafanya wananchi kutambua ukinzani kati ya maadili na mienendo halisi. Ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika familia unatoa mfano hai. Washiriki wa programu ya elimu ya demokrasia ya Tostan walishutumua tabia ya kuwapiga wake na watoto katika familia. Matukio halisi ya vipigo yalitolewa na kujadiliwa katika jumuiya mbalimbali. Kama kiongozi wa kiume wa kaya katika kijiji cha Ngaparou alivyosema “sote tulijua kwamba haikuwa haki kuwapiga wanawake. Tulifanya hivyo kwa mabavu tu. Lakini hatuna budi sasa kubadilika, kwa sababu jambo hili sasa linachukuliwa kuwa ni uovu na watu wote. Ni

jambo lililo hadharani. “Kuwa hadharani”—ingawa kwa kawaida si kwa namna ya ushari—ndiyo imekuwa zana kuu ya mabadiliko haya”.

Haki za watoto ni jambo jingine muhimu linalotiliwa mkazo. Vikundi vingi katika mji wa Thies vilivyoshiriki kwenye programu hii vilibaini kuwa kukosekana kwa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wengi katika jumuiya zao ilikuwa mojawapo ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Jambo hili lilipaswa kurekebisha, kwani liliwazuia watoto hawa kujiandikisha shuleni na kupata fursa nyingine za maisha bora. Washiriki wa programu walishawishi uanzishwaji wa taratibu mpya na upatikanaji na vyeti vya kuzaliwa kwa idadi kubwa ya vijana. Katika baadhi ya maeneo ya mkoa, tatizo la ndoa za utotoni bila ridhaa ya wasichana lilijadiliwa pia kwa kina. Ongezeko la msisitizo juu ya haki za wasichana lilipelekea pia kwenye upigwaji marufuku tabia ya kutahiri wanawake—jambo lililojadiliwa kwenye Tini za MA 3 kuhusu Kiapo cha Malicounda.

### Desturi za uwajibikaji

Mjadala wa demokrasia unaelekea pia kuwa na athari kubwa kwa utendaji kazi wa vyama vya kijumuiya na jumuiya zenyewe. Dhana za uwajibikaji, uwazi, sifa za uongozi, uwakilishi wa vikundi mbalimbali na utawala bora zilijadiliwa sana kwenye mtaala kama ilivyokuwa pia kuhusiana na mbinu za kutatua mizozo inayoletwa na madai ya kutambulika kijamii na ya usawa. Wafanyakazi wa Tostan wanawaona washiriki wa awali wa programu hii wakikiri kuwa pamekuwepo na mabadiliko makubwa katika taratibu na hata watumishi wa vyama vya kijumuiya kutokana na mafunzo haya. “Sasa tunajua vizuri zaidi sifa za kiongozi”, wanasema: na kuna ongezeko kubwa la ushiriki wa wanawake katika shughuli za uongozi. Aidha wanawake hawataki tena kuvumilia utaratibu wa kijadi ambapo kiongozi—wa kiume au wa kike—hutoa maamuzi kwa ajili ya washirika wenzake. Na katika maeneo kadhaa vituo vya kutatua mizozo vimeanzishwa na wanawake waliohitimu mafunzo ya demokrasia.

Zaidi ya hayo, yapo pia madai mengine ya kisiasa. Washiriki wanadhani kuwa idadi kubwa zaidi ya wanawake wanapendelea kupiga kura kuliko ilivyokuwa hapo awali—na wachache wanaukubali utaratibu uliozoeleka ambapo kiongozi wa kiume wa kaya huwaelekeza wanafamilia wote jinsi ya kupiga kura. (Kwa hakika katika baadhi ya vijiji chifu ndiye aliyeamwua namna wakazi wake wote watakvoyopiga kura). Mjadala juu ya sifa za kiongozi umepelekea kuanzishwa kwa vigezo vipya

vya kuwatathimini wagombea wa nafasi za uongozi wa kisiasa katika baadhi ya maeneo. Orodha mahususi ya vigezo hivyo ilitayarishwa na wagombea wakahitajika kuwa na idadi kubwa ya vigezo hivyo kabla ya kuteuliwa kushika madaraka. Wanawake wa eneo la Fouta Toro waliazimia kufuatilia kwa karibu utungaji wa sheria za kitaifa ili uzingatie haki za binadamu.

### **Sekta inayokua**

Dai la mafunzo ya demokrasia limekuwa likiongezeka na kuchochea ari ya kupigia kampeni masuala ya haki za wanawake. Washiriki kutoka visiwa vya Sine Saloum kiangazi hiki walitumia mitumbwi kuzifikia jumuiya mbalimbali katika eneo lao ili kuunda umoja dhidi ya tohara za wanawake. Zaidi ya vijiji themanini, vilivyoenea takribani katika tarafa nzima ya Dabo, vimejiunga na umoja huu kwa hiari yao. Na katika maeneo ya Toucouleur ya Fouta Toro washiriki wa programu ya mafunzo wameanzisha “maonyesho ya barabarani” ambayo huonyeshwa kwenye vijiji mbalimbali vya maeneo hayo.

Matokeo yameonekana pia kwenye maeneo ya mbali kabisa. Washiriki kutoka eneo la Ngirin Bamba walianzisha mradi wa bustani kwa kuomba mashamba kutoka kwa wanaume wa kijijini kwa msingi wa “ardhi kwa mkulima”—na kisha wakaweka bango kwenye lango la bustani yao ya mboga za majani na matunda lililosomeka “haki ya kumiliki ardhi”.

Hivyo dhana za “demokrasia”—zinazozingatia mazingira halisi ya Senegali zinajumuishwa katika madai haya mbalimbali ya haki za binadamu. Neno lenyewe limekopwa moja kwa moja katika lugha za Kiwolof na Kifulani/Kipulaar na kutumika mara kwa mara katika mabishano, matangazo, na utani kwenye vijiji vyote vinavyoshiriki katika programu ya mafunzo. Kama mwanamke mmoja wa Ker Simbara alivyomweleza mwendesha mafunzo aliyetembelea huko kufuatilia utekelezaji wa programu, “tulilazimika kubadilisha uendeshaji wa mikutano yetu ya ushirika kwa sababu tulibaini kuwa ilikuwa haiendani na “demokrasia”. Wakati majaliwa ya serikali ya uwakilishi wa kitaifa yangali mashakani katika bara lote la Afrika, iaelekea demokrasia inayozingatia mazingira halisi ya eneo husika ndiyo itakayopendelewa na nchi nyingi siku za usoni.

# Mipango ya Kieneo, Dira za Wenyeji: Ushirikishwaji katika Kuandaa Mustakabali huko Afrika Magharibi

*Makala hii imeandikwa kutokana na utafiti uliofanywa na watafiti wa ndani kwa kusaidiwa na usimamizi wa kiufundi wa Peter Easton, Profesa Mshiriki, Masomo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, kwa kushirikiana na jumua husika za Kiafrika. Utafiti ulifanyika chini ya usimamizi wa pamoja wa Klabu ya Saheli/OECD, Kamati ya Ushirikiano wa Majimbo ya Kupambana na Ukame katika Saheli (CILSS) na Chama cha Maendeleo ya Elimu barani Afrika (ADEA)*

***Tini za MA 17  
Februari 2000***

Kuanzia mwaka 1990, Klabu ya Saheli—ambayo ni tawi la Chama cha Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ambacho kinahusika na kuratibu mashirika ya misaada ya kutoka kaskazini ya usimamizi wa usalama wa chakula na maliasili katika maeneo ya pembezoni mwa jangwa ya Afrika Magharibi—imeamua kudurusu mpango wa muda mrefu uliopo wa kanda. Katika jambo hili, chama kimeshirikiana na Kamati ya Majimbo ya Kupambana na Ukame katika Saheli (ambayo katika maeneo yanayozungumza Kifaransa inajulikana kwa kifupi kama “CILSS”), asasi ambayo imeshirikisha Wizara ya Kilimo na wakala nyingine za serikali za nchi saba za Kisaheli yenye makao makuu jijini Ouagadougou.

Kazi hii ilifanywa kwa kiasi kikubwa na wataalamu wa uchumi, na siasa waliopewa kazi hiyo na Chama cha Saheli. Wataalamu hao walitumia tafiti na data zilizopo zinazoonyesha mwelekeo wa kikanda na kupanga utaratibu mbadala kwa ajili ya miaka thelathini ijayo ya maendeleo ya Afrika Magharibi. Chapisho lililopatikana, maarufu kwa jina la “Utafiti wa Mitazamo ya Muda Mrefu ya Afrika Magharibi”, au “Utafiti wa WALTPS” ilichochea mitafaruku mingi. Kulikuwa kuna kutokukubaliana watu wa Ulaya waliopendelea utaratibu wenye mwelekeo wa kimji,

na wa Amerika ya Kaskazini walio-pendelea mwelekeo wa vijijini. Vilevile kulikuwa na kutoelewana baina ya wataalamu kutoka kaskazini ambao karibu uchambuzi wote waliufanya wao na watafiti wa Kiafrika ambao walihisi kwa kiasi fulani wanadanganywa. Mradi mzima kwa muda fulani ulionekana umejawa na mitafaruku ambayo imeficha faida ya data zilizokusanywa.

## **Kupeleka mradi uwandani**

Mtafaruku ulikwisha kwa kiasi fulani baada ya kusuluhishwa na wakulima wa Afrika Magharibi. Wakati huohuo, Klabu na Kamati ya Majimbo ya Mapambano dhidi ya Ukame walikuwa wakishirikiana katika utafiti wa ushirikishwaji wa utoaji madaraka na utayarishaji wa nguvukazi katika nchi tano za kanda: Burkina Faso, Ghana, Mali, Niger, na Senegali. Utafiti huo ulijumuisha tafiti za maeneo maalumu za jumua za wenyeji na vyama ambavyo vimejichukulia madaraka vyenyewe makubwa ya maendeleo na uongozi. Wasimamizi wa jitihada za kiutafiti za nchi tano walishauri kuwa njia mojawapo ya kuondokana na mtafaruku uliomo ndani ya Utafiti wa WALTPS ni kupeleka swali la msingi, maangalizo, na mahitimisho

uwandani na kuitisha maoni kutoka kwa wananchi wa jumua husika, kwa msingi kwamba wanajumuia hao wanawakilisha wadau muhimu sana katika mipango hiyo ya muda mrefu. Wataalamu walielezea wasiwasi wao juu ya njia hii ya kiumma: je, wananchi wa kawaida wana upeo unaohitajika wa dira na shauku katika masuala ya kila siku vitu ambavyo vinatakiwa, ili waweze kuchangia katika utayarishaji wa mustakabali? Watetezi wa mwelekeo wa umma wanadai kuwa, karibuni kila kijiji kina watu ambao ama wamesafiri sana katika kanda au kwa sasa wako nje wakifanyakazi katika miji ya pwani, kama sio ng'ambo, na kwa maana hiyo, mseto wa uzoefu wao pamoja maarifa waliyokuwa nayo kuhusu mazingira ya uwandani huwafanya wawe washirika muhimu.

Mwishowe, iliamuliwa kuwa upatikane ushauri kutoka uwaandani kuhusu mipango ya muda mrefu katika nchi zote tano. Watafiti wa Kiafrika na wa kimataifa waliohusika wakatayarisha mbinu ya majaribio kwa kufanya mdahalo na uchambuzi kuhusu mustakabali wa jumua ya karibu na kwa kanda. Kazi hii ilijumuisha kuorodhesha wawakilishi kutoka kwenye makundi mbalimbali ya kijamii wakati wa ukusanyaji wa data, kujadili na kutabiri mustakabali.

### Mwongozo wa mdahalo wa wenyeji wa mahali

Kazi inajumuisha hatua tano zinazofuatana:

1. Kuchunguza mabadiliko muhimu yaliyotokea katika jumua ya karibu, nchi zinazozunguka, na kanda nzima ya Afrika Magharibi kwa kipindi cha miaka thelathini iliyopita, na kwa kuzingatia maeneo matano muhimu ya maisha ya kila siku:

- Mazingira
- Demografia (idadi ya watu)
- Uchumi
- Jamii na utamaduni
- Siasa

Watafiti walitayarisha muhtasari wa matokeo muhimu ya Utafiti wa WALTPS, lakini walijaribu pia kupata maoni ya wananchi. Swali muhimu lilikuwa, "Mambo yamebadilika vipi katika jumua yako na maeneo yanayozunguka katika mambo haya matano muhimu tangu watu wazima vijana walipokuwa watoto wachanga?"

2. Fikiria jambo la msingi ambalo linaweza kuelezea mabadiliko haya, uhusiano uliopo kati yao, na mwelekeo wa muda mrefu unaoakisi hayo.

3. Fikiria hali inayoweza kuwepo katika miakia thelathini ijayo—katika maeneo yote matano yaliyotajwa—kama

mwelekeo kama huu na mambo yake yataendelea kuwepo kwa namna hiyo.

4. Jadili mambo yatakavyokuwa baadaye na hali ambayo kikundi kingependa iwepo katika utabiri huu, yaani aina ya maisha ya baadae ambayo wangependa kuwamilikisha watoto wao.

5. Fikiria kitu kitakachohitajika kufanywa katika kiwango cha kijiji, kitaifa na kimataifa ili kuisogeza hali kuelekea kwenye hali ya baadae inayotakiwa.

Mbinu zilizotumika kuzindua mchakato na kuongoza mdahalo zilitofautiana kutoka nchi moja na nyingine:

- Nchini Ghana, kwa mfano, timu ya utafiti ilipanua wingo wa watafiti wa vyama vya msingi na biashara ili kujumuisha pia shule chache za sekondari na taasisi za mafunzo ambapo wangeweza kupata mwelekeo wa kizazi kijacho cha viongozi wa Afrika Magharibi. (Mbinu zilizotumika nchini Ghana zinawasilishwa kikamilifu mwishoni mwa kiambatisho hiki).
- Nchini Niger na Mali, timu ya utafiti ilitafsiri kijitabu cha wawezeshaji na mwongozo wa mdahalo katika lugha mbalimbali za Kiafrika.
- Nchini Burkina Faso, watafiti waliamua kuuliza kila jumua kuchagua jopo la washiriki kwa mujibu wa umri na jinsia na kufanya kazi kikamilifu na kundi hili lengwa.
- Nchini Senegali, watafiti wa kitaifa waliwapa kila timu ya watafiti wa vijijini seti ya vifaa rahisi vya wawezeshaji, ikiwa ni pamoja na ramani ya Afrika, ramani ya Senegali, na chati mgeuzo na kalamu. Uwakilishi katika zoezi hili ulipewa pia umuhimu mkubwa nchini Senegali, timu ya kitaifa ya utafiti ilialika vyama vyenye mikataba kuendesha mdahalo vyenyewe, kuwapa mafunzo maofisa waliowachagua na kuanzisha mikataba na taasisi hizi za wenyeji ili kuelekeza kazi.

### Dira za wenyeji

Zoezi hili lilichochea hamasa kubwa katika jumua zote zilizoshiriki—jumla zikiwa hamsini na sita katika nchi zote tano. Matokeo muhimu ya utafiti yanaweza kufupishwa kama ifuatavyo:

1. Viongozi na wajumbe wa vyama vya msingi vilivyoshirikishwa—wakiwa wanaume kwa wanawake— walifurahishwa sana na wazo la kutabiri na kujadili mustakabali wa jumua yao, nchi na kanda, na wakawa na uwezo mkubwa wa kushiriki katika zoezi hili. Walifurahishwa zaidi na:

- kupata kwa mara ya kwanza, fursa ya kushiriki katika mijadala ya kisiasa kuhusu mikakati ya kimaendeleo na mustakabali wa mazingira yao;

- nafasi ya kupata “maoni ya kimifumo” ya mabadiliko ya mazingira yao na kukosoa shughuli za wenyeji ambazo haziendani na maendeleo endelevu;
- utafiti huu wa majaribio unaohusu utaratibu ambao utaviwezesha vyama vya msingi kuandaa mpango wa muda mrefu wenye mfumo na kuona mahusiano yao katika mazingira mapana zaidi.

2. Uchambuzi wao wa mabadiliko yaliyotokea katika ngazi ya mitaa, na sababu zake, na mambo yanayoweza kujitokeza kutokana na mabadiliko hayo, lakini ambayo sio moja kwa moja yale yaliyotajwa na waandishi wa tafiti mbalimbali zilizorejewa. Mada zifuatazo zilitawala sana mdahalo:

- Mabadiliko makubwa na kero kubwa zilizobainishwa zilikuwa zile zilizo katika maeneo ya kiikolojia na kiuchumi, yanayohusiana hasa na kilimo. Uwelewa mkubwa uliosambaa kwa watu wengi kuhusiana na uharibifu wa mazingira na nafasi ya binadamu (ongezeko la watu, njia za kilimo, matumizi ya mali ya asili) katika uharibifu huo ulionekana kila mahali.
- Ijapokuwa inatambuliwa kuwa idadi ya watu inaongezeka karibu kila mahali, na wakati huohuo mwingiliano baina ya makundi ya kimbari na kijamii umeimarika zaidi, hakuna jambo mojawapo katika hayo limetafsiriwa kuwa tatizo au chanzo cha migogoro. Maoni kuhusiana na mpango wa uzazi yanatofautiana sasa, hususani kati ya watu wazima na wazee, kwa upande mmoja na kati ya vijana na wanawake kwa upande mwingine. Kwa ujumla, kundi la pili linaunga mkono mpango wa uzazi, na kundi la kwanza wanaelekea kupinga. Mwanamke mmoja mkulima wa Senegali anasisitiza kuwa “sisi sio mashine za kutengeneza watoto.” Hata hivyo, *pater familias* (baba wa familia) anayeishi katika jumua ya jirani, kwa kuangalia maeneo ya Ulaya yenye watu wengi zaidi anadai kuwa: zikiwepo rasilimali za kutosha, hakutakuwa na matatizo katika kukabiliana na ongezeko la watu.
- Washiriki wa mahali husika waliweka mkazo mkubwa kwenye uhusiano baina ya maeneo ya mjini na vijijini, na kuongelea kukamilishana kwa maeneo haya, maoni ya pande mbili, na hata kubadilisha mwelekeo wa uhamaji mara nyingi kuliko hata namna walivyofanya waandishi wa tafiti zilizorejelewa. Baadhi ya watoa habari walioko mjini na katika majiji walikazia haja ya kuongeza vitegauchumi katika maeneo ya vijijini, mahali ambapo wengi wao wanaendelea kuwa na mahusiano nako.
- Kuna kutambulika kwa ujumla kulikoenea sana kwenye nchi zisizo na bahari kama vile Mali na Niger, kuwa

itakuwa jambo la lazima hapo baadaye kutegemea zaidi rasilimali na maarifa ya vijijini, na kwamba kutokana na kukua kwa chuki dhidi ya wageni katika nchi wenyeji, kuhamia nje hakutakuwa tena suluhisho mwafaka.

- Msamaha unakubalika sana mintaarafu tafiti zinazorejelewa kwa kukosa kutilia maanani kuporomoka kwa maadili ya kijamii na mambo ya kimbari na kiutu ya wakati huu. Kuvunjika kwa mfumo asilia wa kifamilia na ongezeko la ubinafsi ni mambo ambayo yametajwa katika maeneo ya mjini na vijijini.

3. Kuna tabia ya kuelezea wakati uliopita (ukiwakilishwa kwa mujibu wa zoezi hili na miaka ya 1960) kwa kusifia: ardhi ilikuwa na rutuba, wanyamapori walikuwa wengi, watu walikuwa wameridhika, n.k. Kwa upande mwingine, matukio ya wakati huu yanaonekana ni makali kila mtu anazungumzia utafutaji wa ufumbuzi

4. Katika uwanja wa siasa, kipindi cha mwanzo cha demokrasia kilichoonekana miaka ya hivi karibuni, kimepewa alama nzuri na washiriki, lakini wamevilaumu vyama vya siasa kwa kuleta mfarakano. Maeleze yao kuhusu hali ya baadaye yalijumuisha kutoa umuhimu zaidi kwa serikali za mitaa. Karibuni watu wote waliweka umuhimu maalumu kwenye vyama vinavyoendeshwa kimitaa, biashara za ushirika, na mashirikisho ya vijiji. Tatizo la kuunganisha vyama hivi vya msingi na mipango ya ugawaji madaraka na mipango ya kukuza demokrasia inayotekelezwa sasa limetajwa mara nyingi.

5. Watafiti ambao wameratibu zoezi hili walizangatia sababu kubwa za kupinga mgawanyo wa madaraka katika ngazi ya mtaa miongoni mwa makundi yalionufaika na hali ya sasa na kuitisha utungaji wa sera zilizo wazi zaidi zinazohusiana na njia za kufuata. Walifikiria kwamba mfumo wa ugawaji madaraka wa kutoka juu kwenda chini ukiunganishwa na vyama vilivyoanzishwa huko uwandani kwa mfumo wa kutoka chini kwenda juu, labda inawezekana ikawa njia rahisi kuzuia upinzani kutoka kwa wananchi na vilevile njia ya kuunda msingi imara wa zoezi la kugawa madaraka.

6. Jambo lingine lililotajwa sana na washiriki lilikuwa ni muungano na ushirikiano mzuri miongoni mwa nchi za Kisaheli. Hitimisho kubwa lilikuwa kwamba, kwa kiasi fulani jina lenyewe “Saheli” na uanachama wa CILSS huonyesha ukubwa wa tatizo, na sio suluhisho. Maendeleo ya kiuchumi katika Afrika Magharibi hutegemea kwa kiasi kikubwa uunganishaji wa maeneo yasiyo na bahari na yale ya pwani kwa kupitia mihimili ya kaskazini-kusini iliyotumiwa na wafanyabiashara kabla ya ukoloni ambayo ilichochea maendeleo ya falme kubwa za ukanda huo, lakini zikaja kuvunjiliwa mbali na mifumo ya kikoloni. Kwa hiyo, suluhisho la muda mrefu



la kudumaa kwa uchumi linaonekana kuhitaji mipango mipya kati ya nchi za Kisaheli na maeneo ya pwani kama vile Nigeria, Benin, Ghana, Cote d'Ivoire, Guinea na Liberia-na kwa nchi zote za Afrika zinazozungumza Kifaransa/Kiingereza-na kwamba CILSS inaweza kusaidia lakini haiwezi kufanya hivyo ndani ya mfumo wake pekee.

### Mafunzo ya kimbinu

Wakati huohuo, "utafiti wa mpango wa muda mrefu wa mitaa" ulikuwa kwanza ni jaribio la kutafuta mbinu za utekelezaji na pili udadisi kamili wa mitazamo ya wananchi kuhusu mustakabali wa Afrika Magharibi.

Washiriki katika warsha ya kuhitimisha walikuwa na fikra kwamba faida ya muda mrefu ya mbinu iliyojari-biwa katika zoezi hili itatokana na kugeuzwa kwake kuwa mkakati na chombo cha *kujifanyia tathmini na cha kuwekea mipango ya kimkakati ya vyama mbalimbali vya msingi na biashara vilivyoshiriki katika zoezi hili*. Chombo hiki kinakosekana kabisa katika vyama vingi, ambavyo mara chache sana huwa na mbinu za kuji-tathmini, uhifadhi wa taarifa, upataji wa taarifa zilizo-hifadhiwa na upangaji mipango.

Matokeo ya utafiti yameonyesha jambo moja lingine muhimu. Jambo hili ni kuwepo kwa haja kubwa ya kuwa

na zana bora zaidi na za kawaida za "uchunguzi wa mambo", upangaji mipango ya kimkakati, na utumiaji wa taarifa *ndani* ya vyama hivi. Kitendawili kinaweza kuwa wakati mbinu ya upangaji wa mradi inakuwa ama haitumiki au inakuwa kitu cha kukosoa ndani ya mashirika ya misaada yenyewe, baadhi ya vyombo hivi vidogo lakini vinavyotumika sana vinaweza kugeuka na kuwa ndio tiketi ya kuingia katika vyama vya kimtaa, jumua na vitegauchumi.

Mojawapo ya timu za utafiti iliombwa kupendekeza mbinu rahisi ya upangaji wa miradi kwenye chama cha kimtaa kilichoshiriki katika zoezi hili la kutabiri hali ya baadae, kwa wasiwasi, chama hicho kikapendekeza mfumo mara moja badala ya ule wa zamani wa muda mrefu. Kwa mshangao wa watafiti, jambo hili lilikuwa pigo la papo kwa papo, kwa sababu wametoa "sampuli" cha kukusanyia maoni ya kimtaa juu ya hali ya baadae inayowezekana kuwa na uwekezaji unaofaa. Labda mapungufu yake kwa kiasi kikubwa ni matokeo yanayoweza kutokea kwa kukitumiachama katika kiwango kisicho, yaani kiwango cha kati badala ya kiwango cha kimtaa. Ni kwa kiasi gani utendaji wa shirika la ufadhili na shirika la kiserikali yanayokosolewa sasa yanaweza kuthibitisha kuwa ni chachu kama yataachwa mikononi mwa watendaji wa kimtaa?

# Usimamizi Shirikishi na Utamaduni wa Mhali: Methali na Mikabala

*Makala hii inatokana na utafiti ulifanywa na watafiti wenyeji kwa msaada wa usimamizi wa kiufundi wa Peter Easton, Profesa Mshiriki, Mafunzo ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima katika Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida. Pamoja na ushirikiano na jamii husika za Kiafrika. Utafiti umefanywa chini ya juhudi za pamoja za Klabu ya Saheli/OECD na kamati za Kijimbo za kupambana na ukame katika Sahel na Chama cha Maendeleo ya Elimu katika Afrika.*

***Tini za MA 18  
March 2000***

Mara nyingi tathmini inafikiriwa ni shughuli inayohitajiwa na wafadhili, kimsingi kutoka nje hadi utamaduni wa wenyeji—ni ujuzi na njia ya kufikiri kuwa ni suala la kigeni. Kama siyo tu linatishia wanufaikaji wa programu na wafanyakazi wake pia.

Mambo mengi yamefanywa katika miaka ya hivi karibuni katika kuanzisha mifumo shirikishi na wenye kutoa uwezo wa kutathmini programu ambayo inawapa wafanyakazi na wadau wajibu tendani wa kutoa maoni ya jinsi tathmini inavyoendesha na jinsi matokeo yake yanavyotafsiriwa. Njia bunifu zimepatikana ili kuonisha ushiriki huu uliozoeleka kwa kuongeza nguvu zaidi, kuminika na kuwa na matokeo wakilishi kupitia nyenzo zifaazo toka kwa wadau. Zaidi ya hayo, kumekuwapo na ongezeko la utambuzi wa hali ya juu wa athari za tathmini za programu zinazotokana na usimamizi makiini wa siku kwa siku na maelekezo ya michakato halisi kwa wanaohusika na maana ya matokeo ya kitakwimu yanakuwa na tafsiri zaidi ya moja hadi hapo yatakapotafsiriwa, na makundi ya wadau tofauti yanayohusika, wakati mwingine matokeo hayo hujipinga.

**Tathmini: Agizo kutoka nje au tendo-hiari la wenyeji?**

Mitazamo hii inaimarisha umuhimu wa wenyeji kushiriki na “umilikaji” wa juhudi za tathmini. Hata hivyo wanaweza wasigusia jambo lenyewe kikamilifu. Je mawazo ya uwajibikaji, kupima utendaji na kufanya maamuzi yanayojikita kwenye data bila kulazimishwa au yanazingatia analogia inayowahusu wenyeji? Kama hivyo ndivyo, kuna uhusiano gani na unachukuliwaje na kutumiwa katika tathmini ili kuifanya iwe zana ya wenyeji na teknolojia sahihi? Swali lina umuhimu mkubwa wakati wa enzi ya kuongezeka kwa ugatuaji katika utawala na elimu ambapo mitazamo inayofanikiwa kwa managementi binafsi ya kweli bado ipo katika hatua ushawishi.

Ukweli ni kuwa moja ya matokeo yasiyotegemewa ya kufanya tathmini shirikishi katika Afrika Magharibi ni kuingiza tabia na mitazamo ya wenyeji katika tathmini. Kufanya hivi kunasaidia kuwa na msingi wa uanzishaji wa mbinu za tathmini zifaazo. Moja ya njia ya ugunduzi ni kwa kutumia methali zinazoeleza tabia za wenyeji na uelewa wao kuhusu masuala ya nayo husiana na tathmini kama uwajibikaji, utendaji wa kazi na wajibu wa jamii.

## Methali: Mila katika mwendo

Katika kanda yote, methali zinakuwa dirisha la kishairi lililotoa kwa muhtasari wa juu uzoefu wa binadamu na jinsi wenyeji wanavyouelewa ulimwengu. Neno lenyewe “methali” linaeleza ukweli katika mila nyingi za kitamaduni. Kwa mfano katika lugha ya Kihausa neno ni “karini Magana” likiwa na maana “hotuba iliyofungwa”. Methali za Kiafrika zina aina ya muundo uliopembuliwa ambapo maana imefungwa ndani na kuleta uhusiano kati ya uzoefu wa sasa katika nyanja tofauti unaoleta mwanga mpya juu ya mambo na mpangilio wa mtazamo. Hai-shangazi kuwa uzoefu huu mara nyingi hauhitaji kufundishwa ambapo wahakiki wa kisasa wanapenda kuuita “ufunguaji” unaweza kuwa ni ushairi ili kuuwekeka ufahamu wa finomena ya pamoja kama katika kusan-yiko lolote la kisiasa.

Katika methali za kiafrika kuna mpya na za zamani. Ni mara chache zinafungwa katika vitabu vya busara. Methali mpya zinabuniwa muda wote na methali za zamani zinaondoka katika matumizi, ni mchakato unaoendelea na wanasimu wanauita “ubunifu wa msamiati” wakati huo huo methali hazitoi majibu ya mizimuni. Kwa kila methali, inasemekana ipo nyingine inayoeleza wazo la kinyume. Methali ni karibu sawa na lugha ya fikra. Hata hivyo, methali zinakuwa njia ya kuhusisha mambo ya sasa na uzoefu wa kihistoria wa kundi na kusaidia kuhakikisha uendelezaji wa mshikamano wa mifumo ya amali na motisha inayohimiza juhudi mpya. Kama msemu kutoka lugha ya Ewe, ya Mashariki mwa nchi ya Ghana unavyoweke wazi, *ka xoxoa nu wogbia yeyea ðo*—“kamba mpya inasukwa mwishoni mwa ya zamani”.

## Tathmini na utendaji

Kufikiria kuwa hakukuwa na uwajibikaji kwa rasilimali katika ngazi ya vijiji kabla ya uafuaji wa programu rasmi za maendeleo ni kama kudhani kuwa hakuna mtu aliyejifunza kitu chochote kabla ya shule rasmi kuanzishwa au kilimo hakikuwapo kabla ya kufika kwa wakala wa uenezi/upanuzi wa kilimo. Methali toka lugha ya Ki-niger inatukumbusha: *Kunkuru ya san makamar matar-shi*: “Kobe anajua jinsi ya kumkumbatia mkewe”.

Kwa kifupi, baadhi ya vitu vinaweza kuonekana haveleweki kwa mtu wa nje lakini kwa kuwa vinahusu afya ya msingi na ustawi wa watu unaweza kuwa na uhakika wale waliohusika walitoa majibu kwa angalau kujiridhisha kwa kiasi fulani muda mrefu uliopita.

Tukiangalia nyuma tathmini ya kisomo chenye manufaa katika Jamhuri ya Mali kwa miongo miwili iliyopita. Kuna kukata tamaa kutokana na matatizo ya kufuatilia

program ambapo matokeo yaliyotangazwa yalionekana kuwa mbali na ukweli uliokuwapo uwandani. Mmoja wa watafiti alitoa methali toka nchi ya Niger iliyoonekana kueleza hali ilivyokuwa kwa lugha ya mkato yenye ucheshi mzuri: *Da an ce da kare tuwo ya yi yawa a gidan biki, ya ce imagani a kas!*: “mbwa alivyoelezwa kuwa kuna chakula kwa kila mmoja katika tafrija ya harusi, alijibu, “tutahakikisha hilo huko huko chini ya meza.”

Ukweli ni kuwa kunaweza kuwa na aina zote za vyakula mezani katika tafrija, lakini mpaka vifikie chini kabisa mbwa anaweza kuwa hana sehemu yoyote. Hivyo ndivyo ilivyo kwa programu nyingi za maendeleo: mambo mengi yanayosemwa hayalingani na faida wanazopata washiriki katika kiwango cha kijiji. Na ni ukweli kuwa tofauti hii inafanya tathmini isaidie upimaji.

Kitu kinachofurahisha hapa si umuhimu wa methali zinapotumiwa wakati wa masuala ya tathmini, lakini kwa kuwa zina ukweli na uhusiano wa kutia uchungu zieleweka haraka na kukubaliwa na watu wa kundi la jamii jirani. Msemu huo ukawa kama wito kwa ajili ya tathmini.

## Uwajibikaji na ufanisi

Uwajibikaji unaweza kuonekana kama fikra iliyoletwa. Lakini msemu wa Kihausa wa kipindi kilichopita unajumuisha taswira zinazofahamika katika tamaduni nyingi za Afrika Magharibi: *In ba kira, me ya ci gawai?* “Kama hakuna kitu kilichoundwa nini nimetokea kwa makaa?”

*Uhunzi bado unafanywa katika maeneo mengi ya Afrika Magharibi kwa kutumia moto wa mkaa. Lakini rasilimali hii muhimu imetumika na hakuna kilichotengenezwa, kuna sababu tu inayohusika.*

Ufanisi ni jambo la kuliangalia mara kwa mara. Kibeti, lugha ya Cameroon inaweka suala hili katika uwazi: *Fà è tɛ̀bɛ̀ nè̀bà̀i è̀ d̀ù̀gà̀n à̀ à̀bà̀m*: “Kama panga halitaki kukata kichaka ni bora ulirudishe kwenye ala.

“Ufanisi” siyo dhana ya kigeni. Misemo mingi ya kienyeji inadokeza tatizo la michakato ya kijamii inayotoa matokeo mabaya au bila ya matokeo yoyote. Hasara za kiutendaji ambapo uwiano wa pembejeo na mazao ni mdogo kwa kutumia istilahi ya wapanga mipango. Moja ya methali inayosifika inatoka lugha ya Wolof ya Senegali “Kumi wanachimba, kumi wanajaza vumbi jingi, lakini hakuna shimo.” Maoni hayahitajiki!

## Kufanya maamuzi ya pamoja

Kufanya tathmini ni njia moja ya kufanya maamuzi ya pamoja juu ya matumizi ya rasilimali na malengo sahihi ya maisha ya jumua. Tathmini shirikishi inalifanya lengo liwe linarudiwarudiwa mara kwa mara. Utamaduni wa Afrika Magharibi ni tajiri kwa busara kuhusu umuhimu wa ushirikiano katika kufanya maamuzi na njia za kuufikia. Lugha ya kihansa inaeleza suala hilo kwa mane-no machache:

*Shawara d'awakar d'aki* "kufanya maamuzi ni kama kuweka paa kwenye kibanda". Kwa kifupi kila mtu lazima ainame na kuinua kwa pamoja!

Msemo wa lugha ya Kiewe unatoa msisitizo juu ya suala hili na hususan umuhimu wa tathmini. *Nunya avemexevie ame ðeka me len o*. "Maarifa ni kama ndege na msitu: mtu mmoja pekee hawezi kumkamata."

Wakati huohuo, methali mara nyingi huweka wazi ukweli unaotofautiana, ni kitu muhimu katika kufanya uamuzi na kwamba hakuna kitu kinachokuwa na tafsiri moja tu. *Sira kelen sira tè*. Watu wa Malinke wanasema "Njia moja si njia kabisa".

Na lugha ya Kihansa ina namna mbili nzuri za kueleza diplomasia na uungwana ambao ujenzi wa maamuzi ya pamoja lazima ushughulikiwe: *Girma da arziki kan sa jan sad a abawa: Ni kutokana na kuheshimu na wema unaomfanya mtu aongoze ng'ombe dume akiwa na kipande cha kamba*.

*Makiyayen kwadi ya yi hankali da sandarshi!* "Mchungu kundi la chura anahitaji kuwa na subira!" Vyura haviendi kwa fimbo yake kwa kasi au vyote uelekeo mmoja bali vina ngozi laini na ni viumbe vinavyoweza kudhurika kwa urahisi na iwapo mchungaji anaviangalia akipata hasira na kuanza kuvichapa na fimbo yake ana uhakika wa kuvichakaza baadhi yake.

## Uchambuzi wa matendo jarabati na sababishi

Ushahidi mara nyingi si muhimu sana katika tamaduni za wenyeji wa Afrika Magharibi kuliko ilivyo katika utamaduni wa nchi za Magharibi za kisayansi, ingawaje haiwezi kuchukuliwa kwa namna moja mara zote. Ukweli ni kama Levi Strauss anavyoeleza katika kitabu chake *La science du concret* "Mila ni utamaduni uliofungamana zaidi kwenye data halisi" ya uzoefu kuliko ule wa kitaaluma. Vitendo vya wenyeji ni matokeo ya miaka mingi ya kuangalia, kubahatisha na majaribio.

Tendohisia hizi ni muhimu katika tathmini na zinaelezwa katika methali na misemo kadhaa katika kanda yote. Katika kupima, mbali na vitu vingine chaguo la sera na madai ya ubadhilifu yanayofanywa na wanasiasa ya mara

kwa mara, Wahansa wanatoa maoni kwa wepesi kabisa: *Ba a gardamar noma ga damana*: "Hakuna sababu ya kujadili stadi za kilimo wakati wa masika!" Kwa kifupi acha kila mtu atumie mbinu yake katika kulima shamba lake, na matokeo halisi tutayona muda si mrefu.

Msemo mashuhuri wa lugha ya Kiewe unasisitiza umuhimu wa kulinganisha taarifa katika madhari yote. "Mkulima ambaye hajapata kwenda zaidi ya shamba lake atasema mbinu zake ni bora zaidi" Usemi mwingine wa Kihansa unasisitiza hali ya mazingira ambayo inapaswa kufahamika ili kueleza mwenendo usiotarajiwa *Abin day a ka'da kusu wuta, ya hi wuta zahi*: "Kile kilichofanya panya kurukia moto ni lazima kiwe cha moto zaidi kuliko moto wenyewe".

Wakati huo huo uwiano wa maelezo yote ya vitendo hivyo na umuhimu wa kugawa tafsiri ikiwa ni pamoja na zile zilizowasilishwa vizuri, unaelezwa vizuri na methali nyingine kutoka Bara la Afrika, hii ni kutoka Zimbabwe "Hadithi za uwindaji zitakuwa vitendawili vya fahari mpaka siku wanyama watakapokuwa na wanahistoria wao!"

## Kujitawala na kujipima

Kujipima ni stadi muhimu katika kujitawala. Methali za Kiafrika zinatoa idadi kubwa ya utambuzi husiani. Msemo toka kabila la Morè la huko Burkina Faso unatumia taswira nzito kutukumbusha kuwa hatujawa huru bila zana na rasilimali zetu wenyewe: "Yule anayelalia mkeka wa kuazima atambue kuwa analala kwenye baridi, baridi ya chini".

Lugha ya Wolof inaizungumzia dhana hiyo tofauti kidogo lakini ikiwa na athari kidogo: *ku la abal I tãnk, nga deni fa ko neex*. "Azima miguu ya mtu na utaenda kule anakotaka yeye uende".

Lakini kuchukua usukani wa majaliwa ya mtu kunahitaji uwezo: *Barawon kakaki bay a da iko ya busa shi*, katika Kihansa wanasema "yule anayeiba tarumbeta la chifu hana nguvu za kulipiga". Na inahitaji uwezo na moyo wa kujituma ili kupima na kujisahihisha makosa. Katika lugha ya Kibambara wanasema *Sa kògòlen be dogo* "Nyoka aliyefichwa anakua na kuwa mkubwa. Hii ina maana makosa na udhaifu tusiorekebisha unakuwa mbaya zaidi. Na lugha ya Kihansa inaongezea *Ranar wanka ba a b'oyon cibiya*. "Katika siku ya kuoga hakuna sababu ya kuficha kitovu!"

### Lugha ya kuhamasisha utambuzi wa wenyeji

Matumizi ya methali za kienyeji katika tathmini yamesaidia mambo mawili: Kwanza inaweza kutoa mwanga mpya kwa mitukutiko ya kijamii inayoathiri utekelezaji wa programu, kama matone haya machache katika utamaduni wa wenyeji—ambapo mengi yake yanafanana na kutambuliwa na makabila mengi, na unaeleza ukweli unaohusu tabia ya mtu binafsi na tabia ya pamoja.

Zaidi ya umuhimu huo, methali na misemo inatoa njia ya kuonyesha kuwa tathmini na uwajibikaji na fikra kama hizo za kuongeza umuhimu wa ugatuaji na maendeleo ya wenyeji siyo vitu vigeni bali ni vipengee vya masuala husika ambayo ni ya zamani kama ulivyo

utamaduni wenyewe. Mtazamo huu unakuwa ndiyo msingi wa kusaidia wanufaika kuanzisha teknolojia ambayo inaendana na utamaduni wa kidemokrasia wa kujitawala na la muhimu zaidi ni wao wenyewe kuwa na madaraka.

Gyorgy Szell alisema kuwa kigawo cha kawaida cha kanuni za imani katika harakati za menejimenti shirikishi za maendeleo ya wakati huu ni fikra kuwa “mtaalamu wa kazi ya mfanyakazi hatimaye ni mfanyakazi mwenyewe” Methali ya Kihausa inaliweka wazo hilo tofauti kidogo lakini katika hali karibu sawa: *Kome yak e cikin aikin d’an tsako, shaho ya dade da saninsh*: “Kwa kila kihusucho tabia ya kifaranga [unaweza kuwa na uhakika kuwa] mwewe alianza kujifunza haya muda mrefu uliopita”.

# Maarifa Asilia na Haki za Amali za Kiakili

Makala hii imeandikwa na Siddhartha Prakash wa Kanda ya Afrika, Benki ya Dunia. Imetolewa kwa kifupi kwa ruhusa ya mchapishaji wa awali: "Towards a synergy between biodiversity and intellectual property rights" na S. Prakash, Septemba 1999, Jarida la World Intellectual Property, Juzuu 2 No. 5.

**Tini za MA 19  
Aprili 2000**

Biashara ya kimataifa katika rasilimali za kijenetiki mara nyingi hurejewa kama biashara ya bio ambayo ni kitegauchumi cha juu kwa hivi sasa. Mauzo ya dawa kwa kuzingatia dawa ya asili peke yake yanafikia zaidi ya dola za Marekani bilioni 32 (bilioni moja ni sawa na milioni 1000) kwa mwaka. Inakadiriwa kuwa kwa kushauriwana na wenyeji watafuta bio wanaweza kuongeza uwiano wa mafanikio katika majaribio toka sampuli moja kati ya 10,000 hadi moja kwa sampuli mbili. Uzoefu wa mtaalam mwingine unaonyesha kuwa maarifa asilia yanaongeza ufanisi wa kuchuja mimea yenye sifa za dawa kwa asilimia 400. Bila nyenzo za maarifa asilia dawa mengi muhimu yanayotumiwa sana leo yasingekuwapo

Kabla ya mwaka 1992 maarifa asilia na rasilimali yalionekana kama ni urithi wa kawaida wa binadamu. Hakukua na sheria za kimataifa (katika nchi nyingi) kuhusu upatikanaji wa rasilimali za kijenetiki. Matokeo yake kulikuwa na ongezeko la matumizi ya kibiashara ya maarifa na rasilimali za kibiojolojia za watu wa asili.

Kumalizika kwa rasilimali za kimazingira na haja ya kuwatunza watumiaji na watoaji kumesababisha kuanzishwa kwa mkataba wa Biolojia anuwai (Convention on Biological Diversity CBD) ambao kwa mara ya kwanza ulitambua thamani ya ma-

arifa asilia na rasilimali. Ulianzisha kiunzi kusaidia upatikaji wa rasilimali za kijenetiki na njia za halali na kugawana faida kwa usawa.

Miliki ya kitaaluma ni njia ya kupata umiliki wa rasilimali maalumu ambayo kwa asili yake haipimiki. Kwa kawaida inahusu kulinda aina fulani ya ugunduzi uliyovumbuliwa kwa akili za mwanadamu. Hii inajumuisha uvumbuzi wa aina mbalimbali toka muziki mpya, riwaya, dawa hadi programu za komputa na mazao yaliyopatikana kutokana na matumizi ya maarifa asilia.

CBD ulianzisha wazo la haki miliki kitaaluma kama mkakati wa kuhifadhi biolojia anuwai kwa kuzipa nchi haki ya kisheria juu ya rasilimali zao. Hii ilikamilishwa na Mkataba wa Biashara unaohusiana na haki miliki kitaaluma (Agreement on Trade-Related Intellectual Property Rights —TRIPS). Kuhusisha TRIPS katika mfumo mkuu wa WTO kulianzisha nidhamu mpya kwa nchi nyingi katika hatua za hakimiliki, viashiria vya kijiografia, alama za biashara na usanifu wa viwanda. Madhumuni makubwa ya mkataba ni kuanzisha viwango vya kimataifa kwa ulinzi wa chini wa haki miliki kitaaluma (Intellectual Property Right (IPR) protection).

## Haki ya amali za kiakili: mgogoro au nguvu ya pamoja?

Ulindaji wa maarifa asilia na rasilimali kwa kuanzisha IPRS kunakuza au kuzuia upelekaji wa faida sawa za kiuchumi kwa watunzaji? Wahakiki wanadai kuwa IPRS ni tishio kwa bioanuwai kwa kupunguza upatikanaji wa rasilimali na mazao yanayopatikana kutokana na rasilimali hizo. Kuna kuhimiza kampuni kuweka hataza kwa ugunduzi unaotokana na rasilimali na maarifa asilia bila kugawana sawa na jumua hizo faida ya kibiashara.

Watetezi wa TRIPS wanadai kuwa inahimiza uhawilishaji wa teknolojia ambao ungekuwa mkakati mmoja wa kugawana sawa manufaa yanayopatikana. Kuna pia masuala mengine yanayoibuka kwenye mjadala ambayo yatashughulikiwa na kulinganishwa kwa kuangalia mikakati ya kufanyia kazi katika mfumo wa IPR na kupanua wigo wake pale itapoonekana kuna umuhimu wa kuhifadhi maarifa asilia na bioanuwai.

## Matatizo ya utumikaji

Asili ya utofauti wa IPR mbalimbali unazua matatizo kadhaa inapotumiwa na jumua za wenyeji. Zinashindwa kuona kuwa jumua hizi zina mtazamo mpana kuhusu mazingira yao. Jumua hizo zinaona vigumu kutofautisha rasilimali kutoka riziki wanaoyopata hadi ubainishi wa kiuchumi na rasilimali za jamii.

Kwa jinsi IPR inavyohusika, hii inaleta tatizo lingine. Ni kwa namna gani mtu atatafsiri uvumbuzi na mfaidika katika jumua za wenyeji, kutokana na uhitaji wa kuwa upekee na usio wa kawaida. Katika jumua nyingi za asili maarifa yanapatikana baada ya muda na yanarithishwa toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Kupitia mchakato huu maarifa yanaendelea kuibuka na kujibadili. Kwa hiyo, ni vigumu kusema kwa uhakika wakati ambapo maarifa ya aina fulani ndipo yalipovumbuliwa na lini yaliingia kwenye miliki ya umma.

Kipengele cha pili cha mtanzuko unahusu kipengele cha maarifa asilia ya jumua. yaliyoanzishwa kwa kushirikiana kwa wanajumua kama vile wazee ambao wana busara zitokanazo na uzoefu wa miaka nenda rudi ambao unaongeza thamani zaidi ya maarifa. Kwa maana hii kila wakati yamekuwa katika miliki ya umma wa jumua na hivyo kushindwa kufikia kigezo cha kuwa sio maarifa ya kawaida. Wakati jumua yote inahusika na uibukaji wa maarifa asilia utawezaje kubainisha mgunduzi? Tatizo linakuwa la kutatanisha zaidi ambapo maarifa asilia yanayofanana yanatumiwa na jumua tofauti katika ulimwengu. Kwa mfano kama mtishamba fulani unatumiwa na Wamasai wa Kenya na wakati huo huo unatumiwa na Wahindi wa misitu ya Amazon ni kwa namna gani mtu atabainisha mgunduzi halali.

## Kuelekea katika nguvu ya pamoja

Mambo haya yanaweza kusuluhishwa kwa kufanyia kazi katika kiunzi cha TRIPS kwa kutumia aina mbalimbali za haki miliki kitaaluma. Hizi ni pamoja na viashiria vya kijiografia ambavyo vinatumika zaidi kwa ugunduzi wenye misingi ya kijumua. Uwezekano mwingine ni kupanua upeo wa IPRS kujumuisha wazo la Haki za Kijumua. Hii inaweza kujumuisha kundi la watu wa aina yake na kuwa na aina za ulindaji ambazo zinaweza kuwa bora zaidi kuliko hataza.

Baadhi wanashauri kuwa sheria za hataza zirekebishwe ili kuhakikisha kuwa matumizi yote ya hataza yanaonyesha nchi ya asili ya nyenzo za kibiojia na maarifa asilia yaliyotumika kupata uvumbuzi. Suala linalohusu ukatazaji wa matumizi ya uvumbuzi wa asili ni haja ya kuwa na nyaraka. Tatizo la mazoea ya asili ni kuwa yanarithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine kupitia masimulizi ya mdomo na siyo kumbukumbu za kimaandishi. Ili kuzuia maarifa ya jadi yaliyo tayari katika miliki ya umma yasiwekewe hataza kama uvumbuzi mpya katika nchi nyingine, ni lazima kuwa na nyaraka za kimaandishi ya desturi hizo. Kwa njia hii, jumua asilia zinaweza kupinga hataza zinazotolewa kwa wengine kwa desturi za kijadi ambazo ni za kwao. Kanzi ya maarifa asilia ya Benki ya Dunia na juhudi kama hizo zilizoanzishwa na WIPO za kusajili desturi za jadi ni juhudi zenye mwelekeo huu.

Zaidi ya hayo, uanzishwaji wa usajili wa maarifa ya jadi utasaidia kugawana faida kati ya viwanda na jumua za wenyeji. Hizo zinaweza kuunga mkono hatua zinazohusiana na IPR kama vile kuimarisha hadhi ya maarifa asilia kama sanaa tangulizi inayoweza machapisho ya kujilinda.

Mbali na hataza, kuna njia nyingine ambazo zinafaa ambazo ni kuanzisha hakimiliki kitaaluma juu ya maarifa asilia na rasilimali. Hii ni pamoja na matumizi ya viashiria vya kijiografia (majina ya mahali au neno linalohusiana na mahali ili kubainisha asili, aina na ubora wa zao. Kwa mfano "chai ya Darjeeling). Juhudi hizi ni za pekee katika kunufaisha mila za pamoja na wakati huo huo kuruhusu mabadiliko. Inasisitiza uhusiano kati ya tamaduni za binadamu na mazingira yao, na kuweza kutunzwa mradi tu mila za pamoja zinadumishwa. Hakuna tatizo iwapo mgunduzi ni mtu binafsi, familia au shirika kubwa. Jumua asilia zinadai maarifa yao yasinunuliwe au kuuzwa ovyo. Vivyo hivyo viashiria vya kijiografia vinakosa sifa asilia za miliki binafsi za kuweza kuhamishika kwa urahisi.

Aina mojawapo ya ulinzi ni kuwa na hakimiliki na siri za biashara. Hakimiliki mara nyingi inatumika kulinda amali za jadi zisidurufiwe bila idhini. WIPO imelinda

sanaa za jadi toka sehemu mbalimbali ulimwenguni kama hakimiliki. Siri za biashara ni njia ya kulinda taarifa za siri ambazo zinaweza kuzipa biashara nyingine faida katika ushindani. Siri za biashara zinaweza kuwa njia zifaazo kulinda maarifa asilia. Jumua za wenyeji zinaweza kuzuia uingaji katika maeneo yao na taarifa zao kwenda nje kupitia mikataba ambao ina usiri na manufaa kiuchumi. Hayo yamefanyika katika nchi kama Ecuador kwa masada wa Inter-American Development Bank.

### **Sui generis: Fursa na ugawanaji manufaa ya haki sawa**

Baadhi ya mambo yenye utata yanayozizunguka IPR mbalimbali inahusu ulinzi wa aina mbalimbali za spishii za mimea. Mkataba wa TRIPS unasema kuwa wanachama wanaweza kujitoka kutoka katika hataza.

*“Mimea na wanyama mbali na viumbe wadogo sana na hasa michakato ya kibiolojia ya kuzalisha mimea na wanyama mbali na michakato isiyo ya kibaiolojia na maikrobiolojia. Hata hivyo Wanachama watatoa ulinzi kwa aina za mimea kwa kutumia hataza au kwa kutumia mfumo wajumla ufaao au kwa kutumia mchanganyiko wowote”—(Ibara 27.3b).*

*Sui generis* inarejea kwenye mbinu za ulinzi mbali na matumizi ya hataza. Aina iliyozoeleka ya kinga ya sui generis kwa aina mpya za mimea inahusisha aina fulani ya haki za wazalisha mimea (plant breeders rights) katika kiwango cha kimataifa zipo nchi zilizoungana pamoja katika Umoja wa Kimataifa wa Ulinzi wa Aina Mpya za Mimea na zilifanya majadiliano ya mkataba wa Ulinzi wa Aina mpya za Mimea. Mkataba uliweka viwango vya chini vya kinga ambayo mifumo ya Kitaifa inaweza kukubaliana. Hii inawawesha wazalishaji kufaidi kile kinachoitwa “upendeleo kwa wazalishaji” unaowapa wazalishaji uhuru wa kutumia aina za mimea inayokingwa katika programu za uzalishaji ili kupata aina nyingine za mimea.

Aina kama hii ya ulinzi imefanya nchi hususani zinazoendelea ziwe na mambo ya kujiuliza, mengi ya hayo ni uvumi huo na msingi. Kuna woga, kwa mfano wakulima hawataweza tena kuruhusiwa kuendelea na kilimo chao cha jadi kutokana na kuwa na ulinzi wa aina ya hataza au sui generis unaotolewa kwa zao ambao wamelitumia kwa muda mrefu, woga huu si wa kweli.

Zao au mchakato uliotumiwa na umma sio mpya na hivyo hauwezi kuwekewa hataza. Ni aina mpya tu za mimea ndizo zitawekewa kinga na hata hivyo ni juu ya mzalishaji kutafuta kinga. Siyo lazima. Hivyo wakulima wanaweza kuhifadhi mbegu kutoka mavuno yao kwa ajili ya kupanda katika mashamba yao (hii imekuja kujulikana kama “upendeleo wa wakulima”).

*Sui generis* inatoa uwezekano wa kwenda zaidi ya aina za jadi za IPR na kuangalia mbinu nyingine za kurekebisha fursa ya kupata rasilimali na ugawanaji sawa wa faida. Hizi zinaweza kujumuisha mikataba kati ya watumiaji na walindaji wa rasilimali kama ule mikataba ya Uhawilishaji Nyenzo (Material Transfer Agreements). Kwa mfano, katika nchi ya Cameroon Taasisi ya Kanzaya Taifa ya Marekani ilitia sahihi mkataba na serikali kufuatia ugunduzi wa spishi za mmea wa msituni ambao una kemikali zinazoweza kupambana na UKIMWI. Cameroon inatoa sampuli za mimea kwa malipo ambayo yanatumiwa na jumua za asili katika miradi ya maendeleo ya kuhifadhi misitu.

Wengine wanadai kuwa mfumo sui generis ambao unaruhusu kufanya mabadiliko katika aina ya kinga inayotolewa unahitaji kupanuliwa zaidi kuingiza haki za jumua na haki za rasilimali za jadi. AZISE kama vile mtandao wa Nchi za Dunia ya Tatu (Third World Network) zinatea kuwa na utaratibu wa haki mbadala unaoakisi utamaduni na kuthamini mfumo wa jumua za wenyeji. Wanao dai kuwa tukizingatia hali ya mitukutiko ya maarifa asilia, dhana ya “uvumbuzi” inahitaji kufasiriwa upya zaidi ya kuwa tu uvumbuzi wa viwandani. Hili linaweza kuingizwa kwenye haki za jumua.

Wanataaluma wana mtazamo wa jumla ulio juu unaunganisha haki miliki, sheria za jadi na desturi. Wanao dai kuwa maarifa asilia hayawezi kutengwa kutoka haki za asili kama vile haki za binadamu, haki ya ardhi na kujitawala. Njia moja ya ufumbuzi ni mtazamo wa kuunganisha haki mbalimbali kwa kuanzisha haki za rasilimali za jadi ambazo zinaweza kutoa kiunzi cha kanuni zinazoshikiria haki za jumua za jadi. Hizi zinaweza kuwa mwongozo wa haki nyingine kama vile Haki Miliki ya sui generis.

### **Hitimisho**

Haki miliki kitaaluma inaweza kuwa mnjia sahihi ya kulinda mifumo ya maarifa asilia na aina mbalimbali za mimea. Matini hii inasisitiza umuhimu mkubwa wa kuweka katika maandishi maarifa asilia ambayo yanaweza kutumiwa badaye kupinga madai ya hataza za maarifa ambayo tayari yamo katika miliki ya umma. Pili, inadokeza manufaa ya aina nyingine za haki miliki za kitaaluma kuliko hataza kama vile viashiria vya kijiografia. Hizi zinaweza kuwa na manufaa zaidi kwa jumua asilia zinazohitaji kurekebisha upatikanaji rasilimali zao. Kama zitakavyotumiwa kwenye maarifa yanayoibuka baada ya muda na kuwa nyenzo za jumua ya wenyeji kwa ujumla. Hii inatoa nafasi ya kupanua mkataba wa TRIPS ili kuhakikisha kuwa hataza inaonyesha asili ya rasilimali za kijenetiki na matumizi ya maarifa asilia na kuichukulia sui generis kuwa aina ya miliki kitaaluma kama haki za jumua ili kuhakikisha ugawanaji sawa wa manufaa.



# Uvumbuzi Mpya wa Uanagenzi na Taratibu za Kuingia Utu Uzima

*Msingi wa makala hii ni utafiti uliofanywa na watafiti wenyeji kwa msaada na ushauri wa kiufundi wa Prof. Peter Easton wa Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida, wakishirikiana na baadhi ya jumuiya za Kiafrika. Utafiti ulifadhiliwa na Club du Sahel/OECD, CILSS na ADEA.*

***Tini za MA 20  
Juni 2000***

Jamii nyingi za kimapokeo katika Afrika Kusini mwa Sahara zina mifumo mizuri ya kuwaingiza vijana katika desturi, stadi na uelewa wa utu uzima. Mifumo hiyo hujumuisha vyama vya marika, unyago na jando, na uanagenzi katika stadi mbalimbali za uzalishaji mali.

Utaratibu wa kimapokeo kwa ajili ya uanagenzi na jando na unyago bado una mashiko katika jumuiya za vijiji ilihali unalegalega kwenye maeneo ya pembezoni mwa miji miongoni mwa watu ambao njaa, ukosefu wa ajira au mvuto wa maisha mazuri zaidi umewafanya wakimbilie mijini. Hapana shaka kuna mambo mbalimbali yanayounganisha maeneo haya mawili, na vyama vya wahamiaji kutoka vijiji na mikoa mbalimbali ni mambo ya kawaida mijini.

## **Kizazi Kilichoachwa Kifanye Kipendavyo**

Kwa ujumla, uhamiaji mijini kutoka vijijini umechangia katika kuvunja polepole uhusiano na nguvu za mila za jando na unyago na utaratibu wa uanagenzi tangu upatikane “uhuru wa bendera”. Mfano wa upeo wa uvunjaji wa desturi hizi za kuingia utu uzima pengine unaonyeshwa na hali ya watoto wa mitaani, wale vijana wasio na elimu, kazi na agha-

labu makazi ya kudumu ambao wanazurura katika barabara kuu na ndogo za miji ya Afrika.

Mashirika ya Umoja wa Mataifa na ‘NGO’ nyingi zinazoshughulikia suala hili huwachukulia watoto wa mitaani kama kikundi cha watoto wanaofanya kazi—yaani, watoto wadogo ambao hawajafikia umri rasmi wa kuajiriwa au hawajakomaa kijamii ambao wanafanya kazi katika mazingira yenye kuleta madhara katika makuzi na maendeleo yao. Watoto wengi katika jamii zinazoendelea, ni kweli, kuwa wanafanya kazi na wataendelea kufanya kazi.

Changamoto iliyo sahihi zaidi sio kukataza aina zote za kazi kwa watoto wenye umri mdogo, bali kuhakikisha kwamba watoto hawalazimishwi kufanya kazi zisizofaa na za hatari kwa sababu ya kuokoa maisha yao, na kwamba wapatiwe fursa nzuri za kuingia katika maisha ya utu uzima.

Lakini hali mbaya ya watoto wa mitaani inadokeza hali ya uchumi ilivyo pembezoni mwa miji, ambako ukosefu wa fursa za kijamii umewanyima vijana wakimbizi nafasi ya kukua utambulisho wa utu uzima. Miundo ya kimapokeo ya jamii si rahisi kujitokeza sasa. Kama methali ya Kihausa inayosema “In rawa ta sake, ki’di ita ma sai ta sake”: Mdundo wa ngoma unapobadilika, uchezaji wa ngoma pia hubadilika. Ipi ni mi-

dundo mipya ya maana katika mazingira ya sasa ya kiuchumi na kiutamaduni, na kadhalika hali iliyobadilika inayoitia changamoto midundo hiyo? Mifano mitatu kutoka Afrika na mmoja kutoka Caribbean inatoa mwangaza kwa kiasi fulani.

### **Kusimamisha wimbi la watoto wa mitaani: Chama cha Undugu cha Kenya**

Chama cha Undugu kilianzishwa kwa juhudi za padri mmoja wa Kiholanzi aliyehamia Nairobi mwaka 1972 baada ya uzoefu wa miaka 17 ya kuishi vijijini nchini Tanzania, ambako alianzisha huduma za kichungaji kwa vijana wa mijini. Vijana wachache waliziitikia programu zake za kidini, lakini aliona kwamba mitaa ya Nairobi ilifurika vijana wasio na ajira, hasa vijana “waegeshaji magari” ambao waliomba ujira kidogo kutoka kwa wenye magari kwa ajili ya kuyalinda na kuyaosha magari hayo katikati ya jiji la Nairobi lenye msongamano wa watu na vitu.

Mwaka 1973, padri alianza kutumia muda wake mwingi mitaani akijenga uhusiano mwema na watoto wa mitaani na kuzungumza nao kuhusu hali halisi ya maisha yao na juu ya matarajio yao. Aligundua kuwa wengi wao walikuwa wameacha shule za msingi na kuhama toka nyumbani kwao kwa sababu familia zao hazikuweza kuwalipia karo za shule na kuwanunulia sare na vifaa vinginevyo vya shule. Wengi wao, kama kiongozi mmoja wa Chama cha Undugu anavyoeleza, walipoulizwa wanahitaji nini, walijibu “Nataka kusoma”.

Kutokana na sababu hizi, awali padri aliamua kwamba jitihada za kuwasaidia watoto wa mitaani zielekezwe zaidi katika kuwarejesha shuleni, na akaanza kutafuta fedha za kulipia karo na vifaa vingine vya shule kwa vijana wengi kadiri ilivyowezekana. Hata hivyo, aligundua punde kuwa mara nyingi wakuu wa shule waliwakataa watoto hao au hawakutaka warejee kwenye shule zao za awali. Wakuu hao walihofu kuwa sababu zilezile zilizowafanya watoto hawa watoroke shule mara ya kwanza zinaweza zikajirudia; ama kutokana na tabia zilizojengwa huko mitaani, watoto hawa hawawezi kuendana na utaratibu wa kawaida wa shule.

### **Namna ya kujifunza**

Matatizo haya ya kwanza yalifuatiwa na mikakati mbalimbali ambayo hatimaye ilikiwezesha Chama cha Undugu kubuni mkabala wenye mafanikio zaidi uliokidhi hali ya vijana masikini wa Nairobi. Mkabala huo ulikuwa na hatua nne. Hatua ya kwanza ilikuwa mtandao wa “shule zisizo rasmi” zilizoenezwa katika makazi ya watu masikini ndani na pembezoni mwa jiji la Nairobi. Shule

hizi zililenga wavulana na wasichana wenye umri wa miaka 10—16 ambao walikuwa hawajaenda shule kabisa ama ambao walishindwa kuendelea na shule, na hivyo kuwa katika hatari ya kuwa watoto wa mitaani wafanyakazi, kama kweli walikuwa hawajawa hivyo tayari. Programu hii ilipangwa ichukue miaka mitatu, iwapatie washiriki elimu ya msingi (kusoma na kuandika) na stadi za kunusuru maisha, pia iwawezeshe kujithamini, na hali kadhalika iwawezeshe wale wanaohitaji kurudi kwenye utaratibu rasmi wa elimu au kujiunga na vyuo vya ufundi stadi.

Kurejea huku kwenye elimu rasmi au mafunzo ya ufundi stadi ndiyo ilikuwa hatua ya pili ya mkabala na ilichukua mwaka mmoja zaidi. Wale waliobaki kwenye programu hii—au wale waliorejea baada ya kumaliza shule rasmi—walipata nafasi ya kujaribu ujuzi wao katika kazi mashuhuri za ufundi za sekta ya uchumi isiyo rasmi za Nairobi: hususani ufundi seremala, ushonaji, ufundi magari na ufundi chuma. Kwa kazi zote hizi Chama cha Undugu kilikuwa na zana za kutosha za kufanyia kazi kwenye karakana yake.

### **Kutafuta nafasi katika jamii**

Hatua ya tatu ilijumuisha kipindi cha mpito kuelekea katika ajira na majukumu ya kiuchumi ya utu uzima. Vijana walioonyesha upendeleo wa kazi ya ufundi mahususi walisaidiwa kumpata fundi stadi katika sekta isiyo rasmi ambaye angewachukua kama wanagenzi kwa kipindi cha mwaka mmoja ili wapate mafunzo zaidi na uzoefu. Chama cha Undugu kilishiriki kama mwenzi katika mapatano haya na kikabuni vigezo vya kuteua mafundi stadi “wenyeji” na taratibu za ukaguzi wa mara kwa mara wa vifaa vya Chama ili kuhakikisha kuwa wanagenzi wanafundishwa na kwamba mazingira na masharti ya kazi si ya kinyonyaji. Wakati wa mwaka huu wa uanagenzi, vijana walirejea kwenye karakana za Makao Makuu ya Undugu kila juma ili “kuinua viwango vya stadi zao”. Mafunzo haya yalihusu hasa matumizi ya zana za kazi ambazo mafundi stadi wengi hawakuweza kuyafundisha, na wakati huo huo yalilenga kuwatayarisha vijana kufanya mitihani ya kwanza ya serikali ya ufundi stadi kwenye stadi walizochagua. Mitihani hii ilifanyika mwishoni mwa mwaka.

Kuwapatia nafasi za kazi wahitimu wa Undugu, au kuwawezesha kujiajiri wenyewe kwa faida kwenye sekta isiyo rasmi ndiyo ilikuwa hatua ya mwisho na ya nne. Kitengo cha Ushauri wa Kibiashara cha Undugu hutoa mafunzo ya kuanzisha miradi midogo midogo na mikopo kwa wahitimu wa programu ili kuwasaidia wajiimarisha

kwenye kazi zao. Chama vilevile kimeanzisha Idara ya Usanifu na uuzaji wa bidhaa na huduma zinazotolewa na sekta isiyo rasmi na hasa katika kazi za ufundi zinazosaidiwa na Undugu na zinazofanywa na mafundi stadi walio na wanagenzi wa Undugu. Wafanyakazi wa Kitengo cha Usanifu Viwanda huendesha warsha kwa mafundi stadi wa sekta isiyo rasmi wanaoshirikiana na Undugu juu ya usanifu na uuzaji wa mazao yao. Kwa kufanya hivyo huwatumia wanagenzi wa Undugu kama nyenzo ya kuboresha mazao yanayotolewa na sekta isiyo rasmi.

### Mikabala Mingine Mbalimbali

*Huduma ya Uchukuzi ya Watoto wa Mitaani mjini Khartoum.* Mikabala tofauti lakini unaohusiana (na ule wa Nairobi) umechukuliwa na shirika lisilo la kiserikali (NGO)—Shirika la Kimataifa la Watoto wa Mitaani (SKWM) linalofanya kazi Khartoum, Sudan (kwa lugha ya kiingereza shirika hili huitwa Street Kids International—SKI). Tatizo la jinsi ya kuwaingiza vijana hawa katika jamii ya mjini na uchumi wa mjini liliwafanya watumishi wa shirika pamoja na vijana wenyewe kutafakari juu ya “unafuu wa kiuchumi” walionao watoto wa mitaani katika soko la mjini. Moja ya stadi zao ni kwamba wanaifahamu vema mitaa—yaani, barabara kuu na ndogo za jiji unganifu la Khartoum, na pia wanaweza kufanya kazi kwa ufanisi katika mazingira ambayo yangewatisha watu wengine. Watumishi na watoto wa mitaani walizingatia ukweli huu dhidi ya kile wachumi wanachokiita sasa “mambo magumu” katika uchumi wa mjini, na hususani ugumu wa kusafirisha vifurushi na vifaa vinginevyo kutoka sehemu moja hadi nyingine ya jiji la Khartoum lenye msongamano wa magari. Ndipo wakaja na wazo la kuanzisha Huduma ya Uchukuzi ya Watoto wa Mitaani.

Mpango huu ulijumuisha mambo yafuatayo:

- Kukopa baskeli kwa wachukuzi, ambapo baadaye kila mtoto angelipia mkopo huo kutokana na ujira wake wa kazi.
- Kuwafunza watoto taratibu za uchukuzi na hatua za usalama.
- Kuwasaidia kuanzisha mpangilio mzuri wa ufanyaji kazi na utunzaji wa mahesabu utakaoufanya mradi utekelezeke.

Kwa hakika mradi ulikuwa na mafanikio ya kutosha; na mfano wake uliigwa na Shirika la Kimataifa la Watoto wa Mitaani la Bangalore, nchini India, miaka michache baadaye.

Chama cha Mafundi Stadi cha Senegali (ENDA/GRAF). Programu zilizosaidiwa na ENDA (Environment and Development = Mazingira na Maendeleo) katika jiji la Dakar, Senegali, zilianza, kwa namna fulani, kinyume na utaratibu. Watumishi wa ENDA walikuwa wakiwasaidia mafundi stadi wa sekta isiyo rasmi—katika ufundi seremala, utengenezaji vinywaji—kuunda vyama vyao ili kuinua teknolojia yao na kutatua matatizo yao ya ugavi na soko. Hata hivyo, kila shughuli ilianza baada ya kufanya “upelelezi” wa kutosha wa mazingira halisi. Ni utaratibu wa ENDA, na hasa wa kitengo chake cha utafiti (*Groupe recherche—action—formation—GRAF*), kutumia utafiti unaowashirikisha wanufaikaji kama msingi wa kazi zote za maendeleo katika makazi ya watu masikini ya mjini. Moja ya mambo muhimu waliloliona mafundi stadi kutokana na utafiti huu ni hali ya vijana wengi walioacha shule na kuzurura mjini.

Kutokana na hali hii, vyama viliamua kuanzisha mfumo wake wa uanagenzi ili kuwawezesha vijana wajuane katika sehemu zao za kazi na waingie vizuri kwenye maisha ya utu uzima. Ushirika wa maseremala ndio ulikuwa msitari wa mbele kabisa katika suala hili na ulibuni mfumo wa kuwazungusha vijana walioacha shule na kuchukuliwa kama wanagenzi wa Ushirika kwa mafundi stadi mbalimbali ambako walijifunza stadi za kazi tofautitofauti, na kisha—kwa msaada wa ENDA/GRAF—wakafundishwa pia utunzaji fedha na uongozi wa miradi midogomidogo.

*SERVOL nchini Trinidad.* Mfano wa mwisho unachukuliwa mahali palipo mbali kabisa na bara la Afrika, lakini panafungamana na bara hilo kwa njia nyingi za kihistoria na kiutamaduni: yaani kisiwa cha Trinidad huko West Indies. Matatizo ya mpito wa vijana kuelekea ukubwani katika mazingira ya mjini ni makubwa kama vile ilivyoonekana kwenye mifano mitatu tulioijadili hivi punde—na kwa namna fulani, chanzo cha programu mashuhuri inayoshughulikia matatizo hayo, SERVOL (Service Volunteered for All—Huduma Inayoletwa Bure kwa Wote) kimefanana pia. Kama Chama cha Undugu, SERVOL ilianzishwa na padri wa Kikatoliki aliyechukizwa na hali duni ya vijana mjini. Kama Undugu, SERVOL kimekuwa chama ambacho sio tu kinatoa ajira bali pia hutoa njia mbadala za vijana kufahamiana wanapoingia katika maisha ya utu uzima. Miongoni mwa njia hizo ni “Vituo vya Maisha” vya SERVOL.

Kama jina linavyoashiria, Vituo vya Maisha ni zaidi ya kuwa fursa za kufunzia ufundi stadi. Kwanza kabisa vituo hivi hujengwa na vijana wakubwa ili kupata majengo ya karakana, madarasa na huduma nyingine za kijumuiya. Pia kila kituo hutumika kama kituo cha chekechea, na washiriki wote hupangiwa majukumu ya

kuwaangalia watoto wadogo au chekechea hao. Kisha mkazo pia huwekewa ushauri nasaha wa marika na kutoa fursa kwa vijana kueleza matatizo yao ya kijamii na yanayotokana na jazba za ujana huku wakizingatia maadili ya dini kuu tatu za kisiwani mwao: Ukristo, Uislamu na Uhindu. Vijana hushiriki katika kuandaa mtaala wao maalum unaojumuisha uelewa wa kiroho, kimwili, kiakili, kiutamaduni na kimhemko. Kutoka hapo, washiriki huweza kuingia kwenye vyuo vya ufundi stadi na kuajiriwa au kuwa na sifa za kupatiwa mikopo midogo ya kuanzishia miradi yao binafsi. Kiwango cha vijana wanaoshindwa kuendelea na programu hii ni asilimia 5 tu, ambapo kiwango cha kuajiriwa au kujijiri baada ya kufuzu mafunzo ya stadi mbalimbali ni asilimia 75.

### **Viambato muhimu: ajira, maana na kujiongoza**

Mifano yote hii inawakilisha juhudi za kujaza pengo katika kuwatayarisha vijana wanagenzi masikini waliopoteza utamaduni wao wa kimapokeo na kutupwa kwenye hekaheka za majiji ya Afrika ili waweze kumudu vema majukumu yao ya kiutu uzima. Na mifano hii inaelekea kufaulu vizuri pale inapoyafufua upya mapokeo hayo, huku ikichanganya taratibu za kimapokeo za uanagenzi na za vyama vya marika na mwelekeo mpya wa kiuchumi na kujiongoza na kujitathimini zaidi kwa washiriki.

Mafundisho mengine machache yanajitokeza kutokana na juhudi za kuwasaidia vijana masikini wa Afrika kujenga utambulisho mpya:

- Mkabala wa “elimu ya watu wazima” hufanikiwa vizuri iwapo utajengwa juu ya uzoefu na stadi walizonazo tayari vijana na kuwapatia nafasi ya kuchangia kutoa maamuzi ya kuendesha programu husika.
- Ajira yenye faida ni msingi wa utambulisho mpya, lakini sio wa mshikamano. Mshikamano huletwa na kuwepo kwa mpango wa maendeleo wa muda mrefu mbele—uwe wa kidini, kiutamaduni ama kisiasa—na fursa ya kuutumia katika maisha ya mtu binafsi. Hivyo ushauri nasaha wa marika mara nyingi ni jambo muhimu la kufanikisha programu.
- Namna za kimapokeo za uanagenzi na vyama vya vijana zafaa zitumike kama rasilimali za kusonga mbele kimaendeleo, pia lazima zihakikiwe. Programu za namna hiyo huwa kama uwanja wa majaribio kwa tamaduni nyingi za jirani.
- Utambuzi wa mazingira yanayomzunguka mtu—na haja ya kuyabadili—ni vijalizo muhimu vya juhudi zozote zile.

# Maarifa Asilia kwa ajili ya Maendeleo

*Uzoefu wa Miaka Miwili*

*Matini hii ya maarifa asilia imeandikwa na Siddhartha Prakash wa Kanda ya Afrika, Benki ya Dunia.*

***Tini za MA 21  
Juni 2000***

Maarifa kama chombo cha maendeleo hakitumiki kikamilifu. Zamani nchi nyingi za Afrika zilifuata sera za uchumi zikiwa na mtazamo wa kubadili jamii kuwa ya kisasa na kufanya mabadiliko katika sekta ya uzalishaji. Maarifa asilia ambayo yangesaidia mchakato huu, au kwa mahali pengine, kutoa mtazamo mbadala, mara nyingi yalidharauliwa na kuonekana ni ya kiwango cha chini. Hata hivyo mkutano wa Ardhi wa mwaka 1992 uliofanyika Rio kupitia wazo la maendeleo endelevu ilitumia mazoea hayo na kuyaweka mbele katika kuelezea maendeleo. Watunga sera kote ulimwenguni kupitia mikutano na warsha wameanza kudokeza jukumu muhimu la maarifa asilia katika mchakato wa maendeleo. Moja ya mikutano hiyo ni Mkutano wa Dunia wa Maarifa (Global Knowledge Conference) uliofanyika Toronto mwezi Juni 1997.

Chini ya msaada wa Ubia wa Habari na Mawasiliano ya Teknolojia kwa Afrika, (Partnership for Information and Technology for Africa—PICTA) Beni ya Dunia ilihimiza kuongoza maarifa asilia kwa juhudi za maendeleo kwa kushirikiana na mashirika mengine kama vile UNESCO, ITU na WIPO. Juhudi hizo zinalenga kuwezesha mazungumzo kufanyika kati ya jumuiya asilia mbalimbali, AZISE, serikali mbalimbali, wana-

nchi na sekta binafsi. Madhumuni ni kuingiza maarifa asilia kwenye shughuli za maendeleo na kutumia kwa manufaa misaada ya maendeleo hususani inayoelekezwa kwa maskini.

Benki ilichukua kiunzi kwa utendaji ambao unatekelezwa kwa ushirikiano na mashirika wabia. Miaka miwili tangu kuanzishwa, ni wakati wa kuhakiki juhudi za Benki katika kufanikisha malengo hayo. Je desturi za maendeleo ya maarifa asilia zimefanikiwa katika kusambaza habari, kuwezesha ubadilishanaji wa habari kati ya jumuiya zinazoendelea, zimewezesha matumizi ya maarifa asilia katika mchakato wa maendeleo au uanzishaji wa ubia?

## **Usambazaji habari**

Tangu hifadhi data ya maarifa asilia na mazoea kwa zaidi ya chunguzi kifani 100 zipo kwenye Webu. Kila moja inachota kutoka mafunzo toka uzoefu wa jumuiya maalumu katika kushughulikia kipengele kimoja cha maendeleo. Chunguzi kifani hazikuwa na maana ghala ya maarifa bali hifadhi data ya kurejewa juu ya maarifa asili. Inajumuisha vitendo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mazoea asilia kuhusu fedha kati ya jumuiya za wakulima katika Nigeria, uziujaji wa UKIMWI kwa kuwahusi-

sha waganga wa jadi katika kampeni za uelewa, kurejesha usanifu majengo wa wenyeji katika Misri, menejiment ya rasilimali maji katika Burkina Faso, na uponyaji wa asili wa watoto walioathiriwa na vita sehemu mbalimbali za Afrika.

Ukubwa na uchangamano wa masomo ambayo yana-weza kushughulikiwa ipasavyo kwa kutumia maarifa asilia na mazoea yameandikwa katika mfululizo wa Tini za maarifa asilia. Tini hizi zimechapishwa kwa njia ya elektroniki na pia katika maandishi katika lugha tatu na kuwafikia zaidi ya wasomaji 20,000. Kila moja ya Tini 19 za maarifa asilia hadi sasa zimetalii kwa undani fulani masuala nyeti kama vile tohara kwa wanawake na kuelezea ufumbuzi unaotokana na wenyewe, kutoka juhudi za wanawake asilia, AZISE ambazo zimefanya kampeni zenye mafanikio dhidi ya vitendo hivyo hadi kushawishi serikali kutunga sheria mpya. Kila mfano unaimarisha mafanikio ya matazamo wa maendeleo wa chini—juu. Sehemu ambazo mashirika ya Kimataifa yamesaidia kama UNICEF yametoa tu msaada zaidi kupitia msaada wa kifedha na kutambuliwa kimataifa. Katika kila mfano, kila mara juhudi zimekuzwa nyumbani na kumilikiwa na wenyeji. Suala hili limeimarisha taasisi za wenyeji na zimepelekea kupunguza kazi katika maeneo ya elimu na kisomo cha korani katika Afrika Magharibi.

Tini za maarifa asilia zimeonyesha kuwa watu binafsi bila elimu yoyote rasmi toka vijijini wakiwa na rasilimali kidogo wanaweza kuboresha maisha yao na mazingira kupitia programu imara zikisaidia kufikia uhuru zaidi na kujitosheleza. Hadithi hizi za mafanikio zinathibitisha jinsi maarifa asilia yalivyo ya kiulimwengu, maarifa hayo yanaweza kusaidia kutoa mchakato wa kuzipa uwezo jumua za wenyeji katika kiwango cha kanda, taifa na ulimwengu mzima.

### Kuwezesha mabadilishano

Benki ya Dunia imesaidia vituo vinane vya rasilimali ya maarifa asilia katika Afrika kwa kuboresha uwezo wake wa kubadilushana habari. Hii imetendeka katika aina mbalimbali. Katika Cameroon, Tanzania, Ethiopia na Zimbabwe mradi uliwezesha kupatikana kwa maarifa asilia kwa kupitia kutafiti chechemua za mazoea ya maarifa asilia kutokana na vituo vya wenyeji. Katika nchi za Burkina Faso na Uganda mradi uliboresha uwezo wa uunganishwaji wa mtando wa mawasiliano ya simu. Matokeo yake vituo vya simu (Telecenters) vinatumika kupata habari kutoka jumua za wenyeji na kusambaza maarifa yaliyopatikana kwenye mikoa mingine.

**Desturi za MA Namba:** 12

**Nchi:** Nigeria

**Miliki:** Fedha za Vijijini

**Teknolojia:** Akiba na mikopo

**Utumizi:** Desturi asilia za kifedha kati ya jumua za wakulima.

**Ufupisho:** Jumua za wakulima katika Nigeria zimeanzisha mifumo mbalimbali ya kuweka akiba na kukopa. Kwa kawaida wakulima huanzisha chama cha akiba kikiwa na msisitizo wa kuweka akiba na kupata rasilimali katika misingi ya mzunguko. Baadhi ya vyama hutengeza kanuni na sheria ndogo ndogo. Vyama vingi vina kanuni na taratibu kali rasmi lakini hazikuandikwa. Mtu anaingia uanachama, kwa misingi ya wakati maalumu unaofahamika hususani wakati wa siku za soko, mikopo inatumiwa kwa mahitaji yasiyo ya chakula lakini pia kwa kulipia ada ya shule au kazi za shamba. Kurudisha mkopo kunadhibitiwa na jamii. Kwa kawaida wanachama hawapati faida kwa fedha zao walizoweka, mikopo inatolewa kwa masharti nafuu. Hakuna mahali panapotaja namna ya kuwashughulikia wakiukaji. Inachukuliwa kuwa udhibiti wa jamii unatosha kuhakikisha vyama vya akiba na mikopo vinaendelea. Hata hivyo kiwango cha kuweka ni kidogo kwa limbikizo au kwa mkopo kwa ajili ya uwekezaji mkubwa. Mpaka sasa kuna kutambuliwa kidogo sana na asasi rasmi za mikopo zile desturi za asilia ya fedha.

**Somo:** Vyama vya asili vya kuweka na kukopa vilivyopo vijijini bado havijitambuliwa na sekta rasmi ya mikopo. Ushirikiano kwa misingi wa usawa unaweza kuongeza athari za asasi rasmi na kuongeza uwezekano wa uwekezaji katika maeneo ya vijijini.

**Chanzo:** Nweze, N.J. Msimamizi wa 2 (2) Agosti 1994.

**Kiungo wa Nje:** Msimamizi wa MA

### Kutumia maarifa asilia

Moja ya mafanikio makubwa ya juhudi za maarifa asilia ni kufanikiwa katika kutumia maarifa asilia katika programu za maendeleo na miradi mbalimbali. Iliisaidia Uganda katika kutayarisha sera ya Taifa ya Maarifa asilia. Pia ilisaidia Ghana katika matumizi ya maarifa asilia kuboresha kilimo. Imesaidia Burkina Faso kudokeza jukumu la wawindaji wa jadi katika kusimamia rasilimali za asili.

Julai, 1999 Benki ya Dunia ilianzisha utafiti kwa kushirikiana na UNCST kutafiti upana wa maarifa asilia nchini Uganda kilimo, sanyansi ya afya na teknolojia. Huu ukawa msingi wa mkakati wa kitaifa ambao ulingejumuisha wadau wote, toka waganga wa jadi hadi wananchi na watunga sera.

Miezi sita baadaye, warsha ya Taifa iliyowahusisha watu muhimu ilifanyika na kuandaa mswada wa mkakati wa Kitaifa na kiunzi cha utekelezaji. Huu ukawa mwanzo wa Azimio la Kampala kuhusu maarifa asilia kwa maendeleo endelevu. Azimio linadai serikali kusaidia maendeleo ya maarifa asilia na wapanga mipango kuingiza maarifa asilia katika mchakato wa mipango Kitaifa. Hili linatekelezwa kwa njia nyingi kama vile kuingiza maarifa asilia katika kiunzi cha maendeleo

makubwa ya Uganda (Comprehensive Development Framework—CDF) inayoongozwa na Wizara ya Mipango. Huu ni ubia wa pamoja kati ya wahisani na serikali mbalimbali zenye lengo la kuchapuzwa hatua za maendeleo katika Afrika. Huko Uganda moja ya malengo ni kuinua tija katika kilimo. Juhudi za maarifa asilia zimechangia katika jukumu la kuwezesha uanzishaji wa kamati ya utendaji za kusimamia mchakato wa utekelezaji na sekretarieti ya kuratibu shughuli hususani zinazohusiana na maarifa asilia.

Juhudi za maarifa asilia zinasogea toka utungaji wa sera kwenda kwenye usimamiaji wa miradi. Zimeanza kutoa ushauri kwa shirika la Taifa la utafiti wa kilimo la Uganda. (National Agricultural Research Organization—NARO) juu ya matumizi ya maarifa asilia katika kilimo kinachosaidiwa na Benki, miradi ya utafiti na mafunzo, Awamu ya pili ya mradi unaoendelea kwa utafiti na mafunzo umekusudia kusaidia mradi wa muda mrefu wa kuendeleza teknolojia na kuisambaza. Jukumu la uanzishaji wa maarifa asilia ni kutoa nyenzo za kimbinu ili kuhawilisha teknolojia husika na maarifa asilia na mazoea ya kilimo yaliyoboreshwa kwenda kwenye mashamba ya wakulima na kuinua matumizi yake. Mfano wa mazoea ni pamoja na kuboresha usimamizi wa kilimo cha matoke ili kupunguza madhara ya ugonjwa ya sigatoka na pembejeo za mashamba madogo yaliyotengezwa kwa ng'ombe asili wadogo wa Uganda kama vile plau lililoboreshwa la Uganda. Ingawaje mradi upo katika hatua zake za mwanzo, inatarajiwa kuwa mafanikio yake yanaweza kutumiwa na wengi na kurudufu matumizi ya maarifa asilia katika uanzishaji wa miradi mipya.

### Uanzishaji ubia

Mradi umepanua uwezo wake wa misaada kwa kuanzisha ubia wa karibu na mashirika kadhaa ya maendeleo,

AZISE na vituo vya maarifa asilia. Asilimia zaidi ya 75 za desturi nzuri zilizosambazwa kwenye Webu zilitolewa na wabia hao. Juhudi hizi zinaendelea kukua hata kufikia wasio wanachama wa PICTA. Kwa mfano imeanza kufanya kazi na WIPO kushughulikia kipengele cha maarifa asilia cha haki miliki kitaaluma. Katika ngazi ya chini, juhudi zimeanza kuhusisha jumuiia za wenyeji na kujifunza kutokana na uzoefu wao. Kwa kuzisaidia AZISE na asasi kama UNCST, Benki imetekeleza jukumu muhimu la kuwezesha kuwaleta pamoja waganga wa jadi, wanataaluma, mawaziri, wananchi na kanisa. Matokeo yake mashirika asilia kama vyama vya wataalamu wa jadi wa mitishamba vinaweza kufanya mazungumzo ya pande mbili na asasi za serikali juu ya kiwango cha uwanja wa shughuli. Kwa kuanzisha njia kwa jumuiia za wenyeji kutoa dukuduku lao katika ngazi ya kanda na ngazi ya kimataifa, mradi umepiga hatua muhimu kuelekea kutumia maarifa asilia kwenye mchakato wa maendeleo katika Afrika.

### Hatua zinazofuata

Changamoto ya mbele ni pamoja na:

- Kuimarisha juhudi za kuelekeza maarifa asilia kwenye mchakato wa maendeleo.
- Wafadhili kujihusisha zaidi na kushiriki kikamilifu.
- Kuwezesha mabadilishano kwa kuanzisha jumuiia za vitendo (kwa kupitia mabaraza mbalimbali—kwa mfano kuanzisha soko.
- Kuanzisha ushirikiano wa wenyeji katika mada zinazohusiana kama IPR kusaidia uwezeshaji na kupata uwezo.

# MA Yaingizwa Shuleni

*Matarajio na Hofu Zinazoikabili Elimu ya Jumuiia huko Saheli ya Magharibi*

*Makala hii imeandikwa kwa pamoja na Peter Easton (Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida), Chris Capacci (Shule ya Jumuiia/Kolondièba, Mali) na Lamine Kane (ANAF/Senegali) Utafiti ulifanywa chini ya usimamizi wa Klabu ya Saheli/OECD Kamati ya majimbo ya kupambana na ukame katika Sahel na Chama cha Maendeleo ya Elimu katika Afrika.*

## **Tini za MA 22 Julai 2000**

Ili maarifa asilia yaweze kuwa na umuhimu mkubwa hapo baadaye kwenye jamii ya Afrika Magharibi, ni lazima yapate nafasi mashuleni, asasi za kijamii zinazoshughulikia rasmi mafunzo, kuthibitisha maarifa na kutoa mafunzo kwa kizazi kifuatacho cha raia. Na bado katika kanda yote elimu ndiyo sekta ambayo haijapokea maarifa ya wenyeji au kuona kuwa sayansi asilia ni chanzo halali cha msukumo. Tofauti kidogo inaonekana katika elimu isiyo rasmi na programu za kisomo ambazo mara nyingi zimeendeshwa kwa lugha za kiafrika na kulenga mahitaji ya wanajumuiia wenyeji.

### **Njia mpya za kupata elimu**

Mabadiliko yaliyoendelea kutokea kote Afrika Magharibi katika elimu ya msingi rasmi kwa miaka ishirini sasa, yameanza kuvunja ukuta uliotenganisha elimu na jamii ya wenyeji. Wakati huo huo kuanzisha nafasi kwa ajili ya mtaala mpya. Mifano mikuu:

- Elimu ya msingi kwa wote ndiyo lengo lisiloepukika. Kwa kupunguza rasilimali zinazotolewa kwa ajili ya elimu na kusitisha ajira katika sekta ya umma, sera ya kurekebi-sha uchumi zinazotumiwa katika nchi za Afrika Magharibi tangu

miaka 1980 imetia doa motisha ya shule na uwezo wa serikali wa toa elimu. Uwiano wa uandikishaji katika kiwango cha shule za msingi ambao ulikuwa asilimia 30 kwa nchi za Sahel mwaka 1980 umeongezeka kidogo sana katika miongo iliyofuata. Mali ilikua na ukuaji hasi (asilimia -3), Niger ikawa na asilimia 4, na kati ya asilimia 1 na 2 kwa mwaka katika nchi ya Burkina Faso, Mauritania na Senegali. Katika maeneo ya vijijini uandikishaji ulikuwa mdogo zaidi.

- Serikali zimeanza kuangalia fomula mbadala na mbinu za ugavi ili kubadilisha mwelekeo wa uandikishaji, kufanikiwa katika kuenea na kuongeza umuhimu. Hii ni pamoja na kuwa na shule za jumuiia, kuongeza msaada kwa elimu isiyo rasmi, na program majaribio mba-limbali.
- Elimu rasmi ya jadi inategemea kuongezeka kwa mashindano ya kiutamaduni na tahakiki toka modeli nyingine: baadhi zimejikita kwenye “maendeleo yafaayo”. Zingine kwenye “mafundisho ya dini, mitazamo ya elimu ya watu wazima, au mtaala unaotumia lugha za Kiafrika. Mageuzi ya shule za msingi na sekondari ni suala lililomo karibu katika kila ajenda.
- Wananchi wana jukumu la kuimarisha ugavi katika elimu. AZISE,



mifuko binafsi na vyama vya wenyeji vinahimzwa kuanzisha shule zao wenyewe. Serikali zinapunguza kwa kiasi kikubwa haki ya ukiritimba katika eneo la elimu ingawaje ina kazi muhimu za udhibiti.

- Mfumo wa elimu rasmi wenyewe unagatuliwa kwa kiwango kisichozoeleka na uwezo wa maamuzi ukiwa katika mikono ya wakaguzi wa mikoa na halmashauri za Elimu za wenyeji. Ni katika utawanyaji huu na kutafuta utambulisho wa kitamaduni ndiyo umefungua mlango, hata hivyo kwa kusita katika kuruhusu mtaala mpya na vyanzo vipya vya msukumo na umeanzisha fursa mpya ya kutambua maarifa asilia.

### Historia ya majaribio

Kwa namna fulani kutafuta aina mbadala wa kupata elimu siyo suala jipya katika Afrika Magharibi. Ukweli ni kuwa fikra ya “Mtaala asilia” limejikita toka wakati wa ukononi, wakati istilahi kama hizi zilikuwa maneno msimbo ya kutofautisha aina ya elimu iliyochukuliwa kuwa inafaa vijijini au “wenyeji” tofauti na elimu iliyotolewa kwa watu wa mijini wasomi. Madai yaliyokidhiri ya elimu ya shule, au matatizo yaliyokuwapo yalisababisha kukawa na modeli mbalimbali katika kutoa elimu baada ya uhuru wa nchi za Afrika. Mfano mzuri ni ule wa Harambee huko Kenya. Shule zilianzishwa na jumua bila msaada wa serikali, ingawaje baadaye nyingi zilichukuliwa na serikali. Mfano wa Bregedi za Serowe huko Botswana na “*Enseigne ment moyen pratique*” za Senegali inafafanua zaidi mfano uliotangulia. Hiyo ilikuwa jitahida ya kufanya mtaala uhusike na maendeleo ya wenyeji kwa kuchukua teknolojia, mafunzo yafaayo ya uzoefu wa biashara kwa vitendo na rejea za kitamaduni za wenyeji.

Kuna tofauti chache muhimu za kitakwimu na kiubora kati ya uzoefu mbalimbali katika shule mbadala au ufadhili wa wenyeji uliozinduliwa mwanzoni mwa miongo ya uhuru katika Afrika Magharibi na hali inayoonekana sasa. Kitakwimu, mbadala na shule zinazomilikiwa na jumua umekuwa kwa mara ya kwanza cheche muhimu ya mfumo wa taifa kwa ujumla wake katika nchi kadhaa kama Mali, Senegali na Burkina Faso. Juhudi kama hizo awali zilikuwa “miradi wa majaribio” iliyokusudiwa, inavyoelekea, kutopanuliwa zaidi ya maeneo yaliyochaguliwa.

Hata hivyo zimejitana zaidi ya zilivyoziwa na kuongezeka. Katika nchi ya Mali zilifikia karibu robo ya shule zote za msingi. Katika nchi ya Senegali zinatarajiwa kufikia asilimia 20 katika miaka michache ijayo. Kiubora, elimu mbadala si tena ni ya daraja la pili, ingawa masuala

ya usawa wa vyeti vya zamani na taratibu za kupanda (zinajadiliwa chini) zimeendelea kuwa kali.

Kuongezeka kwa uhalali wa kufundisha kwa lugha za Kiafrika, taratibu umehamisha uwezo kuelekea wataandaji wenyeji chini ya utaratibu wa ugatuaji na mabadiliko ya matarajio ya ajira ya wahitimu wa shule, yote hayo yamemomonyoa mamlaka ya mtaala mmoja sanifu toka Magharibi na kufungua njia kwa mitazamo mengine. Utafutaji wa mbadala umekuwa wa aina tofauti. Zipo shule za jumua zinazofadhiliwa na serikali. Zipo shule za jumua zinazofadhiliwa na AZISE; shule za majaribio zinazofadhiliwa na serikali au shule za mageuzi (kwa ujumla shule za msingi za zamani zilichaguliwa kutumia mbinu mpya za elimu ya jumua katika mfumo wa elimu rasmi. Ari ya elimu ya Korani iliongezeka au aina ya mfumo chotara yaani mchanganyiko wa Kiislamu na Kimagharibi, shule binafsi au shule za pakashume zilianzishwa na watu binafsi au wajasiriamali, hususani katika maeneo ya mjini.

### Modeli ya kuhusisha Jumua

Katika eneo la Sahel na pengine katika bara la Afrika, shule za jumua zinajikita katika fikra ya uhusika mkubwa wa wazazi na jumua katika kutawala na kutoa elimu. “Umiliki” wa wenyeji wa shule unajengwa na kuelezwa kwa njia kadhaa:

- *Ushiriki kifedha*: Michango ya majengo na zana za madarasa, gharama za uendeshaji wa shule na mishahara ya walimu.
- *Ushiriki kiutawala*: Kujihusisha katika kufanya maamuzi yanayohusu utawala wa shule na taratibu.
- *Ushiriki kimtaala*: Kuna kuongezeka kwa wajibu wa wazazi na wanajumua katika kuchagua na kubainisha mtaala, katika kufundisha madarasa na kupima mafunzo waliyopata.

Ushiriki katika mtaala unajionyesha katika nyenzo mbalimbali za jumua zenye uhusiano mkubwa katika kuingiza maarifa asilia katika elimu mashuleni. Hata hivyo, ushiriki kifedha na kiutawala unaweza kuwa muhimu ili kufanya ufanye kazi. Baadhi ya hatua zilizopendekezwa za kuufanikisha katika shule za jumua zinazohifadhiwa toka nje ni kutumia lugha za wenyeji kutolea elimu; kuwatumia wasanifu wenyeji kama wafundishaji, hii inaweza kuwa kwa kufundisha masomo au ziara za wanafunzi mahali wanapofanyia kazi, kuweka kumbukumbu na kufundisha historia ya mahali pale pamoja na masomo mengine; na pia kuongeza masomo ya dini yatokanayo mahali hapo au elimu ya uadilifu.

Zaidi ya hayo, baadhi ya AZISE na asasi za wananchi zinazojihusisha kufadhili shule za jumua zinahuishwa na shauku ya wazi ya kuanzisha mtaala mpya unaofaa kwa changamoto ya maendeleo ya wenyeji katika Afrika karne ya 21.

Kwa mfano, Taasisi ya Elimu ya Umma (*Institut d'Education Populaire*) huko Mali imefanya kazi kubwa kwa muda mrefu wa kupata ufafanuzi wa programu ya shule ya msingi “Ciwara” (Neno la lugha ya Bambata likiwa na maana ya kichwa cha paa alama ya utambulisho wa Wamali) inayotilia mkazo ufundishaji wa stadi za uongozi—kwa ufupi uwezo wa vijana kuchukua jukumu zito katika maendeleo ya jumua yao.

Zaidi ya hayo, katika Senegali na Mali wabia waliosaidia shule za jumua walikuwa ni vyama vilivyojihusisha pia na sekta nyingine za maendeleo ya wenyeji kama msi-mamiaji wa mali asili, afya na kilimo. Katika Magharibi mwa nchi ya Mali, CEWIGAP (Elimu ya jumua, maji na shughuli za kuongeza mapato) na mashirika kama Tostan na ANAFA katika Mkoa wa Djourbel huko Senegali, kwa mfano waliunganisha ufadhili wa shule na miradi mingine. Huku kuchanganya shughuli kulitoa fursa zaidi za kuanzisha mada za maendeleo ya wenyeji katika mtaala wa shule za msingi na sekondari, ikiwa ni pamoja na vyanzo vya asili vya maarifa husiani.

### Matatizo ya utekelezaji

Kwa bahati mbaya, kazi kubwa imezungumzwa zaidi kuliko kufanyika. Vipengele vya maarifa asilia katika shule za jumua vinaonekana kuwa vinatekelezwa kwa kidogo sana, kwani vinahitaji ubunifu na uwezo, hata bila kutaja nia ya kuachana na kaida zilizopo. Ukweli ni kuwa hali ya jumla inaonyesha kuwa shule za aina hii zinakuwa shule zenye gharama ya chini kama siyo ubora wa chini unaojirudufu wa shule za msingi kutokana na matatizo ya kifedha yanayozikabili shule hizo.

*Tatizo la rasilimali watu.* Walimu kwa ujumla wana mafunzo ya chini na wanaweza pia kuwa na elimu ndogo. Katika modeli nyingine, wanakijiji waliosoma au wazazi wanaochaguliwa na jumua zao hupata mafunzo ya siku chache. Tatizo lingine wanaolipwa na fedha zinazochangwa, wale waliohitimu shule huajiriwa na kupelekwa vijijini.

*Tatizo la fedha.* Modeli za Elimu ya jumua zinaandaliwa ili zisiwe aghali, ufumbuzi wa kupunguza gharama za kuongeza miundo mbinu ya shule zilizopo unategemea kwa kiwango kikubwa vifaa na fedha toka jumua na mara nyingi ni chache. Katika maeneo ambayo wanalazi-

mika kuwalipa walimu mara kwa mara wanapambana na tatizo hilo.

*Tatizo la ufundi.* Kutengeneza mtaala mbadala kunahitaji ujuzi na umakinifu ambao upo mdogo sana. Changamoto kubwa ni kuhusisha maudhui ya kienyeji na programu ya mafunzo ambazo zinaruhusu wengine angalau waweze kuendelea na masomo katika elimu rasmi kama wanapenda. Usanisi huu unaitwa “ufundi-shaji kutana” (pedagogie convergente) huko Mali unategemea sana kupata njia ya kufundisha lugha za kimataifa zinazotumika kwenye shule za sekondari na elimu ya juu kutoka kisomo cha msingi katika eneo la wenyeji au lugha ya taifa. Hufanya hivi kwa msaada wa wafundishaji ambao wenyewe hawajaboea kwenye kisomo cha msingi. Juhudi hizo zinatumia nguvu kidogo inayobaki kwa ajili ya kukuza nyenzo za maarifa mapya katika mtaala.

*Matatizo ya kisiasa.* Kufanikiwa kwa shule za jumua kwa upande mmoja ni kubahatisha uwezekano wa kujenga daraja la kiasasi la kufuatia elimu rasmi. Katika nchi zinazozungumza Kifaransa linaitwa “passerelles” mandhari haya yanaongozwa na watetezi (au wahitimu) wa elimu za msingi na sekondari za jadi. Kejeli iliyopo ni kuwa elimu mbadala inavyozidi kupanuka na kusaidiwa na vyama vya kienyeji na AZISE kuna kuongezeka kwa kusita kwa upande wa kisiasa kwani vyama vya kienyeji vinafikiri kuwa havina uwezo kulipa changamoto jeshi la elimu lililopo katika mazingira haya kuliko wanavyoweza kufanya wawakilishi wa wizara au mashirika makubwa ya kimataifa.

### Masuala ya ubora

“Ubora” na “usawa” ni maneno muhimu katika mjadala juu wa hali ya baadaye ya shule za jumua katika Afrika Magharibi ya Saheli. Ubora unaibua ukosoaji ambao kwa sasa uko katika kiwango kimoja: Elimu inapatikana kwa jumua mpya na wanafunzi, lakini ni elimu ya namna gani? Inawezekana walimu wasiosimamiwa vizuri ambao hawajui vizuri lugha ya mfumo rasmi na shule zisizo na vitabu au mazingira bora kujifunzia. Hali kama hiyo inawapa nini cha maana wanafunzi. Je inalichukulia vipi suala la utoaji wa elimu ya usawa. Kwani kwa kuanzisha mfumo wa elimu wa ngazi mbili maskini wa vijijini na mjini si wanapata kikaragosi tu cha elimu yenyewe?

Siku hizi watetezi wa shule za jumua wanafahamu suala hili na tathmini ya ndani ya mshirika yanayofadhili shule hizo yanalenga kwenye masuala ya ubora. Wakati huo huo watetezi hao wana majibu mawili ambayo angalau yanapanua mjadala. Kwanza nini hasa maana ya “ubora”. Je kujihusisha kwa jumua, masomo kwa lugha

ya wenyeji, kuhusisha maudhui ya utamaduni na uhusiano wa moja kwa moja wa masuala ya maendeleo katika sekta nyingine yanajitokeza katika fasiri, au alama za mitihani na kiwango kinachotakiwa kuingia shule za sekondari ndiyo kigezo pekee? Pili, kwa suala la usawa sifa bainifu ni zipi kati ya usawa kijinsia na kuongezeka kwa tofauti kati ya mijini na sehemu nyingine za mashambani? Shule za jumua zina angalau wastani bainifu wa rekodi nzuri za ushiriki wa wanawake kuliko wenzao katika sekta ya zamani.

### **Elimu inayotolewa na wote?**

Shule za jumua na juhudi za kuingiza maarifa asilia katika elimu ya wenyeji zinakabiliana na vikwazo vikubwa. Shule za jumua zinatoa nafasi moja muhimu ya maarifa asilia ya kutambuliwa zaidi kuwa yameibukia Afrika Magharibi na tayari yamekamilisha mambo kadhaa makubwa. Tathmini ya utafiti katika nchi za Senegali na Mali unaonyesha kuwa kwa ujumla inakubalika kwa

wateja, yaani wazazi na mamlaka za wenyeji, hii ni kwa sababu ya kutumia lugha za kiafrika na umuhimu wake wa kuendana na utamaduni wa wenyeji.

Hatua za hivi karibuni za ufadhili wa AZISE na vyama vya wenyeji umeleta karibu uhusiano na nyanja nyingine za maendeleo ya wenyeji ambapo maarifa asilia yanahitajika na kutumika. Hatua hii imefanya kuwe na kiasi kikubwa na mageuzi ya shule kwa ujumla, kama ilivyoshuhudiwa mara kadhaa. Kwa mfano imetokea katika “Estates General” (au Mabunge ya Taifa ya Elimu) yaliyoitishwa na nchi za Saheli katika miaka ya karibuni kushughulikia masuala ya mageuzi ya elimu. Elimu ya jumua kwa hakika ina kitu kimoja muhimu ambacho ni ELIMU KWA WOTE, mkakati unaohitajika sana kujaziliza umuhimu unaoongezeka wa “ELIMU KWA AJILI YA WOTE” na inatoa nafasi ambapo maarifa asilia yanaweza kuingia yenyewe.

Wakati huo huo hatari na nguvu ya vuguvugu la shule za jumua linaonyesha aina ya mabadiliko ya sera yanayohitajika ili kufanikisha ukuzaji wa utaratibu wa maarifa asilia katika Afrika Magharibi ya wakati huu.

# Mbegu za Uhai: Wanawake na Kilimo Bio-anuwai katika Afrika

Makala hii imendikwa na waandishi wawili, Peter Easton na Margaret Ronald, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida. Utafiti umefanywa chini ya usimamizi wa Klabu ya Saheli/OECD, Kamati ya Majimbo ya Kupambana na Ukame katika Saheli na Chama cha Maendeleo ya elimu katika Afrika.

**Tini za MA 23  
Agosti 2000**

Maendeleo ya Kilimo duniani kote yamesababisha kuanguka kwake. Kubadili spishi za mimea ya asili kwa mazao yanayouzika iliendana na upunguzaji wa aina anuwai za hifadhi za mbegu. Kupotea kwa mimea yenye matumizi ya dawa hususani kwenye maeneo yenye bioanuwai ya juu kama mvua za misitu ya Kitropiki imeonekana sana miaka ya karibuni. Lakini kujikusanya kwenye anuwai asili za spishi zinazoliwa, na wakati mwingine zinabadilishwa kijenetiki, mazao ya fedha na ardhi asili kuweka mbadala (aina za mimea asilia) kwa kuwa na kilimo cha biashara, hii vilevile imesababisha tatizo kubwa.

Juhudi zinafanyika sasa ili kuwa na akiba ya aina za mazao zinazotishwa maarifa asilia ya mimea inayotumiwa kwa chakula ni moja ya “sehemu” muhimu ya bioanuwai katika Afrika na ni moja ya eneo ambalo wanawake wana jukumu kubwa la kufanya.

## Kilimo cha maharagwe Kenya

Kilimo cha maharagwe nchini Kenya ni mfano mzuri. Ushahidi uliopo unaonyesha kuwa wakati kabla ya ukoloni aina mbalimbali za spishi za maharagwe zilikuwa zikilimwa katika milima ya Kenya. Maharagwe

yanafanya sehemu muhimu ya lische ya watu wa vijijini. Hii ilikuwa chanzo kizuri cha protini kujaliza ulaji wa mahindi na vyakula vingine vilivyopatikana. Maharagwe haya hususani ni ya aina ya asili ambayo ni nyeusi inayoitwa “njahe” kwa lugha ya Kikuyu (kwa kiasi kikubwa huyaita *Lablab niger* na *Dolichos Lablab* kwa kisayansi na “lablab beans” kwa Kiingereza), ambayo yalilimwa na wanawake na kufanya sehemu kubwa ya mavuno. Njahe ina maana maalumu kwa wanawake kwani haragwe lilichukuliwa kuwa li-naongeza rutuba ya uzazi na hutibu magonjwa ya akina mama baada ya kujifungua. Wakati huo huo kwa kiasi fulani ni chakula kitukufu. Hulimwa juu ya milima ya Ol Donyo Sabuk, eneo la pili muhimu anakoi-shi mwanzilishaji wa dini ya Kikuyu na lilikuwa linatumwa kwa sherehe takatifu.

Maharagwe nchini Kenya yanalimwa zaidi na wakulima wadogo wadogo na zaidi hulimwa na wanawake ili kulisha familia zao. Kijadi wanawake hulima mazao mbalimbali katika shamba moja na kuhifadhi mbegu za aina mbalimbali kama kinga dhidi ya magonjwa ya mbegu na hali ya hewa isiyotabilika. Vyakula vya kienyeji kama “githeri” na “irio” navyo ni aina mbalimbali ya maharagwe.

Ruwaza hizi zilianza kubadilika wakati wa ukoloni. Utawala wa Waingereza kimsingi ulipenda kuongeza uzalishaji wa mahindi. Mahindi yalikuwa ni chakula rahisi kwa wafanyakazi wa kujenga reli na walianzisha kilimo cha mazao ya fedha kama pamba na mkonge ili kuhakikisha kodi inalipwa.

Mkakati ulianzishwa ili kuendeleza ajenda hii ni pamoja na vivutio vya fedha na bei nzuri kwa kilimo cha mahindi, kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine walianzisha mbegu mpya za maharagwe meupe na mekundu kwa ajili ya kusafirisha nje (hususani Ulaya) ili kuchukua nafasi ya Njaha na spishi nyingine za jadi. Ingawaje aina mbalimbali za maharagwe zilifanyiwa majaribio kwa miaka kadhaa na huduma ya kilimo kipana, aina chache zilistawi katika hali ya Kenya au kukubaliwa katika vyakula vya wenyeji. Aina zilizomudu ni figo ya Kanada, rose coco na *Phaseolus vulgaris*. Taratibu aina hizi ziliingia sokoni na kuanza kuiondoa njaha katika uzalishwaji.

Huduma za nje za kilimo cha kikoloni zilifanya kampeni za kuondoa kabisa kilimo mchanganyiko cha aina mbalimbali za maharagwe na kuhakikisha kuwa aina moja ya zao hulimwa katika eneo moja. Mara nyingi ilikuwa ni zao linaloweza kusafirishwa nje ya nchi. Maharagwe yasiyochanganyika au yaliyochambuliwa yalipata bei nzuri mara mbili au tatu ya mazao mchanganyiko.

### Gharama za kulima zao moja

Tukio hili lilikuwa na madhara makubwa kwa lishe, kwa kilimo bioanuwai katika milima ya Kenya, kwa rutuba ya udongo, na kwa wakulima wanawake wenyewe. Kubadilisha mahindi badala ya maharagwe katika chakula cha wenyeji kulipunguza mzunguko wa chakula kilicholiwa na watu wa vijijini ambacho kwa uchache kilichangia na tatizo hili limeendelea bila kupungua.

Wakati huo huo uondoaji wa aina mbalimbali za maharagwe yaliyolimwa kabla ya uhuru kuna madhara sambamba. Mojawapo ni kufukarisha hifadhi ya kijenetiki iliyokuwapo na ambayo ilizalishwa miaka maelfu ya kilimo cha mwanadamu katika Afrika Mashariki. Kilimo shadidi cha mahindi na kudharau virutubisho vya ardhi vya jamii ya kunde kama maharagwe, matokeo yake ni kufukarisha udongo. Ulimaji wa maharagwe uliongeza uwezekano wa kudhurika kwa baadhi ya mazao yaliyostahimili magonjwa. Mwishowe, kwa vile kilimo cha maharagwe ni shughuli muhimu kwa uchumi wa wanawake na uwezo wao wa kulisha familia zao, shinikizo la kupata fedha na kuacha kilimo cha maharagwe kume-

changia katika kuongeza uhamiaji wa wanawake kuenda maeneo ya mijini.

Sera za kikoloni zilikuwa zinatumika zilipanuliwa wakati wa uhuru, kwa makosa na siyo kwa kukusudia. Sera hizo ziliendelea kushughulikia mazao ya fedha ya kuuza nje. Wanaume ndiyo wakahodhi kazi hizo, shinikizo la kiuchumi kutokana na kudaiwa kodi na ada ya shule kulivuta usikivu wote na kuwaondolea wanawake jukumu lao la uzalishaji wa maharagwe na uhifadhi wa mbegu mbalimbali. Ni baada ya miaka 1970 ndipo chuki dhidi ya spishi za jadi za maharagwe ilipoanza kupungua, baada ya sera za kilimo za Kenya kufanyiwa mabadiliko taratibu ili kuzifanya kuwa za Kiafrika.

### Mifano toka Afrika nzima

Hali iliyoelezwa kwa Kenya siyo suala lililojitenga. Afrika nzima kuna hadithi sawa na hizi zinazoweza kuibuliwa juu ya ufukarishaji wa taratibu za hifadhi ya mbegu chini ya shinikizo la mazao ya fedha sambamba na upuuziaji wa majukumu ya wanawake katika kilimo na kazi yao muhimu kama watunza bioanuwai. Ukweli ni kuwa Afrika ni moja ya kanda za dunia zenye kiwango kidogo cha hisa za mbegu zilizoingizwa, sifa ambayo ipo katika kanda zilizokuwa na kilimo cha masetla kama Amerika Kaskazini na Australia. Hifadhi ya mbegu na prazma ya mbegu inafanya kuwa hazina ya kibotania ya maarifa asilia. Kutokana na majukumu yao ya kuitunza familia, wanawake kwa karne nyingi wamekuwa kitovu cha kuzalisha spishi za mazao ya chakula, uhifadhi wa mbegu kwa kupanda nyumbani na kutumia mimea inayoliwa. Masuala ya kudhuriwa na magonjwa na uhakika dhidi ya mazao kushindwa kupatikana kutokana na matatizo ya hali ya hewa isiyotabilika yamefanya wenyeji wawe na mbegu aina mbalimbali na ruwaza tofauti za kilimo.

Katika nchi ya Burkina faso na katika Afrika Magharibi ya Sahel kwa mfano wanawake wa vijijini wanakusanya kwa uangalifu matunda, majani na mzizi ya mimea ya jadi kama mibuyu (*Adansonia digitata*), majani mekundu (*Hibiscus Soddarifa*) majani ya kapoki (*Ceiba pentandra*) na kweme (*Cyems esculentus*) kwa matumizi ya familia zao ili kujalizia nafaka zitokanazo na kilimo (uwele mtama) ambazo hutoa sehemu moja ya lishe na huweza kukosekana katika mwaka fulani. Zaidi ya spishi 800 za mimea ya porini inayoliwa imeorodheshwa katika eneo lote la Sahel. Katika nchi ya Sudani Kusini, wanawake wana jukumu la moja kwa moja la kuchagua mbegu za kuhifadhi kwa ajili ya kupanda kila mwaka. Wanachagua mbegu za aina nyingi na kuzihifa-

dhi na ambazo zitahimili aina yoyote ya hali ya hewa kama itatokea katika msimu wowote wa upandaji.

### Dhima ya wakulima wanawake duniani

Hadithi zinazolingana zinaweza kusimuliwa kuhusu jinsia na bioanuwai katika kilimo katika kanda za dunia. Katika jamii za wakulima duniani kote, wanawake wamekuwa ndiyo watunzaji wa bioanuwai.

- Watafiti kutoka chuo kikuu cha Kilimo cha Wageningen huko Netherland wamegundua kuwa wanawake katika jimbo la Kalasin nchini Thailand wanachukua jukumu muhimu la kusimamia eneo kati ya spishi za mimea inayoliwa ya porini na mimea inayolimwa majumbani. Wameleta spishi mpya za porini na kuanza kuzilima katika miaka ya karibuni na wakahimiza jumua zao kurekebisha kwa uangalifu haki za ukusanyaji mazao ya porini wakati huu wa kuongezeka kwa ubiasharaishaji.
- Wanawake katika jumua za Dalwa ngan na Mambong katika jimbo la Bukidnon, Mindanao nchini Philippines wana jukumu kubwa katika kutengeza “benki ya kumbukumbu” (memory bank) ya plazma ya mbegu na watafiti wa kilimo kwa sababu wote wanahusika na suala la uanuwai. “Ninalima aina mbalimbali (za viazi vitamu), nyingi kiasi ninachoweza kupata mbegu, mkulima mmoja alisema, “kwa sababu kila moja ina matumizi yake na hakuna isiyodhurika na majanga yote.”
- Katika nchi ya India, upande wa Kaskazini, Mkulima mwanamke mzee mmoja alisema kwa maneno machache wakati akichagua mbegu za kuhifadhi. “Inahitaji jicho kali, mkono nyeti na uvumilivu mkubwa kueleza tofauti kati ya mbegu hizi. Lakini hivi siyo vitu vinavyoheshimiwa tena.”
- Huko Marekani ubadilishaji wa jenetiki za nyanya uliofanywa na viwanda vya kilimo umeleta spishi zinazoweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu bila kuharibika. Mfano, uwezo wa kuiva wakati wa kusafirishwa au inapokuwa dukani baada ya kuvunwa zikiwa bado na rangi ya kijani. Pia kuwa na umbo la mraba linalosaidia katika ufungashaji katika kreti. Sifa hizi zinafanya kilimo cha nyanya kuwa ni shughuli yenye faida na ni rahisi zaidi kuifanya katika mashamba makubwa. Hata hivyo kuna matatizo yanayoendana sambamba na hilo

ambayo ni kuwa na radha isiyoridhisha na kukosa anuwai za kijenetiki. Soko dogo limeanzishwa la nyanya za spishi iliyorithiwa kizazi hadi kizazi. Spishi zilizohifadhiwa mara nyingi na wanawake wakulima wa bustani na sasa zinahifadhiwa na kuzalishwa kwa wateja maalumu.

### Kubadilisha mwelekeo

Je, bado kuna muda kwa nchi kama Kenya? Ndiyo, lakini hakuna kuchelewa. Kupotea kwa hifadhi za mbegu anuwai unafanya uhakika wa chakula kuwa hatarini. Hii ni kwa sababu ya madhara makubwa ya spishi chache kuhimili mabadiliko ya hali ya hewa na madhara mengine ya mazingira. Hali hii inaonekana haiwezi kubadilika bila kuifanyia kazi kwa karibu sana na wakulima wa jadi kwa kutunza mbegu za spishi asilia, pamoja na jukumu kubwa la wanawake katika shughuli hii.

Maharage ya njaha yenyewe kwa kiasi fulani yamerudisha sehemu ya mandhari yaliyopotea katika karne iliyopita. Kuachwa kusafirisha maharagwe meupe, radhi ya kiafrika kwa aina nyekundu na nyeusi za maharagwe zimeanza kurudia. Lakini maharagwe yaliyokaushwa na nguvukazi ya wanawake ambayo kijadi zilikuwa kubwa na na anuwai, bado zimebaki kuwa ni za kusaidia tu uchumi wa Kenya.

Kuongezeka kwa unyeti wa masuala ya bioanuwai uliotokana na mvua za msitu na mifano ya kupotea spishi zenye umuhimu wa kimatibabu, imepanda mbegu mpya ya matumaini katika uwanja huu kwa Afrika na kanda zingine zinazoendelea. Kituo cha Kimataifa cha Kilimo cha Kitropiki cha Cali, Colombia kinaratibu utafiti wa miaka kadhaa juu ya utafiti shirikishi kuhusu majukumu ya jinsia katika kilimo na uzalishaji shirikishi wa mimea katika tovuti yao inayopatikana katika anwani <http://www.prgaprogram.org>. Ofisi ya tawi imeanzishwa nchini Uganda kwa ajili ya shughuli za milima ya Kiafrika ambazo zinaelezea ushirikishwaji wa jinsia kwenye utafiti katika Afrika Mashariki. Wakati huo huo Chama cha Maendeleo ya Mpunga cha Afrika Magharibi kikiwa na makao makuu katika mji wa Bouake, Ivory Coast kimeongeza umuhimu wa kuhifadhi bioanuwai kati ya wakulima wa mpunga wa Sahel na kufadhili utafiti unaohusiana na mazoea ya eneo la Kusini Magharibi mwa nchi ya Mali (angalia <http://www.cgiar.org/warda/>).

# Uimarishaji wa Maarifa Asilia ya Kiufundi: Mfano wa Mvinyo wa Miwa

Makala hii ilichukuliwa kutoka kwenye Kifaransa kama ilivyoandikwa na Luzietoso Nguala, Paul Charles Bom Khonde, na Jean Jacques Magloire Bazabana.

**Tini za MA 24  
Septemba, 2000**

Nchi za Kiafrika zimejaliwa kuwa na uwezo wa kutengeneza chakula na vinywaji (maji ya matunda, mvinyo n.k.) kutokana na mimea mbalimbali (matunda, majani, mizizi, mashina, maua). Katika mazingira ya utandawazi, mazao ya asili ambayo yana soko kubwa katika nchi zinazoyazalisha yanaweza pia kuuzwa nchini na katika mataifa mbalimbali. Ingawa mazao haya ya asili yanapatikana katika masoko ya asili, mengi huwa hayajulikani. Mvinyo wa miwa ni mojawapo ya mazao ya aina hiyo.

Nchini Angola, Kongo na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kuna matumizi ya miwa ya aina tatu. Kwanza miwa hiyo hutumika kama “kinywaji cha mdomoni” *“canne de bouche”* cha kukata kiu, na/au kutuliza njaa. Walaji huchojoa ganda la juu la muwa kwa kisu, hutafuna nyama ya ndani ya muwa na kufyonza maji yake na kisha kutupa ganda (ganda linalobaki baada ya kufyonza maji). Pili, miwa hutumika kama mali ghafi ya kutengeneza sukari. Tatu, miwa hutumika pia kutengenezea mvinyo unaojulikana kama *“lungwila”*.

Makala haya yanazingatia maarifa yatumikayo katika utengenezaji wa mvinyo wa miwa, ambao ni zao la kiasili katika nchi tatu zilizotajwa hapo juu. Kuna sababu nyingi za

uteuzi wa zao hili. (i) Utengenezaji wa mvinyo wa miwa ni desturi ya asili ambayo inarithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. (ii) Matumizi ya mvinyo wa miwa yameongezeka vijijini na mijini. Kwa hakika bidhaa hii inajulikana na inapendwa sana katika miji mikuu ya nchi tatu zilizotajwa, yakiwa na wakazi wapatao milioni 9 (milioni 2 Luanda, 600,000 jijini Brazzaville na milioni 6 jijini Kinshasa). Aidha bidhaa hii inapendwa pia katika miji mikuu na miji minigine ambayo haina wakazi wengi sana na (iii) soko la bidhaa hii ya mvinyo wa miwa ni muhimu sana na usindikaji wake unachangia katika kuongeza ajira na ni njia mojawapo ya kuleta pato litokanalo na shughuli ndogondogo za biashara, ambayo iko hasa vijijini na pembezoni mwa miji. Maarifa yatumikayo ni mahususi katika jamii ya watu wa kaskazini mwa Angola, Kongo ya kusini na magharibi mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Maarifa haya yanawawezesha wajasiriamali wa sehemu hizi kuwa na nafuu ya pekee. Aidha, mahitaji ya uzalishaji wa mvinyo wa miwa unaongeza changamoto ya kuongeza uzalishaji wa zao la miwa na kuongeza haja ya vifaa vya kutengeneza na kuiweka katika vifurushi.

## Kuendeleza maarifa asilia

### **Teknolojia ya miwa**

Ongezeko la soko la mvinyo wa miwa limesaidia kuendeleza viwanda vya uzalishaji na uratibu wa kazi. Katika sehemu ya Kimbongo ambayo ina shughuli nyingi, wazalishaji wa mvinyo wameunda umoja wao ili kupunguza suluba ya kazi. Wanatumia ganda la ndani la muwa kuvundika punje. Ili kubadilisha mtambo wa kusindika wenye wenzote moja, waligundua mtambo wa kusindika kwa mkono wenye wenzote mbili na kisha ule unaosindika kwa mitambo. Mwaka 1997, waliingiza nchini teknolojia ya Mexico na kuwasilishwa katika mikoa mbali mbali iliyokuwa inatengeneza mvinyo. Teknolojia hiyo ilikubaliwa kwa sababu ilifupisha utengenezaji, ilipunguza matatizo katika taratibu za kazi na iliboresha kiasi cha usindikaji wa juisi. Hata hivyo matumizi yake ni madogo kwa kuwa ni aghali sana, na mafundi wanatengeneza aina nyingine za asili.

### **Uenezaji wa maarifa**

Utaratibu wa utengenezaji wa mvinyo unatoka katika ufalme wa zamani wa Congo. Wana ukoo wa jumua mbalimbali ambao walikuwa wanaishi hapo sasa wanapatikana katika baadhi ya sehemu za Angola, Congo, na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo.

Ujuzi huu unatumia wanaume tu na hasa wanaume wazee na wao wenyewe huleta mali ghafi. Wanawake hushiriki katika hatua za mwisho yaani uuzaji wa bidhaa iliyokwisha kamilika. Kihistoria ujuzi huu hurithishwa ndani ya ukoo na familia, toka kizazi kimoja hadi kingine.

Kutokana na kukua kwa miji na upatikanaji wa mvinyo wa miwa katika baadhi ya masoko, njia nyingine za usambazaji zimezinduliwa, hususan kutokana na makundi ya wazalishaji na washirika pamoja na vitongoji vya miji.

Wamiliki wa biashara ndogo ndogo husafirisha bidhaa hiyo kwa waajiriwa wao ambao mara nyingi huwa ni ndugu zao. Ndani ya ushirika wa utengenezaji wa mvinyo, mfumo wa kujifunza unaotumiwa ni tofauti, hutumia mitindo miwili ya uanagenzi inayoendana: watu wazima wanarithisha vijana na wanashirikiana katika ujuzi.

Mbinu ya kwanza ya uanagenzi (mtu mzima kwa kijana) ni ile inayopatikana katika biashara inayomilikiwa na familia, ambapo wanaofaidi ni vijana, au wale watu wasio na ujuzi ambao wanapenda kuanzisha biashara yao.

Mbinu ya pili inazingatia ushirika wa maarifa. Ni mfumo ambao unawawezesha wanachama wa ushirika kubadilishana ujuzi wao. Mwanachama ambaye anamudu utendaji kazi wa aina fulani (kwa mfano uvundikaji) ata-

shirikiana na wenzake na yeye pia atapata ujuzi wa wenzake. Mabadilishano haya ya ujuzi yanachangia katika kuendeleza ujuzi wa kikundi cha wazalishaji kwa ujumla.

Tofauti na mifumo rasmi ya kujifunza, wanufaishwa na mafunzo ya asili hawalazimiki kulipa ili kupata ujuzi huo. Huu ni mfumo wa mshikamano ambao umerithishwa kutoka katika utamaduni wa zamani. Mfumo huu una faida nyingi kwa Wajasirimali: Unapunguza gharama za kuanzia. Kwa hakika mjasirimali anayetaka kuzalisha mvinyo wa miwa anaweza kwa urahisi kupata maarifa hayo. Kwa mfano, katika sehemu ya Kimbongo, mamia ya wazalishaji huanza biashara hiyo bila kupitia hatua za kiutawala na bila taarifa na gharama za mafunzo.

Aidha kila mjasirimali ambaye anajiunga na ushirika wa wazalishaji mijini au vijijini anaweza kuendeleza ujuzi wake kwa kupitia katika utaratibu wa kubadilishana ujuzi kati ya wanachama. Njia hii inaweza kuzingatiwa kama mtindo wa mafunzo ya ufundi unaoendeshwa na wanajamii na pia kama njia ya menejimenti ya uvumbuzi wa pamoja bila msaada wa taasisi rasmi zilizo zoeleka.

### **Matarajio**

Ujuzi wa jamii kiteknolojia mara nyingi hautiliwi mkazo na watafiti endelevu, viongozi na wataalamu. Hali hii imeleteleza athari mbaya katika kubuni na kutekeleza sera.

Mfano wa utengenezaji wa mvinyo wa miwa katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo unaonyesha mafunzo muhimu kuhusu maarifa ya jamii kiteknolojia na umuhimu wake kwa maendeleo ya uchumi katika Afrika. Baadhi ya hoja zinahitaji ufafanuzi. Utaratibu wa uzalishaji wa mvinyo wa miwa unaonyesha uzalishaji mdogo, usio-endelevu, uhaba wa mali ghafi na vifaa (kwa sababu miwa hupatikana katika majira fulani maalumu) tatizo la kuhifadhi mvinyo ukiwa mwingi, n.k. Hili huleteleza upungufu wa mvinyo.

Zaidi ya hayo, maarifa ya teknolojia ya asili hairuhusu utumiaji wa bidhaa nyinginezo (kama ganda la ndani la miwa lililokwifayonzwa juisi ya sukari, ganda la nje la miwa). Kwa kutotumia bidhaa hizi huleteleza uchafuzi wa mazingira kando kando ya kiwanda. Mwishowe, uzalishaji huu wa kiasili unakosa mbinu za ufungaji katika vifurushi na utiaji mvinyo katika chupa kwa ajili ya kusafirisha bidhaa hiyo katika masoko ya mbali.

Kwa kuzingatia mapungufu haya, ni muhimu kwa waendelezaji (wajasirimali, watafiti, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya umma n.k.) kufahamu maarifa hayo ya teknolojia asilia na kuyaimarisha. Katika hali hii, lengo linapaswa kuwa uendelezaji wa njia bora za ufungaji wa virushi, utumizi wa takataka na uendelezaji



wa urahisishaji wa nyenzo za uzalishaji viwandani, n.k. Uimarishaji wa maarifa ya teknolojia ya asili.

### **Uimarishaji wa maarifa ya teknolojia asilia**

Wataalamu wa maendeleo wanatilia mkazo malengo na dhima ya maarifa ya sayansi asilia. Hii haina maana kuwa hapahitajiki misaada kutoka nje—bali ina maana kuwa wataalamu hawa lazima waendeleze maarifa na ujuzi wa asili. Mchanganyiko wa maarifa asilia na yale yasiyo ya asili (yasiyo ya asili lakini ya asili kutoka katika jamii nyingine) unaweza kuongeza uzalishaji. Mbinu hii ni tofauti na ile inayodai kuwa wakala wa maendeleo wanajua “kila kitu” na hivyo wana mbinu bora ya kuhamisha sayansi na teknolojia kutoka katika tafiti na asasi za maendeleo hadi kwenye jumua. Wazalishaji na watumizi wa ujuzi wa asili ndio hasa “wataalamu” hai. Wana sayansi na wana teknolojia wanapojishughulisha na masuala ya maendeleo, lazima wawasikilize na wachote maarifa na ujuzi wao na piawatafute njia za kuoanisha maarifa ya kila upande.

Licha ya matatizo ya kiufundi wanayoyapata na kutoshirikishwa katika mfumo wa taifa wa uzalishaji, watumiaji wa ujuzi wa asilia wana uwezo wa ufundi wa kubadilika kwa kuzingatia mabadiliko ya uzalishaji na kutafuta mbinu za ubunifu dhidi ya matatizo yao. Imegundulika kuwa wanapokuwa na hali ngumu, ndipo wanapokuwa wavumbuzi zaidi. Kwa hakika wanajamii hujiegemeza katika maarifa asilia ili kurekebisha mbinu ya uzalishaji kwa minajili ya kutoa bidhaa bora.

Mashirika ya tafiti na maendeleo yanawajibika kuzingatia maarifa asilia ya kiteknolojia na uendelezaji wa programu za maendeleo zinazokusudia kuongeza thamani. Maarifa ya kiteknolojia ya asili yanaweza kupewa uhai mpya kwa kuyapa madaraka mahali

panapohusika kwa kuzingatia sera ya maendeleo ya jamii. Aidha, muelekeo wa sasa unaopondelea “bidhaa za jamii” unafungua njia mpya ya maendeleo (kwa bidhaa za kutoka nje) ya bidhaa zinazotokana na shughuli za amali za asili.

### **Kuhamasisha maarifa asilia ya kiufundi**

Utandawazi wa sasa wa mabadilishano ya bidhaa unahitaji mabadiliko ya uchumi wa Afrika. Mahitaji haya yanazidi kuwa muhimu na yanaibua matatizo ambayo yanakinzana na mbinu za sasa ambazo madaraka yote yanahodhiwa na serikali hali ambayo haiwezi kutatua matatizo. Jamii ikipewa madaraka inaweza kupata ufumbuzi wa matatizo ya kiuchumi ambayo yanajulikana kwa wanajamii wenyewe ambao wako karibu na wale wanaopaswa kuyapatia ufumbuzi, kuyatumia na kuyafaidi.

Uanzishaji wa biashara unaotegemea maarifa ya teknolojia ya asili unamaanisha pia uanzishaji wa nafasi za kazi katika ngazi ya jamii. Mbinu hii itawezesha mwamko mpya wa shughuli za kiuchumi zinazozingatia guvu kazi za jamii na rasilimali za kifedha. Jitihada hizo za wanajamii zinaweza kuleteleza muundo wa kiwanda cha jamii ambacho kimeundwa na biashara ndogo ndogo. Hali hii itahitaji kuwezesha kwa mazingira na misaada ya kufaa.

Mawakala wa maendeleo wanaweza kuendeleza shughuli hizi kwa kutilia mkazo utaratibu wa ubunifu kwa kushirikiana na mashirika ya wazalishaji. Mashirika haya yanaweza kuingia ubia kwa mfumo wa ushirikiano wa madaraka. Uelewa wa serikali kuhusu athari za kijamii na kiuchumi wa shughuli hizi muhimu, ili kubuni na kutekeleza sera inayozingatia motisha kwa ajili ya kuendeleza bidhaa za biashara za mahali panapohusika.

# Maarifa Asilia: Kuchanganya Mambo Mapya na ya Kale

Makala hii imeandikwa na Peter Easton (Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida) na Guy Belloncle (Chuo Kikuu cha Tours). Kwa maelezo zaidi: baruapepe Peter Easton: easton@coe.fsu.edu

**Tini za MA 25  
Oktoba 2000**

Ni kwa njia ipi maarifa asilia yanatolewa ndani ya maficho ya utamaduni, hadi uwanjani yakifungamanishwa na teknolojia mpya na yakitumiwa katika kazi mpya za maendeleo? Ni katika mafundisho yapi ambapo maarifa hayo yanashawishi, yanafunzwa upya na yanatekelezeka? Mafundisho muhimu ya ujuzi wa zaidi ya miongo miwili yanaelezwa kutoka katika Jamhuri ya Mali.

## **Muundo uliofichika, maarifa yaliyofichika**

Katika nchi ya Mali kama zilivyo nchi nyingi za Afrika kuna ncha mbili kati ya mila na maarifa ya utamaduni wa asili wa vijijini kwa upande mmoja na mfumo na teknolojia rasmi ya jamii za mijini kwa upande mwingine.

Mwishoni mwa miaka ya 1970, kundi la Watafiti wa Mali wakisaidiwa na mwandishi walifanya tathmini ya kina ya elimu ya watu wazi kwa vitendo sehemu za Magharibi na za ustawishaji wa karanga nchini. Sehemu hizo zilikuwa zinaangaliwa na shirika la umma, liitwalo *“Opresheni ya Karanga na Mazao ya Chakula (Peanut and Food Crops Operation au “OACV”)*, shirika ambalo lilipewa jukumu la kuen-

deleza uzalishaji na uboreshaji wa teknolojia ya mashamba. Kwa hakika programu ya kisomo iliendeshwa chini ya ulezi wa OACV na ilijishughulisha—kinadharia—na ujuzi uliohitajiwa na wananchi wa vijijini ili kuboresha na kuongeza mavuno na kuchukua majukumu ya kutafuta mikopo na masoko. Kwa hakika OACV ilikuwa, katika kiwango hicho, imejishughulisha kidogo katika kuhamisha madaraka na rasilimali kwa ajili ya utendaji asilia kwa wanajamii ambao walionyesha uwezo kielimu.

Matokeo ya tathmini ya mwaka wa kwanza yalionyesha kuwa, kama programu ya elimu ingekuwa imefikia lengo lake kiidadi katika sehemu chache za nchi, basi wanajamii wengi waliohusika wangeweza kuzalisha “chanzo” cha wasomi—kwa idadi ya vijana 5 hadi 8. Wanakijiji hawa walipewa majukumu na wenzao ya kuchunguza timu za watafuta soko waliotumwa na OACV kununua mazao ya biashara; ili kuzuia udanganyifu na kuhakikisha bili za kodi na ulipaji wake. Kama timu ya Watathmini ilivyosema baada ya ukaguzi wa thabiti, matokeo yalionyesha tathmini sahihi iliyofanywa na wanajamii wa hali ya mafanikio yatokanayo na kisomo katika mazingira ya vijijini. Soko na uangalizi wa kodi vilikuwa vitu muhimu lakini havikujionyesha

sana kutoka katika mtazamo wa wanajamii kiasi cha kushtahiki ustadi wa kila mtu au familia. Lakini walipojumuishwa na kupangwa katika timu ndogo ndogo za wanavijiji, walifanya kazi ya umakinifu na yenye faida.

Kwa kuzingatia ubora wa tathmini, watathmini walifaulu kuwashawishi viongozi wa OACV kukubali kuhamisha kazi za masoko—na sehemu ya faida itokanayo na uuzaji wa mazao ya biashara kwa wanavijiji kwa kuwa sasa walikuwa na idadi kubwa ya wasomi wanya ambao wangeweza kusimamia kazi hizo. Kwa hiyo mwanzoni mwa mwaka uliofuata wa kampeni ya elimu timu ilipewa jukumu, wakati wa safari zake za kuzunguka vijijini kuwaeleza viongozi wa vijiji mabadiliko ya sera na mtindo wa utekelezaji wake.

Katika kufanya hivyo jambo muhimu lilibainika. Wakati wa enzi za ukoloni, wanavijiji nchini Mali walikuwa wamekubali tabia ya kutaja chifu makansela wa kubuni kukutana na utawala wa Wafaransa wakati walipowatembelea. Kuwasiliana na utawala wa Kikoloni kulionekana, kwa sehemu kubwa, chini ya utukufu wa utawala halisi wa asili na mara chache haukukusishwa na matakwa ya kudumu ya wanakijiji. Mtindo huo huo uliendelea katika sehemu nyingi baada ya uhuru wa bendera wa mwaka 1960, kwa kuwa wawakilishi wa utawala wa kisasa wa Mali walionekana pia kuwa wageni wa utamaduni wa asili. Watawala hao walionwa kuwa hawataunga mkono uhifadhi na uendelezwaji wa utamaduni wa asili. Katika zaidi ya kijiji kimoja, timu ya Watathmini ilianza kuelezea sera mpya na utekelezaji wake kwa wanakijiji mashuhuri. Mara baada ya wanavijiji wenzao kuona kuwa uhamishaji wa kweli wa madaraka na rasilimali vinajadiliwa, basi, watathmini waliomba majadiliano hayo yaahirishwe kwa muda na badala yake, kana kwamba ni jukwa la mapinduzi, timu ya pili ya wapatanishi ilichukua nafasi yao. Timu hiyo iliundwa hasa na watawala halisi wa asili.

### **Kuweka kipaumbele kwa mchakato wa kijamii**

Je, utamaduni wa kiasili na hazina ya maarifa “vinatumikaje” katika miradi ya maendeleo? Utambuzi wa matakwa kama yale yaliyobainika katika maelezo ya uhamishaji wa kazi za masoko kwa wanakijiji kwa hakika ni kiambato kimojawapo. Lakini sayansi ya asili inaweza kuwa ngumu kufichuliwa na kufafanuliwa kuliko utambuzi wa matakwa binafsi kama methali ya Ewe inavyotaja “Ndege mwenye maarifa—mtu mmoja peke yake hawezi kumkamata”. Maarifa ambayo ni ya kijamii na kwa asili yanarithishwa hasa hutokea katika mazingira ya kijamii, ambapo makundi ya watu huundwa

ili kutatua matatizo muhimu au kuwasilisha hekima kwa vizazi mbali mbali.

Katika nchi ya Mali mbinu za kuanzisha utaratibu huu ziliendelezwa na kundi la watafiti wale wale kwa kuhusisha jitihada zilizochukuliwa kuunda matumizi mengine ya elimu. Wizara ya Elimu kwa msaada wa Benki ya Dunia, ilifadhili utafiti wa muelekeo mpya wa elimu isiyo rasmi. Utafiti huu ulijikita katika hoja kuwa elimu mpya iliyopatikana lazima ionwe kama chanzo cha mafunzo mapya ambayo yanakidhi maendeleo vijijini kama lengo linalokusudiwa. Timu ya watafiti ilibuni utaratibu wa aina tatu kwa ajili ya vijana waliofanikiwa hivi karibuni kujua kusoma na kuandika moja kuhusu mbolea ya kilimo, nyingine kuhusu mfumo wa uhasibu kwa ajili ya shughuli za biashara vijijini, na mwingine ni utaratibu wa kutambua na kuinga kuenea kwa magonjwa ambukizi.

### **Mbinu za kupata maarifa asilia**

Mbinu hizi zilifunzwa kwa aina yake. Watafiti walihitaji kuchanganya maarifa ya nje ya kiteknolojia katika kila eneo na utambuzi wa utamaduni wa wenyeji. Ili kufanya hivyo walishirikisha wazee wa jamii waliojua fika utamaduni huo. Hivyo walitengeneza utaratibu ambao ulikuwa na hatua maalumu:

Kwanza, watafiti walikutana na utawala wa kijiji kuwaomba ruhusu ya kujadiliana na wazee matatizo ya jamii yanayowasumbua na njia za kuyatatua katika sehemu hiyo husika (udongo kuishiwa mboji, ugonjwa wa macho, au matatizo katika kuanzisha biashara kijijini). Kwa kuwa jamii zlichaguliwa kutoka katika maeneo ambapo tatizo moja kati ya matatizo haya lilikuwepo kwa kiasi kikubwa makubaliano yalipatikana kwa haraka.

Wakati wa majadiliano hayo na wazee vijijini, watafiti walichukua tahadhari kuelezea kwa kina (a) asili na umuhimu wa tatizo, kama linavyoazingatiwa na wanajamii wenyewe (b) upatikanaji wa mbinu mpya ya kiteknolojia ambayo ikikubalika na kutumika ipasavyo inaweza kuleta matumaini ya utatuzi sahihi; na (c) kuwepo kwa vijana waliohitimu kusoma na kuandika katika eneo la Bambora ambao wana vifaa na hamu ya kujifunza njia mpya na kupeana maarifa hayo na wenzao.

Watafiti walipendekeza wazo la kuwa na warsha ili kubainisha na tatizo na kujaribu njia mpya za utatuzi. Waliahidi kuleta vifaa vya kufundishia, taarifa kuhusu teknolojia mpya na baadhi ya vifaa vya kujaribia. Aidha waliombo wazee wafadhali jitihada hizi na kuwahimiza vijana kuhudhuria warsha hii na kutakiwa kutoa ripoti kwa wazee kuhusu uwezekano wa mbinu hizi mpya. Vijiji

vitatu hatimaye vilikubali kufadhili warsha hii, kila kimoja kikijadili mada mojawapo.

### Mambo yaliyohamasisha mchakato mzima

Changamoto muhimu ilikuwa kutayarisha ujuzi, kiasi kwamba, haikuwa nafasi ya kueneza maarifa ya kiteknolojia na mafunzo ya kiwango cha juu kwa vijana waliohudhuria, bali ilikuwa ni fursa na kichocho cha kuelezea maarifa yanayohusiana kijijini. Ili kuhakikisha mafanikio haya, mafunzo ambayo yalichukua majuma mawili kila moja, yalikuwa na vipengele vitano vilivyohusiana.

- *Maudhui ya kiteknolojia.* Watafiti ndio waliofundisha, lakini walihakikisha kuwa mwezesaji mmoja mjuzi wa kiteknolojia alihusishwa katika kila kikao. Timu ilitengeneza mtaala wa awali uliozingatia uenezaji wa vifaa vilivyotafsiriwa kwa Kibambara.

- *Kazi za maendeleo* Kila mafunzo yalikusishwa kazi ya “maabara” pamoja na vifaa na teknolojia mpya inayozingatia tatizo. Kwa mfano, watafiti waliohusika na programu inayohusu magonjwa ya kuambukiza walikuja na hadubini ambazo washiriki walizitumia kuangalia vielelezo.

- *Uchunguzi wa uwandani au tathmini ya mahitaji ya jamii.* Katika kila mafunzo washiriki wenyewe walihitajika kufanya uchunguzi wa kiwango na hali ya tatizo katika maeneo husika.

- *Kulinganisha na maarifa asilia.* Watafiti kwa ufasaha na utaratibu mzuri walitoa nafasi ya kuelezea maarifa ya wenyeji kuhusu matatizo yaliyokuwa yanajadiliwa na kulingalisha mafunzo hayo na taarifa ambazo zingenezwa.

- *Majaribio ya uchanganuzi.* Kila mafunzo yalielekezwa kubaini vipengele vinavyohusu majaribu halisi ya mbinu mpya na kuzingatia uchunguzi wa matokeo yake.

Mwingiliano muhimu na maarifa asilia ulifanyika kwa njia mbili. Kwanza, wakati wa utafiti wa uwandani kuhusu matendo ya sasa na mahitaji, washiriki wa mafunzo walikuwa makini si katika kuangalia tu matatizo ya watu yaliyokuwa yanawasibu bali pia uelewa wao wa sababu za matatizo hayo na mbinu za kuyatatua. Kila jioni washiriki wa mafunzo walifanya tathmini na majadiliano na wazee wa vijiji. Wakati huu vijana walielezea waliyoyaona uwandani na kueleza wamejifunza nini kutokana na hayo waliyoyaona. Aidha washiriki waliomba maoni na ushauri kutoka kwa wazee kuhusu matokeo hayo yalimaanisha nini na wafanye nini baada ya hapo. Tafakari ya pamoja ilidhihirisha ubora wa

kupata vipengele vya maarifa asilia na kuvilinganisha na vipengele vya “kisayansi” ambavyo vilihudhurishwa katika mafunzo. Katika kufanya hivyo vipengele hivi vya aina mbili vilisaidia kutafuta suluhisho la tatizo.

### Maarifa ya wenyeji kuhusu magonjwa yatokanayo na maji

Ingawa warsha zote tatu zilifuata utaratibu huu, lakini maelezo ya kina yalitofautiana kati ya sehemu moja na sehemu nyingine kwa sababu ya tofauti ya matatizo yaliyojadiliwa pamoja na tofauti ya mazingira ya wana jamii. Kila ujuzi uliongezea jaribu jipya kuhusu mbinu zenyewe.

Warsha kuhusu magonjwa ya kuambukiza ilifanyika katika kijiji cha Fula, karibu na kandokando ya mto Baloue, sehemu nzuri na yenye rutuba kwa ajili ya kilimo. Hata hivyo, sehemu hiyo ilikuwa imeachwa kutumika miaka ya karibuni kwa sababu ya magonjwa ya upofu na kichocho. Watu waliokuwa na dalili za hatua mbalimbali za ugonjwa wa upofu walikuwa wanaonekana dhahiri kijijini, na jumua ilishughulikia magonjwa haya mawili. Wana warsha walibainisha idadi kamili ya waathirika katika jumua nzima na kugundua karibu asilimia 25 ya wanajumua walikuwa na virusi vya ugonjwa huo (onchocerciasis tumor) na zaidi ya theluthi ya watu hao walikuwa wamefikia hatua ya kwanza ya upofu.

Maarifa ya wanajamii kuhusu vimelea na hatua vilipofikia yalionekana kuwa muhimu. Mhamasishaji wa masuala ya teknolojia katika warsha hii—daktari kutoka Chuo Kikuu cha Marseille—alishangaa kuona kuwa wazee wa kijiji walijua ukuaji wa vimelea hivi vya kichocho, jambo ambalo alikuwa akiamini kuwa vimelea hivi vimegundulika katika maabara za Ufaransa miaka miwili iliyopita.

### Kufahamu urutubishaji wa udongo

Warsha iliyohusu urutubishaji wa udongo ilifanyika katika kijiji cha Suransan Tumoto, kasikazini mwa mji wa Kita magharibi mwa Mali sehemu ambayo inalima karanga. Udongo wa rutuba hapa umemalizika kabisa kwa sababu ya mfululizo wa kilimo cha mazao ya biashara na mashamba yalianza kuchoka kabisa. Baada ya utafiti wa awali wa kemia ya udongo, wanawarsha walianza kazi ya kuwahoji wazee kuhusu aina ya udongo inayopatikana katika mazingira ya vijiji na mimea ya asili iliyokuwa inamea katika sehemu hizo. Aidha walianza kukagua kwa makini udongo na mimea kuzunguka kijiji kwa msaada wa bwana shamba kutoka Taasisi ya Taifa ya

Utafiti na walileta matokeo kwa ajili ya majadiliano na wanajamii wote.

Ulinganifu wa mawazo ya kilimo kuhusu urutubishaji wa udongo na maarifa ya wanajamii kuhusu hali ya udongo na mimea ihusikayo ilielekeza uamuzi wa kuanzisha kituo cha kilimo cha majaribio ili kupima mbinu mbalimbali za kuboresha mavuno ya kilimo. Kwa bahati mbaya, wazo hili lilisimamishwa na wana mazingira kutoka OACV, shirika ambalo liliona kuwa si busara kwa wakulima wa kijiji kujaribu jaribio ambalo wakala wa kituo hicho cha kilimo cha majaribio walikuwa hawajalimudu.

### Mifumo asilia ya uhasibu

Warsha ya uhasibu na shughuli za biashara za kijijini ilifanyika katika mkoa unaolima pamba kwa wingi nchini, mahali ambapo soko la mazao lililoendeshwa na vijana wajuao kusoma na kuandika kutoka katika jamii vijana walikuwa wamefungua aina mbalimbali za kiuchumi. Hata hivyo, mwenendo huu ulikuwa umepata kizingiti kikubwa: ukosefu wa mfumo wa uhasibu katika lugha ya Kibambara ambao ungewawezesha wafanyakazi kutoka katika jamii kuwa na madaraka ya soko la mazao na kuanzisha shughuli nyinginezo za biashara.

Baada ya kujifunza mbinu za uhasibu, wana warsha waliowadodosa wazee kuhusu njia ya asili ya kuhakikisha uwajibikaji na waliendesha warsha ili kuorodhesha na kuunda istilahi za lugha ya Kibambara kuhusu hatua mbalimbali zitumikazo. Warsha ilihitimisha mafunzo kwa kutengeneza na kujaribisha mfululizo wa muundo wa uhasibu katika lugha ya Kibambara. Hili lilifuatwa na uwasilishaji, wa namna ya kufanya ukaguzi wa mahesabu kwa jumua nzima.

### Ufundishaji wa namna ya kueleza maarifa asilia

Hoja ya jumla katika warsha hii ilikuwa ni jinsi gani maarifa asilia yangechotwa kikamilifu na kutumika katika kubuni mikakati mipya ya kutatua matatizo yanayokwamisha maendeleo. Hili lilipatikana kwa kutumia njia za busara na bunifu za kanuni za elimu ya watu wazima:

- Tilia mkazo matakwa ya wanajamii
- Anza na yale yajulikanayo kwa watu
- Husisha wanajamii kama walimu katika utaratibu wa kujifunza
- Unda mazingira ya tafakiri ya pamoja na zingatia data ihusikayo iliyotafitiwa.
- Tumia njia nyingi za kuwasilisha mihadhara
- Fuata njia zote za hadi uondoaji wa matatizo.

Lakini kipengele muhimu katika kuhamasisha maarifa ya jamii katika majaribio haya—au kubadilisha “jukwaa la tafakuri” linaloelezwa mwanzoni mwa simulizi hizi kilikuwa cha katika orodha iliyotolewa. Kilihusisha njia za kushirisha “akiba” ya maarifa katika utendaji wa mafunzo halafu nafasi wanayochukua katika kutafuta majibu, vyote vikiwa katika mpangilio ambao unazingatia tafakari ya kikundi. Mbinu hii imekopa kutoka vianzo viwili—kutoka katika mfumo wa asili wa jamii ya Kiafrika, ambao unawapa majukumu ya mashauriano na wazee, majukumu ya menejimenti ya wanafamilia na yale ya kiteknolojia yanawaangukia vijana katika hali ambayo inawafanya wafanye kazi na kushirikiana; na kutoka katika matendo ya kushiriki katika tafiti ambayo inahitaji kuandaa mafunzo kwa kuzingatia kazi zinazotakiwa kutatua tatizo.

Katika hali hii, ulinganisho wa ushirikiano na “sayansi mpya” umekuwa kichocheo badala ya kuwa kizingiti katika kueleza maarifa asilia. Maarifa mengi ya asili—kama yalivyo ya mfumo wa kisayansi—kimsing ni ya *uainishaji*: uangalizi wa makini na mfumo wa matukio mbalimbali halisia yanayotokea na uwiano wake. Kuna utajiri wa hazina, lakini ukosefu wa njia za kurekodi na kulinganisha mabadiliko mbalimbali au kujaribu na kuchanganua miingiliano imefanya agenda hii isikamilike.

Mafunzo yaliyotolewa Mali na kuelezwa hapa yanaanzisha nafasi ambayo si ya kuelezea maarifa asiliaa na kuhusishanisha na matatizo ya maendeleo tu, bali ni kutimiza uwezekano wake wa kuboresha hali ya binadamu kwa kulinganisha na ushirikishaji wa desturi ambazo zimepangwa kwa kuzingatia mabadiliko ya uchanganuzi wa asili na uliopangwa.

# Dawa za Jadi na UKIMWI

*Makala hii inachapishwa upya katika ukamilifu wake kwa ruhusa ya kutoka Lancet, 8 Aprili 2002, juzuu ya 305 uk. 1284. Kichwa asilia cha makala haya kilikuwa "A Regional Task Force on Traditional Medicine and AIDS (Tume Maalumu ya Kieneo Inayoshughulikia Dawa za Jadi na UKIMWI)". Waandishi ni Gerard Bodeker, Donna Kabatesi, Rachel, King, Jacques Homsy, Chuo cha Green, Chuo Kikuu Oxford, Oxford OX2 6HG, UK; THETA, Uganda; na Madaktari Wasio na Mipaka Uganda. Hakimiliki 2000 The Lancet Ltd. kwa ushirikiano na The Gale Group na LookSmart. Hakimiliki 2000 Gale Group.*

## **Tini za MA 26 Novemba 2000**

Timu ya kanda ya dawa za asili na UKIMWI katika Mashariki na Kusini mwa Afrika itazinduliwa (sic) Kampala, Uganda, tarehe 10 Aprili, 2000. Timu hiyo itaratibu shughuli zinazohusu utumiaji wa dawa za asili na watu walioathirika na VVU/UKIMWI katika Afrika na nafasi ya waganga wa asili katika kinga ya UKIMWI. Timu hiyo ya Mashariki na Kusini mwa Afrika inaundwa na watu tisa wa AZISE, mashirika ya kimataifa na timu ya watazamaji kutoka Afrika ya Magharibi. Kazi ya timu hiyo ni kupeana taarifa, kutengeneza orodha ya shughuli zinazohusu dawa za asili, kuandika na kueneza utendaji bora, kuanzisha tafiti zinazohusu dawa za asili na kuhamasisha upatikanaji wa fedha. Timu itazingatia ukweli kuwa katika Afrika, gharama kubwa na ukosefu wa dawa muhimu, ikiwa ni pamoja na dawa za kinga ina maana kuwa watu wengi wenye VVU/UKIMWI wanatumia dawa za asili za miti shamba katika kutibu magonjwa yanayohusiana na VVU ikiwa ni pamoja na maambukizo ya magonjwa nye-melezi. Nchini Uganda kuna mganga wa asili mmoja kwa kila watu 200-400 wakati ambapo madaktari ni mmoja kati ya watu 20,000.

Mpango wa kuanzisha timu hii ulitokana na ufadhili wa UNAIDS wa mkutano wa Kampala mwezi

Februari, 2000. Wajumbe wapatao 100 kutoka nchi 17 za Afrika walikutana kutafakari athari za waganga wa asili katika kuzuia VVU na utunzaji wa waathirika. Wenyeji wa mkutano huu walikuwa ni Shirika la Waganga wa asili na wa kisasa kwa pamoja dhidi ya UKIMWI (Traditional and Modern Health Practitioners Together Against AIDS (THETA)).

Hili ni shirika lisilokuwa la kiseriali la Uganda ambalo linasimamia mahusiano kati ya watendaji wa Afya wa asili na wa kisasa kuhusu vita dhidi ya UKIMWI. Msaada ulitolewa na UNAIDS na shirika la Kutangaza Dawa za Asili (Promotion of Traditional Medicine (PROMETRA)), ambalo ni shirika la kimataifa lililopo Senegali. Shirika la Waganga wa asili na wa kisasa linaongoza katika Afrika ya Mashariki katika kuendeleza ushirikiano kati ya sekta ya dawa ya kisasa na dawa ya kiasili.

Wajumbe wengi wa mkutano wa Kampala walitoa hoja kuwa, kwa kuzingatia matumizi makubwa ya dawa za asili, waganga wa asili kwa hakika wanachukua mzigo wa hospitali za kisasa kwa kushughulikia ugonjwa wa mlipuko wa UKIMWI katika Afrika, jambo ambalo halingatiwi kikamilifu na Wizara za Afya, mashirika ya kimataifa, na wafadhali.

Wajumbe walilenga katika ushirikiano kati ya sekta ya afya ya asili na ya kisasa. Walibainisha miradi ambayo inazingatia vigezo vya “matendo sahihi” ambayo yanakidhi vita dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa UKIMWI. Nchi nyingi ziliripoti ari iliyohusika dawa za asili na madaktari. Dr. Sandra Anderson wa UNAIDS, Afrika ya Kusini, alisema kuwa waganga wa asili wana nafasi muhimu katika jamii za Kiafrika na wanatoa mchango muhimu katika kukinga maambukizo ya UKIMWI na utunzaji wa Waathirika. Mkurugenzi wa THETA, Dr. Donna kabatesi, alitoa data zinazoeleza kufaa kwa dawa za mitishamba katika nchi ya Uganda dhidi ya ugonjwa wa malengelenge ya nevu ngozini (herpes) na VVU vinavyohusishwa na kuharisha na kupungua kwa mwili. Professor Charles Wambebe, Mkuu wa Taasisi ya Nigeria ya Utafiti wa Dawa aliripoti matokeo ya awali ya dawa za mitishamba katika Nigeria zinazoongeza seli za CD4 (CD4-cell counts) na zinazoonyesha mafanikio ya kupata nafuu kwa magonjwa yanayohusiana na VVU; utafiti kuhusu utumizi wa dawa haya umo mbioni. Dr. Mberesero Firmina wa Kikundi cha Waathirika wa UKIMWI Tanga alieleza matokeo ya utumizi wa mitishamba dhidi ya magonjwa ya fangasi (kuvu).

Ingawa afya ya asili inapatikana kwa urahisi na ina kubalika kiutamaduni, lakini haina budi kuhakikishwa usalama wake. Hati hafifu, kutokuwepo na viwango na mfumo wa sheria kwa ajili ya afya ya asili katika nchi nyingi vilionekana kama changamoto ya kukabili kama dawa za asili zitachukuliwa katika mapambano dhidi ya kinga ya UKIMWI na matunzo. Kutoelewana kati ya waganga wa asili na waganga wa kisasa, waganga wa asili kuwa na ushirika dhaifu, maono ya maandishi wa habari kuhusu Waganga wa asili, vyote vinachangia dawa za asili kuwa na hadhi ya ukingoni katika nchi za Kiafrika. Licha ya serikali nyingi na mashirika ya kimataifa kuhimiza kutambuliwa kwa dawa za asili, kutokuwepo na moyo wa kuwajibika na matendo kuhusu jambo hili, vimeonwa kuwa kikwazo cha kutambua mikakati ya kiasili dhidi ya kuzuia UKIMWI. Aidha hali hiyo, haikuwezesha kujenga mashirikiano ya kuunganisha juhudi na mbinu dhidi ya VVU/UKIMWI. Kwa hali hiyo, dawa chache za mitishamba zinazotumika kila siku katika Afrika na ambazo zina uwezo wa kutibu magonjwa yanayoendana na UKIMWI, zinaendelea kutojulikana au kutochanguz-

wa. Wakati huo huo Waafrika wengi wenye VVU/UKIMWI hawawezi kumudu dawa za kisasa ambazo zimethibitishwa kuwa zinafaa.

Baada ya kuzingatia umuhimu wa mfumo wa mtandao wa mashirika yanayofanya kazi kipekee na dawa za asili na VVU/UKIMWI, mkutano ulipendekeza uanzishwaji wa timu ambayo itahudumiwa na THETA kama watendaji. Wanachama wa timu hiyo ni pamoja na ushirika wa waganga na Dawa za Asili wa Zambia, na Ushirika wa Kitaifa wa Waganga wa Asili wa Zimbabwe. Kutakuwa na makundi ya Waangalizi kutoka nchi za Afrika ya Magharibi za Ghana, Nigeria na Cameroon. Washiriki wa kimataifa ni pamoja na Umoja wa Mataifa unaoshughulikia UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO, AFRO) na Shirika la Kimataifa la Mfumo wa Afya ya Asili (Global Initiative for Traditional Systems GIFTS)) na mashirika mwenza-Kundi la kazi la Mfumo wa tiba ya asili na matibabu mbadala la Jumuiya ya Madola (Commonwealth Working Group on Traditional and Complementary Health Systems. Shirika la GIFTS ilikubali kuanza shughuli za awali za mtandao wa Watafiti na Taasisi kujenga programu za Utafiti ambazo zitabainisha, kutathmini na kuendeleza matibabu ya jamii ambayo ni salama na yanayofaa kwa matibabu ya magonjwa yanayoendana na UKIMWI. Programu hii itatumia protokali rahisi lakini zinazozingatia usimamizi thabiti wa kuendesha uchunguzi wa haraka wa matibabu yanayoleta matumaini. Programmu itazingatia hati miliki kulinda haki za wataalamu, ikijifunza kutoka kwa Programmu chache zilizopo katika Afrika. Kwa kuzingatia ulimwengu kwa ujumla, kutohimili shinikizo la mahitaji ya dawa ya mitishamba, kilimo cha bustani kitaendelezwa kwa spishi zinazopewa kipaumbele. Muundo msingi wa tafiti za serikali imara, zikisaidiwa na mashirika ya kimataifa, utahitaji kuendelezwa ili kuhakikisha kufanyika kwa tafiti haraka iwezekanavyo kwa kuitika matokeo chanya ya awali. Mbinu hii itapangwa ili kuongeza matibabu ya mitishamba yanayoleta matumaini hadi kwenye hatua za maendeleo salama, yanayofaa, na yanayotoa dawa rahisi. Mbinu hii italitia mkazo, panapohusika, uzalishaji na usambazaji wa dawa za miti shamba zinazofaa katika kiwango cha taifa, jumuiya na familia katika jitihada za kupata suluhisho la Kiafrika katika kupambana na UKIMWI Afrika.

# Teknolojia ya Habari na Maendeleo Vijijini: Kituo cha Nakaseke cha Mawasiliano Anuwai

Taarifa hii iliandikwa na Siddhartha Prakash wa Benki ya Dunia na inatokana na matembezi yake ya Uandani wa kituo cha Mawasiliano cha Nakaseke.

## ***Tini za MA 27 Desemba 2000***

Mara nyingi inasemwa kuwa teknolojia hazifikii jumuiya za vijijini. Lakini baadhi ya maendeleo ya kisasa ya mawasiliano yameanza kuondoa umbali vijijini na vikwazo vya miundombinu. Kituo cha Mawasiliano cha Nakaseke kilicho umbali wa kilometa 50 kaskazini mwa Kampala, Uganda katika vijiji vilivyo mbali, kimeanzisha teknolojia ya mawasiliano katika kijiji hicho. Katika muda wa miaka mitatu, kituo hicho kimechochea shughuli nyingi za maendeleo katika eneo hili.

Eneo hili la Nakaseke lina idadi ya watu zaidi ya 35, 983 kati yao wanawake wakiwa 18,617. Mji wa Nakaseke wenyewe una idadi ya watu 3000 wengi wao wakiwa wa kabila la Baganda, kabila kubwa katika Uganda ya kati. Hadi kituo hicho cha mawasiliano kinaanzishwa mwaka 1997, magazeti yalikuwa yanapatikana katika mji mwingine ulioko umbali wa kilometa 16 na unaonganishwa na barabara mbaya.

Kituo cha mawasiliano cha Nakaseke ni kimojawapo cha msululu wa miradi inayofadhiliwa na (UNESCO/IDRC/ITU) ambayo inaendeshwa nchini Benin, Mali, Mozambique na Tanzania. Lengo kuu la miradi hii ni kuchochea maendeleo ya vijijini kwa kurahisisha upatanikaji wa habari, nyenzo za kujifunza na teknolojia ya

habari kwa ajili ya jamii za Nakaseke na Kasangombe na kusaidia huduma za afya vijijini.

Shughuli zinazoendeshwa sasa ni pamoja na mafunzo ya matumizi ya kompyuta, na mtandao, barua pepe, simu, faksi, maktaba na huduma za kutoa vivuli (photocopy), kituo cha kujifunzia, maonyesho ya video na kurekodi, na mahali pa jamii pa kusikiliza na kusomea na pia sehemu ya shughuli za michezo kwa vijana.

Ingawa kituo cha Mawasiliano kinalenga katika kuzihudumia jamii zote za Nakaseke na Kasangombe, lakini hasa kinakusudia makundi maalum ya watumizi; wanawake, vijana, watoto, madaktari, walimu, wakulima na viongozi wa jamii. Hivyo maudhui na programu za kituo hicho zinalenga katika matakwa na mahitaji ya makundi haya.

### **Mkakati wa utekelezaji**

Ushirikishaji wa wanajamii ndio kitovu cha utekelezaji wa shughuli za kituo hiki. Tangu kianzishwe, jamii ndiyo imekuwa kiini cha upangaaji na utekelezaji wa shughuli zote. Kamati ya utendaji ya wanakijiji ilichaguliwa kutokana na wanajumuiya ikiwakilishwa na kila kundi lengwa:

- Kusimamia shughuli za kila siku za kituo.



- Kushirikiana na kamati ya menejimenti
- Kuwahimiza wanajamii kushiriki katika shughuli za mipango yote.
- Kuendesha programu za umiliki na kushirikisha jamii katika shughuli zo zote ambazo zinahimiza mwendelezo wa kituo, ikiwa ni pamoja na shughui za kuchangisha fedha.

### Taathari

Jumuia imepata maktaba/kituo cha rasilimali, simu na kitengo cha teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) kwa ajili ya shughuli/huduma zote zinazohusiana na ICT.

Kituo cha mawasiliano kimebadilisha maisha ya watu wa vijijini. Kimteoa huduma za mtandao, simu na faksi, vinavyotumiwa kuendesha shughuli za biashara ya jamii. Mafunzo ya kompyuta yameleta kazi kwa vijana, ambao sasa wanaweza kupata maktaba ambayo ina majarida ya kimataifa na vitabu. Wakulima wameanza kujishughulika na biashara kwa kutumia simu na mtandao wa kituo kupata na kueneza taarifa kuhusu mbinu za kilimo kijijini na bei za mazao. Kituo kimeanza kutekeleza Programu ya maarifa kwa jamii kwa kuwahusisha wakulima vijijini, programu ambayo inaweza kutumika kama kichocheo cha kuendesha mabadilishano ya maarifa kati ya jamii moja na jamii nyingine. Sasa wakulima wanaomba kufahamu bei katika masoko na mwenendo wa jumla kuhusu mazao wanayolima.

Jumuia ya shule (wanafunzi wapatao 7000) pamoja na wafanyakazi wa jumuia na madaktari wamefaidika kutokana na kituo cha maendeleo. Jamii (yenye vijiji 42 na kaya 3,000) inaanza pole pole kutahmini umuhimu wa habari kama inavyohibitishwa na watu wengine kuanza kuulizia kuhusu taarifa ya vipengele vingi. Gazeti la kila siku ambalo linapatikana katika kituo limesaidia pia kuwafanya wana jumuia kujua kinachoendelea katika sehemu nyinginezo za nchi.

### Mradi wa kilimo watumia maarifa asilia

Ingawa idadi ya watu nchini Uganda inatarajiwa kuongezeka mara dufu mnamo kipindi cha miaka 30, ongezeko la lazima la kilimo linaloendana na idadi hiyo linatia wasiwasi. Ukuaji mdogo wa kilimo unasababishwa na, kati ya mambo mengine, udhaifu wa utafiti na uhusishanaji wa mkulima na mfumo hafifu wa upatikanaji wa teknolojia, ikiwa ni pamoja na udhaifu wa utoaji wa habari za kufaa na mfumo wa uwasilishaji wake.

Miradi ya kilimo inakusudia:

- Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kipato cha kaya katika maendeleo ya Nakaseke na Kasangombe.
- Kuwasaidia wafanyakazi wa kilimo katika kutoa taarifa na kuongoza wakulima wa jumuia.
- Kuoanisha kazi za utafiti na vitengo vya wakulima, na hivyo kuzidisha mtiririko wa habari kutoka sehemu zote mbili. Taasisi za kimataifa, kitafia na kijumuia zitahusishwa katika kituo kama kitovu cha shughuli kwa ajili ya ushauri wa kilimo.
- Kutoa nafasi ya kufanya majaribio ya utumizi wa ICT ili kutoa taarifa ya Kilimo kwa wakati muafaka na uenezaji matokeo ya utafiti.

Tangu mwanzo, mradi ulihusisha maarifa ya jamii katika mfumo wa uongozi. Uliunda sehemu maalumu katika maktaba ili kukusanya na kueneza habari zinazohusiana na IK, ambazo zilitumika kuongezea muitikio wa wakulima wa kijijini katika mabadiliko ya sera ya serikali ikizingatia uongezekaji wa bidhaa za kilimo katika kiwango cha mkoa. Maonyesho ya picha yalidhihirisha mbinu za asili katika uongozi wa maliasili, akiba na uenezaji wa habari na mikakati ya utumizi wa dawa ya asili.

Kwa kutumia njia ya kubahatisha kwa zaidi ya miaka mitatu, washiriki wote waliohusika walikuwa wamepata mafunzo ya kudhihirisha mabadiliko. Warsha zilizoshirikisha jamii na matembezi ya mafunzo vimefanyika ili kuwafunza wakulima vijijini kuelewa na kutarajia kufanya shughuli kwa haraka ili kutumia mbinu sahihi zinayotakiwa.

Tafiti za uwandani zilifanyika ili kubaini na kutathmini mbinu za asili za kilimo ambazo zilizingatia mifumo salama ya kilimo. Matembezi ya mafunzo yalionyesha maarifa, ubingwa na mantiki ya wakulima wadogo na masikini. Majadiliano mengi yaliyo rasmi na yasiyo rasmi yaliwezesha mawazo na uwezo wa kuongoza uchanganuzi wao.

Upatikanaji wa habari mbalimbali muhimu kwa wakati muafaka ndio njia iliyowezesha washiriki wote kufanya marekebisho yaliyobadilisha hali kuwa nzuri zaidi. Njia mbalimbali za mawasiliano kama vile mtandao, simu na faksi vilisababisha hali ambayo iliimarisha utaratibu wa majadiliano, mapatano na mawasiliano, kati ya washiriki husika. Kituo cha mawasiliano kilitumika kikamilifu kama mwezesaji kwa kuunganisha Nakaseke na sehemu nyinginezo za nchi ulimwengu na kinyume chake. Kwa mara ya kwanza, jamii ingejihusisha na majadiliano yaliyokuwa yakiendelea katika jumuia nyinginezo na kubadilishana ujuzi wao.

## Taathari

- Mawakala, vyama visivyo vya kiserikali na wakulima wamefunzwa vyema katika matumizi ya ICT.
- Taarifa muhimu za kilimo zinapatikana na kuendelezwa kwa kushirikiana na angalau taasisi tatu za utafiti. Teknolojia na mazao vinajumuisha mavuno, ndizi, kahawa, kilimo cha bustani, mazao ya mzizi na nafaka.
- Vitabu vya mwongozo, vipeperushi vya habari, karatasi za maelekezo na mabadiliko ya ujumbe vilitengezwa.
- Angalau asilimia 65 ya wakulima katika sehemu za Nakaseke na Kasangombe wameelekezwa mbinu hii na asilimia 98 ya mawakala wa kilimo na wana maendeleo wa jumua wanahusika.

Pamoja na kilimo, kituo cha Nakaseke kimeanzisha miradi mbalimbali ambayo inatumia maarifa na ubingwa wa jumua za vijijini hasa katika maeneo ya elimu, jinsia na afya. Hii inajumuisha ubunifu wa Programu ya Afya ya masafa marefu iliyoanzishwa kwa kushirikiana na hospitali ya Nakaseke. Wakati mpango huu utakapokuwa tayari, wazo ni kuwaunganisha wagonjwa kijijini na madaktari walio mjini Kampala na miji mingineyo na kinyume chake. Hili linaweza kudhihirika kuwa ni njia inayofaa ya kutangaza matumizi ya dawa za asili, jambo ambalo linatendaka kwa wingi Afrika. Vituo vya mawasiliano vinaweza kutumika kama jukwaa la kupata na kuhifadhi maarifa ya jamii na kuyasambaza toka jamii moja hadi nyingine.

## Mafunzo yaliyopatikana

Kushirikisha jamii tangu hatua za awali katika upangaji na utekelezaji wa miradi kumesaidia kueneza shughuli za vituo vya mawasiliano katika shughuli za jumua kwa ujumla. Kuifanya ICT kutumika katika kiwango cha jamii kinachoeleweka kwa wanajumuia kimesaidia kukubalika kwa dhana ya mawasiliano. Hili liliwezekana kwa kutafsiri taarifa katika lugha ya Luganda, ambayo ndiyo lugha kuu katika jamii hii. Maonyesho ya dhana mpya na programu ndio njia muhimu ya ukubalifu na uelewaji, hususan kama inawahusisha wanajamii ambao hawajui kusoma wala kuandika. Ni muhimu kuwahusisha “watoto wa sehemu husika” kuendesha shughuli za kila

siku. Wanafahamu jumua vizuri zaidi kuliko mtaalamu mwingine ye yote na wanawasiliana kwa lugha ambayo watu wanaielewa.

Nakaseke ni mfano mzuri wa mafanikio ya kuhamisha gharama za matengenezo kutoka kwa Wafadhali hadi kwa wanajamii wenyewe, ambapo, kwa kufanya hivyo panakuwepo muendeleo wa umiliki wa wanajumuia. Jumua imefanikiwa, kwa kutumia fedha zao za makusanyo ya kodi, kujenga jengo la kudumu la kituo cha mawasiliano na wametafuta njia nyinginezo za kuwezesha kazi za ujenzi. Aidha jumua imeweza kushawishi serikali kuwezesha ujenzi wa mnara wa mawasiliano ili kuwezesha uunganishaji wa zaidi ya njia za simu 50 katika eneo hilo. Hili linadhihirisha kiwango ambacho wanajumuia wanathamini umuhimu wa mawasiliano katika upatikanaji wa maendeleo.

## Changamoto katika siku za usoni

Katika hatua za uanzishaji wa kitu kipya kama kituo cha mawasiliano, kuna umuhimu wa kuweka kumbukumbu. Inaleta vifaa mbalimbali ambavyo vingetumika kika-milifu kuweka kumbukumbu za njia bora anuai za maarifa ya wanajumuia katika eneo. Utaratibu ulianza kwa mafunzo ya mbinu za tafiti za kiethnolojia na kuanzisha mbinu za kukusanya data na kuzirekodi katika benki ya data. Hali hii inapatikana kwa kutumia kanda za sauti na kurekodi mawazo kwa maandishi.

Hatua nyingine ni kuanzisha utaratibu wa kueneza taarifa, kushirikiana na kuanzisha mfumo mtandao. Utaratibu huu umeanza kwa kuongoza mahusiano ndani ya juhudi za ICT ndani na nje ya nchi. Kituo cha mawasiliano kina mpango wa kugawana mifumo ya hati na uwekaji wa rekodi na vituo vingine vya mawasiliano vilivyomo katika majaribio nchini.

Programu zaidi zinaanzishwa kueneza maarifa yaliyopatikana kutokana na kituo cha mawasiliano, ikiwa ni pamoja na biashara za jumua na mwenendo wake. Programu hiyo itawawezesha wafanya biashara waelevu na wamaizi kuthamini na kutafakari kwa makini hali ya shughuli zao kwa ujumla, wakiwa na malengo ya kuanzisha utamaduni wa kuweka akiba na kuzuia matumizi yasiyo ya lazima. Watatilia mkazo uwekaji wa rekodi na uenezi wa matendo ya ujasimali wa asili na utumizi.

# Maarifa Asilia na Sauti ya Wenyeji katika Kupigania mabadiliko huko Afrika ya Magharibi

Makala hii iliandikiwa na Peter Easton (Chuo Kikuu cha Florida) na Guy Bellonde (Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Tours). Kwa maelezo zaidi wasiliana na Peter Easton: [easton@coe.fsu.edu](mailto:easton@coe.fsu.edu).

***Tini za MA 28  
Januari 2001***

Ingawa maendeleo, maelezo na utaratibu wa maarifa asilia katika Afrika mara nyingi vinaonekana kama vipengele vya utamaduni na elimu ya ufahamu (elimu ya asili na kiini cha maarifa), wakati huohuo vipengele hivyo vina umuhimu mkubwa. Uhusiano kati ya kiini cha maarifa asilia—na watekelezaji—kwa upande mmoja na maarifa ya kimagharibi kwa upande mwingine yanadhihirishwa na hali ya madaraka makubwa/madaraka madogo, hali ambayo inabainishwa na wenyeji wa mahali wenyewe. Mpaka hapo “mapatano biashara” kati ya pande hizi mbili yatakapobadilishwa, au yatakapozingatiwa katika mfumo unaowezesha mashauriano basi ifahamike bayana kwamba hazina ya sayansi ya asili itakuwa “nje ya soko.”

## **Mbinu zilizoshindwa za kujua kusoma na kuandika**

Maelezo yatokanayo na tathmini ya utendaji unaotokana na kujua kusoma na kuandika katika nchi ya Mali miongo miwili iliyopita, yanadhihirisha hoja na kutoa fursa ya kutafakari tatizo. Katika miaka ya 1970 juhudi zilifanyika—kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Wizara ya Maendeleo Vijijini na ufadhili wa Benki ya Dunia—kuorodhesha na kutathmini matokeo ya utendaji wa miaka mingi unaotokana na madarasa ya kusoma na

kuandika katika vijiji vya sehemu ya magharibi ya nchi. Mpango wa kusoma na kuandika ulianzishwa na shirika la kilimo ambalo lilikuwa na jukumu la kuendeleza ukulima wa mazao ya chakula na biashara lengo lilikuwa ni kuwawezesha wakulima wa vijijini kuwa na imani na kuweza kuchunguza mapatano ya biashara. Matokeo yalikuwa mchanganyiko. Vipengele viwili vya “mizania” vilivyotolewa na kikundi kilichohusika na juhudi za tathmini shirikishi vilidhihirisha waziwazi hofu ya wanavijiji kuhusu uhusiano wa madaraka.

Kipengele cha kwanza kilihusu tarakimu katika mizania yenyewe. Katika mipango ya awali iliyohusisha kusoma na kuandika katika lugha ya Kibambara, ilidhaniwa kuwa kila jumua itaunda kituo cha mafunzo, kuandikisha wanafunzi kuwa na wahitimu wa naume watu wazima wapatao ishirini katika kusoma na kuandika halafu ilitarajiwa kuwa litaundwa darasa lingine na kuwafunza wengine wa idadi ileile au zaidi. Mwishoni mwa mwaka wa nne ilitarajiwa kuwa kati ya wahitimu thelathini na hamsini wangukuwa wamepatikana katika kila jumua iliyohusika.

Matokeo halisi yanaonyesha kuwa lengo hili halikufikiwa na kwa hakika baada ya uchunguzi wa kina yalionyesha tofauti kubwa. Hapakutokea mahali ambapo “wahitimu” kumi wa-

lipata mafunzo, katika eneo lote. Kwa upande mwingine, hapakutokea mahali ambapo hapakuwa na mtu ambaye hakujifunza chochote, isipokuwa katika sehemu chache ambapo kulikuwa na kushindwa kwa kiasi kikubwa. Baada ya juhudi za miaka mingi ya uchunguzi wa programu mmoja baada ya mwingine ilionyesha kuwepo kwa majigambo mengi na rekodi hafifu ya msaada wa vifaa toka katika mashirika ya serikali katika uongezekaji wa wahitimu wapya hasa kwa kadiri ya kiasi cha vijana wanne hadi saba. Kwa nini idadi hii ilikuwa ndogo au kubwa?

### Ufafanuzi wa rekodi

Jibu lilionekana kuwa katika namna ambayo matumizi halisi ya kusoma na kuandika katika lugha ya Kibambara hutazamwa kwa kuzingatia hali iliyokuwepo magharibi mwa Mali wakati ule. Ingawa programu ilitangazwa kwa majigambo mengi kuhusu umuhimu wa kujifunza na faida za kujifunza, lakini kwa hakika palikuwa na fursa ndogo ya kutumia maandishi ya Kibambara katika mazingira ya kijijini. Shule rasmi zilizomo kijijini zinatumia lugha ya Kifaransa na machapisho machache yaliyoandikwa kwa lugha za Kiafrika yangeweza kupatikana. Aidha maandishi ya Kibambara hayakutumika kwa minajili ya aina yoyote ile na ama serikali za mitaa au katika uendeshaji wa kilimo. Zaidi ya hayo hapakuwa na fursa kijijini za mikopo au uwekezaji ambavyo vingetoe fursa ya kuendesha biashara na kujitegemea.

Lakini kusema kwamba palikuwa na nafasi finyu za wahitimu wa kusoma na kuandika na kuhesabu kutumia ujuzi wao haikuwa na maana kwamba hapakuwa na nafasi kabisa. Udhhibiti wa kuendesha kodi na usimamizi wa biashara ya soko la mazao ya kilimo uliofanywa na serikali ulikuwa na mambo mawili muhimu kwa watendaji kijijini, kwa kuwa walijiona kuwa wananyonywa katika maeneo haya. Kwa mtu binafsi, usimamizi wa ulipaji kodi na biashara ya mazao hazikuwa shughuli za mara kwa mara kuhalalisha kila mtu mzima kujua kusoma na kuandika na muhimu zaidi kuweza “kuhesabu”. Hata hivyo, shughuli hizi “zilipojumuishwa’ na kukabidhiwa kwa wanakijiji wachache (hasa vijana wa kiume), zilileta manufaa kila siku na wakati mwingine ajira ya malipo yanayohititika kama kinga ya jamii wote. Kwa shughuli hiyo, watathmini waliona kuwa programu ya mafunzo katika kila kijiji baada ya kingine, imeleteleza uanzishwaji wa kikundi cha watu wanne hadi saba wajuao kusoma na kuandika ambao waliendesha na kusimamia shughuli hizi. Wanakijiji walionekana kuwa wametathmini kisahihhi ukubwa wa fursa za kutumia maarifa mapya pamoja na umuhimu wa kujitetea vyema na hivyo kurekebisha mwitiko wa programu.

Maofisa watendaji wa kilimo walijulishwa matokeo ya tathmini shirikishi ya mwaka wa kwanza iliyoonyesha ku-

wepo kwa kundi muhimu la wakulima wahitimu wa kuma na kuandika katika eneo zima. Hatua hiyo ilichukuliwa ili kuwahimiza watendaji wawape wanajumuia wa kikundi cha msukumo wa aina hii—na kudhihirisha uwezo wa kufunza idadi ya watu ambao wanajua uchumi na nafasi za kisiasa—nafasi ya kushughuhulikia mauzo ya mazao ya kilimo na kupokea na kupokea faida kubwa ya mauzo hayo kwa ajili ya kupunguza bei kwa wakulima binafsi au uwekezaji mpya katika miradi ya maendeleo inayoongozwa na wenyeji wa mahali wanajumuia. Baada ya majadiliano, mwisho makubaliano yalifikiwa katika mabadiliko haya makubwa ya sera na timu ya watathmini ilianza, mkesha wa msimu wa uuzaji wa mazao ya kilimo, kuwasilisha mawazo haya kwa utawala wa kijiji pamoja na muhtasari wa matokeo ya mzunguko wa awali wa tathmini shirikishi ya kujua kusoma na kuandika. Jitihada zilionyesha somo la pili kubwa juu ya maarifa asilia na utetezi wa pamoja.

### Kupambanua kati ya “kwa ajili ya kuonyesha” na “kwa ajili ya kuondoa”

Kwanza, ingawa neno la mazingira ya kihistoria (mandharinyuma). Wakati wa utawala wa Ukoloni wa Kifaransa, katika sehemu zote za magharibi mwa Saheli, jumua za mahali husika zilikuwa na tabia ya kushughulika na wawakilishi wa mfumo wa utawala wa serikali kuu kwa uangalifu. Kila kijiji kiliteua serikali ya vibaraka—yaani, watawala wa serikali ya mitaa ya kubuni ambao wangukuta na Wafaransa wakati wowote walipohitajiwa. Walikusanya taarifa ambazo zingewasilishwa kwa chifu wa kweli wa kijiji na washauri wake kama zingehitajika. Watawala hawa wa kubuni waliwasaidia watawala wa kweli kutojihusisha na mawakala hawa wa wakoloni. Utaratibu uliendelezwa vyema hadi wakati wa kupata uhuru, kwa sababu wawakilishi wa utawala mpya walionwa pia kama wageni au watu wenye uhasama na maslahi ya wenyeji wa mahali kuliko hata wakoloni waliowatangulia.

Mtazamo huu ulikuwa mgumu kuelezea wakati wa mwaka wa kwanza wa kazi ya tathmini katika matukio zaidi ya moja. Mtathmini mmojawapo wa Mali aliyehusika na majadiliano na mamlaka za jumua aliona kuwa neno ambalo wao walilitumia katika lugha ya Kibambara kwa ajili ya ushirika uliowekwa na serikali kuu ya kushughulikia mazao ya kilimo na mauzo lilikuwa zaidi ya lile linaloonekana kuwa—neno la Kifaransa lililopotoshwa la “cooperative” (ushirika). Aliwaomba watu warudie neno walilokuwa wanasema, alisikiliza kwa makini na kudadisi baadhi ya watu baada mjadala kumalizika. Kwa hakika watu walilokuwa wanasema lilikuwa neno “ko-fara-tinti” neno la Kibambara lililochezewa na neno la Kifaransa ambalo liliamaanisha “chuna mgongo na tumbukiza sime.” Kwa haki-

ka hayo ni maoni dhahiri yanayoeleza jinsi wanajumuia wa mahali walivyooona malengo ya sera ya kilimo ya serikali.

Kwa kuzingatia kiwango cha kutiliwa shaka, haiku-shangaza kwamba timu ya tathmini iliishia kukutana—na maneno yote mawili katika mwaka wa kwanza na wakati wa juhudi za kusambaza taarifa wakati wa mwaka wa pili—pamoja na viongozi wa vibaraka katika jamii zilizotembelewa, hata kama watu hawa hawakuheshimika kwa maofisa wa kweli. Lakini jambo muhimu lilitokea mwanzoni mwa mwaka wa pili wakati watathmini waliporudi kueleza uamuzi wa serikali kuhusu kuhamishia majukumu ya uuzaji na rasilimali husika kwa wanajamii. Mara mada hizi zilipojulikana viongozi vibaraka waliomba mkutano uahirishwe. Waliondoka kimyakimya kutoka katika eneo la mkutano na baada ya muda mfupi, walibadilishwa, kana kwamba wako katika jukwaa linalozunguka, na wenzao wapya—yaani watawala halisi wa vijiji. Kama kulikuwa na nafasi ya kurejesha madaraka na rasilimali zilizokuwa zinatolewa, basi ilikuwa busara kuleta utamaduni wa asili na mamlaka katika mizania.

### Miongo minne ya uzoefu

Somo hili linaimarishwa na ujuzi wa uendeshaji wa programu za kusoma na kuandika pamoja na kilimo kutoka nchi nyinginezo za kanda kama—Burkina Faso, Cameroon, Niger na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Mafanikio makubwa katika upatikanaji wa haraka wa haraka stadi mpya na uhamasishaji wa maarifa asilia katika juhudi zinazohusiana na maendeleo ya kitaasisi vimeshuhudiwa katika mazingira ya kudumu ya uhamishaji wa mamlaka na rasilimali na kuwekwa mikononi mwa wanajamii. Kwa hakika programu ambazo msingi wake ni miundo shirikishi ya mifumo ya maarifa na matumizi ya lugha asilia zinazohitajika ili kuendesha kikamilifu shughuli za uchumi mpya na mamlaka ya kisiasa zinaonekana kutoa chombo muafaka kwa ajili ya “kuorodhesha” na kuelezea maarifa asilia yanayohusiana kwa sababu vinatengeneza mazingira ambamo ni dhahiri au angalau (dhahiri zaidi) kwamba hazina ya utamaduni iliyochimbuliwa na kuenezwa itasaidia maslahi ya wanajamii na kubaki chini ya uhibitaji wao. Na katika mazingira haya, mafunzo ya kusoma na kuandika yanatokea kuwa chombo bora cha kuhamasisha maarifa ya jamii, kwa kuwa kinatoa fursa na njia ya “kutoa jina jipya” la maendeleo na kwa kupanga upya utekelezaji wake kwa ukamilifu.

Hali hii mathalani, ilidhihirika bayana, mahali ambapo mwandishi alishiriki katika tafiti mbalimbali pamoja na utendaji wa shughuli za biashara vijijini ambazo mwandishi alishiriki katika sehemu za katikati mwa Niger katika

miaka ya 1960, Burkina Faso miaka ya 1970, kaskazini mwa Cameroon katika miaka ya 1980 na kwa wafugaji wa Jamhuri ya Afrika ya Kati mwanzoni mwa miaka ya 1990. Katika nchi ya Cameroon palihusika na uundaji wa mfumo mpya wa uhasibu katika lugha ya Kimassa, wakati ambapo nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati ujuzi uliegemezwa katika kuwafundisha wafugaji wa Kifulani ambao walikuwa wanajua kusoma na kuandika katika maandishi ya dini kwa hati ya Kiarabu katika uandishi wa hati ya Kirumi kwa lugha yao. Mafunzo yao ya kusoma na kuandika yalichukua muda mfupi wa majuma matatu au manne ya masomo ya mwendokasi (intensive training) yaliyotayarishwa—na kusimamiwa na—watu wa mahali pale; kipindi cha ufuatiliaji wa utwaaji wa madaraka mapya na wajibu wa usimamizi kilikuwa muhimu na kilichukua muda mrefu.

### Nani anadhibiti maarifa?

Mahitimisho sawa yangeweza kufikiwa kutokana na uzoefu wa tafiti za kazi shirikishi za kilimo na upanuzi zilizofanyika nchini Mali wakati wa tathmini ya mafunzo ya kusoma na kuandika yaliyoelezwa hapo juu. Kishawishi cha washiriki wenyeji kilikuwa ni kuchukua nafasi ya kupata madaraka ya utafiti wa kilimo, wakati huo wakijifunza mbinu mpya zilizotakiwa na kutathmini hazina ya maarifa ya jiumuia ya mahali yanayoendana na jitihada hizo. Hakuna sehemu ndogo ya motisha iliyotokana na fursa ya “geuza meza” kuhusu kazi ya wapanuzi wa kilimo cha asili—ambapo, rasilimali, mbinu na mifumo viliendelea kuwa chini ya mamlaka ya mawakala wa serikali na vilielekezwa katika kuzalisha mazao, na kuweka taratibu katika vituo rasmi vya utafiti kwa ajili ya kueneza habari toka juu hadi chini kwa wakulima. Utawala wa wenyeji wa mahali uliitika ulipokaribishwa—na kuwezesha—kubuni mipango ya tafiti na kutaja majina ya watu ambao wangepata mafunzo husika. Hata hivyo, ahadi hatimaye ilidhoofishwa na upinzani mkali wa maofisa wa huduma ya upanuzi wa kilimo vijijini kwa aina hii ya ushindani na ugatukaji wa madaraka, wajibu na marupurupu yao.

Ulezaji wa maarifa asilia, kama inavyodhihirishwa na mifano ya hapo juu, ni zaidi ya “epistemolojia” (elimu ya ufahamu) na shughuli za utamaduni. Inazingirwa na maswali ya madaraka na “hadidu za biashara” kati yavyama vya mahali na vya serikali ambavyo vinaweza kuthibitishwa upya—katika mazingira mengine tofauti—na matatizo ya hati miliki na hataza ya dawa za asili au maarifa ya mapokeo ya mimea. Ubunifu wa mikakati ambayo inazingatia migogoro na kubuni uhamishaji wa madaraka na rasilimali na kutengeneza upya maarifa ya jamii ndiyo changamoto thabiti.

# Lugha za Afrika ya Magharibi: Njia na Ujumbe

Makala hii iliandikwa na Peter Easton, Profesa wa Masomo ya Uzamili katika Elimu Endelevu na ya Watu Wazima. Kwa maelezo zaidi wasiliana naye kwa barua pepe: [easton@coe.fsu.edu](mailto:easton@coe.fsu.edu)

***Tini za MA 29  
Februari 2001***

Maarifa asilia katika Afrika na duniani kote, yanaelekeza katika lugha, na hasa lugha za “asili” kwa ufupi lugha mama za wakaazi wa sehemu husika, au lugha ya mawasiliano wanayoitumia katika maisha yao. Je lugha hizi hazina sifa zinazobainika kimawasiliano? Je, lugha hizi ni “chombo” kinachotumika kuelezea maarifa na maisha ya kila siku? Au lugha hizi zenyewe zina dhima maalumu, kwa kuzingatia muundo na matumizi yake katika yanayofikirika na yanayojulikana?

Lugha ni muhimu katika Afrika. Kuna zaidi ya lugha 2000, katika bara la Afrika, idadi ikitofautiana kutokana na dhima ya jinsi lugha hizi zinavyochukuliwa katika ukaribu wake au uhusiano wake. Tamaduni za Kiafrika zimekuwa kwa kiwango kikubwa za masumilizi kwa karne nyingi ingawa pamekuwepo aina fulani za uandishi (wa kimagharibi, Kiarabu na misimbo michache ya asili ya Kiafrika) ambayo imejulikana kwa kiasi kikubwa. Katika sehemu kubwa, hadhi ya dhima ya “migambi” inarasimishwa katika hali ambayo tabaka lote la wenye hadhi wanajizatiti maisha yao katika kuji-funza na kutongoa kimasimulizi historia na utamaduni wa sehemu husika na wakazi viongozi. Utamaduni wa kiafrika hasa hutilia mkazo ma-

husiano ya jamii na mawasiliano, yote haya yakijumuisha dhima muhimu inayofanywa na lugha katika mpangilio wa jamii na maarifa.

Mifano itakayotolewa katika makala hii inatokana na lugha ya Kihansa, lugha ya pili kwa ukubwa katika Afrika (baada ya Kiswahili) na ni jamii ya lugha za “kichadic”. Lugha hiyo ya Kihansa inazungumzwa kaskazini mwa Nigeria na katikati ya Niger, lakini pia inatumika katika nchi nyinginezo za kanda hiyo. Ruwaza za lugha hii zinawakilisha utamaduni wa lugha nyingi za Afrika ya magharibi na kati.

## Lugha kama “mtaji”

Wazungumzaji wa Kihansa hulipa kila tamko la lugha umuhimu kama ilivyoelezwa hapo juu. Kama msemu wa kiutamaduni ujulikanavyo *Magana jari ce* “lugha ni mtaji”. Katika isitilahi za Kihansa, neno *hausa* lenyewe halina maana ya lugha ya kundi lizungumzalo lugha hiyo, bali “lugha” kwa ujumla na “lugha” kwa maana ya ndani. Watu watauliza *Me ne ne Hausarka?* “Unazungumza lugha gani” Au kwa fasili ya jumla *“Hausa yako ni nini?”* “*Ban gane ba hausarshi*” ndiyo njia ya kawaida ya kusema “Sielewi ana maana gani.”<sup>1</sup>

1. Lugha ya Hausa ya kaskazini inatumiwa katika mifano na misemo yote.

Viwango vitatu vya lugha ya Kihausa vina uhusiano na namna mawazo yanavyoundwa na jinsi maarifa yanavyoelezwa: sarufi ya lugha, isitilahi na ruwaza jamii zinazotawala matumizi yake.

### Muundo wa ndani wa sarufi?

Kimojawapo cha kumshangaza mtu asiyejua lugha ya Kihausa—na hasa asiye Mwafrica—ni kuwa mfumo wa kitenzi haukupangiliwa katika njeo. Kwa maneno mengi, maelezo muhimu ambayo huibuliwa na muundo wa sarufi wa kifungu kitenzi ni mdogo *wakati* kitu kilipotokea au kitakapotokea kuliko *kwa vipi* kitendo hicho kinaonwa na watu wanaohusika na wanakikusudia nini. Ingawa mgawanyo wa kitenzi unaendana kwa kiwango fulani na njeo za lugha zisizo za Kiafrika, zinaelezwa vizuri kama “hali” (aspects). Kitendo kinagawanywa kiisimu katika vipengele vilivyoorodheshwa hapa chini.\*

Kwa kurudia, maelezo muhimu yanayotolewa na mgawano huu wa “HALI” katika kitenzi unahusu mwelekeo wa makusudio na sharti linalohusu tendo na sio muda, hata kama anayeondoka nyumbani atawaambia wenyeji wake Naa—ambalo, likitafsiriwa kama tamko la muda, litatambulisha “Nimeondoka.” Hata hivyo kinachomaanishwa ni kuwa mtu ameamua kuondoka na hivyo tendo ni kama limetendeka katika eneo la kusudio.

### Kutilia maanani kusudio

Kanuni muhimu ya mzungumzaji wa Kihausa kwa kawaida ni hali ya ahadi au nia ya kutenda jambo na

utaratibu ya uamuzi wenyewe badala ya kuwa na tarehe kamili na muda wa kutenda tendo lenyewe. Wazungumzaji wa Kihausa wakati mwingine huelezea kukatishwa tamaa kwao na watu wa Ulaya kwa matumizi ya neno “labda” (watakila kwa Kihausa) katika mazungumzo na mipango yao. Hali hiyo inaonekana kana kwamba wanakwepa kutoa ahadi. Msemo upendwao unaeleza jambo hili bayana: *Watakila abin da ya hana ma nasara karya!* “labda ni neno ambalo linawaokoa “linazuia” watu wa ulaya kutodanganya.

Utaratibu huu wa maelezo unaepuka msisitizo wa ratiba na muda, na mipango ya nyakati imekuwa muhimu katika maisha ya Wasaheli katika nusu karne iliyopita. Wakati huo huo, taswira hii au “kielelezo” haiwezi kuchukuliwa kihafifu katika mazingira ambapo utaratibu wa kufuata muda umekuwa hautabiriki na ahadi zimekuwa muhimu katika kutenda jambo—na inaweza pia kuwa na uhusiano katika matakwa ya baadaye katika jamii ya Kiafrika.

### Matumizi ya maneno yanapostahili

Dhana kuwa lugha haielezi mawazo tu, bali pia huiunda au kuiathiri kwa kiwango fulani, ina historia ndefu katika isimu za kimagharibi na mawazo ya kiutamaduni kiasi cha kuzua mjadala mkali hadi leo. Benjamini Lee Whorf na Edward Sapir walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza walioibua mjadala huu. Hadi sasa mjadala huu ujulikanao kama nadharia tete za Wharf-Sapir bado umeibua mjadala mpevu. Bila kuingilia mtazamo huo kwa undani, tunaweza kuzingatia dhana kuwa muundo

Hali ya kitenzi	Mifano kirai cha Kihausa	Maana katika Kihausa	Ulinganifu Na maana	Kiingereza Njeo
Kamilifu	<i>Yaa tahi</i>	Uondokaji wake unaweza kuangaliwa kama uliotendeka (limekamiliwa ahadi)	“Aliondoka”	Njeo iliyopita
Endelevu	<i>Ya naa tahiya</i>	Yuko katika hali ya kuondoka au kwenda (lengo liko katika hatua ya kukamilishwa)	Anaondoka au anaenda	Njeo iliyopo
Kusudio	<i>Zay tahiya</i>	Anapanga kuondoka au kwenda	Ataondoka	Njeo ijayo
Uwezekano	<i>Yaa taji</i>	“Anaweza kwenda” (Nia yake ni ya kweli bali sharti)	“Ataondoka kama mambo yote yatakuwa sawa”	Njeo ijayo dhaifu
Kusudio	<i>Ya tayi</i>	Lazima aende (malengo yake yako wazi lakini hayajatekelezeka)	Anaweza kwenda	Dhamira tegemezi
Mazoea	<i>Ya kan tahi</i>	Ana mazoea ya kwenda	Huenda	

\*Uandishi wa maneno na misemo ya Kihausa uliotumika katika makala hii kwa ujumla ni ule ambao kwa sasa hivi umependekezwa na UNESCO, jedwali na kifungu cha maneno kinachofuata ni mfano mmojawapo. Sauti za kuvuta zimewakilishwa kwa kutumia vaveli mbili kwa sababu hakuna namna nyingine rahisi ya kuonesha tofauti za hali za vitenzi. Sehemu ya “bonyeo” la matamshi linaonesha sauti ya chini na matamshi ya namna hiyo katika vaveli ya pili katika kundi inaonesha sauti inayoshuka.

wa lugha ni sehemu kamili ya maarifa asilia na dhana ambayo inapaswa kuchunguzwa na kupendelewa—katika jaribio la kuihifadhi.

Wharf mwenyewe hakushughulikia tu muundo wa lugha bali pia sifa za kileksika yaani, msamiati na hasa tofauti kati ya maeneo ya ujuzi ambayo huelezwa kwa kina katika lugha kwa msamiati wake. Alikuwa anapendelea kutoa mfano wa lugha za Kieskimo ambazo zina msamiati mpana kuhusu theluji lakini wakiwa na msamiati mmoja tu unaohusu magari; wakati ambapo ni kinyume katika Kiingereza. Wapinzani wa hoja hizi wameonyesha kuwa mashabiki wa skii wana maneno lukuki ya Kiingereza kuhusu hali ya theluji. Hata hivyo wazo kuwa maendelo tofauti ya maeneo ya ujuzi katika utunzi wa msamiati katika lugha yanaeleza mengi kuhusu tofauti ambazo ni muhimu kwa wazungumzaji wa lugha na hivyo mawazo haya yanahitaji kuzingatiwa.

Uperuzi wa kamusi ya Kihansa unaonyesha mawazo yanayoshabihiana na mawazo hayo juu. Kuna maneno machache sana yanayohusu magari lakini isitilahi zianzoelezea mahusiano ya watu na tabia mbalimbali za watu ni nyingi. Mifano mitatu ni muhimu hapa: (a) *nurkur-kusa*—neni ambalo linaweza kuelezwa kama “kupuuza kumlipa mtu (deni); *kwakyara* lenye maana ya “kuropoka jambo ambalo lisingepaswa kusemwa”; na *santi* (au *fanya*) ambalo linaonyesha “kusema kitu cha kawaida wakati wa chakula cha pamoja, kwa sababu ya furaha itokanayo na utamu wa chakula, jambo ambalo humfanya kila mmoja kucheka sana”!

### Ubunifu wa msamiati

Lugha yo yote ya Kiafrika inaweza kutumiwa kusema lo lote mtu atakalo, na kusilimisha mawazo mapya yaani kubuni msamiati. Msamiati au istilahi ziko chache katika lugha hizi kuliko za Kiingereza, Kifaransa au Kichina mifano ambayo wana sayansi jamii huita “ubunifu wa msamiati”. Lugha ya Kihansa ina uwezo huo pia. Istilahi mpya zimeundwa kwa miaka mingi, kuelezea dhana mpya wakati mwingine zikiibua hadhi ya kishairi. Umoja wa Mataifa ulipewa jina la utani la *majalisar dinkin duniya* au “baraza la kuunganisha (kushona pamoja) dunia.”

Pikipiki ndogo ya Kifaransa ya Solex iliitwa kwa Kihansa *kare ya dauko tuknya* “mbwa aliyebeba chungu cha kupikia” Pikipiki hiyo ina dubwana lenye mnyororo uliofungwa mbele ya taili la mbele na linaendeshwa kwa msuguanu. Na pikipiki kubwa zaidi “mobylette” ilibatizwa jina linaloendana na mlio wake (onomatopia) *dan bututu*. Kuna Baraza la Kihansa huko Nigeria ya Kaskazini ambalo linashughulikia uundaji wa msamiati

wa Kihansa wa mawazo mapya kama Baraza lile la Kifaransa—Académie française. Lakini kiutamaduni wanajamii lugha waamuapo kuwa na msamiati mmoja badala ya maelezo marefu inayonyesha mawazo na taswira yanayojirudia mara nyingi katika ruwaza ya mawazo na misemo.

### Tabia za semi

Kama lugha ina athari katika mawazo na usemaji, basi inarithiwa pia na ruwaza za matumizi—dhima za watu katika utumizi wa lugha na namna waitumiavyo. Haya hasa yamo katika tanzu ya wana isimu jamii. Deborah Tannen ameandika makala kadhaa zijulikanazo Marekani kuhusu tofauti za tabia za uzungumzaji kati ya Waamerika wanaume na wanawake. Aidha Tannen amelezea tofauti bayana ya kijinsia katika udakiaji (interruptions) na upishanishaji (overlapping); kukatiza mtu mwingine asemayo au kumalizia kwa niaba yao. Kwa ufupi, kwa wanaume inaonekana kuwa ni uchokozi na tendo la ushindani, wakati kwa wanawake linaonekana kama ni tendo la kuunga mkono.

Kipengele muhimu cha ruwaza za mawasiliano kati ya Wahansa ni marudio—na dhima ya mapishano yanayofanana. Mwandishi alikuwa wakati fulani amepewa jukumu la kunukuu neno kwa neno kumbukumbu za mkutano wa kijiji ulioendeshwa kwa Kihansa kuhusu ufugaji. Baada ya kunukuu majadiliano yote na kuanjikwa katika karatasi, jambo la kushangaza lilitokea, jambo ambalo wote tunalifahamu lakini lilikuwa halijazingatiwa kwa makini. Mapendekezo muhimu kuhusu namna ya kutunza ng’ombe kijijini na kuwapatia majani yalijadiliwa (jambo ambalo si la kiutamaduni katika kijiji hicho). Baada ya kuangalia nukuu na kusikiliza kanda kwa makini; ilibainika kuwa hapakuwa na hata mtu mmoja aliyemalizia hoja kikamilifu kuhusu mada hiyo. Badala yake ama mtu mmoja angetaja sentensi au wazo, mtu mwingine ajengejazia wazo hilo, na mtu wa tatu angelisema wazo lile lile vinginevyo. Majadiliano hayo yaliendelea hivyo hivyo pasipokuwana hoja kamilifu iliyotolewa na mzungumzaji mmoja wapo. Lakini katika mfumo huu wa mawasiliano, mawazo mazuri na maazimio yalitolewa.

### Kutoka maneno kwenda kwenye ufanisi wa kiutendaji

Kuna kufanana kwa utaratibu wa kikundi au uhusiano katika maisha ya jamii ya eneo hili. Hadithi nyingine itaonyesha jambo hili. Katika hali inayofanana mwandishi wa makala hii aliwajibika kuonyesha filamu



ya projekta ambayo ilikuwa haijawahi kuonwa katika mji wa Madaoua, Niger. Ilihitajika genereta kwa kuwa hapakuwa na umeme katika mji huu. Kwa bahati mbaya, kutokana na mwendo wa barabara yenye urefu wa km 500, mashini hii haikufanya kazi. Msaada pekee ilikuwa ni gereji ya wilaya mahali ambapo vijana mekanika wasio na viatu walifanya kazi katika kibanda nyuma ya ofisi za serikali. Vijana hawa walikuwa na vifaa vichache vya kutengeneza magari ya Lendrova.

Makenika hawa walikubali kutusaidi lakini mara walipoanza kazi hiyo wasiwasi wetu uliongezeka. Kundi lao la vijana watano hadi sita walianza kufungua sehemu mbalimbali za chombo hicho, wakivuta hiki na like kuelekea pande mbalimbali, wakati huo huo wakibishana kuhusu wafanyalo. Wakati huo tuliona kuwa uhai wa projekta ulikuwa umetoweka. Lakini baada ya dakika kumi na tano projekta ilikuwa imetengamaa kabisa. Kwa namna fulani walikuwa wameweza kutumia ujuzi na

kipaji chao chote kilichojadiliwa kwa kutumia lugha kushughulikia tatizo ambalo walikuwa hawajapambana nalo kabla. Katika nyakati ambapo biashara ya kimataifa inadhihirisha matatizo (na hasa kasoro) ya ujuzi wa kazi ya pamoja, matendo haya, ambayo kwa kiwango fulani yamefungamanishwa katika muundo na utumizi wa lugha, yanaweza kuwa na manufaa.

### **Jambo la kuzingatia**

Mifano hii ya matukio haya isichukuliwe kwa dhahiri sana au kupewa umuhimu mkubwa. Hata hivyo jambo linaloelezwa hapa na ujuzi, vinapaswa kupewa uzito wa kutosha kwa wale ambao wako makini na maarifa asilia: sehemu ya maarifa hayo imo au inajitegemeza katika mawasiliano ya lugha yenyewe.

## Maarifa Asilia na VVU/UKIMWI

Makala hii imeandikwa na Maja Naur, PH.D katika sosholojia, mshauri wa Benki ya Dunia. Miradi iliyohusika ni: Zambia: Programu ya Msaada wa Mazingira, ripoti Nam. 16239, na Ghana: Mradi wa uhifadhi wa Bioanuwai ya Savana ya Kaskazini, makala ya mradi wa kuombea fedha kutoka Global Environmental Facility Trust Fund Mwandishi anapenda kuwashukuru Mameneja wa kazi maalumu, Yves Prevost na Hassan M Hassan na bila kumsahau John Lambert kwa kazi yake kuhusu mitishamba ya dawa. Tafiti za kijamii kuhusu miradi hiyo zimefanywa na mwandishi na kugharimiwa na Danish Trust Fund. Kwa taarifa zaidi, baruapepe:MAJANAUR@msn.com.

### **Tini za MA 30 Machi 2001**

Kwa kawaida imekuwa vigumu sana kuwapatia msaada wa maendeleo watu masikini, hasa inayohusu afya ambapo misaada mingi inawafikia watu wa tabaka la kati katika hospitali za mijini. Kwa watu maskini wa vijijini na zaidi na wa mijini nao, mara nyingi huduma ya afya wanaoweza kuimudu na inayopatikana kwa urahisi ni kwa waganga wa jadi. Zambia yenye wastani wa asilimia 20-25 ya wananchi wenye virusi vya UKIMWI, ina madaktari 900 waliosomea nchi za magharibi (600 kati yao ni wageni) lakini ina waganga wa jadi 40,000 waliosajiliwa kwa watu milioni 10. Ghana yenye asilimia 5 ya wananchi wenye Virus vya UKIMWI, ina madaktari 1,200 waliosomea nchi za magharibi, ingawa ina takribani waganga wa jadi 50,000 kwa watu milioni 20. Kwa hiyo uwiano wa daktari kwa mganga wa jadi ni 1:44 nchini Zambia na 1:42 nchini Ghana. Kwa kuzingatia jukumu muhimu la kiutamaduni la waganga wa jadi katika jamii, wanatoa moja ya matumaini mazuri ya kutibu na kupunguza kasi ya kuenea kwa UKIMWI. Lakini waganga wa jadi wanategemea sana mitishamba na kumekuwa na kupungua kwa kasi kwa aina nyingi za mitishamba muhimu kwa kuwa mazingira yao yanatoweka kutokana na ukataji misitu, kilimo, ulishaji mifugo kupita kiasi, uchomaji moto, ukame,

jangwa, nk. Tatizo hili limeongezwa na mahitaji yasiyodhibitiwa ya nchini na ya kimataifa ya mitishamba.

Aidha waganga wa jadi, wameainisha kama suala muhimu, kupotea kwa maarifa asilia kuhusu dawa za asili, ambayo ni sehemu ya urithi wa kitamaduni wa jamii na kwa kawaida hurithishwa kwa njia ya masimulizi.

Mara nyingi elimu hii inadharauliwa na vizazi vipya, huenda ni kutokana na dawa za asili kutowapatia kipato kikubwa waganga wa jadi.

Kwa kutambua umuhimu wa kulinda na kuhifadhi maarifa haya ya tiba asili, na aina za mitishamba inayotegemea, serikali za Zambia na Ghana kwa msaada wa Benki ya Dunia, zimo katika utaratibu wa kuweka kiungo kati ya mazingira na afya katika kupambana na VVU/UKIMWI. Nchini Zambia asasi ya utendaji ni Chama cha Waganga wa Jadi wa Zambia (Traditional Health Practitioners Association of Zambia-THPAZ) kupitia Programu ya Msaada wa Mazingira (ESP), chini ya Wizara ya Mazingira na Maliasili. Nchini Ghana, juhudi zitakuwa sehemu ya Mradi wa Uhifadhi wa Bioanuwai ya Savana ya Kaskazini. (Northern Savanna Biodiversity Conservation Project-NSBCP), chini ya Wizara ya Ardhi, Misitu na Migodi.

Kimsingi miradi miwili hiyo ina mwelekeo mmoja ingawa inatofautia-

na katika mpango. Nchini Zambia mradi umeingizwa katika programu iliyokuwepo hali ya kuwa nchini Ghana, shughuli zitakuwa sehemu ya mpango wa mradi unaoendelea. Kinachofuata ni kwanza kuwa na muhtasari wa msaada wa UKIMWI unaowahusisha waganga wa jadi chini ya programu ya ESP-Zambia; pili ulinganishaji wa matokeo ya utafiti wa utamaduni-jamii hasa kuhusu tofauti za kijinsia zinazohusiana na dawa za asili katika nchi mbili hizo; na tatu, baadhi ya matatizo yaliyojitokeza wakati wa mchakato wa kuanzisha mradi unaohusisha sekta nyingi zikiwemo kilimo, mazingira, afya na maendeleo vijijini.

Katika mradi wa Zambia, "Ulinzi na Matumizi Endelevu ya Bioanuwai kwa ajili ya Dawa: Mradi wa Kupambana na VVU/UKIMWI" kuna shughuli kuu tatu. Shughuli ya kwanza, "Uhifadhi wa Bioanuwai kwa ajili ya Kinga na Tiba" inajumuisha kuanzisha bustani za mimea, misitu ya akiba kwa ajili ya mitishamba na hifadhi ya mitishamba iliyokaushwa. Baadhi ya mbegu, vipandikizi, na mizizi ya viazi kwa ajili ya kupanda, vitatoka katika misitu ya mizimu yenye bioanuwai nyingi na mimea na miti adimu, iliyohifadhiwa kutokana na sheria, kanuni na miiko ya kimila inayohusishwa nayo.

Shughuli ya pili "Mafunzo na kujenga Uwezo" inawalenga waganga wa jadi na inajumuisha orodha ndefu ya mada zinazoanzia ubadilishaji wa tabia kuhusiana na VVU/UKIMWI, kuelewa mifumo-ikolojia, lishe, maarifa asilia na athari za sumu, elimuvirusi ya msingi, magonjwa ya mlipuko na elimu ya kingamaradhi. Zaidi ya vipengele vya mazingira na tiba, kutakuwa na mafunzo ya sheria ili waganga wa jadi wasivunje sheria, kama vile sheria ya Uchawi, na kuelewa vizuri haki za binadamu.

Shughuli ya tatu "Uenezaji wa Taarifa/Elimu kuhusu Bioanuwai na VVU/UKIMWI" itaweka mkakati wa mawasiliano utakaotekelezwa kwa njia ya vijarida, vipindi vya redio, TV, Maigizo/Michezo ya kuigiza na vipeperushi. Shughuli hii itajumuisha pia kituo cha taarifa na takwimu kuhusu mitishamba ya dawa na uchapishaji wa kiongozi kwa ajili ya waganga wa jadi watakachokitumia katika shughuli zao. Vifaa vyote vya mafunzo, vipindi na machapisho vitakuwa kwa lugha kuu za wenyeji, pia kutaendeshwa masomo ya msingi ya kusoma, kuandika na hesabu ili kuwawezesha waganga wa jadi (ambao mara nyingi hawajui kusoma) kuwasajili wagonjwa wao na kuandika maarifa yao asilia.

Wakati uchambuzi wa jinsia umekuwa muhimu kwa upangaji wa mradi Zambia na Ghana, majukumu ya wanawake yanatofautiana katika nchi mbili hizo. Kwa ujumla mgawanyo wa majukumu kijinsia umekuwa na nguvu zaidi Ghana kuliko Zambia. Hii imeleta athari katika nafasi ya waganga wa jadi wanawake pamoja na uwezo wao wa kushiriki katika shughuli za mradi: Baadhi ya tofauti za kiu-

tamaduni-jamii zinachambuliwa. Nchini Zambia, waganga wa jadi wamepata msaada wa wahisani ili wajiunge kitaifa, na asilimia 60 ya waganga wa jadi waliosajiliwa ni wanawake. Idadi ya waganga wa jadi wanawake inaongezeka sawa na ongezeko la wagonjwa wa UKIMWI.

Wenyeji wanaita maambukizi ya VVU/UKIMWI "Kalaye noko", ikiwa na maana "nenda kaagane na mama yako," kwa sababu watu wengi wanakufia vijijini kwenye nyumba za mama zao.

Ingawa wanawake nchini Ghana pia ndio wanaowatunza wagonjwa, tofauti ni kubwa inapofika kwenye uganga. Nchini Ghana hakuna chama rasmi cha waganga wa jadi cha kitaifa, na mikoa mitatu ya kaskazini ina chini ya moja ya tano ya waganga wa jadi waliosajiliwa. Kati ya wanachana (wachache) waliosajiliwa, wanawake ni chini ya asilimia 10, isipokuwa kwa mkoa mmoja mdogo ambako mganga mmoja wa jadi amefanikiwa kuongeza kiwango kufikia asilimia 49. Hata hivyo, idadi ndogo nchini Ghana inaonyesha imani za wenyeji zaidi kuliko idadi halisi ya waganga wa jadi wanawake. Aidha, mradi huu unaofadhiliwa na Benki umekuwa ukiimarisha ubaguzi wa jinsia bila kutegemea, kwa mfano, kuwafunza waganga wa jadi waliosajiliwa tu, ambao wengi wao ni wanaume. Kwa mujibu wa mganga mmoja wa jadi mwanamke nchini Ghana, wanawake iwapo wanafanya uganga wa jadi "wanaitwa wachawi na kila mkosi wanatupiiwa wao; mara nyingi wanawake hawa wanalaaniwa na kutengwa nje ya jamii zao. Ndio maana ni malikia wa wachawi tu ndiye anayeweza kutibu, kwa sababu ana uwezo mkubwa usioweza kufikiwa na mtu mwingine yeyote katika jamii".

Katika nchi zote mbili hizo ni nadra sana kukutana na mganga wa jadi aliyelima mitishamba ya dawa, na iwapo atatokea, itakuwa mradi uliofadhiliwa na wahisani.

Nchini Zambia waganga wa jadi wanawake wanasemekana kuwa wanaongozwa na mizimu kwenye mitishamba iliyokusanywa na kutayarishwa kwa dawa kwa ajili yao. Nchini Ghana kuna ubaguzi wa kijinsia kuhusiana na ukusanyaji wa mitishamba, utayarishaji wa dawa na hata ujinsia, uliowasaidia sana wanaume kuliko wanawake. Wanawake waganga wa jadi wachache sana nchini Ghana wameolewa kuliko wanaume, ambapo mwanamke mmoja mganga wa jadi ameeleza kwa kusema kwamba, asingeweza kutibu iwapo mume wake angeishi naye. Aidha waganga wa jadi wanaotumia tambiko za dini za asili za Kiafrika katika matibabu hawawapeleki mabinti wao porini kwenda kuchuma mitishamba, "kwa sababu watu wata dhani kuwa ni wachawi. "Hata waume wao hawatawaruhusu wake zao kusaidia kutayarisha dawa "kwa sababu dawa haitafanya kazi" iwapo itatayarishwa na mwanamke. Uhalali uliopo kwa mwiko huu ni mfumo dume na urithi wenye maana kwamba mwanamke anapolewa ata-

hamia kwa mume, na kwamba maarifa ya siri ya familia kuhusu mimea na manufaa yake kwa matibabu, yatakuwa hatarini kufahamika na familia nyingine.

Waganga wa jadi nchini Ghana hawako tayari kuwafunza mabinti wao dawa za asili, hata hivyo wasichana wana macho na masikio, na wanawake wengi wanafanya matibabu ya asili ingawa ni kwa siri sana. Hali hiyo, bila shaka ina athiri uamuzi wa wanawake kwa uongezaji pato kwa uganga. Ni wakunga wa jadi peke yao ndio wanawake peke yao; na wengi wao walipata malipo kidogo, kutokana na huduma zao. Lakini waganga wengi wa jadi wanapata kipato kutokana na kilimo na malipo ya uganga yalikuwa kwa njia ya mazao kutoka shamba.

Nchini Zambia kuanguka kwa uchumi kumefanya waganga wengi wa jadi kuacha kulipwa vitu, na waganga hao sasa wameamua kutoza gharama ya fedha kulingana na aina ya ugonjwa. Gharama kubwa ilikuwa kwa tiba ya utasa, ambayo hutolewa baada ya kuzaliwa mtoto wa kiume.

Nchini Ghana, mgawanyo wa kazi unatoa nafasi ya pekee kupitia kwenye mradi kuwasaidia wanawake na familia zao katika kinga ya VVU/UKIMWI na uondoaji umaskini na hivyo kuimarisha matarajio ya mafanikio ya mradi kwa ujumla. Lengo la muda mrefu la uhifadhi wa bioanuwai litakuwa ndoto kwa jamii zinazokabiliwa na upungufu wa chakula na njaa; hata hivyo shughuli za uzalishaji mali za muda mfupi kwa kulima na kuuza mitishamba na mboga na hivyo kuboresha afya ya watoto ni changamoto kwa mafanikio ya mradi.

Waganga wa jadi, wanawake na wanaume, wameonyesha shauku kubwa ya kutaka mafunzo ya kuboresha kazi yao ya uganga. Nchini Ghana, vipindi vya mawasiliano kwa umma kuhusu VVU/UKIMWI vimefanikiwa katika kueneza habari kuhusu maambukizo ya ugonjwa huo kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia ya damu, kujamiiana, sindano zilizoambukizwa na kadhalika. Lakini elimu ya jamii kuhusu namna unavyoambukizwa mara nyingi si kamili wala sahihi. Baadhi ya jamii zimehusisha hatari ya maambukizo kwa kula au kuoga na mtu aliyeambukizwa UKIMWI; hata kupeana mikono au kutumia nguo za mgonjwa vilitajwa kuwa vinaweza kuambukiza. Hakuna hata jamii iliyokiri kuwepo kwa wagonjwa wa UKIMWI kijijini kwao, na nchini Ghana na Zambia mnyanyapao ulielekezwa kwa watu wenye UKIMWI. Kwa hiyo, watu hawakukiri maambukizo na kuona maambukizo ya VVU/UKIMWI kama maradhi ya kawaida tu ingawa ni ya hatari.

Umaskini na desturi na mila za kitamaduni pia hulifanya bara la Afrika liwe na uwiano mkubwa wa wanawake walioambukizwa UKIMWI kuliko wanaume. Katika vita dhidi ya UKIMWI waganga wa jadi wanahitaji

mafunzo kwa kuwa wanawahudumia asilimia 70 ya watu. Aidha wakunga wa jadi, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, wanazalisha asilimia 95 ya watoto wa maeneo ya vijijini na hivyo kuwafanya wawe watoa huduma muhimu, ingawa pia wanawafanya wawe hatarini kuambukizwa VVU/UKIMWI. Hatimaye, muundombinu wa afya unaotolewa na waganga wa jadi na asasi zao utaupatia mtandao wa usambazaji dawa za UKIMWI baada ya kupatikana kwa bei nafuu. Waganga wa jadi wana nafasi ya pekee kama waelimishaji na wasambazaji wa dawa za UKIMWI—kwa mfano katika kusimamia dawa alizoandikiwa mgonjwa. Hakuna hata nchi moja ya Afika yenye fedha au wafanyakazi wa afya wa idadi inayotakiwa kupambana na ugonjwa thakili wa UKIMWI.

Serikali za Ghana na Zambia hazivasaidii kifedha waganga wa jadi kama wanavyovisaidia vyama vya matibabu ya kisasa, na wala tiba ya asili haikuingizwa kwenye mitaala ya vitivo vya tiba katika nchi mbili hizo. Kwa upande huo, nchi za Kiafrika hazilingani na nchi kama China na India ambapo tiba mbadala ni sehemu ya tiba ya kisasa inayofanywa katika hospitali. Hata hivyo Ghana na Zambia zina wafanyakazi katika wizara zao za Afya, kuratibu sera kwa waganga wa jadi, na nchi zote hizo zinataka waganga hao wasajiliwe. Ghana imeonyesha mwelekeo mzuri wa uhifadhi wa mitishamba na imekubali huduma ya waganga wa jadi kwa kupitisha sheria ya Tiba ya Asili, mwaka 2000. Nchini Zambia, kwa upande wake, ilikuwa mpaka zaidi ya moja ya tano ya watu walioambukizwa UKIMWI ndipo waganga wa jadi walipoalikwa wawe sehemu ya Kamati ya Wataalamu kuhusu Tiba za Asili kwa UKIMWI na magonjwa mengine husianifu chini ya Ofisi ya Rais. Wizara ya Mazingira na Maliasili ambapo ESP iko chini yake, mwanzoni haikuwa tayari kushirikisha jamii ya kiraia katika usimamizi wa maliasili hasa THPAZ, ambayo ni asasi kubwa isiyo ya kiserikali nchini. Waganga wa jadi wenyewe wameonekana wamepitwa na wakati na hivyo watengwe katika mipango ya maendeleo. Hali ya kusita pia, ilikuwa nayo Benki ya Dunia ambapo tiba ya waganga wa jadi ilionekana kukosa uthibitisho wa kisayansi na uhalali. Maoni ya namna hiyo pia yalienea miongoni mwa madaktari wa tiba ya nchi za magharibi, ingawa tiba ya jadi ni ya kale kuliko tiba ya kisasa kama ilivyo kwa matumizi ya mitishamba na mimea ya tiba ni ya kale kuliko matumizi ya sasa ya dawa. Hata hivyo hali hii imebadilika hatua kwa hatua na hivi sasa inakubaliwa kuwa juhudi kama vile zinazofanywa Zambia na Ghana zinawanufaisha maskini moja kwa moja na zina uwezekano mkubwa wa kutibu maradhi yanayohusiana na UKIMWI.

# Kijiji cha Malicounda–Bambara: Matokeo Safari ya Mapinduzi ya Wenyeji

Makala hii imeandikwa kwa pamoja na Peter Easton, Profesa Mshiriki, Mitaala ya Digrii katika Elimu ya Watu Wazima na Elimu Endelevu, EFPS na Dkt. Karen Monkman, Profesa msaidizi wa Elimu ya Kimataifa, wote kutoka Chuo Kikuu cha Florida.

**Tini za MA 31  
Aprili 2001**

Katika kipindi cha takribani miaka minne, harakati za wananchi za kukomesha ukeketaji wanawake zimeenea kutoka kijiji kimoja cha katikati ya Senegali hadi zaidi ya jamii 200 tafa zima, pamoja na nchi nyingi za Kifrika. Mbinu na utaratibu wa uenezaji wake zinaacha mafunzo na maswali mengi kuhusu namna utamaduni wa asili unavyojirekebisha upya.

Uzoefu wa kijiji cha Malicounda-Bambara katika jimbo la Thies la katikati ya Senegali na matokeo yake yalisimuliwa katika toleo la awali la Tini za MA (“Wanawake wa Senegali wanaunda upya Utamaduni Wao” Oktoba, 1998, Nam. 3). Lakini “kisa kizima kimekuwa na mafunzo makubwa.

Muhtasari wa upeo wa juhudi zeneye na matukio makubwa yaliyounda matokeo yake, vitasaidia kudhihirisha kisa cheneye.

## Wakati wa kubuniwa

Kati ya mwaka 1995 na 1997 wanawake na wanaume wachache katika kijiji cha Malicounda-Bambara walishiriki katika programu ya elimu isiyo rasmi iliyofadhiliwa na “Tostan”, Asasi Isiyo ya Kiserikali yenye maskani yake Senegali. Programu hiyo ilihusu mbinu za kutanzua matatizo, mada za afya ya wanawake na haki za

binadamu, na uanzishaji masomo ya watu wazima—kusoma na kuandika.

Washiriki wa Malicounda-Bambara waliamua kuwa na lengo la kipaumbele zaidi ya utayarishaji wa shughuli za uzalishaji mali, uanzishaji wa programu za mtoto bora, kuanzisha miradi ya afya na usafi vijijini na kadhalika: kukiwezesha kijiji Chao kukomesha kabisa ukeketaji. Watu wa Bambara ni miongoni mwa makabila madogo ya Senegali yanayofanya mila ya ukeketaji.

Wakati wa mafunzo, wanawake walibadilishana uzoefu wenye mawimvu makubwa kuhusu mada hii ambayo ni mwiko na kukabiliwa na hisia za mara kwa mara za haki za wanawake. Matokeo yake walionana na viongozi wa serikali za mitaa na wanavijiji wengine ili wawaunge mkono katika nia ya kukomesha ukeketaji. Hatimaye walifanikiwa. Tarehe 31 Julai 1997 wanakijiji wa Malicounda-Bambara walitoa tamko la kulaani ukeketaji mbele ya waandishi wa habari 20 wa Senegali walioalikwa kwa shughuli hiyo.

Tukio hilo halikuleta kishindo sana, pengine lingefanikiwa zaidi kwa maneno kupitia vikundi vya utamaduni kuliko radio, TV na magazeti. Kulikuwa na baadhi ya malalamiko ya kupanga walichosema wanawake wa Malicounda kutokana na “aibu” ya kuzungumzia hadhara

ni mada ambayo ni mwiko kuliko maudhui ya tamko lenyewe.

Ingawa kulikuwa na upinzani, kijiji kingine cha jirani cha Nguerigne-Bambara kinachofanya programu ya mafunzo ya Tostan-kiliamua kuiga mfano wa Malicounda-Bambara, wakiongozwa na mwanamke ambaye alikuwa ngariba wa jadi; na mwingine Ker Simbara alianza kujadili sana tatizo hilo. Hatimaye tukio kubwa likatokea.

### Tukio Kubwa

Imamu wa Ker Simbara- kiongozi wa dini mwenye umri wa miaka 66 na anayeheshimiwa katika mkoa huo amekerwa na matukio na hivyo kwenda kuzungumza na wawakilishi wa Tostan na wanawake wa Malicounda-Bambara. Hakupinga kukomeshwa ukeketaji. Kusema kweli utata umemsababishia kwa mara ya kwanza azungumze na ndugu zake wanawake kuhusu uzoefu na hisia zao kwa ukeketaji, na hivyo kuwa muungaji mkono mkubwa. Hata hivyo alihisi kwamba kulikuwa na matatizo mawili makubwa ya namna mambo yalivyokuwa yakiendeshwa.

Kwanza, Imamu alisema kijiji kimoja hakiwezi kufanya peke yake. “Sisi ni sehemu ya jamii inayooleana, mpaka vijiji vyote vinavyohusika vishiriki, kinyume chake unawaomba wazazi wabatilisha uwezekano wa mabinti wao kuolewa” Pili, kuna tatizo kubwa la lugha na mbinu. Kuna mada ambazo ni mwiko kuziongea, alisema, na zisijadiliwe juu juu au bila uzito unaostahili. Waanzilishi wa kampeni ya kupinga ukeketaji wa mwanzo walitumia maneno ambayo wanavijiji waliona hayafai kutamkwa hadharani na kuonyesha picha na michoro vilivyo-wastaajabisha. Waliona ukeketaji kuwa sawa na ugonjwa wa kuutokomeza na ngariba wake wanafaa kutengwa na jamii. Kwa hiyo hakuna namna ya kubadili utamaduni, au kusaidia ujibadili, aliongeza Imamu.

Walimuunga mkono walisema: Wakati umefika wa kufikiria jambo zuri kwa uangalifu zaidi. Kwa pamoja waliweka mkakati ufuatao:

- Nenda kwenye vijiji vyote katika jamii inayooleana. Anza kwa kuwahakikishia uhusiano.
- Usiwaamrishe wanakijiji jambo la kufanya. Waambie walichofanya wanavijiji vya Malicounda-Bambara na Nguerigne-Bambara na sababu za kufanya hivyo. Halafu waache wajaadili na kufanya maamuzi yao.
- Epuka kutumia maneno na michoro au maandamano kwa shughuli ambazo ni mwiko. Zungumzia ukeketaji kama “mila” kila mtu ataelewa unachozungumzia. Kwa Wabambara wa Senegali “mila” kwa wingi inahusu mila na desturi zote na “mila”, kwa umoja, ina maana ukeketaji.

- Epuka kuwalaani wakeketaji kwa kujitokeza au kwa uwazi. Wamekuwa wakifanya kazi yao kwa nia njema.

Kwa msingi wa makubaliano hayo, Imamu alianza safari, akifuatana na ngariba wa kike kutoka Ker Simbara na mpwa wake, kuvitembelea vijiji kumi vingine vilivyomo kwenye jamii inayooleana. Kulikuwa na mambo ya kushtusha. Wanawake walikuwa wazi-wameeleza yaliyowasibu mabinti wao waliokufa kwa kutoka damu nyingi, wengine walioambukizwa maradhi, au msononeko wa muda mrefu kutokana na kiwewe cha ukeketaji. Hata wale mangariba nao walizungumza kuhusu sababu za kufanya hivyo na kubadili mila. Wanaume nao walitoa mawazo yao.

Kabla ya kampeni kwisha, vijiji vyote 10 viliamua kuungana na wale wanaopinga ukeketaji. Pamoja na wawakilishi wa Malicounda-Bambara, Nguerigne-Bambara na Ker Simbara yenyewe, walikutana katika kijiji cha Diabougou, watu hamsini wakiwakilisha wanavijiji 8,000 na kutangaza “kutorudia” hapo tarehe 15 Februari, 1998. Habari zilizidi kuenea.

Kampeni hiyo iliendelea katika mkoa wa kusini wa Senegali karibu na Gambia ambapo kabila la Wafulani walikuwa wakikeketa. Kundi la kwanza la vijiji 14 walijifunza mtaala wa Tostan, walisikiliza habari za Malicounda-Bambara, waliazimia kuchukua hatua kulingana na mazingira yao na kuongeza jamii nne zaidi ndani ya eneo la wanaooleana ili kutoa tamko la pamoja lililotangazwa rasmi katika kijiji cha Medina Cherif tarehe 12 Juni, 1998.

### Mkakati asilia wa uenezaji

Inafaa kwanza niache kwa muda kueleza kilichotokea kwa sababu inaeleza zaidi kuhusu uenezaji-mafanikio, upinzani au vikwazo vilivyokutana navyo, na mafunzo yanayotarajiwa.

Kimsingi, mkakati ulioanzia na mwitikio wa wananchi na nyenzo una mambo matatu ya msingi.

Kwanza ulikuwa *wa pamoja*, kuliko kuwa wa binafsi. Mbinu imedhihirisha wazi kwamba familia haziwezi kuacha mila ya muda mrefu bila ya kuwa na nia ya pamoja ya kubadili miundo ya vichochea na hali iliyofanya kuwepo na mila hizo. Wakati vijiji 13 viliposhirikiana, wahusika walibadili soko la ndoa na kujenga na masharti ambayo watu *wangeweza* kukubaliana nayo, na jamii yao.

Pili, mbinu hiyo, imetoa mafunzo ya msingi kwa mtazamo wa wenyeji na kuibua baadhi ya maadili na mila zenye nguvu za utamaduni wa watu—mapenzi ya wazazi,

utiifu wa mafunzo ya Korani-kuwapa changamoto wengine. Kwa hiyo imefahamika zaidi kama kampeni ya kuleta msimamo wa ndani na ukombozi kuliko kuwa shutuma kutoka nje. Hakuna anayezungumzia “ukomeshaji” wa ukeketaji kama tauni ya kutokomezwa bali “uachaji” wake—ambacho ni kitendo cha kujua na kuamua kwa wanaohusika. Kuwepo kwa Imamu aliyewakumbusha watu kuwa Uislamu haukuamrisha ukeketaji kulikuwa muhimu sana. Wanaume hawakutengwa kabisa. Kusema kweli kuunga mkono kwao kulikuwa muhimu sana kwa maendeleo ya Kampeni.

Mwisho, mbinu hiyo ilikuwa inaongeza uwezo- yaani, wakati inahusu ushuhuda wa mtu binafsi na uenezaji wa habari mpya, imeachia uamuzi na hatua ya kuchukua kwa juhudi za kila jamii na watu wake, imelihusisha tatizo la ukeketaji na afya ya wanawake na haki za binadamu, mada zinazowahusu sana hata wanaume. Matokeo yake ni kwamba watu si kama wameamua kufuata hiari zao, bali wako tayari kueneza ujumbe.

### Kukabili njia mbili

Kutokana na hali hiyo, mabadiliko ya Kampeni yamefuata mihimili miwili-mmoja ni kuwa mstari wa mbele kwenye vyombo vya habari na jumuiya ya kimataifa na mwingine kwa wananchi. Kama ilivyodhihirika, kampeni ya vyombo vya habari haikushinda hali halisi ya wananchi, shughuli hiyo imebaki mikononi mwa kanuni za kijiji.

Vyombo vya habari viliitikia wito haraka, nchini Senegali na nje ya nchi. Notisi ilitolewa kama amri fupi kwenye vyombo vya habari nchini Senegali. Mwezi Oktoba 1997, makala kuhusu “Kiapo cha Malicounda-Bambara” yalitokea gazeti la *Le Monde* mjini Paris. Tangu wakati huo wawakilishi wa Tostan wamekuwa wakialikwa mikutano, mikusanyiko na matukio mbalimbali yanayohusu kampeni dhidi ya ukeketaji. Katika takribani kila tukio, wadhamini wamehakikisha kuwa wanawake na wanaume wenyeji wametoa maoni yao kupitia wakalimani, inapobidi waanzilishi wa kampeni hiyo-Imamu mzee na mangariba wanawake na waandaji-wamehutubia Bunge la Uingereza, Wizara ya Maendeleo na Ushirikiano ya Ujerumani, Umoja wa Nchi za Ulaya, Brussels, kwenye Mutano wa Haki za Wanawake, Washington, na katika Kamati za Umoja wa Mataifa, New York. Lililo muhimu zaidi wamekuwa wakitembelea nchi za jirani za Burkina Faso na Mali, kuzungumza na wanawake wengine wenye matatizo kama yao.

Kuendesha kampeni nje kulikuwa na matatizo yake. Kuridhiwa kwa “Kiapo cha Malicounda na Rais wa Senegali Abdou Diouf-ni muhimu, hata kama yeye

mwenyewe anatoka katika kabila kubwa la Wolof, wasiokeketa- hatimaye ilifuatiwa na hatua ya Bunge kupitisha sheria inayokomesha ukeketaji na kutoa adhabu kali kwa watakaokiuka. Wanaounga mkono Tostan waliposikia walikwenda Dakar kutoa hoja zao kupinga Sheria hiyo-si kwa sababu wanataka ukeketaji uendelee, bali wanaamini kwamba kukomeshwa kisheria na vikwazo si njia bora ya kukabili tatizo. Walihisi kuwa sheria ifuate na kulenga mabadiliko kwenye maeneo ya matukio na si kujaribu kutoa amri. Kama alivyofanya Imamu wa Ker Simbara alivyotumia mfano wa kabila lake dogo. “Jaribu kuwaambia Wabambara jambo la kufanya kuhusu mila zao na kwamba jukumu liko mikononi mwenu”.

Wasiwasi wa awali umethibitisha kuwa kweli: Sheria ilipitishwa bila ya kuzingatia maoni ya wananchi, halafu malalamiko ya wananchi yalitokea. Katika kuonyesha kupinga, ngariba mmoja mwanamke kutoka mkoa wa kabila la Tambacounda alihakikisha kuwa “*anakeketa*” si chini ya watu 120 siku chache baada ya sheria.

### Kudumisha Kampeni ya Wananchi

Hali ilikuwa tofauti kabisa kwa wananchi. Imamu na ngariba mwanamke wa zamani kutoka Ker Simbara na Nguerigne-Bambara waliamua kuendesha kampeni kwenye kundi jingine la vijiji 12 katikati ya Senegali. Wanawake waliokuwa viongozi katika mkoa wa Kolda wamepanua juhudi zao hadi kwenye jamii za jirani, kutafuta kuungwa mkono na Imamu wa Medina Cherif iwe ni kampeni iliyoidhinishwa na dini. Wakati huo huo wameamua kupeleka juhudi za mabadiliko mpaka mkoa wa Futa Toro, kaskazini magharibi ya Senegali, eneo la utamaduni wa Toucouleur umbali wa kilometa 250 wanakoongea lugha moja ya Kifulani.

Aidha, Samba Dia ni miongoni mwa vijiji vilivyoshiriki katika tamko/azimio la Diabougou kiliamua kufanya juhudi zake. Kusema kweli Samba Dia kina nasaba na “Serere Niominka” kizalia cha kabila la Serere ambalo kihistoria lilichanganyika na makabila ya Mandinka na Bambara. Wanawake wa Samba Dia waliamua kampeni hiyo ienezwe miongoni mwa watu wao, wavuvi wanaoishi visiwa vya Sine Saloum kwenye mwambao wa Senegali, kusini mashariki mwa Dakar. Wanawake na wanaume wamepata msaada wa usafiri kutoka Tostan na wakaanza kusafiri kwa mitumbwi kutoka kisiwa kimoja hadi kingine na kutembelea jamii 26 za visiwani katika eneo lote la funguvisiwa.

Katika mkoa wa Futa Toro kulikuwa na upinzani mkali kutoka kwa baadhi ya viongozi wa dini na utamaduni.

Wanawake wenzao wanaowaunga mkono wameona kwamba hawawezi kutangaza kuhusu ukeketaji katika mazingira haya, hata hivyo wamepata mbadala mzuri. Takribani vijiji 87 vilipeleka wawakilishi katika mkutano ulioitishwa Aere Lao katika mkoa wa Podor (mashariki mwa St. Louis) ambapo tarehe 4 Novemba, 2000 walitia saini azimio/tamko la pamoja la kuacha mila zote zinazoathiri afya ya wanawake na maendeleo. Kwa kutumia msingi wa haki za binadamu, wameushinda upinzani.

Kusini zaidi ya visiwa vya Sine Saloum, wawakilishi wa vijiji 26 vilivyopashwa habari kwa mitumbwi-ambavyo hakuna hata kimoja kilichohudhuria mafunzo chini ya programu ya Tostan-walikusanyika kwa ridhaa yao kwenye Kisiwa cha Niodior tarehe 7 Aprili, 2000 kutayarisha azimio lao la kuacha ukeketaji na kufanya maandalizi ya kuanza masomo yao. Katika mkoa wa Kolda, idadi ya jamii zinazotoa maazimio na kuchukua mafunzo ya programu ya Tostan imeendelea kuongezeka kutoka 18 za kwanza hadi 30, na ilipofika mwisho wa mwaka jana (2000) kuongezeka jamii 75 za jirani. Wawakilishi wa Tostan wanaripoti kuwa ilipofika Februari 2001, mwitiko ulikuja kutoka kundi jingine la wanawake waliomaliza mafunzo na kufanikiwa kuzikusanya jamii zote za wilaya ndogo ya vijijini ya Mampatini kutokana na juhudi: takribani vijiji vingine 100 vimeongezeka vilivyopanga azimio lao mwezi Machi 2001.

### **Kuiga mfano wa wenyeji**

Hakuna mwenye uhakika kuwa wimbi la wananchi litaleta hatima gani. Kama Mkurugenzi wa Tostan anavyosema, "Mengi ya haya yametushukiza Tutayafuatilia. Hata hivyo idadi ya matokeo zaidi ya takwimu za vijiji vilivyohamasishwa na vikundi vinavyokataa ukeketaji ni dhahiri.

- Mawasiliano yanafanywa kila mahali kati ya kuandaa ukeketaji kulikoshawishiwa na wenyeji na masuala ya demokrasia na haki za binadamu. Kusema kweli, masuala ya msingi yamekwishajidhihirisha na hivyo kuibua juhudi mbalimbali: uchunguzi wa wananchi kuhusu ugomvi wa majumbani, utetezi wa wananchi kuhusu haki za wasichana kusoma, madai ya kuongezeka kwa uwajibikaji katika utawala wa wananchi.
- Wanaume wamekuwa mhimili mkuu wa juhudi hizo, madarasani na nje "katika vuguvugu la kampeni". Hata katika programu zinazolenga kwa kiasi kikubwa afya na haki za wanawake, ushiriki wa wanaume ni takribani asilimia 30.
- Mtindo wa maazimio ya wananchi hadharani umetumiwa katika maeneo mengine mengi ya maendeleo ya vijijini yaliyohimizwa na wananchi, kuanzia maazimio kuhusu ugomvi wa majumbani hadi mengine ya kupinga uchomaji misitu kama njia ya kusafisha shamba.
- Juhudi hizo hivi sasa zimeanza kuenea taifa zima. Jitihada zinafuata mfano wa Senegali, ingawa imerekebishwa kulingana na utamaduni wa mahali hivi, sasa zinaendelezwa nchini Burkina Faso, Mali na Sudan na nchi za Afrika Mashariki nazo zimekuwa zikiulizia. Wanawake na wanaume wanaofanyakazi na wananchi nchini Senegali wamekuwa mabalozi wakuu, hali ya kuwa Tostan inapanga kufungua kituo cha mafunzo Thies kwa watu wa nje wanaopenda kutembelea, kubadilishana mawazo na kujifunza kutoka kwa watetezi wenzao wa haki za wanawake katika vijiji vya Senegali.

Kama methali ya Afrika Magharibi inavyosema kwa ufasaha, "Mara jua linapokwishapambazuka, kiganja cha mkono wako hakiwezi tena kulifunika".



# Waganga wa Jadi wa Kiafrika: Uchumi wa Tiba

Makala hii imeandikwa na Kenneth L. Leonard, Department of Economics, Chuo Kikuu cha Columbia, Mail Code 3308, 420 W 118 Street, New York, NY 10027; baruapepe: KL206@columbia.edu

**Tini za MA 32  
Mei 2001**

Waganga wa Jadi ni chanzo cha huduma ya afya ambacho Waafika wengi wamekuwa wakikilipia. Pamoja na kukua kwa tiba ya kisasa waganga wa jadi bado ni maarufu na wanadai ada inayozidi gharama ya matibabu ya wastani kwa madaktari wa kisasa. Je waganga wa jadi ni wafanyakazi wa miujiza au matapeli? Kusema kweli jibu lolote litakuwa limekiuka mpaka. Waganga wa Jadi si wakamilifu: ingawa sote tumewahi kusikia habari za tiba za miujiza, hali ya afya ya mkulima wa wastani wa Kiafrika haiwezi kuchiwa kudura ya waganga wa jadi. Hata hivyo, wala hawawezi kuwa matapeli: watu hawawezi kuwa wajinga wa kutambua uwezo wa mtu wanayeishi naye. Makala haya yanaendeleza hoja ya waganga wa jadi isiyotegemea miujiza wala ujinga wa watu. Yanapendekeza kuwa waganga wa jadi bado ni maarufu ingawa kuna tiba nyingi za kisasa kwa sababu wametumia kwa busara sana mkataba muhimu wa kiuchumi kwa manufaa ya uganga wao na watu wanaowahudumia.

Ingawa kuna tofauti kubwa na nyingi kati ya dawa za asili na tiba ya kisasa, makala yanazingatia tofauti za namna waganga wa jadi na wa kisasa wanavyolipwa. Sehemu muhimu ya kazi yao ilipuuzwa: waganga wa jadi wanalipwa sehemu kubwa ya malipo iwapo tu mgonjwa ametibiwa au kupona.

## Nadharia ya uchumi

Wakati walaji wanaponunua huduma ambapo ubora unazingatiwa ingawa hauwezi kuchunguzwa au kutathiminiwa moja kwa moja, nadharia ya uchumi inaonyesha uwezekano wa kushindwa kupata soko. Huduma ya afya ni mfano hai wa aina hii ya kushindwa, mara nyingi huitwa wakala. Wagonjwa wanaamua kuwaona madaktari kwa sababu madaktari wanajua zaidi kuliko wagonjwa. Mgonjwa hawezi kutathimini nachofanya daktari kwa manufaa yake, na wala hawezi kufanya uamuzi wa juhudi za daktari dhidi ya matokeo. Kwa kawaida wagonjwa wanatibiwa ingawa kwa huduma mbaya, au wanashindwa kutibiwa hata kama kuna huduma ya mtaalamu. Iwapo wagonjwa hawawezi kusema wanachofanya madaktari, kwa hiyo madaktari hawatakuwa na sababu za kutumia utaalamu wa zaidi kwa niaba ya mgonjwa.

Kwa hiyo, ingawa wagonjwa wako tayari kulipia huduma ya kiwango cha juu cha madaktari wako tayari kuitoa, soko linaweza kushindwa na huduma ya afya ya kiwango cha juu haita-  
tolewa.

Ufumbuzi wa kiuchumi wa kawaida ni kumlazimisha wakala (mtu anayetoa huduma isiyofuatiliwa) kupata faida au hasara ya matendo yake. Kwa hiyo wauzaji wanalipwa kwa kipungu-

zo au kamisheni na maofisa watendaji wakuu wanapokea bidhaa. Afya kwa upande wake Hufuata mkataba wa lipa iwapo utapona au matokeo yasiyo na uhakika. Iwapo wagonjwa watawalipa madaktari wao iwapo watapona, au wakipona, wasipopona je, gharama ya kiuchumi ya wakala itapungua.

Ingawa huduma ya afya inakabiliwa na tatizo lililoainishwa kwenye nadharia uchumi wa afya kwa ujumla umepuuza ufumbuzi wa kiuchumi kwa tatizo, kama ni jambo lisilowezekana kwa huduma ya afya. Kutotilika mkataba ni moja ya sababu zilizotajwa kwa kupuuza ufumbuzi huu. Utilianaji mkataba maana yake makubaliano kuhusu malipo yanatekelezeka. Mkataba wa matokeo yasiyo na uhakika huonekana kuwa hautiliki mkataba kwa sababu wagonjwa wanaweza kudanganya kuhusu matokeo na daktari atashindwa kuthibitisha suala lake kwa mtu wa tatu. Maana ya kupona au kutopona hutegemea mhusika binafsi na inaweza kupotoshwa kusudi.

#### **Desturi za kiuchumi za waganga wa jadi barani Afrika**

Mkataba huu wa kiuchumi ambao ni “muhimu” lakini ulipuuziwa, ni mbinu ambayo waganga wa jadi wa Kiafrika wamekuwa wakifanyia biashara. Wagonjwa wanawalipa zaidi waganga wa jadi iwapo wamepona kuliko ambavyo hawakupona. Matokeo ya mahojiano na waganga wa jadi wa Cameroon, Tanzania na Ethiopia yaliyoandikwa kwenye chapisho na mwandishi huyu, yametolewa muhtasari hapa. Waganga wa jadi waliohojiwa walipokea malipo ya awali na zaidi, walipatana na mgonjwa kuhusu malipo yatakayofanywa baadaye. Kwa waganga wote, iwapo matibabu hayakuweza kuleta nafuu kwa mgonjwa, hatalipa zaidi ya yale malipo ya awali.

Walipoulizwa kuhusu desturi ya “kuwalaani” wagonjwa kwa kutolipa, waganga wengi walikataa katakata kuwa hawakuwalaani, ingawa takribani wote walikiri kuwa babu zao au hasa wazazi wao walifanya hivyo. Desturi hiyo inafanywa kama ifuatavyo: mgonjwa anapokataa kulipa, mganga ama atamlaani mgonjwa au atabatilisha tiba. Desturi hii inaleta hofu kwa wanavijiji wote, na watu wote wasio waganga wanaamini kwamba iwapo watahinda kulipa watalaaniwa. Waganga wote walieleza habari za wagonjwa walioondoka bila ya kulipa, lakini walirudi baada ya miaka kadhaa, kuomba waruhusiwe kulipa. Wagonjwa wanaamini kwamba kulaaniwa bado kupo, kuwaruhusu waganga wasubiri mpaka baada ya matibabu ndiyo walipwe bila hofu kuwa mgonjwa atakataa kulipa.

Mkataba wa matokeo yasiyo na uhakika maana yake ni kwamba waganga wana vivutio vya kuwafanya wote matibabu mazuri na bora hata kama mgonjwa hawezi kutathimini au kuchunguza ubora huu. Lakini kuhusu tatizo la kutotilika mkataba je? Waganga wa jadi wataku-

balije kupokea malipo iwapo mgonjwa anaweza kuongopa kuhusu matokeo ya matibabu na kukataa kulipa chochote? Kuna sababu kuu mbili: kwanza, waganga wa jadi wanaishi kijiji kimoja na wagonjwa wao na hivyo wanaweza kuchunguza wanachofanya wagonjwa wao: pili, wagonjwa wanaamini kuwa waganga wanajua iwapo wamepona.

Kinyume chake mikataba ya matokeo yasiyo na uhakika haitumiki katika tiba ya kisasa popote duniani. Badala yake, wagonjwa wanalipa ada ya kiwango maalumu kwa huduma zote zinazotolewa, wawe wamepona au hapana. Hakuna hata mmoja anayetarajia aina hii ya mpango wa malipo kuweza kutoa huduma bora. Badala yake inachukuliwa kwamba huduma bora inahakikishwa kwa masharti ya shughuli za madaktari kuwa inatoka katika vyanzo vingine (vikiwemo vyama vya madaktari, mitandao ya rufaa, mitandao ya hospitali na sheria zinazowahusu madaktari).

Barani Afrika, madaktari katika hospitali za kisasa kama vile za Serikali au mifumo ya afya inayotoa huduma nafuu (hasa inayoendeshwa na makanisa) huendeshwa na tabaka la viongozi, ambapo madaktari wanatathmini ubora wa madaktari wengine na hadhi ya ajira au bahashishi hutegemea matokeo ya tathimini. Kwa kuwa malipo (au ustawi) ya daktari hayategemei matokeo bali juhudi anazozifanya, hii huitwa mkataba wa juhudi zisizokuwa na uhakika. Zingatia kwamba ili umsimamie daktari mwingine, huna budi angalau kuwa umefunzwa kama yeye: ni madaktari tu ndio wanaoweza kusimamiana.

#### **Kulinganisha mikataba ya matokeo-yasiyokuwa-na-uhakika na juhudi zisizokuwa-na-uhakika**

Mkataba wa matokeo yasiyokuwa na uhakika wa waganga wa jadi unawapa sababu nzuri ya kuongeza juhudi katika kuwatibu wagonjwa ingawa mgonjwa hawezi kutathimini anachofanya mganga. Hata hivyo, iwapo daktari wa kisasa anatoa huduma katika shirika linalojali ubora, atakuwa na kila sababu ya kutoa huduma bora. Waajiri wake watahakikisha kuwa anafanya hivyo. Kwa hiyo, wakati itaonyesha kuwa mkataba wa waganga wa jadi hauna manufaa yoyote ya ziada kulinganisha na mkataba uliotekelezwa vizuri katika hospitali yoyote ya kisasa, hii si kweli.

Hoja ya kwamba waganga wa jadi wanatia mkataba kuhusu matokeo kuliko juhudi ina matokeo muhimu kwa kazi yao. Chukua mfano wa mgonjwa wa pumu anayevuta sigara. Daktari wa kisasa anayemtibu mgonjwa huyu atatathiminiwa na daktari mwingine anayejua kinachotakiwa kufanyiwa mgonjwa huyu. Anaweza kutathiminiwa kutokana na vipimo vitakavyoagizwa, dawa alizoandikiwa, au ushauri aliopeva, bali hatatathiminiwa kujua iwapo amepona (au kwa mfano huu, iwapo dalili zimetoweka): Iwapo mgonjwa ataka-

taa kuacha kuvuta sigara, hatapona, lakini kwa daktari wa kisasa hili si tatizo.

Kwa upande wa mganga wa jadi, hawezi kulipwa iwapo mgonjwa hataacha kuvuta sigara. Iwapo atashindwa kumshawishi mgonjwa kuacha kuvuta, atakataa kumtibu mgonjwa, au angalau kukataa kukubali mkataba wa matokeo yasiyokuwa na hakika. Tofauti kati ya aina mbili hizi za mikataba haitokani na juhudi za matibabu yaliyotolewa bali na uhusiano kati ya juhudi za daktari na juhudi za wagonjwa. Kwa sababu matokeo (kuliko nyenzo) ni muhimu zaidi, mganga wa jadi anajali zaidi kuliko daktari wa kisasa, kuhusu hatua wanazochukua wagonjwa.

### Utambuzi wa wagonjwa kuhusu kazi za waganga wa jadi

Nadharia ya kiuchumi inasema kwamba mkataba unaotumiwa na waganga wa jadi utawawezesha kufanya juhudi ya kiwango cha juu katika huduma ya afya. Madaktari wa kisasa pia wanaweza kufanya juhudi za kiwango cha juu, ingawa hawatafanikiwa kwa wagonjwa katika mazingira ambapo juhudi ya mgonjwa ni muhimu kwa matokeo.

Je wagonjwa wanawatumiaji waganga wa jadi? Iwapo nadharia ni sahihi, waganga wa jadi watakuwa na nafuu (kuviweka vipengele vingine imara) wakati wagonjwa wanaumwa maradhi yanayohitaji juhudi za matibabu na za mgonjwa. Hata watakuwa na nafuu katika mazingira ambapo vifaa au ustadi/utaalamu maalumu vinahitajika. Linganisha mfano wa pumu na malaria na kidoletumbo. Malaria ni rahisi kidogo kubaini na hauhitaji juhudi kubwa kwa madaktari wala mgonjwa-badala yake unahitaji kuwepo kwa dawa za kutosha. Wagonjwa lazima waende kwenye hospitali zilizo nafuu sana, zenye dawa zinazotakiwa bila kujali ubora. Kwa upande wa ugonjwa wa kidole tumbo, unahitaji upasuaji-huduma ambayo hospitali zina vifaa vya kutosha kuliko waganga wa jadi; wagonjwa hawana budi kufuata tiba ya kitaalamu.

Hapana shaka, barani Afrika kuna mifumo ya aina moja ya kuchagua daktari wa kutibu maradhi kutegemea haki ya ugonjwa: baadhi ya hali husababisha kwenda kwa baadhi ya madaktari. Mwandishi wa makala haya amejaribu mifumo iwapo itaendana na mifumo itakavyotabiriwa na nadharia. Ili kufanya hivyo, kila hali ya ugonjwa inachunguzwa na madaktari waliotathimini kiwango ambapo matokeo yatategemea juhudi za madaktari na za mgonjwa.

Katika mkoa wa kusini-magharibi mwa Cameroon, wagonjwa wanapendelea kwenda hospitali ya misheni kuliko ya Serikali wanapokuwa na hali inayohitaji juhudi kubwa za matibabu. Kwa kuwa hospitali za misheni zimedhibitiwa zaidi ya hospitali za Serikali, hii ina maana;

wagonjwa wanataka na wako tayari kulipia hatua hii ya ubora iwapo tu wataona kuwa ni muhimu kweli kufanya hivyo, aidha, kama itakavyotabiriwa na nadharia ya kiuchumi, wagonjwa huenda wakawafuata waganga wa jadi (hata kama hospitali za misheni zina huduma bora) wanapofikia hali ya ugonjwa inayohitaji kiasi kikubwa cha matibabu na juhudi za mgonjwa. Tabia ya mgonjwa hufuata mfumo uliotabiriwa na uelewa wa kiuchumi wa mpango wa malipo unaotumiwa na waganga wa jadi.

### Hitimisho

Wakati waganga wa jadi wanafanya majukumu mengi katika jamii zao, makala haya yanalenga jambo moja muhimu la utendaji wao: wanatumia zana ya kiuchumi ya busara na uwiano katika kazi yao na tabia yao na tabia ya wagonjwa zinaonyesha matumizi ya manufaa ya zana hiyo. Mkataba wa lipa tu iwapo utapona au wa matokeo yasiyo na uhakika huwapa waganga wa jadi vivutio sahihi ili watoe huduma bora na wagonjwa nao wanatekeleza kama vile wanaelewa matokeo au athari za mkataba wa aina hiyo. Muhimu zaidi, vipengele vya kimaajabu na kimiujiza vya kazi zao ni muhimu kwa ufanyaji kazi wa mkataba huu. Bila ya imani kwamba waganga wa jadi wanajua matokeo ya tiba, mkataba wa matokeo yasiyo na uhakika hautatilika. Kwa hiyo, ingawa mkataba huu unaonyesha mafanikio kwa waganga wa jadi, hautatumika sehemu nyingi.

Waganga wa jadi, tofauti kabisa na kuwadanganya watu wajinga, wanajifanya wenye busara na kuwahudumia wananchi wenye busara. Maadamu tiba ya kisasa inatolewa katika muktadha ambapo ubora hauna hakika, waganga wa jadi wataendelea kuvuta wagonjwa.

### Marejeo

- Leonard, Kenneth L., "Afrika Traditional Healers and Outcome-Contingent Contracts in Health Care," mimeo (available on-line at [www.columbia.edu/~k1206/research.html](http://www.columbia.edu/~k1206/research.html)) Columbia University 2000.
- , "Incentives and Rural Health Care Delivery," in David K. Leonard, ed., *Africa's Changing-Markets for Human and Animal Health Services*, London: Macmillan, 2000. chapter 4.
- , "When States and Markets Fail: Asymmetric Information and the Role of NGOs in African health Care," mimeo (available on-line at [www.columbia.edu/~k1206/research.html](http://www.columbia.edu/~k1206/research.html)), Columbia University 2000.

# **Kukarabati Athari za Vita Nchini Msumbiji: Jamii za Jando na Unyago na Shule za Jumuiia**

*Makala hii imeandikwa kwa pamoja na Agostinho Mamade, Zuber Ahmed na Peter Easton ambao kwa mfuatano ni: Mkurugenzi Mtendaji, Associação Criança, Família e Desenvolvimento, Mshauri wa Mafunzo na Maendeleo, na Profesa Mshiriki wa Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Florida. Habari zaidi zinaweza kupatikana kutoka Criança, Família e Desenvolvimento; barua pepe: cfd@tropical.co.mz, au kutoka kwa Agostinho Mamade; barua pepe asmamade@tropical.co.mz. Faksi: 258-1-493345*

## **Tini za MA 33 Juni 2001**

Uganga asilia umethibitisha kuwa ni tiba inayofaa kwa kiwewe walichokipata watoto katika nchi zilizoharibiwa na vita barani Afrika (angalia Tini za Ma 10). Uzoefu wa hivi karibuni nchini Msumbiji umedhihirisha kuwa nyanja nyingine za utamaduni zinaweza kuwa muhimu katika kuwafunza kijamii kizazi kipyaa kili-choathiriwa na migogoro ya kivita na kukarabati athari za vita.

Miaka ya vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini imewaacha watoto wa vijijini na jamii zao wakiwa wamejeruhiwa kwa namna mbalimbali. Watoto wamefiwa na wazazi wao. Wengine wametenganishwa na familia zao katika haraka ya kukimbia vita na kuishia kuishi na wazazi wa kuasilisha au katika makambi ya kijeshi kwa kipindi kirefu. Vijana pia walijeruhiwa na kunajisiwa. Baadhi waliandikishwa katika jeshi la waasi na kulazimishwa kufanya uhalifu.

Wakati huohuo, jamii za vijijini ziliharibiwa vibaya sana na kunyang'anywa miundo mbinu michache na midogo waliyokuwanayo. Shule zimekuwa chache na mbalimbali mno katika maeneo ya vijijini nchini Msumbiji. Wakati wa utawala wa ukoloni, kulikuwa na maendeleo kidogo nje ya maeneo ya mijini. Wakati wa kipindi kifupi cha utulivu baada ya uhuru uliopatikana kwa taabu mwaka 1975, idadi ya shule na

wanafunzi iliongezeka haraka sana. Bidhaa hazikulingana na mahitaji, na kama ilivyo kwa maeneo mengi barani Afrika, shule za jamii zilozengwa na wananchi zilianza kuenea nchi nzima mwishoni mwa 1970. Nyingi ya shule hizo zilikuwa na walimu vijana wenye elimu ndogo na hivyo kufundisha walichokijua kwenye mtaala.

Hata hivyo, muundo mbinu huru ulioanza kukua uliharibiwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyozanzishwa na vikundi vya waasi mwaka 1977. Shule na vituo vya afya nchini kote vilibomolewa kwa sababu uvurugaji wa maisha ya jamii na hasa huduma za serikali kwa wananchi ndiyo yaliyokuwa malengo makuu ya waasi hao. Takwimu za uandikishaji shule zilipungua sana nchini kote katika mwongo uliofutilia na zilianza kurudia hali ya kawaida baada ya juhudi za amani kuanza mwaka 1990.

### **Kuunganisha wananchi tena**

Ilipofika mwishoni mwa miaka ya 1980, uadui ulianza kupungua na juhudi mbalimbali zilianza kuchukuliwa kuwaunganisha tena watoto waliotengana na familia zao, kusahau yaliyopita na kuanza kujenga nchi. Asasi ya The Mozambican

National Directorate of Social Action (DNAS) ilifadhili kundi la kwanza la programu kwa kushirikiana na Mradi wa “Children and War” (C + W) wa asasi ya kimataifa isiyo ya Serikali ya Save the Children.

Hata hivyo programu hiyo ilikuwa na ukiritimba mkubwa kiasi cha kushindwa kufika maeneo ya vijijini. Kwa hiyo C+W ilianza peke yake kwa kushirikiana moja kwa moja na jumuiya zilizokuwa tayari. Mpaka mwaka 1992 ilishaunda mtandao wa zaidi ya mavalantia/watu wa kujitolea 14,000 na kufanikiwa kuwaunganisha tena na familia zao watoto 12,000.

Mafanikio yote haya ni matokeo ya juhudi za jamii yenyewe. Hadi wakati walipoweza kukusanya nguvu, kuunganisha tena familia na kurudia mkusanyiko wa maisha ya kawaida, hakukuwa na hata sehemu ya huduma za jamii, na serikali iliyokuwa na mzigo wa madeni imeshindwa kutoa msaada wenye uhakika. Kwa hiyo wenyeji walianza kurudi kazini. Ili kushughulikia mahitaji ya watoto wasiokuwa na wazazi na waliounganishwa upya, baadhi walianza kujenga shule za jamii, walianzisha programu za kuwakutanisha watoto za kijamii, na kubuni na kutekeleza vituo vya mafunzo ya stadi kwa vijana. Ili kuhakikisha msaada wa muda mrefu kwa juhudi hizo, C+W ilibadilishwa kuwa asasi isiyo ya serikali ya Msumbiji iliyokuwa na jina “Watoto, Familia na Maendeleo” “(Children, family and Development) (CFD).

### Kijiji chachukua madaraka

Juhudi ziliza matunda yasiyotarajiwa katika tarafa ya Itoculo, kikundi cha jamii kilichoko ndani ndani katika mkoa wa kaskazini wa Nampulo, nchini Msumbiji. Watu wa Itoculo ni Wamakua, moja ya makabila makubwa. Si rahisi kufika Itaculo na mawasiliano yake na nje ni ya taabu. Watu wanaofika mara kwa mara ni wakataji magogo wa haramu, waliodhamiria kufaidika na rasilimali nyingi za misitu hiyo, na wanunuzi wa pamba, wanaofika mara moja kwa mwaka wakati wa msimu wa mauzo ya pamba. Kulikuwa na shule moja ya msingi katika kijiji cha katikati cha Itoculo, iliyowahudumia sehemu ndogo ya watu 30,000 jirani na hakuna shule kwa watu 20,000 wanaoishi katika vijiji vilivyotapakaa katika eneo, kilicho mbali zaidi ni kilomita 22 kwa njia ya mkokoteni.

Ilipofika mwanzoni mwa 1990 watoto wengi wa Itoculo waliokuwa yatima au waliokosa malezi ya utoto ya kawaida katika kipindi cha vita sasa wamekuwa watu wazima na wakuu wa kaya. Hawakutaka watoto wao nao wakose huduma kama wao, kwa hiyo walitaka kujenga upya jamii zao. Wakati huo idara ya Serikali ya Social Action waliwafuata viongozi wa jamii za Itoculo kujadili

namna ya kushughulikia mahitaji ya kielimu na maendeleo ya watoto wadogo. Ilikubaliwa kuwa zianzishwe shule tatu za watoto wadogo za jamii-*escolinhas* *Comunitarias*; hata hivyo shule hizo zilidumu kwa miaka miwili tu: mtaala rasmi, ugumu wa utekelezaji na uzoefu wa mazoea ya kutegemea vyombo vya Serikali vilivyoshindwa kutekeleza ahadi, vimevunja moyo ushiriki wa wananchi.

Tatizo la watoto wasio na huduma limebaki kuwa kubwa na kushughulisha sana jamii zinazoanza kustawi. Ufumbuzi wa kwanza ulikuja wakati wakazi wa eneo la Itoculo waliowahi kufanyakazi na C+W wakati wa vita walipofikiria kutumia jamii za jando la jadi na kuingiza katika *escolinhas* ili kutanzua tatizo. Katika utamaduni wa Kimakua, kama ilivyo katika tamaduni nyingine barani Afrika, vijana huwa waingia katika jando na unyago wakati wanapoelekea utuuzima. Katika tambiko hizo, vijana wanakusanywa katika vikundi visivyo rasmi vya marafiki na ndugu wakati wakielekea balehe. Mara kwa mara baada ya idadi fulani kufikiwa ya kati ya wasichana au wavulana 10 hadi 15—watoto huchukuliwa mafichoni na mtu mzima mbali na jamii. Kule wanafundishwa maarifa ya mapokeo ya utu uzima: majukumu ya wanawake na wanaume, maana ya balehe stadi za jamii na stadi muhimu. Wavulana wanafundishwa uvuvi na uwindaji, ujenzi wa nyumba, na shughuli za namna hiyo. Wasichana wanafundishwa kuhusu miili yao na majukumu ya kuwa mama na mke wa nyumabni; na wanafundishwa kujilinda na kuacha mawasiliano na wavulana.

### Kuiga modeli ya kimapokeo

Wazo la awali lilikuwa kufufua *escolinhas* *Comunitarias* zilizokufa kwa namna nyingine, chini ya udhibiti wa wenyeji. Baadhi ya vijana wachache wa vijijini waliowahi kusoma, watasimamia vikundi vya vijana wakubwa katika madarasa ya nyumba za nyasi. Mbali na miji na kuwafundisha misingi ya kusoma, kuandika na kuhesabu: *Escolinhas* tatu za aina hii zilianzishwa. Ingawa juhudi hiyo ilifanikiwa, wananchi hawakuona kuwa zinafanya vya kutosha. Vijana wadogo walihitaji malezi pia na mambo mengine yaliyomo kwenye mtaala zaidi ya kusoma, kuandika na kuhesabu. Kwa hiyo jamii iliomba msaada kutoka CFD kupanua na kuendeleza wazo. Wafanyakazi wa CFD walikubali kuwafundisha *animadores* kwa ajili ya shule za jamii na kutoa msaada wa usimamizi na uendeshaji iwapo wakazi wa Itoculo walijifunza kusaidia vifaa na kusimamia. Kamati iliundwa, na ushirikiano ulianzishwa.

Msaada wa CFD ulichochea kupanuliwa kwa kuchanganya au “kuzalisha” kati ya shule za jamii na ma-

jando ya jadi, zilizoendeshwa chini ya maelekezo ya wananchi. Ingawa waliendelea kuunga mkono wazo la watoto kuelimika kwa Kireno ili waweze kuwasiliana na ulimwengu, wanakamati wa Itoculo walihoji iwapo aina hii ya masomo itawatosha watoto hao kuwa wanajamii kamili. Kwa hiyo walianza hatua kwa hatua kufafanua mtaala na kufufua muundo wa *escolinhas*, wakachagua mawazo miongoni mwa jamii za jando na unyago na mifano yenye maana na kuvumbua mingine kadri walivyoendelea.

Majadiliano kuhusu mitaala na uendeshaji *escolinha* kwa kawaida yaliwahusisha watu mbalimbali wakiwemo wajumbe wa kamati, wazazi *animadores* na watoto. Miongoni mwa uvumbuzi uliofanywa na Itoculo katika kipindi hicho ni:

- Wazee walialikwa kutamba hadithi za mila za jamii na uzoefu wao wa maisha.
- Kamati iliwahimiza wanajamii kuchangia michezo, wanasesere, nyimbo na ushauri vitakavyotumiwa na watoto. Nyimbo za utamaduni zilizotumika kufundisha hesabu “zilifufuliwa” kutumiwa na kuingizwa kwenye mitaala. Shule nazo zilianza kufadhili au kujiunga na matukio ili kubadilishana rasilimali hizi za utamaduni na *escolinhas* za mkoa.
- Wasanii wenyeji walialikwa kutoa mafunzo kuhusu sanaa zao. Wanawake wanaofinyanga vyungu vya kupikia na vya maua waliwafundisha stadi zao watoto, kama walivyofanya wasusi na wacheza ngoma.
- Ratiba ya masomo ilirekebisha na kuboreshwa ili kuendana na misimu ya kilimo na shughuli za kijamii za Itoculo.
- Baada ya kuanza kutumia mtaala wa serikali wa shule za awali kama marejeo ya sehemu za “masomo” za programu ya *escolinha*, kamati iliamua kuchukua-na kurekebisha-sehemu muhimu za mtaala wa taifa wa elimu ya watu wazima kuwa unafaa zaidi kwa malengo yao.

## Kueneza Ujumbe

Miaka michache ya kwanza ya uzoefu wa *escolinhas comunitarias*—kuanzia 1995 hadi 2000- ilikuwa ya mafanikio sana. Idadi ya shule hizi Itoculo imeongezeka hadi kufikia nane, na juhudi hizo zimeanza kujikusanyia umaarufu katika mkoa wote. Kuanzia mwaka 1998, jamii nyingine za Nampulo zilianza kuomba msaada kwa Kamati za Itoculo ili waanzishe miradi ya namna hiyo, na wanakamati wamekuwa hodari zaidi kama “washauri” na “wakufunzi” wa utaalumu wao. Mpaka sasa shule nyingine sita zinafanyakazi katika maeneo ya jirani.

Aidha, uzoefu katika kusimamia shughuli iliyoongozwa na wenyeji kama *escolinhas* umewapa wanakamati na jamii kwa ujumla stadi muhimu na zinazoweza “kuhawilishika” katika ujasiriamali wa pamoja stadi ambazo wameanza kuzitumia katika mfululizo wa changamoto nyingine za maendeleo, zikiwemo huduma ya maji na afya. Kusema kweli, kikundi hicho kimeanzisha shule mbili rasmi za umma ili kuanza kubadili zile za jamii na kutoa fursa za mafunzo zaidi angalau kwa baadhi ya watoto waliopitia shule za jamii. Kwa kila shule, fomyula iliyotumika kwa *escolinhas*-msaada wa nje na fedha za kutosha zitakazochangiwa na jamii, uwajibikaji na udhibiti wa moja kwa moja wa wananchi-imefanyakazi. Mwaka 2000 kijiji kilianzisha Chama cha Marafiki wa Watoto wa Itoculo—*Associação dos Amigos da Criança de Itoculo* (AMICI), ili kuratibu juhudi zote, cha kwanza kuanzishwa kisheria katika historia ya jamii.

AMICI kinatoa nafasi ya pekee ya kuunganisha zamani na baadaye katika mkoa wa Nampula na kutumia ipasavyo mila na desturi katika majando na unyago vya vijana kwa fursa zenye manufaa ya baadaye kwa vijiji vya Msumbiji. Uchanganyaji na uchaguzi wa mambo ya asili yanayofaa umedhihirisha kuwa ni kipengele muhimu kwa ufumbuzi wa matatizo ya jamii iliyoharibiwa na vita.

# Usambazaji wa Maarifa ya Wenyeji kuhusu Kilimo

Makala hii imeandikwa na A.H Mgumia, Mratibu Msaidizi wa Mradi wa Maendeleo ya Kilimo wa Milima ya Uluguru (UMADEP), S.L.Posta 3094, Morogoro, Tanzania. Kwa maelezo zaidi, baruapepe: [umadep@mail.suanet.Ac.Tz](mailto:umadep@mail.suanet.Ac.Tz)

## **Tini za MA 34 Julai 2001**

Kiungo kati ya utunzaji kumbukumbu za elimu ya wenyeji na uenezaji wa teknolojia za wenyeji zinazofaa kwa wakulima ni dhaifu sana katika mchakato wa maendeleo ya teknolojia asilia. Kuna maarifa mengi ya wenyeji yaliyohifadhiwa katika kumbukumbu, lakini mara nyingi taarifa ya namna hiyo huwa haiwafikii wakulima katika hali ya kuweza kuitumia kuinua uzalishaji wa kilimo. Pale ambapo taarifa inawafikia, huwa ni ya jumla mno na/au haihusiani na mazingira na utamaduni wa walengwa.

Ili kuziba pengo hili, Mradi wa Maendeleo ya Kilimo wa Milima ya Uluguru (UMADEP) umekuwa ukishirikiana na wakulima wenyeji kuanika maarifa yao kuhusiana na uhi-fadhi wa mazao kiasili (NCP) na kuenza maarifa haya kwa wakulima wengine katika milima ya Uluguru kwa kutumia vifaa vya kuelimishia vyenye uhusiano na kuwavutia wakulima na warsha za mafunzo zinazoongozwa na wakulima wenyewe. Mbinu iliyotumiwa na UMADEP ime-wahusisha jamii katika mchakato mzima wa ukusanyaji wa maarifa, kuyandika na kuyaeneza.

Mgeta ni tarafa katika wilaya ya Morogoro vijijini, Mkoa wa Morogoro, upande wa Mashariki wa Tanzania, katika miteremko ya Milima ya Uluguru. Hali ya hewa ni ya joto/tropiki na kuwezesha uzalishaji wa

aina nyingi za mboga na matunda km. Kabichi, koliflawwa, njegere, salad, kotimiri, liki, matunda ya mimea inayopukutisha majani (mapichi, plamu).

UMADEP imekuwa ikifanyakazi katika Tarafa za Mgeta na Mkuyuni tangu 1993 kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa kilimo na hali za kiuchumi na kijamii za wakulima wadogo wadogo katika eneo la mradi. Mradi huo unaendeshwa kama mradi wa maendeleo ya kilimo wa uwiano kwa kutumia mbinu mchanganyiko na unatekelezwa kwa juhudi za ushirikiano kati ya asasi za serikali na wahisani. Maofisa kilimo wanaohusika na shughuli za maendeleo ya mazao wamefanya miradi mingi na ya utafiti mdogo mdogo kuhusu NCP kuhusisha matumizi ya dawa za kuulia wadudu waharibifu za mimea; mazao ya mtego na mboji kwenye mashamba ya majaribio ya UMADEP na baadaye kutumiwa kwenye mashamba yanayosimamiwa na wakulima.

Kabla ya kuingia kwa pembejeo za viwandani, wakulima wa Mgeta wali-tegemea sana NCP, wakitumia baadhi ya mimea ya asili iliyotayarishwa kwa namna mbalimbali kwa ajili ya uhi-fadhi wa mazao na dhidi ya magonjwa ya wanyama. Baada ya kuingia kwa kemikali za kilimo, wakulima haraka haraka waliacha njia za asili/jadi za kudhibiti wadudu waharibifu na ma-

gonjwa na kukimbilia kemikali za kilimo za viwandani. Sababu zao ni nyingi: Serikali ilitoa ruzuku kwa ajili ya pembejeo za kilimo, zikiwemo kemikali za kilimo; dawa za kuulia wadudu za kemikali zinahitaji muda mchache wa matayarisho na matumizi, kemikali zimethibitika kufaa zaidi ya dawa za kuulia wadudu za mimea, na makampuni yanayozalisha na kuuza kemikali za kilimo, zimetangaza na kuzitafutia soko kwa nguvu sana.

Hata hivyo, Serikali imesimamisha ruzuku kwa pembejeo za kilimo, na bei ya kemikali za kilimo ni ghali. Aidha kutokana na kampeni zinazoendelea kuhusu uhifadhi wa mazingira, wakulima wa Mgeta, kama walivyo wa shemu nyingine za Tanzania, wanazidi kuelewa madhara ya kemikali za kilimo za viwandani.

Kwa kushirikiana na mabwana shamba wa serikali wa eneo hilo, UMADEP imeanzisha juhudi za kuwahimiza wakulima kurudia NCP. Kwa kuwa maarifa asilia kuhusu NCP umeanza kutoweka kutoka kwa jamii za wakulima, mimea ya asili inayotoa malighafi ya NCP imepoteza thamani na inapotea. Uauaji wa kwanza wa UMADEP ulikuwa ni kuendesha kampeni ya matumizi salama ya dawa za kuulia wadudu za kemikali wakati huo huo kuwahimiza wakulima kufanya utafiti wa dawa za kuulia wadudu za mimea zinazofaa kwa njia ya majaribio yanayosimamiwa na mkulima.

Wakulima wengi waliohusishwa katika aina hizi za utafiti walikuwa wanachama wa vikundi vya wakulima vinavyojulikana kama *Ujuzi asili* kutoka Kata ya Tchenzema, waliotenga eneo la ardhi yao kuzalisha mboga zisizotumia kemikali. Hii ni kwa sababu wana ardhi ya kutosha, pia wana maarifa kuhusu NCP au kupata maarifa ya wenyeji kuhusu matumizi ya dawa za kuulia wadudu za mimea kutoka kwa wazee.

UMADEP, kwa kutumia mashamba ya majaribio yaliyoko kijijini, pia wamefanya majaribio pamoja na wakulima. Wafanyakazi wa UMADEP pia wamewasaidia wakulima kuratibu na kufuatilia matokeo. Wakulima wamefundishwa namna ya kulinganisha udhibiti na ukusanyaji taarifa kuhusu wadudu waharibifu wa kiasili na mbinu za kisasa.

Huko Mgeta, kama ilivyo katika sehemu nyingine nyingi za Tanzania, mabwana shamba wanafundishwa kuwahimiza wakulima kupunguza matumizi ya kemikali za kilimo za viwandani kutokana na madhara kwa afya za binadamu na mazingira. Hata hivyo, ni vigumu kwao kufanya hivyo kwa kuwa maarifa ya NCP wanayo wanajamii wachache sana na kwamba wananchi hawana mbadala. Aidha, wakulima wengi wanaamini kuwa dawa za kuulia wadudu za mimea zipo kwa ajili ya kutumiwa na wazee na wakulima wasioweza kununua kemikali na si wakulima vijana na wenye uwezo. Kusita huku kutumia dawa za kuulia wa-

dudu za mimea ni kipengele cha msingi katika kupunguza kuenea kwa mbinu za uhifadhi wa mazao wa asili.

### Hatua na Mikabala

Ili kuwasilisha kwa ufanisi ujumbe kuhusu NCP kwa jamii, UMADEP imetayarisha vielelezo (mabango, vijitabu na vipeperushi) vyenye maelekezo rahisi ya namna ya kutumia dawa za mimea na michoro iliyo katika mtindo wa gazeti la hadithi za katuni. Vifaa hivyo vimechorwa na kubuniwa na msanii mwenyeji, vyenye lengo la kuwavutia, kufaa na kuwa na maana kwa wenyeji. Zifuatazo ni hatua na mikabala vilivyotumiwa katika utengenezaji wa mabango yanayohusu matumizi ya dawa za kuulia wadudu za mimea katika tarafa ya Mgeta.

#### (i) *Kufikia ujuzi wa uvumbuzi*

Kwa sababu matumizi ya vielelezo vya kuelimishia vya kienyeji hayafahamiki sana Mgeta, UMADEP iliendesha warsha ambapo wakulima wataalamu wa dawa za kuulia wadudu za mimea walikutana na msanii, wafanyakazi wa mradi na mabwana shamba. Lengo la warsha lilikuwa kuongeza uelewa wa aina mbili tofauti za nyenzo zinazotakiwa kwa ajili ya vielelezo, kv maarifa asilia kuhusu dawa za kuulia wadudu za mimea na ubunifu wa msanii unaofanya taarifa ivutie.

Warsha ya siku mbili ya kulala ilitayarishwa ambapo wakulima wataalamu walialikwa kutoka kwenye vijiji sita vya Tarafa ya Mgeta. Wakati wa warsha wakulima wataalamu waliwasilisha uzoefu wao na matokeo ya utafiti kuhusu matumizi ya dawa za kuulia wadudu za mimea kwa kulindia mazao. Kwa kutumia taarifa hii, wafanyakazi wa UMADEP waliamua kulenga uenezaji wa taarifa kuhusu mimea miwili maarufu sana kutegemea ni wakulima wengi gani wanye imani nayo kwa kufaa kwake katika kudhibiti wadudu waharibifu.

#### (ii) *Kufafanua mahitaji ya mawasiliano*

Masuala makuu yaliyopendekezwa kuandikwa kwa ajili ya matumizi ya jamii ni pamoja na: maelezo ya mimea na mazingira yake, uenezaji wa mbinu, matayarisho na matumizi, udhibiti na usimamizi wa wadudu waharibifu, na namna mimea itakavyotumiwa kwa uhifadhi wa udongo na maji pamoja na kuongeza rutuba ya udongo. Mbinu za uenezaji zilisisitizwa kwa sababu, kwa mfano, *kibembeni* (spishi ya mimea wa kienyeji unaolingana na *Buddleia*) unapatikana kwenye msitu wa akiba ulioko umbali wa kilomita 5 kutoka maeneo ya makazi. Kwa hiyo ili kuongeza upatikanaji, mimea hii inahitaji kupandwa mashambani.



*(iii) Kuwafikia walengwa*

Kwa madhumuni ya kushirikiana taarifa na kueleza matumizi ya dawa za kuulia wadudu za mimea, washiriki wa warsha walipendekeza kuwa vifaa vya kufundishia vitakavyotayarishwa vilengwe kwa wakulima vijana., hii ni kwa sababu wakulima vijana hawako tayari kutumia NCP kwa sababu ya kikwazo cha mawasiliano katika matumizi ya NCP kati ya wakulima wazee na vijana. Aidha, washiriki wamependekeza kuwa mradi utayarishwe ziara ya mashambani kwa ajili ya wasanii kuona na kuweza kufahamu mahali pa kufanyia kazi, vifaa na zana na mazingira ya mimea iliyoteuliwa katika masikani halisi.

*(iv) Kuona na kutayarisha michoro*

Msanii alitembelea wakulima wachache walioshiriki katika warsha. Katika ziara hizo, msanii alipata picha halisi ya mazingira ya mimea, majina ya kienyeji ya mimea na wadudu waharibifu na madhara yao kwa mimea. Aidha alijifunza namna wakulima walivyotayarisha na kutumia dawa za kuulia wadudu za mimea na vifaa walivyotumia ili kuonyesha taarifa hii kwa michoro. Baada ya kumaliza kazi ya ugani, msanii alitayarisha rasimu ya mabango sita yanayoeleza na kufafanua matumizi ya mimea hiyo miwili iliyochaguliwa.

*(v) Majaribio ya Ugani*

Kabla ya nakala za mwisho za mabango, msanii wakifuatana na mabwana shamba na wafanyakazi wa UMADEP walifanya majaribio ya ugani ya mabango hayo kwa wakulima wawakilishi kutoka kwa jamii. Lengo lilikuwa kuhakikisha:

- Iwapo wakulima wameelewa mabango na maudhui
- Uwezo wa wakulima kutambua michoro, mazingira, tatizo na ufumbuzi na sifa bainifu (umri na uhusiano wa kijinsia). Hii ilisaidia kujua iwapo uwasilishaji taarifa kwa njia ya michoro na matatizo vilikuwa halisi au hapana

*(vi) Uenezaji wa mkulima kwa mkulima*

Kwa kuwa mabango yalionyesha taarifa ya kuwazika kuhusu matumizi ya dawa za kuulia wadudu za mimea, wafanyakazi wa mradi walidhani kuwa walimu wazuri na waenezaji wa taarifa katika kampeni za kielimu watakuwa wakulima wataalamu wenyewe. Kwa kuwatumia katika warsha za uenezaji kutawapa fursa ya kueleza kwa kina uzoefu wao wa dawa za kuulia wadudu za mimea kwa wakulima wenzao. Kuwawezesha wakulima kushirikiana uzoefu wao na wakulima wengine, kutasaidia pia kuongeza imani na kujiamini katika kutumia dawa za kuulia wadudu za mimea kwa wakulima vijana na wenye uwezo. Ili kufikia lengo hili, wafanyakazi wa UMADEP walitayarisha warsha

ya mipango ili kufafanua wajibu na majukumu ya wakulima na mabwana shamba katika kampeni ya elimu.

Kwa lengo la kuwafikia wakulima wengi kadiri iwezekanavyo, ilikubaliwa kuwa, kuendeshwe semina katika kiwango cha vijiji na shule za msingi. Mabango yabandikwe katika maeneo ya hadhara kama vile sokoni, kwenye ofisi za Serikali za kijiji na kwenye mabaa ya pombe. Wakulima wataalamu wamejitolea kuendesha semina kwa wakulima wengine kwa msaada wa mradi, hasa kwa utayarishaji wa hadhira na kugharimia mahitaji mengine ya uendeshaji. Washiriki wakulima (wa kujitolea) kutoka kila kijiji walipangiwa vitongoji vichache karibu na wanapoishi, ambako watawafundisha wakulima wenzao. Kwa kutumia mabango yaliyokwihatayarishwa kama mwongozo.

**Mafunzo yaliyopatikana**

- Kujaribu mabango au vifaa vya kufundishia kunaleta mwitiko muhimu na wenye thamani kubwa kutoka kwa hadhira kwa ajili ya kuboresha vifaa hivyo kabla ya uzalishaji wa mwisho.
- Ushirikishaji wa walengwa kuanzia hatua ya awali ya kupanga vifaa vya kuelimishia kunajenga hisia ya umiliki wa vifaa hivyo. Mtumiaji wa mwisho atathamini zaidi vifaa hivyo vya kufundishia na kwa hiyo kuna uwezekano mkubwa wa kutumia taarifa hiyo na kushirikiana na wengine.
- Wakulima wanapenda masuala ambayo wanatambua haraka kuwa ni sehemu ya mazingira yao halisi. Kwa hiyo matumizi ya wasanii wenyeji ni muhimu pamoja na kutumia michoro inayoonyesha kwa ukamilifu wenyeji, picha, vifaa, shughuli, miitikio na mazingira.
- Uenezaji wa maarifa ya wenyeji kuhusu mimea ya asali kwa kutumia mbinu za kisasa kama vile mabango yaliyochapishwa, kuliongeza thamani kwa maarifa ya mimea asilia inayohusika. Kwa hiyo, hukuza uhifadhi na uongezekaji wa mimea ya asili. Aidha huwatia ari, wakulima ya kutafiti na kuendeleza maarifa mengine ya wenyeji yanayohusu uzalishaji wa kilimo.
- Ubia kati ya wakulima na UMADEP umesaidia wakulima kupata uthibitisho wa kutosha wa manufaa ya kiuchumi ya mbinu za Uhifadhi wa Mazao Kiasili (NCP). Aidha umeongeza stadi zao katika kufanya majaribio yenye lengo la kutayarisha mfumo wa kilimo unaohusu hali, mahitaji na malengo yao. Pia, wakulima wanaoshiriki katika warsha za uenezaji wa mkulima kwa mkulima wanaweza kukuza stadi zao za mawasiliano.

## Dawa za Jadi na Daraja la Kuelekea kwenye Afya Bora

Kwa habari zaidi, tafadhali mwandikie barua pepe John Lambert: [Jlambert@worldbank.org](mailto:Jlambert@worldbank.org)

### ***Tini za MA 35 Agosti 2001***

Katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, maelfu ya kilo za mitishamba na/au sehemu zake hukusanywa na kutumiwa kila siku na kinamama majumbani, waganga wa jadi.<sup>1</sup> Wafugaji na wachungaji mifugo. Kwa watu zaidi ya milioni 500 na mamia ya mamilioni ya mifugo hicho ndicho chanzo pekee kinachopatikana kwa wingi kwa huduma ya afya ya wanyama na binadamu katika kiwango nafuu. Hata hivyo, upotevu wa hekta milioni 5.5 za ardhi kila mwaka kutokana na ukataji misitu, kilimo, malisho kupita kiasi, moto, mmomonyoko, n.k hupunguza sana chanzo hiki.

Dawa, chakula na bidhaa nyingine za maliasili vilivyowaendeshea maisha watu wa vijijini kwa karne nyingi hivi sasa vinatishiwa sana na aina nyingi za mitishamba huenda vikatoweka kabisa. Ongezeko hili la uadimikaji wa aina za mitishamba unawakilisha mwelekeo ambao hauna budi kushughulikiwa haraka.

Wananchi wengi wa Ethiopia wanategemea mitishamba kama chanzo pekee cha matibabu, hasa katika maeneo ya vijijini ambako hakufikiki kutokana na kukosekana barabara zinazopitika kwa gari. Huduma za afya za kisasa kupitia ujenzi wa hospitali mpya na kupandisha hadhi zile zilizopo, vituo vya afya na zahanati, dawa kutoka nchi za nje na mafunzo ya madaktari na wauguzi

havina thamani kwa sasa kwa wananchi wengi wa vijijini (zaidi ya watu milioni 40). Mitishamba na maarifa ya matumizi yake inatoa mchango mkubwa na muhimu kwa afya ya binadamu na mifugo nchini kote. Mimea huwa inapatikana kwa wingi, ina madhara madogo na ni bure au inapatikana kwa gharama nafuu. Ni sehemu muhimu sana ya sekta za kilimo na mazingira na ina uwezo wa kutoa mchango mkubwa na mdogo katika ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini nchini. Uharibifu wa mazingira, ukataji misitu, upanuzi wa shughuli za kilimo, kuvuna kupita kiasi na ongezeko la watu ndiyo mambo makuu yanayohatarisha mitishamba nchini. Hasara kutokana na kutoweka kwa mimea inaweza kusababisha hasara kubwa ya kiuchumi-jamii kwa Ethiopia na inaweza kuwa muhimu pia duniani.

Kwa sasa katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, hakuna taarifa na takwimu za nchi nzima kuhusu ugavi wala mahitaji ya walaji wa mitishamba na faida inayopatikana kwa kutumia mitishamba na mchango wao kwa huduma ya afya. Halikadhalika, wakusanyaji/wazalishaji wengi na watumiaji hawaelewi kiwango cha kupanuka kwa mahitaji ya mitishamba kinavyotishia uhai wa idadi kubwa ya aina za mitishamba. Bei wanayolipwa wakusanyaji zina-

elekea kuwa ndogo sana, na rasilimali kwa kawaida zina-milikiwa na wote au zinakwenda kuvunwa ovyo kila mara. Matokeo yake ni kwamba, wakusanyaji mimea kibiashara mara nyingi “wanaichimba” badala ya kuidhibiti.

Sera za afya na dawa za Wizara ya Afya ya Ethiopia zinatambua umuhimu wa mitishamba na mifumo ya dawa za jadi katika huduma ya afya. Kwa bahati mbaya, kumefanywa mambo madogo sana katika miongo ya hivi karibuni kuimarisha na kuendeleza vipengele vya manufaa vya dawa za asili, ukiwemo utafiti na uunganishaji wa hatua kwa hatua katika dawa za kisasa. Ingawa Ethiopia imedhamiria kuboresha sekta ya afya, uwezo wake wa kuongeza fedha kwa ajili ya utafiti na matumizi endelevu ya mitishamba umekuwa mdogo sana.

Katika nchi nyingi za Kiafrika bila ya kuisahau Ethiopia, kuna kada ya wataalamu waliopewa mafunzo ambao vipaji vyao na utaalamu katika uwanja wa kemia ya mimea, uwezo wa kidawa, utengenezaji wa dawa, usimamizi wa maliasili, na matumizi ya viwandani ya bidhaa za mitishamba hautumiwi kwa ukamilifu. Wataalamu hawa wanakiri kuwa na deni kwa waganga wa jadi na wakunga wa jadi na kwamba wanahitaji kushirikiana kuandaa michakato ya kusimamia na kuhakikisha dawa za asili. Mpaka sasa, viwango vyote vya mtaji wa maarifa (ya asili na ya kisayansi) havitumiwi kiasi cha kutosha.

Ongezeko kubwa la mahitaji ya dawa za mitishamba kwa nchi zilizoendelea limeongeza shinikizo la ugavi wa malighafi iliyopo katika nchi zinazoendelea. Ethiopia inaelewa upoteaji wa rasilimali zake za asili, hasa kutokana na kwamba rasilimali hizo ndizo vyanzo vya msingi, kama si vyanzo pekee vya huduma ya afya kwa wananchi wa vijijini na wa mjini walio masikini. Kwa kutayarisha Kitabu cha Taifa cha Orodha ya Dawa na matumizi yake, Serikali itaanzisha mchakato wa kurasimisha taratibu za uziduaji, uwekaji viwango, usalama na ufanisi, matumizi, kanuni za dawa. Uwianishaji rasmi wa mifumo ya dawa za jadi na za magharibi utajenga urithi wa utamaduni wa kale na unaokubalika, kuzipa nguvu programu za uhifadhi wa bioanuwai na usimamizi na kutoa kiwango cha huduma ya afya kwa raia wote kitakachoonekana katika ustawi wa baadaye wa kijamii na uchumi.

Baada ya kupitia njia ndefu ya maendeleo, serikali ya Ethiopia, kwa msaada wa Benki ya Dunia, hivi karibuni itanza kutekeleza uhifadhi na matumizi endelevu ya kwanza ya mradi wa mitishamba katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Madhumuni ya jumla ya mradi ni kuanzisha msaada kwa ajili ya uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya dawa za mitishamba kwa ajili ya huduma za afya kwa binadamu na wanyama. Madhumuni


mahususi ya mradi ni (i) kuimarisha uwezo wa kitaasisi, (ii) kuthibitisha na kuandika baadhi ya mitishamba inayotumiwa mara kwa mara. Kwa matibabu ya maradhi matatu makuu ya binadamu (maambukizo ya minyoo/tegu, nimonia ya kifua na shinikizo la juu la damu) na maradhi matatu ya mifugo (maambukizo ya minyoo, kinyungi na ugonjwa wa ngozi); (iii) kuanzisha uchunguzi kwa ajili ya matumizi salama ya mitishamba inayofaa kutibu maradhi makuu matatu ya wanyama na matatu ya binadamu, (iv) kutathimini manufaa ya kiuchumi yanayotokana na mitishamba kwa huduma ya afya ya binadamu na wanyama kwa kiwango cha taifa (v) kuanzisha kituo cha taarifa na takwimu za mitishamba cha taifa; (vi) kusaidia uhifadhi na usimamizi wa *mahali pa asili* na kuanzisha kilimo cha *palipokuwa mahali pa asili pa* mitishamba katika eneo la Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Bale.

Gharama za mradi zitakuwa kwa njia ya mkopo na msaada. Mkopo utagharimia: uanzishaji wa kituo cha taarifa na takwimu cha mitishamba cha taifa; tathimini ya viwango vya sasa vya matumizi; manufaa ya kiuchumi yanayopatikana nchini kutokana na matumizi ya mitishamba; mafunzo na uimarishaji wa kitaasisi; utayarishaji wa miongozo ya Haki Miliki ya Kazi za Kitaaluma kwa kutumia maarifa ya dawa za asili; kubainisha usalama na ufaaji wa mitishamba inayotumika kutibu magonjwa makuu matatu ya mifugo na matatu ya binadamu; kuanzisha utafiti wa mbinu za uenezaji na kilimo cha mitishamba iliyoteuliwa; na utekelezaji, ufuatiliaji na tathimini ya mradi.

Fedha za msaada zitasaidia uhifadhi wa bioanuwai na usimamizi endelevu wa rasilimali za mitishamba ya *mahali pa asili* katika na karibu na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Bale kama njia ya kupunguza uvunaji mkubwa wa mimea ya porini. Msaada pia utatumika kugharimia kampeni za elimu na uhamasishaji, mafunzo ya nchini, majaribio ya kilimo yanayomshirikisha mkulima kwa mitishamba iliyoteuliwa iliyo hatarini kutoweka katika bustani za nyumbani, za jamii, mipakani na maeneo yanayozunguka hifadhi ya taifa. Wakala kiongozi na wakala shiriki, taasisi na jamii vimebainishwa katika Kielelezo Na. 1.

Mapendekezo ya matumizi ya dawa zinazotokana na mitishamba katika vituo vya afya vya msingi yatapewa uzito tu baada ya uchunguzi utakaothibitisha kuaminika na usalama. Matumizi ya dawa za namna hiyo kwa muda mrefu yatatoa taarifa muhimu kuhusu athari za dawa kwa binadamu na mifugo ya baadhi ya makundi ya michangan-yiko ya kemikali—taarifa ambayo mara nyingi haipatikani wakati wa kupima dawa sanisi mpya. Masharti ya upimaji yaliyotolewa na mamlaka zinazosimamia ili kuhakikisha

**Uhifadhi na matumizi endelevu ya mitishamba ya tiba, wahasika wakuu na taasisi zinazochangia, mashirika na jamii nchini Ethiopia**



usalama wa “dawa” mpya si lazima kwa dawa za asili. Majaribio machache ya kabla ya kuingia maabara juu ya athari na asili ya sumu huenda yatatosha.

Mitishamba na maarifa ya matumizi yake ni kama uzi unaunganisha elimu na taasisi za maarifa, masuala ya afya na ya watu, maendeleo endelevu, masuala ya kitamaduni na mazingira, jinsia na mikakati ya vijijini, mijini na sekta binafsi. Kwa hiyo mradi huu hauna budi kufuatiliwa kwa makini na idara zinazohusika katika Benki ya Dunia na asasi nyingine za maendeleo ili kuona namna utakavyoweza

kuwianishwa kwa manufaa ya maskini. Ingawa si tiba ya kila kitu, zinafaa kuondolea umaskini na kusaidia maendeleo na hazina budi kuangaliwa kiujumla kwa muda mrefu na mpango mkakati.

1 Waganga wa jadi kwa muktadha huu wanawajumuisha waganga wa mitishamba, waunganishaji mifupa, waponyaji vichaa na maradhi ya akili na wakunga wa jadi. Waponyaji kidini, wauguzi na tiba ya kiroho pia hutumia mitishamba ya tiba lakini si kama chanzo cha msingi cha uponyaji.

## Mchakato wa Kumiliki Maarifa Asilia

Kwa habari zaidi wasiliana na: Krishna Pidatala (baruapepe: [kpiduala@worldbank.org](mailto:kpiduala@worldbank.org)); Simu 202-473-7353; Wizara ya Serikali za Mitaa, Idara ya Utafiti &HRD, Asmara, Eritrea (Simu: 291-1-121877/291-1-115534) au (Faksi: 291-1-120014)

### ***Tini za MA 36 Septemba 2001***

Ikiwa katika pembe ya Afrika, Eritrea ina mikoa sita na makabila ya asili zaidi ya tisa (Tigrigna, Tigre, Rashayda, Saho, Bilen, Hidareb, Kunama, Nara, Afar) kila kabila likiwa na mila na desturi zake.

Wakati maarifa asilia yamebebwa kwenye shughuli za jamii, taasisi, uhusiano na tambiko, mara nyingi si rahisi kutambua kutokana na tabia yake ya ukimya. Kutokana na kuongezeka kwa haraka kwa utanda-wazi, nchi nyingi na asasi za maendeleo hivi karibuni zimetambua tishio la kupotea kwa MA na wanakusanya nguvu za pamoja zenye lengo la kuhifadhi na kufufua rasilimali hii muhimu.

Mwaka 1982, kikundi cha Waeritrea kilijikusanya na kuanzisha mpango wa kuainisha na kuandika maarifa yao ya asili. Lengo la juhudi hizo za miaka 20 lilikuwa ni kuainisha na kueleza MA ya wananchi wa Eritrea katika muktadha wa uchungu-mi-jamii. Kimejaribu kuchunguza shughuli za utamaduni-jamii na za kiuchumi za kila moja ya makabila tisa ya Eritrea kwa kuanza na chimbuko la jamii ya Waeritrea kuanzia wakati wa ukoloni mpaka sasa. Katika mchakato huu, lengo lilikuwa kuchunguza mila na desturi za makabila hayo na kuelewa, kuweka makundi na kuandika kwa lengo

la kuhifadhi na kuchapisha. Jambo lililo bayana hapa ni kwamba fedha kwa ajili ya juhudi hii ya MA ilitolewa na Idara ya Utawala wa Umma mpaka mwaka 1990 na Wizara ya Serikali za Mitaa kuanzia mwaka 1995 mpaka sasa.

Mpango huu ulibuniwa ili kwamba utekelezwe kwa awamu mbili, ambapo mbapo ni wa kwanza tu ndiyo uliofanikiwa kushuhudia maendeleo ya maana:

- Awamu ya I—Ukusanyaji wa Taarifa za MA
- Awamu ya II—Maelezo ya uhalalishaji na uchambuzi

#### **Mfumo wa ukusanyaji**

Ukusanyaji wa maarifa asili ulifanyika kwa hatua zifuatazo:

1. Kupanga MA katika makundi kama vile—matumizi ya ardhi, kilimo, unajimu, tambiko za kitamaduni, dawa za asili, familia n.k.
2. Kuchagua utamaduni lengwa—kwa mkoa na/au kabila; kuainisha wamiliki wa MA katika jamii hiyo
3. Kukusanya MA—kwa kutumia madodoso, majadiliano ya vikundi n.k.
4. Uhalalishaji—kuthibitisha kwenye vikundi, ziara za uwandani
5. Kurikodi na kuhifadhi kwenye Kompyuta kwa makundi

6. Kuchapisha—kufafanua na kupanga katika taarifa ya umma na ya faragha; kuchapisha MA ya umma kwa maandishi (encyclopaedia).

Mbinu ya ukusanyaji wa MA ya Eritrea ililenga kwenye kuchunguza kabila mojamoya. Mchakato mzima wa kuchunguza MA ya kabila moja kabla ya jingine ulichukua kati ya miezi 18 na miaka miwili. Ukusanyaji wote ulifanywa kwa hatua nne.

#### *Hatua ya 1*

Hatua ya kwanza ilikuwa kubainisha mkoa linakopatika kabila hilo. Uchunguzi wa majaribio ulifanywa katika baadhi ya maeneo ya mkoa huo kupata taarifa ya jumla kuhusu eneo, watu na mila na desturi zao. Baada ya hapo yalifuata mahojiano mbalimbali na viongozi wa wilaya na eneo, jamii zilizopo na wazee wa vijijini ili kujua hasa mahali pa kuanza kukusanyia MA. Kwa misingi ya majadiliano ya awali, madodoso ya mwanzo yalifanyiwa marekebisho na kuboreshwa. Madodoso haya yalitumiwa kama zana za kufanyia utafiti ili kusaidia kubainisha mambo muhimu ya MA na wamiliki muhimu wa maarifa haya katika kila kabila.

#### *Hatua ya 2*

Hatua ya pili ni muhimu kwa sababu ilisaidia kubainisha idadi ya watu walioelewa sana utamaduni, mila na desturi ndani ya kila kabila. Matokeo ya utafiti (kuanzia madodoso) pamoja na mahojiano yaliyotangulia katika Hatua ya 1, yaliainisha kundi hili la msingi, ambalo kwa kawaida lilikuwa kati ya watu ishirini na thelathini. Kundi hili la msingi lilikuwa na Wazee, ambao wamekuwa na maarifa hayo asilia. Baada ya hapo ilifuata kukubaliana kwa muda na mahali pa kukutania watu wote hawa kwa kipindi kirefu (siku 50 hadi 60) ili kuwezesha mchakato wa ukusanyaji wa MA kuedelea.

#### *Hatua ya 3*

Majadiliano ya vikundi ndiyo yaliyokuwa msingi wa hatua hii ya mchakato wa ukusanyaji wa MA. Wenye maarifa asilia walioteuliwa waligawanywa katika vikundi vitatu hadi vinne na majadiliano ya vikundi yalifanywa ndani ya kila kikundi kwa vipindi vilivyochukua kiasi cha siku 60. Majadiliano haya yalikuwa ya kina na yaliyolengwa, na washiriki walipewa chakula na malazi (pamoja na kulipwa kiasi fulani cha posho ya kujikimu ili kufidia mapato waliyoyakosa) katika kipindi chote. Lengo la hatua hii lilikuwa kutathimini kuaminika kwa taarifa na takwimu, kuangalia migongano na hatimaye kuthibitisha tena na taarifa iliyokusanywa na kikundi kimoja na ile ya vikundi vingine.

#### *Hatua ya 4*

Hatua ya mwisho ya mchakato wa ukusanyaji wa MA ni kufanya ziara za ugani ili kuhakiki taarifa zilizokusanywa katika hatua zilizotangulia. Katika mchakato huu, timu ya ukusanyaji wa MA ilikutana na waganga halisi wa jadi na watu wengine ndani ya makabila katika mazingira yao. Madhumuni ya mikutano hii yalikuwa ni kuikutanisha kila timu ya wokusanyaji wa MA na uzoefu asilia ili kuwezesha kupata ukweli kamili na uhakiki mwingine. Iwapo baadhi ya maswali hayakujibiwa kwa ukamilifu katika hatua ya majadiliano ya vikundi, juhudi zilifanywa ili kuongeza au kubadilisha wajumbe wapya katika vikundi vilivyoteuliwa katika hatua hii kwa lengo la kupata mwitiko wa kutosha.

#### **Vikwazo**

Katika kipindi cha miaka ishirini ya kuwepo kwake, timu ya ukusanyaji wa MA imepitia matatizo mengi ya kijamii na kisiasa. Vita vya uhuru, mgogoro na Ethiopia, ukame, tatizo la VVU/UKIMWI na ukosefu wa fedha, vyote vimekuwa na athari fulani kwa kasi ya ukusanyaji na uchambuzi wa mchakato wa MA. Madodoso ambayo yalitayarishwa nusunusu (ambayo ni zana muhimu ya msingi ya ukusanyaji taarifa) ni waraka hai ambao umekuwa ukibadilika uwiano ulio sawa, na marekebisho ya mwisho kwenye madodoso hayo yalifanywa mwaka 1998. Jamii ya Eritrea imekuwa ikibadilika polepole katika kipindi ambapo uzoefu wa ukusanyaji wa MA umekuwa ukikua. Jambo la kuisimua akili ni kwamba katika jitihada ya miaka ishirini yote hii, kumekuwa na shauku kubwa miongoni mwa Wazee (wenye maarifa ya jadi katika makabila mbalimbali) ya kuhifadhi na kuhuisha utamaduni na mila na desturi zao kwa ajili ya karithisha kizazi kipya. Tofauti na ilivyotarajiwa, ni Wazee ndio ambao hawakukata tamaa. Uhodari na uvumilivu wao vilikuwa muhimu sana katika kufanikisha machakato wa ukusanyaji wa muda mrefu.

#### **Taathari**

MA yaliyokusanywa katika kipindi cha miaka ishirini bado yamo katika muundo wa mkusanyiko wa taarifa za takwimu zisizochambuliwa. Hata hivyo, baadhi ya sehemu za jamii ya Eritrea zimefanikiwa kuona sehemu ya mkusanyo huu mara mojamoya na katika namna ya mtawanyiko; na hivyo kusababisha taathari zisizo za moja kwa moja. Mifano ya matumizi na manufaa visivyo vya moja kwa moja ni pamoja na:

- Kitivo kimoja na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Asmara wametumia mkusanyo wa MA wakati wa kuandika tasnifu zao;
- Wizara ya Elimu imetumia mkusanyo huo kwa ajili ya elimu ya jadi na utayarishaji wa ujumbe wa utamaduni unaolenga makabila;
- Wizara ya Afya imetumia mkusanyo huo kwa huduma ya afya ya jadi baada ya kujifungua na mazoezi, ukunga, matibabu ya watoto wenye umri wa kati ya mwaka mmoja hadi mitano;
- Wizara ya Sheria imetumia mkusanyo huo kutokana na utajiri mkubwa wa sheria za kimila, utumiaji wa wazee na mbinu za kimila za kutatua migogoro ndani ya jamii; na
- Wizara ya Serikali za Mitaa imetumia baadhi ya MA ili kusaidia kupanga upya nasaba za mikoa na kuwapanga watu wanaohusika.

### Changamoto za usoni

Awamu ya kwanza ya mradi imekamili. Bado kuna changamoto nyingi—zikihusu uchambuzi wa kina wa pamoja wa taarifa na takwimu zilizokusanywa na pia kuhusu matumizi ya matokeo yanayotarajiwa kupatikana kutokana na uchambuzi huo. Changamoto hizo ni pamoja na:

- Urithishaji wa MA kwa vijana ni wa polepole sana kutokana na sababu mbalimbali kama vile vijana hao kuhamia mijini kutafuta ajira, ongezeko la wimbi kubwa la athari za utamaduni wa nchi za magharibi na vipaumbele katika uthamanishaji na utandawazi;
- Kwa kawaida wakusanyaji wa MA ni wanaharakati wa ukombozi wenye uzoefu mkubwa lakini wasio na mafunzo rasmi ya nadharia ya uchambuzi na uwasilishaji wa matokeo;
- Utafiti uliotarajiwa haukuendelea haraka kama ilivyotarajiwa kutokana na sababu mbalimbali, kwa mfano ukosefu wa fedha, zana za kisasa, mgongano wa uamuaji n.k;
- Taarifa na takwimu za MA zilizokusanywa hazikupangwa kwa kanuni, kuorodheshwa na mara nyingi hazikusahihishwa na zimekaa ovyoovyo; na
- Baadhi ya taarifa na takwimu (hasa kutoka kabila la Tigrigna) zimo katika lugha ya kikabila na zinatakiwa kufasiriwa kwa Kiingereza.

### Nini kifuate

Kati ya watu tisa walioanza juhudi za ukusanyaji MA takribani miongo mwili iliyopita, ni wanne tu ndio bado wangali wakihusika na juhudi hizo. Baada ya kutumia sehemu kubwa ya maisha yao ya kazi kwenye utafiti huo, wanashauku ya kuona matokeo ya kazi yao nzito ya MA ya yatachambuliwa kitaalamu na kuwasilishwa kwa manufaa ya watu wa Eritrea. Eritrea imetumia kiasi ya Nakfa milioni 1.5 (ambazo ni wastani wa Dola 190,000 za Marekani bila kujali mfumko wa bei na kutumia wastani wa Nakfa 8 kwa Dola moja ya Marekani) kwa sasa (tangu uhuru, mwaka 1991), kwa ajili ya utafiti huu na kuna kurasa zaidi ya 30,000 za taarifa na takwimu zinazohitaji kupitiwa. Hatua za haraka za kuchukuliwa ni:

- Fedha na msaada wa wataalamu wa fani mbalimbali (wakiwemo wanaanthropolojia, na wengineo) kuthibitisha ukweli na kuchambua taarifa na takwimu ghafi zilizokusanywa hadi sasa.
- Mafunzo yanayofaa kwa timu ya ukusanyaji MA katika vyo vyuo maarufu nchi za nje (yasiyopungua mwaka mmoja) ili kuwawezesha kuzungumza/kuelewa lugha ya timu ya wataalamu wa fani mbalimbali (kwa upande wa dhana na istilahi/lugha ya kitaalamu), na hivyo kuwezesha ubadilishaji wa mawazo wa kutosha na unaofaa.
- Ushirikishaji wa wasomi wa Eritrea katika juhudi ya MA ili maarifa ya kitaalamu kuhusu ukusanyaji wa MA yaenezwe kutoka kwa wafanyakazi wanne waliobaki kwenda kwao. Hii inahitaji kujielimisha vya kutosha wakati wa kujenga uwezo na shauku katika MA ndani ya nchi hii.

Hatimaye wanufaika wa juhudi hizi za ukusanyaji wa MA watakuwa watu wa vijijini wa makabila tisa ambao maisha yao ya kila siku, shughuli zao za kujipatia riziki, na taasisi za kitamaduni zitakuwa wazi zaidi kwa asasi zinazozisaidia huduma na kushiriki katika maendeleo yao. Maarifa asilia na desturi zilizokusanywa katika mradi huu na juhudi hizi si kama vitatoa muktadha kwa shughuli za maendeleo, bali pia kusaidia katika uhifadhi na uhuishaji wake.

# VVU/UKIMWI: Waganga wa Jadi, Jitihada ya Jumua Kuji-tathmini na Uwezeshaji

Makala hii imeandikwa na Maja Naur, Ph.D katika sosholojia, na mshauri wa Benki ya Dunia. Kwa habari zaidi, waandikie, baruapepe: [majanau@msn.com](mailto:majanau@msn.com) au [mnaur@worldbank.org](mailto:mnaur@worldbank.org)

***Tini za MA 37  
Oktoba 2001***

Nchi nyingi za Kiafrika zimeridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Watu, unaotoa tamko juu ya haki za afya, elimu na “kuhamasisha, kulinda na kuimarisha kuheshimiana na kuvumiliana.” Katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara peke yake kiasi cha watu milioni 17.2, wamekufa kutokana na VVU/UKIMWI, idadi inayojumuisha watoto milioni 3.7 walio chini ya umri wa miaka 15. Mpaka sasa vita dhidi ya maradhi haya vimeelekezwa katika kinga wakati ambapo ni juhudi za matibabu na vipengele vya kijamii na haki za binadamu vinavyohusiana na janga hili vimepewa uzito mdogo sana. Hii inaelekea kuupa mtihani Mkataba huo. Ingawa makampuni mengi ya dawa ya nchi za magharibi yamepunguza bei za dawa za kurefusha maisha kwa wenye VVU/UKIMWI, dawa hizi bado ni ghali mno na haziwafikii Waafrika walio wengi. Hata kama dawa zingetolewa bure, nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara hazina miundombinu ya usambazaji dawa, na jambo hili linaleta wasiwasi iwapo mifumo ya hospitali itaweza kupanuliwa kwa kasi na ubora unaotakiwa. Mwisho kuna uwezekano mkubwa kwamba fedha zilizotengwa kupambana na maradhi hazitawafikia walengwa. Kwa hiyo, mkazo hapa ni kwa namna gani waganga wa jadi na maarifa

asilia vinavyoweza kuipa jamii uwezo wa kukabiliana na matokeo ya kijamii ya janga hili, na wakati huohuo kuweza kuhakikisha kuwa rasilimali zinazolengwa serikali zinatumiwa kweli kwa manufaa yao.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Kofi Annan, hivi karibuni ameomba dola bilioni 7 zaidi kwenye dola bilioni 10 kwa mwaka kama kima cha chini cha fedha kutoka nchi tajiri kwenda Afrika kupambana na VVU/UKIMWI. Hata hivyo baadhi ya wataalamu wa bara hilo wamesema hata kiasi hicho cha fedha kitaleta matokeo madogo mpaka Mataifa ya Kiafrika yatakapojenga na kuimarisha mifumo yao ya afya ya kusimamia dawa hizo na kufuatilia afya za wagonjwa waliopewa dawa hizo. Mfumo rasmi wa huduma ya afya unawafikia kati ya asilimia 10 na 20 tu ya watu ambao zaidi ni wale tu walioko kwenye vituo vya mjini kwenye hospitali na kliniki. Waganga wa jadi wanatoa huduma ya afya ya msingi kwa asilimia 80 ya watu katika wanaishi na jumua ambako msaada unahitajika; wao ndio hivi sasa wanaowatibu wagonjwa wengi wenye maradhi yanayohusiana na VVU/UKIMWI. Baadhi ya waganga wa jadi wamefanikiwa kuongeza urefu wa maisha ya wagonjwa wa VVU/UKIMWI kwa kutumia dawa za mitishamba zinazopandwa katika



maeneo yao. Mfano mzuri ni mafanikio yaliyopatikana huko Tanga, nchini Tanzania.

Iwapo dawa za nchi za magharibi hatimaye zita-patikana na kwa bei nafuu kwa jamii masikini, waganga wa jadi ndiyo watakaokuwa wasambazaji wakubwa wa dawa hizo na kuhakikisha kuwa wagonjwa wanatumia kiwango kinachotakiwa. Wakati waganga wa jadi watahitaji mafunzo ya kazi hiyo, haitakuwa ghali kuinua kiwango chao cha maarifa kuliko kupanua mfumo rasmi wa afya. Kutegemea mifumo iliyopo inaelekea kuwa na uwezekano mkubwa wa uendelevu.

VVU/UKIMWI hauheshimu mipaka wala tabaka, utamaduni wala rangi, lakini ukosefu wa maarifa na kuelewa vibaya namna maradhi haya yanavyoenezwa kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine mara nyingi husababisha ukiukaji wa haki za binadamu kwa kuwatenga au kuwabagua watu na familia zenye VVU/UKIMWI. Aidha athari za kijamii huwahusu maskini zaidi. Jamii nyingi zimeelewa kwamba VVU/UKIMWI huenezwa kwa njia ya damu na kujamiiana, lakini kuna wengi sana wanaoelewa vibaya kwamba ueneaji unatokea kwa kupeana mikono, kula au kuoga pamoja, kushirikiana nguo, kutumia vyombo vya aina moja, au kwa watoto wanaolala kitanda kimoja. Elimu na habari kuhusu namna VVU/UKIMWI unaenezwa hivi sasa ndio imekuwa juhudi ya msingi katika kupambana na maradhi hayo. Mpaka sasa ni juhudi ndogo ambazo zimefanywa katika kuondoa mnyanyapao unaohusiana na janga hili licha ya kwamba “lile tusiloweza kulikemea hatuna hatuna chochote tunachoweza kulifanyia.” Katika kuongeza uwezo wa mtu au jamii ni muhimu kwa jamii kushughulikia changamoto jambo ambalo huachiwa watu binafsi katika patashika la VVU/UKIMWI.” Aidha, mpaka hapo rasilimali za Benki ya Dunia kwa Programu ya sekta nyingi ya UKIMWI (MAP) itakapoanza kumiminika, jamii haina budi kupewa uwezo wa kupata na kufuatilia fedha zilizolengwa kwao. Zana nzuri ya uongezaji uwezo ilitumiwa katika kipindi cha mpito kuanzia siasa za ubaguzi mpaka uchaguzi nchini Afrika Kusini ambapo asasi zisizo za serikali ziliweza kuwahamasisha wananchi nchi nzima. Kampeni hiyo ilikuwa kubwa na haijapata kufanywa mahali pengine popote wakati huo. Mbinu iliyotumiwa ilikuwa na mizizi yake katika uwezeshaji wa jamii kuandaa mkataba wao wenyewe wa haki za binadamu kwa msingi wa demokrasia na kuwaheshimu watu wa rangi na makabila yote (Dorsey 1997). Wazo hilo lilitokana na mapendekezo ya Kidemokrasia ya Paulo Freire ya utatuaji wa matazito ya kielimu ambapo “wanaume na wanawake wanajenga uwezo wao wa kutambua ipasavyo namna wanavyoishi katika ulimwengu wanaojikuta wamo, wanatokea

kutambua kwamba ulimwengu sio kama hali tuli bali hali halisi uliyo katika mchakato wa mabadiliko” (Freire 2000).

Kutumia uzoefu uliofanikiwa wa uhamasishaji wa kijamii katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI, utafiti mdogo kuhusu elimu ya magonjwa ya mlipuko lazima ufanywe na *wanajamii kwa ajili ya jamii*. Waganga wa jadi (hasa waganga wanawake) huenda wakawa wawezeshaji wakuu katika mchakato huu. Kilicho muhimu katika utafiti unaosimamiwa na jamii ni mchakato wanaopitia wanajamii hao, ambao hutofautiana kimsingi na upimaji wa Kijamii ambapo ukusanyaji wa taarifa na takwimu ni muhimu zaidi.

Mchakato wa utafiti unaosimamiwa na jamii unaweza kuwezeshwa, ukitoa waganga wa jadi na Asasi Isiyo ya Kiserikali/Shirika la Kijamii, ili kuwianisha juhudi zozote za wasomi wenyeji kutawala mchakato huo. Miongoni mwa masuala ya kushughulikiwa ni pamoja na:

- Je, jamii inadhani VVU/UKIMWI unatoka wapi?
- Mtu anapataje maradhi hayo?
- Je, kuna mahali mahususi ambapo hatari ya kupata maradhi hayo ni kubwa?
- Je, kuna wanajamii wengi wanaokwenda katika sehemu hizo mara kwa mara?
- Je, kuna makundi mahususi yaliyo hatarini zaidi kuambukizwa?
- Ni kina nani walio mahututi katika jamii?
- Watu wanaoumwa walikuwa wakifanya kazi gani wakati walipoambukizwa?
- Je, tangu hapo kumekuwa na mabadiliko yasehemu ya kazi tangu waumwe?
- Je, dalili za ugonjwa zimeendeleaje katika kipindi hicho?
- Je, walimwona nani walipoanza kuumwa?
- Je, walipata msaada wa dawa, na waliupata wapi?
- Hali zao za kijamii zimebadilika baada ya kuumwa, na imebadilika vipi?
- Je, kunatokea nini kwa familia (kijamii na kiuchumi?) yenye mwanafamilia mwenye VVU/UKIMWI?
- Je, juhudi gani zimechukuliwa na jamii, serikali, au manispaa/wilaya kuhusiana na VVU/UKIMWI?
- Je, kila mtu anaelewa kuhusu rasilimali ambazo jamii inaweza kuomba ili kupambana na VVU/UKIMWI?

Madhumuni ya utafiti wa jamii wa aina hiyo ni (i) kuanza mchakato ndani ya jamii kushughulikia VVU/UKIMWI, ili kuwawezesha watu kuzungumzia kuhusu ugonjwa huo; (ii) kuongeza ufahamu kwamba ugonjwa huo si jambo la kidhahania linalozungumziwa na watu tu kwenye redio, bali ni jambo linalowahusu watu wa jamii yao wenyewe; (iii) kupata habari za watu binafsi

zitakaowasaidia wengine wenye hali ya namna hiyo; (iv) kuinua kiwango cha uelewa miongoni mwa watu walio hatarini; (v) kuufanya ugonjwa huo kuwa ni tatizo la jamii—km. kuhusu namna ugonjwa unavyoweza kulingwa na jamii na namna wagonjwa na familia zao, wakiwemo mayatima, wanavyoweza kusaidiwa; na mwisho, tena muhimu sana (vi) kuiwezesha jamii kutunga sheria zao za Haki za Binadamu. Kila sheria ya Haki za Binadamu ya kila jamii itakuwa na vipengele vya kipekee kutegemea hali ya mahali husika. Lakini watakachokubaliana jamii pia watakuwa na shauku ya kutekeleza na kuwawekea vikwazo vya kijamii dhidi ya wale wanaokiuka kile kilichopo kwa manufaa ya jamii kwa ujumla.

### Marejeo

- Dorsey, Ellen (1997). "Uandaaji wa Mikataba na Utafiti Shirikishi," katika *Elimu ya Haki za Binadamu kwa ajili ya Karne ya Ishirini na Moja* kilichohaririwa na George J. Andreopolos na Richard Pierre Claude, Philadelphia: Shirika la Uchapishaji la Chuo Kikuu cha Pennsylvania.
- Freire, Paulo. (2000). *Taaluma ya Ufundishaji Watu Waliokandamizwa*, Toleo la 30 la Maadhimisho, New York: Continuum.

# Lugha za Asili, na Fasihi kama Biashara Isiyolenga Faida

Makala hii imetayarishwa na Dkt. Peter Easton wa Chuo Kikuu cha Florida na Dkt. Sonja Fagerberg—Diallo wa ARED. Kwa habari zaidi wasiliana na ARED, Villa 8253, Sacre Coeur 1, Dakar, Senegali, Simu (211) 825—7119, 824-5098, Faksi (221) 824-7097, baruapepe: ared@enda.sn.

**Tini za MA 38  
Novemba 2001**

Toleo namba 13 la mfululizo huu (“Lugha za Sahel, Maarifa Asilia na Kujisimamia, Oktoba 1999) lilionyesha kwamba, maandishi katika Lugha za Kiafrika, ambayo hivi sasa yanaongezeka katika nchi nyingi barani humo, yanatoa chombo muhimu cha kujieleza na maendeleo ya maarifa asilia. Programu za kisomo na elimu isiyo rasmi barani humu yanatoa kipimo cha “sauti” ya wananchi—angalau katika kiwango cha mahali fulani—hadi vikundi vya jamii na vya ma na hali hiyo hapo zamani. Hata hivyo, daima hukabiliwa na kikwazo kimoja: kukosekana kwa fasihi miongoni mwa wanafunzi wapya wote waliojua kusoma na kuandika zilizo katika lugha za kufundishia.

Tatizo hilo linaanza kutanzuliwa miongoni mwa wazungumzaji wa KiSenegali wa Lugha ya Kifulani au Lugha ya Pulaar katika baadhi ya njia za kufundishia. Makala haya yanaeleza kwa muhtasari uzoefu wa ARED (Washiriki katika Utafiti na Elimu kwa Maendeleo) na CERFLA (Centre d’Etudes pour la Recherche et la Formation en Langues Africaines), asasi mbili zinazohusiana zisizo za kibiashara zinazofanyakazi katika mikoa ya wazungumzaji wa Lugha ya Pulaar nchini humo, ambayo yamekuwa yakifanyakazi kwa zaidi ya miaka 12 kuendeleza kusoma na kuandika kwa Lugha hiyo.

Hivi sasa ARED inasimamia kam-puni ya uchapishaji inayouza kati ya vitabu 30,000 hadi 50,000 kwa mwaka, ambavyo zaidi vimeandikwa kwa Lugha za nchini Senegali. Vitabu hivyo vinasambazwa nchini Senegali na gharama ya uchapishaji wake zinalipiwa na asilimia 75 ya mapato ya mauzo ya vitabu vyenye-we. ARED pia iko motomoto katika kutoa mafunzo (CERFLA ilianzish-wa ili kuendeleza chuo cha ufundi cha asasi) na upataji wa maarifa ya wenyeji. Je, imefanikiwa namna gani na nini mafunzo ya uzoefu huu kati-ka “kuongeza nguvu kwenye maarifa ya wenyeji?”

## Muktadha wa kiutamaduni

Utamaduni wa Pulaar unafanya sehemu kubwa ya jamii ya watu wa-chache kabila hilo nchini Senegali. Takribani theluthi moja ya watu milioni 9 wa nchini humo wana-zungumza Pulaar, ni ya pili tu kwa Wolof, ambayo ni lugha ya Kiafrika inayozungumzwa na watu wengi nchini. Katika Afrika Magharibi, kuanzia Senegali mpaka Cameroon ya Kaskazini, wazungumzaji wa Pulaar na lugha za Kifulani wanafi-ka milioni 25, si lugha kubwa sana katika taifa lakini ni lugha maarufu katika baadhi ya nchi za eneo hilo.

Wafulani ni wafugaji wa tangu kale na kwa hiyo ni watu wanaohamama, ni kabila linalosemekana kuwa na asili ya Wamisri wa kale, walioenea katika ukanda wa savana wa kati na Afrika magharibi na kubaki wakazi katika baadhi ya nchi fulani kutokana na kubadili dini na mapambano ya kisiasa. Aidha wamehamia katika nchi nyingine barani Afrika na miji mingi ya Ulaya, Mashariki ya Kati na Kusini mwa Asia.

Kuanzia miaka ya 1950, uzoefu huu wa utamaduni imara na hadhi ya kabila dogo imesababisha kuzaliwa kwa uhuishaji wa utamaduni. Mwaka 1958 mzungumzaji wa Pulaar wa Senegali aliyeishi Cairo kwa miaka ishirini alichapisha riwaya kwa lugha ya Kipulaar—*Ndikkiri Joom Moolo*, au “Ndikkiri, Kifungua Mimba, Mpiga Gitaa”—kilichoandikwa kama njia ya kukumbuka nchi yake. Ni hadithi—ambayo inaanza na hamu, usafihi na kikwakwa—ya Pulaar asiyependa ushujaa aliyeacha nyumba na kwao kufanyakazi yenye mafanikio kama msanii wa jukwaani, kasisi wa dini na mwisho kiongozi mwenye kipaji alichopewa na mungu, aliyefuatiliwa mara kwa mara na viongozi wa kisiasa, lakini hatimaye alishinda na kuendelea kushikilia utamaduni wake na familia. Mwandishi aliamua kutumia maandishi ya Kilatini ya lugha hiyo badala ya “ajami” au maandishi ya Kiarabu, ambayo ni matumizi yaliyowekewa mipaka kwa miaka mingi miongoni mwa wasomi wa kidini.

Ingawa kimetapakaa makosa ya uchapishaji kutokana na Wamisri kushindwa kusahihisha vyema, kitabu hicho hatua kwa hatua kimejipatia wasomaji katika mtawanyiko wa Wapulaar wenye shauku. Msomaji mmoja wa kwanza ambaye baadaye alitokea kuwa mhariri wa machapisho ya Lugha ya Kipulaar anasimulia jinsi kitabu hicho kilivyomwingia. Amejikuta akiisoma riwaya hiyo nje ya nyumba yake saa tisa alfajiri ili wenzake walale bila usumbufu.

*Mara nyingine nilikaa kandokando ya barabara nikisoma riwaya ya Ndikkiri. Kwa kila ukurasa, nilishindwa kujizuia kucheka kwa sauti wakati nilipokuwa nimeketi mtaani.... siku ya pili, niliwasimulia marafiki wangu hadithi kutoka Ndikkiri—wakati tukinywa chai pamoja. Hatimaye marafiki wangu wote waliojua kusoma Pulaar walishindwa kujizuia kusoma kitabu hicho...*

### Kuzaliwa kwa vuguvugu

Shauku ya namna hii ilisaidia kuzaliwa kwa mabadiliko ya kufufuliwa kwa usomaji na uandikaji wa utamaduni wa Kipulaar miongoni mwa watu wanaoishi Mashariki ya Karibu, yaani Uturuki na Afrika Kaskazini. Kutokea

hapo, juhudi hiyo ilienea hadi Ufaransa na mwaka 1982 iliingia Senegali kwa sura ya *Chama cha Mwamko Mpya wa Pulaar* (ARP), asasi inayowaunganisha wazungumzaji wa Kipulaar wanaoishi nchi za ng'ambo na wale wanaoishi maeneo ya mijini ya Senegali waliotaka watoto wao waelewe utamaduni wao.

Miaka iliyofuata, ARP ilipiga hatua jubwa kutokana na kuenea kwa programu za kusoma na kuandika lugha za Kiafrika kwa upande mmoja na kutokana na tishio la kutumia Kiwolof kama lugha rasmi ya mawasiliano nchini humo na hivyo kuelekeza nguvu zake katika kukuza madarasa ya kusoma na kuandika kwa Pulaar nchini Senegali. Mamia ya madarasa ya namna hiyo yalianzishwa katika kipindi cha miaka mitano iliyofuata—madarasa hayo yalifadhiliwa na wakala za serikali au miradi rasmi ya maendeleo pamoja na madarasa mengine mengi yaliyoanzishwa na jamii zenyewe. Hata hivyo viwango vilikuwa vya chini sana; mifumo ya maandishi iliyotumiwa ilitofautitofautiana; na ufuatiliaji wa maandishi ulikuwa adimu sana. Hata hivyo shauku ilikuwa halisi na juhudi hiyo ilikuzwa nyumbani kwa upendo.

Ili kurekebisha udhaifu uliojitokeza katika kampeni, kikundi cha waandishi wa Pulaar kiliunda Kikundi kwa ajili ya Juhudi za kukuza Vitabu kwa Lugha za Kitaifa au GIPLLN, kukusanya vitabu vilivyopo na kuwezesha usambazaji wake kwenye madarasa ya kusoma na kuandika. Silika yenyewe ilikuwa nzuri, ingawa juhudi yenyewe inaonyesha matarajio makubwa kuliko vile ambavyo timu ya waandishi ingeweza kumudu. Hatimaye mwaka uliofuata shughuli zake zilihamishwa kwa chama kisicho cha kibiashara cha ARED kilichosajiliwa Marekani. Wanachama wa GIPLLN walikuwa sehemu kubwa ya Bodi, ingawa WaSenegali wenye utaalumu na Mtafiti wa Kimarekani aliyeoana na mzungumzaji wa Kipulaar waliletwa kama watendaji wa chama. ARED ilianza kwa kuchapisha upya vitabu vya lugha ya Pulaar vilivyopo na kuandika vingine, kimsingi kama huduma kwa vituo vipya vya kisomo.

### Mafanikio yasiyotarajiwa

Jitihada hizo zilifanikiwa sana kuliko wahamasishaji wake walivyotarajia. Mchanganyiko wa kozi za kisomo, kuzidi kupata mwamko kwa jamii iliyotawanyika, na kukua kwa AZISE na kufungua maeneo mazuri zaidi ya uenezaji na mawasiliano na watu wanaozungumza lugha ya Pulaar, imetoa “soko” zuri la vitabu hivyo. Idadi ya vitabu iliongezeka kutoka 6,000 mwaka 1988 na kufikia 41,000 mwaka 2000, na majina ya vitabu yaliyochapishwa yalianza machache hadi kufikia zaidi ya 150. Asilimia 95

ya mauzo yalikuwa ya wateja wa Senegali. Bei zilipangwa ili kufidia gharama za uchapishaji na kuwezesha wauzaji kupata faida ya asilimia 25 ya uhakika.

Kusema kweli, “wauzaji hawakujumuisha hata duka moja kubwa la vitabu la nchini, ambalo lilikuwa linafanya biashara ya vitabu vya fasihi ya lugha za Kiafrika. Hata hivyo ARED inategemea idadi ndogo ya wafanyabiashara wanaotaka vitabu vyao kwa ajili ya wasomaji wenyeji na kununua vichache ili kuviuza. Hadithi wanayoipenda wasomaji inahusu kijana aliyetembea kuanzia Kayes (nchi jirani ya Mali) mpaka Dakar, mji mkuu wa Senegali, huku akiswaga kundi kubwa la ng’ombe. Aliuza ng’ombe wake kwenye mnada na kufika ofisi za ARED akiwa na sehemu kubwa ya mapato yake. Zaidi ya faranga 1,000,000 za Afrika Magharibi (kiasi cha Dola 1,500 za Marekani). Kwa fedha hizo alishakusudia kununua vitabu kwa lugha ya Pulaar na kuviuza tena jimbo la Kayes, idadi ambayo tayari imetakiwa na wauzaji wengine wadogowadogo nchini huko. Kijana huyo alibeba maktaba ndogo mpaka kituo cha garimoshi, akiwa na uhakika wa kupata faida kubwa atakaporudi nyumbani.

### Machapisho anuwai ya vitabu

Ilipofika mwisho wa mwaka 2000, ARED na mtangulizi wake, GILLPIN, walisambaza nakala 350,000 za machapisho yao, yanayowakilisha majina ya vitabu 168 tofauti, 85 kati yao yakiwa katika lugha ya Kipulaar au kufasiriwa kwa lugha hiyo na vilivyobaki vilikuwa kwa lugha nyingine za Senegali, kikiwemo Kifaransa. Rundo hili la vitabu linaweza kugawanywa katika angalau makundi mawili ya mada na chanzo. Vitabu hivyo viliandikia mada zifuatazo:

- *Miongozo ya kusoma, kuandika na kuhesabu* (majina saba ya vitabu yalichapishwa mwaka 2000 na viwili kati yao vilikuwa vipya).
- *Riwaya, hadithi na hadithi nyingine za fasihi* (kitabu kipya mwaka jana).
- *Habari za maendeleo na jamii ya kiraia* (majina sita ya vitabu yalichapishwa mwaka 2000, viwili kati ya hivyo ni vipya).
- *Tasnifu kuhusu maarifa asilia na desturi za kimila au kidini* (majina matatu, mawili yalikuwa mapya).
- *Kitabu cha Kiada kwa ajili ya ujenzi wa uwezo wa menejimenti* (kitabu kimoja kipya).

Vimetumika vyanzo vinne tofauti vya kuandikia vitabu hivyo. Chanzo cha kwanza ni vitabu—hasa vya kidini au vya kubuni—vilivyoandikwa na waanzilishi wa GILLPIN na ARED. Vya pili ni maandiko yaliyotayarishwa na

kuchapishwa na wafanyakazi wa ARED, hasa mfululizo wake wa miongozo ya mafunzo ya kusoma na kuandika ya msingi. Kundi la tatu lina vitabu vipya vilivyotayarishwa na wafanyakazi, au machapisho yaliyopo yaliyotafsiriwa nao kwa Lugha za Senegali, kutokana na ombi la baadhi ya wafadhili wa nje. Machapisho ya kundi hili hujumuisha kila kitu kuanzia miongozo ya mabwanashamba wa ugani hadi tafsiri ya Pulaar ya *L’Aventure Ambigue*, riwaya maarufu ya mwandishi wa KiSenegali, Cheikh Anadozi Kane, kilichotafsiriwa chini ya usimamizi wake. Kinachofurahisha ni kwamba, mifano yote iliyotajwa, wafanyakazi wa ARED na wauzaji vitabu wanaushahidi kutoka kwa wasomaji miongoni mwa watumishi wa Serikali na Wanafunzi wa Chuo Kikuu waliokiri kuwa hawakuelewa kitu katika nakala za lugha za kigeni mpaka waliposoma nakala ya lugha ya Kipulaar.

Kundi la mwisho, si kwa ubora bali kwa mfuatano ni miswada isiyoombwa bali huwasilishwa na waandishi wa kujitegemea. Vitabu vya aina hiyo vimekuwa vichache sana mpaka miaka ya karibuni, kwa sababu ARED haikuandaa kanuni za mikataba za wazi za malipo kwa waandishi wa kujitegemea. Hata hivyo matatizo hayo hivi sasa yametanzuliwa: Waandishi ambao vitabu vyao vilivyochapishwa walilipwa asilimia 10 ya mrabaha wa mauzo ya vitabu vyao kwa awamu mbili. Aidha asasi imeamua katika mkutano mkuu wa hivi karibu, kuwashawishi mara kwa mara waandishi wa kujitegemea kuwasilisha kazi zao ili kukuza wingi wa uandishi wa machapisho ya wenyeji; mpaka sasa vitabu vilivyochapishwa vimeongezeka na kufikia majina sita.

### Sera za kifedha

ARED haisambazi vitabu vyake bure, bali inajaribu kupanga bei zake katika kiwango cha kufidia gharama za uchapishaji na ziada ndogo kwa ajili ya kamisheni ya wauzaji, bei ambayo ni nafuu kwa hali ya Senegali. Vitabu vingi vinauzwa kwa wastani wa sawa na dola 1.50 za Marekani. Baadhi ya vitabu vinapata ruzuku na wafadhili wa nchi za nje, kwa mfano AZISE zenye shauku ya kutumia miongozo ya kusoma na kuandika au kugharimia machapisho kuhusu mada za maendeleo; au mashirika ya misaada yanayotaka kuchapisha vitabu vitakavyofaa kwa kazi za mabwanashamba wa ugani kwa miradi wanayoifadhili. Vingine huchapishwa kwa “fedha za uwekezaji” za ARED, au akiba waliyojiwekea kutokana na utoaji wa mafunzo mbalimbali na shughuli za uchapishaji kwa miaka mingi.

*Kwa jumla*, hivi sasa ARED inagharimia asilimia 75 ya gharama za uchapishaji wake kutokana na mauzo ya

vitabu na asilimia 25 kwa ruzuku na fedha zake za uwekezaji, na kufanya ikaribie kuwa mfuko wa kujitegemea wa machapisho ya Lugha za Kiafrika katika nchi za Afrika Magharibi zinazozungumza Kifaransa.

Katika kipindi cha miaka iliyofuata cha muongo uliopita, mfuko wa shirika hilo ulitunishwa sana na wateja wawili. Mteja wa kwanza alikuwa programu za kisomo za serikali zinazofadhiliwa na nchi za nje, ambapo chini ya programu ya Senegali ya *faire faire* au mkakati wa utoaji wa huduma uligatuliwa madaraka, zilifadhili asasi mbalimbali zisizo za serikali ili kutekeleza miradi yao wenyewe ya kisomo na ziliidhinishwa kununua miongozo na vitabu kutoka mashirika ya uchapishaji kama ARED yaliyochapisha vitabu bora vilivyoidhinishwa. Kutokana na ukubwa wa ununuzi wao, kwa mfano, vitabu vya msingi vya kisomo kwa Lugha ya Pulaar mauzo yake yalipanda kutoka takribani nakala 9,000 mwaka 1995 hadi kufikia zaidi ya 40,000. Chanzo kingine kilikuwa msaada mkubwa kutoka Mfuko wa Msaada wa Kilutheri Duniani (LWR) katika miaka ya mwanzo na ya kati ya muongo, kwa ajili ya mafunzo ya vyama vya wenyeji na utayarishaji na uchapishaji wa maandiko mbalimbali. Machapisho 47 ya mwisho yaligharimiwa yote au sehemu tu na LWR. Hata hivyo msaada wake, ulipunguzwa ghafla kuanzia mwaka 1998 kutokana na matatizo ya shirika hilo katika kuchangisha fedha. ARED ililazimika kupunguza wafanyakazi wake kuunganisha shughuli zake, na kuelekeza nguvu zake kwenye maeneo yenye mahitaji makubwa yatakayoweza kuzalisha biashara mpya. Hatimaye juhudi hizo zinaonekana kufanikiwa. Katika mwaka 2000, ARED ilizalisha vitabu vipya 12 na CERFLA iliendesha mafunzo mapya 26, hali ya kuwa jumla ya vitabu vilivyozwa ilipungua hadi 23,000 katika mwaka uliofuatia upunguzwaji wa ruzuku kwa machapisho yake ilifikia 41,000.

### Mambo ya kujifunza

Je, uzoefu wa ARED umetoa mafunzo gani? Kutokana na hali iliyoelezwa kuhusu ARED, ni dhahiri kwamba kutokana na hali ya Senegali ambapo chama kimekabibiliana nayo katika miongo miwili iliyopita, inawezekana kuendesha biashara isiyo na faida na shirika la uchapishaji kwa ajili ya kisomo kwa Lugha za Kiafrika na

kwa uenezaji wa maarifa asilia. Kuna kanuni zinazoweza kufanyakazi zitakazotegemea zaidi mauzo na mapato ya huduma (ingawa hutolewa kwa kiasi fulani na AZISE na mtandao wa fedha za msaada), bila ya hata msaada mkubwa kutoka mashirika ya misaada. ARED imefanikiwa kipindi hiki na kuweza kuendelea kukua. Hata hivyo vipengele vingi visivyo vya fedha vimetoa mchango mkubwa katika mafanikio ya chama:

- ARED na CERFLA ni “vuguvugu” na mashirika ya biashara yasiyotengeneza faida. Michango kutoka kwa baadhi ya viongozi wa muhimu kisiasa za jamii za Wanaozungumza Pulaar nchini Senegali na nje ya nchi, imekuwa muhimu sana kwa kukomaa na kukua kwao.
- Uwezo wa kusoma na kuandika na kutambua yanayofaa kwa maendeleo ya machapisho ya lugha za Kiafrika na maendeleo ya kisomo umekuwa muhimu pia. Kutokana na ari iliyopo ya ugatuaji madaraka, uwezesaji wenyeji na ufufuaji wa utamaduni unasababisha kanuni hiyo ifanye kazi, hata hivyo ari zaidi ya ujasiriamali na busara inatakiwa kufanikisha lengo hilo.
- Msaada mzuri wa kiasasi kwa ajili ya utunzaji wa hesabu na usimamizi umekuwa muhimu. ARED inafaidika na mfumo na sifa nzuri kwa usimamizi wa rasilimali na kutokana na hadhi yake kama chama kilichosajiliwa Marekani na Senegali.
- Kinyume chake, pengine, vipengele vya mapinduzi ya habari vimerahisisha na kuunga mkono kazi ya uchapishaji kwa Lugha za Kiafrika. Kompyuta zinaweza kushughulikia miundo maalumu ya miandiko (chapa) kwa ajili ya sauti mahususi za lugha zilizoleta vipingamizi vikubwa katika enzi ya taipu, uchapishaji kwa “desk-top” unarahisisha sana usanifu na uchapishaji wa nyaraka, na barua pepe inarahisisha mawasiliano ya mitandao na marafiki wa mbali.

### Kutambua rasilimali inayotoweka

Juu ya mambo yote hayo, hakuna budi kuongezwa hadhi ya makabila madogo na unyumbufu wa jamii ya Pulaar, zilizochangia katika juhudi kiasi fulani cha uzuri au wa “juhudi hii ya dhiti.” Hakuna kitu kinachounda vipaumbele vya maarifa asilia na ari ya kudumisha hata zaidi, inaelekea, kama ambavyo watu wengi wanavyofahamu, kuwa yamo hatarini kupotea.

# Uunganishaji wa Vigezo vya Kisayansi na Asilia katika Utabiri wa Mvua

Makala hii iliandikwa na Carla Roncoli, Keith Ingram, Paul Kirshen na Christine Jost wa Mradi wa Utabiri wa Hali ya Hewa kwa ajili ya Rasilmali za Kilimo (CFAR), mradi wa utafiti unaoshirikisha taaluma mbalimbali ulioanzishwa kwa ushirikiano baina ya Chuo Kikuu cha Georgia na Chuo Kikuu cha Tufts na kufadhiliwa na Ofisi ya Programu ya Dunia ya Usimamizi wa Bahari na Hewa ya Taifa. Toleo refu zaidi linakuja katika jarida la *Society and Natural Resources*, juzuu 15. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Carla Roncoli kwa: (404) 524-8833 au [croncoli@gaes.griffin.peachnet.edu](mailto:croncoli@gaes.griffin.peachnet.edu).

## ***Tini za MA 39 Desemba 2001***

Uchunguzi kifani huu unaeleza jinsi wakulima wa Burkina Faso wanavyotabiri mvua za msimu na kuchunguza jinsi utabiri wao unavyofanana na utabiri wa kisayansi. Katika miaka ya karibuni, sayansi ya metorolojia imekuwa na mafanikio makubwa sana katika utabiri wa hali ya hewa. Kutambua kuwa joto la juu ya bahari huathiri mzunguko wa pepo duniani na huwawezesha wanasayansi kupanga utabiri wa mvua za msimu. Huu huwasilishwa kama uwezekano wa jumla ya kiasi cha mvua za msimu kuwa juu ya kiwango, chini ya kiwango, au kawaida ikilinganishwa na wastani uliotokana na tathmini ya mfululizo wa miaka thelathini. Katika Afrika Magharibi, mvua za msimu huhusishwa na miezi mitatu ya Julai, Agosti na Septemba, ambapo asilimia 90 ya mvua za msimu hunyesha.

Badala ya kuona ujuzi wa kienyeji na kisayansi kutofautiana kabisa, utafiti wetu unaonyesha kuwa wakulima wamezoea kufanya kazi katika mifumo tofauti ya utambuzi na kuwa wana hamu ya kupata utabiri wa kisayansi kwa sababu wanaona kuwa utabiri wa kienyeji unakuwa na mafanikio kidogo sana kutokana na hali ya hewa kuzidi kubadilika. Lakini ili kufanya utabiri wa hali ya hewa wa kisayansi tunahitaji kuelewa watu wanafikiri nini kuhusu mvua,

pamoja na wanaonaje na kutabiri mabadiliko. Kuelewa utamaduni wa wenyeji ni muhimu kwa ajili ya kuunganisha bidhaa za utafiti na teknolojia ya maendeleo.

### **Mahali na njia za kujipatia maisha**

Bonam ni kijiji kilicho katika jimbo la Namentenga, moja ya majimbo maskini zaidi miongoni mwa majimbo arobaini na tano nchini Burkina Faso. Sehemu kubwa ya wakazi wa Bonam ni wa kabila la Mossi, kabila lenye watu wengi zaidi nchini, na hupata riziki zao kwa kilimo cha nafaka na mazao jamii ya maharage kwa kutegemea mvua, wakichanganya na uzalishaji wa mifugo, biashara ndogondogo na kwenda kufanya kazi Côte d'Ivoire. Baadhi ya wafugaji wa kabila la Fulani pia wanaishi katika eneo hilo.

Mvua hunyesha katika msimu mmoja kuanzia Mei hadi Oktoba, ku kiwa na mvua nyingi za mwaka na kiasi cha mvua kisicholingana katika misimu. Kiasi cha chini cha mvua za muda mrefu ni milimita 674. Wakati wa mwanzo wa mvua za msimu, wakulima huamua watapanda nini, lini na wapi. Hufanya hivyo kulingana na matarajio yao kwa mvua za msimu, hujaribu kupunguza hatari kwa kuangalia uwezo wa kuhifadhi maji wa aina tofauti za udongo na nafasi za

mashamba yenye mahitaji ya maji kwa aina mbalimbali za mazao.

Ujuzi wa wakulima wa kutabiri unajumuisha ujuzi wa pamoja na watu binafsi. Wakulima wenye uzoefu zaidi (zaidi wanaume wazee) hubuni nadharia tete kuhusu mvua za msimu kwa kuchunguza matukio ya asili, wakati wataalamu wa kitamaduni na matambiko hufanya utabiri kutokana na ubashiri, maono au ndoto.

### Ujuzi wa pamoja wa utabiri

Dalili za kimazingira ambazo wakulima hutumia kutabiri mvua za msimu huonekana kwa ajili ya uchunguzi kwa nyakati tofauti za mwaka. Miongoni mwa dalili za mwanzo kabisa zinazotegemewa ni wakati, ukali na urefu wa kipindi cha baridi sehemu ya awali ya msimu wa ukame (Novemba—Januari). Wakulima huamini kuwa baridi kali (chini ya nyuzijoto 15 za sentigredi) wakati huu inalingana na kipindi cha mvua nyingi wakati wa msimu wa mvua na kuwa iwapo kipindi hiki cha baridi kitaanza mapema na kuchelewa kuisha, mvua pia zitafuata mpangilio huo. Kipindi kinachofuatia kipindi cha baridi kavu ni kipindi cha joto na ukavu (Februari—Aprili): joto kali wakati huu pia linaaminiwa kuwa ni dalili za mvua za kutosha.

Dalili ya pili ya utabiri wa hali ya hewa uliozoeleka ni utoaji matunda wa baadhi ya miti ya kienyeji, unaotokea kati ya Aprili na Juni. Kulingana na maelezo ya wakulima, mavuno mazuri ya matunda kama vile *taanga* (*Butyrospermum parkii*) na *sibga* (*Anogeisus leiocarpus*) yanaashiria msimu mzuri. Kwa upande mwingine, wakulima huhusisha utoaji wa matunda mengi kwa miti ya *nobga* (*Sclerocarya birrea*) na *sabtuluga* (*Lannea acida*) na ukame.

Miti pia hutumika kama dalili za kuonyesha kukaribia kunyesha mvua au kuwepo kwa maji. Wakati miti ya *sigba* inapoanza kutoa matunda na *sabtuluga* inapoanza kupukutisha majani wakulima hutambua kuwa wakati umefika wa kuandaa mashamba. *Kankanga* ni mti jamii ya mtini ambao huota mahali ambapo maji yako karibu na usawa wa ardhi. Hivyo, huwaashiria wafugaji mahali panaofaa kuchimba visima ili kunywesha mifugo yao na wakulima mahali wanapoweza kupanda mazao yanayohitaji maji mengi, kama vile pamba.

Dalili nyingine inayopatikana katika mvua za mwanzo zinaponyesha ni kiwango cha maji katika mifereji na madimbwi. Iwapo maji yataendelea kuwa mengi baada ya mvua ya kwanza, wakulima wanaamini kuwa msimu utakuwa mzuri kwa kuwa mvua nyingi wakati wa mwanzo zinaaminika kuwa dalili za neema. Wafugaji ambao huchunga wanyama msituni huangalia ujenzi wa viota unaofanywa na ndege wadogo wazuri (wajulikanao kama

*koobre* huko Moré) na wanaamini kuwa kama viota vitajengwa juu sana katika miti basi mvua zitakuwa nyingi; iwapo viota vitajengwa katika matawi yaliyo chini, kutakuwa na upungufu wa mvua.

Wanawake pia huchunguza tabia za wadudu katika vyanzo vya maji na katika malundo ya taka nje ya nyumba. Kwa mfano, *bugvaré* ni wadudu weusi wa jamii ya *Orthoptera* ambao hutoboa matundu ya mvingo katika malundo ya taka nje ya nyumba. Baada ya mvua za kwanza, lava hutokea na kisha hujaza matundu kwa uchafu. Wanawake wameeleza kuwa hutarajia msimu utakuwa mzuri kwa kilimo iwapo *bugvaré* watajaza matundu yao hadi juu kwa uchafu, ambao huonyesha dalili za ghala kujaa nafaka.

Lakini, wakati dalili huchunguzwa wakati wote wa msimu wa ukavu, ni wakati mvua zinapoanza ndipo wakulima wanapounganisha matarajio yao kwa msimu wa mvua. Mvua za mwanzo, hasa zikiwa na mafanikio ya mara kwa mara ya mvua zinazosaidia mimea kuota vizuri, ni dalili za msimu mzuri zinazochukuliwa na wengi. Jinsi mkulima anavyoweza kupanda mazao mara nyingi pia ni njia muhimu ya kutathmini hali ya msimu na kutabiri mafanikio katika kilimo. Kwa mfano, ukame ulipoathiri kanda mwaka 1977, wakulima walijua kuhusu tatizo la kubwa la upungufu wa chakula lililoonekana mapema mwishoni mwa msimu wa upandaji (mwanzoni mwa Agosti), nusu mwaka kabla mifumo rasmi ya kutahadharisha kuhusu njaa haijatoa dalili za dhiki.

Baadhi ya wazee pia wanaweza kutafsiri duru ya mizunguko ya nyota na mwezi. Kwa mfano, huangalia duru za kuonekana kwa mwezi, hasa mwezi mzima, ni dalili ya mvua kutonyesha kuliko duru ya giza kwa sababu mwanga wa mwezi hutoa nguvu zinazozuia mvua kunyesha. Nyota pia huonyesha dalili za wakati mwafaka kwa kulima mashamba mbalimbali na aina mbalimbali za mazao. *Souci* (Pleiades) kuonekana mwanzoni mwa mwezi Mei ni dalili kuwa ni wakati mwafaka kuandaa mashamba yaliyo mabondeni kwa kulima. Kubadilika katika nafasi za *Budb Kutoega* (Ursa Major) kunaonyesha mwanzo na mwisho wa msimu wa kupanda mtama. Kuonekana kwa *Tabta* (Orion) mwezi Julai kunagongana na mvua nyingi (*sa nyanga*) zinazosaidia kilimo cha mahindi.

### Ujuzi maalumu wa utabiri

Tofauti na uchunguzi wa dalili za mazingira zinazopatikana kwa wakulima wengi, utabiri wa nyota na matendo mengine ya kiroho ni haki ya vikundi maalumu au watu binafsi. Mwenye mamlaka kuu zaidi miongoni mwao ni *Tengsoba*, mtu wa kwanza katika ukoo aliyeanza kuishi



katika eneo hili. Hutoa sadaka ili kuunganisha watu walio hai na mababu na mizimu inayoishi katika maeneo ya kuabudu ambayo baadhi yao huathiri mvua. Utabiri huchukuliwa kutokana na tabia za wanyama wanaotolewa dhabihu, itamchukua muda gani kuanguka, ataanguka kuelekea upande gani, na damu itatiririka wapi. *Tengsoba* na wataalamu wengine wa jadi pia wanaweza kupata utabiri toka kwa mababu au miungu kwa ndoto au maono.

*Marabouts* ni watu ambao huamini mizimu na kujiingiza katika utamaduni wa kiislamu, ingawa imani za Kiislamu zinachukua shughuli zao. Waumini hawa wa mizimu ni kuanzia viongozi wa Kiislamu (*Limam*) ambao wametajwa katika Kurani kuwa watabiri wanaouchanganya Uislamu na imani na shughuli za jadi. Sherehe ya *Zambende*, inayofanyika kusherehekea kuanza kwa mwaka wa Kiislamu, ni wakati muhimu wa kukutana kwa *Marabouts* kufanya utabiri wao. *Marabouts* katika utabiri wao huangalia siku ya juma inayosherehekewa kama siku ya kwanza ya *Zambende*. Kila siku inahusishwa na manabii mbalimbali na mwaka unaofuata hufafanuliwa kwa dalili za matukio katika maisha au wakati wa nabii huyo. Ubashiri umeandikwa kwa maandishi ya Kiarabu pamoja na maelekezo ya sadaka na hatua nyingine za kuepusha matukio yenye kuleta balaa.

Tofauti na *Tengsoba* na *marabouts* ambao huweza kutoa utabiri na sala za maombi tu, kuna wataalamu wengine wajulikanao kama *sa tatta*, ambao hudai kuwa na uwezo wa moja kwa moja kutoa amri dhidi ya mvua. Lakini nguvu zao huogopwa kwa kuwa utengenezaji wa mvua huonekana kuhatarisha wataalamu pamoja na jamii. Mvua za kuomba zinaaminika mara nyingi hunyesha kwa fujo (*saraogo*) zikifuatiwa na upepo mkali, radi yenye mngurumo mkali na vimulimuli inayoweza kuharibu mazao, nyumba na wanyama. Kwa sababu hii, mradi wa serikali wa upandaji mbegu katika hali ya mawingu mwanzoni mwa msimu wa mvua za 1988 ulisababisha hasira badala ya nafuu miongoni mwa wakulima huko Bonam.

Baadhi ya watabiri walitabiri ukame wa mwaka 1997 na majibu yao yana athari kwa jukumu lao kuu katika uenezaji wa utabiri wa kisayansi vilevile. *Tengsoba* alikubali kuwa na wasiwasi mkubwa katika msimu wa ukame, lakini hakuonyesha. Watabiri wengine wamekubali kuwa wana tabia ya kutoeleza wasiwasi kwa sababu kufanya hivyo "itakuwa kama kushusha laana" dhidi ya wale walio chini ya mamlaka yao. Kueleza utabiri wa matukio mabaya kutawaweka katika matokeo yasiyoepukika kwa kubatilisha uwezekano wowote wa kufanya maombi na kuongea na mizimu. Kushindwa kubadilisha utabiri wa kutisha kunaweza pia kupunguza imani ya watabiri wanaowajibika kuwa kiungo kati ya walio hai na mizimu. Zaidi ya hayo, utabiri usiokamilika unaweza kukatisha

watu tamaa ya kulima na kuwafanya wahame, kwa kudharau mpango wa kijamii yalipo mamlaka ya wazee.

### Kuchanganya utabiri wa kienyeji na wa kisayansi

Wakulima wa Bonam wanatambua kuwa jamii pamoja na hali ya hewa imekuwa na mabadiliko fulani katika miongo michache ya hivi karibuni. Viongozi wa jadi wanasikitika kuwa elimu rasmi, dini zenye kuabudu Mungu mmoja, na itikadi za kufuata mambo ya kisasa zimepunguza mamlaka yao, hasa miongoni mwa vijana. Mabadiliko ya hali ya hewa pia yamedhoofisha imani ya wakulima kwa ujuzi wa wenyeji. Wazee wamekumbuka kuwa siku za nyuma walikuwa na uwezo wa kutabiri mwanzo wa mvua kwa usahihi kiasi ambacho waliweza kufanya kazi kifamilia ya kusia mbegu katika ardhi kavu, wakijua kuwa mvua zitanyesha punde, lakini sasa watoto wao wanakataa kwenda shamba mpaka mvua zinyeshe.

Lakini hii haina maana kuwa wakulima wanatambua taarifa za kisayansi kuwa ni tishio kwa utamaduni wa wenyeji. Kinyume na hivyo, kwa sababu wanatambua kuwa utabiri wa kienyeji hauaminiki, wakulima wako tayari kutumia vyanzo mbalimbali vya habari. Kuliko kusimama mahali pamoja na kufanana, uwanda wao wa utambuzi tayari umekuwa na ujuzi wa aina mbalimbali. Utabiri wa kienyeji umechanganya uchunguzi wa kuangalia moja kwa moja na maono ya kiroho yanayotokana na utamaduni wa dini mbalimbali. Wakulima huchanganya utabiri wa kienyeji na teknolojia na familia huchanganya dawa ya kisasa na kienyeji kwa vitendo wakati mmoja wa mwana familia anapougua. Ni matumizi mabaya ya mfumo wa ujuzi wa yeyote kama jumla ya ukweli ambao umekasirikwa au kupingwa.

Hivyo, maelezo ya kisayansi lazima yawasilishwe kwa njia ambazo hufuata fikra za kitamaduni kuhusu aina ya ujuzi, uzalishaji wake na uhalali, na uhusiano wake na jamii. Mifumo ya kienyeji ya mawazo inasisitiza asili ya upendeleo wa uelewa wa binadamu, ambao humaanisha kuwa chanzo kimoja cha habari hakichukuliwi kuwa na picha iliyopo. Mifumo ya utabiri ya kienyeji hutegemea dalili tofauti zinazoonwa na watu tofauti na kwa wakati tofauti. Wakulima hawatatui migongano iliyopo miongoni mwa dalili kuwa picha yenye maana. Tofauti miongoni mwa tabiri au baina ya tabiri na matokeo hufafanuliwa kwa tofauti ya mafanikio ya kiekolojia na mifumo ya upandaji. Sifa ya kubahatisha ya utabiri pia inaweza kuelezwa kwa kuangalia sifa ya kutokuwa na uhakika wa bahati kama matokeo ya mazungumzo baina ya walio hai na mizimu na uamuzi wa mizimu.

Kuna vipengele kadhaa vya njia na yaliyomo ambapo ujuzi wa kienyeji na kisayansi wa kutabiri unakutana. Kwa mfano katika kufanya utabiri, watabiri wa kidini hutumia njia za kukumbuka mambo yaliyopita ya utabiri wa kisayansi. Ubashiri wa *Zambende* hutokana na fasili ya maandiko na ushauri miongoni mwa watu wanaowasiliana na mizimu, ambao baadaye huyawasilisha rasmi katika umma. Katika uwanja wa taaluma ya mazingira, utabiri wa mkulima hufanana na mbinu za kisayansi katika kutegemea uchunguzi unaofuata utaratibu rasmi wa matukio ya asili. Uendelezaji wa ujuzi kutokana na kuona unaendana na mbinu za mafunzo ya utamaduni ambapo watoto hujifunza kwa kuwaona watu wazima kuliko maelekezo kwa maneno au kuuliza maswali.

Wataalamu wa hali ya hewa huweza kuchunguza kutokana na utambuzi wa wenyeji kuhusu uhusiano baina ya joto na mvua na kufafanua masuala ya kiufundi ya utabiri wa kisayansi kwa kuangalia joto la juu ya uso wa bahari. Tafsiri ya wakulima ya mawimbi ya upepo pia imetambua bahari kama chanzo cha mvua wakati wa kiangazi, wakulima hutegemea upepo uvume kuelekea magharibi, ikimaanisha kuelekea baharini kuchukua maji na kisha kugeuka na kuvuma kuelekea mashariki wakati wa mwanzo wa msimu wa mvua. Wakulima walitabiri na kufafanua kuhusu ukame kwa kuchunguza pepo kama hizo.

Lakini utabiri wa wakulima unatofautiana na ule wa kisayansi katika njia muhimu, hasa vipimo na vigezo wanavyotumia. Tofauti na utabiri wa kisayansi, ambao hufanyika kwa kuzingatia “kanda” utoaji na matumizi ya utabiri wa wenyeji hufanyika kienyeji mno. Hufanya kutokana na maingiliano ya ndani na mazingira finyu ambayo mahadhi yamepotana na duru za maisha ya familia na jamii. Si *sibga* au *taanga* ambao wakulima wanawaamini katika utabiri wa mvua, bali miti fulani maalumu karibu na nyumba zao au mashamba yao ambayo wameichunguza kwa muda wote wa maisha yao.

Wakati utabiri wa kisayansi unategemea makadirio ya jumla ya wingi wa mvua za msimu, wakulima hutathmini misimu kwa kuangalia aina na muda mvua iliponyesha. Kwa mfano, wanatambua kuwa wingi wa aina moja cha mvua kinaweza kusababisha matokeo tofauti ya uzalishaji iwapo zitanyesha kama *sa nyanga* (mvua za muda mrefu lakini kwa kiwango sawa wakati wote kiasi cha kufanya udongo kuloa kwa siku kadhaa) au kama *saraogo* (ngurumo za radi zikifuatiwa na upepo mkali). Vipindi vya upungufu wa maji vinavyotokea wakati wa kupanda au

ufugaji vitasababisha uharibifu zaidi kwa mazao kuliko vile vinavyotokea katika hatua nyingine za kukua kwa mazao.

Wakati wa mwanzoni na mwishoni mwa mvua, kuonyesha kipindi cha mvua, ni kigezo muhimu ambapo utabiri wa kiwango cha mvua za msimu zilizo “juu ya wastani” kimeeleweka kwa wakulima wa Bonam kutabiri msimu mrefu. Kwa sasa, sayansi inashindwa kutabiri kwa hakika ama muda au mtawanyiko wa mvua za msimu, lakini kuunganisha utabiri wa kisayansi na ujuzi wa wenyeji kunaweza kutatua baadhi ya matatizo ya utambuzi kama huo. Kwa mfano, mvua nyingi zisizo kawaida zilizonyesha Julai na Agosti 1999 zingeweza kutabiriwa kwa kuchanganya utabiri wa wakulima wa kuchelewa kunyesha mvua na utabiri wa kisayansi kwa mvua zinazozidi kiwango cha kawaida cha mvua za msimu.

### Hitimisho

Uchunguzi wetu umeonyesha kuwa si uzoefu wa kuunganisha mifumo ya utaalumu wala dhana za utabiri wa mvua si ngeni kwa wakulima wa Burkina Faso. Utabiri wa wenyeji hufanana na ule wa kisayansi katika baadhi ya vipengele vya utabiri na njia, lakini pia hutofautiana katika utekelezaji na maana za utabiri. Tofauti hizi hutoa changamoto kwa sayansi katika pande zote.

Kwa upande mwingine, uhakika wa vigezo vya utabiri wa kienyeji unaifanya sayansi kuwajibika zaidi kwa mahitaji ya taarifa kwa wakulima na kufuata zaidi maamuzi ya njia za maisha wanazozikabili. Kwa upande mwingine, mfumo wa kienyeji wa utaalumu na uongozi kwa karibu sana unaunganisha ujuzi na majukumu ya kijamii, kuwataka wanasayansi kuwa macho zaidi na kuwajibika na athari za ujuzi wanaotoa na kuwapatia watumiaji.

Majukumu haya yanatupeleka mbali zaidi ya jukumu la kuunganisha ujuzi wa wenyeji na kisayansi katika muundo na jinsi ya utabiri, kupata changamoto ya kueleza matokeo na muktadha wa matumizi yake. Kwa hakika, utoaji wa taarifa unahitaji kuingizwa kwa kutumia uingiliaji kati ulio sahihi ambao utaongeza uwezo wa wakulima kupata matokeo bora ya utabiri uliofanyika. Wanasayansi, wataunga sera, wafadhili, na watendaji wa maendeleo lazima washirikiane kubuni njia zinazolingana na endelevu ili kuboresha uwezo wa kubadilika wa mifumo ya kienyeji ya uzalishaji na uthabiti wa uhakika wa njia za maisha kwa wakulima maskini wa kanda ya Sudan-Saheli.

# **Huduma ya Akinamama Wajawazito Maeneo ya Vijijini Uganda: Uboreshaji wa Mifumo ya Maarifa Asilia na ya Kisasa**

*Makala hii imeandikwa na Dkt. Maria G.N. Musoke (PhD), Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala, Uganda.*

***Tini za MA 40  
Januari 2002***

Uganda ni moja ya nchi zenye maendeleo duni sana ya miji katika Afrika, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya watu wake karibu milioni 20 huishi vijijini. Uchumi wa Uganda hutegemea zaidi kilimo na wanawake huchangia asilimia 60—80 ya nguvu kazi. Hivyo, afya ya wanawake ina maana kubwa kijamii na kiuchumi kwa maendeleo ya taifa. Hata hivyo, miongoni mwa wanawake wa kiganda wenye umri wa kuweza kuzaa, masuala ya afya ya mama ni tatizo kuu kama ilivyoonyeshwa na viashiria vifuatavyo: idadi kubwa ya vifo vya kina mama inayokadiriwa kufikia 506/100,000; idadi kubwa ya uzazi karibu 6:9; karibu asilimia 38 tu ya wazazi huzalishwa na wafanyakazi wa afya waliopata mafunzo, asilimia 62 iliyobaki huzalishwa na wakunga wa jadi na wanandugu. Ili kushughulikia matatizo haya Wizara ya Afya Uganda imepanga mbinu kadhaa na utekelezaji. Baadhi ya utekelezaji huo ni pamoja na kupanua mfumo wa rufaa na kuboresha mtandao wa wakunga wa jadi na vilevile kuwapatia mafunzo wakunga wa jadi. Mradi wa Upanuzi wa Huduma za Afya Vijijini kwa Msaada wa Dharura ulianza kama moja ya juhudi hizo.

## **Maelezo kuhusu mradi**

Mradi wa Upanuzi wa Huduma za Afya Vijijini kwa Msaada wa Dharura

ulifunguliwa Machi 1996, kwa ajili ya majaribio, katika Wilaya ya Iganga, Mashariki mwa Uganda. Kimsingi ni mradi wa rufaa, uliobuniwa kushughulikia tatizo la idadi kubwa ya vifo vya kina mama. Mradi ulianzishwa na Wizara ya Afya, UNFPA, na Sekretarieti ya Idadi ya Watu Uganda. Kikundi maalumu cha wataalamu wa sekta mbalimbali Wilaya ya Iganga kinaendesha mradi huu, wakati UNFPA na Wizara ya Afya zinafanya kazi ya ufuatiliaji.

Mradi wa Upanuzi wa Huduma za Afya Vijijini kwa Msaada wa Dharura una vitengo vitatu: mawasiliano, usafiri na utoaji wa huduma bora za afya.

## **Mawasiliano**

Aina ya teknolojia ya habari na mawasiliano iliyochaguliwa ilitokana na sababu kadhaa, baadhi yao ikiwa ni pamoja na: kutokuwepo huduma ya ni-shati ya umeme katika maeneo mengi vijijini, kutokuwepo simu za kutumia waya, haja ya teknolojia ya habari na mawasiliano kupatikana masaa ishirini na nne kwa siku, uwezo wa kubadilika, haja ya kuutumia mfumo katika maeneo mengine nchini na uendeleu kiuchumi wa mfumo pale msaada wa mfadhili utakapokoma. Kwa sababu hizi, redio ya mawasiliano ilichaguliwa kama aina ya teknolojia ya habari na mawasiliano itakayotumika katika mradi. Hii ni pamoja na stesheni za

kudumu katika vitengo vya afya, redio ya kupokea na kupeleka habari kwa kuwasiliana na wakunga wa jadi, na simu za magari katika magari ya wagonjwa ya hospitali za rufaa na gari la Mganga Mkuu wa Wilaya. Mawasiliano ya redio ya mawasiliano huendeshwa kwa nguvu za mionzi ya jua, kuepuka ukatikaji wa umeme au matatizo ya mawimbi.

Mradi wa Upanuzi wa Huduma za Afya Vijijini kwa Msaada wa Dharura uliandaliwa kuunganisha wakunga wa jadi na mfumo rasmi wa utoaji huduma kwa gharama nafuu, kiasi kwamba dharura ya uzazi inapotokea kijijini, mkunga wa jadi atumie redio yake ya mawasiliano kuomba msaada kutoka katika kitengo chochote cha afya kilicho karibu. Ujumbe kuhusu nini la kufanya hutolewa mara moja kupitia mfumo wa redio. Iwapo mkunga wa jadi atashindwa kumudu tatizo, usafiri hutumwa kutoka katika kitengo cha afya pamoja na mkunga rasmi kumchukua mgonjwa. Iwapo tatizo haliwezi kutatuliwa katika ngazi ya kituo cha afya, hospitali hupigiwa simu na gari la wagonjwa hutumwa kumpeleka mgonjwa katika hospitali ya rufaa.

### Usafiri

Pikipiki za matairi matatu zilitolewa kwa kila kitengo cha mwanzo cha rufaa cha afya kilichoshiriki ambavyo kwa ujumla vilikuwa vituo vya afya vijijini. Gari la zamani la wagonjwa lililokuwa katika hospitali kuu ya rufaa lilifanyiwa ukarabati na kuwekewa mawasiliano ya redio. Wakunga wa jadi walipewa baiskeli ili zivasaidie kwa usafiri kwenda katika vitengo vya afya kuongeza chaji betri za redio zao za mawasiliano na kukusanya takwimu ya mwezi.

### Utoaji wa huduma bora za afya

Hii ilikuwa pamoja na ujenzi wa uwezo (k.m. mafunzo kwa wakunga wa jadi, wakunga rasmi, mafundi), kuajiri angalau wakunga wawili na tabibu mmoja katika vitengo vyote vishiriki vya afya, ukarabati wa wadi za wazazi (ikiwa ni pamoja na kutoa vitanda vya uzazi, oksijeni, na visimamishio vya I.V.) na utoaji wa zana za dharura za uzazi na vifaa vingine.

### Utekelezaji

Kikundi maalumu cha wilaya kinachoundwa na Mkurugenzi wa Huduma za Afya Wilayani (aliyejulikana kama Mganga Mkuu wa Wilaya), na maafisa kutoka katika sekta nyingine katika wilaya kiliundwa ili kusimamia mipango, maendeleo, na utekelezaji wa mradi. Kinawajibika katika safu ya juu zaidi ya uongozi wa wilaya, ambaye ni mwenyekiti wa LC5. Kikundi cha kazi huendeshwa chini ya uenyekiti wa Mkurugenzi wa Huduma za Afya wa Wilaya, na kimeundwa na wawakilishi kutoka sekta zinazohusiana na afya wilayani.

### Matokeo na taathari

Mnamo Julai 1999, mwandishi alifanya uchunguzi kuhusu athari za mfumo wa mawasiliano katika huduma za afya ya mama, na mchango wake katika mradi wa rufaa. Alitaja sababu zinazoathiri mradi, na vilevile gharama na uendelevu wa mradi. Data ilikusanywa kutoka katika vyanzo vikuu na vidogo. Vyanzo vidogo ni pamoja na ripoti ya maendeleo na hati nyingine za mradi. Data kuu ilikusanywa kwa ubora, kwa kufanya mahojiano na kuzingatia matukio yaliyoelewa na wafanyakazi wa afya na wakunga wa jadi. Sampuli ya utafiti inalenga wilaya ya Iganga ambapo mradi umekuwa ukiendeshwa tangu Machi 1996.

Ongezeko la idadi ya uzazi chini ya wafanyakazi waliopata mafunzo na ongezeko la rufaa kwenda katika vitengo vya afya vya rufaa limesababisha kupungua kwa karibu asilimia 50 ya vifo vya kinamama wajawazito katika miaka mitatu kama ilivyoonyeshwa hapo chini:

“Uchunguzi uliofanyika hivi karibuni katika wilaya tatu za Arua, Iganga na Tororo, ambapo wilaya zote wakunga wao wote wa jadi walipatiwa mafunzo, umeonyesha kuwa idadi ya vifo vya kinamama wazazi wa Iganga imepungua kutoka 500/100,000 mwaka 1996 hadi 271/100,000; wakati viwango vya Tororo na Arua vimepungua, lakini zote zilikuwa na idadi iliyo juu ya 350/100,000. Hii imeonyesha kuwa vifaa vya mawasiliano na usafiri kule Iganga vimechangia kupungua kwa Idadi ya Vifo vya Kinamama wazazi. Kabla ya mradi kulikuwa na matatizo ya ukosefu wa vifaa vya mawasiliano na usafiri, ambavyo vimefanya rufaa kwenda polepole na mara nyingine kusababisha vifo vya mama au mtoto au wote pamoja” (Msimamizi).

Vitengo sita vya afya na hospitali moja ya rufaa vilishiriki katika mradi. Kati ya hivyo, vitengo vinne vya afya na hospitali ya rufaa vilifanyiwa uchunguzi na wakunga wao walihojiwa. Kwa kuongezea, wakunga kumi wa jadi, waendeshaji mradi watatu na wanawake wanne wanufaika walihojiwa.

Kwa wakunga wa jadi, teknolojia ya redio za mawasiliano ilikuwa chanzo kikuu cha uwezeshaji kwa kuwa iliboresha hadhi yao na heshima, hivyo kuongeza heshima ya ushauri wa rufaa na pia kuongeza mapato yao kwa kuongeza idadi ya wanawake wanaowazalisha. Wale ambao hawawezi kuandika zaidi wametaja kuwa:

“Kwa kuwa siwezi kuandika, ni vigumu kwangu kuwapatia rufaa wanawake; Ilibidi niende nao katika kitengo cha afya na kueleza ... lakini sasa, redio za mawasiliano zime-niokoa kutokana na matatizo hayo, kwa sababu ninaweza kumpigia mkunga na kueleza hali ya mtu ninayempatia rufaa ... Silazimiki kwenda kumsindikiza kila mtu ninayempatia rufaa” (TBA7).

Teknolojia ya mawasiliano imewaleta wakunga wa vijijini karibu baina yao, hivyo kupunguza kutengwa na kusaidia kutoa ushauri. Hali za kuwa na wasiwasi wa utatuzi usio-

kuwa na hakika wa matatizo ilipunguzwa kwa kiasi kikubwa.

Katika hospitali ya rufaa, mawasiliano yaliripotiwa kuifanya kazi ya wakunga kuwa rahisi zaidi kwa kuwa waliweza kujua mapema wategemeo nini na kujiandaa kwa dharura. Wanawake wanufaika waliripoti kuwa mawasiliano haya yamewapa matumaini katika hali za hatari.

### Mafunzo yaliyopatikana

Uchunguzi umeonyesha idadi kubwa ya mafunzo.

#### **Kukamilishana**

- Idadi kubwa ya shughuli za ziada inahitajika ili kuleta athari kamili. Kwa mfano, uchunguzi umegundua kuwa ingawa sehemu ya mawasiliano imetoa mchango mkubwa katika mafanikio ya Mradi wa Upanuzi wa Huduma za Afya Vijijini kwa ajili ya Msaada wa Dharura, haikuweza kusimama yenyewe. Ili mradi utimize malengo yake ya uboreshaji wa rufaa zitakazosaidia kuboresha huduma za uzazi zitolewazo na wakunga waliopata mafunzo, vipengele vingine viwili (usafiri na ubora wa utoaji huduma) ilibidi vitekeleze wajibu wao wa ziada. Pale usafiri ulipoharibika, hata hivyo, iliripotiwa kuwa kuwepo kwa mkunga na mfumo wa mawasiliano ulichukua jukumu kubwa la kuokoa maisha: Wakunga wa jadi waliitwa kupeana ushauri na vitengo vya afya, hivi pia viliombwa kushauriana na wenzao na wakuu wao. Hata hivyo, pale dharura ilipolazimu kufanya rufaa, haja ya kupata usafiri ilikuwa muhimu sana.

#### **Teknolojia**

- Athari za teknolojia ya habari na mawasiliano huongezeka kama teknolojia ni sahihi kwa mazingira ya mahali husika. Kama ilivyoonyeshwa, uchaguzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano ulifanyika baada ya kuchambua kwa kina matatizo ya maeneo ya vijijini nchini Uganda.
- Matumizi ya nishati ya mwanga wa jua kwa mfumo wa mawasiliano yangevinufaisha vitengo vya afya vijijini ambavyo havina umeme. Kwa hakika, uchunguzi umependekeza kuwa nishati ya mwanga wa jua itumike zaidi kutoa mwanga katika wadi za uzazi/vyumba vya kuzalishia kwa vitengo vya mwanzo vya rufaa.
- Muundo rahisi wa mfumo wa mawasiliano ya redio ulisaidia matumizi yake kulingana na watu wote waliohojiwa.

- Kusikika kwa sauti kubwa kwa mawasiliano ya redio kumesaidia kuzuia matumizi mabaya au kutumia kwa manufaa binafsi. Watu waliohojiwa waliripoti kuwa miito iliyofanyika kwa kawaida ni mifupi na kwenda mahali husika, na kuwa muundo wa aina hii ya teknolojia ya habari na mawasiliano unailinda kutokana na wizi.

- Njia ya kuwepo madaraja mengi katika teknolojia ya habari na mawasiliano kunaweza kusaidia kuleta manufaa ya teknolojia mpya kwa watu wa vijijini katika Afrika Kusini mwa Sahara. Njia kama hiyo itasaidia kutokana na uwezo tofauti katika hali ya Afrika. Kwa mfano, huduma ya matibabu kwa njia ya simu (telemedicine) na vifaa vingine vya teknolojia ya kisasa (k.m. Intaneti) inaweza kuwekwa katika hospitali ya wilaya, wakati teknolojia rahisi kama redio zinaweza kusaidia ngazi za chini (vituo vya afya vijijini, wakunga wa jadi, n.k.). Mashauriano yaliyofanywa na vituo vidogo kwenda katika hospitali za wilaya yatahakikisha kuwa watu wa vijijini wananufaika moja kwa moja kutokana na teknolojia.

#### **Uwezo wa taasisi**

- Mradi umeundwa katika miundombinu iliyopo na uwezo uliokuwepo, ikiwa ni pamoja na mifumo ya ujuzi wa jadi. Ujuzi wa wakunga wa jadi kuhusu utamaduni wa wenyeji, maadili na uwezo wao kuunganisha huduma za jadi na za kisasa ulikuwa muhimu kwa mradi. Ukweli mradi ulianza katika ngazi za mwanzo na ujuzi wa asili uliofanywa na wakunga wa jadi, na ukaboreshwa kwa kuwapa mafunzo mafupi na kuwapatia wakunga wa jadi na vilevile wafanyakazi wataalamu wa afya, teknolojia rahisi ya habari na mawasiliano, usafiri na zana za kazi za kutosha.
- Kusawazisha mifumo ya utaalamu wa jadi na kisasa kunaweza kuongeza athari. Kwa mfano, mradi wa Mradi wa Upanuzi wa Huduma za Afya Vijijini kwa ajili ya Msaada wa Dharura umewakutanisha pamoja wakunga wa jadi na wa kisasa na kuleta maelewano na imani kwa pande zote mbili kulioongeza huduma za afya ya mama.

- 1 Mkunga wa jadi ni mtu kutoka katika jamii asiyekuwa na mafunzo rasmi, lakini ambaye ana ujuzi wa tiba asilia aliopata kwa uanagenzi na hutoa huduma za kuzalisha akinamama, hutoa ushauri wa tiba kwa afya ya familia kwa kutumia mitishamba na/au dawa nyingine za asili na utabibu. (Toka: National Traditional Birth Attendants' curriculum for Uganda. MoH/Maternal and Child Health and Family Planning division. Kampala.)
- 2 Chanzo: UNDP (1988). Uganda Human Development report.
- 3 Wilaya ya Iganga ilikuwa na watu 706,476 ambao kati yao asilimia 52 walikuwa wanawake. Hii ilikuwa kabla Muyage haijatengana na Iganga mwaka 2000. Chanzo: Iganga District Planning department.

## Kufutilia Mbali Desturi Mbaya

Makala hii imeandikwa na Peter H. Wolff M.D., wa Chuo cha Udaktari cha Harvard, Boston MA 02115, Marekani. Kwa maelezo zaidi, baruapepe: [wolff\\_p@tch.harvard.edu](mailto:wolff_p@tch.harvard.edu)

***Tini za MA 41  
Februari 2002***

Ukeketaji wa wanawake hufanyika katika sehemu nyingi za Afrika na kwingineko. Hasa kwa kawaida hufanyika wakati wa utoto na una madhara makubwa sana ya kiafya, kimaumbile ya uzazi na uzazi kwa wasichana. Madhara huendelea kuwepo wakati wa kubeba mimba na kuendelea. Mara chache yamegundulika matatizo ya kisaikolojia, unyan-yasaji wa heshima ya kijamii na mitazamo binafsi ya wasichana na wanawake walioathirika na vitendo hivi vya jadi.

Ufyataji ambao kwa kawaida hufanyika wakati wa utoto ni aina mbaya zaidi ya ukeketaji wa wanawake yenye kuleta madhara makubwa. Pia una madhara makubwa kwa maumbile ya mwanamke na uzazi. Ufyataji umesambaa sana katika nyanda za chini za Eritrea, na hususan miongoni mwa wahamamaji. Wakati wa vita ya miaka thelathini kwa ajili ya uhuru wa Eritrea, idara ya utabibu ya majeshi ya ukombozi ambayo haikuwatibu wapiganaji pekee bali pia wananchi wa kawaida katika maeneo yaliyokombolewa, mara kwa mara iliwabidi kuwatibu wasichana na wanawake wenye hitilafu kubwa za sehemu za uzazi. Wengi wao walikuwa wamefanyiwa ukeketaji. Hivyo tatizo lilijadiliwa miongoni mwa wapiganaji kuwa hatua gani zichukuliwe ili kupungu-

za tatizo hili kubwa kwa wanawake ili kupunguza matatizo makubwa ya magonjwa kwa wanawake. Wakati huo iligundulika kuwa tabia hii haikubaliani kabisa na juhudi za kuboresha hadhi ya kijamii ya wanawake katika jamii.

Wataalamu wageni katika uwanja huu walipewa taarifa kuhusu tabia ya ukeketaji wanawake miongoni mwa wahamamaji wa Eritrea, na wengine huko ulaya waliosikia kuhusu tabia hizo walishtushwa na haraka wakasisitiza kuwa ufyataji upigwe marufuku, adhabu kubwa zitolewe kwa wale watakaoendelea na tabia hii yenye kuleta madhara makubwa. Wataalamu hawa walishindwa kuelewa hatari ya uhusiano baina ya majeshi ya ukombozi na wananchi wa kawaida, au kuwa sera ya jumla ya majeshi ya ukombozi kunganisha nchi ilitegemea ushirikiano na uhusiano wa pamoja miongoni mwa sekta zote za wananchi. Watu wengi toka nje walichukulia kuwa, kwa wakati uliopo, kuwa kimsingi wanaume ndio waliolazimisha ukeketaji huu wa wanawake. Kihistoria, tabia hizi mbaya sana bila shaka ziliendeshwa na wanaume kuwafanyia wanawake, lakini baada ya karne kadhaa wanawake wamesimilishwa umuhimu wa zoezi hilo kitamaduni, kwa imani kuwa wanawake ambao hawakukeketwa au kutahiriwa wali-

kuwa hatarini kuwa wazinzi au malaya. Ili kulinda heshima yao katika jamii, wanawake walisisitiza ukeketaji, na bado unaendelea kufanyika katika nchi nyingi.

Hivyo idara ya utabibu ya majeshi ya ukombozi ya Eritrea ilipitisha uamuzi wa kupiga marufuku ukeketaji katika nyanda za chini au kutoa adhabu yoyote kwa wale watakaendelea na vitendo hivyo. Walitambua kuwa kujaribu kuukomesha kwa kutumia mabavu kutawatenganisha wananchi na kufanya zoezi kuendelea kwa siri. Badala yake, mikutano ya hiari iliitishwa ambapo Wakunga wa Jadi ambao walikuwa raia wa kawaida waliofanya kazi ya ukeketaji walialikwa kushiriki katika warsha zilizoendeshwa kwa mwezi mzima na wauguzi na madaktari kwa hiari. Katika warsha hizi wakunga wa jadi walipewa maelezo ya kina kuhusu madhara makubwa ya papohapo ya kutokwa damu nyingi na maambukizi; na vilevile kuhusu madhara makubwa ya sehemu za uzazi, ongezeko kubwa la vifo vya watoto na akinamama, na mengineyo kama hayo. Pia walipatiwa kozi za mbinu za usafi wa kisasa, tiba za uzazi, n.k. Kama ilivyo kawaida warsha za Eritrea, usambazaji wa habari ulifuatiwa na majadiliano makali. Baadaye, wakunga wa jadi walirudi katika vijiji vyao.

Ingawa hakukuwa na uchunguzi wa ufuatiliaji rasmi, ripoti fupi zilieleza kuwa kulikuwa na upungufu mkubwa wa madhara mabaya ya ukeketaji wakunga walipotumia ujuzi wao. Hata hivyo, haikuweza kutegemewa kuwa

zoezi liliachwa kabisa wakati wa vita, au hata baada ya vita. Tangu uhuru, Umoja wa Kitaifa wa Wanawake wa Eritrea hufanya ziara za mara kwa mara kwa wahamamaji kuendeleza majadiliano haya kwa kuheshimiana na kushirikiana. Mtazamo wa jumla ni kuwa tabia hii inaendelea kutokomea polepole.

### Taathari

Ufumbuzi wa haraka kwa ajili ya kukomesha tabia ya ukeketaji wa wanawake (na pendekezo moja lililotolewa na mshauri asiye rasmi toka nje) unaweza kuonekana kuwa ni kupiga marufuku zoezi hili na kuwaadhibu wale watakaendelea na zoezi. Hata hivyo, kwa mtazamo wa uhusiano dhaifu baina ya majeshi ya uhuru na wananchi wa kawaida kwa hali yoyote isingekuwa sahihi kisiasa kuchukua hatua za kisheria kama hizo. Zaidi ya hayo, zoezi lingeendelea kichinichini. Badala yake, majeshi ya uhuru yalitegemea akili na nia safi ya wakunga wa jadi kurekebisha haraka tiba zao za uzazi, mara wanapopewa taarifa muhimu za kitabibu inayohusu jinsi ya kuzirekebisha, na kuwaelimisha wananchi kwa vitendo kuliko kwa amri. Njia hii pia imejenga msingi wa kuendeleza elimu kwa wanawake itolewayo na wanawake baada ya uhuru—hatua ya ziada kuhakikisha kuwepo kwa usawa kwa wanawake.

# Kuendeleza Maarifa Asilia katika Nchi Zinazozungumza Kifaransa barani Afrika

Ujumbe katikati ya 2001 ulikuwa na maandishi wa makala hii, Peter Easton (mshauri), Emanuel Nikiema (Mfanyakazi wa Benki ya Dunia, Ofisi ya Burkina Faso), na Suzanne Essama (Mfanyakazi wa Benki ya Dunia, Washington D.C.). Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana kwa baruapepe: [sessama@worldbank.org](mailto:sessama@worldbank.org)

## Tini za MA 42 Machi 2002

Maarifa asilia yanaendeleaje na kuhushwaje katika sera ya maendeleo na utekelezaji katika nchi zinazoongea Kifaransa za Afrika Magharibi na Kati? Matokeo ya ujumbe wa Benki ya Dunia mwanzoni wa kiangazi 2001 kwa mataifa haya manne—Senegali, Mali, Burkina Faso Faso na Cameroun—unatoa maelezo mafupi ya hali ilivyo kwa sasa. Maelezo haya yanatokana na kukutana na wenzao wa sekta ya umma na binafsi waliohusika katika pande mbalimbali za uhamasishaji wa maarifa asilia na mahojiano yaliyojitokeza, katika matukio mbalimbali kutokana na kukutana huku kwa awali. Hali katika kila nchi ilikuwa tofauti—kazi ya historia yake yenyewe na changamoto na fursa inazopata; bado kulikuwepo kufanana sana vilevile. Yote yamefafanuliwa kwa kifupi hapo chini.

### Wingi wa juhudi

Mengi yanaendelea kuhusiana na maarifa asilia katika nchi zote nne, kote katika sekta ya umma na isiyo ya kiserikali na mashirika ya kijamii. Shughuli zinaongezeka katika nyanja nyingi za maendeleo: afya, kilimo, elimu, usimamizi wa maliasili, masuala ya utamaduni. Mifano michache:

- Shirika lisilokuwa la kiserikali limejitolea “kuongeza misuli katika maari-

fa asilia” (*muscler le savoir local*) hu-pokea wanafunzi kutoka Afrika Magharibi kuhudhuria semina kuhusu uwezo wa maarifa asilia na kufanya utafiti wa awali—hasa katika kanda ya kilimo ya Ofisi ya Niger—kuhusu jinsi wakulima wenyeji walivyokubali njia za asili za urutubishaji wa mazao na uzalishaji wa mazao ya dharura kwa ajili ya biashara.

- Kituo katika maeneo ya vijijini nchini Senegali huwakusanya pamoja waganga wa kienyeji zaidi ya 400 kubadilishana mbinu na kujaribu ufanisi wa utumishi wao na upimaji magonjwa kisasa.

- Wizara ya Utamaduni na Sanaa nchini Burkina Faso hufadhili, kupitia “Kurugenzi yake ya Utamaduni na Urithi”, mfululizo wa majumba ya makumbusho kwa ajili ya kuhifadhi sanaa asilia na mpango wa mabaraza ya ujuzi wa wenyeji.

- Mtafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Asili nchini Cameroun amefanya utafiti chini ya ufadhili wa OAU, utafiti wa ethobotania wa matumizi ya jadi hifadhi kubwa mno ya mimea nchini.

Maarifa asilia kwa sasa yanaonekana kuwa mada nyeti. Kuna vyanzo vya ufadhili, binafsi na vya misaada toka nje, kwa ajili ya utafiti na juhudi katika eneo hili, na inazidi kuwa sahihi kisiasa kuidhinisha juhudi kama



hizi. Haya hufanyika kwa nchi nzima. Wizara ya Utamaduni nchini Mali siku za karibuni iliendesha mkutano wa kimataifa wa wawindaji wa jadi na “viongozi wa koo” (*chefs de la brousse*) kutoka nchi kadhaa za Afrika Magharibi kujadili njia za asili za kuhifadhi maliasili; na Shirika lisilokuwa la kiserikali la PROMETRA (*Promotion des médecines traditionnelles* au “Promotion of Traditional Medicine”) nchini Senegali limeungana na mashirika mengine kama hilo au kuunda matawi ya aina yake katika nchi nyingine kumi na mbili za Afrika. Ni wazi kwamba juhudi nyingine zozote zilizoanzishwa katika nchi hizi lazima zizingatie kwa makini kuwa kitu mambo gani yameshafanywa na kuhusu mafunzo yaliyopatikana kutokana na zoezi hilo hadi leo.

### Maendeleo yasiyo sawa

Umaarufu mkubwa wa maarifa asilia kama bango kwa ajili ya utekelezaji, na ufadhili, huvutia watu wengi wenye tamaa na wachangiaji kuwa hoja za kujaribu matokeo ya uwandani ni njia muhimu kwa ajili ya kutambua utendaji bora na kutenganisha ngano na pumba. Hata hivyo tathmini kama hiyo bado haijawa sheria.

Hata hivyo, kuna ongezeko la wingi wa mambo katika uwanja wa maarifa asilia katika nchi zote nne zilizotembelewa, lakini kunabakia kuwepo maendeleo yasiyolingana katika baadhi ya masuala.

- Mbali na uanzishaji wa Wizara za Utamaduni (kama huko Mali na Burkina Faso), ongezeko la shughuli linabakia katika mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta ya kujitolea. Ukuzaji wa maarifa asilia mara chache huwa sehemu ya sera au shughuli za mashirika ya umma. Nchini Senegali, kwa mfano, majaribio yote ya dawa ya asili yalifanyika chini ya ufadhili wa mashirika binafsi, na watetezi wao walipata mafanikio kidogo ya kuuridhisha mfumo mkuu wa utabibu katika juhudi kama hizo.

- Pia kuna tofauti kubwa kati ya kile kinachoweza kuitwa sekta “ngumu” na “rahisi” za maendeleo. sehemu kubwa ya juhudi za Maarifa Asilia zimekuwa zikifanyika katika uwanja wa huduma za jamii kama vile afya, utamaduni na elimu. Kuna baadhi, ingawa chache, katika kilimo. Nyingine hutoka katika uwanja wa maendeleo ya jamii kuelekea katika ukandarasi, fedha na sekta nyingine za maendeleo ya kiufundi, watu wachache wanaweza kupatikana wanaoewa jukumu la Maarifa Asilia au wako tayari kuyazingatia. Usimamizi wa maliasili huchangia labda upekee unaonekana.

- Matumizi ya lugha za Kiafrika kwa masuala mengi yanahusiana kwa karibu na juhudi za kurekodi, kuendeleza, na kuhusisha ujuzi wa wenyeji; lakini utekelezaji kwa hali hii hutegemea kukubalika kwa masuala mengine ya sera. Kawaida ni vigumu zaidi kupitisha sera zina-

zoambatana na uhamasishaji wa ujuzi wa lugha za Afrika katika nchi za pwani zenye mamia ya lugha za Kiafrika kuliko katika nchi zilizo ndani au za Sahara zenye idadi ndogo zaidi ya lugha na lugha chache za mawasiliano mapana. Cameroun, kwa mfano, lazima itumie lugha rasmi (Kifaransa—Kiingereza) na lugha mbalimbali za Kiafrika na hivyo bado inapambana na sera zake kuhusu matumizi ya lugha hizo katika mfumo wa elimu.

Kwanini rekodi hii ya maendeleo yasiyokuwa na usawa? Miundo ya maendeleo iliyotawala muda mrefu ni vigumu kuibadili, ni kweli, na jinsi uwanja unavyokuwa wa kiufundi zaidi ndiyo unavyofungwa zaidi katika kanuni za kimataifa za taratibu na ufanisi. Hivyo maarifa asilia kimsingi ni jambo ambalo balagha na utendaji hujaribu kuachana kiasi fulani: kila mara kuna mchezo wa kisiasa kuipitisha lakini gharama ya kweli ya kisiasa kufanya jambo kamili kuihusu.

Lakini kuna sababu nyingine zilizo hai kwa maendeleo yasiyolingana. ASIZE hutoa maabara nzuri kwa ajili ya kuchunguza njia za uvumbuzi kabla ya kujaribu kuingiza njia zenye mafanikio na sahihi zaidi kati yao katika sera za umma; hivyo inashangaza sana kuwa juhudi mpya zinaanzia pale. Katika muktadha wa tamaduni nyingi, maarifa asilia ya *nani* yapewe umashuhuri ni swali gumu, kama lilivyo suala la lugha *ipi* au *zipi* za Kiafrika zitafikia hadhi ya kuwa lugha rasmi. Kuna sababu nzuri za kuendeleza taratibu na maamuzi kama hayo.

Tokeo moja la maendeleo haya yasiyo sawa ni kukosa mshikamano na mawasiliano katika “sekta ya maarifa asilia.” Washiriki katika uwanja mmoja hawajui wanachofanya walio katika uwanja mwingine, kuna viwango vichache vinavyokubalika kwa kazi, na kuna ushindani mkubwa. Hii si mbaya hata kidogo, hata hivyo. Wengi wa juhudi angalau husaidia kupatikana kwa mawazo mapya na huunda njia mbalimbali ambazo uzoefu unaweza kusaidia kuzichuja.

### Kutambua aina mbalimbali za MA

Okeo moja la ongezeko la uzoefu wa kuendeleza maarifa asilia katika nchi nne zilizotembelewa ni ongezeko la ustaarabu wa kuelewa maana mbalimbali na matumizi ya maarifa asilia. Kikundi kilichofanyiwa mahojiano nchini Senegali kilitoa huenda tathmini iliyo wazi zaidi ya fafanuzi mbalimbali na zinazokamilishana za maarifa asilia ambao sasa umejumuishwa uwanjani. Walitofautisha njia tatu mbadala:

- *Maarifa Asilia kama urithi kutoka zamani* utakaohifadhiwa kwa makini na kuheshimiwa—njia inayoonyesha heshima kuu kwa busara zilizojaa za vizazi vilivyotangulia

hivyo vimeelezwa kwa msisitizo mkali katika maneno maarufu kutoka kwa Amadou Hampate Bâ, “kila mara anapofariki mzee ni kama vile maktaba imeungua na kuteketea.”

- *Maarifa Asilia kama uingizaji wa mtindo tofauti na hasa wa Kiafrika wa mawazo*—“epistemolojia” ya kiafrika ni njia ya kufikiria upya mbinu za maendeleo katika maeneo kama afya, kilimo, na usimamizi wa maliasili. Watetezi wa njia hii wanaeleza kushindwa kwa methodolojia za maendeleo kama ushahidi wa haja ya dhana mpya zilizotokana na urithi wa utamaduni wa watu zamani.

- *Maarifa Asilia kama njia na utaratibu kwa ajili ya kueleza yale wenyeji wanayoyajua, na kuwahusisha katika kubuni maarifa yanayotakiwa kwa ajili ya maendeleo*, na hivyo kuyapokeza katika vizazi vijavyo yale mazuri ambayo kizazi kilichopo kinaweza kutoa. Watetezi wa njia hii wanasisitiza kuwa maarifa asilia ni suala la kuwawezesha watendaji wenyeji kuzalisha maarifa *mapya*—yanayotegemea urithi toka siku za nyuma na tathmini kwa macho makavu changamoto za sasa—kama moja ya njia rahisi ya kuorodhesha na kuhifadhi tamaduni zilizorithiwa toka zamani.

*Muungano* wa haya mambo matatu unaelekea kuwa na uwezekano mkubwa sana wa kuchochea heshima kubwa ya maarifa asilia. Lakini mifano ni michache, ingawa watu wanaotumia huzidi kuonyesha matumaini tofauti. Washiriki wetu katika mazungumzo wameongelea kuhusu “kurejelea” au kuwa na “kutafuta msaada” katika maarifa asilia katika kujenga mitindo mipya kwa maendeleo, kuliko kuibana. Wengi walihamasika, zaidi ya hayo, katika manufaa ya njia ya tatu, ambayo hufanya maarifa asilia kuwa utaratibu hai, kuliko kuwa suala la diwani na makumbusho, na kuyafunga katika ajenda ya ushiriki na ugawaji majukumu kwa watu.

### Kujenga kiungo kinachokosekana

Mabadiliko yanaelekea wapi katika nchi hizi nne? Zipi ni changamoto kuu zinazowakabili watetezi? “Kiungo” kikubwa kabisa kinachokosekana katika maeneo yote yaliyotembelewa ni kutokuwa na uwezo au fursa ya “kuingiza” matokeo ya juhudi za maarifa asilia katika sera na taratibu zinazoongoza maendeleo ya wenyeji, kusogea toka katika mikutano ya kufurahisha kufikia kutia moyo utafiti wa mabadiliko halisi katika sera na viwango vya utendaji.

Hali inaonekana katika nchi zote zilizotembelewa na katika mashirika ya misaada kama vile Benki ya Dunia. Masuala ya maarifa asilia kama yangetambuliwa mara kwa mara wakati huu kuliko siku za nyuma, yanaelekea yangeweza kutenganishwa katika huduma mahsusi au

wakala ambao wana malengo haya lakini wana athari ndogo kwa sera katika sekta za “kazi” za maendeleo. Katika ngazi ya taifa, inaweza kuwepo wizara au wakala anayejishughulisha na utamaduni, hata hivyo akifanya kazi katika hewa bila kuwa na athari katika masuala ya utendaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika mashirika ya misaada, programu kwa ajili ya uhamasishaji wa maarifa asilia zinaweza kushamiri lakini hukingamana kidogo na ofisi kuu zinazopanga sera za misaada na utekelezaji. Kukatisha hapa inabakia changamoto kuu. Vipimo vinne vya shughuli vinaelekea kuwa muhimu hasa:

- Kuhamasisha ushirikishaji wa maarifa asilia katika miradi ya maendeleo kupitia *taratibu zilizo wazi zaidi kwa kuwahusisha watendaji wenyeji katika kubuni mbinu za uingiliaji kati* na mbinu za kutoa maamuzi. Katika masuala mengi, hii humaanisha kusimamia ushiriki na viwango vya hatua za utafiti kuwa taratibu za uendeshaji katika mashirika ya maendeleo.

- Kuendeleza, kuandaa na kusambaza rasmi *zana* na *mbinu* kwa njia hii ya ushiriki wa wenyeji katika maendeleo.

- Kufanya *shule za ndani ya nchi kuwa kitovu cha kukusanyia maarifa asilia* na mahali pa kukutana baina ya wakala wa maendeleo na watendaji wenyeji katika kujadiliana vitega uchumi na juhudi zinazoyahusu.

- Undaji, majaribio na utumiaji wa *zana na njia kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi wa maendeleo kabla ya kuajiriwa na walio katika ajira* ambayo huwachochea kutumia kwa mapana maarifa asilia na kuwasaidia kugundua njia za kuunganisha mapya na ya zamani.

Ni dhahiri kuwa mikakati lazima iandaliwe nchi hadi nchi, ingawa huambatana na njia nyingi za mabadilishano ndani ya taifa. Hatua ya kwanza ya maendeleo inaweza kuwa uchambuzi wa “tathmini ya sekta” au *état des lieux* unaofanywa na watafiti wa taifa ili kuorodhesha na kulinganisha juhudi mbalimbali zinazofanyika katika nchi husika na yale yanayojulikana katika matokeo yake. Hii itasaidia kama utangulizi na vigezo vya kutoa kipaumbele juhudi za siku zijazo. Wizara za serikali na mashirika wahisani lazima yawe sehemu ya uchunguzi huu makini, ambao utahitaji vilevile “ukaguzi wa hesabu” wa sera zao kwa kutegemea ushiriki wa wenyeji katika kupanga maendeleo na matumizi ya maarifa asilia.

Katika nchi zote nne, maarifa asilia ni uwanja wenye ongezeko la shughuli na uwezekano mkubwa. Kwa wakati mmoja ni uwanja ambao msaada toka kwa jamii ya wahisani unaweza kusaidia sana kuimarisha juhudi zilizopo na “kupembua” juhudi zinazoleta matumaini zaidi kutoka katika nyingi zinazofanyika, lakini ambapo maamuzi ya sera za nchi wenyeji lazima mwishoni yaongoze kanuni.

# Maonyesho ya Mbegu Kusini mwa Tanzania

Makala hii imeandikwa na O.K.K. Mponda (Mzalishaji Mbegu na Mtafiti Mwandamizi, Maonyesho ya Mbegu Kanda ya Kusini, ARI Naliendele, Mtwara) na E.M. Kafiriti (Mchumi wa Kilimo, Oilseeds Research Programme, ARI Naliendele, Mtwara), Chuo cha Utafiti wa Kilimo Naliendele, P.O. Box 509 Mtwara, Tanzania, Faksi Na. 255 23 334023; baruapepe NARI@RAHA.COM

**Tini za MA 43**  
**Aprili 2002**

## Kwa nini maonyesho ya mbegu vijijini kanda ya kusini?

Uzalishaji mdogo wa mazao ya kilimo ni miongoni mwa sababu zinazopelekea kuwa na mapato kidogo na upungufu wa chakula kwa wakazi wa vijijini katika Kanda ya Kusini mwa Tanzania. Matumizi ya mbegu bora ni njia mojawapo ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Ilionekana kuwa usambazaji wa mbegu kutoka katika mikoa inayozalisha mbegu katika Kanda ya Kusini ulikuwa hauendi kwa mtiririko mzuri kwa kiasi fulani kutokana na miundombinu iliyopo katika kanda. Katika Muundo wa kawaida wa Uhamishaji wa Teknolojia, utaratibu wa usambazaji wa mbegu huanza kwa utafiti ambapo kazi ya uzalishaji hufanyika na kuishia kwa wakulima ambao hupata bidhaa ya mwisho ya mbegu bora/aina tofauti. Vyanzo mbalimbali vya Mifano ya Uvumbuzi hutambua mchango wa mfumo usio rasmi wa uzalishaji mbegu. Hivyo, inadaiwa na wataalamu wa maendeleo kuwa wataalamu rasmi na wasio rasmi wa maendeleo ya mbegu/aina mbalimbali wanaweza kukamilishana na kuboresha usambazaji wa mbegu bora kwa wakulima vizuri kuliko juhudi za kila mtaalamu peke yake.

Maonyesho ya mbegu katika maeneo ya vijijini kwenye Kanda ya Kusini yana malengo yafuatayo:

### **Malengo ya muda mfupi**

- Kujenga utambuzi wa na upatikanaji wa mbegu za ziada mbadala na vifaa vya kilimo kutoka katika vyuo vya utafiti, kampuni za mbegu na wakulima;
- Kuwawezesha watafiti, wakala wa vitengo na wakulima kukutana na kubadilishana mawazo kuhusu mikakati yao, ujuzi wanaotumia katika kuendeleza mbegu na aina zake na kuuza na kubadilishana mbegu; na
- Kujenga mawasiliano ya kikazi kati ya wakulima wataalamu wa mbegu, wakala wa vitengo, wazalishaji/watafiti na wazalishaji mbegu wa taifa. Mawasiliano haya ya kikazi yanaweza kusaidia kuboresha yaliyopo katika vitengo na kuanzisha mbegu mpya/mpango wa kuendeleza aina mbalimbali za mbegu ikiwa ni pamoja na juhudi za ziada vijiji na ushirikiano kati ya watafiti na wakulima kwa ajili ya maendeleo ya teknolojia.

### **Malengo ya muda wa kati**

- Kujenga utambuzi na upatikanaji wa mbegu mbadala na mbalimbali za mazao yaliyozalishwa katika Vyuo vya Utafiti vya Taifa, kampuni za

mbegu na mifumo ya uzalishaji mbegu unaofanywa na wakulima katika kanda ya kusini.

- Kuhamasisha wakulima kuzalisha mbegu zao wenyewe na mfumo wa kubadilishana kiasi kwamba juhudi rasmi, kwa kujazia njia rasmi za biashara, pia kuzidi kuendelea kuwezesha mifumo asilia; na
- Kuunga mkono maelewano baina ya uendelezaji wa mbegu rasmi/uzalishaji mbegu na wakulima katika mbegu zao ya ziada/uendelezaji wa aina za mbegu.

### **Malengo wa muda mrefu**

- Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, upatikanaji wa chakula na mapato kwa wanavijiji katika kanda ya kusini.

### **Maandalizi na utekelezaji wa maonyesho ya mbegu**

Kwa kipindi cha miaka ya 1997–1999, maonyesho ya mbegu yaliandaliwa na kuendeshwa na Chuo cha Utafiti wa Kilimo, Naliendele na Halmashauri za Wilaya msaada wa fedha ukitoka FINIDA katika Misaada ya Mchanganyiko wa Miradi Vijijini (Rural Integrated Project Support [RIPS]). Hata hivyo, tangu mwaka 2000, Halmashauri za Wilaya zimekuwa zikigharamia maonyesho ya mbegu vijijini.

Kabla ya kila onyesho la mbegu, uchunguzi wa kitaalamu wa mbegu za mkulima hufanyika na mahali pa kufanyia maonyesho ya mbegu huchaguliwa na kila wilaya. Wataalamu wa mbegu za wakulima ni wale wakulima ambao katika jumuiya yao wanachukuliwa kuwa wataalamu katika baadhi ya mazao kwa kutumia uzoefu na ambao husambaza mbegu kwa wengine. Wakulima hawa hualikwa kufanya maonyesho wakati wa maonyesho ya mbegu. Wakulima ambao hawakutambuliwa kama wataalamu pia huruhusiwa kuhudhuria na kushiriki bure. Wanaweza kuleta mbegu, maarifa asilia na kuwaonyesha wengine. Uwanja wa maonyesho ya mbegu huchaguliwa na wilaya kwa kuzingatia ubora wa eneo kwa uzalishaji wa kilimo, upatikanaji wa malazi, kufikika kwa urahisi na kuwe katikati ya vijiji vingine ili wakulima kutoka vijiji vya karibu waweze kuhudhuria maonyesho.

Chuo cha Utafiti wa Kilimo Naliendele kilikuwa kiki-saidiwa fedha na RIPS kununua mbegu bora kutoka sehemu mbalimbali nchini—hususan kutoka vyuo vya utafiti, kampuni za mbegu, maduka ya Chama cha Wakulima Tanzania na baadhi ya mbegu ambazo ni vigumu kuzipata kutoka kwa wakulima. Sampuli ndogo za gramu 5-200 za aina zote za mbegu za mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na nafaka, jamii ya kunde, mbegu za mafuta, mazao ya mboga na matunda na mbegu za miti hukusanywa na kufungashwa katika pakiti ndogondogo. Pakiti hizi za

mbegu huuzwa au kubadilishwa kwa wakulima ambao hupeleka kuzijaribu katika mashamba yao.

Kueneza utambuzi kuhusu maonyesho ya mbegu, matangazo ya redio hutolewa wiki 2-4 kabla ya tukio na hufanyika matangazo ya moja kwa moja siku ya sherehe.

Wakulima katika vijiji vilivyochaguliwa huandaa vibanda kwa ajili ya maonyesho ya mbegu. Pia huandaa ngoma za asili kwa ajili ya siku ya ufunguzi wa maonyesho ya mbegu kuwaburudisha washiriki na kuyafanya maonyesho ya mbegu kuwa hai. Ili kuratibu maonyesho ya mbegu katika ngazi ya wilaya, kamati mbalimbali huundwa, k.m. kamati ya ujenzi, kamati ya chakula, kamati ya utamaduni, na kamati ya ulinzi na usalama.

Halmashauri za Wilaya hutoa maafisa wa vitengo pamoja na fedha kwa ajili ya kuhudhuria na kushiriki katika maonyesho ya mbegu. Pia hutoa wataalamu wa mbegu pamoja na chakula na usafiri kwenda na kutoka katika uwanja wa maonyesho.

Maonyesho ya mbegu huendelea kwa siku mbili katika kila kijiji kilichochaguliwa. Wakuu wa Wilaya hualikwa kufungua maonyesho ya mbegu. Maonyesho huanza jioni kwa ngoma za asili. Na kuanzia saa moja jioni hadi saa nne usiku, wakulima huonyeshwa picha za video kuhusu teknolojia mbalimbali za kilimo. Maonyesho halisi ya mbegu huendelea kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 11.00 jioni baada ya hapo maonyesho ya mbegu huhamia katika kijiji kingine kilichochaguliwa katika wilaya nyingine. Katika siku ya maonyesho ya mbegu, mbali na maonyesho ya mbegu, maonyesho hufanyika kuhusu upandikizaji, uzalishaji wa zana za kilimo, n.k. Watafiti hurekodi maarifa ya wataalamu wa mbegu kwa kuandika, kupiga picha na mikanda ya video. Ushiriki wa wanasiasa, watafiti, vitengo, wakulima, na wauzaji binafsi wa mbegu hujenga mawasiliano kikaza na hivyo kuboresha uhusiano miongoni mwa wadau.

### **Uendeleu wa maonyesho ya mbegu**

Maonyesho ya mbegu ya Kanda ya Kusini yalianza mwaka 1997 katika vijiji vitatu vya Marambo huko Nachingwea, Mbonde huko Masasi na Kitangari katika Wilaya ya Newala. Mwaka 1998, maonyesho ya mbegu yalipanuliwa na kuhusisha Halmashauri za Wilaya tisa za Kanda ya Kusini na mwaka 1999 yalifanyika katika Halmashauri za Wilaya kumi. Ili kuendeleza maonyesho ya mbegu vijijini katika kanda, kuanzia mwaka 2000 Halmashauri za Wilaya zilishauriwa, kama ilivyoelezwa awali, kuchukua nafasi ya uongozi katika maandalizi ya maonyesho bila msaada toka RIPS, na Chuo cha Utafiti wa Kilimo Naliendele kichukue nafasi ya uratibu.

## Mafanikio ya maonyesho ya mbegu

- Ongezeko la utambuzi wa mbegu bora na upatikanaji wa mbegu kwa wakulima. Wakulima kwa sasa wanahitaji mbegu za ubora unaofaa.
- Maonyesho ya mbegu yameonyesha kuwa wakulima wana mbegu bora walizozalisha wenyewe, ujuzi na maarifa ambayo yanaweza kuandikwa, kusambazwa na kuuzwa.
- Maonyesho ya mbegu yamekuwa zana muhimu ya uhamishaji wa teknolojia kutoka katika utafiti kwenda kwa wakulima.
- Zaidi ya aina sabini za mazao kuanzia nafaka, mimea jamii ya kunde, mboga na mbegu zinazotoa mafuta zilizoalishwa katika mfumo rasmi zimeweza kuwafikia wakulima.
- Maonyesho ya mbegu yamesaidia kuongeza ufahamu miongoni mwa watafiti na vitengo kuhusu mbegu za kienyeji na yamewasaidia kupata maarifa ya wenyeji kuhusiana na mazao.
- Maonyesho yameonyesha jinsi mazao yanavyoweza kulindwa kutokana na uharibifu wa kijenetiki; hivyo, inawezekana kuokoa aina fulani za mbegu ambazo zingeweza kupotea katika eneo/kijiji kimoja kwa kuzipata toka kwa wakulima wengine.
- Maonyesho ya mbegu yameongeza majadiliano kuhusu masuala ya mbegu katika kanda na kusaidia juhudi za kanda kuongeza uzalishaji wa mbegu.
- Chuo cha Utafiti wa Kilimo Naliendele kwa sasa kinawaunganisha watu binafsi, vikundi vya wakulima watafiti, vyo vya ndani ya nchi kuzalisha mbegu za aina zinazopendekezwa kama vile mbegu zinazotoa mafuta.

- Ukulima wa maharage umeanzishwa katika Kata ya Chilangala likiwa kama zao mbadala la biashara/chakula.

## Tofauti kati ya maonyesho ya kilimo na maonyesho ya mbegu

Kumekuwepo maswali kuwa kwa nini maonyesho ya mbegu vijijini yasichanganywe na Maonyesho ya Taifa ya Kilimo Nanenane (tukio la kitaifa katika kila wilaya na ngazi ya Taifa) ili kupunguza gharama. Sababu zimefupishwa hapo chini.

Kuelewa tofauti hizi ni muhimu sana kwa sababu sehemu kubwa ya wakulima nchini Tanzania ni wakulima wa mazao ya chakula, wakulima wa kiwango kidogo ambao wanaweza wasifae kwa maonyesho ya kilimo. Wakulima wa mazao ya chakula hulima mazao mbalimbali kwa ajili ya kupata uhakika wa chakula. Maonyesho ya kilimo yanaelekea kuandaliwa kwa ajili ya wakulima walioendelea na wanaolima kwa ajili ya biashara. Inaelekea kuwa hata wakulima maskini kabisa wanaweza kufaa kushiriki katika maonyesho ya mbegu. Maonyesho ya mbegu vijijini yanatia moyo ushiriki wa wakulima wasiokuwa na rasilmali ya kutosha katika hifadhi ya rasilmali ya jenetiki ya mazao ambayo huchangia uhakika wao wa chakula na njia za maisha vijijini. Hii, hata hivyo, huwawezesha maskini wa vijijini na hujenga kujiamini katika maarifa yao na rasilmali asilia ya jenetiki ya mimea.

## Maonyesho ya kilimo

- Wafanyakazi wa vitengo hushawishi kwa kile kinachonyeshwa.
- Hudharau maarifa asilia na utamaduni wa kimapokeo.
- Huonyesha mafanikio kutokana na utafiti rasmi tu.
- Ulinganifu ni suala linalozingatwa
- Husisitiza ongezeko la uzalishaji.
- Huwashauri wakulima kutumia njia bora zaidi.
- Huonyesha mazao na wanyama.
- Hushauri kulima mazao ya aina moja.
- Kilimo cha biashara husababisha kuharibika kwa jenetiki ya mbegu.
- Baadhi ya mazao madogo hudharauliwa.
- Hufanyika baada ya mavuno ya mazao mwezi Agosti.
- Lengo kuu ni kuonyesha mafanikio rasmi ya kisayansi

## Maonyesho ya Mbegu Vijijini

- Wakulima huamua nini cha kuonyesha.
- Huhamasisha maarifa asilia na utamaduni wa kimapokeo.
- Huonyesha mafanikio kutokana na utafiti na mfumo wa mbegu unaomilikiwa na wakulima.
- Wingi wa aina za mazao ni tatizo kuu.
- Husisitiza uhakika wa chakula.
- Hufuatilia upatikanaji wa mbegu za aina mbalimbali.
- Msisitizo umewekwa katika mazao ya chakula.
- Huwapa moyo wakulima kulima mazao mengi.
- Hulinda mazao kutokana na uharibifu wa kijenetiki.
- Mazao madogo ambayo yanaweza kuwa na sifa za dawa hushauriwa kuwa yaonyeshwe.
- Huhamasisha rutuba ya udongo kwa kulima mazao mengi yenye mahitaji tofauti ya virutubisho, baadhi yao husaidia kuongeza rutuba ya udongo.
- Hufanyika mwanzoni mwa mvua za msimu.
- Lengo ni kuboresha usambazaji wa mbegu zilizoalishwa kutokana na utafiti na mbegu zilizoalishwa na wakulima vijijini.

# Mchango wa Mbogamboga kwa Uhakika wa Chakula cha Kaya

Makala hii imeandikwa na E.B. Rubaihayo, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kawanda, P.O. Box 7065, Kampala, na ilichapishwa kwa mara ya kwanza katika Jarida la Sayansi ya Mazao la Afrika, Kumbukumbu za Mkutano wa Mazao barani Afrika, Kitabu. 3, uk. 1337-1340. Toleo hili limehaririwa kidogo na kuondolewa ufupisho wa Kiingereza na Kifaransa.

**Tini za MA 44  
Mei 2002**

Juhudi nyingi zimefanywa na Serikali ya Uganda kuzalisha chakula cha kutosha watu wa Uganda na ziada kwa ajili ya kusafirisha nje. Hata hivyo, mboga asilia, mara nyingi hujulikana kama mboga za kienyeji, zimekuwa zikidharauliwa kwa kupendelea mboga za kigeni zilizoletwa nchini (Rubaihayo, 1995). Hivyo, nafasi ya mboga za kienyeji bado haijazingatiwa.

Mboga za kienyeji huharibika haraka, hutoa mazao kidogo na thamani yake kama mazao ya biashara bado haijachunguzwa. Hata hivyo, sehemu kubwa ya wakulima wenyeji hawawezi wakati wote kuzalisha mboga za kisasa kwa sababu ya kutopatikana kwa mbegu na/au gharama kubwa za uzalishaji wa mboga hizi. Bahati mbaya, watu maskini kifedha waishio mijini na vijijini kila mara hupata shida ya kununua mboga za kisasa katika masoko ya wenyeji kwa sababu ya gharama kuwa kubwa. Hivyo, hutegemea mboga za kienyeji kama mboga za kawaida au supu inayotumika pamoja na chakula kikuu kama vile mahindi, mihogo, viazi vitamu, ndizi, serena, mtama na viazi vikuu (Rubaihayo, 1994). Vyakula vikuu hutoa kalori zinazohitajika kwa ajili ya nguvu ya mwili lakini vina upungufu mkubwa wa virutubisho vingine wakati mboga za kienyeji zina virutubisho vingi. Zina vitamini

A, B na C, protini na madini kama vile chuma, kalisi, fosforasi, aidini na florini kwa viwango tofauti lakini vinavyotosha kwa ajili ya ukuaji na afya ya kutosha. Kwa mfano, vitamini A mbayo huhitajika kuzuia upofu hasa kwa watoto hupatikana katika mboga zote za kienyeji za kijani kilichokoza kama vile *Amaranthus* (dodo), *Solanum aethopicum* (nakati), *Manihotesculenta* (majani ya mihogo) na *Ipomea batatas*

(majani ya viazi vitamu). Kwa upande mwingine mboga za majani kama vile *Solanum indicum* subsp. *Ditichum* (Katunkuma) zinaaminika kudhibiti shinikizo la damu. Hivyo, mboga za kienyeji, zina virutubisho vya protini na kalori muhimu hasa kwa watoto, wagonjwa, wazee, kinamama wajawazito na wanaonyonyesha (FAO, 1988). Bahati mbaya, wateja bado hawajahamasishwa kutambua nafasi ya mboga za kienyeji kukidhi mahitaji yaliyotajwa hapo juu.

Sehemu kubwa ya mboga za kienyeji huzalishwa katika nchi zote zinazoendelea hasa katika bustani za nyumbani. Kwa sababu ya umuhimu wa bustani hizi, Warsha ya Kimataifa kuhusu Miradi ya Bustani za Kaya ilifanyika Bangkok, Thailand mwezi Mei 1991 kuunganisha mafunzo waliyojifunza kutokana na uzoefu wa miradi ya bustani za kaya. Warsha

ilichambua uhusiano na ufanisi wa uzalishaji wa chakula cha kaya kama uingiliaji kati maendeleo, uliolenga watu wote wasiokuwa na uwezo wa lishe na kiuchumi na kupanga mikakati ya utekelezaji inayofaa ya bustani za kaya (Midmore et al., 1991).

Lengo la makala haya ni kuwadokeza wapanga sera na wasimamizi wa maendeleo wakague upya na kuweka uzito zaidi katika uzalishaji na matumizi ya mboga za kienyeji uliosahauliwa ili kuongeza lishe, uzalishaji wa mapato na uhakika wa chakula kwa kaya zenye uwezo mdogo. Mawazo yaliyotolewa katika makala haya ni matokeo ya usaili wa watu kadhaa kutoka nchi nyingi ikiwa ni pamoja na Uganda, Ethiopia, Kenya, Tanzania, Zimbabwe, Zambia, Rwanda, Cameroun, Nigeria, Ghana, Côte d'Ivoire, Gaboni, Senegali, n.k. ingawa Uganda imeangaliwa kwa undani zaidi.

*Bustani ndogo.* Bustani ndogo ni maarufu zaidi mijini na pembezoni mwa miji. Kwa kawaida huwa vipande vidogo vya shamba ambavyo hupandwa mboga za asili na huwa sehemu ya bustani ya nyumbani. Mboga huzalishwa kwa urahisi katika bustani hizi kwa kutumia mbolea ya samadi badala ya mbolea za viwandani (Midmore et al., 1991).

Mboga za kienyeji ambazo kwa kawaida hupandwa ni pamoja na *interalia* yenye majani, jamii ya *Amaranthus*, *Basellalba*, *Solanumaethiopicum*, *Solanum gilo*, *Solanum indicum sub sp distchum*, jamii ya *Capsicum*, *Colocasia-esculenta*, *Phaseolus vulgaris*, *Gynendropsis gynandra*, *Vigna unguiculata*, *Bidens pilosa*, *Manihot esculenta*, *Corchorus oltoris*, *Solanum nigrum*, *Abelmoschum esculenta*, *Cucurbita maxima*, na *Acalipha biparlita*. Mboga za kigeni kama vile *Brassica oleracea*, *B. Oleracea* na *Daucus carota* pia hulimwa sana. Mavuno ya baadhi ya mboga mbichi nchini Uganda yameonyeshwa katika chati 1.

*Bustani kubwa.* Bustani kubwa hupatikana vijijini. Bustani hizi huwa na eneo kubwa kuliko bustani ndogo na mboga nyingi huchanganywa na mazao mengine ikiwa pamoja na matunda, mboga za majani, mimea inayotoa dawa, mazao ya chakula na miti ya vivuli. Bustani kubwa katika vijiji vinavyozunguka miji hupandwa kabichi, koliflawwa, karoti, *Amaranthus lividus* (zinazoota katika sehemu yalipotua maji au ardhi yenye unyevunyevu), *Solanum gilo*, *Solanum indicum subsp. dischum* mara nyingi kama zao moja. Mboga hizi za majani huuzwa katika miji jirani na masoko yao ya vijijini.

### Mchango wa mboga asilia kwa uhakika wa chakula cha kaya

Bustani kubwa za mboga za kienyeji katika vijiji zina sifa ya kuwa na mfumo wa kuchanganya mazao na kuota

mimea wakati wa msimu wa mvua. Katika nchi nyingi zinazoendelea, ambapo bustani hizi ni nyingi, mchango wa kilimo cha bustani za mboga za asili kama mkakati wa uzalishaji wa chakula umekuwa hautiliwi maanani na watunga sera na wafanyakazi wa vitengo kutokana na kuzingatia mboga za kigeni ambazo huzalishwa kwa malengo ya kibiashara (Rubaihayo, 1994). Bahati mbaya, kaya maskini vijijini hazinufaiki na ongezeko kubwa la uzalishaji kibiashara wa mboga za kigeni kutokana na gharama kubwa za pembejeo za kilimo zinazohitajika kwa ajili ya ufanisi katika uzalishaji wake. Hivyo, ni muhimu sana kubuni mikakati ya utafiti na uzalishaji ambayo moja kwa moja huwawezesha watu maskini zaidi kuzalisha si mboga za kienyeji pekee bali pia mazao ya chakula.

Ingawa mchango wa bustani hizi kwa ustawi wa familia ni wa ziada, mchango wa wastani kama hii ni muhimu sana kwa wale wenye mapato madogo sana vijijini na mijini. Watu hawa maskini mara nyingi huweza kupata ardhi ndogo yenye rutuba kidogo sana na wengi wana vipande vidogo sana vya ardhi. Ukulima wa bustani ndogo na kubwa kwa wingi unaweza kuigeuza ardhi hii kuwa chanzo cha uzalishaji wa chakula na uhakika wa kiuchumi kwa kutumia maelekezo ya taratibu za kilimo na mboga za asili ambazo zimezoolewa na wenyeji.

*Umuhimu wa mboga za asili.* Sehemu kubwa ya watu wa Uganda hawatumii kiasi cha kutosha cha mboga za majani kukidhi mahitaji yao ya kila siku ya vitamini, madini na protini. Hata kile kinacholiwa kina sehemu kubwa ya virutubisho hivi kilichoharibiwa wakati wa mapishi. Kuna mapungufu katika ufanisi katika kuhakikisha uhakika wa chakula kwa mwaka mzima kutokana na ukweli kwamba mboga asilia chache sana hulimwa, na nyingi zaidi hukusanywa kutoka msituni au mashambani na kwenye mashamba makubwa. Katika baadhi ya mifumo ya kiekolojia huonekana kama nyasi na mara nyingi hufyekwa na hazipatikani katika msimu wa ukame (Rubaihayo, 1994). Lakini hali hii inaweza kubadilishwa kwa juhudi za pamoja za serikali kuelimisha watu na upanuzi wa huduma kushughulikia mboga za asili na kuongeza utafiti ili kuzalisha mbegu bora, utayarishaji, utafutaji masoko na mbinu za kuhifadhi. Hili lingelela ongezeko la matumizi ya mboga za asili na mchango wao katika uhakika wa chakula utaongezeka.

Bustani za familia ni maarufu zaidi katika kaya zenye hali ya maisha ya wastani, na huwa ndiyo chanzo kikuu cha chakula baina ya mavuno na wakati mavuno yanapokosekana. Hutoa chanzo muhimu cha nishati na protini, hasa kwa watoto walioacha kunyonya maziwa ya mama, wagonjwa na wazee. Baadhi ya mboga za majani za asili huweza kuendelea kuzaa hata wakati wa ukame ingawa kwa kiwango kidogo kutokana na kudumaa.

Uharibifu wa makazi na uhamiaji katika maeneo ya mijini humaanisha kuwa vyakula vya msituni havipatikani tena kwa hawa wakulima maskini. Zaidi ya hayo, kugeuzwa kwa kilimo kuwa cha biashara kumeondoa mazao mengi asilia yaliyokuwa yakitumika kuhakikisha kuwepo mlo kamili kijijini (Rubaihayo, 1992).

Ni muhimu kukubali kuwa mboga za asili, hasa zile za majani kama *Amaranthus*, (dodo, Bugga) *Solanum aethiopicum* (Nakati), n.k. huweza kupatikana katika dharura au matatizo yanayotokea kutokana na ugomvi wa wenyewe kwa wenyewe na majanga ya asili yanayosababisha kuhamishwa kwa jamii. Mboga hizi za asili huanza kumea mara baada ya mvua za kwanza kunyesha na huweza kuvunwa baada ya wiki tatu hadi nne baada ya kuota. Mboga hizi za majani huweza kufuatiwa na mazao kama maharage ambayo huchukua miezi miwili hadi mitatu ili kuleta nafuu ya chakula, ili chakula kitakachonunuliwa kiwe cha muda au cha ziada (Rubaihayo 1995b).

*Wanawake na mboga za asili.* Nchini Uganda, ingawa wanawake wa vijijini wanawajibika kulisha kaya zao, hata hivyo hupata nafasi ndogo ya kuwa na rasilmali. Kilimo cha kaya huwapatia wanawake njia muhimu ya kupata mapato bila kuvunja miiko ya kitamaduni na kijamii katika shughuli zao. Bustani kubwa na ndogo huweza kuongeza uwezo wa wanawake kifedha na uzalishaji wa chakula ambao una athari za moja kwa moja kwa lishe, afya na uhakika wa chakula kwa kaya.

Pale mboga za asili zinapofanywa kuwa za kibiashara kama vile, Malakwang (*Hibiscus* spp.) Nakati (*Solanum aethiopicum*), Egobe (*Vigna unguiculata*), Entula (*Solanum gilo*), Katunkuma (*Solanum indicum* subsp. *Disticum*), Doodo (*Amaranthus dubius*), Bbugga (*Amaranthus lividus*) hasa katika jiji la Kampala na katika maeneo mengine ya miji, wanaume ndio wanaolima mboga hizi. Wachuuzi hununua mboga hizi kutoka kwa wakulima (wanaume) na kuzisafirisha kwenda sokoni, sokoni wanawake huzinunua na kuziua rejareja kwa umma. Mauzo ya mboga za asili katika masoko yenye wanawake hayatoi tu uhakika wa chakula kwa wale wenye uwezo wa kununua lakini wanawake wauzaji huweza kusomesha watoto wao, kuvalisha na kununua vitu muhimu kwa kaya zao hivyo kuepuka umaskini kabisa.

*Bustani kubwa na ndogo na mazingira.* Ingawa hakujawa na utafiti wa kina wa athari za kilimo cha

mboga za asili kwa mazingira, inaaminiwa kwa ujumla kuwa kilimo cha bustani hufuata mifumo bora ya kiuchumi ya usimamizi wa ardhi. Uzalishaji wa chakula cha kaya hutumia mbolea ambazo hazina madhara katika mazingira. Mtindo wa kawaida wa bustani za kaya pia ni muhimu katika kuhifadhi rasilmali ya mimea mbalimbali (Midmore et al., 1991).

### Hitimisho

Mboga za asili ni chakula cha kawaida cha kaya na hutoa mchango mkubwa katika kuleta uhakika wa chakula kwa watu vijijini katika nchi nyingi za Afrika, ingawa kwa nadra mchango huo hutambuliwa. Hivyo, elimu kuhusu umuhimu wake kama chakula chenye lishe ya kutosha na kama njia ya mapato ya moja kwa moja na mzunguko hasa kwa familia maskini, lazima itolewe kwa upana na serikali za Afrika.

### Marejeo

- FAO (Food and Agriculture Organization), 1988.  
 "Traditional Food Plants." FAO Food and Nutrition Paper 42. FAO, Rome.
- Goode, P.M. 1989. "Edible plants of Uganda. The value of wild and cultivated plants as food." FAO Food and Nutrition Paper 41/1. FAO, Rome.
- Midmore, D.J., Vera Nines & Venkataraman, R. 1991.  
 "Household gardening projects in Asia: past experience and future directions." *Technical Bulletin No. 19.* Asian Vegetable Research and Development Center.
- Rubaihayo, E.B. 1992. "The Diversity and potential use of Local Vegetables in Uganda." Pages 109-114. In: *The First National Plant Genetic Resources Workshop: Conservation and Utilization.*
- Rubaihayo, E.B. 1994. "Indigenous Vegetables of Uganda." African Crop Science Conference Proceedings 1, 120-124.
- Rubaihayo, E.B. 1996b. "Conservation and use of traditional vegetables in Uganda." In: *Proceedings on Genetic Resources of Traditional Vegetables in Africa: Option for Conservation and Use, 29-31 August 1995,* ICRAF Kenya (in press).



## Utumiaji Maarifa Asilia Kuinua Tija ya Kilimo

Tini hii iliandikwa na Siddhartha Prakash wa Benki ya Dunia, na inatokana na ziara ya ugani kwenye chuo cha wakulima na maeneo ya mradi mwaka 2001. Kwa maelezo zaidi tumia baruapepe: [Sprakash@worldbank.org](mailto:Sprakash@worldbank.org)

### **Tini za MA 45 Juni 2002**

Maarifa huhamishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kutoka nchi moja hadi nyingine kwa njia ya mahusiano ya kibiashara na maingiliano ya kijamii baina ya jamii mbalimbali. Hii imesababisha kuwepo na idadi kadhaa za mabadilishano katika eneo kubwa na shughuli za kushirikishana maarifa ndani ya Afrika na hata nje ya bara. Wakulima na waganga wa jadi kutoka Msumbiji wamebadilishana maarifa ya utendaji bora na wenzao kutoka nchini Uganda. Miradi kadhaa ya kikanda kama vile Mradi wa Usimamiji Mazingira katika Ziwa Viktoria imezikutanisha jumuia jirani za wavuvi kutoka Kenya, Tanzania na Uganda.

Shughuli hizi huimarisha dhana ya kuwepo kila mahali Maarifa Asilia (MA), ambayo yamejikita katika desturi za jadi za jamii katika maeneo mbalimbali. Licha ya tofauti za kijio-grafia, namna jamii nchini India, kwa mfano zinavyotumia vizuri rasilimali zao za kijamii na kima-zingira, inaweza kuwa funzo kwa jamii kama hizo katika Afrika.

Mradi wa Urutubishaji Ardhi ya Sodi (The Sodic Lands Reclamation Project) nchini India ni mfano mzuri wa jinsi utumiaji wa maarifa ya jadi katika shughuli zinazosaidiwa na Benki unavyoweza kugeuza ardhi tasa kuwa ardhi inayolimika yenye

rutuba. Katika jimbo la Uttar Pradesh, India ya Kaskazini, mavuno ya kilimo yalipungua, wakati ambapo idadi ya watu iliendelea kupanda katika kipindi chote cha miaka ya 1980. Desturi za umwagiliaji maji zisizo sahihi zilisababisha chumvi kuingia katika udongo, wakati huo-huo wadudu waharibifu (nzige wa kihakawia) waliharibu asilimia 40-60 ya mazao ya mpunga na ngano. Sehemu kubwa ya ardhi hii ilikuwa inamilikiwa na wakulima maskini.

Ili kuongeza tija ya kilimo, mawakala ugani wa serikali walijitahidi kueneza matumizi ya teknolojia na taratibu mpya za kilimo. Lakini wakulima, ambao hata hivyo, hawakuwa na imani na mawakala wa serikali, hawakutekeleza taratibu hizi. Hata hivyo, kutokana na mbinu mbovu za ushirikishaji, uenezaji wa teknolojia haukuwafikia wakulima.

Mwaka 1993 Serikali ya Uttar Pradesh ilizindua Mradi wa Urutubishaji kwa msaada wa Benki ya Dunia wa Ardhi ya Sodi unaoendeshwa na wakulima. Shabaha ilikuwa ni kuimarisha taasisi za kienyeji, kuwawezesha wanufaika kwa kuanzisha mfano wa ufikishaji huduma kwa jamii.

Changamoto ya kwanza ilikuwa ni kuondoa chumvi nyingi kutoka mashambani. Udongo huu una ukolezo wa juu wa sodi ambamo ndani yake chembechembe laini za udongo zime-

tapakaa. Matokeo yake ni kwamba maji na hewa haviwezi kupenyeza, na kusababisha kuwepo kwa kiwango cha juu cha alikali. Udongo huu unaojulikana kama udongo wa sodi hutoa sumu kwa mimea, huathiri vibaya kilimo, afya ya binadamu na mimea.

### Utumiaji wa maarifa ya jadi

Wakulima waliunda kamati za mahali husika za utekelezaji na vikundi vya kujisaidia. Kwa kutumia maarifa yao wenyewe na uzoefu, wakulima walirejesha rutuba kwenye hekta zaidi 68,000 zilizomilikiwa na familia 247,000. Walisambaza jasi, wakajenga boma, wakachujua udongo, wakaanza kupanda mazao mengi, kutia mbolea mbichi na upandaji mazao kwa zamu wakatimia mboleavunde na kutifua ardhi. Uendelezaji wa kufunika ardhi kwa kupanda sana mazao kuliweza kuhami udongo usirejelewe na chumvi kwenye tabaka la juu.

Kuanzia mchakato wa upangaji hadi utekelezaji, mameneja wa mradi, AZISE na wakulima walifanya kazi kwa pamoja ili kuendeleza mikakati yao wenyewe. Mikakati hii mara kwa mara ilibuniwa, kubadilishwa na kurekebisha ili ioane na hali mahsusi au ya mahali husika. Kwa mfano, baadhi ya desturi za kisasa kama vile matumizi ya mbolea za kemikali zimeonekana kuwa wa madhara zaidi kuliko manufaa. Katika muktadha huu, wakulima waliendeleza teknolojia asilia zinazotokana na maarifa na desturi za jadi zilizothibitika kuwa za gharama nafuu na zenye kujali mazingira.

Wakati mwingine, wakulima walijifunza shughuli za kilimo bora kutoka majimbo mengine. Huko Maharashtra, mkulima mwenyeji mmoja alikuwa amebuni mbinu mpya ya kutengeneza mboleavunde. Mboleavunde ya "Nadep" hutegemea muundo wa mboleavunde unaozumia matofari badala ya shimo na ulitumiwa katika zaidi ya vijiji 100 katika eneo la mradi.

Viwango vya juu vya virutubisho vya udongo vilivyopatikana katika aina hii ya mboleavunde vilipunguza kwa takribani robo mahitaji ya mbolea na viuawadudu, na pia kupunguza gharama za pembejeo za kilimo. Utumiaji wa mbolea ya kemikali pungufu uliongeza ubora, muonjo na uzani wa nafaka za chakula. Ladha na rangi ya nafaka zenye kunukia kama ngano na mchele wa bismati navyo viliongezwa na kuwawezesha wakulima kupandisha bei.

Awali wakulima walitumia viuawadudu mbalimbali kama vile vumbi ya "Melathia". Hivi sasa wanatumia mbinu asilia za udhibiti wa wadudu waharibifu, kama vile kupanda Daincha (zao la mbolea mbichi) katika mipaka ya mashamba ya mpunga. Katika baadhi ya vijiji kama

Jively, Devari na Dhanepur, wakulima hutumia nduni za "mwarobaini" kuhami mazao yasishambuliwe na wadudu waharibifu.

Mwaka 1997, kulikuwa na shambulio kubwa la nzige wa kikahawia na zaidi ya asilimia 40 ya zao la mpunga liliharibiwa kote katika *Uttar Pradesh*. Wakulima wa sehemu hiyo walijua kwamba mafuta ya taa hufukuza nyoka na yanaweza hata kuua baadhi ya aina za nyoka. Mmoja kati ya wakulima wenye maarifa zaidi katika eneo hilo aliwaza kwamba iwapo mafuta ya taa yanaweza kuua nyoka, ni wazi yanaweza pia kuua nzige wa kikahawia.

Ili kufanya majaribio ya wazo hili, alinyunyizia mafuta ya taa katika meta moja ya mraba ya shamba lake pale shambulio lilikofanyika. Katika muda wa dakika chache, wadudu waharibifu wote walikuwa wameangamizwa. Kutokana na matokeo haya, mafuta ya taa yalinyunyiziwa kwenye kona za shamba na vilevile kwenye mashamba jirani. Mwanzoni, lita 10 za mafuta ya taa zilitumika kwenye eneo la robo hekta. Kadiri muda ulivyopita, mkulima alirekebisha teknolojia hii kwa kutumia lita tano za mafuta ya taa yaliyochanganywa na makapi ya mpunga kwa ajili ya kunyunyizia robo hekta ya ardhi iliyorejeshewa rutuba.

### Taathari za kiuchumi

Njia hizi mbalimbali zilijaribiwa na wakulima 600 katika wilaya tofautitofauti. Matokeo yalikuwa ni kupungua kwa kiasi kikubwa kwa madhara yaliyoababishwa na nzige wa kikahawia kutoka asilimia 49 hadi asilimia 2. Habari hii ya mafanikio ilienea haraka kiasi kwamba wakulima katika jimbo lote walianza kudhibiti mashambulio ya nzige wa kikahawia kwa kutumia viziduo vya mwarobaini, maganda ya mpunga na mbolea mbichi. Aidha, baadhi ya desturi nyingine asilia ambazo zilikuwa zikitumiwa na vizazi vya nyuma vya wakulima zilianza kuonekana za kisasa. Miongoni mwa hizi ni desturi za jadi za ufugaji, tiba ya magonjwa ya kawaida kama minyoo, ugonjwa wa nyayo na maumivu yanayowapata zaidi ng'ombe na nyati.

Kadiri muda ulivyopita, maarifa na hekima ya wakulima vilianza kuzaa matunda. Ushadidi wa kupanda uliongezeka kutoka asilimia 37 hadi asilimia 200. Mavuno ya ngano na mpunga kwenye ardhi iliyorutubishwa tena yalizidi mara mbili ya makadirio. Katika baadhi ya maeneo thamani za ardhi ziliongezeka mara nne baada ya ardhi kurejeshewa rutuba. Viwango vya ujira viliongezeka mara mbili ikiwa ni matokeo ya kukua kwa shughuli za kiuchumi. Vikundi vya kujisaidia vya wanawake

vilijiongezea mapato kwa kujiingiza pia katika ufugaji wa jamii ya ndege na kilimo cha bustani.

Kumekuwepo pia hali ya kupungua kwa uhamaji wa msimu wa watu wanaotafuta kazi kutoka vijiji vyenye mradi. Mmoja wa wanufaika katika kijiji cha Shobapur alisema “kwa sababu mashamba yangu ya *usar* (sodi) yalikuwa tasa, nilikuwa na kawaida ya kwenda Bhopal, Bombay na Calcutta kutafuta kazi. Hivi sasa yakiwa yamerejeshewa rutuba yake, muda huo nitaupata wapi?”

### Shule ya Wakulima huko Pratapgarh, Uttar Pradesh

Uenelevu wa mradi wowote wa urutubishaji ardhi kwa vyovyote vile hutegemea sana usimamiaji mzuri wa ardhi hiyo. Upatikanaji wa mara kwa mara wa taarifa kuhusu mbinu mpya za kilimo na teknolojia ni baadhi ya viambato muhimu vinavyohitajika ili kuendeleza mifumo ya upandaji mazao mengi kwenye maeneo kama hayo. Kwa kuzingatia hili na ukweli kwamba msaada wa Benki hautakuwepo muda wote, kikundi cha wataalamu muhimu na wakulima waliopata mafunzo walijumuika pamoja kwa lengo la kubuni mikakati mipya kwa kutumia rasilimali na maarifa asilia kuhusu desturi za kilimo.

Jambo hili lilisababisha kuanzishwa kwa Shule ya Wakulima huko Pratapgarh. Desturi hizi zilirasimishwa na kuenezwa kupitia chuo. Mwanzoni kulikuwa na wakufunzi wakuu 12 katika shule. Kila mmoja ilibidi aonyeshe kwa vitendo katika shamba lake mwenyewe namna njia fulani za kilimo zilivyothibitisha kuwa za manufaa, kabla wengine hawajaanza kuiga mbinu hizo. Mafunzo yaliendeshwa kwa kutumia lahaja ya wenyeji kama vile Avdi.

Mada zilizoshughulikiwa ni pamoja na mitandao bora ya utiririshaji, utiaji mbolea mbichi, utengenezaji mboleavunde, matumizi ya samadi, menejimenti ya mkopo, vikundi vya kujisaidia na upandaji wa mazao mengi. Kila moja ya mada hizo ilitumia uzoefu asilia wa miaka mingi katika kushughulikia changamoto kama vile mashambulio ya nzige wa kihakawia. Mara baada ya matokeo kuonyesha mafanikio, yalienezwa na wakufunzi kutoka kijiji kimoja hadi kingine.

Mafunzo mara nyingi ni ya vitendo na huhusu ubadilishanaji uzoefu mkulima kwa mkulima. Kwa mfano, kikundi cha wakulima hupelekwa kwenye eneo la ardhi lililorejeshewa rutuba mapema zaidi ili kujionea tofauti katika rutuba za udongo na kiwango cha maendeleo. Aidha wakulima kutoka eneo moja la mradi walifanya ziara za mafunzo na kutembelea sehemu nyingine za nchi (Haryana, Andhra Pradesh na Gujarat) ili kubadilishana na kujifunza njia bora za kilimo za

wakulima wengine. Ziara kama hizo zimepanua msingi wa maarifa yao kwa njia ya kujionea aina tofauti za mifumo ya maarifa ya jadi. Leo hii, jimbo la Uttar Pradesh limeanza kutoa mafunzo na huduma za ugani kwa vyuo vya wakulima, vinavyowahudumia wakulima zaidi ya 7,200 katika vijiji 65 nje ya eneo la mradi.

### Kijiji cha Dhanepur

Mwaka 1996, katikati ya ardhi iliyokuwa tasa huko Narangpur, ile iliyorejeshewa rutuba, mkulima wa mradi alipanda mti wa *bale*. Ardhi ya sodi ilikuwa na weupe wa majivu na imetelekezwa kabisa. Hapakuwepo na dalili ya uoto wowote.

Taratibu, mti ulianza kustawi na wakulima wa vijiji vya jirani walianza kulima ardhi hiyo. Muda si mrefu mbogamboga zikaanza kupandwa. Makazi yakaanza kuibuka yakiuzunguka mti wa *Sarof*. Siku hizi kijiji chote kimesambaa katika eneo liljulikanalo kama *Dhanepur*.

Kijiji kina pampu ya maji inayomilikiwa na jumua, mashine ya kukamua miwa, mashine ya kusaga na kukoboa mpunga, na mashine ya kutengeneza chakula cha wanyama. Vyote hivi viko karibukaribu, ili viendeshwe kwa pamoja na umeme au injini ya dizeli. Mtambo umefanyiwa marekebesho kwa kutumia ubunifu wa wenyeji ili uweze kufanya kazi katika mazingira ya mahali hapo.

Awali, wakulima waliweza kuvuna zao moja tu kwenye mashamba yao. Leo hii, wanapanda mazao manne kwa kutumia mbinu za upandaji mazao mengi walizofunzwa na chuo, wakipanda dengi, mtama na choroko. Mazao haya yanalimwa pamoja katika mashamba yanayopata maji kwa kutumia umwagiliaji matone. Matokeo ni mavuno mengi zaidi mara nne/tano kutoka mashamba yaleyale.

Mapato yameongezeka mara tano kutokana na kuongezeka kwa mavuno. Kipindi cha nyuma, wakulima waliweza kuweka akiba ya dola za Marekani 110 kwa mwaka. Siku hizi akiba zao kwa mwaka zimepanda hadi dola za Marekani 555.

Akiba hizi zimewekezwa kwa uangalifu katika ujenzi wa nyumba, umeme na barabara zinazounganisha kijiji na masoko na maeneo mengine. Awali palikuwa na matatizo makubwa ya usafiri na mawasiliano.

Mapato ya juu yameboresha kwa haraka hali ya maisha kijijini. Watu walio wengi walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Hivi sasa kuna programu za elimu kwa watoto.

Kumekuwepo pia na mabadiliko muhimu katika mtizamo wa watu. Awali, wakulima walikuwa wamegawanyika kuhusu mradi. Kundi moja lilikuwa tayari

kushirikiana na mawakala wa utekelezaji wakati kundi jingine linalojumuisha wakulima wenye kumiliki mashamba makubwa lilipinga mradi. Lakini wakulima hawa walipoona ardhi za wale walioshiriki kikamilifu katika mradi zinageuka kuwa kijani, wakati ardhi zao zimeendelea kuwa tasa na kuwa na rangi ya majivu, walianza kujisogeza karibu. Hivi sasa, wana shauku kubwa ya kushiriki katika awamu ya pili ya mradi.

#### **Vikundi vya kujisaidia vyawezesha wanawake**

Mafunzo yanayotolewa na vyuo vya wakulima kwa wanawake yamekuwa na matokeo muhimu kwenye ngazi ya kaya, kwa kusukuma mbele mabadiliko ya kijamii na kiuchumi kwa lengo la kuboresha ustawi wa familia nzima. Hivi leo zaidi ya vikundi vya kujisaidia vya wanawake 175 vimeanzishwa kama vile Kikundi cha Kujisaidia cha Kaveri Mahela.

Kikundi cha Kaveri kilichoundwa mwaka 1995, mwanzoni kilikuwa na wanachama 15. Kila mwanachama aliweka akiba ya senti 10 kwa mwezi, ambayo iliongezeka kutoka senti 40 hadi 80 katika kipindi cha miezi sita iliyofuata. Hivi leo, kila mwanachama huweka akiba inayofikia dola za Marekani 6 kwa mwezi. Fedha hizo zimewekwa akiba katika benki ya hapo kijijini chini ya mfuko wa pamoja ujulikanao kwa jina la Mfuko wa Kujisaidia wa Kaveri.

Baada ya kuweka akiba ya kiasi cha kutosha, wanawake walianzisha mpango wa ndani wa kukopeshana

baina yao. Aidha walichukua mikopo binafsi yenye thamani ya kati ya dola za Marekani 100 na 200 kutoka benki iliyopo katika sehemu yao kwa ajili ya kuwekeza katika teknolojia ya kisasa kama vile mashine ya kukamua miwa.

Vikundi hivi vya kujisaidia vimekuwa pia mawakala wazuri wa mabadiliko ya kijamii huko vijijini na vimeshughulikia masuala mbalimbali nyeti kama vile mfumo wa mahari. Hivi sasa, idadi kubwa ya wanawake katika wilaya wanaweza kusoma, kuandika na kuelewa vipengele changamani vya miamala yao ya biashara.

Waziri wa Kilimo wa Jimbo alitembelea shule na kupendekeza kwamba mbinu kama hizo za ubunifu za kilimo zinapaswa kuigwa katika jimbo zima. Umoja wa Ulaya unafadhili mradi wa urejeshaji rutuba kwa kutumia mpango kama huo katika wilaya nyingine tatu. Mradi huu utatumia kama nyenzo mafunzo ya msingi yaliyopatikana katika awamu ya kwanza ya mradi; kutumia kama msingi maarifa asilia huongeza uzalishaji endelevu wa kilimo na huwa kama mfano wa namna ya ufikishaji wa huduma kwa jamii.

Mawasiliano ya jamii kwa jamii yanaweza kuwa kipitishio cha kuhawilisha maarifa kama hayo hadi nchi na mabara mengine. Ikizingatiwa kwamba kilimo ndiyo shughuli kuu katika chumi za nchi nyingi za Afrika na nchini India, uenezaji na matumizi sahihi ya maarifa asilia vyaweza kuwa vya manufaa sana.

# Dhima ya Visasili na Kaida katika Kusimamia Maliasili Kwenye Mwambao wa Msumbiji

Makala hii iliandikwa na Fernando Dava, Zuber Ahmed, na Peter Easton. Fernando Dava ni Mkurugenzi wa ARPAC—Arquivo do Patrimonia Cultural, Msumbiji; Zuber Ahmed ni Mshauri wa Kujitegemea huko Maputo, Msumbiji; na Peter Easton ni Profesa Mshiriki, Mitaala ya Uzamili katika Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu cha Jimbo la Florida.

**Tini za MA 46  
Julai 2002**

Msumbiji ni nchi tajiri kwa maliasili na ambayo pia kwa kiasi kikubwa inatishiwa na kuisha na kupungua thamani kwa urithi huu. Miaka ya vita, shinikizo la kiuchumi, kushuka kwa bei ya mazao, uhamiaji mijini na mabadiliko ya hali ya hewa vimeanza kuwa na athari kubwa kwenye msingi wa rasilimali ya nchi. Ingawa asilimia 10 ya nchi iko chini ya hifadhi ya misitu, sehemu kubwa ya nchi imepoteza uoto wake wa asilimaha kandokando na mipaka na nchi za Zimbabwe na Afrika Kusini. Maeneo mengi ya pwani yameathiriwa vibaya na uchafuzi wa mazingira unaotokana na mtiririsho unaosababishwa na shughuli za kilimo na kutoka viwandani. Shinikizo la idadi kubwa ya watu limesababisha kutoweka kwa karibu wanyama pori, wengi ambao wakati fulani waliishi katika sehemu kubwa ya nchi.

Umalizikaji wa maliasilia ni suala la kitaifa, lakini linahusu pia hata maeneo ya wenyeji. Kama ilivyo katika nchi nyingi zinazoendelea, idadi kubwa ya jamii nchini Msumbiji hutegemea matumizi ya busara ya mazingira yao ya asili ili waendeleo kuishi. Kuya-tunza ili yaendeleo kuwepo kizazi hadi kizazi ndiyo changamoto muhimu. Sehemu iliyoathirika zaidi kuliko mahali pengine ni eneo kubwa la mwambao lenye urefu wa karibu kilometa 3,000 kutoka kwenye mpaka na Tanzania

upande wa Kaskazini hadi kwenye mpaka na Afrika Kusini. Jamii zilizoko kwenye kizuizi hiki asilia hutegemea sana uvunaji wa rasilimali za bahari: samaki, kome na aina nyingine za viumbe wa baharini vyote hivi ni vyanzo vya protini na pia vyanzo vya mapato. Umuhimu wa zawadi hii kwa ustawi wa jamii umesababisha kuibu-ka kwa changamani za kaida, visasili na matambiko. Vyote hivi husaidia kutunza umuhimu wa pekee wa mazingira na “kusimamia” utumiaji wake kwa manufaa ya watu wote.

Je, mbinu hizi “asililia” hufanya kazi vipi na iwapo—kama kweli—zinaweza kutumika kudhibiti changamoto mpya kwenye chanzo cha maliasili: shinikizo la idadi ya watu na uchafuzi wa mazingira? Nchini Msumbiji taasisi za kienyeji zimeanza kuelewa suala hili, na uzoefu wake ni wa kuelimisha.

## Wakulima wa kome wa Zimilene

*Zimilene* ni kijiji kidogo kilichopo kwenye mdomo wa mto Limpopo katika Jimbo la Gaza, kusini mwa Msumbiji, kilometa mia kadhaa kaskazini mwa Maputo. Kwa wenyeji kinajulikana kwa majina mengine kama Kamhula, *Inhampurca*, au *Zongoene*. Katika eneo hili la Bahari ya Hindi, miundo asilia ya miamba imekuwa chanzo cha kustawi kwa uchumi wa eneo na

mlengo kwa ajili ya uelewa mahsusi wa mizimu kuhusu uhusiano wa watu na mazingira yao.

Miamba iko karibu na sehemu ya juu katika eneo la maji lenye *fitoplanktoni* nyingi, hali inayotoa mazingira murua kwa ajili ya ukuaji wa makoloni ya kome. Kwa muda wa miaka mingi, vijiji vimekuwa vikivuna rasilimali hii kila mwaka, wakiitumia kama chanzo cha protini na mapato. Kwa mujibu wa imani yao miamba hiyo imekuwepo hapo kwa sababu ya utashi wa kimungu na imekuwepo hapo kwa muda mrefu kadiri kumbukumbu ya pamoja ya binadamu inavyoweza kukumbuka.

Jamii ina imani kuwa wahenga wao walikuwa wamiliki na wasimamizi wa miamba hii tangu walipolowea katika eneo hili. Familia anzilishi zilizoweka maskani kwenye sehemu hii ya mwambao—Bunzula, Palate, Machava, Nhancuma na Nhabanga—ziligawana rasilimali na kuchukua wajibu ya kusimamia miamba ya kome, zikiongozwa na mizimu walezi wa koo zao. Kila familia iliweka walinzi wa kuhami maeneo ya kome. Hata hivyo, wawakilishi wa familia hizi, hufanya kazi chini ya uangalizi wa mamlaka ya juu zaidi, Chifu Zimila, dhuria wa mtu wa kwanza aliyeishi eneo hili, ambaye mzimu wa ukoo wake unafikiriwa kuwa na nguvu zaidi kuliko ule unasaba wa familia. Mfumo unatoa uhakika wa chanzo cha kutatua migogoro na kugawa haki za kutumia ambazo zinakubaliwa hadi huko chini kwa mwanajamii binafsi.

### Uvunaji wa kome

Kwa kawaida huko Msumbiji kome huvunwa katika kipindi cha majira ya baridi, kati ya mwezi Machi na Agosti. Kwenye miezi ya awali ya mwaka dalili za kwanza za kome hutokea katika maji ya kina kifupi, na makoloni huanza kustawi. Mara baada ya dalili hizi kuonekana, walinzi wa kila eneo la kome huwarifu wakuu wa familia kuhusu tukio hili, wakiwaomba ruhusa ya kuanza kusafisha mwani na magugu mengine yanayosaidia ukuaji wa kome na kurahisisha uvunaji. Uondoaji huu wa magugu kwenye maeneo ya kome huhitaji uangalifu, kwa kuwa ni rahisi kuharibu kome wachanga. Fimbo nyembamba na panga hutumika kwa madhumuni hayo. Mara “shamba” likisha kuwa safi, kome hukua kwa wingi sana.

Katika hali ya kawaida, wanavijiji hawaruhusiwi kuanza kuvuna mpaka hapo kome watakapokuwa wamepevuka. Hata hivyo, kibali maalumu hutolewa inapotokea dharura au mahitaji dhahiri kama vile njaa au ujio wa ugeni usiotarajwa. Mavuno haya ya awali yanaratibiwa na kuwekewa mipaka na familia husika pamoja na machifu wakuu. Aidha, jukumu la machifu ni kuhakikisha kunakuwepo na mgawanyo sawa wa rasilimali kati ya vijiji. Na hili linathibitishwa na msemo wa wenyeji—“kome huliwa miongoni mwa jamii.”

Kome wanapofikia kipindi cha kuvunwa, walinzi hupiga filimbi ili kumwarifu kila mmoja katika jamii, hata wale wasiotoka katika kijiji hicho, kuwa mwindo unaweza kuanza. Kwa desturi wageni wanaruhusiwa kuvuna kome pamoja na wenyeji kama ishara ya ukarimu. Kila mtu hukusanya kadiri ya mahitaji ya familia yake na mamia kwa mamia ya watu huja kuvuna kome. Kazi yenyewe ni ngumu na inaweza kuwa ya hatari. Kwa sababu hiyo, ukusanyaji haufanyiki bila mpango na mahali popote kwa wakati mmoja. Badala yake kazi huanzia kwenye mwisho mmoja wa mwamba na taratibu huendelea hadi mwisho mwingine. Utaratibu huu huwezesha familia na machifu katika jamii kudhibiti matukio na kutoa huduma mara moja kwa yeyote anayejeruhiwa. Wana pia jukumu la kuhakikisha kuwa kila mmoja anapata mgao wa haki.

### “Mizimu” na utawala wa sheria

Mamlaka ya machifu ya kuratibu uvunaji wa kome yamefungamana na imani madhubuti kuwa mizimu ya wazee wa kale hulinda miamba ya kome. Walinzi waliowekwa na kila familia huondoka miambani wakati wa machweo na walinzi mizimu wa kila ukoo huaminika kuchukua jukumu la ulinzi hadi mawio. Huo ulinzi wa mizimu huadhimishwa katika kaida na visasili.

Chifu wa ukoo wa Bunzula anaeleza, “Tunazungumza na mizimu kupitia makuhani wetu wa jadi (*curandeiros*) au yenyewe hutuita. Mizimu hutufundisha namna ya kuhifadhi miamba. Na tunafanya ibada za matambiko kwa lengo la kuifurahisha ili iendelee kulinda miamba na kome.”

Ibada za matambiko hufanyika kwenye ngazi mbili; ndani ya kila ukoo au familia na kwenye ngazi ya jamii nzima. Chifu wa kila familia huchukua jukumu la kufanya ibada kwa ajili ya sehemu ya miamba ya kome ambayo iko chini ya ulinzi wa ukoo. Ibada inayohusu jamii nzima huendeshwa na Chifu Zimila mwenyewe na hujumuisha familia zote katika eneo. Kabla ya kuandaa ibada kubwa, mkuu wa machifu hushauriana na machifu wote wa familia husika katika mkutano wa baraza la wazee. Machifu wa familia wana wajibu wa kutoa huduma kwa ajili ya shughuli hiyo.

Wanajamii wote hutarajiwa kushiriki katika tukio hilo kubwa na pia kuchangia bidhaa kwa ajili ya kuhudumia ibada na shughuli nzima. Michango hukabidhiwa kwa machifu wa familia ambao nao huikabidhi kwa Chifu Zimila. Ibada moja hufanyika kabla ya msimu wa kuvuna kuanza ili kuomba mavuno mazuri ya kome, na nyingine hufanyika baada ya mavuno kwa ajili ya kutoa shukrani kwa zawadi waliyopokea.

Inaaminika kuwa mizimu ina jukumu muhimu la kutoa adhabu kwa wale wanaokiuka taratibu. Kama chifu mmoja wa familia anavyoeleza: “Wakati wa kutwa nzima kila

familia ina mlinzi anayedhibiti njia ya kufikia miamba. Usiku mizimu ya kila familia hulinda miamba hadi mapambazuko. Kila mmoja anajua kwamba hakuna wa kupuuzia jambo hili. Wanaovunja taratibu wana hatari ya kutupwa baharini [na mizimu] au kutoweza kuondoka eneo hilo la ukusanyaji kwa kukosa kabisa njia ya kurudi nyumbani. Njia ya kuelekea makwao hukumbwa na giza nene.”

Inaaminika pia kuwa kome walioibwa ni mlo usiofaa kuliwa. Chifu anasema, “Kome wanaweza kupikwa kutwa nzima na wasiive. Hakuna mtu anayejua sheria hizi halafu akataka kukabiliwa na adhabu za mizimu.”

### Changamoto ya mifumo ya utambukizaji uzazi

Mfumo mahalia wa visasili, imani na kaida huko Zimilene ilisaidia kuhifadhi makazi ya kome kwa vizazi na vizazi, lakini chini ya shinikizo la mabadiliko yanayoendelea nchini Msumbiji kome wamekuwa siyo rasilimali ya wenyeji tu. Katika miaka ya karibuni wakazi wa miji ya jirani kama Zai-Zai wamekuwa wakifikia kwa urahisi miamba ya kome ya Zimilene, na wakati huohuo shinikizo za umaskini na msongamano wa watu vimewalazimisha kuvuna kome kwa njia ambazo hazifuati taratibu za usimamiaji wa jadi na kuendelea kuwepo kwa rasilimali.

Familia za *Zimilene* zilitoa ombi kwa mamlaka za utawala ili wasaidie kutatua tatizo na kuokoa kome. Baada ya ushauriano, iliamuliwa kuunda Kamati ya Usimamiaji wa Miamba ya Kome, iliyoundwa na viongozi wa jadi na mwakilishi mmoja au zaidi kutoka mamlaka za utawala. Chifu wa eneo husimamia uteuzi wa wajumbe kutoka koo za familia wanaowajibika kwa kila eneo la makazi ya kome. Kwa upande wa utawala mkuu wa kituo cha utawala cha *Chilaulene*, eneo linalojumuisha *Zimilene* ama hushiriki mwenyewe katika Kamati au huteua mtu wa kumwakilisha.

Kazi za kamati ni pamoja kutoa uhalali wa matambiko, ibada na kanuni za *Zimilene* na kushughulikia wanaokiuka taratibu, hasa wakazi wa mijini na watu wengine wanaoendelea kuja kwenye makazi ya kome. Kimsingi “wavunja taratibu” ni watu wanaotoka nje ya eneo kwa sababu, wakati ambapo imani thabiti huwazuia wenyeji kufanya ujangili kwenye makazi ya kome, wakazi wa mijini kwa asili hawana mfumo wa imani kama hizo. Kwa hiyo, kamati ina mamlaka ya kupendekeza adhabu mbalimbali za kiutawala au hata za kifungo kwa wale wanaovunja sheria za utumiaji wa miamba ya kome.

Hivyo, katika shughuli za awali za kamati, mfumo wa usimamiaji unaokubalika kijadi na kiimani ulikuwa ukitumika pamoja na ule ambao ni wa “kisasa” na

kiutawala. Ule wa kwanza ulitumika kwa wenyeji, na wa pili kwa wanaotoka nje ya eneo husika.

Hata hivyo, suluhisho hili la “kutenga watu katika mafungu mawili” pia lilikuwa na upungufu wake. Kwa upande mmoja, watu kutoka nje ya kijiji inawezekana kuwa rahisi zaidi kwao kukwepa adhabu za kiutawala kuliko wenyeji wanavyoweza kukwepa gadhabu za mizimu. Kwa upande mwingine, ongezeko la shinikizo kutoka nje kwenye msingi wa rasilimali laelekea kusababisha vyombo vya utawala na mfumo wa adhabu kuchukua nafasi muhimu wakati dhima ya jadi na mizimu ikipungukiwa umuhimu hadi kubakia tu katika masimulizi ya jadi.

Kwa hiyo, changamoto inayokabili kamati ni namna ya— kuchanganya mifumo yote miwili—namna ya “kutambukisha” mfumo wa kanuni zinazokubalika sehemu kubwa pamoja na nafasi ya usimamiaji wa jadi pamoja wenye sifa ya kuheshimu rasilimali asilia na mfumo wa ndani wa utimizaji.

Mielekeo miwili iko wazi, lakini hakuna uhakika kama ama yote miwili au hata mwingine kimsingi utakubaliwa. Suluhisho mojawapo linahusu upanuaaji wa dhima ya walenzi wa familia kwenye ngazi ya mahitaji ya vifaa na mambo ya kiroho kwa kuwasaidia kufanya uangalizi wa karibu wa miamba ya kome kwa muda wa saa ishirini na nne kama mfano halisi wa shughuli takatifu za wahenga za kuhifadhi msingi wa rasilimali ya taifa zima. Mwelekeo mwingine, pengine kama nyongeza lakini wa muda mrefu unahusu kutumia baadhi ya viongozi wa dini za jadi (curanderios) kufundisha shuleni uwajibikaji wa kiikolojia na kuendesha kampeni ya maadili mapya ya kuheshimu mazingira.

Taratibu za jadi huonyesha kwamba jamii za vijijini zina namna zao za kuuzelea ulimwengu na kulinda rasilimali zao. Mifano kama hiyo inaweza kupatikana katika maeneo mbalimbali ya nchi ambapo rasilimali kama vile misitu, ardhi na samaki na vyakula vya baharini zinalindwa kwa kutumia taratibu hizi. Ziliruhusu rasilimali hizi kutumiwa na vizazi na vizazi vya watu bila kuhatarisha upatikanaji wake.

Matumizi ya visasili na matambiko kama haya si rahisi kuyaeneza sehemu nyingine za nchi kwa sababu vitu hivyo hufungamana na mahali na uzoefu wa kihistoria, na huidhinishwa na kundi mahsusi la wahenga. Wananchi wengine wa Msumbiji hawana historia na “*kosmogonia*” inayofanana na ya watu wa *Zimilene*. Lakini kwa kiasi fulani kama jamii wana majaliwa ya pamoja, hatari ya pamoja ya upoteaji wa rasilimali na kutenganishwa na mazingira yao ya asili. Tatizo la miamba ya kome linalojirudia siku hizi katika maeneo mengi ya nchi, ni namna ya kuchanganya mifumo ya taratibu za kisheria, visasili na matambiko pamoja na zana muhimu za kiutawala ili kujenga uelewa mpya wa pamoja wa jamii na utamaduni mpya wa usimamiaji wa rasilimali.

# Kutumia Maarifa Asilia ya *Jatropha*

## Matumizi ya mafuta ya *Jatropha curcas* kama malighafi na nishati

Makala hii iliandikwa na Reinhard K. Henning, baruapepe: [henning@bagani.de](mailto:henning@bagani.de). Intaneti: [www.bagani.de](http://www.bagani.de). Kwa taarifa zaidi kuhusu mfumo wa *Jatropha* tazama pia: [www.jatropha.org](http://www.jatropha.org).

### **Tini za MA 47 Agosti 2002**

Mali ni nchi isiyopakana na bahari iliyoko katikati ya Afrika Magharibi kwenye ukingo wa kusini wa Jangwa la Sahara. Wastani wa nchi wa kiasi cha mvua kwa mwaka unaanzia milimita 200 kaskazini hadi milimita 1200 maeneo ya kusini mwa nchi. Kwa muda mrefu, wakulima wamekuwa wakihami bustani zao kwa kutumia uzio wa aina ya mti ujulikanao kwa jina lake la kisayansi *Jatropha curcas* au “njugu dawa,” ambao hauliwi na wanyama na hivyo kuhami mazao ya chakula kama uzio hai.

*Jatropha curcas* ni mmea wenye asili ya Amerika ya Kusini ambao kwa sasa umeenea kote duniani kwenye maeneo ya kitropiki na ukame na nusu ukame. Ukiwa jamii ya mojawapo ya familia ya mimea ya *Euphorbiaceae*, ni mmea wa kudumu uhimilio ukame, unaweza kuishi hadi miaka 50 na kustawi kwenye udongo usio na rutuba. Ukiwa jamii ya karibu ya mbarika, mafuta yake yana sifa zilezile za tiba. Mbegu za *Jatropha* zina asilimia karibu 35 ya mafuta yasiyoliwa. Uzalishaji wa mbegu unafikia 0.8 kg kwa meta ya uzio kwa mwaka, zinazotoa kiasi cha lita 0.171.<sup>1</sup> ya mafuta! Kwa sasa Mali ina karibu kilomita 10,000 za urefu wa uzio ikiwa na kuongezeka kiwango cha cha kilomita 2,000 kwa mwaka, kiasi hicho kikiwa na uwezo wa kuzalisha lita 1,700,000 za

mafuta kwa mwaka. Katika maeneo yale ya Mali ambako hupatikana zaidi, urefu wa wastani wa uzio huu, ni kati ya kilomita 2 hadi 15 kwa kijiji, kiwango cha juu sana kikifikia hadi kilomita 40 kwa kijiji.<sup>2</sup>

Kwa jumla mmea wa *Jatropha curcas* unafahamika sana miongoni mwa watu wa Mali na kwa muda mrefu unatambulika kama mmea wenye matumizi mengi. Ukipandwa kwa uangalifu, *Jatropha* siyo tu kwamba huhami bustani dhidi ya mifugo yenye njaa bali pia hupunguza uharibifu na mmomonyoko vinavyo-sababishwa na upepo na maji. Kwa desturi mbegu zake zilikuwa ziki-vunwa na wanawake na kutumiwa kwa ajili ya matibabu na utenge- nezaji wa sabuni kwa njia za kienyeji.

Kurudi nyuma mpaka kwenye mwisho wa miaka ya 1930 pia uwezo wa mafuta yake ulitambulika kama chanzo cha nishati.<sup>3</sup> Kwa sasa yanaweza kutumika kama mbadala wa *gazoil* mchanganyiko unaotumika katika injini za dizeli kutoka India zinazoendesha mashine za nafaka na pampu za maji katika maeneo ya vijijini nchini Mali. Mafuta ya ubora wa hali ya juu yanayoziduliwa na mitambo inayoendeshwa kwa injini au vinu vya kushindilia vya “*Bielenberg*” vinavyoendeshwa kwa mikono au mashapo ya mchakato wa usafishaji wa mafuta yanaweza kutumika



katika utengenezaji wa sabuni katika maeneo ya vijijini na hivyo kuwapa wanawake fursa ya kujipatia kipato cha ziada na kuimarisha hali yao kiuchumi. Keki ya mashudu kama zao jingine la ziada la uziduzi inaweza kutumika kama mbolea mahuluku ya daraja la juu.

Shughuli za *Jatropha* zilianzishwa nchini Mali mwaka 1987 na Shirika la Misaada ya Kiufundi la Ujerumani (GTZ) katika muundo wa programu ya nishati rejeshi. Mradi wa *Jatropha* wenyewe ulianza mwaka 1993 na kumalizika mwaka 1997. Ulifanya kazi kwa kuunganisha yaliyotajwa hapa juu na vipengele vingine katika “mfumo wa *Jatropha*”. Mfumo huu siyo kwamba unasisitizia tu kuhusu matumizi ya mafuta ya *Jatropha* kama nishati lakini pia matumizi ya mafuta haya kama msingi muhimu wa kuamilisha mfumo wa mduara unaunganisha matokeo ya kiikolojia, kiuchumi, na ya kuzalisha mapato, siyo ya mwisho ikiwa mahsusi kwa wanawake.<sup>4</sup>

Hivyo basi, mfumo wa *Jatropha* huendeleza vipengele vinne muhimu vya maendeleo ambavyo huungana kusaidia kuleta uhakikisho wa njia endelevu za maisha kwa wakulima wa vijijini na ardhi inayowasaidia:

- Kudhibiti mmomonyoko na kuongeza ubora wa udongo
- Kuendeleza wanawake
- Kupunguza umaskini
- Nishati rejeshi

#### **Kudhibiti mmomonyoko na kuongeza ubora wa udongo**

“Uzio hai” wa *Jatropha* nchini Mali haudhibiti tu wanyama wasiotakiwa kufika katika mashamba; lakini hupunguza pia mmomonyoko unaosababishwa upepo na, iwapo utapandwa sambamba na mteremko, unaweza kudhibiti mmomonyoko unaosababishwa na maji. Mizizi ya mmea huota karibu na eneo la juu la ardhi, ikizuia udongo kama viboma vidogo au vizuizi vya udongo. Maboma hupunguza kwa ufanisi kasi ya mtiririko wa maji wa juu ya ardhi wakati wa mvua kubwa, ambayo ni ya kawaida, na hivyo kusababisha maji zaidi kupenya ardhini na kuongeza mavuno.

Keki ya mashudu inayobaki baada ya uziduzi wa mafuta ni mbolea mahuluku nzuri sana ikiwa na vijenzi vya madini vinavyoweza kulinganishwa na vile vya mbolea ya kuku. Mbolea hii ina thamani kubwa kwa kilimo katika nchi za Saheli, kwa kuwa udongo wa kule hupoteza kwa haraka mboji na mbolea za kemikali ni ghali sana.

Kampuni ya Kilimo cha Pamba ya Mali hutumia uzio wa *Jatropha* kuhakikisha programu ya kilala iliyoboreshwa, mashamba ya pamba yanalindwa na uzio wa

*Jatropha* ili kuzuia ng’ombe, ambapo mashamba hupandwa mikundekunde ili kuongeza ubora wa rutuba ya udongo.

#### **Kuendeleza wanawake**

Asasi nyingi za serikali na zisizo za serikali huwapa wanawake wa vijijini nchini Mali mashine za kusaga nafaka zinazoendeshwa na injini ili kuwapunguzia kazi za utayarishaji wa chakula. Hata hivyo, mashine hizi huhitaji rasilimali kutoka nje kwa ajili ya nishati, mafuta ya kulainishia, spea na matengenezo. Kwa hiyo, uanzishwaji wa mashine kama hizo husababisha vijiji kuwa maskini na fedha taslimu inayotakiwa kununulia na kusafirishia rasilimali hizi zitokazo nje hadi kijijini. Kwa kutumia mafuta ya *Jatropha* yaliyozalishwa mahali hapo kama nishati na mafuta ya kulainishia, kiasi cha fedha kinachoenda nje ya kijiji kinaweza kusimamishwa.

Kijadi, wanawake wa vijijini walitumia *Jatropha curcas* kwa ajili ya dawa (mbegu kama haluli—dawa ya kuharisha, ulimbo wa mpira kuzuia uvujaji wa damu na dhidi ya maambukizo, majani dhidi ya malaria) na kwa ajili ya kutengeneza sabuni. Mchakato wa jadi wa kutengeneza sabuni huhitaji nguvukazi kubwa, inayozalisha kiasi kidogo cha sabuni zenye ubora hafifu. Wakati mafuta ya *Jatropha* yanapotumika, ama peke yake au kwa kuchanganywa na mafuta ya mimea mingine kama vile “siagi ya shea,” kiasi kikubwa zaidi cha sabuni yenye ubora zaidi huzalishwa. Wanawake wanaweza kuuza kwa urahisi sabuni hii katika masoko ya vijijini au ya miji jirani, kwa njia hiyo wakiongeza uwezo wao wa kujiingizia mapato kwa kutumia rasilimali za kijijini hapo.

Baadhi ya maelezo ya uchumi wa uzalishaji sabuni kwa kutumia mashine ya kutumia mikono ya Bielenberg yameonyeshwa katika jedwali lifuatalo (bei kwa dola za Marekani 500 FCFA = dola 1 ya Marekani):

#### **Kupunguza umaskini**

Kwa kuhamasisha matumizi wianifu ya mmea wa *Jatropha*, mfumo wa *Jatropha* unaweza kutoa manufaa ya kifedha ya moja kwa moja kwa uchumi wa vijijini. Ili kuonyesha hili kwa kutumia mkokotoo rahisi, chukulia kwamba kwa wastani kijiji kimoja katika eneo la mfano kina kilometa 15 za uzio wa *Jatropha* ambao ni sawa na tani 12 za mbegu.

Hizi tani 12 za mbegu zinaweza kuzalisha mapato ya fedha taslimu ya dola za Marekani 1,800 wakati mafuta yameziduliwa na bidhaa kuuzwa:

	(Dola za Marekani )
• Kilo 9,000 za keki ya mashudu kwa 0.03 =	270
• Lita 2,400 za mafuta kwa 0.60 =	440
• Kilo 600 za mashapo kwa 0.15 =	90
	<i>Jumla: 1,800</i>

Tukichukua mfano halisi wa mjasiriamali katika kijiji kidogo karibu na mji wa Bamako ambaye hununua mbegu kwa ajili ya uzalishaji wa sabuni na anayeajiri watu kwa shughuli za uzalishaji (Uziduzi kwa kutumia mashine ya kushindilia ya *Bielenberg*, uzalishaji wa sabuni, angalia jedwali hapo juu) mapato ya fedha taslimu kwa watu wa kijiji hicho, akiwemo pia mjasiriamali, hufikia kiasi cha dola za kimarekani 3,630:

	(Dola za Marekani )
• Kilo 12,000 za mbegu kwa 0.10	1,200
• Kilo 5,000 za kazi kwa 0.20	1,000
• Faida ya mjasiriamali	1,430
	<i>Jumla: 3,630</i>

Iwapo takwimu hizi zinatumiwa kutabirika mashamba ya *Jatropha*, basi faida inayokaribia kulingana na ya kilimo cha pamba ni rahisi kupatikana. “Mfumo wa *Jatropha*” husaidia pia kupunguza umaskini kwa:

Kupunguza hasara zinazosababishwa na mifugo inayorandaranda au madhara ya upepo;

- Kuongeza upenyaji wa maji ya mvua, na hivyo kupunguza kazi ya umwagiliaji maji inayohitajika kwenye bustani za vijijini;
- Kuongeza rutuba ya udongo kwa kutumia keki za mashudu kama mbolea;
- Kuongeza matumizi ya malighafi nafuu zipatikanazo kijijini badala ya zile ghali zitokazo nje;
- Kupunguza migogoro kati ya wakulima na wamiliki wa mifugo kuhusiana na mipaka ya mashamba yao;
- Kutoa nafasi za kazi, na hivyo kupunguza ulazima wa wanavijiji kuhamia mijini kwa ajili ya kutafuta kazi.

Kutokana na manufaa ya kiuchumi, watu wa vijijini wanapanda uzio mpya wa *Jatropha* kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano huko Kita, moja ya maeneo ya majaribio ya mradi wa *Jatropha*, urefu wa wastani wa uzio umeongezeka kutoka kilometa 5 hadi 15 katika miaka 8 iliyopita.

#### Nishati rejea

Katika maeneo ya vijijini nchini Mali, injini za aina ya “Lister” hutumika kuendeshea mashine za kusaga nafaka na pampu za maji. Hizi injini za dizeli zenye

Maelezo	Kiasi	Kizio	Bei yakizio Dola ya Marekani	Jumla kwa Dola ya Marekani
<b>Viingizia</b>				
Mbegu (hutoa lita 3 za mafuta kwa mashine ya kushindilia kwa mkono)	12	kg	0.1	1.20
Magadi	0.5	kg	1.2	0.60
Nguvukazi (saa 4 kushindilia, saa 1 kuzalisha sabuni)	5	saa	0.2	1.00
Uchakavu/matengenezo (miaka 5, lot/a, 240,)		Dola ya Mar/kg	0.02	0.24
<b>Jumla ya gharama</b>				<b>3.04</b>
<b>Mapato</b>				
Keki ya mashudu	9	kg	0.03	0.27
Sabuni nyeupe	28	vipande (170 g)	0.15	4.20
<b>Jumla ya mapato</b>				<b>4.47</b>
<b>Faida halisi</b>				<b>1.43</b>
<b>Faida kwa kila lita ya mafuta</b>				<b>0.48</b>
<b>Faida kwa kila kilo ya sabuni</b>				<b>0.31</b>
<b>Bei kwa kila kilo ya sabuni</b>				<b>0.89</b>

chumba—mwako zisizo ghali zitokazo India huhitaji tu nyongeza ya chujio la nishati ili ziweze kuendeshwa kwa mafuta ya *Jatropha* peke yake, na hivyo kuondoa kabisa mahitaji ya *gazoil*. Zaidi ya hayo, kwenye hali ya juu ya utendaji, mafuta ya *Jatropha* huwa na ufanisi hata kuliko *gazoil* kwa sababu ya kuwa na kiwango cha juu cha oksijeni<sup>5</sup>. Kutokana na majaribio yaliyoendeshwa na mradi wa *Jatropha*, mafuta yanaweza pia kutumika kwa mafanikio kama kilainishio cha injini<sup>6</sup>.

Kwa mazingira yaliyosawa, nishati inayohitajika kuzalisha mafuta ya *Jatropha* kwa kutumia mitambo ya kugandamiza hufikia karibu asilimia 10 ya mafuta yanayopatikana. Kwa kuwa mafuta ya *Jatropha* yanaweza kuzalishwa kwa gharama nafuu<sup>7</sup>, vilevile yanaweza kuuzwa kwa bei ya chini kuliko bei rasmi ya *gazoil* kwenye vituo vya kuuzia mafuta. Na kilicho muhimu zaidi hata kuliko bei ni uwezekano wa uzalishaji wa nishati tano kijijini, kwa sababu ya kutokupatikana mara kwa mara kwa *gazoil* maeneo ya vijijini kunakosababishwa na ukosefu wa barabara zinazopitika wakati wa msimu wa mvua.

Teknolojia ya kutumia mafuta menyu asilia ya *Jatropha* kama mbadala wa mafuta ya taa kwa ajili ya taa na majiko bado haijapatikana. Vituo mbalimbali vya utafiti vinashughulikia suala hili.

## Hitimisho

Matokeo ya Mradi wa *Jatropha* hadi hivi sasa yanadhihirisha kuwa uwezekano wa kutumia mfumo huu kwa mafanikio ni mkubwa, ilimradi mkabala ulio makini unachukuliwa. Zaidi ya yote, tahadhari lazima kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa wanawake wanabakiwa na wajibu wao wa kuvuna na kusindika mbegu.

Zaidi ya hayo, Mali ni nchi halisi ya Saheli; ukubwa wake kieneo na aina mbalimbali za tabia ya nchi zinaakisi hali za kiikolojia zinazopatikana kote katika eneo la Saheli. Kwa sababu hiyo juhudi zinazofanywa tayari nchini Mali za kufaidika na mimea inayotoa mafuta zinaweza kuchukuliwa kama mfano na kutumika kuelezea kinagaubaga “dhana ya uzalishaji na matumizi ya mafuta ya mimea kama nishati ambayo inafaa kwa eneo la Saheli kwa ujumla, na hata kwa nchi nyingine za Afrika.

Kwa muhtasari, mfumo wa *Jatropha* unabainishwa na vipengele vingi vizuri vya kiikolojia, kinishati na kiuchumi ambavyo vinahusiana na utumiaji wa mmea huu kiuchumi. Kadiri mmea huu unavyotumiwa, ndivyo mazingira yanayozidi kuwa bora na pia uzalishaji wa chakula.

## Marejeo

- 1 Reinhard K. HENNING, Production und Nutzung von Pflanzeöl als Kraftstoff in Entwicklungsländern. In: VDI-Berichte Nr.1126, 1994, 215—229.
- 2 Reinhard K. HENNING, 3. Fachlicher Zwischenbericht zum Projekt: Produktion Und Nutzung von Pflanzeöl als Kraftstoff; unpublished project report, Project Pourghère, GTZ, 1996.
- 3 Siaka KONE, Les activités précédentes sur le Pourghère au Mali, unpublished project report, Programme Special Energie Mali, 1998.
- 4 Reinhard K. HENNING, Klaus V. Mitzlaff, Produktion und Nutzung von Purgieröl als Kraftstoff und Rohstoff für die locale Seifenherstellung im Saheli. In Witzenhauser Hochschulwochen, 1995.
- 5 Carl BIELENBERG, personal communication (1994).
- 6 Reinhold Metzler, Plant Oil as Fuel and Lubrication Oil, unpublished project report, Project Pourghère, 1996.
- 7 Hans-Jürgen WIEMER, Rapport de mission: Etablissement d'un système de suivi et évaluation des effets du projet, unpublished project report, Projet Pourghère (1995).

# Uwezo wa Bima ya Jamii ya Kijadi katika Kusaidia Huduma ya Afya

Makala hii iliandikwa na Prof. Damen Haile Mariam, Profesa Mshiriki na Mkuu wa Idara ya Afya ya Jamii, Kitivo cha Tiba Chuo Kikuu cha Addis Ababa, Ethiopia. Kwa maelezo zaidi tumia baruapepe, [hcfp.aau@telecom.net.et](mailto:hcfp.aau@telecom.net.et)

**Tini za MA 48  
Septemba 2002**

Katika nchi nyingi zinazoendelea, mipango ya sasa ya kugharimia shughuli za afya inayobainishwa na migao ya bajeti ambayo nayo inazidi kupungua hatua kwa hatua na mipango zaidi ya kuchangia gharama imesababisha kuwepo na haja ya kuchunguza mikabala mbadala na ya ziada ili kuboresha hali ya ugharimikiaji. Miongoni mwa njia mbadala zinazopendekezwa ni mbinu zinazojumuisha mipango yenye msingi katika jamii ambazo huchota uwezo wa mipangilio ya kijamii ya jadi.

Nchini Ethiopia, *eders* ni aina ya mipangilio ya jadi inayotumika hasa kuwasaidia wale waliofiwa na kwa ajili ya kutekeleza shughuli zinazohusiana na maziko. Vyama hivi pia huombwa msaada wakati wa shughuli mbalimbali za kujisaidia na wakati mwingine hufanya kazi kama bima za afya ingawa kwa namna isiyo rasmi. Vina uwezo dhahiri wa kutoa huduma kama mbinu za jamii za ugharimiaji. Kwa kuwa hivi ni vikundi ambavyo tayari vinafanya kazi, gharama za utawala kwa ajili ya shughuli za ziada zinazohusiana na masuala ya afya si za kutisha kama unapoanzisha chombo kipya cha bima. Kwa kuongeza, *eders* ni vikundi vyenye msingi wa uelewano baina ya wanachama, hali inayopunguza uwezekano wa uteuzi mbaya.

## Mpangilio na muundo wa eders

*Eder* ni aina ya taasisi ya kijamii ya jadi inayoanzishwa kutokana na makubaliano ya hiari baina ya wanajamii ili kushirikiana miongoni mwao wakati wowote mmoja wao anapofikwa na matatizo. Kazi ya msingi ya *eder* ni kushughulikia masuala ya kufariji na maziko na kufariji pale unapotokea msiba miongoni mwa wanachama. *Eders* pia hutoa msaada kufidia hasara kwa mwanachama (kwa tukio kama la wizi, n.k.), wakati wa harusi ya mwanachama, n.k. Zaidi ya hayo, *eders* huwa na umuhimu mkubwa katika shughuli nyingine za maendeleo kwenye jumuiia inayowazunguka. *Eders* hushiriki kwa kuchanga fedha au kuratibu kazi za kujitolea za wanachama katika shughuli kama vile ujenzi wa barabara, shule, taasisi za afya na nyingine kama hizo. Baadhi ya *eders* hutoa mchango wa fedha kwa wanachama waliopoteza nyumba zao kutokana na moto au kumfidia yule aliyepoteza maksai wake, ambapo nyingine hutoa pia msaada kwa wanachama ili kulipia gharama za matibabu.

Muundo wa *eders* zilizo nyingi ni wa kawaida sana. Vikundi hivi vina mwenyekiti au “mwamuzi” na karibu vyote vina Katibu na Mweka Hazina. Inasemekana kwamba *Eders*

ni vikundi vya kijamii vinavyoendeshwa kidemokrasia na kwa usawa kuliko vingine nchini Ethiopia—uanachama uko wazi kwa kila mtu bila kujali hadhi yake ya kijamii na kiuchumi, dini, jinsia, na kabila. Ingawa wahojiwa wachache walitaja uwezo wa kulipa michango kuwa sababu ya wao kutokuwa wanachama wa *eders*, vikundi karibu vyote vya *eders* vina taratibu maalumu kwa wanachama wanaokabiliwa na matatizo ya kiuchumi na hivyo kushindwa kulipa michango yao baada ya kuwa wanachama kwa muda fulani. Wanachama wa aina hii huchukuliwa na vikundi vya *eders* kama “wastaafu” na wanaruhusiwa kupata haki zote wanazostahiki wanachama wengine.

### Uwezo wa *eders* katika kugharimia huduma za afya

Muundo wa kishirika wa vikundi vya *eders* ambavyo kwa sasa hutoa huduma za afya hautofautiani sana na ule wa vikundi visivyotoa huduma hii—hapana shaka pangetakiwa kuwa na msititizo wa wazi katika hili kwenye masuala ya afya. La muhimu hapa ni uhusiano wa karibu na mawasiliano yanayoendelea pamoja na taasisi za afya zinazotoa huduma kwa wanachama.

Mantiki ya kifedha ya *eder* haitofautiani na mfumo wowote wa bima. Katika mazingira yaliyo mengi wanachama huchanga kiasi cha fedha kilichopangwa kwa wiki au kwa mwezi. Wakati wowote mwanachama anapopata tatizo, kiasi kilichopangwa (kutegemea kanuni mahsusi za *eder*) hutolewa kwenye ule mfuko wa pamoja na kupewa yule mwanachama. Kuna pia vikundi vichache vya *eder* vinavyochangisha hicho kiasi kilichopangwa kila tatizo linapotokea. Katika upembuzi yakinifu wa bima ya afya yenye msingi katika jamii iliyofanywa na mwandishi (wa makala hii) na mwakilishi wa BASICS\* (“*Basic Support for Institutionalizing Child Survival*”, shirika linalosaidia kutekeleza mipango inayosaidiwa na USAID) katika miji mitatu, Adama katika Jimbo la Oromo na *Yirgalem* na *Arbaminet* katika Jimbo la Kusini, vikundi vya “*eders*” vimeonekana kutoa msaada wa kifedha kwa matatizo ya afya ya wanachama.

Kwa mfano, katika mojawapo ya kikundi kilichohusishwa katika upembuzi, kiasi kinachofikia hadi dola za Marekani 15 kilitolewa kwa kaya ambamo mwanafamilia alitakiwa kulazwa hospitalini. Kiasi hiki hulipia gharama za awali zinazohitajiwa na hospitali kabla ya mgonjwa kulazwa.

\* Dkt. Logan Brenzel (Mshauri wa mambo ya fedha katika masuala ya huduma za afya na BASICS)

Uchunguzi wa ufuatiliaji ulifanywa pia na mwandishi mwaka 1999 katika vijiji vilivyoteuliwa kwa utaratibu maalumu nchini humo. Data kwa ajili ya sehemu hii ya uchunguzi zilikusanywa kupitia utafiti uliofanywa katika kaya na mahojiano ya wanaoruhusiwa kutoka hospitalini. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu wa baadaye, karibu asilimia 87 ya wahojiwa kutoka kwenye kaya na asilimia 72 ya wahojiwa wanaoruhusiwa kutoka hospitalini walikuwa wanachama wa vikundi vya *eder* wakitoa malipo ya mwaka ya dola za Marekani 7 (1.5 hadi 60) na dola za Marekani 8 (*Birr* 1.5 hadi 68) kwa wanakaya na wahojiwa wanaoruhusiwa hospitalini kwa mfuatano huo. Muhimu zaidi, asilimia 21.5 ya wahojiwa kutoka kundi la wanakaya na asilimia 16 ya wahojiwa wanaoruhusiwa kutoka hospitalini walidai kuwa vikundi vyao vya *eder* hutoa msaada wakati wa mahitaji ya tiba. Aina ya msaada unaotolewa yaweza kuwa mkopo au pengine kulipia gharama zote za matibabu za mwanachama. Wahojiwa kutoka makundi hayo yote mawili waliulizwa iwapo wangependa kujiunga na mpango wowote wa bima ya afya unaosimamiwa na vikundi vya *eder*. Asilimia 86 kutoka kundi la wanakaya na asilimia 90 katika kundi la walioruhusiwa kutoka hospitalini walikuwa wanapendelea kujiunga na mipango kama hiyo. Wastani wa michango ya kila mwezi ambao wahojiwa walidai kuwa wangeweza kuulipa ulikuwa ni

*birr* 2.5 (dola za Marekani 0.3) kwa mfiko wa *birr* 1 hadi 36 (dola za Marekani 0.13 hadi dola za Marekani 4.5) katika kundi la wanakaya na *birr* 3.4 (dola za Marekani 0.4) kwa mfiko wa *birr* 1 hadi 48 (dola za Marekani 0.13 hadi dola za Marekani 6) katika kundi la wahojiwa walioruhusiwa kutoka hospitalini. Wahojiwa katika kundi la walioruhusiwa kutoka hospitalini (ambao karibuni wamepata uzoefu wa gharama za ugonjwa) walionyesha kiwango cha juu cha mwelekeo wa kujiunga na mipango ya bima ya afya inayosimamiwa na *eder* wakiwa na utashi wa juu kidogo wa kulipia kwa masharti ya michango ya kila mwezi. Manufaa ambayo wahojiwa wengi waliyathamini ilikuwa huduma za dharura zikifuatiwa na dawa. Ni dhahiri kwamba watu wa maeneo ya vijijini ambako hakuna fursa za kutosha za huduma za dharura (ikiwa ni pamoja na huduma za ukunga) wangukuwa tayari kujiunga na mipango ambayo ingewawezesha kupata huduma hizo. Mfano wa hali halisi ni *eder* iliyo katika eneo moja la utafiti ambayo ilitoa mkopo wa Dola za Marekani 25 kwa mama mjamzito aliyekuwa anakabiliwa na matatizo ya kujifungua. Fedha hiyo ilitumika kukodi usafiri wa dharura wa kumpeleka mama mjamzito kwenye kituo cha afya kilichokuwa umbali wa karibu kilometa 40 kutoka kijijini hapo.

Umaarufu wa *eder* miongoni mwa watu wa kila aina umekuwa ukiongezeka. Hizi taasisi zisizo za biashara zenye kutegemea msingi wa mshikamano, urafiki na kusaidiana miongoni mwa wanachama zinaweza kuwa na mbinu za kushurutisha utiifu na vivutio sahihi vya kuzitumia—sifa muhimu zinazoangaliwa wakati wa kuchunguza wajibu wa taasisi asilia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa jumla, inadhaniwa kwamba mipango inayosimamiwa na *eder* ingeweza kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

### Marejeo

- Aredo, D. The Iddir: A study of an indigenous informal financial institution in Ethiopia. *Savings and Development*. 1993, XVIII (No.1): 77-90.
- Haile Mariam, D., & Brenzel, L. Feasibility of Community-based Health Insurance in Ethiopia. BASICS Publication, 1998, Arlington, VA.
- Klitgaard, R. *Including Culture in Evaluation Research*, in Piciotto, R. and Rist, RC. eds. *Evaluating Country Development Policies and Processes*. 1995. San Francisco: Jossey-Bass.
- Pankhurst, R., & Eshete, E. Self-Help in Ethiopia. *Ethiopia Observer*. 1958;2(11):354-364.
- Seifu, A. Eder in Addis Ababa: A Sociological study. *Ethiopia Observer*. 1968; 12(1)8-33.

# Wakulima Wafanya-Majaribio: Teknolojia ya Kujibunia

Makala hii iliandikwa na Roland Bunch, mratibu, na Mateo Canas, mtafiti, COSECHA, Honduras.

**Tini za MA 49  
Oktoba 2002**

Nchini Honduras, ikiwa ni matokeo ya kazi ya mashirika ya maendeleo ya kilimo yapatayo 20 katika miaka ya mwanzoni ya 1990, mamia ya wakulima wafanya-majaribio wamekuwa wakijaribisha wao wenyewe kwa muda unaoanzia miaka miwili hadi kumi mara baada ya kufunga programu ambayo awali walikuwa washiriki wake. Mwaka 1999, nchini Honduras, shirika lijulikanalo kama "Association of Advisors for Sustainable Ecological and People-centered Agriculture" [COSECHA] liliamua kuchunguza teknolojia iliyokuwa ikien-delezwa na wajaribishaji hawa wakulima, na jinsi teknolojia za namna hii zinavyoweza kuenezwa vizuri kwa wakulima wengine. Kwa nia hiyo, COSECHA liliwahoji watu 50 miongoni mwa wakulima wafanya-majaribio hawa. Teknolojia zilizoordheshwa ni zile tu ambazo wakulima wadogo walikuwa wamebuni wenyewe, baada ya programu kuwa imefika mwisho, na kwamba zilikuwa hazijawahi kuenezwa au kujulikana ndani ya nchi kabla ya ugunduzi uliopangwa na wakulima hao.

Utafiti unaonyesha kuwa wakulima hawa wana uwezo wa kubuni idadi kubwa ya teknolojia muhimu na halisi, na hivyo kuthibitisha kuwa ukusanyaji na uenezaji wa teknolojia za Majaribio ya Wakulima katika mataifa mengine duniani kote ingekuwa

shughuli ya manufaa kwa asasi zinazojihusisha na maendeleo ya kilimo.

## Programu za maendeleo ya teknolojia shirikishi [PTD] nchini Honduras

Ikianzia na uanzishwaji wa "World Neighbors-managed Guinope Program" Januari mwaka 1981, PTD imekuwa mbinu inayotumika sana kwa ajili ya maendeleo ya kilimo nchini Honduras. Kiasi cha asasi 20 za maendeleo ziliwafunza wakulima kufanyia majaribio angalau programu 30 tofauti nchini kote. Nyingi kati ya programu hizi zilifikia mwisho mapema kwenye miaka ya 1990, zikiwa na matokeo yanayoifanya Honduras kuwa mojawapo ya nchi zenye utajiri mkubwa kwa msingi wa wingi wa wakulima-wafanya majaribio bila msaada wa kitaasisi. Hata hivyo, hakuna taasisi iliyowahi kutafiti jambo hili.

## Uchunguzi

COSECHA limefanya ziara sehemu zote mbili nyumbani kwa wakulima hawa na mashambani mwao wanakotumia teknolojia waliyoibuni. Katika ziara hizi, mahojiano hufanywa kwa mtindo wa maongezi yasiyo rasmi ambayo kupitia kwake

mhoji huhakikisha kuwa kila suala katika orodha ya masuala 20 linashughulikiwa. Baada ya kila ziara (ambayo kwa kawaida huchukua nusu siku) orodha ya maswali yote yaliyotayarishwa mwanzoni mwa uchunguzi hupitiwa ili kuhakikisha kuwa yameshughulikiwa, na yale yaliyosahaulika yanaulizwa.

Maswali hushughulikia masuala kama vile ni teknolojia zipi ambazo wakulima wamekuwa wakifanyia majaribio na ni zipi zinazoonekana kuwa na mafanikio (yaani ni zipi wakulima walikubali kuendelea kuzitumia). Maelezo ya kina ya teknolojia zenye mafanikio yanachukuliwa pamoja na uchanganuzi wa gharama kwa kila teknolojia kwa kulinganisha teknolojia hii inavyodhibiti mashamba. Data kuhusiana na mwinuko, kiasi cha mvua, ukubwa wa miliki wa ardhi, mteremko wa mashamba, n.k. nazo huchukuliwa. Mkulima huulizwa kuhusu mwitikio wa wakulima wengine kuhusiana na kukubalika kwa teknolojia. COSECHA pia hudodosa ili kujua ni vitu gani mkulima anavyofikiria vinamkwaza, na iwapo angependelea kushirikiana na baadhi ya makampuni ya kutafuta masoko, iwapo mkulima angependa kujiunga na umoja wa wakulima wafanya-majaribio ya kilimo kitaifa, na ikiwa ndiyo malengo makuu ya umoja huo wangependa yawe yapi.

#### Matokeo hadi sasa: teknolojia zilizogunduliwa

Jumla ya wakulima wafanya-majaribio hamsini na wawili kutoka wilaya 10 kati ya 23 za nchi ya Honduras wamehojiwa. Hawa wanajumuisha pia wakulima ambao hapo awali walikuwa wamepewa mafunzo na asasi 17 tofauti, yakianza na AZISE 12 hadi asasi 3 za serikali na asasi 2 za kitaaluma. Palikuwemo pia wakulima wafanya-majaribio wanawake 7, ingawa hata hivyo wanawake wa Amerika ya Kati, kwa ujumla, hawajihusishi sana na kilimo kikubwa (yaani, nje ya bustani za kaya) mpaka kipindi cha mavuno, wala hawakupatiwa mafunzo ya kuwa wakulima wanaofanya majaribio na miradi ya miaka ya 1980 na mapema 1990.

Hawa wakulima wabunifu 52 walibuni teknolojia 82, nyingi ya hizo zikiwa kwa ajili ya kilimo cha mashamba makubwa, lakini pakiwemo na chache za shughuli za baada ya kuvuna na za utayarishaji wa chakula. Kumekuwepo na juhudi za kuweka teknolojia hizi katika madaraja ya makundi matatu. Kundi "A" linawakilisha zile teknolojia zinazoonekana kuwa na thamani kwa mujibu wa manufaa anayoyapata mkulima na upana wa matumizi miongoni mwa wakulima wengine nchini Honduras, manufaa yanayozifanya kustahili uthibitisho zaidi na hivyo, kutegemeana na matokeo ya mchakato wa uthibitisho, kuendelea kuenezwa kwa wakulima wengine.

Kundi "B" hujumuisha zile teknolojia zinazoweza kufaa kuthibitishwa, lakini kunakoweza kufanyika baadaye. Kundi C hujumuisha zile teknolojia ambazo inaelekea hazifai kuenezwa. Ingawa hizi tathmini ni za lazima kuliko kuwa za dhahania, COSECHA hutumia orodha ya vigezo 19 vya teknolojia mwafaka (Bunch 1982) vinavyotusaidia kutathmini kila teknolojia.

Kati ya teknolojia asilia 82 zilizobuniwa, 39 zimeainishwa kuwa katika Kundi A. Kati ya hizi 39, idadi ifuatayo ilifungamana na kila mojawapo ya makundi yaliyoorodheshwa hapa chini:

Udhibiti wa wadudu	15
Urutubishaji	10
Udhibiti wa magonjwa ya mimea	8
Udhibiti wa magugu	2
Utayarishaji wa chakula	2
Ufugaji	2
Uenezaji wa mimea	1
Utiaji wa mbolea mbichi	1
Uhifadhi wa udongo	1
Nyinginezo	<u>3</u>
	<b>45</b>

Jumla ya teknolojia ni kubwa kuliko zile 39 kwa sababu baadhi ya teknolojia zilihusisha vipengele vya makundi mawili.

Kutokana na orodha hii inaweza kudhihirika kwamba wakulima wafanya-majaribio walichagua kujaribu aina nyingi za teknolojia zinazotofautiana, ikiwa ni pamoja na hata baadhi kwa mfano utayarishaji wa chakula) zile ambazo kwa kawaida hazihusiani sana na uwanja wa kilimo.

Hata hivyo, ni jambo la kushangaza pia, kwamba makundi machache ya teknolojia yameachwa kabisa. Hakuna hata mkulima mmoja katika kundi hili la wabunifu aliyefanya majaribio ya uvunaji wa maji au matumizi, ingawa maeneo mengi ya Honduras yana ukame mbaya sana; katika sehemu kubwa ya kusini mwa Honduras, upungufu wa maji wa vipindi au wa jumla hapana shaka ni kikwazo muhimu katika mifumo ya uzalishaji ya wakulima wa vijijini. Zaidi ya hayo, uzoefu wa wakulima wabunifu katika miradi ya sasa hutoa ushahidi wa maana kwamba wakati ambapo wana shauku sana ya kufanya majaribio katika uvunaji na matumizi ya maji kwa ufanisi zaidi, hakuna hata mmoja wa wakulima hawa aliyejumuishwa katika uchunguzi kwa sababu mradi huu wa COSECHA bado unaendelea.

Ni jambo la kushangaza pia kufahamu kwamba hakuna teknolojia hata moja iliyohusiana na uanzishwaji wa mazao mapya (ingawa vigezo vilivyotumika katika uchunguzi, pengine vikiwa na vikwazo sana, vingeondoa uwezekano wa kuanzisha zao lolote ambalo tayari lipo



mahali pengine popote nchini Honduras) au matumizi ya mazao ya miti au kilimo mseto. Kwanza inawezekana kwamba baadhi ya makundi ya teknolojia (kwa mfano, uvunaji wa maji) hayakufanyiwa majaribio kwa sababu wakulima ama hawakufikiria hata kidogo kama wanganikiwa kupata ufumbuzi wowote, au kwa sababu tu wazo linalohusu teknolojia hizo halikuwajia. Kwa hiyo, miradi ya baadaye ya kilimo inatakiwa kujadili na wakulima kabla ya kuhitimisha kazi yao katika eneo ili kubainisha ni teknolojia zipi zinazoweza kutumika katika siku za baadaye.

Pili, wakulima wanaweza kuwa wanafahamu aina fulani za teknolojia wanazoweza kuzitumia, lakini wakawa hawazioni kama teknolojia zenye umuhimu mkubwa kwao. Mhalani, katika suala la mazao ya miti. Wakulima wabunifu kwa hakika wanatambua kwamba mazao hayo yapo na yana faida, lakini wanaweza kuhisi kuwa mtu anayotakiwa kusubiri kwa miaka mingi kabla ya kurudisha faida jambo linaloweza kufanya teknolojia hizi kuwa na umuhimu mdogo kuliko zile zinazorudisha faida haraka. Hali kama hiyo inaweza kufananishwa na mfumo wa kilimo mseto, ingawa wakulima kusini mwa Honduras katika mradi wa FAO, unaoweka msisitizo kwenye miti iliyotawanyika, wanafanyia sana majaribio mabadiliko mbalimbali ya mfumo wa miti iliyotawanyika.

Bila shaka, wakulima wabunifu pengine hawakufanya majaribio mazao mapya kwa sababu, ili yahusishwe katika utafiti, yangetakiwa kuwa mazao yanayolimwa tu nje ya Honduras, jambo ambalo lingesababisha ugumu kwa wakulima wabunifu kujifunza kuhusu mazao hayo au kupata mbegu za kupanda.

### Teknolojia zenye kuleta matumaini zilibunwa

- Wakulima waligundua kuwa vidukari hufa ikiwa vitakaushwa. Kwa hiyo walijaribu kwa kutumia unga wa ngano uliochanganywa na maji kwa ajili ya kunyunyizia kwenye miti ya matunda katika bustani zao za miche, na kugundua kuwa wangedhibiti vidukari na wadudu wengine wenye tabia hiyo ya kufyonza kwa njia hiyo rahisi.

- Maji ya sukari au kidogo maji ya chumvi, yakiwekwa kwenye ncha ya juu ya mmea unaoota, yalifanyiwa majaribio kwa mafanikio kama njia ya kudhibiti wapekecha nafaka.

- Mkulima mwingine mbunifu aligundua kuwa sungu wanaokata majani hawapendi kuishi karibu na miarobaini. Kwa kupanda miarobaini karibu na mikusanyiko mbalimbali ya hawa sungu, aliweza kuwafukuza (walihamishia makazi yao mahali pengine).

- Mbolea za majani zilibunwa na kutengenezwa kwa kutumia ama mbolea ya wanyama, uozo wa majani ya mkakao, majani ya magugu mbalimbali ya kawaida, au hata vumbi la mbao (ya mwisho ikiwa imethibitika kuwa ya manufaa sana katika kuzuia magonjwa).

- Mkulima mmoja mbinifu mwanamke aligundua kuwa rojo la kahawa linaweza kukaushwa kwa kulitandaza tu juani ili kulikausha. Mkulima mbunifu mwingine aligundua kuwa kwa kuchanganya rojo la kahawa oevu na mbolea ya kuku au unga wa mbao ungeweza pia kulikausha. Likiwa limekauka, rojo la kahawa ni mbolea nzuri sana, ambalo hapo kabla lilikuwa likichafua mito nchini humo.

- Myeyusho wa uozo wa majani ya kakao na mkaratusi uligunduliwa kuwa kiuakuvu kizuri sana kwa ajili ya bustani za miche.

- Mkulima mmoja aligundua kwamba angeua bakteria waliokuwa kwenye udongo katika kitalu kwa kulima udongo huo vizuri na kisha kuufunika kwa plastiki safi ili uweze kupata joto sawasawa la saa za mchana.

- Kunyunyizia mimea na unga wa mbao ulioyeyushwa ndani ya maji na pia kuweka unga huo wa mbao kwenye mashina ya mimea, njia zote mbili zimeonekana kufanikiwa kudhibiti magonjwa ya mimea kadhaa hata yale magonjwa hatari sana kama baka jani (*Phytophthora infestas*) kwenye mimea ya nyanya na viazi.

- Chakula cha wanyama kinachotokana na mahindi kilitengenezwa kwa kuongezea majani ya m-tithonia na maganda ya mayai na hivyo kuongeza uzalishaji wa mayai.

- Mkulima mmoja mbinifu aligundua kwamba kwenye miinuko ya zaidi ya mita 500, upandikizaji wa mwarobaini kwenye mti wa shina la mizizi uliopo mahali hapo husababisha kukua kwa haraka sana kwa mwarobaini.

- Mkulima mbunifu mwingine aligundua kwamba kwa kuchanganya mimea (kilimo mseto) ya (*Canavalia ensiformis*) ndani ya mimea ya mhogo, alipunguza kwa kiasi kikubwa muda wake wa kupalilia na kuongeza uzalishaji wake wa mhogo kwa zaidi ya asilimia 25.

Inatakiwa ifahamike kwamba teknolojia hizi kwa namna yote ile ni teknolojia zinazoweza kujumuishwa chini ya utambulisho wa teknolojia zinazotumia viingizia kidogo na za kiikolojia, na mara nyingi kuna pia teknolojia zinazofaa sana kwa ajili ya wakulima wa vijijini wenye mtaji mdogo. Kwa ujumla, ni nafuu sana (baadhi hazihitaji fedha taslimu za kutoa hata kidogo), hutumia rasilimali iliyopo mahali pale, haziongezi mashaka, hutoa mapato ya haraka na yanayotambulika, na karibu zote ni za gharama nafuu sana, na karibu zote zinatumiwa vizuri sehemu nyingi. Orodha hiyo hapo juu inadhihirisha

waziwazi kwamba wakulima wabunifu wa vijijini si kwamba tu wanaweza kubuni teknolojia zenye bidhaa bali hata teknolojia hizo wanazobuni zinafaa sana wakulima wengine wadogowadogo.

Mojawapo ya matokeo ya kukatisha tamaa ya utafiti ni kwamba teknolojia zilizobuniwa na wakulima wadogowadogo hazikusambazwa sana. Hakuna teknolojia iliyobuniwa na mkulima iliyosambazwa kwa zaidi ya wakulima 10 wengine kwa kutumia juhudi pekee za wanavijiji.

### Mafunzo yaliyopatikana

- Utafiti huu unatuacha bila shaka yoyote kwamba wakulima wabunifu wa vijijini, kwa juhudi zao wenyewe, wanaweza kubuni teknolojia za msingi na zinazoweza kubadilishwa na ambazo zinazonekana kuwa na uwezo mkubwa kwa wakulima wote nchini, na pengine kote duniani. Wakati teknolojia hizi bado zinahitaji uhakiki zaidi, uwezo wake, kwa mujibu wa vigezo vinavyokubalika vya ufaaji wake na uwiano wa gharama na faida kiuchumi, zingeonekana kuwa kubwa sana.
- Asasi mbalimbali nchini Honduras zimetumia mbinu mbalimbali katika mafunzo kwa wakulima wabunifu. Wakati wa utafiti huu, ilionekana kwamba asasi zilizotumia mbinu zinazoleta mafanikio ya kiwango cha juu katika majaribio machache ya kwanza waliyofanya, yaliwahasisha wakulima wengi zaidi kufanya majaribio kwa siku za baadaye kuliko yalivyofanya mashirika yaliyobaki. Kupata mafanikio ya haraka, yanayotambulika

miongoni mwa wakulima wabunifu mapema kuanzia mwanzo ni sehemu muhimu ya mchakato mzima wa kushajiisha ambao ni wa lazima kwa ajili ya watu kutumia juhudi kufanya majaribio ya mara kwa mara.

- Katika baadhi ya mifano miradi haitaweza kupata teknolojia ambayo tayari imethibitishwa, yenye mafanikio tayari ikiwa inatumiwa na miradi mingine katika mazingira yanayofanana (kiikolojia, kiutamaduni, n.k.). Mradi utajikuta ukifanya majaribio ya aina kadhaa za teknolojia kabla ya kufanya kazi na wakulima. Hata hivyo, kadiri muda unavyopita miradi michache zaidi itajikuta katika hali hiyo.

- Kwa hiyo, miradi iliyotoa kipaumbele cha hali ya juu kwa kuruhusu mchakato wa PTD kuanza na wakulima wabunifu wa siku za baadaye kujichagulia teknolojia kutoka kwenye orodha ndefu ya teknolojia zenye manufaa makubwa, inaweza kufikiria kupunguza orodha ili iwe fupi kidogo kuliko teknolojia ambazo tayari zimethibitika kutoa mafanikio ya haraka na yanayotambulika katika fursa zilizo nyingi.

- Utafiti unatoa ushahidi muhimu kwamba ukusanyaji, uthibitishaji, na uenezaji zaidi wa teknolojia zilizobuniwa na wakulima wabunifu vinaweza kuwa shughuli yenye thamani kwa baadhi ya watafiti na/au AZISE kujishughulisha nazo. Asasi za maendeleo zinatakiwa, kwa hiyo, kusaidia kueneza mawazo hayo duniani kote kupitia magazeti, teknolojia ya habari, mikutano ya kimataifa, kama huu wa sasa, na kozi na warsha ili kusambaza taarifa kuhusu uwezekano na manufaa yake.

## Majukumu ya Pamoja kwa Ajili ya Yatima wa Vita

Chanzo cha makala hii ni Wizara ya Kazi na Ustawi wa Jamii, serikali ya Eritrea, Asmara, Eritrea. Makala iliandikwa na Peter H. Wolff, M.D, Chuo cha Udaktari cha Harvard, Boston, Massachusetts, Marekani. Kwa maelezo zaidi wasiliana naye kwa kutumia barua pepe: [wolff\\_p@tch-harvard.edu](mailto:wolff_p@tch-harvard.edu).

**Tini za A MA Na. 50**  
**Novemba 2002**

Kabla ya mgogoro wa miaka thelathini kati ya Ethiopia na Eritrea, dhana ya “yatima” kama inavyofafanuliwa katika jamii za magharibi ilikuwa kwa kweli haijulikani. Ila walikuwepo watoto waliokuwa wametelekezwa kwa sababu mbalimbali na walitunzwa na taasisi (nyumba za yatima) zilizosaidiwa na mashirika ya dini ya nje. Katika jamii ya jadi ya Eritrea, kwa ujumla lilikuwa ni jambo lililo wazi kwamba watoto waliopoteza wazazi wote wawili wangeweza kuchukuliwa na ndugu zao kiukoo; au ikiwa hakuna ndugu aliyepatikana, walichukuliwa na majirani au marafiki wa familia. Watoto waliopoteza wazazi wote wawili moja kwa moja huwa kama wanandugu katika familia mpya na walikuwa na haki zote na wajibu kama watoto wengine katika familia hiyo. Utaratibu huu unaopatikana “ngazi ya chini” wa kutunza watoto katika mahitaji ya dharura ya ulinzi ulikuwa umeenea nchini kote na hasa katika jamii za vijijini na miongoni mwa jamii za wahamaji. Kwa kuwa utaratibu ulichukuliwa kuwa jambo la kawaida, hapakuwepo na haja ya makubaliano rasmi au nyaraka za kisheria, na uasilishaji na ulezi wa kimkataba wa watoto vilikuwa dhana genji.

Ikiwa ni matokeo ya vita vya miaka thelathini, idadi ya watoto

waliopoteza wazazi wote iliongezeka kwa kiwango kikubwa kimahesabu. Wakati huohuo, mfumo wa kijamii wa jadi ulikuwa umevurugika kwa kiasi kikubwa. Matokeo yake ni kwamba desturi asilia za kutunza watoto wasio na wazazi zilikuwa hazifanyi tena kazi, na Utawala wa Eritrea ilibidi uandae utaratibu maalumu wa kuwatunza kwa pamoja kwa muda wote vita ilikuwa inaendelea. Mara baada ya uhuru, uchunguzi wa kitaifa ulioendesha na mamlaka ya mambo ya Kijamii ya serikali mpya ya Eritrea ulibainisha kwamba jumla ya watoto 14,000 wenye umri chini ya miaka kumi na sita walikuwa wamepoteza wazazi wote wawili kwa sababu ya vita; na kwamba zaidi ya hiyo, kiasi cha watoto wasiopungua 100,000 walikuwa wanahitaji uangalini maalumu kwa sababu wazazi wao wanaoendelea kuishi hawakuwa na uwezo tena wa kuwapa watoto wao mahitaji ya msingi ya chakula, malazi na fursa za elimu. Kwa nia ya kusaidia, AZISE kutoka nje na asasi za kanisa zilianza kujenga au kukarabati na kupanua nyumba za yatima katika maeneo ya watu wengi, na kufanya juhudi za pamoja za kuanzisha dhana ya kukabidhi watoto hawa kisheria kwa nchi za kigeni kama watoto wa kupanga au wa kulea kama mikakati iliyokuba-

lika kama suluhisho la kutunza watoto wasio na wazazi. Hata hivyo, wakala wa huduma za jamii nchini Eritrea yaliwahi kuwa na uzoefu mbaya na uasiliaji wa nje wakati wa vipindi vya nyuma vya kutawaliwa. Kwa hiyo, walikataa misaada yote iliyohusisha upangaji watoto au huduma ya ulezi wa kimkataba na kufanya juhudi kubwa za kufunga nyumba zote za yatima haraka kadiri iwezekanavyo. Badala yake, waliandaa mpango wa kitaifa kwa ajili ya kuokoa na kurejesha katika maisha ya kawaida watoto wasio na wazazi ambao kwa kiasi kikubwa ulijiegemeza kwenye desturi za jadi za kutunza watoto.

Sehemu kuu ya mpango huu ilikuwa ni kuunganisha tena yatima pamoja na watoto wengine wasiokuwa na kuwatunza na ndugu zao katika familia pana. Uchunguzi katika taifa zima ulitekelezwa ili kwanza kujaribu kutafuta ndugu wa kiukoo (shangazi, wajomba, mababu na wengine kama hao), na kisha kuteua wale ndugu ambao wako katika hali nzuri ya kutoa ulinzi muhimu wa kijamii na kiuchumi kwa watoto. Hata hivyo, familia zilizo nyingi, zikiwemo hata zile zilizokuwa katika hali nzuri ya kiuchumi, zilikuwa zimefukarishwa na vita vya miaka 30 kiasi kwamba suala la kupokea mtoto mmoja au zaidi kungewaongezea mzigo wa ziada usiokubalika katika maisha yao. Mradi wa kuzalisha mapato ulibuniwa na kutekelezwa ambapo kila familia yenye uwezo wa kupokea mtoto mmoja au zaidi ilipokea msaada wa kifedha kwa namna ya mali ambao ungeimarisha uwezo wao kiuchumi kwa mujibu wa njia zao za kawaida za kuendesha maisha. Kwa mfano, wakulima walipewa ng'ombe mmoja au zaidi, plau au mbuzi kadhaa. Wakazi wa mjini walipokea vitu ambavyo viliwawezesha kuanzisha maduka madogo au kuanzisha viwanda vidogo.

Mpango huu wa kuunganishwa tena katika koo kwa kutumia njia za kuimarisha kimapato una zaidi ya miaka saba sasa. Unafuatiliwa kwa uangalifu ili kuhakikisha kuwa msaada wa vitu unatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kwa kweli unatoa ulinzi

wa kijamii na kiuchumi kwa watoto pamoja na familia zilizowapokea. Kwa ufupi, mashirika ya huduma za jamii ya Eritrea yameweza kutoa mazingira mazuri ya kifamilia kwa maelfu ya watoto wasio na wazazi kwa kutegemea na baada ya mabadiliko madogo, desturi za jadi za utunzaji wa watoto ambazo zimekuwa sehemu thabiti ya Utamaduni wa jadi wa Eritrea kwa karne na karne.

Pamoja na juhudi zote kubwa na za muda mrefu za kutafuta, haikuwezekana hata hivyo, kupata koo zote za watoto wote yatima wa vita. Kwa hiyo, mpango mbadala ulitekelezwa sambamba ili kuwapa ulinzi watoto ambao haikuwezekana kuunganishwa na koo zao. Nyumba za kikundi kidogo hivi sasa zinajengwa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Zimepangiliwa ili kutoa mazingira mazuri ya kijamii na kimaumbile kwa watoto kumi na wawili wanaoishi pamoja na mama msimamizi wa nyumba wa kudumu mmoja au wawili. Kila inapowezekana, yatima ambao ni ndugu hupangwa kuishi katika nyumba ya kikundi moja na kikundi chochote cha watoto kumi na wawili wanaoishi katika nyumba ya vikundi kimoja huchaguliwa kwa makusudi ili wawe na umri unaotofautiana kuanzia miaka miwili hadi kumi na sita, ili baada ya muda, pamoja na mama yao mlezi, waweze kuunda familia pana yao wenyewe. Zaidi ya hayo, watoto wanapangwa katika nyumba za kikundi zilizo karibu na kijiji au miji walikotokea, ili baada ya muda waweze kuingizwa katika jamii zao. Mpango mbadala bado upo katika hatua za awali za maendeleo, lakini ufuatiliaji wa nyumba za vikundi ambazo zimekuwepo kwa muda wa miaka karibu miwili unaashiria kuwa na mafanikio katika kushughulikia mahitaji ya watoto. Kama ulivyo mpango wa kuunganishwa upya, nyumba za kikundi zina msingi wake katika desturi za jadi za utunzaji wa watoto ambamo kwamo jamii pana, badala ya familia ndogondogo, huchukua jukumu la kutunza watoto ambao hawana wazazi na wana mahitaji ya ulinzi maalumu.

# Tiba ya Jadi huko Tanga Katika Zama Hizi

Makala haya yaliandikwa na David Scheinmman

***Tini za MA 51  
Desemba 2002***

Kwa karne nyingi, waganga wa jadi wamekuwa watoaji wakuu wa huduma za afya za msingi. Siku hizi barani Afrika, hasa huko Tanga bado wana dhima muhimu kwa kuwa—mbali na majukumu yao kama watoaji wa huduma za afya za msingi—wanabeba mzigo wa kutibu wagonjwa wa VVU/UKIMWI. Huko mkoani Tanga, “Kundi la kushughulikia UKIMWI (TAWG) ambalo ni asasi isiyo ya serikali iliyo ndani ya Jengo la Hospitali ya Bombo lililo juu ya mteremko mkali kando ya bahari imekuwa ikishirikiana kwa mafanikio na waganga wa jadi tangu mwaka 1990. Hii ni hadithi ya ubia unaoleta matumaini kati ya dunia kongwe na ya kisasa katika kupambana na VVU/UKIMWI.

## **Maelezo mafupi kuhusu mitishamba**

Kwa muda wa miaka mingi mimea imetumika kama vyanzo vya dawa na ilikuwa ndiyo dawa hasa za mwanzo. Zaidi ya miaka 4,000 iliyopita, Mfalme wa himaya ya Uchina alitangaza orodha ya mitishamba ipatayo 4,000. Maandishi kuhusu mitishamba iliandaliwa miaka 1770KK. Wamisiri wa zamani waliweka hata mimea ya dawa ndani ya Piramidi ili kuwatibu mafarao wao katika mai-

sha baada ya kifo. Mafarao walio-kaushwa walihifadhiwa kwa mimea, mitishamba, viungo, na madini. Mpaka miaka 150 iliyopita, sayansi za botania na dawa zilikuwa zilezile.

Mimea ina sifa za dawa kwa sababu ya dutu inayotoa kwa ajili ya kujilinda yenyewe dhidi ya wadudu waharibifu na pathojeni. Tunachofanya ni “kukopa” tu dutu hizi ili kutibu maambukizi yetu wenyewe yatokanayo na virusi, kuvu na bakteria. Dawa nyingi huchukuliwa kutoka kwenye mizizi, magome ya mimea kwa kuwa maeneo haya ni rahisi kushambuliwa na ndiyo sehemu ya kwanza ya kinga kwa mmea dhidi ya mvamizi.

Sekunde chache baada ya shambulio, mimea huanza kuzalisha na kutoa dutu ambazo zina uwezo wa kuua au sumu dhidi ya virusi, bakteria, kuvu, wadudu wanaoshambulia—au hata mamalia. Baadhi ya mimea inaweza kuzalisha kiasi cha kemikali zinazotofautiana karibu 1,000. Kwa hiyo kinga asilia dhidi ya virusi inayozalishwa na mmea kwa ajili ya kujihami inaweza pia kutumiwa na binadamu kama kinga dhidi ya virusi.

Nchini Tanzania, waganga wa jadi wamekuwa wakitambua, wakifanyia majaribio, na kutumia dutu hizi kwa kutibia wagonjwa kwa milenia kadhaa. Kwa kushirikiana nao, tuta-

kuwa tumefanikiwa kufikia matokeo ya utafiti wa maelfu ya miaka. Haya ndiyo yanayojulikana kama maarifa asilia (MA).

Dawa za kisasa zilizo nyingi hutokana na mimea. Zaidi ya bidhaa 120 za kifamasia zinatokana na mimea, na asilimia 74 ilitumiwa mwanzo na tamaduni za asili! Uhusiano kati ya matumizi ya mganga wa jadi na matokeo mazuri ya maabara uko dhahiri. Takwimu zinaashiria waziwazi kwamba mimea iliyokusanywa na waganga hutoa miongozo thabiti zaidi katika utengenezaji wa dawa mpya kuliko uchujaji wa kubahatisha. Asilimia ishirini na tano ya dawa wanazoandikiwa wagonjwa siku hizi zinatokana na mimea. Zinazojulikana sana ni dawa iitwayo “quinine” itokanayo na mti uitwao “sinchona”, dawa iitwayo “morphine” itokanayo na mti uitwao “poppy”, dawa iitwayo “asprin” itokanayo na mti uitwao “willow”, dawa iitwayo “digitalis” itokanayo na mti uitwao “foxglove”, dawa ziiwazo “vinblastine” na “vincristine” (chaguo la kwanza la dawa za kutibu ugonjwa wa Hodgkin, Leukemia kali, limfoma mbalimbali kansa ya matiti iliyo katika hali mbaya, na sasa saratani kaposi inayohusishwa na VVU) zitokanazo na mti uitwao “ros periwinkle”—unaopatikana hapa Tanga—na sasa “cotexin” itokanayo na *Artemisia annua* kwa ajili ya kutibu malaria.

### Waganga wa jadi mkoani Tanga

Wilaya ya Tanga ina waganga wa jadi takribani 670. 337 wako katika wilaya ya Tanga mjini na 333 wapo Tanga Vijijini. Walio wengi ni Waislamu na wako katika shughuli hiyo kwa wastani wa miaka 19. Yupo mganga mmoja wa jadi kwa kila wakazi 343 wa Tanga Mjini na mganga mmoja kwa kila wakazi 146 Tanga Vijijini. Nchini Tanzania kuna daktari mmoja aliyepata mafunzo ya tiba ya kimagharibi kwa wakazi 33,000. Kwa hiyo, watu wengi zaidi hupata huduma ya afya kutoka kwa waganga wa jadi kuliko wanavyopata kwa watumishi wa afya wa kawaida. Waganga wengi wameshiriki katika Semina za TAWG.

Takwimu hizi zinawiana vizuri na data za Afrika kusini mwa Sahara. Waganga tayari wapo; wizara za afya hazihitaji kuwapanga kwa kuwa karibu vijiji vyote vina waganga wakazi na wakunga wa jadi. Hii ni hali halisi hasa katika maeneo ya vijijini ambako dawa za kisasa zinapatikana kwa kiasi kidogo kuliko mijini. Kwa hiyo, kushirikiana na waganga wa jadi kupambana na VVU/UKIMWI na kukuza afya ya umma ni jambo linaloeleweka.

Waganga wa Tanga kwa kiasi kikubwa ni waganga wa kutibu kwa mitishamba, wapiga ramli, makuhani,

wapasuaji, wakunga na wataalamu wa matatizo ya akili wa jadi. Walio wengi hutumia baadhi ya mitishamba inayopatikana katika mkoa wenye uanuwai wa kibiolojia. Safu ya Milima ya Mashariki, inayojumuisha Amani katika wilaya ya Muheza ni mojawapo ya maeneo 20 tu duniani ambayo ni maarufu kibiolojia. Eneo maarufu kibiolojia lina sifa ya kuwa na aina anuwai isiyo ya kawaida ya spishi, nyingi kati ya hizo zikiwa za asili ya pale. Amani ni ya pili kwa kuwa na kiwango cha juu cha bioanuwai barani Afrika—eneo moja huko Cameroon ndilo la kwanza.

Waganga wa jadi wana maarifa maalumu kwa ajili ya kutibu maradhi ya kimaumbile, kiutamaduni, na kisaikolojia. Waganga wanapatikana, ni wa gharama nafuu, na kwa kawaida wana uaminifu, na Tanga ina dafina ya uanuwai kibiolojia ambamo mimea inayofaa hukusanywa.

### Waganga wa jadi na madaktari kushirikiana huko Tanga

Ili malengo ya afya ya umma yaweze kutekelezwa barani Afrika, inabidi waganga wawe washiriki imara katika mfumo wa afya. Hili linaeleweka kwa kuwa kila jamii ina waganga asilia wake wenyewe. Huko Tanga, TAWG imetambuliwa kimataifa kutokana na kazi zake za ubunifu za kushirikisha waganga wa jadi, na imepokea msaada kutoka OXFAM, Benki ya Dunia, na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani.

Hivi leo Tanga, waganga wa jadi na madaktari wa kisasa na wafanyakazi wa afya wanashirikiana katika mradi wa kulisimua na kuleta matumaini unaotekelezwa na TAWG. TAWG ni Asasi Isiyokuwa ya Serikali yenye ubunifu ambayo huunganisha waganga wa jadi, madaktari na wafanyakazi wa afya, wabotania, wanasayansi-jamii, na watu waishio na VVU/UKIMWI (WAVIU). Lengo la TAWG ni kuziba pengo kati ya tiba asilia na ile ya magharibi kwa kutibu WAVIU kwa kutumia dawa asilia.

TAWG ilitokana na mikutano iliyoanzishwa na daktari Mjerumani na madaktari wenza wa Kitanzania pamoja na waganga wa jadi mwaka 1990 huko Pangani, mji wa mwambao uliopo kilomita 50 kusini mwa Tanga. Wafanyakazi wa afya waligundua kwamba wagonjwa wengi—hili ni sahihi kote kusini mwa jangwa la Sahara—walikwenda sehemu zote mbili hospitalini na kwa waganga wa jadi. Kuanzia wakati huo, waliamua kufanya mawasiliano na waganga wa kienyeji kwa matumaini ya kuanzisha mtandao wa rufaa. Walikuwa na mafanikio, na mtandao wao ndio uliogeuka kuwa TAWG.

Waganga waliitikia jitihada hizo kwa shauku. Walifurahia kuonekana kama watu makini na kuchukuliwa kama wataalamu wenza. Mazungumzo ya awali yaligeuka na kuwa mikutano ambamo washiriki walijadili jinsi ya kutibu maradhi mbalimbali, wakati gani wa kumwelekeza mgonjwa kwenda hospitalini, masuala ya afya ya umma, na namna ya kushirikiana na watumishi wa tiba ya mitishamba. Siku moja mada ilikuwa VVU/UKIMWI.

Waziri Mrisho, mganga wa jadi mwenye umri wa miaka 84, aliomba apewe wagonjwa wa VVU/UKIMWI ili awatibu. Kikundi kilikubali, na Waziri aliwatibu wagonjwa wachache waliohibitika kuwa na VVU kwa kutumia mimea mitatu ambayo bado TAWG wanaendelea kuitumia hadi leo.

Mimea mitatu ya awali—pamoja na mingine iliyoongezwa—bado inatumika kutibu aina mbalimbali za maambukizo nyemelezi yanayosababishwa kwa kawaida na VVU/UKIMWI. Waziri alikuwa mwasisi halisi. Alikuwa radhi kuwagawia wenzake maarifa yake na kwa ukarimu alikubali kutoa mimea yake ichunguzwe kisayansi na wabotania kutoka *Hebarim* (hifadhi ya mimea iliyokaushwa) ya Lushoto huko wilayani Lushoto, katika mkoa wa Tanga.

Hatimaye TAWG ilianzisha huduma za majumbani ili kutoa tiba ya mitishamba kwa wagonjwa wa VVU/UKIMWI na familia zao. Ziara za majumbani ni msingi wa shughuli za kila siku za TAWG. Shughuli hizo hujumuisha ufuatiliaji wa afya kwa ujumla, kutoa tiba asilia, na kunasihi wagonjwa na familia zao.

Mwaka 1994, TAWG ilisajiliwa rasmi kama “Tanga AIDS Working Group” (TAWG) katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

TAWG ni AISE maarufu ya VVU/UKIMWI mkoani Tanga. Wafanyakazi wake wana sifa za hali ya juu, wenye bidii ya kazi, na wenye kuwajibika kwa lengo la kuboresha hali ya maisha ya WAVIU. Wanachama wana utaalamu wa kunasihi, saikolojia, tiba, elimu, botania, utafiti, anthropolojia ya tiba na menejimenti. Kazi ya TAWG ni mfano mzuri sana wa namna matokeo mazuri yanavyoweza kufanikisha mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuunganisha utaalamu wa kienyeji, maarifa asilia, na wafanyakazi wa afya wa kisasa ili kutoa matibabu ya ufanisi ya gharama nafuu kwa ajili ya watu wanaoishi na UKIMWI.

### **Mpango wa matibabu wa TAWG**

Shughuli rasmi za TAWG ni kutibu wagonjwa hospitalini au majumbani kwa kutumia mitishamba. Katika gazeti la Nipashe la tarehe 23 Februari 2002, TAWG lilitoa taarifa

kwamba tiba yake kwa ujumla hurefusha maisha ya mgonjwa na kwamba baadhi ya wagonjwa waliokuwa katika hali mbaya walipata nafuu baada ya kutumia dawa asilia (Dkt. Samuel Mtullu, Nipashe, Februari 23, 2002). Dawa zina ufanisi zaidi, iwapo tiba itaanzishwa wakati wa hatua za awali za VVU/UKIMWI. Dawa ni za gharama ya chini, hutibu kwa ufanisi maambukizo nyemelezi, zinapatikana kwa urahisi, hutolewa kwa wagonjwa bila malipo, na zimetumiwa na waganga wa jadi wa Tanzania kwa karne nyingi. Zikitolewa katika hali sahihi na kiasi kinachotakiwa, hazina madhara.

Dawa za TAWG huongeza hamu ya chakula, husaidia wagonjwa kunenepa, husimamisha kuhara, hupunguza homa, huondoa kuvu wa kinywani, hukomesha ukurutu wa ngozi na maambukizo ya kuvu, hutibu *tutuko zosta* (mkanda wa jeshi) na huondoa vidonda. kutibu wagonjwa kunawaongezea maisha marefu, huboresha hali yao ya maisha, na hupunguza idadi ya mayatima kwa kuwa wazazi huendelea kuishi.

TAWG pia hufanya kazi kwa karibu na serikali, huendesha semina kwa ajili ya waganga wa jadi, na wana programu nzuri ya elimu na kinga dhidi ya VVU/UKIMWI.

Kwa sasa hutibu wagonjwa kiasi cha 400 kutoka Wilaya za Tanga, Pangani, na Muheza. Tangu kuanzishwa kwa TAWG mwaka 1990 imetibu karibu wagonjwa 2,000. Katika kipindi cha miezi 6 iliyopita, kiasi cha wagonjwa waliotibiwa kimeongezeka maradufu, hali inayoashiria kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa wa VVU/UKIMWI.

Ushirikiano wa TAWG na waganga wa jadi pamoja na Wizara ya Afya umejenga kisiwa kidogo cha matumaini katika mji huu wa ufukoni. Hivi sasa wagonjwa wanaishi muda mrefu zaidi, na maisha mazuri zaidi, na matokeo yake ni kwamba kuna watoto wachache ambao hivi karibuni wamekuwa yatima. Waganga wa jadi wamepeleka ujumbe kuhusu kinga na afya ya umma huko vijijini na wengi hivi sasa wanajua ni lini wanatakiwa kumshauri mgonjwa kwenda hospitalini.

Ingawa bado si tiba, mitishamba hurefusha uhai kwa kupambana na pathojeni kama zile zinazoshambulia mimea. Angalau hivi sasa wagonjwa mkoani Tanga, na Tanzania wana tiba mbadala ya gharama nafuu tofauti na dawa ghali zinazoagizwa nje.

Kwa bahati mbaya, hizi tiba mpya ambazo ni ghali mara nyingi hupoteza uwezo wake baada ya muda mfupi. Kwa hiyo, kutibu wagonjwa kwa kutumia dawa asilia kuna thamani kubwa zaidi hivi sasa kama zilivyofanya maelfu ya miaka iliyopita. Kwa kuwa na ushirikiano kati ya waganga wa jadi na madaktari kumeanzisha hatua mpya zinazonufaisha kila mtu.

---

*TAWG inakaribisha maulizo na ziara. Jionee mwenyewe au piga simu kwa maelezo zaidi: Anuani ya TAWG: Jengo la Cliff, Hospitali ya Bombo Tanga, Box 1374, Tanga.*

*Simu/Faksi: 255-27 264-2266*

*Barua pepe: tawg@tanga.neg*

*Tovuti: <http://user.tanga.net/tawg>*

*Wasiliana na: Dkt. Samuel Mtullu—Mratibu*

*Dkt. Anna Chaze—Mwenyekiti*

*Dkt. Firmina Mberesero—Mwenyekiti wa zamani na Mjumbe wa Bodi*

*Ken Down—Mshauri wa Mradi*



# Uelewa wa Kina wa Maarifa ya Jadi na Mimea ya Dawa

Makala hii imeandikwa na Hareya Fasil, Chuo Kikuu cha Oxford, Kituo cha Kimataifa cha Maendeleo, Nyumba ya Malkia Elizabeth (QEH), 21 Giles, Oxford OXI 3LA, Uingereza. Kwa taarifa zaidi, baruapepe: hareya.fasil@green.oxford.ac.uk.

**Tini za MA 52  
Januari 2003**

## Takwimu halisi zaidi ya zile asilimia 80

Huenda katika wasaa huu, mahali fulani kule katika Nyanda za Juu za Safu ya Milima ya Ethiopia, mkulima fulani amekusanya majani au mizizi ya dawa kutoka mti ulio jirani na makazi yake. Wakati huohuo, jirani yake anaandaa dawa inayoaminika kuwa 'inarudisha nguvu', inapunguza maumivu ya tumbo, inatibu mata-tizo ya ngozi au pengine inaponya matatizo ya kifua yanayomsumbua mwanae. Hiyo ndiyo hali halisi katika maeneo anuwai ya vijijini Ethiopia, nchi ambayo ina hiyo asilimia 80 ya wakazi wanaoendelea kutegemea mitishamba kwa ajili ya mahitaji yao ya msingi ya huduma za afya (Bannerman, MOH, 1985; Abebe and Hagos, 1991, IBCR, 1999).

Wakati ambapo sasa kuna utambuzi wa tafiti mbalimbali za elimu na matumizi anuwai ya maarifa asilia ya afya, imeonekana kwamba eneo hili linahitaji umoja wa wanataaluma mbalimbali tofauti na ule wa kwanza ambapo wataalamu wa mimea, wakemia asilia, wataalamu wa dawa, wataalamu wa mambo ya kale na watumishi wa idara za afya wamekuwa wakifanya tafiti kila mmoja akiwa peke yake na bila ushirikiano. Katika Ethiopia kume-kuwa na maeneo machache sana

ambapo watafiti hawa wameshiriki- kiana katika kufanya kazi zao.<sup>1</sup>

Zaidi ya hayo, maandishi mba- limbali kuhusu yanayohusu dawa zitokanazo na mimea nchini Ethio- pia, yanatawaliwa na mtazamo ule wa kuuangalia mmea mmojammoja. Mtazamo huo umetokana na ile 'ajenda ya utafiti wa mkondo mkuu' ambao ulitawaliwa na sifa za kutibu za mmea mmojammoja. Katika kuta- futa taarifa zaidi, watafiti wa dawa ya asili wa Ethiopia wamezingatia hasa vyanzo viwili. (i) Waganga waliobobea wa jadi (ii) Herufi za maandiko juu ya mitishamba ya tiba ya kidini za kale za Ethiopia (angalia k.m Adebe na Ayehu, 1993)

Kinyume chake, hakuna utafiti wowote uliojikita katika dawa asilia sawasawa nje ya ule 'wa ubobevu' ulioangalia tu matibabu asilia kwa jumla. Madhumuni ya makala haya iliyotokana na utafiti mpana ni kushirikishana baadhi ya matokeo ya utafiti wa hivi karibuni uliolenga hasa katika ujuzi wa kawaida wa dawa asilia za Ethiopia kwa mujibu wa muktadha huo.<sup>2</sup>

## Malengo na mbinu

Utafiti huu wa ugani ulilenga kuona hasa ujuzi wa dawa za kienyeji kwa watumiaji wenyewe, wanaume na

wanawake, kwenye kaya zao ambazo zina wakazi wengi zaidi katika Ethiopia. Nia hasa ya utafiti huu ni kuchangia katika fasihi zilizopo na zinazozidi kukua zinazohusu ujuzi na taaluma ya kienyeji ya dawa za asili na mchango wake katika maendeleo. Zaidi ya hilo, kuna ile imani kwamba afya ndio mhimili wa mchakato wa maendeleo, yaani kwa maneno mengine, afya ni mwanzo na mwisho wa maendeleo.

Utafiti ugani ulifanyika kwa kuzishirikisha jamii za Bahir Dur Zuria katika wilaya ya Gojam (ambayo sasa ni sehemu ya mkoa wa Amhara) ambayo iko Nyanda za Juu Kaskazini Magharibi ya nchi. Utafiti huu ulitumia zana mchanganyiko za utafiti. Masuala ya kijinsia yalizingatiwa na yalipewa kipaumbele kwa vile ilitarajiwa kwamba yatajitokeza katika mambo ya ujuzi wa matibabu asilia na ugawaji wake kwa jumla. Baadhi ya mbinu zilizotumika kukusanya taarifa ni pamoja na:

- Utafiti wa kaya (ndio uliokuwa kiini hasa cha utafiti);
- Historia za kusimuliwa (mazungumzo na wazee mashuhuri);
- Mijadala na vikundi vya akinamama katika vituo vya afya;
- Uchunguzi wa kina maeneo ya sokoni;
- Madodoso yaliyoandaliwa kwa wanafunzi wa vidato vya juu; na
- Mahojiano na matabibu wa kisasa na wa jadi.

#### Tathmini ya awali ya data

Uchambuzi wa kina wa ubora na upana wa data bado haujakamilika lakini maoni yafuatayo yanatoa mwanga wa data hizo:

#### **Imani na undani wa maarifa asilia ya afya**

Kwa jumla, maarifa asilia kuhusu mitishamba na matumizi yake yalionekana kueleweka wazi kwa wanawake na wanaume katika jamii zote zilizotafitiwa. Ujuzi huu ni sehemu ya shughuli za kila siku na za kawaida katika jamii hizi. Huu ni ugunduzi muhimu kwa sababu unaonyesha jinsi jamii inavyojihusisha na dawa za asili.

#### **Jinsia na msukumo wa umri**

Suala la uelewa tofauti wa ujuzi wa tiba hizi asilia kulingana na jinsia na umri wa wale waliotafitiwa liliweza kung'amuliwa. Kwa mfano, watu wazima, wanawake kwa wanaume, walionekana kuwa na ujuzi mpana wa tiba hizi. Zaidi ya hayo, wanaume walionyesha kuwa na ujuzi mkubwa wa mitishamba ipatikanayo porini zaidi ya wanawake wakati wanawake walionyesha

ujuzi mkubwa wa dawa zinazotokana na magugu na mimea iliyo karibu na makazi ya watu.

#### **Vyanzo vikuu vya maarifa asilia**

'Ule uchunguzi na mazoezi ya kila mara wa kawaida' au 'kujifunza kwa kutenda' ndio mtindo mkuu unaotumika kueneza ujuzi wa matibabu asilia. Wanaume wengi walionyesha kupata ujuzi waliokuwa nao kwa njia hii. Hii iliashiria tofauti za kijinsia za kupata ujuzi huo.

#### **Vyanzo vya msingi vya mitishamba**

Katika utafiti huu, majina na matumizi ya aina 80 za mimea ya dawa na matumizi yake ilikusanywa. Mingi ya mimea hii ni aina ya magugu na majani ambavyo viko karibu na makazi ya watu au mashambani ambayo haihitaji uangalizi wowote. Ugunduzi huu ni muhimu kwa sababu unaungamkono lile wazo la awali kwamba ujuzi wa dawa asili uko zaidi katika jamii kuliko kwa waganga rasmi. Hii ilidhihirisha zaidi pale watoa habari walipokuwa wakitaja majina ya mimea hiyo na matumizi yake kwa namna isiyotofautiana toka mmoja hadi mwingine.

#### **Wajibu wa waganga wa jadi walioboea**

Kwa jumla, ilionekana kwamba waganga rasmi wa jadi hawashiki nafasi ya kwanza katika suala la matibabu kama ilivyodhaniwa hapo mwanzo hasa katika sehemu za vijijini. Magonjwa mengi hutambuliwa na kutibiwa katika ngazi ya kaya na wanakaya wenyewe. Wale waganga rasmi hufuatwa tu pale magonjwa hayo yanapotokea kuwa sugu au kuwashinda wanakaya.

#### **Ubora wa maarifa asilia**

Mtazamo wa kina kuhusu sifa mbalimbali za ujuzi wa dawa asilia kama ulivyochezwa hapo juu unaibua baadhi ya maswali, mashaka yake asilia pamoja na vifunguomacho. Haya yanahusiana na dhima tarajiwa ya maarifa ya jadi kiafya, asili ya mchakato wa kutoa mafunzo wa jadi na tabia asilia zinazotofautiana na maarifa haya.

*Wajibu wa ujuzi wa dawa asilia, changamoto na upungufu:* Neno 'changamoto' linaleta ile picha ya lile tatizo kubwa la afya katika eneo la utafiti- malaria. Hakuna mmea wowote wa kutibu malaria uliotajwa katika utafiti huu. Hii inaashiria jinsi ugonjwa wa malaria ulivyo 'mpya' katika jamii hizi na jinsi uelewa wa ugonjwa huo ulivyo mdogo. Hili la mwisho linasisitiza umuhimu wa elimu ya afya ya jamii na mipango ya kinga. Hii inaweza kufanikiwa pale elimu hiyo itakapozamishwa katika nyoyo za jamii kama yale maarifa mengine waliyo nayo ya dawa za asili.

Tatizo jingine ni uduni wa huduma za afya k.m. vyoo na maji vijijini. Jamii hizi ambazo zinategemea huduma za dawa asili zingetegemewa kuwa na mazingira safi ya mimea hiyo ya dawa zao lakini hali sivyo ilivyo. Kwa hiyo, ukosefu wa utumiaji wa vyoo na maji yasiyo safi wala salama na kuwepo maji taka vinaweza kuchukuliwa kama *sababu za kuwepo* kwa tiba nyingi za asili. Hata hivyo, inaweza kusemwa kwamba endapo huduma hizo za msingi na muhimu zingalikuwapo labda, juhudi za huduma za afya katika ngazi husika zingalikuwa na ufanisi zaidi na zenye maana zaidi zilizolenga katika kuzuia baadhi ya matatizo sugu ya kiafya katika eneo husika, *kama vile malaria*. Hivyo kasoro hizi, kwa kweli, zinaweza kuchukuliwa kama vizingiti katika kufikiwa kwa matarajio kamili ya maarifa ya wenyeji na mikabala ya kijadi katika kutimiza mahitaji ya kiafya ya eneo husika.

*Mchakato wa usambazaji wa maarifa:* Ni kwa namna gani hasa ujuzi huu unavyoenezwa toka kizazi hadi kizazi? Je, njia za asili za zamani bado zinatumiwa? Haya ni maswali muhimu yanayohitaji upekuzi na upembuzi mpana na mgumu kupata majibu. Hata hivyo kwa kuangalia jinsi watoto wanavyopata ujuzi huu ilionekana kwamba watoto wa miaka kati ya 6-7 wana ufahamu mkubwa wa mimea hii ya dawa. Waliweza kutofautisha mimea anuwai inayoota karibu na makazi ya kaya zao. Lakini je, hawa watoto wanajua kugundua ugonjwa na jinsi ya kutengeneza dawa hizi na kiasi cha kumpa mgonjwa? Au ujuzi huu umehifadhiwa hadi umri fulani? Majibu ya maswali haya yatapatikana baada ya kuchambua zaidi data zilizopatikana kwa ukamilifu.

*Tabia tofauti za utumiaji wa dawa za asili:* Jinsi mwamko na hamu ya kujua matumizi na ujuzi wa dawa za asili unavyozidi kuongezeka ndivyo ufanisi wa dawa hizi unavyozidi kubainika. Ni muhimu kuzingatia uamsho zaidi katika maeneo yale ambayo kwa jumla hayajajidhirisha kutoa mafanikio ya kutosha. Maeneo haya hasa ni kama vile katika elimu za upasuaji kama vile ukataji wa kimeo, tezi, shingo, ung'oaji meno, na hata kutahiri wanawake<sup>3</sup>—haya yote yameenea katika jamii zilizotafitiwa. Labda zaidi kuliko mambo mengine, hasa masuala tata yaliyoingizwa katika mazoea kama hayo ya kijadi, ni kwamba yanafanya utambuzi wa kijamii-kiutamaduni na uelewa mkubwa wa mazingira mahalia ambamo mambo mambo hayo yanakutikana kuwa ni lazima.

## Hitimisho

Inatumainiwa kwamba mahitimisho muhimu yatapatikana kutokana na utafiti huu unaoendelea. Kwa jumla kinachoweza kusemwa katika hatua hii, ni baadhi ya maana pana na michango inayotarajiwaya utafiti huu.

Kwanza, zaidi ya muongo au zaidi uliopita hivi, hamu na shauku za kujua jinsi dawa za asili zinavyotibu imekuwa bayana kila mahali na umiliki wake pamoja na haki za watendaji wanaohusika. Haya yanapewa msukumo na nguvu zilizo nje ya uwezo wa wadau ambazo jumua ya kimataifa inaziendesha katika mijadala yake inayohusiana na dawa za asili. Hili ni jambo ambalo wote Kaskazini na Kusini wanapaswa kulizingatia kwa makini katika vikao vyao vya kimataifa. Lakini suala hili limefanywa la kisiasa na kuondolewa mahali pake: uelewa sahihi wa dawa za asili na mchango wake katika siku zijazo katika nchi zinazoendelea kama vile Ethiopia. Inatumainiwa kuwa utafiti huu na tafiti nyingine kama hizi zitaelekeza msisitizo wa baadhi ya tafiti: kwenye ngazi ya jamii.

Pili kama utafiti huu wa jumua za vijijini za Nyanda za Juu za Kaskazini Magharibi ya Ethiopia ulivyoonyesha, ujuzi asili wa mimea ya dawa si miliki ya mfumo dume wala ya waganga wa jadi. Ni wazi kwamba dawa nyingi za jadi hutengenezwa na wanajamii wa kawaida katika kaya. Hii inaonyesha kwa nini ile asilimia 80 ya wakazi ambao wanategemea tiba za asili hawalazimiki kuomba ushauri kwa waganga wa jadi. Ni bahati kwamba ujuzi wa dawa hizi umeenea katika jamii na ni muhimu hili likazingatiwa na wale wanaowajibika na elimu ya afya ya jamii na wafanyakazi wa afya kwa ujumla na wenzao wa mali asili.

Mwisho, imeonekana dhahiri kwamba juhudi za utafiti na maendeleo zinapaswa pia kutambua na kushughulikia changamoto na vitisho vinavyokabiliwa na mifumo ya maarifa ya jadi ya afya *kwa ujumla*. Shabaha ni kuimarisha na kuboresha msingi mpana wa maarifa haya kwa manufaa ya watu walio wengi wa nchi zinazoendelea ambao kwa karne nyingi walitegemea dawa hizo na wataendelea kufanya hivyo kwa siku zijazo.

## Marejeo

- Abebe, D. and Hagos (1991). "Plants as a primary source of drugs in traditional health practices of Ethiopia" In *Plant Genetic Resources of Ethiopia*. J.M.M.Engels J.G. Hawkes and M.Worede.(eds) Cambridge University Press, Cambridge: 1001-113.
- Adebe, D. and Ayehu (1993). *Medicinal Plants and Enigmatic Health Practices in Northern Ethiopia*. World Health Organisation, Ethiopian Ministry of Health (Project No. AF/ETH/TRM.001 RB) and the United Nations Development Programme.
- Bannerman, R.H. (1983). *Traditional Medicine and Health Care Coverage*. WHO, Geneva
- MOH(1985). *Ministry of Health Care Review*. Ministry of Health, Addis Ababa.
- IBCR (1999). Biodiversity Conservation and Sustainable Use of Medicinal Plants: Project Proposal. Addis Ababa, Institute of Biodiversity Conservation and Research (IBCR) Addis Ababa.

- 1 Suala la pekee ni muundo unaotia moyo wa mkusanyiko wa wanafani wa taaluma nyingi katika jumuiia nzima uliochukuliwa na mradi wa taifa wa R& D unaodhaminiwa na Benki ya Dunia uliozinduliwa hivi karibuni kuhusu uhifadhi/uendeleu wa matumizi ya mitishamba inayotumiwa kwa ajili ya huduma za afya kwa binadamu na mifugo. (Tazama pia Tini za MA 35).
- 2 Utafiti bado unaendelea (hatua ya mwisho) katika kutimiliza kwa kiasi shahada ya udaktari wa falsafa (PhD) katika Masomo ya Maendeleo katika Chuo Kikuu cha Oxford, Oxford Uingereza.
- 3 Sambamba na Tini za MA 41: Eritrea; *Kufutilia mbali vitendo viovu vya jadi*.

# Uchumi wa Maarifa Asilia ya Kiafrika

Mwandishi wa makala hii, Hilary Nwokeabia, ni mchumi katika kitengo cha Uchumi na Sera ya Mipango (ESPD) Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa (UNECA) P. O. Box 3001, Addis Ababa, Ethiopia. Simu: (251-1) 44533/517200. Ext. 35333 barua pepe: hnwokeabia@yahoo.com au Nwokeabia@UN.ORG. Tini hizi za MA ni ufupisho wa chapisho jipya la UNECA la mwandishi huyu liitwalo “Kwa nini mapinduzi ya viwanda hayakutokea Afrika: Mtazamo wa maarifa asilia.”

## ***Tini za MA 53 Februari 2003***

Maarifa asilia ya Mwafrika yanaelezwa tofauti na kwa njia za kukanganwa katika vikao mbalimbali vya kima-taifa na katika maandishi ya kisasa. Mara nyingi utasikia misemo ya “isiyoendelea”, “yenye thamani ndogo” na “ya ubunifu wa kale” huko katika masuala yanayohusu haki za amali za kiakili (Trade Related Aspects of Intellectual Property Rights (TRIPS)) ya shirika la Biashara Duniani. Mara nyingi utakutana na misemo “ajabu”, “ya nyuma”, “ya thamani ndogo” na “yenye miujiza” katika mazungumzo yanayohusu maarifa asilia ya Mwafrika. Mafanikio ya dawa asilia huonekana kama ni bahati tu na yasiyo na viwango vya kisayansi. Upotofu huu huchochewa zaidi na kutoelewa mazingira ambamo wanga hufanyia kazi na kule kutoona eneo hilo likikua k.m. kuona wanga wa asili wakifundisha katika vyuo vizazi vipya ujuzi wao. Na kwa bahati mbaya zaidi, hata maandishi yaliyotolewa kuhusu sekta hii hayakuzungumzia sababu za upungufu huo.

Makala hii inakusudia kutoa maelezo ya msingi ya ukosefu wa uelewa huo wa maarifa asilia ya Mwafrika. Hoja kuu inazingatia ile sheria ya mila ya Mwafrika ya utambuzi wa elimu ya jumua na isiyojali sana ujuzi binafsi. Huu ujuzi

asilia wa jamii kwa ujumla umepewa mitazamo tofauti toka kwa waanzilishi na watu binafsi katika sekta anuwai. Katika sekta ya kipato kikubwa kama ile ya tiba, waanzilishi waliweka usiri ili kuhifadhi ujuzi wao usitawanyike ovyo. Katika sekta za kipato kidogo kama zile za kilimo, waanzilishi hawakuweza kufanya lolote kuzuia ujuzi usienee. Hii ilizaa kile tunachoita mwendelezo usio na faida dhidi ya ule mwendelezo wenye faida. Katika hali hii ujuzi hubaki mdogo na kwa wachache na hakuchangia sana katika uchumi wa jamii.

Katika mtazamo huohuo, kile kinachoonekana kama kutoendelea na mnyanyapao wake ni matokeo ya ukosefu wa motisha kwa watu binafsi wabunifu unaosababishwa na ile sheria ya kimila ya kujali jumua zaidi kuliko mtu binafsi. Matabibu ya Kiafrika na wabunifu wengine wanaweza kufanya utafiti na waka-wa na ubunifu mkubwa kama wale wataalamu wenzao wa tiba za kisasa. Uungaji wa mifupa, tiba za nyoka, kuzuia shinikizo wakati wa dhoruba katika jamii, yote haya yanaonyesha uwezo mkubwa ulio katika elimu ya jadi ya Mwafrika. Mada hii inatoa hoja ya kwamba ni ule usiri uliochangia katika kasi ndogo ya maendeleo ya elimu ya tiba za jadi. Ni usiri huu uliopunguza thamani ya

shughuli zinazohusu tiba. Hata hivyo, makala haya yataeleza upungufu uliosababisha kujenga usiri huo katika kile mwandishi alichaita “Modeli ya Usiri-Motisha.”

Swali linalotarajiwa kujibiwa hapa ni kwa nini waganga wa jadi hufanya uganga wao siri kwa watu wengine. Je, usiri huu unawaongezea chochote waganga hawa? Ni ujuzi gani hasa walio nao unaohitaji usiri kiasi hicho? Yote haya huchangiaje katika pato la jumla la jamii.

Ili kujibu maswali haya mwandishi ameweka vigezo vitatu vya usiri huo wa tiba za asili: kutokuwepo motisha kwa wagunduzi na wabunifu; kutokuwepo kwa hati miliki katika sekta nzima ya utabibu katika sheria za jadi za Kiafrika; na tishio la wizi wa kibiashara unaotokana na ujio wa wanataaluma wapya. Ubunifu hautabiriki hasa katika utabibu wa asili na kilimo ambapo utafiti ni ghali na huchukua muda mrefu huku matokeo yake yakiwa hayajulikani vizuri. Katika hali hizi wabunifu na waganga hufanya kazi zao huku wakijaribu kuhifadhi siri zao zisiibwe na wafanyabiashara.

### Maelezo

Mwandishi aliita mfumo huu “Modeli ya Motisha” kwa sababu ya kuwepo au kuwepo haja ya motisha ambayo hasa ndiyo maelezo mazuri ya usiri wa tiba, mchakato wa utafiti na gharama zake na matarajio ya matokeo yake. Katika hali ya kawaida ugunduzi haufanywi na mtu mmoja. Pale wa kwanza alipokomea ndipo wa pili anapoanzia na kuendelea hadi ugunduzi unakamilika. Matokeo ya ugunduzi wowote huipa faida jamii kwa ujumla au huwapa faida watu binafsi katika jamii hiyo. Ni kwa mtazamo huu mada hii inaeleza sababu za tabibu wa jadi kupenda siri yake ya tiba isijulikane kabisa.

Katika maelezo haya, tabibu wa jadi huwekeza akili na mali katika lile analotafiti, pengine anaweza akagundua utaalumu mpya wakati akishughulikia tatizo fulani. Utaalumu huu mpya huunganisha na ule ujuzi wake wa awali na huwa amegundua kitu kipya ambacho hakutarajia. Kwa vile yeye mwenyewe hakutarajia ugunduzi huo, kwa kawaida huwa hatangazi hayo mafanikio yake kwa wenzake kwa vile ametumia muda wake na akili kuufikia.

Wakati wa utafiti au wa tiba, mgunduzi huwa hana hakika na kile kitakachojitokeza. Kwa vyovyote vile gharama huwa juu kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa matokeo ya utafiti. Kushirikishana matokeo ya ugunduzi katika jamii kungemnyang’anya mapato yatokanayo na ugunduzi, kwa kuwa unaweza kuigwa na

kunakiriwa kirahisi sio tu na waganga wengine lakini pia na wanajumuia wenzake katika utumiaji wa kitabibu wa fanya-wewe-mwenyewe.

Ni hofu wa kuibiwa-kibishara kama matokeo ya kuwa na uwazi ambalo ndio maslahi ya utafiti na kitu cha kuzingatiwa na *yule aliyeshikilia maarifa* hayo. Kwa njia hii, inawezekana kabisa kwa mgunduzi ambaye ni mgeni katika sekta hii akiwa mjanja anaweza kuuiba ule wa watangulizi wake na kuonekana ndiye tabibu mzuri zaidi huku akiwa amewekeza muda mfupi sana katika fani hiyo.

Kuhusianisha jambo hili na gharama za ugunduzi, mtu hudhani kwamba gharama/matumizi ya utafiti yanagharamiwa kwa kiwango kilicho sawa na rasilimali pamoja na nguvu kazi iliyotumiwa kwenye utafiti. Ni kiwango tu cha rasilimali na fedha ambacho kitazalisha malengo ya utafiti. Iwapo gharama na faida pia vimepimwa katika viwango vya matokeo ya mwisho, gharama za pembeni ni juu na zaidi ya uwekezaji wa mwanzo.

Pale mapato kamili yanayotarajiwa yanapopatikana kutokana na matumizi ya ugunduzi yaliyojumuishwa, mhusika hupata matokeo tofauti, ambapo faida inakotolewa wakati huo. Katika sula la wizi wa kibishara, hasara itahesabiwa kama upotevu wa rasilimali iliyowekezwa pamoja na faida iliyotarajiwa. Hasara ya pande mbili, hii ndi sababu ya kuficha dhana mpya au ugunduzi pale ambapo hakuna msaada wa kitaasisi na msaada pamoja na ulinzi mwingine wa kisheria.

Katika mazingira kama haya ugunduzi wowote “mpya” unaleta changamoto mpya kwa kipato na namna ya kuishi ya mhusika aliyepita wa ugunduzi. Katika hali hii ya kutarajia kupata hasara ndio inayosababisha hofu ya kuweka wazi ugunduzi “mpya” kwamba mgunduzi atasababisha mkanganyiko kuhusiana na ubora wa bidhaa na huduma anazotoa kuweka habari za kitaaluma bila kuzitangaza na kuziweka siri.

Pia akijua kutokuwepo kwa taasisi zozote za umma za kulinda maarifa yake ya kienyeji, mmiliki ni lazima atafute namna ya udadisi ili kuweka ukiritimba kwa maarifa hayo ndio unakuta tabano, kuvaa vinyago, kutoa makafara, na ujanja wa kutishatisha ili yasiigwe na yasiangukie katika mchakato wa wizi wa kibishara. Katika matumizi, mambo mengine hufuata katika namna ya kuyaingiza katika mfumo wa jamii. Kwa njia hii, hata wagonjwa au wateja ambao wanaruhusiwa kuingizwa katika mfumo wa maarifa hayo hawapati kujua hasa ni tendo gain au dawa ipi imesababisha kupona. Hivyo inaonekana kama mambo ya *kichawi*.

Pale ambapo hakuna kuficha maarifa uwezekano wa kwamba watumiaji wa bidhaa za kitabibu wanaweza kuziiga huongezeka na kuondosha utabibu wa fanya-kila-

kitu-mwenyewe na hivyo kuwanyima watendaji faida ya umiliki. Mtazamo huu wa kujilinda humsaidia mgunduzi au mdhibiti wa maarifa mapya kuendelea kukusanya pesa kwa sababu ya ukiritimba pamoja na kuyalinda dhidi ya “wageni” ambao wanaweza kuiba na kuendeleza sehemu yake na kufanya wazo la mwanzo liwe lililopitwa na wakati.

Hoja kubwa kwa mara nyingine ni kwamba wale wanaofanya kazi katika sekta ya dawa za jadi za Kiafrika wana rasilimali kidogo kama yeyote, na maslahi katika kuwekeza kwenye kazi yao. Katika hali ya kutokuwepo kwa ulinzi wa umma wa ugunduzi wao na mashaka yanayohusiana na ugunduzi wa ufumbuzi mpya, hawataki kuingiza ugunduzi katika umma. Lengo lao ni kwamba umma hauwezi kuiga na kufanya, na hivyo kuwanyima fedha wanayopata kwa kutoa dawa. Mchakato wa kuficha huhusisha uharibifu na kufanya uchawi unaohusiana na shughuli zao. Maelezo hayo hapo juu yamejaribiwa kwa kutumia data zilizopo. Matokeo yake kwa kiwango kikubwa yanaunga mkono hoja kuu ya modeli hii.

Katika sekta nyingine ya kipato kidogo kama vile kilimo, kile ambacho kinaonekana ni kwamba mgunduzi au mmiliki wa MA hafichi maarifa yoyote. Kwa kawaida, huwa wanakuwa wasiojali iwapo ugunduzi wao umefuchuliwa ama la (labda kwa sababu nyingi za shughuli zao zinaweza kuonekana shambani). Wanapoulizwa wanafichua kile wakijuacho lakini mara nyingi, hakuna mtu awaulizaye. Pia kwa kuwa kwa kawaida huwa hakuna fursa za kubadilishana na maarifa yao, wamiliki huyaweka kwa ajili yao wenyewe.

Hata hivyo, mwishoni matokeo ya vyote viwili “usiri” na “kutojali” bila utata huwea ni vitu hasi kuhusu ukuaji

mkubwa wa uchumi na maarifa asilia yenyewe. Pale wenye maarifa hayo wanapokufa, maarifa hayo hutoweka nayo. Hii inamaanisha kwamba kizazi kijacho itabidi kianze upya kuutafuta ugunduzi wake. Matokeo ni kile ambacho mwandishi anaita “ugunduzi unaoendelea lakini sio unaoongezeka” kama dhidi ya “ugunduzi unaoongezeka na unaoendelea.” Katika kukosekana kwa mwongezeko wa ugunduzi, maarifa hayawezi kuzalisha ukuaji mkubwa. Hitimisho kutokana na hili ni rahisi. Nchi za Kiafrika hazijaweka sera ya motisha ambayo inaweza kusaidia kufikia “ugunduzi unaoongezeka na unaoendelea” katika mfumo wa maarifa asilia. Mfumo wa sheria za kimila pia haujajisahihisha kwa ajili ya jambo hili. Hivyo, uchocheaji wa kukua kwa mfumo wa maarifa ya ndani unabaki mdogo, na hivyo kwa uongo kusaidia dhana potofu juu ya mfumo mzima wa maarifa asili kama usiobadilika. Ni mahitimisho gani mengine ambayo mtu anaweza kuyafikia? Muundo wa motisha kwa ajili ya kukuza ugunduzi wa maarifa ya ndani na maendeleo ni lazima uwekwe. Kwa kufanya hili, haiwezi kuwa ama vibaya au vizuri, ila kunashikilia uwezekano wa faida kubwa. Utafiti zaidi unaweza pia kuwa juu ya mabadiliko ya moyo juu ya maarifa asilia ya Kiafrika, kwa namna ya pekee, dawa, usimamizi wa mali asili, kilimo na utuzaji wa mifugo. Kuachwa kwa unyanyapaa unaohusika na ukosefu wa sera unaweza kukiukwa kwa kuwezesha uundaji wa umoja wa waganga wa jadi ambao ni hatua ya kwanza. Uwezekano wa ukuaji na upunguzaji umaskini na michango inayotarajiwa katika hifadhi ya maarifa kwa ajili ya utatuzi wa matatizo sugu ya kidunia, ambao unaweza kutoka hazina hii iliyofungwa, ambayo ni *kichocheo cha utendaji*.

# Matumizi ya Dawa za Jadi nchini Uganda katika Zama Zetu

Mwandishi wa taarifa hii ni Anke Weisheit, mshauri wa kujitegemea, aliyeitoa katika kuzuru Shirikisho la Waganga wa Jadi nchini Uganda 2002 akishirikiana na Male Moses, mshauri katika MA. Utafiti huu ilifadhiliwa kwa pamoja na Benki ya dunia na shirikisho la Waganga wa Jadi wa MAKO.

## ***Tini za MA 54 Machi 2003***

Matumizi ya dawa za jadi huhusisha mwambatano tata wa ujuzi wa imani na mila ili kufikia lengo la kutambua ugonjwa, kuuzuia au kuuondoa kabisa kutoka kwa mwathilika, hii huhitaji kuoanisha utatuzi wa mata-tizo ya kimwili na yale ya akili na ya kijamii wa mhusika.

Matumizi ya dawa za asili hutegemea na huendana na ujuzi asili, jamii na uzoefu wa jamii hiyo katika mazingira yake-matumizi ya dawa za asili hubadilika kufuata wakati na hali halisi.

Tiba za asili huhusisha waunga mifupa, waganga wa kawaida, wataalamu wa kutibu vichaa, wakunga wa jadi, wanaojishughulisha na imani, waleta neema na wanaoshughulikia roho za watu ambao kila mmoja hujitoa mzima katika eneo lake ili kutatua matatizo ya wateja wake kulingana na upeo wa ujuzi wake.

### **Hali ya huduma za afya**

Kiwango cha uhusiano wa waganga wa jadi na wale madaktari waliosomea utabibu wa kisasa Uganda kama ilivyo katika nchi nyingine za Afrika kinaonyesha tofauti kubwa sana.

Nchini Uganda kuna mganga mmoja wa jadi kwa watu 290 ukilinganisha na daktari mmoja wa kisasa kwa watu 10,000 mijini na

watu 50,000 vijijini. Wakazi wengi wa Uganda wana uwezo wa kutafuta ushauri na tiba kwa waganga wa jadi kuliko walio na uwezo wa kukutana na daktari. Waganga wa jadi wana-kubalika katika jamii na kimila na kwa vile wao pia ni wanajamii hizo wanaonekana kama ndio hasa waganga. Zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wa Uganda wanategemea waganga wa jadi kwa vile ndio wanaofikika na wanaokubalika na jamii kuliko madaktari (Bannerman, et al. 1993)

Nchi ya Uganda inaagiza dawa nyingi kutoka nje na mara nyingi hukabiliwa na upungufu mkubwa. Jambo hili linaashiria hajaj ya watendaji wa dawa za jadi kuhitaji mimea ya dawa na ukweli kwamba watu walio wengi vijijini na mijini kadhalika, hutegemea sana miti-shamba kwa ajili ya kutibu magonjwa mbalimbali (Esegu, J. F. O 2002).

### **Umuhimu wa dawa za asili kiuchumi**

Ukosefu na gharama ya dawa za kisasa hufanya wakazi kwenda kwa waganga wa jadi. Hii pia hutaka hifadhi na uoteshaji wa mimea ya dawa za asili.

Huu uoteshaji unahitaji kuwekewa mikakati kwa vile utawahakikishia



wakazi kuwepo kwa zile dawa adimu nchini kwa kutumia ujuzi na utamaduni wao wenyewe. Kwa njia hii huduma za afya zitaachana na hali ya kuwa tegemezi kwa tiba za kisasa ambazo wengi hawawezi kuzimudu. Mikakati hii inawezekana kwa ushirikiano na taasisi zoefu katika nyanja hizo kama “Entebe Botanical Gardens of the National Agriculture Research Organisation” na “National Chemotherapeutics Research Laboratory”.

### Juhudi za serikali kuendeleza tiba za jadi

*Tume ya marekebisho ya sheria ya Uganda* hivi sasa inatunga sheria ya kutambua, kulinda na kueneza matumizi ya tiba za jadi (Kakooza, J.M.N. 2002). Hii itawezesha taasisi za kitaifa na kimataifa kuendeleza na kuweka katika mipango yao ya maendeleo tiba za jadi.

*Asasi ya Utafiti wa Kilimo ya Taifa* hivi sasa inaziingiza sekta za chakula, manukato, dawa, vipodozi na vinyago katika kitengo chake cha biashara ili watu wengi zaidi waweze kufaidika.

*Mikakati na Sera za Wizara ya Afya* pia inatunga sheria ya kuziweka dawa za jadi katika sekta yake ya huduma za msingi.

*Baraza la Taifa la Sayansi na Teknolojia la Uganda* linatekeleza mradi wa ujuzi asilia na uendelezaji wa taasisi.

*Maabara ya Taifa ya Utafiti wa Tiba za Kikemikali* ndiyo maabara kuu ya utafiti iliyowekwa na serikali na inafadhiliwa kimataifa—baadhi ya mambo iliyofanya ni haya:

- Uchunguzi wa jumla wa dawa za jadi
- Kupima sumu zilizomo
- Kuanzisha na kutunza kitengo cha dawa za asili
- Kuweka viwango kwa dawa zinazozalishwa

### Asasi zisizo za serikali zinazoendeleza tiba za jadi

*Prometra ya Uganda* ni tawi la Prometra ya Kimataifa, shirika linaloshughulikia kuendeleza dawa za asili kwa ajili ya kupata afya bora ya jamii zisizoweza kufikia au kumudu dawa za kisasa kwa kushirikiana na sekta ya afya. Makao yake makuu yako Kawempe-Kampala mji mkuu wa Uganda. Nembo yake ni chungu chenye matundu ambayo yanatarajiwa kuzibwa na juhudi za taaluma nyingine. Madhumuni yake kwa kifupi ni:

- Kupata na kusambaza ujuzi asilia ili uenee na kutumika katika sehemu kubwa zaidi
- Kuhamasisha utumiaji wa dawa za jadi vijijini na mijini

- Kutambua na kupiga vita mila potofu zinazohusiana na tiba za jadi kwa kutumia programu za kielimu, kuanzisha vituo vya utamaduni na maeneo maalumu ya kutolea tiba
- Kuunganisha wataalamu wa tiba za jadi na matibabu wengine ili kuongeza ubadilishanaji wa habari zinazohusu tiba za jadi

- Kuanzisha na kuhamasisha programu za jamii zinazohusu matumizi bora ya mazingira, hifadhi, na utunzaji wa jamii zote za mimea yenye thamani ya dawa.

*THETA—Waganga wa Jadi na wa Kisasa Pamoja Dhidi ya UKIMWI* na magonjwa mengine, ni shirika la afya la Uganda ambamo waganga wa jadi na wa kisasa hufanya kazi pamoja. Baadhi ya shughuli zake ni pamoja na:-

- Kutoa mafunzo kwa waganga wa jadi yanayohusiana na magonjwa ya kuambukiza kwa ngono ikiwa ni pamoja na VVU/Ukimwi

- Kutoa mafunzo ya njia bora za kuwahudumia waathirika wa VVU/Ukimwi

- Kubadilishana habari kwa kupitia kituo cha habari kilichoanzishwa kwa madhumuni hayo ya kujua kwa undani habari zinazohusiana na dawa asilia na VVU/Ukimwi

- Kuwa na maktaba, kuandika kijigazeti, kuanzisha mazungumzo ya kila mwezi ambapo mtaalamu ataalikwa kutoa mada kuhusu matumizi ya dawa za asili.

- Kutoa mafunzo sanifu kwa waganga wa jadi kama wawakilishi wa THETA wilayani

- Kutoa mafunzo ya usindikaji na utunzaji wa bustani za dawa za asili

*IIACM-Taasisi ya Kimataifa ya Dawa Mbadala na Kamilishi* hujishughulisha na yafuatayo:

- Utunzaji wa aina zaidi ya 10,000 za mimea ya dawa ya Uganda na nje katika bustani yake

- Kuendeleza utengenezaji wa dawa zitokanazo na mimea

- Utengenezaji na usindikaji dawa

- Kufundisha mbinu bora za kutengeneza dawa za asili hii ikiwa pamoja na mbinu za Kichina, Kihindi, matumizi ya vijiti, tiba ya muziki ya Yoga.

*MAKO Umoja wa Waganga wa Mitishamba* (Herbalist Association) inashughulikia yafuatayo:

- Kuwafundisha waganga wa jadi misingi ya kisasa ya kugundua maradhi na kumhudumia mgonjwa

- Kuandika taarifa za dawa na kuzigawa kwa waganga ili wajiweke katika hali ya usasa na kushirikiana na watafiti

- Kuwasaidia wakunga wa jadi kwa kutumia njia za kisasa kama vile Uzazi wa Mpango

- Kuziba mapengo yaliyopo kati ya tabibu za wazee na wale vijana kuhusu ujuzi wa tiba za jadi
- Kukaribisha wadau wenza wenye nia ya kuendeleza tiba za jadi
- Kila wakati kujaribu kutambua mimea ya asili ambayo ni dawa
- Kuhimiza haja ya kuotesha mimea ya asili ya dawa

Taasisi anuwai zinajihusisha na uendelezaji wa tiba za asili na kushirikiana na: mashirika ya dini, makampuni binafsi, vyombo vya habari na watu binafsi. Hata hivyo haupo mpango maalumu wa taifa wa kushughulikia masuala haya.

### Utafiti ujao

Ongezeko la uhamiaji mijini na mabadiliko katika jamii unahitaji kwenda sambamba na uendelevu wa dawa za asili kwa vile tabia, utamaduni, mazingira na hali za kiuchumi pia zimebadilika. Hii itahitaji sheria ya kuzuia uvamizi wa ujuzi asili na wa maliasili. Mpaka hapa picha inayoonekana ni kwamba Uganda ina uwezo wa kukuza ujuzi wa dawa za asili.

### Marejeo

- Bannermann, R.H. Burton J & Chien Wen-Chieh (1993). *Traditional Medicine and Health Care Coverage*, WHO, Geneva.
- Esegu, J.F.O. (2002) *Research in Medicinal Plants in Uganda*, International Presentation, Forest Resources Research Institute, Kampala Uganda.
- Kokooza, J.M.N. (2002) Personal Communication 12.07.2002 Uganda Law Reform Commission, P. O. Box 12149, Kampala Uganda.

*Kwa habari zaidi wasiliana na: Anke Weisheit, Springstiller Str. 41, D-98547 Viernau, Germany: barua-pepe: ankeweisheit@web.de, tovuti: <http://www.herbplant.org>, au Male Moses, Mkurugenzi, MAKO Herbalist Association, P. O. 8022, Kampala, Uganda, baruapepe: makoherbal@yahoo.com*

## **Maarifa Asilia: Ubadilishanaji wa Mafunzo Afrika Mashariki na Asia ya Kusini**

*Tini hizi zimeandikwa na Siddhartha Prakash wa Benki ya Dunia. Ubadilishanaji Taaluma wa MA ulianzishwa kwa pamoja na Siddhartha Parakash, Krishna Pidatala na E.V. Shantha. Kwa maelezo zaidi wasiliana na: Sprakash@worldbank.org au Kpidatala@worldbank.org.*

### ***Tini za MA 55 Aprili 2003***

Mnamo Machi, mwaka 2002 timu ya sekta mbalimbali ya wafanyakazi 33 wa Benki ya Dunia kutoka Eneo la Afrika ilianza safari ya kitaaluma ya nchi tano za Asia Mashariki—Japan, Singapore, Malaysia, Thailand na Vietnam—ili kufahamu vizuri mchakato wa maendeleo ya Kiasia. Kusudi kubwa lililopelekea ziara ya kitaaluma katika nchi hizi lilikuwa kuwawezesha wafanyakazi kutoa huduma bora kwa wateja kwa kuwasaidia kuongeza maarifa yao ya kiutendaji wa kuelekea maendeleo, na kuongeza ujuzi wao wa tabia ya kuiga utendaji mzuri kutoka eneo moja hadi jingine.

Likiwa limetiwa moyo na mafanikio ya safari ya uchunguzi, Eneo la Afrika lilianzisha jitihada za kujenga ubia miongoni mwa maeneo ya Afrika Mashariki na Asia Kusini kwa lengo la kutafuta maarifa asilia (MA) na utendaji unaoshauriwa na Benki. Madhumuni yalikuwa ni kuongeza uzoefu wa utendaji mzuri wa MA kutoka Asia Kusini kwenda katika miradi inayoshauriwa na Benki katika Afrika Mashariki. Hili lingesaidia kukuza ubia mpya wa mazungumzo ya nchi za Kusini, ushirikiano na misaada ya kiufundi.

Kipaumbele kilikuwa ni katika maarifa asilia ambayo ni kigezo muhimu cha mtaji wa kijamii wa watu maskini, kuwasaidia katika

jitihada zao za kuboresha maisha yao, kwa mfano, wakulima wametumia samadi kuongeza rutuba katika sehemu za Asia na Afrika kwa karne nyingi, vilevile waganga wa jadi wametumia dawa za mitishamba nchini India na Tanzania kutibu magonjwa ya kawaida ya binadamu na mifugo.

Asasi nyingi za ndani, taasisi na jumuiia zina utajiri wa ujuzi wa utendaji wa MA. Hata hivyo, utendaji huu hausambazwi vilivyo kwa sababu Mashirika ya Kijamii hayana uwezo wa kuuchukua, kuuhifadhi, kuuthamini na kuutumia pamoja. Matokeo yake, MA yanatumika kidogo katika mchakato wa maendeleo, na jumuiia za ndani zinabanwa na uwezo wao wa kubadili mjadala wa vipaumbele vya kimaendeleo na kukosa mbinu za kuyafikia. Kuunganisha maarifa, Eneo la Afrika liliandaa ziara ya ubadilishanaji taaluma kati ya Afrika Mashariki na Asia Kusini.

Hatua ya kwanza ilikuwa kubainisha miradi bora huko Asia Kusini na Afrika Mashariki ambayo ama tayari imeshaendeleza vizuri MA kuendeleza maendeleo ya Jumuiia na zile ambazo hazina vigezo hivi. Kusudi lilikuwa kuoanisha jamii zinazofuata maarifa na zile zinazotumia vizuri rasilimali zao za ndani kwa kwa maendeleo.

## Shughuli zinazopendekezwa

Ubia wa kuingiliana—kimaeneo utaundwa katika awamu nne. Awamu ya kwanza itaunganisha miradi ya Afrika Mashariki na Asia Kusini. Awamu ya pili itatoa nafasi za kujifunza kwa wafanyakazi wa mradi na wabia wa asasi za kijamii kutoka katika miradi nchini India na Sri Lanka. Awamu ya tatu italenga katika kujenga uwezo wa kukamilisha MA katika shughuli za miradi na kuboresha kiwango cha nchi cha uanzishaji katika miradi ya Afrika Mashariki. Awamu ya nne itaisaidia miradi kuendeleza ubia kwa ushirikiano zaidi na mafunzo. Shughuli hizi zimeundwa katika hatua hizi nne kusisitiza umuhimu wa kuunda na kuendeleza ubia zaidi ya kufanya ziara za kimafunzo tu.

### Awamu 1: Kujenga uhusiano

**Zoezi la upimaji.** Shughuli ya kwanza kufanywa ilikuwa kubainisha watu wa mfano kutoka katika kila miradi shiriki na kuendeleza utambuzi wa pamoja juu ya kusudi la uanzishaji na wajibu wa wabia. Habari na maelekezo yaliyopo tayari juu ya uunganishaji MA na utendaji wa mpango wa mradi na utekelezaji ulichangiwa na miradi.

**Uanzishaji mazungumzo.** Mawasiliano kati ya wabia mbalimbali yalianzishwa na habari za mwanzo juu ya uanzishaji zilijadiliwa pamoja. Matumizi ya MA kwa ajili ya kubadilishana habari yalilhamasishwa. Miradi yote ambayo tayari ina mitandao itahamasishwa katika habari za baadaye zinazohusu MA na maendeleo ambayo tayari yameshafanywa katika kubainisha MA na utendaji. Kama itahitajika ukurasa wa mtandao wa pamoja kwa ubia utatengenezwa kuunganisha habari za mradi maalumu.

**Kutafuta mwezeshaji.** Kuwepo kwa mtandao mpana wa wateja na maeneo mbalimbali ya kushughulikiwa wakati wa ubadilishanaji, kulileta umuhimu wa kumchagua muwezeshaji ili kuhakikisha muundo wa mchakato wa mafunzo wakati wa ubadilishanaji. Mkurugenzi Mten-daji wa Baraza la Taifa la Sayansi na Teknolojia la Uganda (UNCST) alichaguliwa kama mwezeshaji.

**Mkutano wa video na ubadilishanaji wa habari.** Mkutano wa video uliandaliwa ukishirikisha wateja washiriki wote ambapo habari maalumu juu ya matumizi ya MA (Uchunguzi kifani) uliwasilishwa na kujadiliwa. Hii iliwapa nafasi kuelewa umuhimu wa MA na kuzungumza mawazo yao katika kile walichotegemea kukipata kutoka katika ubadilishanaji kwa kuwapa waandaaji nafasi ya kuandaa safari za mafunzo katika namna itakayotekeleza mahitaji ya wateja. Mkutano

maalumu wa video ulifanywa na mwezeshaji, ili kuzizoea shughuli zilizopangwa na kukubaliwa ziwe za mfano.

### Awamu ya II. Upatikanaji mafunzo kwa nchi za Afrika Mashariki

Mnamo Septemba 2002 kundi la wateja (wataalamu 16 wa maendeleo) kutoka Ethiopia, Kenya na Uganda, wakishirikiana na wafanyakazi 5 wa Benki walitembelea India na Sri Lanka. Washiriki walijumuisha wafanyakazi wa mradi wa makuzi ya mtoto na miradi ya dawa za mitishamba, wawakilishi wa wafanyakazi wa Serikali, Mganga wa Jadi, Mbunge na Waziri. Mafunzo ya wazi yalijumuisha (a) ziara za eneo kwenye mahali pa mradi/jumuia kujua jinsi mchakato unavyofanya kazi, (b) kujumuika na watendaji wa eneo ili kujua jinsi MA inavyochochea mazingira ya jumua na rasilimali za jamii katika maendeleo ya kiuchumi (c) kukutana na Mawaziri muhimu watatu wa nchi ya India kufahamu namna utawala bora na uongozi ulivyopelekea katika sera za maendeleo endelevu.

**Kujifunza kwa picha.** Pamoja na mijadala na wabia na safari za maeneo ya miradi huko Asia Kusini, ubadilishanaji taaluma ulijumuisha nafasi za kundi kutafakari mafunzo yao kwa kuuliza. Mkabala huu wa mafunzo, unaoanzishwa sasa katika eneo la Afrika, unajumuisha masimulizi ya picha za video kuhusu masuala ya wazi yaliyoandaliwa kutoa “hadithi”. Zaidi ya maswali matano washiriki walilhamasishwa kujikum-busha walivyojifunza umuhimu wa mafunzo kwa muktadha wa Afrika Mashariki, na yepi ya kuiga katika mambo yaliyoona yatahitajika katika Afrika Mashariki. Majibu ya maswali yalirekodiwa katika kanda za video ambazo zipo katika mtandao.

### Awamu ya III. Ujengaji uwezo na uimarishaji juhudi katika kiwango cha nchi

Washiriki kutoka Kenya, Uganda na Ethiopia walianzisha mikakati ya utekelezaji ya kuboresha uingizaji wa MA na utendaji katika miradi yao na pia kuchangia uzoefu wao wa mafunzo na wabia wengine katika nchi yao kama vile AZISE na Wizara za Afya. Shughuli hizo zitajumuisha mafunzo na misaada ya kiufundi ya uanzilishaji kwa kutumia MA kwa maendeleo na pia kuungana na wabia wengine nchini. Kila timu ya nchi lililenga katika maeneo yafuatayo ya ushirikiano wa nchi za kusini

- *Ubia na uunganishaji* (kuelekeza MA katika sera za maendeleo, kuandika na kubadilishana utendaji wa MA,

matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa maendeleo vijijini).

- *Kujenga uwezo wa kitaasisi wa kushirikiana* (utaasisishaji wa dawa za jadi, tafiti za usirikiano za dawa za mitishamba, uundaji wa sera na usimamiaji wa rasilimali)
- *Kiwango cha sera* (utunzaji wa kisheria wa maarifa ya Jadi, utumiaji wa MA kuingiza katika Pogramu za ECD).
- *Kuanzia chini* (uingizwaji wa kuwapa uwezo wanawake katika Programu zote, kuzishirikisha Jumua katika uandaaji wa miradi na utekelezaji, kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano kuunganisha Jumua na Masoko).
- *Kukuza utambuzi na usambazaji* (semina za kuchangia uzoefu wa Asia Kusini na wadau wa Taifa, Mikutano ya ndani ya Wizara kuinua MA katika kiwango cha sera, mikutano ya hadhara ya kusambaza uzoefu kwa Umma).

Ujumbe wa Afrika Mashariki uliona kuwa Asia Kusini ilikuwa imeendelea zaidi katika maeneo muhimu mengi yanayohusu maarifa asilia katika utendaji wa makuzi ya mtoto, uhifadhi wa dawa za mitishamba na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa maendeleo. Walivutiwa hasa na mikabala ya Jumla ya maendeleo ya India na Sir Lanka na walikuwa tayari kujaribu baadhi ya njia hizi katika mazingira ya Afrika. Katika kubadilishana, waliona pia kuwa Asia Kusini ingeweza kujifunza kutoka Afrika Mashariki hasa kutokana na jitihada zao za kukabiliana na maradhi ya VVU/UKIMWI. Mambo muhimu waliyojifunza na maeneo ya baadaye ya ushirikiano wa kimaendeleo yanajumuisha yafuatayo:

### **Ethiopia**

Uhifadhi na matumizi endelevu ya mradi wa mitishamba unakusudia kuanzisha msaada wa uhifadhi, utawala na utumiaji endelevu wa dawa za mitishamba kwa ajili ya matumizi ya kiafya ya watu na mifugo nchini Ethiopia. Mradi uko katika mwaka wake wa pili wa utekelezaji. Wafanyakazi wa mradi waliutembelea mradi unaofanana wa dawa za mitishamba nchini Sir Lanka ambao unakaribia kwisha. Kulikuwa na mambo mengi yaliyopatikana kutokana na ujuzi wa Wasirilanka ambayo Waethiopia wanapanga kuyaingiza katika mradi wao. Mambo hayo ni pamoja na usimamizi wa kisheria wa MA na mfumo wa uchangiaji faida, uwekaji katika maandishi ya utendaji wa MA na kubadilishana ujuzi, utaasisishaji wa dawa za Jadi, ulimaji wa dawa za Jadi. Katika mwisho huu, timu ya mradi ilikusudiwa kuwashauri IUCN Sir Lanka juu ya mradi wa dawa za mitishamba na taasisi ya bustani ya Tropiki ya India juu ya uhifadhi na mfumo wa uchangiaji faida.

### **Uganda**

Lishe na mradi wa maendeleo ya makuzi ya mtoto inakusudia kuboresha ukuaji na maendeleo ya watoto chini ya umri wa miaka mitano, katika lishe, Afya, Saikolojia ya Jamii na vipengele vya utambuzi. Mradi unakaribia kwisha na hatua ya pili inakaribia kuanza. Mambo mengi yaliyopatikana India na Sir Lanka yanapangwa kuingizwa katika mradi mpya. Haya yanajumuisha uingizaji wa MA katika sera za ECD, uingizwaji wa mikabala ya maendeleo ya makuzi ya mtoto, mafunzo kwa watunzaji na balehe katika uingizaji wa huduma za ECD na uzazi, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ajili ya ukusanyaji wa data za Jumua, maandishi na upashanaji habari kuboresha kiwango cha upataji habari kwaajili ya utoaji maamuzi na upataji masoko. Katika muktadha huu, kama ufuatiliaji wa ubadilishanaji taaluma, Waziri wa Afya ya msingi hivi karibuni aliongoza ujumbe mwingine wa Kiserikali kwenda India kupanga juu ya kuwa mwenyeji wa warsha ya mafunzo nchini Uganda juu ya dawa za jadi. Baraza la Taifa la Uganda la Sayansi na Teknolojia (UNSCT) linafadhili kikundi cha wataalam wa MA kutembelea India na Sir Lanka. UNSCT pia inapanga kuendeleza mapendekezo ya MA ya ushirikiano wa nchi za Kusini na NASTEC wabia wake wa Sir Lanka.

### **Kenya**

Mradi wa maendeleo ya mtoto unakusudia kuboresha thamani na elimu ya wakazi maskini wa Kenya, lengo likiwa ni kuboresha utendaji wa Walimu wa kuinua uwezo wa Jumua. Mafundisho yaliyopatikana Asia Kusini yanayofanana na MA na teknolojia ya habari na mawasiliano yalikuwa sawa na yale yaliyotajwa katika habari ya Uganda. Mradi uko katika mwaka wake wa tatu wa utekelezaji na pia umelenga katika masuala yaliyoshughulikiwa nchini India na Sir Lanka. Haya yalijumuisha: kuipa uwezo jamii, vikundi vya kujisaidia vya wanawake, shughuli za uongezaji pato, mikopo midogo, mkabala wa sekta mbalimbali wa maendeleo na upunguzaji wa umaskini unaoshirikisha viwango vyote vya upangaji na utekelezaji wa jumua.

### **Awamu ya IV: Uendelezaji muungano kwa ajili ya ushirikiano zaidi**

Hatua ya mwisho itakuwa na shughuli ambazo zitahakikisha kuwa ushirikiano unaendelea zaidi ya ubadilishanaji na ziara za mwanzo. Shughuli mbili hufanyika katika hatua hii: (a) Miradi ya Asia Kusini na Afrika Mashariki itapata na kutumia habari za MA

ambazo tayari zipo kwao kupitia katika mtandao na kuwa sehemu ya ubia wa eneo unao jengwa kupitia katika MA na ushiriki wa watu; (b) Miradi shiriki pia itajumuisha barua za magazetini juu ya uundaji wa MA na ushiriki M&E. Ikiwa zaidi ya mradi mmoja inafanywa katika nchi, moja ya Taasisi/mradi itachaguliwa kama wakala wa mfano.

### ***Majibu ya wateja***

Katika utafiti kwa wateja, ujumbe wa Afrika Mashariki ulitoa majibu yafuatayo kuhusu ziara ya mafunzo:

- Hii ni nafasi ya kufungua taasisi za programu kwa kila mmoja.
- Mtu anaweza kuona uchaguzi na mbinu tofauti zinazoweza kutumika ili kutekeleza shughuli
- Za maendeleo. Mabadilishano ya matembezi ya kujifunza yana manufaa katika kuelekeza madhumuni ya sera na kulenga makundi yasiyo salama; na kusaidia kuelekeza upya juhudi za kutumia mbinu kamilifu kuhusu maendeleo.

- Washiriki wanapaswa kuteuliwa kutoka katika sekya na maeneo ya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanasheria, watafiti na wafanyakazi wa jamii.

- Kuna umuhimu wa kuanzisha mtandao kwa ajili ya maeneo yote mawili na pia kati ya taasisi ambazo zina programu zinazoshabihiana. Timu za nchi za Afrika ya Mashariki hazina budi kuanzisha matembezi ya mabadilishano kati yao.

- Uzoefu wa mafunzo ukishaandikwa na kusambazwa katika jamii za vijijini unaweza kuboresha jitihada za kupunguza umaskini kwa kila nchi.

# ***Kanye Ndu Bowi: Muktradha wa Falsafa wa Utatuzi wa Migogoro***

*Matini hii imeandikwa na Ben K. Fred-Mensah, Prof. Msaidizi wa Uhusiano wa Kimataifa na Mshauri katika maendeleo ya Kimataifa huko Chuo Kikuu cha Howard, Washington, DC. Barua pepe: bfred-mensah@earthlink.net*

***Tini za MA 56  
Mei 2003***

Tangu mwishoni mwa miaka ya 1980 kumekuwa na utafutaji<sup>1</sup> wa mbinu mpya za utatuzi wa migogoro ili kukabiliana na migogoro ya mara kwa mara itokeayo sehemu nyingi za Afrika. Inaweza kusemwa kuwa tatizo kubwa linalopelekea kushindwa kwa utatuzi wa migogoro katika Afrika ni kuwa mbinu zilzopo za utatuzi wa migogoro ya tawala mpya za eneo hili kwa ujumla si zile za muendelezo zilizo igwa na jamii asilia ambazo walizitumia tangu wakati wa ukoloni. Kwa maneno mengine, kikwazo kikubwa katika utatuzi wa migogoro katika Afrika ni kuwa hakuna uhusiano kati ya mbinu za tawala za sasa na zile za majimbo ya kikabila. Hivyo kufahamu mbinu za utatuzi wa migogoro Afrika kwa ujumla kutaendelea ili kuboresha ujuzi wetu na mikakati ya uzungumzaji mgogoro hii inayoendelea jimboni.

Matini hii inakusudia kufupisha matokeo ya uchunguzi uliofanywa na mwandishi katika kpindi cha baridi cha 1995 na cha joto cha 1996 miongoni mwa Wabuem wa upande wa Ghana katika mpaka wa Ghana na Togo. Kusudi la kitini hiki ni kubainisha na kujadili muktradha wa kifalsafa ambao kwao mfumo wa utatuzi wa Wabuem wa asili utafanya kazi. Matini pia inapima ubora wa kanuni kwenye utatuzi wa migogoro

ya sasa katika jimbo, hasa migogoro ihusianayo na ardhi.

Kwa kusudi la uongozi, eneo la uchunguzi linaitwa Buem-Kator,<sup>2</sup> linajumuisha nusu ya mashariki ya utawala mkubwa wa kichifu katika Wilaya ya Jasikan ya Mkoa wa Volta nchini Ghana. Kutokana na Programu za Ghana za kugawa madaraka, eneo hili ni kata, moja ya kata sita zinazounda Wilaya ya Jasikan. Watu wa asili ambao kitini hiki kimeandika habari zao wanaitwa Wabuem. Kwavile eneo kwa ujumla linakaliwa na misitu ya mvua, ambayo ni sehemu nzuri kwa kilimo cha kakao na kahawa, tangu karne iliyopita linawavutia idadi kubwa ya waku-  
lima wahamiaji.

## **Kanye Ndu Bowi**

Wabuem wanasisitiza kuwa jukumu kubwa la jamii yao ni kuendeleza amani katika mfumo wa jamii. Msingi wa kifalsafa wa mfumo wa dunia hii umewekwa katika hatua Kanye Ndu bowi, ambao tafsiri yake sisisi ni “uendelezaji wa amani ya jamii”. Kanye Ndu bowi ni falsafa pana ya maelekezo ya mazingira, ambayo yanatoa matumaini na misingi halali ya aina zote za uthibiti<sup>3</sup> wa jamii inafasiriwa katika utendaji kupitia katika uwekaji wa

kibali cha asili. Kibali cha asili katika mazingira ya Buem ni vyote chanya na hasi. Ni mikataba, iliyoenea kote, ni namna ambayo wanajumuia wotewanafanywa kufuata sheria za kawaida. Ambapo kibali chanya kinajumuisha zawadi za moyo ambazo watu hupokea wanapofanya jambo zuri, kibali hasi, ni hali ya kuadhibiwa mtu anapofanya vibaya.

Ingawa Wabuem wanasisitiza kuwa amani ya jamii ni itikadi inayoongoza katika uhusiano miongoni mwao, ambapo hayahitajiki kiutawala, watu hawafuati udikteta wa utawala usioepuka hisia kali. Migogoro ni hali ya kawaida ya maisha ya jamii ya Wabuem. Migogoro hutokea katika kiwango cha ukoo na watu wa makundi ya koo mbalimbali. Pia hutokea katika jamii miongoni mwao na pia na majirani zao wasio Wabuem. Katika kueleza hali ya migogoro, Wabuem wanatofautisha kati ya hasira (konyi), ugomvi (kador) mapigano (bekpeligiti), na vita (kekpe). Machafuko mara zote huleta kuvunjika kwa mikataba, kashfa, na uchawi na matusi. Migogoro pia husababishwa na matatizo ya kisiasa, matatizo ya ndoa, kujeruhiana, na uharibifu wa mali. Mipaka ya ardhi na haki ya kumiliki ardhi maranyingi huathiri. Hata hivyo, kutokana na kanuni za amani ya jamii, machafuko mara zote hutegemewa kumalizwa kwa kutumia mbinu bora zilizopo. Hivyo, uhalifu hasa humalizwa mara zote na jamii kwa ujumla ambayo jukumu lake ni kuwaleta maofisa wa Umma kusaidia kuirudisha jamii katika hali ya kawaida.

### **Nguzo za amani ya jamii katika Buem–Kator**

Itikadi ya Buem ya amani ya jamii inasaidiwa na kuendelezwa na hali ya kisiasa miongoni mwao watu wa mataifa ya Benyaogba Ukpikator na Lelorkalorbunu na misisitizo yao isiyokubaliwa juu ya uaminifu wa kibinafsi na kitaasisi.

#### **(i) Benyaogba Ukpikator**

Njia moja ambayo itikadi ya Kanye ndu bowi inaendeleza ni kupitia katika misisitizo imara, ambao watu huuita benyaogba okpikator. Benyaogba okpikator, kama muhimili muhimu katika itikadi ya Kanye ndu bowi, inatoa nafasi kwa pande zinazopingana katika mgogoro na kuzishauri juu ya kutojali kile kilichosababisha mgogoro kati yao, matumaini ya kutokuwepo kwa uhusiano wa kahasama ni makubwa kuliko ugomvi. Kwa maneno mengine, kwa kuhimiza Benyaogba Okpikator kama njia ya utatuzi wa matatizo, wagomvi hufanywa kuepuka hali ya kushinda au kushindwa ambayo kwa kiasi kukubwa huhusishwa na hukumu, ambayo watu

huiita batekate. Kwa asili yake benyaogba Okpikator kwa ujumla ni njia nyepesi ya amani ya kutatua matatizo. Hii ni njia nzuri kwa Jumua ambayo watu wake huishi katika namna ya ana kwa ana na kuunganiswhwa na mtandao wa jamii, uhusiano wa kidini na kiuchumi.

Waongozaji wa benyeogba okpikator kwa kawaida ni wazee wa ukoo, makasisi, na watu mashuhuri wanaojulikana kwa busara zao na ujuzi katika ofisi zao na uwezo wao wa kitaalam, na pia katika mambo yao binafsi. Watu hawa kwa kawaida wanajulikana katika jamii yao na wana uwezo wa kutatua mafarakano ambayo huonekana kuvuta usikivu. Mara nyingi hutokea kuwa watu hao mara kwa mara hukaribishwa kusuluhisha mgogoro nje ya makundi ya koo zao au jumua. Wakatii wa uchunguzi huu, mwandishi alikutana na kesi za asili hii. Mzee mmoja wa Ayoma Mpya alikuwa mara zote akitajwa kama msuluhishi hodari. Alikumbukwa hasa kwa kutatua mgogoro wa ardhi uliodumu katika maeneo mawili ya kilimo. Usuluhishi huu ulichukuliwa kuwa wa mafanikio kwa vile wakati wa mahojiano, ilishapita karibu miaka 13 tangu mgogoro uliposuluhishwa na haujatokea tena.

#### **(ii) Lelorkalorbunu**

Nguzo nyingine moja katika itikadi ya Ndu bowi ni juu ya ugomvi na misisitizo juu ya Lelorkalorbunu. Lelorkalorbunu inawakilisha dhana ya watu ya amani na haki. Wabuem wanasisitiza kuwa lengo la msingi la baraza la usuluhishi ni kufikia Lelorkalorbunu. Lelorkalorbunu kwa tafsiri ya kawaida ni makubaliano ya pamoja, si tu kama njia ya utatuzi wa matatizo, lakini pia kutoa hukumu ili kanuni ya msingi miongoni mwa Wabuem ambayo kwayo hadi pande zilizo kwenye mgongano hukubali hukumu iliyofikiwa katika baraza lolote la usuluhishi, mgogoro hauwezi kuchukuliwa kuwa umetatuliwa kama matokeo yake, utatuzi na/au adhabu (kornu) haiwezi kushauriwa. Kwa maneno mengine, mara Lelorkalorbunu inapofikiwa, ambayo humaanisha kuwa vikundi vyenye ugomvi vimekubaliana na hatua na hukumu, waongozaji wa hatua ya usuluhishi wataanza kupendekeza njia za kuboresha uhusiano ulioharibika kwa makundi yaliyokuwa na mgogoro ili kuyarudisha yaliyokuwa kuyarudisha katika hali ya zamani ya uhusiano wao. Inaaminika kuwa njia nzuri ya baraza la usuluhishi halilazimishi maamuzi kwa pande hizo bali huzipelekea kukubaliana.

#### **(iii) Hali ya kuaminiwa kwa taasisi na watumishi**

Nguzo ya tatu inayotumiwa na wenyeji wa Buem kama mbinu ya usuluhishi ni kwa walio katika mgogoro



kusisitizwa juu ya Taasisi na wadhamini. Hapa ni lazima ionekane kuwa sio kuna mgawanyo wa majukumi miongoni wanasiasa wa Buem. Maofisa walewale wa umma, machifu, makasisi na wazee wa koo ambao wako katika utawala pia hutumika kama watunga sheria na wasimamizi wa sheria.

Hata hivyo, ni tofauti na matarajio ya sasa ambapo ujazaji huo wa madaraka unaweza kupelekea udikteta, ujazaji huo wa madaraka miongoni mwa wabuem umesaidia kuweka ukweli katika siasa, uamininifu, na uwazi kwa wote katika viwango vya watumishi na kitaasisi. Kwa kutatua matatizo, maofisa wa siasa- sheria hii hukutana sio tu kwa matarajio ya mgogoro ambao suluhisho lake lilishatolewa, pia huimarisha imani watu waliyo nayo kwao. Kwa maneno mengine mafanikio ya utatuzi mzuri wa migogoro hauhakikishi tu amani ya jamii, unaimarisha pia sheria na msimamo wa siasa uliopo katika taasisi za umma na maofisa.<sup>4</sup> Wabuem mara zote husema kuwa kiongozi yeyote wa jamii ambaye hawezi kutatua mgogoro wa jamii ni *kwesia panin*—mzee asiye faa.

## Hitimisho

Jambo moja linalohusu uendeleaji wa kanuni za asili za kutatua matatizo nchini Buem—Kator ni kuwa kama masharti yaliyowekwa siku za nyuma bado yanaendana na mabadiliko ya jamii ambayo eneo husika linayaona tangu wakati wa ukoloni.<sup>5</sup> Hii ni kwavile utendaji bora wa kanuni za asili sikuza nyuma uliwezekana kwa vile walishirikishwa, na kurekebishwa, kwa kiwango cha jamii na uharakishaji wa wakati huo. Kama ilivyo katika maeneo yote ya Ghana, na hata Afrika nzima, kanuni asilia na maadili zimebadilishwa na tawala za kisasa, uanzishaji wa Mtindo mpya wa elimu wa Magharibi, dini za duniani, uongezekaji wa fedha katika uchumi na kuongezeka kwa miundo mbinu na vyombo vya mawasiliano. Wabuem ambao mwandishi anawaongelea hufikiria suala hili. Mabadiliko yameweka mabishano juu ya uongozaji na matumizi ya kanuni za asili katika kuzuia migogoro ya siku hizi.

Eneo moja ambalo kanuni za asiliza Buem zina mgogoro na zile za tawala za leo ni uamuzi juu ya haki ya ardhi, ambalo limetokea kuwa chanzo kikuu cha migogoro katika eneo. Mgogoro hu wa kanuni hutokea mara nyingi katika taifa licha ya tawala kutumia mbinu za uzuiaji wa ardhi. Kwa mfano mnamo mwaka 1972, Serikali ya Ghana ilipitisha sheria, kifungu cha 10<sup>6</sup> ambacho hasa kilisema kuwa mtu aliyemiliki ardhi moja kwa moja kwa miaka kumi na mbili au zaidi hawezi

kunyang'anywa ardhi. Sheria hii haiendani na sheria za asili za ardhi za Wabuem. Sheria za ardhi za wenyeji wa Buem haziwafungi watu juu ya muda ambao mmliki anaweza kuathirika. Hivyo, Wabuem husema kuwa umilikaji wa ardhi, hasa kwa wahamiaji (ambao mara nyingi huchukuliwa kama wageni), usijali urefu wa muda wa kukaa ardhini, sio hali inayojitosheleza kuifanya iwe mali ya mtu kuimiliki. Jambo la msingi hivyo sio vizuri kwa Serikali ya Ghana na Afrika kwa ujumla na washiriki wao wa maendeleo kutafuta namna ambazo mifumo mizuri ya utatuzi wa matatizo ya jamii za asili inaweza kushughulikiwa pamoja na tawala za kisasa ili kuleta faida kwa mifumo yote miwili.<sup>7</sup>

- 1 Neno utatuzi wa migogoro kama lilivyotumika hapa linamaanisha njia yoyote ambayo kwayo mgogoro huzuiwa, hupunguzwa au kutatuliwa.
- 2 Eneo hili ni la jamii za kilimo, Ayoma ya kale, Baglo, Odumase, Kute na Lakante.
- 3 Uongozaji jamii katika mazingira haya unamaanisha maadili, ujumuishaji wa imani na maadili, yanayaoathiri mienendo ya watu na tabia.
- 4 Maelezo zaidi kuhusu hii yanaweza kupatikana katika Marc J. swartz "Bases for political." Bases for Political Compliance among Bena Villages" Mark J Swartz, Victor W. Turner, na Artheu Tuden, wah., Political Anthropology, Aldine Publishing Company, Chicago, 1996 na kazi ya hivi karibuni ya Ben K. Fred-Mensah, "Bases of Conflict Management among the Buems of the Ghana-Togo Border Area, I.W.Zartman, mh., Traditional Cures for Modern Conflicts, Lynne Rienner Publishers, Boulder, 2000.
- 5 Swali kama hilo mwanzo liliulizwa na Hareya Fassil katika makala ya "A Qualitative Understanding of Local Traditional Knowledge and medicinal Plant," Tini za MA 52 Januari 2003, uk. 2.
- 6 Tamko la serikali ya Ghana la mwaka 1972. Tamko hili la serikali linakumbusha sheria za Kiingereza, hasa sheria ya mwaka 1983.
- 7 Jaribio hili limeshuriwa na Ben K. Fred-Mensah katika makala yake, "Capturing Ambiguities: Communal Conflict Management Alternative in Ghana, World Development, Juni, juzuu la 27, na. 6, 1999. Lazima ifahamike kuwa kwa uadilifu wa utekelezaji wa sheria yake ya mwaka 1960 na Katiba ya 1992, sheria za asili (ziitwazo za kimila) za makabila ya majimbo ya nchi zinatambuliwa kama miongoni mwa sheria za nchi. Hata hivyo, kiuhalisia, sheria za nchi zimezizidi na pia matumizi yake yako tu kwa makabila ambako zilianzia.

# Haki za Kitamaduni katika *Upekee wa Mfumo wa Sheria za Zimbabwe*

Mwandishi wa tini hii Chloe Frommer, alifanya utafiti huu chini ya Chuo Kikuu cha Mc Gill, kama mtafiti wa Jumuiya kuu ya Sayansi na Teknolojia na maendeleo ya jamii (STANDD), na kituo cha Eneo la mafunzo ya maendeleo ya (CDAS) huko Montreal, Quebec. Unaweza kuwasiliana naye kwa [Chloe@culturalrights.com](mailto:Chloe@culturalrights.com). Nakala nzima ya makala hii na orodha nzima ya kazi iliyoonyeshwa inapatikana katika [www.culturalrights.com](http://www.culturalrights.com)

## ***Tini za MA 57 Juni 2003***

Katika kipindi chote cha miongo miwili cha shughuli ya maendeleo, ripoti juu ya “mgogoro” wa jangwa, uhaba wa chakula na uchumi duni vimekuwa na ushindani dhidi ya masimulizi ya jadi yanayoonyesha kujiingiza kusio na mfano katika mazingira yao katika namna ambazo zinazuia vichocheo muhimu vya kiuchumi (Lasing 1995, Leach na Maearns 1996, Appadurai 1990).

Kwa sasa, Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) linazibainisha rasilimali za jenetiki ya mimea kama “urithi wa binadamu” (Cullet 2001) ili kueneza utunzaji wake duniani. Kama ilivyo kwa Shirika la Biashara la Dunia (WTO) na Shirika la Haki Miliki ya Taaluma (WIPO) la sheria limewezesha kampuni za bioteknolojia kuambatanisha nyanja za urithi huu miongoni mwa haki za kitaaluma (IPR) kwa njia za msingi za tasnia ya kimataifa cha uchocheaji, matokeo yake, utendaji wa jadi wa kufanana na rasilimali za kibaolojia hazikosekani kama zisizo muhimu au kujadiliwa kama vikwazo vya maendeleo. Hili laweza kuanza na ukweli kwamba uhusiano kati ya utendaji wa kiutamaduni wa nchi, rasilimali za kibaolojia, na rasilimali za taaluma hazijatumika. Mwandishi aliona tofauti za msingi zifuatazo.

*Rasilimali za kibiolojia* (mimea, madini na wanyama) ni rasilimali za asili za dawa, kilimo, kosmolojia. Uwepo wao unasaidia kusawazisha ekolojia kwa jumla na afya ya jamii katika mazingira ya nchi husika. Pia ni matabaka ya rasilimali ya Jadi, utendaji na mfumo wa maarifa ya jadi.

*Rasilimali za kiutamaduni (utendaji)*: ni urithi wa nchi (desturi na isiyo ya desturi) utendaji unaofuata mfumo wa uzalishaji wa jadi, mzunguko na uzalishaji tena wa mazingira—asili na jamii ambao unawabainisha. Wanaendelea kujihusisha na kuungana na watu wengine na mazingira ya nchi. Pia wanatoa matabaka ya rasilimali ya kitaaluma.

*Rasilimali ya Kitaaluma (mtaji)* ni zao lililoongezwa, lililoundwa na kutengenezwa kutoka katika jadi au rasilimali baolojia. Ili kupata hifadhi, rasilimali jadi au baolojia zimebadilishwa kutoka katika mazingira ya asili ya nchi na ama (a) kusafirishwa (kama fungu la habari lisilolulikana) kwenda katika mazingira mapya ili ziweze kujumlishwa “riwaya” au (b) yaliyomo ndani yake kupunguzwa, kurekebisha na kufanywa mfano mdogo wa uzalishaji mkubwa na kusambazwa pamoja na kuchukuliwa kwa matumizi ya kiuchumi.

Hivyo, wanatengeneza au kudhani kupokea haki ya mali taaluma (IPR).

Katika mazingira ya kieneo, kikanda na kitaifa inakuwa wazi kwamba hakuna mali za kitaaluma (hata inayofanana na rasilimali jenetiki ya mmea) bila ya uzalishaji wa maarifa ya kiutamaduni na kiutendaji.

Hivyo, uanzishaji bora kwa upande wa kuendeleza nchi umetoa utungaji sheria wa pekee wa taifa ili (sui generis) kuwezesha vyote, matakwa ya kimataifa na ya ndani katika upatikanaji, utunzaji, utumiaji, uchangiaji na uthamini wa kibaolojia, kiutamaduni na rasilimali taaluma zote mbili (mkutano wa Wizara wa WTO wa mjini Seattle, mwaka 2000). Umoja wa Afrika (UA) umekuwa ukijihusisha hasa na kuweka uhusiano wa pekee kati ya rasilimali ya jenetiki ya mmea na utendaji wa jadi na umefanikiwa kuwa na *Baraza la Jutunga Sheria la Afrika kwa ajili ya Uhifadhi wa Haki za Watu wa Ndani ya Jamii, Wakulima, Wafugaji na kwa ajili ya Masharti ya Upatikanaji wa Rasilimali za Kibaolojia* (mfano wa sheria za Afrika 2001) kama miongozo ya nchi wanachama katika kuendeleza Sheria za Taifa za Jenetiki. Hata hivyo, kwa vile, Sheria za Taifa za Jenetiki (kulingana na Haki ya Biashara Zinazofanana na Taaluma kifungu cha 23 (b) cha Shirika la Biashara Duniani) uchangiaji duniani pote wa vichocheo umekuwa una msaada mdogo kimataifa. Hivyo, umefanywa bila ya uhusika wa jumua za ndani ambazo zinapata, kunatunza, kutumia, kuchangia na kuthamini uthamini wa kibaolojia na rasilimali za jadi katika njia za desturi na zisizo za desturi.

### Swali la utafiti

Kwa kuwa mageuzi ya kitaasisi ni sharti la kupata uanachama wa Shirika la Biashara Duniani, sharti hilo linaleteleza mahitaji mapya katika nchi zinazoendelea kama Zimbabwe, wahuusika wa maendeleo wanaweza kusaidia kwa ufanisi maendeleo ya taifa kwa kufanya ushirikiano na lengo la taifa la kuunda sheria za Jenetiki za Sui. Hili lingefanyika vizuri kwa kuchukua elimu ya anthropolojia ya namna ya kukusanya maarifa ya awali<sup>1</sup> hali ya jamii ya mwanzo. Kwa kuzingatia data hizi, mchanganuo wa utendaji wa jadi ambao kwa pamoja huboresha na kuendeleza mfumo wa maarifa ya jadi sharti ufuatiliwe. Mwandishi alifanikiwa kufanya hivi kwa kutumia mkusanyiko mmoja tu wa maarifa ya Zimbabwe, Maarifa ya Dawa za Jadi (TDJ), kwa kuchunguza namna zinavyopatikana, kutunzwa na kuthaminiwa kwa namna zote mbili njia za desturi na

zisizo za desturi. Taratibu hizi zimesaidia mapendekezo mbalimbali ya maendeleo nchini Zimbabwe.

### Mbinu

Kwa kutambua mabadiliko ya dunia na shughuli kuu ya maendeleo, eneo la utafiti la mwandishi lilifanyiwa kazi katika sehemu tatu (1) Mji Mkuu wa Harare ambapo makundi ya Wabantu lugha tofauti kutoka Afrika chini ya Jangwa la Sahara walikutana katika namna ya kreoli kuunda mawasiliano kwa kutumia lugha ya Kiingereza. (2) kando ya eneo la mipaka miwili nchini Zimbabwe Mashariki ya vilima ambako Msumbiji imetagua, na kuelekea kaskazini kwenda katika ardhi mbichi ambayo imeenda hadi Zambia, na (3) katikati ya uwanda wa majani, *veld*, eneo la Zimbabwe ambapo desturi za jadi za Washona<sup>2</sup> bado zinaendelezwa.

Utafiti kwa ujumla na uchambuzi ulifanywa na watoa habari kuu, wasimulizi wa jadi, historia ya jadi, watazamaji wa matambiko na watumiaji wa dawa za mitishamba, masomo ya zamani ya ethnografia yaliyofanywa na wanaantropolojia, pia na mazungumzo rasmi na chama cha taifa cha waganga wa jadi. Mwandishi alizungumza na waganga wa jadi (*n'iangas*), wasaidizi wa waganga (*makumbi*), vyombo vya—mizimu (*svikiros*), wafanyabiashara ya mimea (muti), wazee, machifu na washauri wao, maofisa wa wilaya za vijijini na Wazimbabwe wakao mijini. Mahojiano yote haya yalifanywa kwa msaada wa mkalimani wa Kishona.

### Matokeo ya utafiti

Nchini Zimbabwe, matabaka ya asili ya MDJ yanachukuliwa kama uchawi<sup>3</sup> na dawa (*mishonga*) Bado matabaka haya yanajidhihirisha kama uchawi na/au dawa wakati ule tu yanaposhikiliwa na watu binafsi wote wa utendaji, matambiko, dini, ishara na kuwahi muda kunakoongozwa na familia na jamii, utamaduni, mazingira na maumbo ya mazingira (*hun'anga*).<sup>4</sup> Kwa kuongezea, katika watendaji binafsi, watu binafsi wanaounda sehemu ya jamii kubwa wanauthamini uwekaji wakfu wao hata uchawi na dawa zinapofanya vizuri (*kushanda*).

Upatikanaji mwingi wa maarifa ya wahenga ya dawa za jadi (*vadzimu hun'anga*) unanza wakati vijana na ndugu wa familia kuu za waganga walipochagua mmoja miongoni mwa wale wa chini yao kuwasaidia katika utendaji (Chavanduka 1997, Reynolds 1996). Wakati uongozi ulihitaji mikono katika utendaji wa MDJ—

kubainisha, kuelewa na kuponya wagonjwa pia ulihitaji masomo juu ya desturi kuu, ishara na jamii enezi. Jumla ya uanagenzi ulioendelezwa ni kufikiwa kwa uwezo uliodharauliwa (*mapipi*) unaolingana na uhusiano na msimbo wa jadi unaoongoza muundo mzima wa MDJ. Kwa Wazimbabwe, wazee (na pia wahenga waliokufa) ni nguzo muhimu za kuendeleza na kurithi MDJ kupitia ndoto zao mahususi (*kurotswa*) na matambiko ya kidini (*kusvikirwa*) ambao maarifa hufunuliwa kama zawadi (Frommer 2002).<sup>5</sup>

Hivyo, wakati mazoea kwa ujumla ya dawa za jadi za mimea yanafanywa na wengi ndani ya jumua ya ndani, ni watu waliochaguliwa na kufundishwa tu wanaopata uzoefu wa MDJ kujua na mambo mengine yahasuyo mimea, matambiko, ucheshi, ubashiri na kutambua ugonjwa vinafanyika katika namna zipi. Matokeo yake ni kuwa koo tofauti na jamii ya MDJ wanaendelea kiasili—kwa kuwa na baadhi ya mbinu, desturi, uwezo wa juu kuliko wengine, kulingana na tofauti ya maeneo au hali.<sup>6</sup>

### Mtaji wa ishara na jamii

Wakati ungunduzi wa MDJ ni wa muhimu ili kukabili mahitaji ya jumua za ndani ya Zimbabwe. Hatua hii hata hivyo haitekelezwi na vichocheo vya kiuchumi. Waganga wa Jadi ambao wamechaguliwa rasmi kuendeleza na kutunza maarifa ya wahenga hujiona wameaminiwa katika kazi hiyo ambayo hutakiwa kuchangia na kutibu kabla hata ya kufikiria malipo<sup>7</sup>. Pia, haitakiwi kuwa umahiri na uwezo wa kuelewa na ungunduzi na utendaji wa mtu uchangiwe ili kupata malipo kwavile waganga huthaminiwa zaidi kama mamlaka za Kijadi na pili kama mabingwa tatu kama wanasayansi. Hivyo, waganga wa Jadi hupokea malipo tafauti—yale ya uwekaji wakfu wa jumua (ishara ya rasilimali)<sup>8</sup>. Mamlaka ya juu na zawadi hupewa kwa wale waganga ambao hutekeleza vizuri MDJ (*kuchengetera*) na wanaoheshimu matambiko ya jadi, utabibu, vielelezo ishara, methali, na masimulizi ambayo hutumika kutajirisha na kufafanua uwanja mzima wa jamii.<sup>9</sup> Kwa mfano, pamoja na utabibu mishonga hutumika kiishara kushawishi kuyakubali maamuzi ya kijadi, matambiko, na shughuli yoyote ionyeshayo mambo yaliyo katika mazingira, mfano kufanikiwa katika biashara, sasa, kushinda katika hoja, uwezo wa kushawishi, au utatuzi wa migogoro. Kwa vile, utendaji huu ni eneo linalokubaliwa, zungumziwa, na kueleweka linakuwa “*kushanda*”, au imara. Hata hivyo, kwavile tu desturi hizi ni za “kiutamaduni” na zinategemea misimbo ya

kijadi haimaanishi ni kuwa si ya kisayansi au ungunduzi. Hakika, ubora mmojawapo wa desturi hizi upo katika urahisi wake katika utafutaji tatizo na utatuzi wa kila tatizo au ugonjwa peke yake. Matokeo yake, desturi makini (tofauti na njia zilizopo za utambuzi) hutoa nafasi nyingi za ungunduzi na kuendelea katika desturi hizi.

### Desturi zisizo za kimila

Kwasasa, hata hivyo, desturi zisizo za Kimila ambazo zinaendana na umbo la tabaka la MDJ (*mishonga*) pia hudharau umuhimu wa utamaduni na matambiko. Kama wafanyabiashara wa Zimbabwe, wanasayansi na muungano wa biashara wa wagangawa jadi wameanza kuonoda umbo la *mishonga* kwa ajili ya maendeleo ya uzalishaji na usambazaji, uzalishaji mzima wa desturi wa MDJ (*hun'anga*) na pia desturi nzima za kiishara za kijadi zinafishwa.

Aidha, wakati desturi hizi zisizo za kimila zinapokutanishwa na kampuni za dawa za kgeni, lengo la maendeleo ya uzalishaji hudhoofisha zawadi na urithi wa wahenga na kadhalika matarajio ya kazi na wajibu kwa jumua za ndani zinazotegemea desturi hizi (Wyneberg 1999; 2000). Kwa vile, MDJ mara zote ina uwezo wa kujumuisha pamoja, kutoweka wakfu na mambo yasiyo ya desturi yameweza kuchukua uhuru wa *mishonga* katika namna ambayo imeanza kuleta kutotumiwa kwa rasilimali za ndani, utambuzi na hali ya ulaghai.<sup>10</sup> Matokeo ya kuepuka desturi hizi utengano kati ya waganga wa jadi na jamii yao umewekwa katika namna ya kuwa uzalishaji mzima wa desturi za kijadi na uhusiano uliochochea ungunduji wa mfumo elimu dawa za jadi unafifishwa.

### Utabiri

Hata hivyo, Zimbabwe ina mabadiliko na inaendelea kitamaduni. Miaka ya hivi karibuni imeshuhudia vielelezo vya kimila vya zamani za kale (*PasiChigare*) au “Vita vya Ukombozi”<sup>11</sup> vimetumika kushawishi taasisi ya utalii. Kinadharia, desturi mpya za ndani haziwezi kuchukuliwa kama sio “utamaduni” kwa sababu tu ya kuwa hazikutokana moja kwa moja na desturi halisi. Hivyo kuudhibiti mfumo utoao desturi kama rasilimali, zote mbili desturi za mila na zisizo za mila lazima ziruhusiwe kusaidia na kulinda maarifa ya tiba za jadi kama sehemu ya sekta ya jamii.

## Hitimisho

Wakati nchi za viwanda zinaamini kuwa IPR kwa rasilimali ya taaluma inachochea ugunduzi kwa kutoa zawadi, ongezeko la thamani kwa rasilimali ya kibaolojia kwa rasilimali za utamaduni ina ishara ya mjini inayolisukuma. Mtazamo mmoja wa mzunguko wa maendeleo ya kulinda “rasilimali za jenetiki ya mimea” unatazama zaidi uhusiano kati yake na rasilimali nyingine na unakanusha kuwa rasilimali za kitamaduni ni muhimu kwa kuendeleza afya ya uzazi na uvumbuzi kwa kila aina ya rasilimali.

Matokeo ya mwandishi yanaonyesha kuwa MDJ yanapimwa, kuwekwa na kutumiwa na watu binafsi welediili kugawana kikamilifu na kupata uthamanisho kamili katika jumua inayozunguka ikipambana na dhana kutoka sehemu zilizoendelea kuwa MDJ kimsingi ni rasilimali ya pamoja. Ni muhimu kuangalia zaidi ya dhana hii ambayo inaoanishwa na utaratibu uliopanuliwa wa haki miliki za kitaaluma, hususani hili limetumika kuhalalisha utengano kati ya watu binafsi, familia na jumua kwa upande mmoja na tamaduni zao na urithi wa kibiolojia kwa upande wa pili.

Wakati rasilimali za kijenetiki za mimea zimeitwa “dhahabu ya kijani” miaka ya hivi karibuni, ukweli ni kuwa imekuwa ndiyo mlango wa rasilimali za kitamaduni wa eneo (zikiwa msingi wa desturi au mazoea yasiyo desturi ya mimea ya dawa ya wenyeji) lililozaa matumizi ya dawa yakawa na kinga miliki ya kitaaluma (Wyneberg 1999; 2000). Kwa hivyo, mazoea ya kitamaduni (desturi na yasiyo desturi) yanayohusiana na urithi wa kibiolojia yanahitaji mfumo wa kinga unaimarisha uwezo wa kuendelea kuwa na mahusiano, mifumo ya kijamii, matriki za kijamii/ishara zinazozalisha maarifa muhimu yaliyo hai katika eneo husika. Mwandishi ametoa kwa ufupi jinsi jambo hili linavyoweza kufanyika kwa kufuata Makataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Jamii, Uchumi na Haki za Kitamaduni (1966) kwa undani zaidi kwa ajili ya Zimbabwe.

- 1 Awali au haki za awali ni zinatambuliwa kwa ajili ya jumua za wenyeji katika Mfano ya Sheria ya Umoja wa Afrika (2001)
- 2 Kishona ni lugha ya Taifa la Zimbabwe kutoka urithi wa Kibantu. Umuhimu wa kufanya utafiti katika lugha ya nchi inaeleza katika ugunduzi wa dhana ambazo ni mahususi katika mila za Kibantu ambazo ni vigumu kutafsiriwa katika Kiingereza bila kuwa na wasiwasi wa ukweli usio wa kichawi e.g hirizi, uganga
- 3 Uganga kulingana na Leah (1976) ni alama ya uwezekano. Wakati sababu iliyoleta matokeo fulani haijulikana, nguvu ya athari bado ni hatari kwa waumini wake. Katika utafiti huu mwandishi pamoja ya imani kuu ushahidi wa kawaida unaweza kuvuka mipaka na matambiko na mishoga
- 4 Jadi na cosmolojia, uganga na mizimu, mangimeza na usasa vyote hivi vinaweza kuwakilisha wakati huohuo ukweli, ukweli kidogo, ukweli uliotiwa chumvi kwa Wazimbabwe wanaokinga imani, desturi na njia za watu binafsi wanaoishi vijijini, mila, mijini kisayansi ujasiliamali, utaratibu wa mizimu na uganga na jumua.
- 5 Usemi maalumu, zawadi toka mizimu (*chipo vadzimu*) inaashiria kanuni maalumu kuhusu urithi na zawadi kinyume za bidhaa. Wana Anthropolojia kama Marcel Mause, Bronislav Malinowski na Annette Weiner wote wameandika kuhusu injini na kanuni za kutoa zawadi. Uchambuzi wao unafanana kwa msisitizo wa vitu maalumu haviingii kwenye uhalali wa kiuchumi bali vimefungwa kwenye katika alama za upatikanaji wa hadhi.
- 6 Utafiti wa mwandishi umebaini kuwa “*godobori*” n’anga inasemekana kuwa ndiyo yenye nguvu sana na hivyo ndiyo yenye uwezo mkubwa wa kukamata *mishonga*. Zaidi alibainisha ruwaza zilizoashiria kuwa kuna tofauti kati ya *mishoga* ya mikoa, familia, uzaaji watoto, mazingira na uganga.
- 7 Kwa kawaida kitu cho chote kidogo au kupewa kitu baadaye kunatosha
- 8 Katika miaka ya hivi akribuni, maofisa maendeleo wameanza kutoa umuhimu wa mtaji wa ishara (Bourdieu 1977). Hata hivyo, mtaji huu unaweza kubadilishwa kwa aina fulani ya mazao, huduma au thamani au hata ufanisi palipokuwa hakuna nyenzo ya kifedha. Hadi leo haijapata sifa za kutosha katika kuwaendeleza watu binafsi, desturi hizo au jamii. Mtaji wa ishara uko wazi zaidi katika nafasi katika familia.
- 9 Hii inasaidia kujenga hadhi na mamlaka katika familia hiyo au ukoo (*dunhu*) na/au mizimu (*mutopa*)
- 10 Ninaandika kuhusu suala la kiasi cha Kiafrika (*Hypoxesis hemericallidae*) katika utafiti wangu uliyochapishwa: “*Haki ya Kitamaduni ya Maarifa ya Dawa za Jadi katika Zimbabwe*” (2002) Chuo Kikuu cha McGill.
- 11 *Chimurenga* ni vita ya pili ya ukombozi ilipiganwa kwa ajili ya uhuru wa Zimbabwe toka serikali ya ukoloni wa Waingereza.

# Mbinu za Wanawake wa Kawaida za Kujiwezesha

Masimulizi yaliyotolewa hapa ni sehemu ya utafiti wa kidaktari ulioandaliwa na Preeti Shroff-Mehta katika Chuo Kikuu cha New York huko Buffalo katika kipindi cha 2000-2002. Prof. Anil Gupta wa Jumuiya ya Utafiti na Uanzishaji wa Teknolojia Endelevu na Taasisi (SRISTI), India, [www.sristi.org](http://www.sristi.org) iliongoza utafiti huko Gujarat na Jimbo la Tamilnadu nchini India.

**Tini za MA 58  
Julai 2003**

## Muktadha wa maarifa asilia ya mwanamke mgunduzi wa tabaka la chini

Malatiben Chaudhari ni mkulima mwanamke huko Gujarat, India ambaye anapambana kuendesha maisha yake katika mazingira magumu ya kijijini katika jumuiya inayomnyima haki. Ili kukabiliana na hali hii amejenga na kuboresha uwezo asilia wa kuanzisha mradi bora na wa faida wa mifugo, na unaochangia maendeleo endelevu katika jumuiya yake na nje ya hapo. Kwa uvumbuzi wake Malatiben amefanikiwa kubadili shughuli za kiuchumi za kilimo za eneo hili la chini katika Wilaya ya Mehasana huko Gujarat. Kwa miaka mingi, amefanikiwa kutengeneza shamba lenye ufanisi na mradi wa mifugo.

Muhtasari wa masimulizi ya Malatiben Chaudhari unaowasilishwa hapa unapambanua nyanja mbili za maarifa asilia:

- Uelewa wa watu wa jumuiya kuhusu mahitaji yao muhimu na uwezo wao wa kupata masuluhisho ya pekee na endelevu ya matatizo ya msimu na ya muda mrefu.
- Uwezo wa wanawake wa tabaka la chini katika kutatua matatizo na kujenga uwezo wa ndani za jumuiya na maeneo yao.

## Masimulizi ya Malatiben Chaudhari

Mimi ni mkulima na mfugaji mwanamke. Mara zote hushawishika kufanya kitu kipya licha ya hali ngumu. Nilizaliwa katika familia ya *Prajapati* (familia ya tabaka la chini) katika jumuiya maskini ya kijijini huko Gujarat India. Nilipokuwa mtoto nilizoea kumwona mwalimu wa kijijini akitembelea Jumuiya ya *Harijan* (Dalit) kila jioni kufundisha madarasa ya elimu ya watu wazima. Baada ya muda nilipata nguvu za kumuuliza kama ningeweza kuhudhuria masomo hayo. Hili lilikuwa somo langu la kwanza katika kusoma na kuandika. Hatukuwa na vifaa vya shule wala darasa. Wote tulianzika kwa vijiti mchangani. Nilifanikiwa kusoma hadi darasa la nne kisha niliacha kwa vile shule ya masomo ya juu ilikuwa mbali sana. Katika siku hizo si wanawake wengi walioweza kuendelea na elimu zaidi ya ile ya shule ya msingi.

Mume wangu anatoka katika familia ya Chaudhari. Hadhi yake katika jamii ni ya juu kuliko ya familia yangu. Baada ya ndoa familia hii ilitupatia chumba kidogo katika nyumba yao pale kijijini. Familia ya mume wangu haikumiliki ardhi ya kilimo na haikuwa ikiingiza kipato kikubwa. Tulijaribu kuanzisha duka la vyakula lakini tulishindwa kuli-

modu. Sikuwa na furaha na nilitaka utaalumu wangu mwenyewe ambao ungenifanya niwe na furaha kwa kazi yangu. Kwa sababu ya historia ya umaskini wa wazazi wangu *prajapati* (wafinyanga vyungu) familia ya mume wangu kamwe haikunikubali kabisa na kuniona kama ninao uwezo wa kuweza kufikiri mwenyewe.

Walinichukulia kama sikuandaliwa kwa kurithi ardhi au kilimo. Nilinyanyasika, kila siku waliniambia kwa njia nyingi kwamba maarifa yangu hayakuwa na thamani na kwamba sikuwa na 'Avadat' (maarifa yanayofaa).

Nilibaki kimya kwa muda mrefu lakini niliendelea kuchunguza hali ya pale kijijini. Karibu familia zote zilikuwa zinazalisha zao la aina moja tu la biashara la Bajara (*Pennisetum glaucum*, Mtama). Ardhi duni na ukame usioisha ulizuia kilimo cha biashara chenye faida. Watu walifuga sana sana kwa ajili ya kazi za shamba. Watu walijishughulisha na kilimo na siyo ufugaji wala uzalishaji wa maziwa kama chanzo cha kipato. Nyati na ndama hawakutunzwa vizuri. Mifugo ilisongana na kuwekwa sehemu ambazo si safi. Ndama walipewa mabaki na walipata huduma duni. Ilichukua miaka 6-7 kwa nyati na ng'ombe kutoa maziwa. Wastani wa utoaji wa maziwa kwa nyati mmoja ulikuwa lita 2-3 kwa siku. Ilikuwa dhahiri kuwa watu katika ukanda huu walikuwa wanapoteza fedha nyingi katika ufugaji. Ilikuwa ni mzigo mkubwa kwa wanawake kushughulika na shughuli za kilimo, watoto, kazi za nyumbani na ufugaji kwa wakati mmoja.

Nilifikiri kuwa ingewezekana kuotesha nyasi za asili kwenye udongo duni. Kwa nini nisjaribu ufugaji ili nipate pesa kutokana na kuuza maziwa? Nilishawishika kuwa kama tutazingatia ufugaji, wanyama lazima watoe maziwa ndani ya miaka 2-3 na tungeokoa gharama na nguvu za ziada kwa miaka 4-5. Changamoto ilikuwa ni kufikia lengo: hakuna dawa za kuuza wadudu, matumizi ya mali asili, utunzaji bora wa mifugo, kustahimili kazi nzito, uzito wa kazi, kuimarisha uzalishaji wa maziwa na mapato na jamii kutambua ujuzi wangu. Hakuna yeyote aliyeniamini. Kwa hiyo ilikuwa muhimu kuonyesha mtazamo huu mpya kwa kijiji kizima.

### ***Kudarati Niyam na mkabala wa kisayansi (mantiki asilia na jatihada za hatua kwa hatua)***

Jinsi watoto wetu wanavyohitaji chakula chenye virutubisho na malezi ya kudumu, ndama pia wanahitaji matunzo ya pekee. Hivyo, mwaka 1970, niliamua kujaribu ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Nilidhamiria kuthibitisha kuwa nilikuwa na maarifa na uwezo wa kufanya kazi ngumu mwenyewe. Hakuna mtu anayempa mwanamke nafasi...ni lazima tuitafute na tuifanye.

Mwanzoni nilikopa fedha na nilinunua ndama wawili kwa (Rs) rupia 40 katika soko la ndani. Niliwatunza mchana na usiku kama watoto wangu. Nilifikiria kwa makini kuhusu mahitaji ya kila siku ya nyati na ndama, kama vile ulazima wa nyasi kavu na za kijani, matatizo ya afya na marekebisho ya nyumba, upatikanaji wa maji wa kudumu, mazingira safi, mzunguko wa mimba na mahitaji mengine ya misimu. Watu wa familia yangu na wanakijiji walinidhihaki kunikumbusha kuwa sikuwa na ujuzi na maarifa ya kustahimili ufugaji na kwamba nilikuwa punguani kutunza mifugo kama watoto wangu. Bado, nilidhamiria kufanya kazi kwa bidii na kusoma zaidi pamoja na kuwa sikupewa moyo kutoka kwenye familia yangu mwenyewe na katika jamii. Nilihitaji pesa zilizotokana na maziwa ili kutunza familia yangu.

Daima nilitaka kuelewa 'sayansi' ya menejimenti ya ufugaji na wakati huo huo kutegemea ujuzi wangu wa *Kotha Suz* (ujuzi kwa muktadha maalumu na ufahamu). *Kotha Suz* haijitegemea kama elimu ya darasani na ujuzi wa utaalumu—hata wanawake wasiosoma na maskini wanayo na wanaitumia. Mama yangu alinifundisha kuhusu utunzaji wa wanyama. Alipata mahitaji yote ya haraka pale pale nyumbani au kutoka msitu wa karibu kwa ajili ya utunzaji wa mifugo. Pia nilijifunza na bado ninaendelea kujifunza mengi kwa kuangalia mabadiliko ya elimu ya mahusiano ya viumbe na mazingira pamoja na uchumi kijijini mwangu.

Daima niliamini kuwa *Chila per chalava karata chilo padvo vadhare agatyano che* (kuanzisha mtindo kuna maana zaidi kuliko kufuata mtindo). Ninakubali kuwa ni muhimu kujifunza kutoka maarifa ya nje lakini kazi ngumu ni kuelewa matumizi ya maarifa yoyote katika muktadha wetu mahsusi. Ni muhimu pia kulenga katika mchakato wa kuanzisha jambo na kuliboresha ili kupunguza taathari kubwa kimkoa na kitaifa.

### ***Uwekaji mipango kwa mradi wenye mafanikio wa mahali: kanuni na vipaumbele vya msingi***

Vitu muhimu katika ufugaji ni pamoja na: Ujuzi wa mchakato wa kila siku wa utunzaji; ujuzi wa upatikanaji wa nyasi; kuendelea kujifunza kuhusu mabadiliko ya shughuli za ufugaji. Tangu mwanzo nimelenga katika mtindo wa kuendesha kilimo na ufugaji.

Utumiaji wa masalia ya kilimo: Niliona kuwa mabaki mengi ya bajara kavu (*Pennisetum glaucum*, Mtama) yanaachwa mashambani baada ya kuvuna. Nilijaribu kuchanganya mabaki na nyasi na kupata mlo maalumu kwa mifugo. *Hiki kilikuwa chakula chenye virutubisho vya hali ya juu vinavyotumiwa na wakulima na jamii nyingine katika kanda.* Daima mchanganyiko hutengezwa kwa ajili ya wanyama kutegemeana na afya zao,

uzito, kimo, na hali aliyonayo. Mchanganyiko maalumu wa vitu vya asili kama nyasi kavu na za kijani, masalia ya mazao, vyakula vingine vilivyopendekezwa na serikali na vingine vingi kutoka majumbani kama vile Jaggery (sukari guru) vinachanganywa kutengeneza chakula cha asili; Ninapinga kabisa matumizi ya kemikali na viini viambatano bandia katika uendeshaji wa kilimo na ufugaji. *Jumla ya uzalishaji wa maziwa kwa nyati /ngombe katika uangalizi wangu ni mara 2-3 zaidi ya wastani katika eneo letu.*

### **Utunzaji Bora**

Watu kijijini walishtuka wakati nyati wangu walipotoa jumla ya lita 17.3 za maziwa kwa siku mara ya kwanza. Kiasi hiki kilikuwa ni mara mbili ya wastani wa maziwa yanayopatikana kwa wanyama wengine kijijini. Hivi karibuni wataalamu wa uendeshaji ufugaji, wanasayansi kilimo na madaktari wa mifugo wa serikali walikuja kuona shamba langu dogo na shughuli za uboreshaji. Nyati wote wawili walishinda katika shindano la ndani kwa ufugaji na kwa ubora wa maziwa katika eneo lote. Kwa mara ya kwanza katika maisha yangu, nilishinda (Rs) rupia 25 (inakadiriwa kuwa sawa na dola za kimarekani 0.50 kwa kiwango cha sasa) na randi 200 kama zawadi katika mashindano mengine. Mwisho bidii zangu zilonekana na jitihada zangu zilitambulika kwa kila mtu. Ujuzi wangu ulikuwa na thamani. Wakati tu shughuli yangu ya ufugaji ilipoimarika na kuweza kupata msaada nilianza kulenga zaidi mahitaji mahsusi ya wanyama wangu hata kuliko uzalishaji pekee wa maziwa. Swali nililojiuliza “Kama ninahisi kunywa maji kila wakati labda na wanyama wanahisi vivyo hivyo”. Kwa hiyo niliunganisha mfumo wa kudumu wa upatikanaji wa maji ya kunywa na kukazania ufugaji wa wanyama kwa usafi madhubuti. Kwa sasa wafanyakazi watano wanawaangalia usiku na mchana. Wanyama wote wanaogeshwa mara tatu kwa siku. Ninahakikisha kuwa hawapati minyoo. Mazingira masafi huzuia minyoo na sio dawa. Mabaki ya chakula /nyasi yanatolewa kwenye zizi ili kutunza usafi madhubuti. Ndama wadogo, nyati na ngombe wanapata mchanganyiko huu wa nyasi kulingana na umri, ukubwa na uzito. Wafanyakazi wote wanahakikisha kuwa nyasi hazipatwi na unyevu. Wakulima wengine wengi hawazingatii jambo hili. Wakulima wengi wanaume humiliki wanyama kati ya 4 na 6 na wanatumia nguvu kutoka kwenye familia (zaidi wanawake) kuendesha ufugaji wao. Ni vigumu sana kwa mwanamke kutunza wanyama wengi, huku wakiwa na majukumu ya nyumbani na shambani. Ni muhimu kuwa na idadi ndogo ya mifugo ambao wanawake wanamudu katika familia.

### **Kushirikishana maarifa na elimu**

Pia niliamini kwamba wataalamu katika kitengo hiki na taasisi bingwa lazima wajaribu uzoefu uliopo na maarifa mapya. Ninahudhuria warsha za ubunifu za katika eneo letu na za kitaifa zinazohusiana na uendeshaji wa ufugaji. Daima ninashirikiana na serikali na madaktari wa mifugo kutoka nje, wanasayansi kilimo na wataalamu wengine wanaosimamia maziwa wanapotembelea eneo hili au wakati wa mkutano katika ngazi ya kijiji au warsha. Wanawake hawapaswi kuhudhuria katika mikusanyiko ya taasisi kama hizi lakini ninachukulia kama sehemu yangu ya kushiriki. Ninajaribu kuwashawishi wanawake wengine katika kijiji changu kufanya hivi lakini siyo rahisi. *Ni muhimu kwa wanawake wa vijijini kuwa na taasisi zinazohusu maarifa na mitandao ya nje.*

### **Taathari katika eneo zima**

Miaka michache iliyopita, nilisikia juu ya mchanganyiko wa chakula maalumu cha wanyama kilichosambazwa na kampuni ya utafiti ya AGRO na kiwanda cha maziwa cha Doodth Sagar ambacho ni kiwanda cha ushirika cha maziwa katika kanda ambacho hakikuwa kimezoeleka katika eneo hilo. Wanyama hawakukipenda sana na kwa hiyo wakulima hawakukinunua. Nilichanganya chakula hicho na nyasi za asili zilizokuwepo kwa namna nyingine na wanyama walianza kula chakula hiki kipya, chakula chenye virutubisho vingi. *Sasa ninaona fahari kwa sababu wakulima katika wilaya yangu wanatumia chakula kilekile kwa kutumia mbinu zangu ili kuongeza uzalishaji wa maziwa.* Ninafurahia kuanzisha mambo mapya. Wawakilishi wa makampuni hutembelea shamba langu na wanawashukuru kwa kuboresha upya mazao yao asilia.

Wakulima wengi katika eneo hili sasa wanalenga katika ufugaji ya ufugaji kwa ajili maziwa kuliko kilimo. Mwanzoni wanawake katika ukanda huu walikuwa wakiagalia shughuli yangu kwa makini na hatimaye wakajifunza. Wakulima wanaume iliwachukua muda kugundua mtindo huu mpya. Kwa sasa tunapanda mazao ya chakula tu na nyasi kwa uzalishaji wa maziwa. Wakulima na jamii nyingi katika ukanda huu wanategemea ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. *Tunaunga mkono ushirika mkubwa wa Pili wa Maziwa—Mehsana Doodh Sagar Dairy—katika kanda.*

### **Ushiriki wa wanawake wa tabaka la chini na umiliki wa mali**

Leo hii ninamiliki nyati wawili na ng'ombe kumi na tisa (Sankar Gai—mbegu ya kienyeji). Mifugo yangu inatoa wastani wa lita 10-12 za maziwa kwa kila mnyama kila siku, ambazo ni zaidi ya mara mbili ya wastani katika



kanda. Ninapata mapato mazuri na kuishi maisha ya raha. Kiwanda cha maziwa cha Mehsana Dudh Saga kijijini kinafanya shughuli zake kwa kompyuta na sasa sisi wanawake tunaweza kupima kiwango cha mafuta katika maziwa tunayozalisha na kupata bei halisi ya maziwa. Njia hii ni rahisi sana kuweka rekodi ya uzalishaji wa kila siku wa maziwa na mapato ya kila mwezi. Nimenunua ardhi kwa kipato hiki, nimeajiri wafanyakazi wanne wa kudumu, nimekarabati nyumba, nimetengeneza kisima katika shamba langu na nimempeleka kijana wangu wa kiume chuo kikuu.

Hadhi yangu katika familia na katika jamii imebadilika—sasa ninapewa heshima na ninatoa ushauri. Kamwe maisha si rahisi kwa wanawake, lakini lazima wajifunze kukazana licha ya mazingira magumu. Ninaamini kuwa ‘Mushkeli to Sanshodhanni Janamdata Che’ (Ugumu ni mama wa ugunduzi).

Wasiwasi wangu pekee ni kwamba kizazi kijacho kinatarajia matokeo ya haraka na kinasahau kuwa vipengele kama vile usafi madhubuti au upatikanaji wa kudumu wa maji ni mambo muhimu ya kufanikisha ufugaji. Vizazi vya sasa vimepata elimu ya darasani na haviheshimu ‘mabingwa wa vijiji’ au maarifa ya watu maskini. *Ni masikitiko kwamba kupata elimu ya darasani kunamaanisha kupotea kwa maarifa asilia. (Kotha Suz na Atmagyan)* Matumaini yangu ni kuwa mashirika kama SRISTI, ambayo yanatambua na kuunga mkono jitihada zetu, yatahifadhi na kuendeleza shughuli asilia.

*Simulizi na Malatiben Chaudhri, Gujarat, India.*

*Maandishi, tafsiri na mapokeo kwa MA. Mfumo wa matini na Preeti Shroff-Mehta, Washington, DC, Marekani. (prtshroff@aol.com)*

# Adzina: Mfumo Asilia wa Uendeshaji Mashtaka wa Wazee wa Mahakama katika Eneo la Mpakani mwa Togo na Ghana

Mada hii iliandikwa na Ben K. Fred-Mensah, Profesa Msaidizi wa uhusiano wa Kimataifa na mshauri katika maendeleo ya kimataifa katik Chuo cha Howard, Washington, D.C. Barua pepe: [bfred-mensah@howard.edu](mailto:bfred-mensah@howard.edu) au [bmens@earthlink.net](mailto:bmens@earthlink.net).

**Tini za MA 59  
Agosti 2003**

Katika mada ya hivi karibuni katika mlolongo huu, mwandishi alijadili taratibu asilia ambazo zinategemeza maisha ya jamii miongoni mwa Wabuem wa Buem- Kator upande wa Ghana mpakani mwa Ghana-Togo, katika eneo lililo asili ya Buem, Wilayani Jaskani ukanda wa Volta Ghana. Mada hii pia inahusu Wabuem hao hao. Katika mada hii mwandishi anaeleza mfumo wa jadi wa mahakama unaoitwa *adzina*. Lakini kabla ya kujadili asili na mchakato wa *adzina*, anajadili kwanza *bate kate*, ambalo ni baraza la hukumu na *adzina* ni sehemu yake muhimu.

## Bate kate

*Bate kate* inaweza kumaanisha hukumu na pia inaweza kumanisha suluhu. Katika mfumo wa asili wa kusimamia migogoro katika jamii ya Buem, *bate kate* ni njia ya kuhimili hali ya watu wengine tofauti na wale walio katika mgogoro ambayo inatetea pande zinazotafuta utetezi kutoka mtu wa tatu. Mfumo huu wa usimamizi, unaweza kuendeshwa na kiongozi wa ukoo au mkuu wa mji, na unakuwa na umuhimu wakati watetezi wanaposhindwa kuaminiana. Matokeoya kukosa uaminifu kunaruhusu mamlaka kutoka nje,

ambayo yanatafuta chanzo cha mgogoro na njia mbadala za kufikia usuluhishi.

Kufuatana na wazee wa Buem, Wabuem hufanya jitihada kujaribu kuepuka *bate kate* ambayo wanafikiri kuwa ushauri hukuchukua muda mrefu siyo kwao tu bali pia kwa mizimu ambayo kimila wanawasindikiza katika maongezi. Tofauti na *benyaogba ukpikator*—uliojadiliwa katika mada iliyotajwa hapo nyuma—*bate kate* ni mchakato unaoeleweka, ambao unaendelea katika hatua na kawaida unahusu uhakiki wa kina na kukusanya mashahidi na, ikiwa lazima uthibitisho. Kwa upande wa pesa, *bate kate* unaweza kuwa ni ghali. Hii ni kwa sababu faini na wakati mwingine gharama zinatozwa kwenye pande zenye hatia.

Kesi zinazopelekwa kwa *bate kate* kwa kawaida ni zile ambazo anaona zimeshindikana kutatuliwa na *benyaogba ukprkator* au zinatambulika kikatiba kuwa ni za jinai. Kesi za jinai zinahusisha zile za mauaji, uhaini na kauli za kukashifu watawala wa jadi au viongozi wa umma. Kuvunja miiko ya utawala pia ni kesi ya jinai ambayo uvumbuzi lazima utolewe na *bate kate*.

*Bate kate* imependekeza sifa kuhusu taratibu pamoja na maudhui yake. *Bate kate* inaweza kuongozwa ama katika mahakama ya kiongozi

wa ukoo au mahakama ya viongozi wa jadi wa mji kutegemea uzito wa kosa. Katika kanuni, *bate kate* inaweza kufuata hatua nyingi kabla hukumu haijatolewa. Kwa maneno mengine, upande mmoja au pande zote mbili zinaweza kueleza kutokuridhika na hukumu iliyotolewa na zinaweza kuamua kupeleka tatizo kwenye mahakama ya juu. Rufani kutoka mahakama za chini lazima zipelekwe kwenye mahakama inayofuatia kwa daraja. Kwa mfano, rufani kutoka mahakama ya kiongozi wa ukoo lazima ipelekwe mahakama ya kiongozi mkuu wa mji na rufani kutoka mahakama ya mkuu wa mji lazima ipelekwe kwa kiongozi mkuu wa eneo hilo, anayejulikana kama *akwamuhene*. *Akwamuhene* ni kiongozi mkubwa kupita wote katika mgawanyo wa Buem-Kator; hivyo moja kwa moja chifu mkuu mwakilishi katika eneo. Kama suluhu haifikiwi katika ngazi ya mahakama ya *Akwamuhene* kesi inapelekwa kwenye mahakama ya chifu mkuu katika makao makuu ya jadi.

Hata hivyo, katika utendaji hukumu nyingi zinasuluhishwa katika ngazi ya mji sana sana kwa sababu ya gharama (kwa maana ya muda na vitu) zinazotakiwa wakati kesi zinapopitia hatua nyingi kabla ya kutolewa uamuzi wa mwisho. Kuna dhana miongoni mwa Wabuem kwamba kama suluhu inaweza kufikiwa ni lazima viongozi wa ukoo au machifu wa miji na wazee wake walitatie katika ngazi ya chini kadiri inavyowezekana.

Mashauriano ndani ya *bate kate* yanaweza kuwa mchakato unaohitaji kufafanunuliwa. Pamoja na utaratibu wa kawaida kila mtuhumiwa anawasilisha kuhusu jambo lililotokea. Baada ya wote wawili kusikilizwa, majaji wanamwuliza kila mmoja maswali kulingana na yale aliyosema. Lengo ni kufikia makubaliano ya aina moja kwa kuondoa vipengele vya utata katika kauli za wapinzani. Kuna matumizi makubwa ya kutumia uthibitisho ushahidi, na udadisi mashauri ya mahakama daima yanakuwa ya wazi na kila mtu aliyehudhuria ana nafasi ya kumhoji/kumdadisi mtuhumiwa yeyote yule. Amri mahakamani inalindwa sana na lugha chafu hairuhusiwi kwani inaweza kusababisha kudharau mahakama.

### **Adzina**

Neno *adzina* kwa mujibu wa makala hii linaweza kufasiriwa kama “kujitenga ili kutafakari jambo”. *Adzina* inakuwa na baraza dogo ambamo maoni yaliyotolewa na *bate kate* yalikuwa kwa misingi ya kuhakikisha haki katika pande mbili za mgogoro au mtuhumiwa aliyeletwa mahakamani. Inasemekana *Adzina* inawapa wasimamizi wa *bate kate* nafasi ya “kushauriana na *abrewa*”. *Abrewa*

kimaandishi humaanisha bibi au mwanamke mzee ambaye anasadikiwa kuwa na hekima ya ajabu, haki ambayo haisailiwi na uwezo wa kuongoza mashauri ya *adzina*.

Kama nakala ya shtaka lililofanywa na baraza la wazee wa Buem, *Adzina* inafanya kazi hivi: kesi za aina zote zilizofikishwa kwa mkuu wa ukoo au chifu wa mji ili kufikishwa kwenye hukumu, baadhi ya washiriki wa mahakama, ambao walikuwepo katika kusikiliza kesi hizo na kufuatilia mwenendo wa kesi hizo wanachaguliwa kwa makusudi ya kwenda kwenye hukumu. Pamoja na wengine, baraza la wazee wa mahakama linaundwa na wawakilishi wa jaji kiongozi, baraza la hukumu na pande zinazobishana. Baraza jipya la wazee wa mahakama lililoteuliwa litaondoka kwenye chumba cha mahakama na kwenda kutafuta sehemu ambayo watapima na kusikiliza watu wengine wa mahakama. Hapa watakaa wenyewe mpaka wafikie hukumu. Kwa kufanya hivi, inasemekana wanashauriana na *abrewa*.

Hukumu inapofikiwa, baraza la wazee wa mahakama watarudi kwenye chumba cha mahakama na kuwasilisha matokeo kwa jaji. Kupitia kwa wazee wa baraza, *abrewa* atatuma maneno ya maonyo kwenye upande usio na hatia. Hukumu ama inakubalika na upande ulio na makosa kutozwa faini au unakataliwa na kupelekwa kwenye mahakama ya juu zaidi.

Jaji kiongozi atatoa hukumu namna hii:

*Abrewa onini, fula le temi libo emimi. Osu boda mi borsaka. Bokisi bobo mi nte. Osuni bafouo. Osi mui, siwu tsuedi otilikpi na onwa lelormi benu nkudor. Omui ni keny kenui kebo kuboryo* (Inafasirika kumaanisha kwamba “kulingana na hukumu ya Mwanamke Mzee ambayo kwayo jopo la washiriki, waikubalia, mtu fulani ameonekana ana hatia. Mwanamke Mzee ametuma ujumbe wa onyo kwa upande wenye hatia na maneno ya faraja kwa upande usio na hatia”).

Kesi inapomalizwa, inachukuliwa kwamba *lekorkalorbunu*, ambayo inawakilisha ukweli na haki imefikiwa. Faini (*banyinkortu*) zinapendekezwa. Faini kwa kawaida ni za vitu, kama vileo, sana sana pombe ya mnazi—inayoitwa *kubo nte*—pamoja na mifugo. Kiwango cha faini kinategemea uzito wa kosa, jinsi upande wa mashtaka ulivyojiendesha katika shauri, na taarifa nyingine za makosa yaliyopita. Mara tu faini zinapolipwa, inachukuliwa kwamba suluhu imekubaliwa na wapinzani. Vinywaji vinatumika kama tambiko ili kuridhisha miungu (*atibluku*). Vinamwagwa na kasisi anayeheshimiwa na kama hayupo mzee anachukua nafasi.

Akiwa na kibuyu cha vinywaji mkononi, mheshimiwa kasisi, atamwaga tambiko likiambatana na maneno kama:

Mwenyezi Mungu uliye juu mbinguni, dunia tuliyosimamia (*Oh! Atibluku atsa kator, kalor kemenge*), na kinywaji hiki, tunawaomba miungu mtusaidie sisi kudumisha amani katika pande hizi zinazopingana. Pande zote mbili zitakapokunywa kutoka katika kibuyu hiki asiyepo atakayemdhuru mwingine. Mwadhibu mtu yeyote atakayeonyesha nia mbaya dhidi ya mwingine, au kudharau mamlaka ya majaji au kujaribu kuleta maafa katika jumua.

Ni lazima ikumbukwe kwamba katika kesi zinazohusu makosa makubwa kabisa, hasa kesi ambazo mhalifu amepatikana na kosa la kutumia silaha za kudhuru kuliko kupigana ngumi, na kufanywa hivyo amemtoa damu mwabuem mwenzie, anaweza kufungua faili mahakamani ambayo itadai mifugo, kwa kawaida kondoo (*kofonu*). Hii faini inatolewa hata kama imeonekana kuwa upande huo una makosa au hauna. Katika kesi kama hii mheshimiwa kasisi atamwaga kafara na kuita mizimu ya pande zinazopingana mara tatu wakitaja dunia (*kalor*) mara tatu na kuwaomba “watakase jamii kutokana na kufuru na hatari” (*ntedie musue*) ambayo inaweza kuletwa na damu iliyomwagika. Baada ya haya, kondoo atachinjwa mahali palepale damu ya mtu ilipomwagikia. Kinywaji na nyama ya mnyama itagawanywa kwa watu wote waliokuwepo. Kwa sherehe hii ya tambiko, inaaminika kwamba miungu imeridhishwa na dunia pamoja na pande zote mbili zimetakaswa.

## Uchambuzi

Tofauti na mfumo wa baraza la wazee wa mahakama wa sasa, ambapo wazee wa baraza wanachaguliwa kabla ya kuanza kwa shitaka, wazee wa baraza katika mfumo wa Buem wa *adzina* wanateuliwa baada ya shitaka na utetezi kumalizika. Faida ya kuchagua baraza kwa namna hii unatokana na ukweli kuwa kwa vile hakuna mtu anayeweza kusema ni nani watakuwa wazee wa baraza kwa vile mtu yeyote aliyekuwepo kwenye mwenendo wa kesi, na ambao wanadhaniwa kuwa na msimamo mzuri katika jamii ya Buem anaweza kuchaguliwa. Pia jamii ya Buem wanaishi karibu karibu wanaunganishwa na vipengele vya mtandao wa matambiko, siasa na uchumi ni vigumu kwa wazee wa baraza kuweza kuepuka upendeleo.

Kuomba nguvu za asili kama njia ya kutekeleza maamuzi miongoni mwa Wabuem inaonyesha kwamba njia za usimamizi wa migogoro inatoa sio tu njia ya mwongozo kwa wapinzani kutafuta mwafaka, bali pia ni njia ambayo miungu wanategemewa kuendeleza utawala wa sheria za jamii. Hii haishangazi kutokana na ukweli kuwa mfumo wa kisiasa wa mahakama wa Buem hauna aina yoyote ya idhini au vitisho vya kutumia nguvu, kwa kawaida vinafanywa na polisi kwa mfungwa na dola ndiyo inayohusishwa kulingana na mfumo wa kisasa.

# Vikwazo vya Kitaasisi katika Uhamasishaji wa MA

## Ufikiaji wa Jumua katika Mitandao ya Kijamii na Taasisi Rasmi

Makala hii imeandikwa na PreetiShroff-Mehta na inalenga eneo la utafiti wake wa shahada ya udaktari wa falsafa (PHD) uliofanyika nchini India katika kipindi cha 2000-2001. Utafiti huu umepata taarifa zake kutokana na masimulizi ya watu binafsi kumi na sita ambao ni wabunifu wenyeji na uzoefu wa wanajamii katika kupitia upya na kurekebisha taratibu za maarifa asilia. Kazi hii ilisimamiwa na Prof Anil Gupta wa Chama cha Utafiti na Mabadiliko kwa Teknolojia Endelevu na Taasisi (SRISTI) na Bwana P. Vivekanandan wa Kilimo Endelevu na kikundi cha mazingira cha kujitolea (SEVA). Bi, Shroff-Mehta alichukuliwa na Chuo Kikuu cha Maryland na atafundisha kozi za Elimu ya Jadi na Vitendo vya Kidunia itakayoanza msimu wa Machipuko (Spring) 2004.

**Tini za MA 60  
Septemba 2003**

Katika miaka ya hivi karibuni mashirika mengi ya kimataifa na asasi zisizo za serikali zilifufua jitihada zao za kutoa na kuinua maarifa asilia katika kupanga na kutekeleza maendeleo. Juhudi hizi zinasisitiza mifumo ya maarifa ya wenyeji pamoja na vitendo kama vyanzo vya kuthamini katika maendeleo ya dunia. Vipengele muhimu vinavyohusiana na maarifa asilia katika maendeleo vinavyojadiliwa mara kwa mara ni:

- *Uwekaji kumbukumbu*: Maarifa asilia ya uwekaji kumbukumbu, mawasiliano na urandanaji na hali halisi.
- *Umiliki*: Umiliki wa kienyeji juu ya suala zima la maarifa maalumu
- *Mfumo wa motisha*: Kumotisha marekebisho ya maarifa asilia (kwa kupitia maandishi na usambazaji, kutumbulika katika eneo moja hadi jingine, kufaa kwake kwa ulimwengu mzima na ongezeko la thamani yake) na
- *Ufikiwaji wa maarifa na taasisi*: kuunganisha taasisi za asilia na zile za kisasa kwa maendeleo endelevu na kuwezesha jamii za mahali kupata masoko, wakala wa serikali, taasisi za kifedha, vituo vinavyohusu utafiti chuo kikuu na maendeleo ya uchapishaji kimataifa.

Kazi hii ya uboreshaji asilia nchini India inalenga vipengele hivyo vya MA vilivyoonyeshwa hapo juu lakini inasisitiza mtazamo wa nafasi ya taasisi katika kuchochea /kuinua mitazamo ya uboreshaji asilia. Ni wazi kuwa kuna kufanana kwingi kuliko kutofautiana kati ya kile kinachoelezwa hapa na hali halisi katika nchi nyingine za kusini zinazoendelea.

### Ufufuaji na urandanishaji wa maarifa asilia: Malengo ya jumua asilia

Juhudi zinazoendelea za kufufua jumua na kilimo kilicho maalumu katika kanda fulani, afya, elimu na shughuli za maisha za uchumi katika juhudi za maendeleo ya dunia zinagusa thamani ya uboreshaji wa maarifa asilia katika kiwango cha kimataifa. Katika mfululizo wa mahojiano na waboreshaji wenyeji yaliyoendeshwa wakati wa utafiti wa MA, wanachama kumi na sita katika jumua katika majimbo mawili nchini India waliorodhesha malengo ya kufufua utendaji wa MA.

- (1) Kushughulikia masuala ya umasikini na mbinu za maisha;

- (2) Ufanisi katika gharama na ufanyaji kazi katika uzalishaji wa kilimo;
- (3) Kuendeleza na kuhifadhi mazingira;
- (4) Kusimamia majanga ya misimu kama vile ukame, mafuriko na ukosefu wa kazi;
- (5) Jumua kujitegemea na kuhifadhi mila na vipaumbele vyake;
- (6) Kuboresha hali ya uchumi wa jamii na kuanzisha ajira;
- (7) Uwakilishi kwa wanawake;
- (8) Mahitaji ya wanajumuia ya kujifunza.

Wakati wanaorodhesha malengo ya kufufua maarifa asilia na kuyatumia, wanajumuia waligusia pia mlolongo wa vikwazo katika uboreshaji wa maarifa asilia.<sup>1</sup>

(1) *Vikwazo kutoka kwenye familia na jumua:* Wagunduzi wengi kutoka ndani wanapata vikwazo kutoka kwa wanafamilia. Katika sehemu hizi za majaribio ya kilimo, wanafamilia husita kuwekeza katika miaka kadhaa na kupoteza kipato chao cha sasa hivi bila kuwa na uhakika wa mapato yale ya siku za usoni yatakayotokana na majaribio ya ubunifu wa mazao. Wanajumuia hawakubali uanzishaji wa kilimo na shughuli asilia za kilimo mpaka faida za huu uzalishaji wa watu wengi unapoonyeshwa matokeo mazuri katika kipindi kifupi na uzalishaji wa mazao unapoimarishwa katika soko. Wakati mwingine wakulima maskini wa ndani wanakuwa hawana ardhi kwa kilimo cha mbegu na ujuzi wa kilimo pamoja na maarifa ya uthibitisho halali na njia muafaka kwa masoko.

(2) *Vikwazo vya msimu:* Kikwazo kikubwa cha ndani katika kufufua na kurekebisha mifumo ya maarifa asilia ni vipengere vya kimsimu. Kikundi cha wakulima asilia katika majimbo ya Taminadu na Gujarat waligusia kwamba majaribio ya uwekezaji wao katika shamba la dawa za mitishamba yameshindwa kutokana na pepo hafifu za monsuni na ukame wa mfululizo, ukosefu wa maji ya kunywa na ya umwagiliaji, upotevu wa mifugo na uhamaji wa wafanyakazi. Kikwazo kingine ni kuelewa mazingira ya kihistoria ambayo shughuli asilia zinaweza kuwepo, kwa mfano ukubwa wa shamba, uwiano wa watu na ardhi pamoja na aina ya vyakula. Kufufua shughuli fulani asilia kwa nyakati hizi kunahitaji kuzichukua na kuzifanyia marekebisho ili ziendane na mazingira asilia.

(3) *Vikwazo kutoka taasisi rasmi:* Vikwazo kutoka asasi rasmi kama vilivyoonyeshwa na wanajamii vinaonyesha ni wenyeji kukosa nafasi kwenye “mitandao mipya ya kijamii” kama vile teknolojia ya kilimo na wakala wengi, asasi za elimu ya juu na utafiti, asasi za fedha, vyama vya siasa, AZISE na mashirika ya kimataifa (tofauti na mitandao ya vijiji na jumua).<sup>2</sup>

Jedwali linaonyesha muhtasari juu ya mtazamo wa wanajumuia asilia kuhusu vikwazo vya asasi katika kuendeleza marekebisho asilia na jitihada zao za kutatua vikwazo fulani. Linaorodhesha mlolongo wa vikwazo vya kitaasisi vilivyoonyeshwa na wagunduzi asilia na wanajumuia wengine. Linajumuisha wajibu wao kuhusu mtaji hasa wa jamii kama vile—gharama za kuweza kuwa na mitandao na kushiriki katika mitandao hiyo ya jamii, kawaida ya “kujitua” kwa mitandao fulani ya mijini na vijijini na mzigo kwa mitandao ya jamii (juu ya—undani, ufinyu na ugumu).

- 1 Wagunduzi wenyeji wameainisha vikwazo vingi vya kiasasi ambavyo vinaonyesha ufinyu au kutokuwa na haki ya kuanzisha taasisi rasmi au zisizo rasmi pamoja na mitandao yake inayohusu jamii. Taasisi zinazowakilisha miundo ya mashirika, itikadi zinazohusu mifumo fulani ya maendeleo, mitandao ya ndani na nje, mila na desturi dhahiri. Pia, taasisi zinazofuata sheria na kanuni na zinatumia mbinu fulani kusimamia utekelezaji wa sheria. “Wanzishaji wa taasisi wanaweza kuwa wengi, kama vile wanasheria, wafanyabiashara au wanajumuia. Sheria za ushirika, za wazawa na za ufilisi wa benki ni taasisi za umma. Vilevile wakala wa mahakama, ukusanyaji wa kodi na wakala wa sheria. Mabenki, makubaliano baina ya wanajamii na taratibu za kurithishana ardhi ni asasi binafsi. Asasi nyingi binafsi zipo kwenye usimamizi wa asasi za umma. Kwa mfano, benki binafsi zinafanya kazi kwa kutumia muundo wa sheria za umma. Kanuni za kijamii zinaweza kuwa au kutokuwa na sheria za umma.” (*Ripoti ya Maendeleo ya Dunia 2000, Sanduku 1.2, uk.6*)
- 2 Dhana ya mtaji wa jamii humaanisha mali halisi anayopata mtu kutokana na kufahamiana na watu wengine, au kuwa sehemu ya mtandao ambao jamii inao au wao kumfahamu mtu pamoja na kuwa na sifa nzuri. Vipengele viwili vya mtaji wa jamii ni: uwezo wa jamii kuweza kutumia mali kulingana na nafasi yake katika mtandao fulani wa jamii na uwezo wa jumua kutumia mitandao mingi ya jamii. Bourdieu na Coleman wanasisitiza tabia ya kutogusika kwa mtaji wa jamii tofauti na aina nyingine. Wakati mtaji wa uchumi uko katika akaunti za watu wenyewe, mtaji watu umo vichwani mwao, mtaji wa jamii uko katika muundo wa mahusiano yao. Ili kumiliki mtaji wa jamii, mtu lazima ahushwe na wengine, na ni hao ndio chanzo cha faida yake. [...] Lengo la watu wengine kumilikisha mali si sawa kwa kila mtu. Kwa kiwango kikubwa mtu anaweza kutofautisha kati ya malengo ya muda dhidi ya malengo yenye kuleta motisha.

## Vikwazo vya kitaasisi katika Kuchukua Maarifa Mapya

Ugunduzi (Hatua pevu)	Vikwazo vya Kitaasisi/Sekta	Mkakati ya Mgunduzi	Matokeo
Usimamizi wa mchakato wa ufugaji (Hatua ya juu)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Wapanga mipango ya maendeleo na jumua asilia kutoamini maarifa ya wanawake wa vijijini.</li> <li>Wagunduzi wanawake kukosa uwezo wa kufikia taasisi mijini na vijijini pamoja na mitandao ya kijamii</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuanzisha na kuonyesha shughuli mpya kwa wanajumua wa kijiji au taasisi za nje.</li> <li>Kuelimisha wataalamu kutoka nje na wakala mbalimbali wa maendeleo.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mabadiliko ya maisha ya kanda nzima</li> <li>Ushiriki hai wa mgunduzi wa mwanzo katika mtandao wa maarifa</li> </ul>
Hakuna Nishati/Teknolojia ya kustawisha kilimo/mitambo (Hatua ya juu)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kukosekana kwa uwekezaji kibiashara katika mfumo wa wenyeji</li> <li>Ufinyu wa masoko na usambazaji.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kushirikisha maendeleo ya mazao na juhudi za soko pamoja na SKISTI.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mahitaji ya kanda na kitaifa kutokana na kuongezeka kwa mazao na mauzo.</li> </ul>
Mfumo wa zao linalotoa matunda kwa wingi (Mpya)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ukosefu wa mbinu za kusimamia ukame katika kilimo- ukosefu wa maji</li> <li>Uhimizaji wa Serikali katika nyenzo za kilimo pamoja na mbinu za kilimo.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuendeleza mazao mbalimbali yaliyoanzishwa, kuanzisha kwa misimu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Usambazaji wa ndani wa mauzo yanayozaa mapema na mbegu zinazotoa mapato ya juu.</li> </ul>
Mfumo mpya wa mazao mbalimbali (Hatua ya juu)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jamii kutokuwa na nia na moyo kuhusu kilimo na kukosekana kwa jamii ya wanasayansi.</li> <li>Mchakato wa kisiasa wa serikali katika kuidhinisha ubora wa mbegu</li> <li>Ukosefu wa ufadhili wa serikali na ajira mbadala majira ya ukame</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kushirikiana na mtandao wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kutambua aina mpya mbalimbali.</li> <li>Juhudi za pamoja katika kufanya majaribio ya kuendeleza shamba la mbegu na wakala wa kujaribu mbegu</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ukosefu wa vifaa vya maabara katika uwekaji wa viwango vya dawa za mitishamba, mifugo inahitaji majaribio kwa kutumia mchanganyiko wa madawa mbalimbali asilia na namna ya kutumia dawa.</li> <li>Madaktari wa Allopathy wa madawa kukosa imani katika matibabu ya kutumia dawa za mitishamba</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kushirikiana na jamii kwa utafiti na uanzishaji wa Teknolojia endelevu na Taasisi (SKISTI) na maabara ya utafiti wa dawa za miti shamba.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mpango wa kusambasa dawa za mwitu shamba zilizothibitishwa</li> </ul>
Mganga wa kutumia mitishamba (Mpya)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kukosekana kwa aina fulani ya mali ghafi kavu za dawa za miti shamba (kutegemea mgavi wa kibiashara)</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Matibabu ya dawa za mitishamba na matatizo ya msimu ya afya ya wanawake</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jukumu la wagunduzi wanawake kuendeleza akiba za wanawake maskini.</li> </ul>
Usimamizi wa asilia (shamba, gesi asilia, mifugo) (Hatua ya juu)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Muda mrefu unahitajika kubadili kutoka katika biashara kwenda kwenye mfumo wa shughuli za kilimo.</li> <li>Hasara kifedha kutokana kutegemea uzalishaji wa aina mbalimbali za mbuzi na njia za biashara za kilimo hapo awali</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Familia inashiriki katika shamba lao, usimamizi wa mifugo na shughuli ya gesi</li> <li>Kushiriki katika mifumo ya wenyeji ( Chama cha wakulima)</li> <li>Kuwa na mtandao na ofisi ya kodi, mashirika ya kilimo na asasi za kitaifa za utafiti</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Usambazaji wa njia za asili za kulima.</li> <li>Chama cha wakulima wa ndani kuunga mkono njia asilia za kilimo na njia za kujifadhili kwa wakulima wa eneo husika</li> </ul>
Teknolojia ya kufua nazi (Mpya)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kukua kwa mahitaji ya nazi mjini na misimu ya kazi ambapo haitoshelezi kijijini.</li> <li>Usimamizi mwafaka na usambazaji wa nazi kwenye makampuni ya mjini.</li> <li>Ukosefu wa uwekezaji wa fedha katika kuendeleza mazao ya biashara.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuendeleza zao moja ili kuwa na ugavi wa nazi wa wakati wote na kumudu ukosekanaji wa nguvu kazi</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Upatikanaji wa kudumu na wa kuaminika wa zao la nazi kwa makampuni ya mjini.</li> </ul>
Aina mpya ya mpunga unaostahimili ukame (Hatua ya juu)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kukosa ushirikiano toka serikalini pamoja na mgogoro unaoendelea wa wataalamu wanasayansi wa kilimo.</li> <li>Mashindano mbali mbali ya aina mpya ya mbegu yaliyoanzishwa na wanasayansi wa kilimo.</li> <li>Hatua za kisheria zilizochukuliwa na serikali kama changamoto kwa serikali kutokana na usambazaji wa mbegu asilia katika soko.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kushirikiana na AZISE za wenyeji ili kupambana na kesi ya uhalali</li> <li>Kuonyesha aina bora ya mbegu ya mpunga inayostahimili ukame, na yenye ladha nzuri</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Usambazaji wa haraka na mafanikio wa mpunga wa kienyeji na kuanzisha mbinu za uzalishaji wa mbegu za mpunga.</li> </ul>
Mfumo asilia wa utengenezaji wa vitu vya kuchezea (mpya)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kukosekana kwa mapato katika kilimo ili kufanya kipanuliwe zaidi</li> <li>Kukosekana kwa aina fulani ya malighafi (lacquer) nchini.</li> <li>Kutokuwepo kwa wakala wa maendeleo serikalini.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kukuza aina ya asili ya toi ( kutumia vifaa asilia)</li> <li>Kushirikiana na AZISE za wenyeji na kitengo cha utangazaji cha SRISTI(GYAN)</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Utafiti wa kudumu kuhakikisha upatikanaji wa lacquer kutoka jimbo jingine kuendeleza michezo ya kuchezea</li> </ul>
Vifaa vya kukatia magugu shambani (Mpya)	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ukosefu wa pesa za kuendeleza aina hiyo ya mazao.</li> <li>Ushindani katika soko, zao hilo hilo linaingizwa soko la kitaifa kwa njia ya mashirika ya kimataifa.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kutafuta kwa bidii kwa mwekezaji na ushirikiano unaoendelea na AZISE za wenyeji zilizoko katika mji wa Madurai- Kilimo endelevu na huduma ya kujitolea ya mazingira (SEVA)</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mgunduzi sasa ni mwanachama wa mtandao wa wagunduzi wenyeji katika jimbo la taminadu.</li> <li>Ushirikiana na wawekezaji wa ndani.</li> </ul>
Mfumo asilia wa uchugaji wa mifugo	<ul style="list-style-type: none"> <li>Aina ya mifugo chotara isingeweza kuishi kwenye ukanda wenye hali ya milima.</li> <li>Serikali ikimiliki misitu, wafugaji wanahangaika kupata nyasi kwa ajili ya mifugo yao asilia.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kutegemea mifugo ya asilia</li> <li>Mgogoro na mamlaka ya misitu.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mashirika yasiyo ya kiserikali kuingilia na kuhusika katika mgogoro baina ya wakala wa serikali na</li> </ul>

• Vipengele vya fedha vya ugunduzi wa wenyeji vilishirikishwa kwa mtafiti tu, wagunduzi wenyeji hata hivyo waliomba kwamba habari hii iwekwe kama siri kwa ajili ya sababu binafsi na sababu maalumu za jumua.

